# UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

## *KIPINDI CHA MABABA WA IMANI:*
## *MWANZO 12-50*

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO
AGANO LA KALE, VOL.1B

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2009

# ORODHA YA YALIYOMO


Maelezo sahihi ya zana za kiufundi zilizotumika katika fasili hii ... i

Maelezo sahihi ya muundo wa maneno ya Kiebrania yanayogonganisha fasili ya maandiko ... iii

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasihi Hii ... viii

Agano la Kale kama Historia ... ix

Uandishi wa Historia ya Agano la Kale Ukilinganisha na Tamaduni za Kisasa za Mashariki ya Karibu ... xiii

Uwasilishaji na Ufasiri: Simulizi za Agano la Kale ... xiv

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ... xvi

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ... xviii

Utangulizi wa Kitabu cha Mwanzo 11:24-12:20 ... 1

Mwanzo 12 ... 3

Mwanzo 13 ... 20

Mwanzo 14 ... 27

Mwanzo 15 ... 37

Mwanzo 16 ... 57

Mwanzo 17 ... 64

Mwanzo 18 ... 73

Mwanzo 19 ... 85

Mwanzo 20 ... 96

Mwanzo 21 ... 108

Mwanzo 22 ... 115

Mwanzo 23 ... 123

Mwanzo 24 ... 127

Mwanzo 25 ... 138

Mwanzo 26 ... 147

Mwanzo 27 ... 155

Mwanzo 28 ... 165

Mwanzo 29 ... 171

Mwanzo 30 ... 177

Mwanzo 31 ... 183

Mwanzo 32 ... 193

Mwanzo 33 ... 201

Mwanzo 34 ... 206

Mwanzo 35 .......... 213
Mwanzo 36 .......... 222
Mwanzo 37 .......... 230
Mwanzo 38 .......... 240
Mwanzo 39 .......... 247
Mwanzo 40 .......... 252
Mwanzo 41 .......... 257
Mwanzo 42 .......... 268
Mwanzo 43 .......... 275
Mwanzo 44 .......... 281
Mwanzo 45 .......... 288
Mwanzo 46 .......... 300
Mwanzo 47 .......... 306
Mwanzo 48 .......... 316
Mwanzo 49 .......... 324
Mwanzo 50 .......... 339
Kiambatisho cha Kwanza: Mchoro wa Agano lote la Kale .......... 349
Kiambatisho cha Pili: Kauli ya Kimafundisho .......... 351

## MADA MAALUM

## ORODHA YA YALIYOMO


Majina ya Uungu, 12:1 ........ 4

Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob, 12:3 ........ 9

Masihi, 12:3 ........ 10

Kuuabudu Mwezi, 12:4 ........ 12

Waisraeli wa Mwanzo Wanaishi Palestina, 12:3 ........ 13

Malaika wa Bwana, 12:7 ........ 16

Jina la YHWH, 12:8 ........ 16

Shetani Akijaribu Kuzuia Uzao wa Masihi Katika Kitabu cha Mwanzo, 12:12 ........ 18

Agano, 13:15 ........ 23

Milele, 13:15 ........ 24

Maneno Yaliyotumika kwa Mashujaa Wenye Nguvu au Makundi ya Watu, 14:5 ........ 29

Ibada ya Ustawi, 14:5 ........ 29

Mtazamo wa Kibiblia Kuhusu Ulevi na Kileo, 14:18 ........ 33

Zaka Katika Utungaji Sheria ya Musa, 14:20 ........ 35

Utoaji Zaka, 14:20 ........ 35

Kuamini, Tumaini, Imani, na Uaminifu, 15:6 ........ 42

Haki, 15:6 ........ 46

Wafu Wako Wapi?, 15:15 ........ 51

Amani, 15:15 ........ 54

Moto, 15:17 ........ 55

Ahadi za Agano kwa Mababa wa Imani, 15:18 ........ 56

Asiye na Hatia, asiye na kosa wala mawaa, 17:1 ........ 66

Mungu anaelezwa kama mwanadamu (Lugha ya kibinadamu), 18:1 ........ 75

Uzani na Vipimo vya mashariki ya Karibu ya kale (usomaji wa vipimo), 18:6 ........ 77

Kumjua, 18:9 ........ 81

Kujamiiana kwa Jinsia moja, 19:4 ........ 87

Wema (hesed), 19:19 ........ 91

Ujinsia wa Mwanadamu, 20:4 ........ 98

Unabii wa Agano la Kale, 20:7 ........ 101

Utatu, 20:13 ........ 105

Mungu Huwajaribu Watu wake, 22:1 ........ 116

Namba Kumi na Mbili, 26:16……141
Istilahi kwa ajili ya Ufunuo wa Mungu, 26:5……150
Edomu na Israeli, 27:40……162
Teraphim, 31:19……186
Israel, 32:28……199
Grieving Rites, 37:29……238
Cremation,50:2 ……340

# MAELEZO MAFUPI YA VYANZO VYA KIUFUNDI VILIVYOTUMIKA KWENYE MFULULIZO WA FASIHI HII

I. Maneno/misamiati

Kuna maneno mengi mazuri mbali mbali yanayopatikana katika lugha ya Kiebrania cha kale.

A. *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* kilichoandikwa na Francis Brown, S. R. Driver, na Charles A. Briggs. Yanaegemea juu ya misamiati ya Kijerumani ya William Gesenius. Yanajulikana kwa vifupisho vya BDB.

B. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na Ludwig Koehler na Walter Baumgartner, yaliyotafasiliwa na, M. E. J. Richardson. Yanajulikana kwa vifupisho vya KB.

C. *A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na William L. Holladay na inaegemea juu ya maneno ya Kijerumani (#A).

D. Idadi tano mpya za usomaji wa neno la kithiolojia lililoandikwa *The New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, kilichohaririwa na Willem A. Van Gemeren. Yanajulikana kwa vifuapisho vya NIDOTTE.

Ambapo kuna aina ya maneno muhimu, nimeonyesha tafasiri mbali mbali za Kiingereza (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB) toka kwenye tafasiri za "neno-kwa-neno" na "mlinganyo wa nguvu" (kama vile Gordon Fee & Douglas Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 28-44).

II. Visarufi

Utambulisho wa kisarufi mara nyingi huzingatia juu ya John Joseph Owens' *Analytical Key to the Old Testament* katika juzuu ya nne. Hili limehakikiwa na Benjamin Davidson's *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon of the Old Testament.* Vitu vingine vya kusaidia kwa ajili ya visarufi na sintaksi ambazo zinatumika sana katika vipengere vya juzuu za agano la kale za mtiririko wa "kuelewa Biblia" ni "ule msaada wa mfuatano wa watafasiri" toka kwa United Bible Societies. Kimeandikwa "kitabu kidogo cha mkononi ________ ."

III. Kimaandiko

Mimi nimejikita kwenye uvuvio wa konsonanti za maneno ya Kiebrania(sio katika hoja za voweli za Kimosoreti na maoni.kama ilivyo katika maandiko yote yaliyonukuliwa kwa mkono,kwenye maandiko ya kale, kuna baadhi ya sura zenye maswali. Hili huwa hivyo mara nyingi kwa sababu ifuatayo:

A. *hapax legomenon* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano la Kale la Kiebrania)

B. Maneno ya kinahau (maneno na vifungu ambavyo maana yake iliyo wazi imekwisha potea)

C. Kutojulikana kihistoria (kukosekana kwa habari kuhusu ulimwengu wa kale)

D. Wingi wa elimu-maana ya Kisemitiki wa misamiati finyu ya Kiebrania

E. Matatizo yanayohusianishwa na uandishi wa maaandishi ya Kiebrania ya kale ya waandishi wa mwanzo kwa kutumia mkono.

F. Waandishi wa Kiebrania waliosomea huko Misri waliojisikia kuwa huru kuyahariri maandiko waliyoyanakili kwa ajili ya kuyafanya kuwa kamili na ya kueleweka wakati wa siku zao (NIDOTTE kur. 52-54).

Kuna vyanzo mbali mbali vya maneno na maandiko ya Kiebrania nje ya tamaduni ya kimaandiko ya Kimasoreti.

1. Torati ya Kisamaria
2. Magombo ya Bahari ya Chumvi

3. Baadhi ya sarafu, herufi na vigae vya vyungu vilivypatikana baadaye (vipande vya vigae vya vyungu vilivyotumika kuandikiapo maandiko), lakini kwa maeneo mengine, hakuna uhusiano wa kimachapisho katika Agano la Kale kama yale yaliyoko katika machapisho ya Agano Jipya la Kiyunani. kwa ajili ya ufasaha wa makala mazuri juu ya uendelevu wa kimaandiko ya andiko la Kimasoreti (miaka ya 900 B.K) angalia “Uendelevu wa andiko la Agano la Kale” na Bruce K. Waltke katika toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, kur. 51-67.

Andiko la Kiebrania lililotumika ni *Biblia Hebraica Stuttgartensia* toka German Bible Society, 1997, ambayo inaegemea juu ya Leningrad Codex ( 1009 B.K). Mara chache, matoleo ya kale (maandiko ya kale ya Kiyunani, Kiarama Targums, Syriac Peshitta, na Latin Vulgate) yanazungumzika kama Kiebrania ni kigumu au kinatatiza kwa wazi.

## MAELEZO SAHIHI YA MUUNDO WA KIVITENZI VYA KIEBRANIA AMBAVYO VINAGONGANA NA FASILI YA MAANDIKO

I. Maendeleo mafupi ya kihistoria ya Kiebrania

Waebrania ni sehemu ya kifamilia ya lugha ya Shemu kusini mwa Asia. Jina (lililotolewa na wasomi wa sasa) limetokana na Mwana wa Nuhu, Shemu (kama vile Mwa. 5:32; 6:10). Kizazi cha Shemu kimeorodheshwa katika Mwa. 10:21-31 kama Waarabu, Washamu, Waarameni, na Waashuru.

Kiukweli, baaadhi ya lugha za Kisemiti zinatumia na mataifa yaliyoorodheshwa katika ukoo wa Hamu (kama vile Mwa. 10:6-14), Wakaanani, Wafoeniki, na Waethiopia.

Waebrania ni sehemu ya kikundi cha kaskazini Magharibi mwa lugha hizi za Kisemiti. Wasomi wa leo wana mifano ya kikundi cha lugha ya kale toka :

A. Waamori (*Mari Tablets* tokea karne ya 18 K.K. huko Akadi
B. Wakaanani (*Ras Shamra Tablets* tokea karne ya 15 Ugariti
C. Wakaanani (*Amarna Letters* tokea karne ya 14 wakaanani wa huko Akadi)
D. Wafoeniki (Waebrania walitumia alfabeti za Wafoeniki)
E. Wamoabu (Mawe ya mfalme Mesha, 840 K.K)
F. Waaramaiki (lugha rasmi ya Himaya ya Uajemi iliyotumika katika Mwa. 31:47; Yer. 10:11; Dan. 2:4b-6; 7:28; Ezr. 4:8-6:18; 7:12-26 na iliongewa na Wayahudi katika karne ya kwanza huko Palestina

Lugha ya Kiebrania iliitwa "lugha ya Kaanani." Mara ya kwanza iliitwa "Kiebrania" katika utangulizi Mhubiri (Hekima ya Yoshua Bin Sira) kuhusu 180 K.K. na baadhi ya maeneo mengine ya awali, kama vile *Anchor Bible Dictionary*, juzuu 4, kur. 205na kuendelea) sana sana yanakaribiana kufanana na Wamoabu na kabila lililotumika huko Ugariti. Mifano ya ya Waebrania wa kale wanaopatikana nje ya Biblia ni

1. Kalenda ya Gaza, 925 K.K. (andiko la kijana wa shule)
2. Andiko /ujumbe wa Siloam, 705 K.K (maandiko yaliyopatikana katika njia za chini)
3. Vigae vya waebrania, 770 K.K (kodi inanakiriwa kwenye vigae vya chungu)
4. Herufi zilizoandikwa kwenye vigae, 587 K.K (mawasiliano kwenye vita)
5. Mihuri na sarafu za watu wa Makabi
6. Baadhi ya maandiko yaliyopatikana katika magombo ya Bahari ya Chumvi
7. Maandiko mbali mbali (kama vile "lugha[Kiebrania], " ABD 4:203 nakuendelea)

Kama ilivyo lugha zingine za Kisemiti, inaainishwa na maneno yaliyoundwa na konsonanti tatu (mizizi mitatu ya kikonsonanti). Ni lugha thabiti isiyopindika. Mizizi mitatu ya konsonanti inabeba msingi wa maana ya neno, wakati kiambishi awali, kiambishi tamati, au maneno ya nyongeza yanaonyesha utendaji wa kisarufi (voweli zinaongezeka baadae, kama vile Sue Green, *Linguistic Analysis of Biblicla Hebrew*, uk 46-49).

Misamiati ya Kiebrania inaonyesha tofauti kati ya lugha ya mjazo na ushairi. Maana ya neno imehusianishwa na asili ya ngano/hadithi (sio usanifu wa lugha). Mchezo wa neno na mchezo wa sauti ni vitu vya kawaida (*paronomasia*)

II. Dhana ya utabiri

A. VITENZI

Neno la kawaida linalotarajiwa ni KITENZI, KIWAKILISHI, KIIMA (likiwa na vivumishi vyake), KISHAMIRISHO (kikiwa na vivumishi chake). KITENZI cha msingi kisicho pungua ni *Qal,* chenye muundo wa UMOJA, JINSI YA KIKE, na TIMILIFU. Ni namna misamiati ya Kiebrania na Kiaramaiki inavyopangwa. VITENZI vinanyumbulishwa majina kuonyesha

1. Namba-umoja, wingi, umiliki wa vitu viwili
2. Jinsi-jinsi ya kiume na jinsi ya kike (isio na jinsi)
3. Dhamira-elekezi, tegemezi, shurutishi (kwa kulinganisha lugha za Magharibi ya leo, uhusiano wa kitendo kuelekea ukweli halisi)
4. Njeo-(dhana)
   a. WAKATI TIMILIFU, inayomaanisha kutimiliza, kwa maana ya kuanza, kuendelea, na kuhitimisha kitendo. Mara zote muundo huu ulitumika kwa ajili ya kitendo kilichopita,

tukio linatokea. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "muundo mzima ulioelezewa kwa wakati timilifu pia umezingatiwa kuwa wenye uhakika. Wakati usiotimilifu unaweza kuonyesha hali ya kuwezekana au shauku au yenye kutarajiwa, lakini wakati timilifu unaliona hili kama lenye uhakiki, halisi na kweli" (uk. 36). S. R. Driver, *A Treatise on the Use of the Tenses in Hebrew*, inaielezea kama: wakati timilifu unaofanya kazi kuonyesha vitendo vyenye kutimilizwa ambavyo hakika vinasimama wakati ujao, lakini vinachukulia kama vyenye kujitegemea juu ya kusudi lisilobadilika la nia thabiti ambalo laweza kuongewa kama kitu halisi kilichochukua nafasi: kwa hiyo suluhisho, ahadi,au tamko, hasa lile la ki-Ungu mara nyingi linatamkwa katika njeo ya wakati timilifu"(uk. 17 mf., utimilifu wa kinabii). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anauelezea muundo wa kimaneno kwa namna hii:

"….inaiangalia hali kutokea nje, kwa ukamili wake. Kwa namna hiyo kinaelezea ukweli mrahisi, ingawa kinawezakuwa ni kitendo au hali (ukijumuisha hali ya kuwa au fikra). Kinapotumika katika vitendo, mara nyingi inakitazama kitendo kama kilicho kamili toka kwenye hoja ya mzungumzaji mwenye ustadi au msimuliaji (ikiwa ni kamili au sio kamili kwa maana ya uhalisia au ukweli na sio hoja). Utimilifu unaweza kuhusika katika kitendo /hali ya wakati uliopita, uliopo ao ujao. Kama ilivyoelezewa hapo juu, muda, ambao unashawishi namna gani mtu anaweza kutafasiri utimilifu kwenda kwenye njeo ya lugha iliyobobea kama Kiingereza, lazima ipimwe toka kwenye muktadha"(uk.86)

b. WAKATI USIOTIMILIFU, unaoelezea kitendo kilichoko katika mchakato (kisichotimilifu, chenye kujirudia, chenye kuendelea, au chenye udharura), mara nyingi huenenda kuelekea lengo. Mara nyingi muundo huu ulitumika kwa kitendo cha wakati uliopo na ujao. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "NYAKATI ZOTE ZISIZOTIMILIFU zinawakilisha hali yakutokukamilika. Zinaweza kuwa ni zenye kujirudia au kuendelea au za dharura. Kwa maneno mengine, au kwa sehemu Fulani inaanza au kiasi Fulani inahakikiwa. Kwa namna zozote katika baadhi ya maana haijamalizika, yaani., haijakamilika" (uk. 55). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anasema "ni vigumu kupunguza kiini cha kutokutimia kwenda dhana moja, kwa vile inajumuisha vyote dhima na dhamira. Muda mwingine wakati usiotimilifu hutumika kwa namna ya kuarifu na kutengeneza maelezo pingamizi. Wakati mwingine inakitazama kitendo zaidi kitegemezi, kama kinadharia, dharura, chenye kuwezekana na nakadharika" (uk. 89)

c. Neno lililoongezewa *waw,* linalounganisha KITENZI kwenye kitendo cha KITENZI kilichopita

d. Dhana SHURUTISHI, inayosimamia juu ya uhiari wa mnenaji na kitendo muhimu cha wasikilizaji

e. Katika Uyahudi ya kale muktadha mpana uliweza kuamua mwelekeo wa muda wa uandishi uliokusudiwa.

B. Miundo mikuu saba iliyobadilishwa na maana zake. Kiuhalisia miundo hii inatenda pamoja na nyenzake katika muktadha na haipaswi kutengwa

1. *Qal* (*Kal*), ni muundo wa kawaida na wa msingi katika miundo yote. Unadokeza kitendo rahisi au hali ya nafsi. Hakuna kisababishi au ulazima uliotumika.
2. *Niphal*, ni muundo wa pili ulio wa kawaida sana. Mara nyingi huwa katika hali ya KUTENDWA, lakini muundo huu pia hutenda kama wenye kubadilishana na kujirejea. Pia hauna kisababishi au ulazima uliotumika.
3. *Piel*, muundo huu ni muundo tendaji na huelezea kuhusu kukifanya kitendo kuwa katika hali ya nafsi. Maana ya msingi ya shina la neno *Qal* inajitokeza au kuendelea kwenye hali ya nafsi.
4. *Pual*, ni neno mfanano TENDWA wa neno *Piel*. Mara nyingi huelezewa kwa KIAMBATA
5. *Hithpael*, ambalo ni shina la kujirejea au kubadilishana. Linaelezea usisitiaji wa kitendo au hali ya kudumu ya kitendo kulinganisha na shina la neno *Piel* . Muundo adimu TENDWA unaitwa *Hothpael*.

6. *Hiphil*, ni muundo tendaji wa usababishaji shina tofauti na neno *Piel*. Unawezakuwa na dhana ya ruksa, lakini mara nyingi unarejelea kwenye sababu ya tukio. Ernst Jenni, Mjerumani mwenye asili ya kiebrania mwana sarufi, anaamini kuwa neno *Piel* linadokeza kitu fulani kuja kwa hali ya nafsi, wakati *Hiphil* inaonyesha jinsi inavyotokea.
7. *Hophal,* ni neno mlingano TENDWA kulinganisha na neno *Hiphil*. Haya mashina ya mwisho mawili ndiyo madogo yaliyotumika kati ya yale mashina saba.

Wingi wa habari hii unapatikana toka *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, cha Bruce K. Waltke na M. O'Connor, kur. 343-452

Chati ya kundi na kisababishi chake. Namna moja katika uelewa wa muundo wa KITENZI cha Kiebrania ni kukiangalia chenyewe katika kipengere cha mahusiano ya IRABU. Baadhi ya mashina ya maneno yanatofautiana na mashina ya maneno mengine (yaani *Qal - Niphal; Piel - Hiphil)*, chati iliyoonyeshwa hapa chini inajaribu kuangazia kwenye utendaji wa msingi wa mashina ya KITENZI na visababishi vyake.

| **IRABU au KIIMA** | **HAKUNA KUNDI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDAJI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDEWA LINALOFUATA** |
|---|---|---|---|
| TENDAJI | *Qal* | *Hiphil* | *Piel* |
| YA KATI TENDWA | *Niphal* | *Hophal* | *Pual* |
| KUJIREJEA/KUTENDEANA | *Niphal* | *Hiphil* | *Hithpael* |

Chati hii imechukuliwa toka katika majadiliano mazuri ya muundo wa kivitenzi katika uelewa wa utafiti wa lugha ya Akkadia (kama vile Bruce K. Waltke, M. O'Conner, *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, ukurasa wa 354-359)

R. H. Kennett, *A Short Account of the Hebrew Tenses*, ametoa onyo lenye kufikirika kuwa muhimu. "mara nyingi nimeweza kuanzisha katika mafundisho, kuwa kiongozi cha wanafunzi kilicho kigumu katika vitenzi vya Kiebrania ni kupata maana iliyoelezewa katika fikra za Waebrania wenyewe; kuwa ndiyo kusema, kuna tabia ya kutoa kwa mwelekeo wa kufanana kwa kila njeo za Kiebrania kama namba fulani ya muundo wa Kilatini au Kiingereza ambapo njeo hiyo mahsusi kwa kawaida yaweza kutafasiriwa. Matokeo ni kushindwa kutofautisha wingi wa hivi vivuri venye maana, ambavyo vinatoa uhai aina hiyo na nguvu kwenye lugha ya Agano la Kale. Ugumu katika matumizi ya vitenzi vya Kiebrania uko tu katika hoja ya mtizamo, kwa hiyo moja kwa moja yanatofautiana na ya kwetu, kutokana na kile Waebrania wanaangalia kitendo; muda wa mambo, ambao pamoja nasi ni upendeleo wa kwanza, kama neno lenyewe, "njeo" linavyoonyesha, kwao kuwa ni chaguo la pili. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa mwanafunzi kwa uwazi aweze kuchukua, sio kwa wingi miundo ya Kilatini au Kiingereza ambayo inaweza kutumika kutafasiri kila njeo za Kiebrania, bali kiasi Fulani dhana ya kila kitendo, kama kilivyowasilishwa katika fikra za Waebrania. Jina la 'njeo" kama lilivyotumika katika vitenzi vya Kiebrania vinapotosha. Kile kinachoitwa 'njeo' za Kiebrania hakielezei muda lakini kwa kidogo hali ya kitendo. Hakika hakikuwekwa kwa ajili ya kuleta mkanganyiko ambao ungaliweza kutokea kupitia matumizi ya neno 'kauli' kwa namna zote mbili ya nomino na vitenzi, 'kauli' zingalikuwa nzuri zaidi kwenye usanifu kuliko 'njeo.' Mara nyingi ni lazima kitu kiwekwe akilini kuwa haiwezekani kutafasiri kitenzi cha Kiebrania kwenda kwenye Kiingereza bila kutumia udhibiti ambao haupo kabisa katika Kiebrania. Waebrania wa mwanzo kamwe hawakufikiria kitendo chaweza kuwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao, lakini walifikilia tu kwenye *utimilifu* yaani., kitendo kilichokwisha tendeka, au *kisicho timilifu,* yaani., kama katika njia ya kusonga mbele. Tunaposema kuwa njeo Fulani ya Kiebrania wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao katika Kiingereza, hatumaanishi kuwa mawazo ya Kiebrania ya hicho kama wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao, lakini tu kuwa lazima itafasiliwe katika Kiingereza.

Wakati wa kitendo Waebrania hawakujaribu kuelezea kwa namna yeyote ya muundo wa kuongea kwa maneno (utangulizi na uk.1). kwa angalizo la pili, Sue Groom, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, anatukumbusha sisi, "hakuna namna ya kuweza kujua ikiwa muundo wa wasomi wa sasa wa elimu-maana na uhusiano wa maana katika lugha zilizokufa au kupotea ni taswira ya fikra zao, au lugha zao mama, au maeneo hayo yalikuwepo katika Waebrania wenye hadhi" (uk. 28).

C. Dhamira (ambazo ni mifanano ilichukuliwa toka kwenye lugha za kimagharibi ya sasa)
   1. Imetokea, inaendelea kutokea (NI KAULI ELEKEZI), mara nyingi inatumia njeo WAKATI TIMILIFU au WAKATI UNAOENDELEA ( KAULI ZOTE ENDELEVU ziko katika KAULI ELEKEZI).
   2. Itatokea, ingalia tokea (KAULI TEGEMEZI)
      a. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU ya wazi
         1) Zenye KUFUNGAMANA (likiongezewa herufi h), nafsi ya kwanza KAULI ISIOTIMILIFU ambayo mara nyingi huelezea kutakia heri, hitaji, au kutia moyo (yaani., matendo ya hiari ya mzungumzaji)
         2) ASILI NA UFAFANUZI ZAIDI WA NENO (badiliko la ndani), mtu wa tatu KAULI ISIOTIMILIFU (inawezakuwa mtu wa pili katika sentensi kanushi) ambayo mara nyingi inaelezea ombi, ruhusa, maonyo, au ushauri
      b. Hutumia njeo ya WAKATI TIMILIFU ikiwa na *lu* au *lule.* Miundo hii inafanana na sentensi YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI katika lugha ya Koine ya huko Uyunani. Maelezo yasiyo sahihi (Kishazi chenye kuelezea tamko ndani ya sentensi yenye masharti) yenye kuleta hitimisho lisilo sahihi (Kishazi kikuu ndani ya sentensi yenye masharti).
      c. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU na muktadha wa *lu,* vile vile maelekezo wa wakati ujao, kuangalia matumizi ya KAULI TEGEMEZI. Baadhi ya mifano inapatikana kwa J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament ni* Mwa.13:16; Kumb. 1:12; I Fal. 13:8; Zab. 24:3; Isa. 1:18 (kama vile kur. 76-77).

D. *Waw* – Kinyume chake/yenye matokeo yaliyofuatana/rejeshi. Huu muonekano wa kipekee wa isimu zenye kushughulikia kupanga maneno ya kisarufi ya Kiebrania imeleta mkanganyiko mkubwa kwa miaka mingi. Imetumika kwa namna nyingi mara nyingi ikizingatia juu ya uwasilishaji. Sababu ya mkanganiyiko ni wale wasomi wa mwanzo walikuwa watu wa Ulaya na wakajaribu kutafasiri katika ulelewa wa lugha zao za asili. Na hili lililopoonekana kuwa gumu wakaanza kulaumu lugha ya Kiebrania kuwa ni ya zamani, lugha ya kikale. Lugha za Ulaya ni NJEO (za muda) zinazoegemea kwenye VITENZI. Baadhi ya namna na madokezo ya visarufi yaliainishwa na herufi WAW ambayo iliongezwa kwenye shina la KITENZI TIMILIFU au KITENZI ISIOTIMILIFU. Hii inabadilisha namna ya kitendo kilivyo tazamwa.
   1. Katika simulizi za kihistoria VITENZI vinaunganishwa pamoja katika mfuatano vikiwa na mwongozo wa kawaida
   2. Kiambishi awali cha *waw* kinaonyesha uhusiano maalum kikiwa na KITENZI kilichopita.
   3. Muktadha mpana mara nyingi ni kiini cha uelewa wa mfuatano wa KITENZI. VITENZI vya Kisemiti haviwezi kutathimini utengano. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anaeleza utofauti wa Waebrania katika matumizi ya neno *waw* kabla ya KAULI TIMILIFU na KAULI ISIOTIMILIFU (kur. 52-53). Kama wazo la msingi la KAULI TIMILIFU ni muda uliopita, kuongezeka kwa neno *waw* mara zote linatenda kwa dhana ya wakati ujao. Hili pia ni kweli kwa KAULI ISIOTIMILIFU ambayo wazo lake la msingi ni la wakati uliopo au wakati ujao; kuongezeka kwa neno *waw* lililowekwa katika wakati uliopita. Hili ni badiliko la muda lisilo la kawaida ambalo linaelezea kungezeka kwa neno *waw,* sio kwenye badiliko la maana yake ya msingi ya njeo yenyewe. KAULI TIMILIFU ya neno *waw* inatenda kazi vizuri kwenye unabii, wakati KAULI ISIOTIMILIFU ya neno *waw* inatenda vizuri kwenye simulizi (kur. 54,68). Watts anaendeleza ufafanuzi wake, " kwa ajili ya kuonyesha tofauti iliyopo ya msingi kati ya neno *waw* kiunganishi na neno *waw* linalojirudia, utafasiri ufuatao unatolewa:
      1) Neno *waw* ambalo ni kiunganishi hutokea mara nyingi kuonyesha ufanano.

2) Neno *waw* kwa mfululizo linatokea mara zote kuonyesha mwendelezo. Ni muundo pekee wa neno *waw* unaotumika ukiwa na mfululizo wa kauli isiotimilifu. Uhusiano kati ya kauli zisizotimilifu zilizounganishwa nayo yaweza kuwa ni mfuatano wa muda, matokeo ya kimantiki, sababu za kimantiki, au tofauti za kimantiki. Kwa namna yeyote ile kunamfuatano"(uk.103)

E. KITENZIJINA-Kuna aina mbili ya vitenzijina
   1. KITENZIJINA CHA MOJA KWA MOJA, chenye "nguvu, kinachojitegemea, kinachoshambulia maelezo yaliyotumika kwa ajili ya matokeo ya kuvutia…..kama kiima, mara nyingi hakina kitenzi kilichoandikwa, kitenzi 'kuwa" kikiwa kinaeleweka, hakika, neno linabaki kusimama lenyewe wazi,"(J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament,*" uk. 92).
   2. KITENZIJINA KINACHOJENGA, ambacho "kinahusiana kisarufi kwenye sentensi na vihusishi, viwakilishi milikishi, na uhusiano uliojengeka" (uk.91). J. Weingreen, *A Practical Grammar for Classical Hebrew*, anaelezea hali ya muundo:

      > "ikiwa maneno mawili (au zaidi) yanaunganikana kwa karibu ambapo kwa pamoja yanatengeneza wazo moja ambatani, neno lenye kujitegemea (au maneno) yanasemekana kuwa katika hali ya muundo." (uk. 44).

F. VIWAKILISHI VYA KUULIZA
   1. Mara zote huonekana kwanza kwenye sentensi.
   2. Umuhimu wa kufasiri
      a. *ha-* haitarajia mwitikio
      b. *halo'*- mwandishi anategemea jibu la "ndiyo"

   KAULI HASI
   1. Mara nyingi hujitokeza kabla ya maneno yenyewe yanayo kanushwa.
   2. Neno mojawapo kanushi ni *lo'.*
   3. Neno *al* lina kidokezo dharura na hutumika likiwa na asili na ufafanuzi zaidi wa neno.
   4. Neno *lebhilti*, linamaanisha "ili kwamba……sio" linatumika likiwa na VITENZIJINA.
   5. Neno *'en* linatumika likiwa KAULI ENDELEVU.

G. SENTENSI ZENYE MASHARTI
   1. Kuna aina nne ya sentensi zenye masharti ambazo kimsingi zinafanana katika lugha ya Koine ya huko Ugiriki.
      a. Kitu Fulani kinaonekana kuwa kikitokea au mawazo kama yalivyotimilizwa (DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani)
      b. Kitu Fulani kinyume na ukweli ambacho utimilisho wake hauwezekani (DARAJA LA PILI)
      c. Kitu fulani ambacho kinawezekana au hata kuonekana kutokea(DARAJA LA TATU)
      d. Kitu fulani ambacho ni yumkini kutokea, kwa hiyo utimilisho ni agharabu(DARAJA LA NNE)
   2. ALAMA ZA VISARUFI
      a. Vinafikiliwa kuwa kweli au hali iliyopo inatumia KAULI TIMILIFU ELEKEZI au KAULI ENDELEVU na mara zote kishazi kidogo kinatambulishwa kwa
         1) *'im*
         2) *Ki*
         3) *hin* au *hinneh*
      b. muundu ulio kinyume na ukweli mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU kikiwa na utangulizi wa KIAMBATA *lu* au *lule*
      c. zaidi muundo wenye uyumkini mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU katika kishazi kidogo, mara zote *'im* au *ki* vinatumika kama kauli ya mwanzo ENDELEVU
      d. Yumkini muundo mdogo hutumia KAULI TEGEMEZI ISIOTIMILIFU katika kishazi kidogo na mara zote *'im ni* utambulisho wa KAULI ENDELEVU.

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

| | |
|---|---|
| AB | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman |
| ABD | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman |
| AKOT | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens |
| ANET | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard |
| BDB A | Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs |
| IDB | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick |
| ISBE | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr |
| JB | Jerusalem Bible |
| JPSOA | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner |
| LAM | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa |
| LXX | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| MOF | A New Translation of the Bible by James Moffatt |
| MT | Masoretic Hebrew Text |
| NAB | New American Bible Text |
| NASB | New American Standard Bible |
| NEB | New English Bible |
| NET | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition |
| NRSV | New Revised Standard Bible |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren |
| NIV | New International Version |
| NJB | New Jerusalem Bible |
| OTPG | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith |
| REB | Revised English Bible |
| RSV | Revised Standard Version |
| SEPT | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| TEV | Today's English Version from United Bible Societies |
| YLT | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young |
| ZPBE | Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney |

# AGANO LA KALE KAMA HISTORIA

Ukristo na dini ya Kiyahudi ni imani za kihistoria. Imani zao zinasimama juu ya matukio ya kihistoria (yakiambatana na tafasiri zao). Tatizo linakuja pale inapojaribu kuelezea "historia" ni nini au "usomaji wa kihistoria." Matatizo mengi katika utafasiri wa thiolojia ya sasa unasimamia juu ya fasihi ya sasa au ubashiri wa kihistoria uliotarajiwa huko nyuma dhidi ya fasihi ya kibiblia ya kale huko Mashariki ya Karibu. Sio tu kutokuwepo kwa utambuzi mzuri wa tofauti za muda na kitamaduni, bali pia utofauti wa fasihi. Kama watu wa Magharibi ya sasa kwa uwazi hatuelewi uwasilishaji na mbinu za fasihi za maandiko ya kale ya Mashariki ya karibu,kwa hiyo tukayatafasiri kwa mwanga wa uwasilishaji wa kimagharibi. Mtizamo wa karne ya kumi na tisa kwenye usomaji wa kibiblia unarahisisha na kushusha thamani kitabu cha agano la kale kama historia, nyaraka zilizowekwa pamoja. Mashaka haya ya kihistoria yameathiri kanuni za ufasiri na uchunguzi wa kihistoria wa agano la kale. Tabia ya sasa dhidi ya "kanuni za ufasiri kuhusu sheria za kanisa" (Brevard Childs) imesaidia kuangazia juu ya muundo wa sasa wa andiko la agano la kale. Hili, kwa maoni yangu ni kiunganishi chenye msaada dhidi ya utupu wa lawama za Kijerumani za karne ya kumi na tisa. Lazima tushughulike na andiko la sheria za kanisa ambazo tumekwisha kupewa toka kwa taratibu za kihistoria zisizojulikana ambazo uvuvio wake ni wa kufikirika. Wengi wa wasomi wanarudia kwenye fikirio la historia yenyewe ya agano la kale. Hakika hii sio kumaanisha kukataa uhariri wa wazi na kulifanya kisasa agano la kale na wale waandishi wa baadaye wa Kiyahudi, lakini ni kurudi kwenye msingi wa agano la kale kama historia yenye kushawishi na uwekaji wa kumbukumbu za matukio ya kweli (ukiwa na uatafasiri wake wa kihistoria).

Nukuu toka kwa R. K Harrison in *The Expositor's Bible Commentary*, juzuu ya 1, katika makala, ya " shutuma za kihistoria na kubuni za agano la kale" ni za msaada:

> "usomaji wa uandishi wa historia linganishi umeonyesha kuwa, wale Waebrania wa kale walikuwa ni waweka kumbukumbu sahihi wa historia Mashariki ya Karibu waliohusika. Miundo muhimu ya usomaji wa vitabu kama vile Mwanzo na Kumbukumbu la Torati, yenye kuegemea juu ya aina maalum ya vidonge vilivyovumbulia kwenye maeneo yanayojumuisha Mari, Nuzi, na Boghazköy, imeonyesha kuwa mambo ya sheria za kidini zina vitu Fulani visivyofanana na fasihi katika tamaduni za huko Mashariki ya Karibu. Matokeo yake, inawezekana kuyaangalia katika kiwango cha kujiamini na kuheshimu wale wote katika tamaduni za mwanzo za Kiebrania walidai kuwa wana historia kiasili" (uk.232).

Hasa ninashukuru kwa kazi ya R.K Harrison kwa sababu anaifanya kama kipaumbele cha kutafasiri agano la kale katika mwanga wa matukio ya sasa, tamaduni na uwasilishaji.

Katika madarasa yangu mimi juu ya fasihi ya mwanzo ya Kiyahudi (Mwanzo – Kumbukumbu la Torati na Yoshua), najaribu kuanzisha uhusiano wa kuaminika na fasihi zingine za kale za huko Mashariki ya Karibu na watengenezaji wengine wa makala:

A. Fasihi ya kitabu cha Mwanzo inafanana na ile ya Mashariki ya karibu ya kale
   1. Fasihi ya mwanzo iliyojulikana inayofanana na muundo wa kitamaduni wa Mwanzo 1-11 ni kikabari cha vigae vya chungu vya Ebla toka Kaskazini mwa Shamu iliyoandikwa yapata miaka 2500 K.K, ikiandikwa katika lugha ya Akkadi.
   2. Uumbaji
      a. Habari za karibu sana za Mesopotamia zinazoshughulika na uumbaji, *Enuma Elish*, zilizoandikwa toka mwaka 1900-1700 K.K, zilipatikana kwenye maktaba ya Ashurbanipal huko Nineva na sehemu zingine. Kuna vikabari vya vigae vilivyoandikwa kwa lugha ya Akkadi vyenye kuelezea uumbaji wa Marduk.
         1) Miungu, *Apsu* (maji baridi-jinsi ya kiume) na *Tiamat* (maji chumvi-jinsi ya kike) ilikuwa na watoto watukutu, wenye kelele. Miungu hii miwili ilijaribu kuinyamazisha ile miungu midogo.
         2) Mmoja wa watoto wa mungu, *Marduk*, alisaidia kumwangusha mungu *Tiamat*. Aliumba dunia toka kwenye mwili wake.

3) *Marduk* alimuumba mwanadamu toka kwa mungu mwingine aliyemshinda, *Kingu*, ambaye alikuwa mume wa mungu *Tiamat* baada ya kufariki kwa mungu *Apsu*. Mwanadamu alitokana na damu ya mungu *Kingu*.
4) *Marduk* alifanywa kuwa mkuu wa mahekalu yote ya Kibabeli

b. "muhuri wa uumbaji" ni kikabari cha kigae ambacho kilikuwa na alama ya mwanaume na mwanamke wakiwa uchi pembeni yake kukiwa na mti wa matunda wenye nyoka akiwa amezunguka shina la mti na kujielekeza kwenye bega la mwanamke kama vile wanazungumza.

3. Uumbaji na gharika- *The Atrahasis Epic* inaweka kumbukumbu ya uasi wa miungu wadogo kwa sababu ya kufanya zaidi na uumbaji wa wenza saba wa kibinadamu kutenda kazi za hawa miungu wadogo. Kwa sababu ya (1) ongezeko la watu na (2) kelele, wanadamu wlipunguzwa kwa idadi yao kutokana na mapigo, njaa mara mbili na baadaye gharika, yakipangwa na mungu *Enlil*. Haya matukio makubwa yanaonekana katika utaratibu ule ule wa Mwanzo 1-8. Hiki kikabari ambatani kinaandika kuhusu muda ule ule kama *Enuma Elish* na *Gilgamesh Epic*, yapata 1900-1700 K.K. Yote yapo katika lugha ya Akkadi.
4. Gharika la Nuhu
   a. Kigae cha Kisummeri toka Nippur, kilichoitwa *Eridu Genesis*, kilichoandikwa toka mwaka 1600 K.K., kinazungumza kuhusu *Zivsudra* na kuja kwa gharika.
      1) *Enka*, mungu wa majini, akaonya kuhusu kuja kwa gharika
      2) *Zivsudra*, kuhani mkuu, aliokolewa kwenye merikebu kubwa
      3) Gharika ilidumu siku saba
      4) *Zivsudra* alifungua dirisha la merikebu na kuwaachia ndege wengi kuona kama ardhi imekauka
      5) Pia alitoa dhabihu ya dume la ng'ombe na kondoo alipotoka nje ya merikebu.
   b. Habari ambatani za gharika la Babeli toka kwenye hadithi nne za Wasummeri, zilizojulikana kama *Gilgamesh Epic*, mwanzoni ziliandikwa toka mwaka 2500-2400 K.K., ingawa muundo ambatani ulioandikwa ulikuwa ni wa kikabari cha Akkadi, ni wa zamani za kale. Unatuambia kuhusu wale waliookoka kwenye gharika, *Utnapishtim*, anayetuambia kuhusu *Gilgamesh*, mfalme wa *Uruk* namna alivyookoka kwenye gharika kubwa na kupewa maisha ya milele.
      1) *Ea*, mungu wa majini, anaonya kuhusu kuja kwa gharika na anazungumza juu ya *Utnapishtim* (muundo wa Kibabeli wa *Zivsudra*) alitengeneza merikebu
      2) *Utnapishtim* na familia yake, pamoja na miti ya uponyaji iliyochaguliwa, waliokoka kwenye gharika
      3) Gharika ilidumu kwa muda wa siku saba
      4) Merikebu ikaja kutuama huko Kaskazini Mashariki wa Uajemi, kwenye Mlima Nisir
      5) Aliwatuma ndege watatu tofauti kuona kama ardhi ilikuwa imekauka
5. Fasihi ya Mesopotamia ambayo inaelezea kuhusu gharika iliyotokea huko nyuma inaelezea kutoka katika chanzo kile kile. Mara zote majina hutofautiana, lakini eneo ni lile lile. Mfano ni kuwa *Zivsudra*, *Atrahasis*, na *Utnapishtim* wote ni wafalme wa mwanadamu.
6. Ufanano wa kihistoria kwenye matukio ya mwanzo ya kitabu cha Mwanzo yanaweza kuelezewa katika mwonekano wa maarifa na uzoefu wa Mungu wa kuwatawanyisha wanadamu hapo mwanzo. Hivi vitovu vya kumbukumbu vya kweli vya kihistoria vimekwisha elezewa na kubuniwa ndani ya habari za gharika za sasa zinazofahamika pote duniani. Kile kile pia kinaweza kusemwa juu ya: uumbaji (Mwanzo 1-2) na muunganiko wa mwanadamu na malaika (Mwanzo 6).
7. Siku ya wakuu wa kaya (zama za shaba)
   a. Vigae vya Mali- kikabari cha kisheria (tamaduni za Amoni) na maandiko binafsi yaliyoandikwa katika lugha ya Akkadia yapata miaka ya 1700 K.K.
   b. Vigae vya Nuzi – vikabari vya kumbukumbu za familia fulani (tamaduni za Hori au Huri) zilizoandikwa kwa lugha ya Akkadi yapata maili 100 Kusini Mashariki mwa Nineva mwaka wa 1500-1300 K.K. Waliweka kumbukumbu za utaratibu wa familia na biashara. Kwa ajili ya mifano zaidi, angalia Walton, kurusa za 52-58.
   c. Vigae vya Alalak – vikabari vya maandiko toka Kaskazini mwa Shamu yapata mwaka wa 2000 K.K.

d. Baadhi ya majina yaliyopatikana katika kitabu cha Mwanzo yametajwa kama majina ya mahali katika vigae vya Mari: Serugi, Pelegi, Tera, Nahori. Majina mengine ya kibiblia ambayo pia yalijulikana ni : Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Labani, na Yusufu.

8. "uchunguzi wa kihistoria wa pamoja umeonyesha kuwa, pamoja na Wahiti, Waebrania wa kale walikuwa sahihi zaidi, muhimu na wenye kuhusika kuweka kumbukumbu za historia ya Mashariki ya Karibu," R. K Harrison in *Biblical Criticism*, uk. 5.
9. Mwanaakiolojia amethibitisha kuwa wa msaada katika kuimarisha historia ya Biblia. hata hivyo, neno la tahadhari ni la muhimu. Elimu-kale sio hasa ya mwongozo sana wa kuaminika kwa:
   a. Mbinu dhaifu za uchimbuaji ule wa mwanzo ,
   b. Tafasiri nyingi zenye upendeleo wa makala yaliyogunduliwa,
   c. Hakuna makubaliano juu ya utaratibu wa kupanga matukio ya huko Mashariki ya karibu ya kale.

B. Habari za uumbaji wa ki-Misri waweza kupatikana katika John W. Walton's, *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*. Grand Rapids, MI: Zondervan, 1990. kur. 23-34, 32-34.
1. Katika fasihi ya ki-Misri uumbaji ulianza na maji yasiyo na umbo, yaliyochafuka. Uumbaji ulionekana kama umbo linaloanza nje ya maji yaliyochafuka.
2. Katika fasihi ya ki-Misri toka kwa Memphis, uumbaji ulitokea kwa neno lililotamkwa na Ptah.

C. Fasihi ya Yoshua inafanana na ile toka Mashariki ya Karibu ya mbali
1. Elimu-kale imeonyesha kuwa kati ya miji mingi ya Kaanani iliyokuwa imezungushiwa kuta iliangamizwa na kwa haraka ikajengwa tena yapata miaka ya 1250 K.K.
   a. Hazori
   b. Lachish
   c. Bethell
   d. Debiri (mwanzoni uliitwa Kerioth Sepher, 15:15)
2. Wanaakiolojia wameshindwa kuthibitisha au kukataahabari za kibiblia juu ya kuanguka kwa Yeriko (kama vile Yoshua 6). Kwa sababu ya kile kinachoonekana kuwa sehemu yenyewe iko katika hali ya umasikini:
   a. Kwa ajili ya hali ya hewa/sehemu yenyewe
   b. Majengo ya kizamani kwenye miji ya kizamani wakitumia vifaa vya kizamani.
   c. Haijulikani tarehe za uwepo wa matabaka
3. Wanaakiolojia wamepata madhabahu juu ya Mlima Ebal ambayo huenda inahusiana na Yoshua 8:30-31 (kumb. 27:2-9). Yanafanana na maelezo yaliyopatikana huko Mishna (Talmud)
4. Maandiko ya Ras Shamra yaliyopatikana huko Ugariti yanaonyesha maisha ya Wakaanani na dini zao mwaka wa 1400 K.K:
   a. Asili za ibada ya miungu wengi (kushamiri kwa madhehebu)
   b. *El* alikuwa mungu wao mkuu
   c. Mwenza wa *El* alikuwa Asherah (baadaye akawa mwenza wa Ba'al) ambaye alikuwa akiabudiwa kwa muundo wa mti ulio hai ambao ulimaanisha "mti wa uzima"
   d. Watoto wao walikuwa Ba'al (Haddad), mungu wa kimbunga
   e. Ba'al akaja kuwa "mungu mkuu"wa hekalu la Wakaanani. Anat alikuwa mwenza wake.
   f. Sherehe zao zilifanana na Isis na Osiris wa Misri
   g. Ibada ya Ba'al ilikuwa inaangazia juu ya "sehemu zilizoinuka" za mahali au majukwaa ya mawe (ibada za kikahaba)
   h. Ba'al alikuwa akiashiriwa na nguzo yam awe iliyoinuka (sura ya dhakari)
5. Uhakika wa majina yaliyoorodheshwa ya miji ya kale yanaendana na wandishi wa kisasa, na sio wahariri wa zamani:
   a. Jerusalem iliitwa Jebus, Yoshua 15:8; 18:16,28

b. Hebron iliitwa Kiriath-arba, Yoshua 14:15; 15:13,54; 20:7; 21:11
c. Kiriath-jearim inaitwa Baalah, Yoshua 15:9,10
d. Sidoni inarejelewa kama mji maarufu wa Foenike, na sio Tiro, Yoshua 11:8; 13:6; 19:28, ambao baadaye ukajakuwa mji mkuu.

# UANDISHI WA HISTORIA YA AGANO LA KALE UKILINGANISHA NA TAMADUNI ZA KISASA ZA MASHARIKI YA KARIBU

**VYANZO VYA MESOPOTAMIA**

1. Kama fasihi nyingi za kale dhima mara nyingi huwa ndiye mfalme baadhi ya mashujaa wa kitaifa.
2. Matukio mara nyingi ndiyo yalielezewa zaidi kwa kusudi la kipropaganda.
3. Mara nyingi hakuna maswala yeyote ya kinyume yaliyowekwa kwenye kumbukumbu
4. Kusudi ilikuwa ni kusaidia hali ya sasa ya taasisi au kuelezea kuinuka kwa mfumo wa utawala.
5. Kubadilika kwa historia kunaambatana na
   a. Kukuzwa kwa madai ya ushindi mkuu
   b. Mafanikio ya mwanzo ukilinganisha na mafanikio ya sasa
   c. Dhana chanya tu zilizowekwa kwenye kumbukumbu
6. Fasihi iliokoa sio tu kazi ya propaganda, lakini pia ilikuwa ni kazi ya kuelimisha

**VYANZO VYA KI-MISRI**

1. Waliunga mkono mtazamo wa maisha yaliyotuama, ambayo yalikuwa hayaathiriwi na muda.
2. Mfalme na familia yake ndio kusudi zima la sehemu kubwa ya fasihi.
3. Kama ilivyokuwa fasihi ya Mesopotamia, ina propaganda nyingi,
   a. Hakuna mtizamo hasi
   b. Mtzamo uliostawi

**VYANZO VYA SHERIA ZA KIYAHUDI**

1. Jaribio la kufanya maandiko kuwa muhimu na Midrash, ambaye anatoka nje ya imani ya kwenda kwenye andiko na haiangazii juu ya kusudi la kiuandishi wala muundo kihistoria wa neno
   a. *Halakha* anashughulika na kweli au sheria kwa ajili ya maisha
   b. *Haggada* anashughulika na maombi na utiaji moyo kwa ajili ya maisha
2. Pesher –maendeleo ya baadaye yaliyoonekana katika magombo ya bahari ya chumvi. Inatumika kama mtizamo wa uainishaji ili kuona utimilifu wa kinabii wa matukio yaliyopita katika muundo wa sasa. Muundo wa sasa ulikuwa ni matukio ya siku ya mwisho yaliyotabiriwa (kuja kwa zama mpya)

Ni dhahiri kuwa uwasilishaji wa fasihi ya Mashariki ya kale na baadaye fasihi ya Kiyahudi ni wa tofauti katika maandiko ya Agano la Kale. Kwa namna nyingi uwasilishaji wa Agano la Kale, ingawa mara nyingi zinashirikishana tabia za fasihi ya kisasa, lakini wa kipekee, hasa katika kuyatafasiri matukio ya kihistoria. Ule ulioko karibu sana na historia ya Kiebrania ni fasihi ya Wahiti. Lazima ikubarike ni kwa namna gani historia ya kale inatokana nah ii ya sasa, historia ya kimagharibi. Ndani ya haya kuna tatizo kwa ajili ya utafasiri. Wana historia wa kisasa wanajaribu kuwa na malengo (sio watu wa propaganda, kama hili linawezekana) na kuyaandika na kuweka kumbukumbu katika mtiririko wa kimatukio kwa kile “kilichotokea!” inajaribu kuandika “sababu na athari” za matukio ya kihistoria. Inaanishwa na maelezo! Kwa sababu tu historia ya Mashariki ya Karibu sio kama historia ya sasa isivyofanya kuwa ya kupotosha, ya hali ya chini, isioaminika. Historia ya Magharibi ya sasa inaaksi upendeleo (dhahanio) wa waandishi. Historia ya kibiblia kiasili yenyewe ni ya kitofauti. Kuna namna ambavyo historia ya Biblia inaonekana machoni pa imani ya mwandishi aliyevuviwa na kwa ajili ya thiolojia, lakini bado inakuwa habari ya historia inayokubalika. Huu ujuaji wa historia wa agano la kale ni wa muhimu kwangu kama njia ya kutetea imani yangu kwa wengine. Kama biblia inaweza kuonyeshwa kuwa kama historia hivyo madai yake ya imani yana rufaa ya nguvu kwa wasio amini. Imani yangu haikai juu ya uthibitisho wa kihistoria wa elimu-kale na elimu ya binadamu, lakini hili linasaidia kuupenyeza ujumbe wa Biblia, na kusababisha kuaminika vinginevyo isingalikuwa nao. Kuweka kwenye muhtasari, uhalisia wa historia hautendi kazi katika eneo la uvuvio, bali katika eneo la uinjilisti na utetezi.

# UWASILISHAJI NA UFASIRI:
# SIMULIZI ZA AGANO LA KALE

I. Maelezo ya ufunguzi
   A. Uhusiano kati ya Agano la Kale na njia nyingine za kuandika matukio
      1. Fasihi nyingine za Mashariki ya Karibu ni za kubuniwa
         a. Waabudu miungu wengi (mara nyingi miungu ya kibinadamu inaaksi nguvu ya asili inayotumia mawazo ya kimigongano kati ya mtu binafsi)
         b. Ikiegemea juu ya mizunguko ya asili (kufa na kufufuka kwa miungu)
      2. Utawala wa Wagiriki-Warumi ulikuwa ni kwa ajili ya kufurahisha na kutia moyo kuliko kuweka kumbukumbu za matukio ya kihistoria kwa yenyewe (wakazi wa mahali kwa namna mbali mbali waliaksi mawazo ya Mesopotamia)
   B. Yumkini utumiaji wa maneno matatu ya Kijerumani yanaelezea kwa mifano tofauti katika aina au maelezo ya historia
      1. "Historie," uwekaji kumbukumbu wa matukio (ukweli halisi)
      2. "Geschichte," utafasiri wa matukio ukionyesha umuhimu wake kwa mwanadamu
      3. "Heilsgeschichte" inarejelea kipekee kwenye mpango wa ukombozi wa Mungu na shughuli ndani ya mchakato wa kihistoria
   C. Simulizi za agano jipya na agano la kale ni "Geschichte" ambazo zinatuongoza kwenda kwenye uelewa wa Heilgeschichte. Wanachagua matukio ya kihistoria ya thiolojia
      1. Chaguzi za matukio tu
      2. Utaratibu wa kupanga matukio sio wa muhimu kama wa thiolojia
      3. Matukio ya kushirikishana kudhihirisha ukweli
   D. Simulizi kwa kiasi kikubwa ni uwasilishaji uliozoeleka katika Agano la Kale. Imekadiriwa kuwa 40% ya Agano la Kale ni simulizi. Kwa hiyo, huu uwasilishaji ni wa msingi katika Roho katika kuwasiliana na ujumbe wa Mungu na tabia kwa mwanadmu aliyeanguka. Lakini, imekwisha tendeka, lakini si kwa ulinganifu (kama waraka wa Agano Jipya), lakini kwa matokeo yake, ujumla wake au mdahalo ulio chaguliwa. Mtu lazima aendelee kuuliza kwa nini hili limewekwa kwenye kumbukumbu. Ni kipi kinajaribu kusisitizwa? Ni lipi kusudi la kithiolojia? Hili kwa namna yeyote halimaanishi kushusha thamani ya historia. Lakini, ni historia kama mtumishi na njia ya ufunuo.

II. Simulizi za kibiblia
   A. Mungu ni mtendaji katika ulimwengu wake. Wandishi wa Biblia waliovuviwa wanachagua matukio fulani kumthihirisha Mungu. Mungu ni muhusika mkuu wa agano la kale.
   B. Kila simulizi zinatenda katika njia tofauti:
      1. Mungu ni nani na nini anakifanya katika ulimwengu huu
      2. Mwanadamu anadhihirishwa kupitia Mungu kushughulika na mtu mmoja mmoja na utambulisho wa utaifa
      3. Kama mfano hasa akiangalia ushindi wa Yoshua kijeshi uliohusianishwa kwenye utendaji wa agano (kama vile 1:7-8; 8:30-35).
   C. Mara nyingi simulizi huwekwa pamoja ili kutengeneza sehemu kubwa ya fasihi ambayo inadhihirisha kweli moja ya kithiolojia.

III. Kanuni za ufasiri kuhusu simulizi za Agano la Kale
   A. Majadiliano mazuri niliyo yawahi kuyaona kuhusu utafasiri wa simulizi za Agano la Kale ni wa Douglas Stuart in *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. za 83-84.
      1. Kuwa mara zote simulizi za Agano la Kale hazifundishi moja kwa moja kanuni/imani.
      2. Kuwa mara zote simulizi za Agano la Kale zinaelezea kanuni/imani au imani iliyofundishwa sawasawa na imani zingine sehemu yeyote ile.

3. Simulizi zinaweka kumbukumbu kile kilichotokea—sio muhimu kile ambacho kingetokea au kile kinachoweza kutokea kila wakati. Kwa hiyo, sio kila simulizi ina habari adilifu ya kipekee inayoweza kujulikana.
4. Kile watu wanachokifanya katika simulizi sio kwa umuhimu wake mfano mzuri kwetu sisi. Mara zote, huwa kinyume.
5. Kwa kiasi kikubwa wahusika wakuu katika simulizi za Agano la Kale wako mbali na kile kinachotakiwa, pia na matendo yao.
6. Mara zote hatuambiwi mwisho wa simulizi ikiwa kile kilichotendeka kilikuwa kizuri au kibaya. Tunatarajia kuweza kuamua kuwa juu ya msingi wa kile Mungu ametufundisha moja kwa moja na kwa usahihi popote pale katika maandiko.
7. Simulizi zote ni za kiubaguzi na zisizo kamili. Sio kwamba maelezo yote muhimu mara zote hutolewa (kama vile Yohana 21:25). Kile kinafanyika kwenye simulizi ni kila kitu kile mwandishi anakiona kuwa ni muhimu kwetu kukijua.
8. Simulizi hazikuandikwa kujibu maswali yote yale tuliyonayo ya kithiolojia. Zina makusudi maalum, yasiyo kamili na hushughulika na mambo fulani, zikiacha mengine kushughulikiwa mahali pengine, kwa namna nyingine.
9. Simulizi zinaweza kufundishwa kwa uwazi (kwa kuelezea kitu fulani kwa uwazi) au pasipo uwazi (kwa kudokeza kitu fulani pasipo maelezo).
10. Katika hatua ya mwisho ya utafiti, Mungu anabaki kuwa ndiye shujaa wa simulizi za Kibiblia

B. Mjadala mwingine mzuri wa utafasili wa simulizi ni wa Walter Kaiser's *Toward Exegetical Theology*:

> "dhana pekee ya sehemu ya simulizi ya maandiko ni kuwa mwandishi mara zote anaruhusu maneno na vitendo vya watu katika simulizi zake kuelezea ile nguvu ya ujmbe wake. Hivyo, badala ya kutuelezea sisi kupitia maelezo ya moja kwa moja, kama yale yanayopatikana katika kanuni au sehemu ya mafundisho ya maandiko, mwandishi anajaribu kubaki kwa namna Fulani katika mazingira ya nyuma kama vile mafundisho ya moja kwa moja au tathimini ya maelezo inavyohusika. Kwa matokeo hayo, inakuja kuwa muhimu sana kutambua muktadha mpana mahali pale simulizi inafaa na kuuliza ni kwa nini mwandishi alitumia uchaguzi wa matukio Fulani katika mtiririko mzuri vile alivyo uweka. Uwili unaodokeza kwenye maana sasa utakuwa ni mpangilio wa matukio na uchaguzi wa maelezo toka kwenye mkanganyiko wa hotuba, watu, au matukio. Kingin zaidi, mrejeo wa ki-Ungu na tathimini ya watu hawa na matukio lazima mara zote yaamuliwe kutokana na namna mwandishi anaruhusu mtu au kikundi cha watu kuitikia kwenye kilele cha uataratibu wa matukio uliochaguliwa; ndio kusema kama hakuingilia simulizi kutoa tathimini yake ya kile kilichotokea" (uk. 205)

C. Katika simulizi ukweli hupatikana katika sehemu ya fasihi yote na sio kwenye maelezo. Kuwa mwangalifu kwenye uhakiki wa maandiko au utumiaji wa simulizi za Agano la Kale kama mwongozo wa maisha yako.

VI. Hatua mbili za utafasili

A. Ukombozi wa YHWH, matendo ya kimafunuo kwa ajili ya uzao wa Abraham
B. Mapenzi ya YHWH kwa kila maisha ya muumini (kwa kila lika)
C. Mtazamo wa kwanza juu ya "kumjua Mungu" (wokovu); wa pili juu ya kumtumikia Yeye (maisha ya Mkristo ya imani, kama vile Rum. 15:4; I Kor. 10:6,11)

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la ($UBS^4$). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
Juni 27, 1996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## I. DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa "uhakiki wa andiko"
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama "mwitikio wa msomaji" (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa vitu nyote lazima kweli hivi vitatu vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji"  (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

   Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuataao:

### 1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira

d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    1) Agano la kale
        a) Simulizi za waebrania
        b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
        c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
        d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
        a) Simulizi (Injili, matendo)
        b) Hadithi za mafumbo (Injili)
        c) Barua/nyaraka
        d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mzunguko pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mzunguko wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
    1) Mwandishi
    2) Tarehe
    3) Wapokeaji
    4) Kusudu mahsusi la uandishi
    5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
    6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mzunguko wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
    1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
    3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo
        c) Itifaki
    2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na

uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.

3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kile kile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
   1) Soma biblia
   2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
   3) Tangulizi za biblia
   4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18

"Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."

2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi
   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni

    c. Habari za kisarufi
    d. Usomaji wa neno
    e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
    a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
    b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
    c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
    d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
    a. Tofauti za mswada
    b. Maana ya maneno mbadala
    c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
    d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

## UTANGULIZI WA MWANZO 11:24-13:18

A. Hii sehemu ya kitabu cha Mwanzo inaanza na maelezo kamili ya uzao wa Kimasihi kupitia Ibrahamu.
B. Sura ya Hamsini ya kitabu cha Mwanzo inahusiana na ukombozi wa watu wa Mungu wa agano, na sio uumbaji. Kumwita mtu mmoja kwa ajili ya kuwaita wote ndio mtazamo wa kitabu .
C. Abramu anaonekana katika udhaifu huu vile vile pia katika uaminifu wake. Mungu wa uchaguzi na rehema akamwita toka kwenye kusudio lake la ukombozi.
D. Mungu akamchagua Ibrahamu kuuchagua ulimwengu (kama vile 12:3c; Kut. 19:4-6; II Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Mungu anahitaji watu wote aliowaumba kwa sura yake waweze kukombolewa(kama vile Mwa. 3:15; Ezek. 18:23,32; I Tim. 2:4; II Pet. 3:9)
E. Buku la sheria za Kiyahudi linaelezea juu ya Baraka saba za wito:
    1. Abramu angalikuwa baba wa mataifa yote.
    2. Angelibarikiwa katika maisha yake yote.
    3. Jina lake lingalijulikana vizazi hadi vizazi.
    4. Angalikuwa ni Baraka kwa wengine.
    5. Wangalibarikiwa wengine wanaomheshimu.
    6. Wengine wangelilaaniwa wanao mkataa.
    7. Mamlaka yake yangelikuwa ya kiulimwengu

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:24-25**
**[24]Nahori akaishi miaka ishirini na kenda, akamzaa Tera. [25]Nahori akaishi baada ya kumzaa Tera miaka mia na kumi na kenda, akazaa wana, waume na wake.**

**11:24 "Tera"** "Tera" yumkini linamaanisha "lami," "kuchelewa," au "kuhamahama" (BDB 1076). Tokana na Yosh. 24:2 ni dhahiri kuwa Yeye na familia yake walikuwa ni watu wa kuabudu miungu wengi. Jina la familia yake kimsingi linapendekeza kuwa waliabudu mungu wa mwezi aitwae *Zir*. Huyu mungu aliabudiwa huko Uru, Tema na Harani. Ingawa, Mwanzo 31:53 inadokeza kuwa alimfahamu YHWH.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:26**
**[26] Tera akaishi miaka sabini, akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani.**

**11:26 "Abramu, Nahori and Harani"** Huu waweza kuwa ni utaratibu uliowekwa na sio umri. Jina la Abramu laweza kumaanisha (1) "baba aliyeinuliwa"; (2) "yeye amwinuaye baba"; au (3) "pekee aliyeinuliwa ni baba yangu" (BDB 4). Jina la Nahori linamaanisha "kupwita" au jina mojawapo la sehemu huko Ashuru (BDB 637), wakati Harani linamaanisha "mpanda milima" (BDB 248).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:27-30**
**[27]Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu. [28]Harani akafa kabla ya baba yake Tera katika nchi aliyozaliwa, yaani, katika Uru wa Wakaldayo. [29] Abramu na Nahori wakajitwalia wake. Jina la mkewe Abramu aliitwa Sarai, na jina la mkewe Nahori aliitwa Milka, binti Harani, ambaye alikuwa baba wa Milka na wa Iska. [30]Na Sarai alikuwa tasa, hakuwa na mtoto.**

**11:27 "Lutu"** Angalia BDB 532 II.

**11:28 "Harani akafa kabla ya baba yake"** Hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya Harani akifa kabla ya baba yake.

◙ **"Uru wa Wakaldayo"** Utamaduni wa Wakaldayo ulistawi (yaani. Ulijengwa juu ya nguvu za tamaduni za Kisummeri)na kustawi baada ya siku za Abramu (BDB 505).

**11:29 "Sarai"** Angalia BDB 979.

◙ **"Milka"** Angalia BDB 574.

◙ **"na Iska"** Mtu huyu (BDB 414) na sababu za uwepo wake katika mstari huu haijulikani. Walimu wa dini ya Kiyahudi (Yosefati, Jerome, na Augustine) wanasema ni Sarai, lakini andiko linadai kuwa walikuwa na baba tofauti.

**11:30 "Sara alikuwa tasa"** Kutokuweza kwa Sarai, Raheli, na Rebeka kupata watoto (BDB 785) ilikuwa ni njia mojawapo ya Mungu kuonyesha uwezo na udhibiti wa historia ya mwanadamu na uzao wake. Kizazi cha mwanadamu sio dhana muhimu kwenye uzao wa Kimasihi. Huu mtindo wa aina moja wa dhana ya thiolojia kwa historia ya Israel pia inaonekana katika ukweli kwamba mzaliwa wa kwanza hayuko katika uzao wa Kimasihi. Kitamaduni mzaliwa wa kwanza alipaswa kuwa mkuu wa ukoo, lakini sivyo kati ya watu wa YHWH. Ilikuwa ni uchaguzi wake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:31-32**
**[31]Tera akamtwaa Abramu mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkwewe, mke wa Abramu mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka Harani wakakaa huko. [32]Siku za Tera zilikuwa miaka mia mbili na mitano; Tera akafa katika Harani.**

**11:31 "wakatoka wote"** Kuna majadiliano mengi ikiwa Tera alichukua familia yake au ikiwa Abramu aliwachukua. Baadhi wanabashiri ni wito wa kwanza wa Mungu kwa Tera lakini alipoka na kurudi kwenye ibada ya sanamu. Inaonekana kwangu kuwa Ibrahamu ndio kitovu cha kipengere chote, na sio Tera. Kwa kuondoka kwake Uru Abramu alikuwa haachi tu familia yake, lakini pia miungu ya taifa lake. Aliacha maisha ya raha, yaliyo imarika kumfuata Mungu mpya ambaye aliongea naye kwa mtindo wa ajabu..

**11:32 "siku za Tera zilikuwa miaka 205"** Mtu akiongeza miaka ile ya Mwanzo 11:26 na ya Mwanzo 12:4 ambayo ni sawa na miaka 145 na kutoa hii kwenye miaka 205, inakuwa dhahiri kuwa Tera aliishi miaka 60 baada ya Abraham kuondoka Harani. Hili linaonekana kutofautiana na hotuba Stefano katika Mdo. 7:4. Mitazamo mbali mbali ya uchunguzi wa kihistoria wa Stefano unatofautiana na uelewa wetu wa leo wa historia ya agano la kale. Yumkini alikuwa akitumia njia ya utafasiri wa sheria za Kiyahudi. Wasomi wengine wanadai kuwa Abramu, ingawa ametajwa katika 11:26, alizaliwa muda kitambo na Stefano alikuwa sahihi. Inafurahisha kuwa torati ya Kisamaria ina "144" hapa

# MWANZO 12

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Ibrahimu anasafiri Kwenda Misri | Ahadi kwa Ibrahimu | wito wa Mungu kwa Ibrahimu | wito wa Mungu kwa Ibrahimu | wito wa Ibrahimu |
| 12:1-3 | 12:1-3 | 12:1-3 | 12:1-2 | 12:1-3 |
| (1-3) | (1-3) | | (1-2) | (1-3) |
| | | | (3) | |
| 12:4-9 | 12:4-9 | 12:4-9 | 12:4-5a | 12:4-5 |
| | | | 12:5b-9 | |
| | | | | 12:6-9 |
| | Ibrahimu akiwa Misri | Sara katika tatizo | Ibrahimu akiwa Misri | Ibrahimu akiwa Misri |
| | | (12:10-13:1) | | |
| 12:10-16 | 12:10-13 | 12:10-16 | 12:10-16 | 12:10-20 |
| | 12:14-20 | | | |
| 12:17-20 | | 12:17-13:1 | 12:17-20 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:1-3**

**1 Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; 2 nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; 3 nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.**

**12:1-3** Mara kwa mara ni ngumu kuelezea tofauti kati ya ushairi wa Kiebrania na tamthiliya "iliyokuzwa". Tazama namna gani fasiri za kingereza, angalia aina ya fasihi katika mistari tofauti.

| | NASB/NKJV | JPSOA | NRSV | TEV/NJB/REB/NIV |
|---|---|---|---|---|
| Ushairi | 1b -3 | 1 | | 3 |
| Lugha ya mjazo | 1a | 2 - 3 | 1-3 | 1-2 |

Inavyoonekana, hakuna alama za kimuktadha, ni maoni tu ya kamati za ufasiri. Mistari hii inarudiwa katika sura zinazofuata kukiwa na marekebisho na maelezo kidogo yenye utofauti, lakini muktadha huu ni mwanzo mkubwa wa ahadi ya Mungu inayotumiwa na Paulo katika Warumi 4 (yaani Mwanzo 15:6). YHWH atatenda kupitia Ibrahimu na uzao wake kujifunua yeye mwenyewe kwa ulimwengu wote. Agano (Angalia Mada Maalum katika 13:15) inakuwa dhana ya ufunguo ya Biblia. Mungu mwenye nguvu anaanzisha na kuweka ajenda, lakini ameweka mamlaka kwamba wanadamu lazima watoe mrejesho ulio sahihi na wenye mwendelezo!

**12:1 "Sasa"** "Sasa" na "alikuwa amesema" vyote vimewekwa katika mstari huu na mfasiri anayeamini kwamba mistari hii inarejerea wito wa Mungu wa awali katika Uru (kama vile Mwanzo 15:7; Neh. 9:7; Mdo. 7:2).

◙**"BWANA"** Hili ni YHWH, jina la agano la Mungu (kama vile Kut. 3:14). Tazama wito huu umejikita katika ukaribisho wa neema, sio hali ya kustahili ya Ibrahimu (kama vile mistari ya 10 na kuendelea). Mungu siku zote ndiye anayeanzisha (kama vile Yohana 6:44,65; Efe.2:8-9)

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El* (BDB 42, KB 48)
   1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra)
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe"), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
      d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
      e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), Waamuzi 9:46
   4. *El* inalinganishwa na
      a. YHWH katika Zaburi. 85:8; Isa. 42:5
      b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
      c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
      d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
      e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31; "mwaminifu" katika Kumb. 7:9; 32:4
      f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
      g. "maarifa" katika I Sam. 2:3
      h. "kimbilio langu" katika II Sam. 22:33
      i. "mlipa kisasi wangu" katika II Sam. 22:48
      j. "mtakatifu" katika Isa. 5:16
      k. "muweza" katika Isa. 10:21
      l. "wokovu wangu" katika Isa. 12:2
      m. "mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
      n. "anayepatiliza: katika Yer. 51:56
   5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)
  1. Maana yake ya msingi "juu," "aliyetukuzwa," au "kuinuliwa" (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
     18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
  2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
     a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
     b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
     c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
     d. *El* - Hes. 24:16
     e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya "Mungu aliye Juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
  3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
     a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
     b. Balaamu, Hes. 24:16
     c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
     d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (WINGI), *Eloah* (UMOJA), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
  1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
  2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
  3. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
  4. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*elohim*) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
  5. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
  6. Neno hili linapatikana katika vinywa vya wasiokuwa Waisraeli kama jina la Uungu.
     a. Melkizedeki, Mwanzo. 14:18-22
     b. Balaamu, Hes. 24:2
     c. Musa anapozungumzia mataifa, Kumb. 32:8
  7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
     a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
     b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.
     c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)
  1. Hili ni jina ambalo lianaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi,

mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo (1) Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili) na (2) Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu. Mwanzo 2:4 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.

2. Katika Mwanzo 4:26 it is said inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
    a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
    b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
    c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
    d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KISABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
    e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
    f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
    g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
    h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
        (1) *Yah* (mfano Hallelu - yah)
        (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
        (3) *Yo* (majina mfano Joeli)

3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.

4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
    a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa, BDB 217 & 906), Mwanzo. 22:14
    b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako, BDB 217 & 950, *Qal* KAULI ENDELEVU), Kutoka. 15:26
    c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu, BDB 217 & 651), Kutoka. 17:15
    d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye BDB 217 & 872, *Piel* KAULI ENDELEVU), Kut. 31:13
    e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
    f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi, BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
    g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu, BDB 217 & 944, *Qal* KAULI ENDELEVU), Zab. 23:1
    h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6

| |
|---|
| i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa, BDB 217 & 1027), Ezek. 48:35 |

◙**"Bwana akamwambia"** Hii kwa nguvu inamaanisha mazungumzo bayana ya mdomo, sio ufunuo kupitia ndoto au maono, ingawa hilo lazima libakie lenye kuwezekana. Mstari wa 7 unamaanisha uonekano wa kimwili unaofanana na 3:8-12; 4:9-15; 6:13-22; 8:15-19; 9:1-7,8-17.

◙**"Abramu"** Katika uwezekano wa kimaana wa jina angalia kidokezo katika 11:26. Ibrahimu hachukuliwi kama mtu maalumu. Familia yake ni ya watu waaminio miungu wengi, yawezekana waabuduo mwezi wa kike au kiume. Tena hata hivyo kusema ukweli Ibrahimu sio mtiifu katika

1. kutoiacha familia yake
2. kuondoka Kanaani kuelekea Misri
3. kumshawishi mke wake kudanganya ili kwamba aweze kumuokoa maisha yake yeye (mara mbili)
4. kumdanganya Farao na Abimeleki ili kuokoa maisha yake

Hii inaonekana tu katika 22:15-18 imani yake inapopita kwa mg'ao, japokuwa inaelezewa katika 15:6.

◙**"Toka wewe katika nchi yako"** KITENZI (BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI) inamaanisha "kuondoka." Kidokezo cha ziada cha NASB kinaeleza kuwa inamaanisha "kuondoka kwa ajili yako mwenyewe." Ilidhaniwa kuhusiana na tungo zote tatu za mstari wa 1b,c,d. Ni nchi gani inayorejerewa, Uru au Harani? Tazama kwamba 11:31 inazungumzia Tera kuondoka Uru kwa ajili ya kuelekea Kanaani, lakini akiweka makazi yake Harani. Uru na Harani vyote vilikuwa vituo kwa ajili ya kuabudu mwezi na Tera na familia yake. Kwasababu ya maana inayodhaniwa ya majina yao (hatahivyo, maana ya jina la familia yake halijulikani), inawezekana kuwa ilijumuisha katika kuabudu mungu mwezi wa kiume/kike *Sin, Nana* (kama vile Josh. 24:2). Hii ndio maana alikuwa tayari kuhama.

Kwa Abramu kuiacha familia yake na ardhi ya uzao wake ingekuwa utambuzi wa wazi kwamba alikuwa tayari kuacha yote ikijumuisha madai yake ya urithi nyuma. Kujitenga huku na familia yake kunaweza kuwa kuliashiria kujitenga na miungu ya familia. Hii ndio sababu ya Tera na Lutu walikatazwa na Mungu kuambatana naye, kwa hivyo ilishangaza sana. Je lilikuwa ni tendo la kutotii wito wa YHWH au ilikuwa ni njia ya kutimiza ategemeo ya familia (yaani kutunza wazazi) na wakati huo huo kumtii YHWH? Kama kawaida aina ya uandishi ya fasihi ya "masimulizi ya kihistoria" (angalia viambatisho kadhaa vinavyofanana) havijibu kibayana aina za maswali kama haya. Mtu lazima aangalie masimulizi mazima na "kuunganisha nukta."

◙**"na jamaa zako"** Wito wa YHWH ulikuwa wa kimasharti kwa mwitikio wa Abramu. Abramu hakutimiza sehemu yake (Ondoka kutoka kwa jamaa zako na nyumba ya baba yako) kwa haraka. Utii ni muhimu (kama vile 18:19; 22:18).

◙**"na nyumba ya baba yako"** Mdo. 7:4 inasema kwamba Tera alikuwa Harani kabla Abramu hajaondoka, lakini ukiunganisha 11:26 na 12:4 na kuhusianisha hii na 11:32, inaonekana Tera aliishi miaka sitini baada ya Abramu kuondoka. Yawezekana 11:26 ndio ufunguo. Abramu inawezekana kuwa alikuwa ameorodheshwa kama mtoto wa kwanza si kwasababu ya umri, lakini kwasababu ya umuhimu wake wa kiutawala. Inaonekana majukumu ya kidesturi ya kifamilia aliyokuwa ametwishwa Abramu yalikuwa kikwazo kikubwa na kizuizi kwa wito wa Mungu.

◙**"uende mpaka nchi nitakayokuonyesha"** Kutoka 11:31 tunafahamu hii kuwa ni Kanaani. Kanaani inahaidiwa kwa

1. Ibrahimu – Mwanzo. 12:1; 15:18-21
2. Isaka – Mwanzo. 26:3-5
3. Yakobo – Mwanzo 28:13-15; 35:9-12

4. Israeli– Mwanzo 15:16; Kut. 6:4,8; Kumb. 4:38,40; 5:31; 19:10; 20:16; 21:23; Yosh. 1:2,3,6,11,13,15; 2:9,24; 18:3; 21:43; 24:13

Imani ya Abramu inaainishwa katika Ebr. 11:8. Ahadi hii ya ardhi ya nyumbani maalumu inakuwa shabaha ya Agano la Kale (yaani Israeli alipewa ardhi na YHWH).

**12:2 "nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa"** Neno kwa ajili ya Taifa (BDB 156) inamaanisha kupewa ardhi ya nyumbani. Pia inamaanisha uzao (yaani 22:17). Inaweza pia kumaanisha taifa jipya ambalo halikutajwa katika Mwanzo 10. Mstari wa 2 una kauli tatu za KITENZI AMRISHI juu ya matendo yaliyoahidiwa na YHWH.

1. "Nitakufanya kuwa taifa kubwa" – BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya KITENZI AMRISHI
2. "Nitakubariki" – BDB 138, KB 159 *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya KITENZI AMRISHI
3. "Nitalifanya jina lako kuwa kubwa" – BDB 152, KB 178, *Piel* KITENZI AMRISHI

Ahadi hii ya "uzao" itakuwa tumaini litakalo wekewa shabaha juu ya uzao/ kizazi kimoja maalumu, Masihi ambaye ataleta mataifa yote kwa YHWH. Ibrahimu ni tendo moja tu katika tamthiliya nzima ya ukombozi! Kithiolojia pia ni muhimu kwamba uumbaji wa asili (kama vile. 1:28; 9:1, 7), lakini dhambi imeathiri shauku ya YHWH. Sasa anaanza tena lakini na mtu mmoja, familia moja, taifa moja kulikuza katika watu waliokombolewa kutoka katika mataifa yote (Kugeuzwa kwa Mnara wa Babeli: wao pia walitaka "jina" kwa ajili yao wenyewe, 11:4).

Kifungu hiki cha habari ni vyote Baraka iliyohaidiwa na ahadi yenye masharti. Hatahivyo, shabaha ni juu ya Baraka asiyostahili (tendo la neema, 15:7-21; 28:13-15) linalofanywa na YHWH. Baraka/Ahadi hii ni ya kimasharti (kama vile mstari wa 1) juu ya utii (mfano ulio juu zaidi wa Mwanzo 22) na kutoka Mwanzo 15:5, imani. Inakuwa kielelezo cha namna gani ya kuhusiana na Mungu (kama vile Warumi 4; Wagalatia 3).

◙ **"kulikuza jina lako"** Walimu wanaona hili katika namna ya kutamkiwa Baraka kwa jina lake. Inamaanisha kwamba watu wote watamjua na kumuheshimu.

◙ **"nawe uwe baraka"** Hii ni *Qal* KAULI SHURUTISHI katikati ya VITENZI AMRISHI. "kufanyika baraka" inamaanisha kitendo upande wa Abramu. Baraka ya YHWH ilikuwa kumsaidia Abramu kuwa Baraka na kutoka mstari wa 3, Baraka ya kiujumla.

**12:3 "nitawabariki wakubarikio"** Baraka ya YHWH itakuja kupitia Baraka ya Abramu. YHWH anaamua kutenda lakini katika njia fulani.

VITENZI katika mstari 3 inatengeneza utaratibu.

1. YHWH anabariki – BDB 138, KB 159, *Piel* KITENZI AMRISHI
2. wale wanaombariki Abramu – BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI ENDELEVU
3. kuwabariki wale wanaomlaani Abramu – BDB 886, KB 1103, *Piel* KAULI ENDELEVU
4. YHWH anawalaani – BDB 886, KB 1103, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika namna ya KITENZI AMRISHI

◙**"naye akulaaniye nitamlaani"** Kuna maneno ya kiebrania mawili hapa kwa ajili ya "laana." La kwanza ni "kuzungumza mabaya juu ya" (BDB 886, KB 1103, kama vile. 8:21; 16:4,5; Kut. 21:17; 22:28; Law. 19:14; 20:9 [mara mbili]; 24:11,14,15,23; Kumb. 23:4) na ya pili ni laana ya kimahakama ya Mungu (BDB 76, KB 91, kama vile 3:14,17; 4:11; 5:29; 9:25; 27:29 [mara mbili]; 49:7; Kut. 22:28; Hes. 5:18,19,22,24 [mara mbili],27; 22:6 [mara mbili],12; 23:7; 24:9 [mara mbili]; Kumb. 27:15-26; 28:16-19). Wale wanaoenenda kinyume na Ibrahimu

wanajitenga wenyewe mbali na YHWH na wanafuatiwa na laana. YHWH anajifunua yeye mwenyewe kimsingi kupitia Ibrahimu na familia yake (tazama Melkizedeki, Ayubu, Yethro).

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV NRSV, Peshitta** | **"na katika wewe familia zote za nchi zitabarikiwa"** |
| **NRSV tanbihi, JPSOA** | **"kwa wewe familia zote za nchi zitajibarikia zenyewe"** |
| **TEV** | **"na kupitia wewe nitayabarikia mataifa yote"** |
| **TEV tanbihi** | **"mataifa yote yatakuja kwambgu ili niwabarikie kama nilivyowabarikia"** |
| **NJB** | **"na koo zote za nchi zitajibarikia zenyewe kupitia wewe"** |
| **LXX** | **"katika wewe makabila yote ya nchi yatabarikiwa"** |
| **REB** | **"watu wote wa nchi watatamani kubarikiwa kama nyie mlivyobarikiwa** |
| **REB tanbihi** | **"watu wote wa nchi watabarikiwa kwasababu yako"** |

Hii *Niphal* KAULI YA WAKATI ULIOTIMILIFU (BDB 138, KB 159) shina siku zote ni KAULI TENDWA (LXX, NASB, "utabarikiwa," kama vile 18:18; 28:14), lakini katika 22:18 na 26:4 the *Hithpael* shina la KAULI YA WAKATI TIMILIFU inatumika, ambayo ni ya KUJIREJEA ("kubarikiana"). Inawezekana kwamba *Hithpael* inaashiria kuendelea kwa kitendo kwa muda. Ni muhimu kwamba anajumuisha mataifa yote katika Ahadi yake kwa Abramu, ambayo ni muhimu katika ufahamu wa uasi wa jumla wa sura ya 11. Mungu alimchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote waliofanywa kwa sura yake (kama vile Zab. 22:27; 66:4; 86:9; Isa. 66:23; 49:6; Mdo. 3:25; Gal. 3:8)! Pia angalia kidokezo katika 22:18.

Hiki ni kifungu kikubwa kwa habari kweli kweli. Inaonesha kiuhalisia Mpango wa Mungu wa kumtumia Abramu kuufikia ulimwengu. Ahadi ya kiujumla ya Mwanzo 3:15 inafanyiwa kazi, hata katikati ya uasi uliokusudiwa wa watoto wa Nuhu (yaani Mwanzo 11). Si tu kwa wale wanaoonesha kibali kwa Abramu, bali wale watakaoonesha kibali kwa uzao wa Abramu (yaani masihi, kama vile. Gal. 3:16). Kulikuwa/kuna kusudi la jumla la uchaguzi wa YHWH juu ya mtu kuleta ukombozi uliotabiriwa kupitia umaalumu wa "mmoja" wa uzao wake. Katika taswira kubwa, haya sio maandiko kuhusu mtazamo juu ya wayahudi, lakini mwitikio wa imani kwa "Aliyehaidiwa" wa Kiyahudi.

## MADA MAALUM: UPENDELEO WA KIINJILISTI WA BOB

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Jer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walioumbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaoanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israeli. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahimu, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
   a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
   b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
   c. Mika 4:1-3
   d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihilishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya limejikita shabaha yake juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumaini utaendelea kuchukua muda kusoma Mada Maalum: Kwanini Ahadi za kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti sana na Ahadi za kiagano za Agano Jipya. Unaweza ukaipata mtandaoni katika wavuti www.freebiblecommentary.org.

## MADA MAALUM: MASIHI (kutoka Dan. 9:26)

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika kwa kuweka mafuta maalumu juu ya mtu kuashiria wito wa Mungu na kuwezesha uongozi wa majukumu yaliyotolewa

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6,10; 2 Sam. 19:21; 23:1; Zab. 89:51; 132:10,17; Maombolezo 4:20; Hab. 3:13; "Mwana wa mfalme alyetiwa mafuta" katika Dan. 9:25

2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani "makuhani waliotiwa mafuta," Kut. 29:7; mfano Law. 4:3,5,16; 6:15; 7:36; 8:12; yawezekana Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. liotumiwa na Wazee wa kale, na manabii (kama vile Mwanzo 26:7; 1 Nyakati 16:22; Zab. 105:15, ambalo linamaanisha watu wa agano kwa umoja wao; yawezekana Hab. 3:13)
4. lililotumiwa na manabii (kama vile 1 Wafalme 19:16; yawezekana 1 Nyakati 29:22)# 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.
5. lilitumiwa na Koreshi (kama vile Isa. 45:1)
6. #1 na #2 zinaunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4
7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
   a. uzao wa Yuda (kama vile Mwanzo 49:10)
   b. nyumba ya Yese (kama vile 2 Sam 7)
   c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)
   d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu ya

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne
2. kutambulishwa kwa "mwana Adamu" katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima itambuliwe kuwa hiki ni cheo nadra katika Agano la Kale, yawezekana ni Dan.9:25 tu. Lazima itambuliwe kwamba Yesu hashabihiani na maelezo ya jumla ya Agano la Kale ya Masihi

1. sio kiongozi katika Israeli
2. hakupakwa mafuta rasmi na Kuhani
3. sio mwokozi wa Israeli tu
4. sio tu "mwana wa mtu," lakini cha kushangaza "mwana wa Mungu"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:4-9**

**4 Basi Abramu akaenda, kama Bwana alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani. 5 Abramu akamchukua Sarai mkewe, na Lutu mwana wa nduguye, na vitu vyao vyote walivyokuwa wamejipatia na hao watu waliowapata huko Harani, wakatoka ili kwenda nchi ya Kanaani; nao wakaingia katika nchi ya Kanaani. 6 Abramu akapita katikati ya nchi mpaka mahali patakatifu pa Shekemu; mpaka mwaloni wa More. Na Wakanaani siku zile walikaa katika nchi hiyo. 7 Bwana akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhabahu Bwana aliyemtokea. 8 Kisha akaondoka huko akaenda mpaka mlima ulio upande wa mashariki wa Betheli, akaipiga hema yake; alikuwa na Betheli upande wa magharibi, na Ai upande wa mashariki, akamjengea Bwana madhabahu huko, akaliitia jina la Bwana. 9 Naye Abramu akasafiri, akazidi kwenda pande za kusini.**

**12:4 "Abramu akaenda"** Josephus (*Antiq.* 1.8.1) anasema kwamba Ibrahimu aliondoka kwasababu familia yake ilikataa ujumbe wake mpya ya kufunuliwa imani kwa Mungu mmoja .

◙**"Lutu akaenda pamoja naye"** Josephus (*Antiq.* 1.8.1) anasema kwamba Abramu alimchukua Lutu kwasababu hakuwa na watoto. Hii inawezekana kuwa mfano mwingine wa Abramu kujaribu kumsaidia Mungu kutimiliza Ahadi yake ya uzao (kama vile Sura ya 16). Kumchukua Lutu (na pia baba yake Tera, kama vile 11:31) inaonekana kuvunja maelekezo/maagizo ya YHWH ya 12:1c.

◙**"miaka sabini na mitano"** Watu waliotajwa mwanzoni katika Mwanzo (sura za 4-9) waliishi katika nyakati zilizopitiliza. Haijulikani kwanini.

1. dhambi ilikuwa haijaiharibu nchi
2. miaka ilikuwa ikihesabika kiutofauti
3. kutumia ishara za kifasihi (kama Wafalme wa Ki-Sumeri kabla ya gharika)

Kwasababu yoyote ile, Abramu alikuwa bado kijana "mdogo". Mtu anapolinganisha Mstari wa 7:4 na Mwanzo 11:32, kunaonekana kuwepo kama tofauti ya miaka 6. Hatahivyo, yawezekana Abramu hakuwa ameorodheshwa kama mtoto wa kwanza kwasababu ya umri bali kwakuwa alikuwa anajulikana kwa ushujaa wake wa kimajukumu (kama vile *Hard Sayings of the Bible*, ukurasa wa 49). Mara kwa mara wafasiri wa kisasa wanachukulia maandiko ya kiebrania ya Kale na deturi kama vile ni za kwao. Mtazamo wao wa historia "sahihi" na ya kwetu si moja inayofanana. Moja si bora kuliko nyingine, ni tofauti tu.

◙**"Harani"** Katika Mwanzo 11:26 "Harani" (BDB 248) ni mtoto wa Tera ambaye alifariki huko Uru. Hili hapa ni jiji (BDB 357) kuelekea kaskazini magharibi. Yote miji ya Uru na Harani ilikuwa vituo kwa ajili ya ibada ya kuabudu mwezi, *Zin*. Jina linamaanisha "barabara" (BDB 357) hivyo ilikuwa yawezekana njia kuu ya biashara katika Sumeri (Ninawi, Kakemish kuelekea Dameski). Katika Mwanzo 48:7 Yakobo anasema alikuja kutoka "Padani" (BDB 804), ambayo pia inamaanisha "barabara" na labda njia nyigine ya kuonesha Harani katika Aramu au Shamu (kama vile Kumb 26:5). Pia inawezekana "jiji la Nahori" (kama vile Mza 24:10) ambayo kutokea kwa Yakobo alipata mke wake mke wake Rebeka, dada wa Labani.

## MADA MAALUM: KUABUDU MWEZI

Kuabudu mwezi kulikuwa ni simulizi iliyosambaa Mashariki Karibu ya kale ikianzia na Sumeri (ustaarabu wa kwanza unaojulikana). Kulikuwa na namna ya wote mwanamke na mwanaume kwenye simulizi. Kiasili mungu mwezi alikuja kutokana na ubakaji wa mungu mke wa ngano, *Ninlil* by *Enlil*, mungu wa anga. *Enlil* alifukuzwa nje ya miungu na kuhukumiwa chini ya ulimwengu kwa matendo yake, lakini wakati *Ninlil* alipojua kwamba alikuwa na mtoto alijiunga naye. Mtoto, *dhambi* (au *Zin*), alikubaliwa kupanda katika anga kila usiku.

Kuabudu mwezi kulikusudiwa katika vipindi/hatua tofauti tofauti:

1. Mwezi mpya – *Asimbabbar*
2. Mwezi mmeguko – *Sin*
3. Mwezi wote – *Nana* (ki-Sumeria "kuangaziwa" kutoka *En-su*, "bwana wa hekima")

Majina haya kimsingi yanamaanisha "bwana mwenye hekima" (yaani *Suen*) au "kumulikia" (*Nanaa*), waliabudu katika Uru ya Wakaldayo. Jiji lenyewe mara kwa mara liliitwa Nannar. Jozi zenye rutuba ziliabudiwa katika ziggurats (piramidi kubwa zilizo tambarare juu) zilizokuwa katika mji. Yule Mungu jua (*Shamash*) alikuwa mzaliwa wa kwanza kwa wenzi na baadaye *Ereshkigal* (malkia wa ulimwengu wa chini) na *Inanna* (Malkia ya anga/mbingu).

Ibada/ dini ilisambaa maeneo yote ya Kusini Mashariki ya Mashariki ya Karibu ya kale, lakini maeneo makubwa na vituo vikubwa vilikuwa ni

1. Uru
2. Harani
3. Tema
4. Kanaani
5. Makka

Kimsingi hadithi hii imeunganisha na mkazo wa ustawi pamoja na kuabudu vitu vya anga.

Agano la Kale linakataa ibada ya vitu vya anga (kama vile Kumb. 4:19; 17:3; II Wafalme. 21:3,5; 23:5; Yer. 8:2; 19:13; Sefania. 1:5) na kuabudu rutuba (yaani *Ba'al* na *Asherah*, mashairi ya Ugarit). Waebrania kwa asili walikuwa wafugaji na wakulima wa msimu wa kuhamahama, walikuwa makini sana kukataa ibada za mwezi kwasababu kiujumla ibada ya mwezi ilikuwa ni tabia ya wafugaji wa kuhamahama na kusafiri wakati wa usiku, wakati jua lilikuwa kwa ujumla likiabudiwa na watu walio na makazi ya kudumu na wakulima. Mwishowe wafugaji walipata makazi ya kudumu na ibada ya mwezi sasa kiujumla likawa tatizo.

**12:5 "Abramu"** Jina hili (BDB 4) linamaanisha "baba aliyeinuliwa," "mtukuzaji wa baba," au "yeye aliyeinuliwa ni baba yangu." Angalia kidokezo katika 11:26.

◙**"Sarai"** Maana ya muundo wa jina hili la mke wa Abramu haijukani (BDB 979, KB 1354). Muundo mpya katika 17:15 unamaanisha "binti wa kifalme" au "binti mfalme" (BDB 979 II, KB 1354 II, kama vile Waamuzi. 5:29; I Wafalme. 11:3; Isa. 49:23).

◙**"na hao watu waliowapata huko Harani"** "kupata" kulimaanisha "kufanyika" (BDB 793). Imani/mafundisho ya kumfikia Mungu kwa tafkira ya Kiyahudi (*Kabbalah*) yanasema kwamba Abramu aliwafanya watu kupitia miujiza ili kuonesha nguvu za Mungu. Walimu wa Kiyahudi wanasema hii inamaanisha waongofu kutoka katika mahubiri ya Abramu, lakini katika muktadha inamaanisha kwa watumwa na watumishi walioletwa na pia watoto wao..

◙**"nchi ya Kanaani"** Neno "Kanaani" (BDB 488) kiasili linamaanisha kwa mwana wa Hamu (moja ya watoto wa Nuhu, kama vile Mwanzo 9:18, 22, 25, 27; 10:15). Sehemu ya eneo lililokaliwa na uzao wake ulichukua jina hili. Lilikuja kumaanisha "nchi ya chini" ikitofautishwa na "ardhi na nchi ya juu" (vilima vya chini), hivyo ilimaanisha uwanda wa pwani kutoka Misri mpaka Sidoni huko Foenike. Hata hivyo baada ya Wafilisti waliokaa pwani ya kusinimagharibi, hapo kaskazini mwa Misri, ilikuja kumaanisha eneo la pwani kaskazini mwa Filistia. Kama ilivyo vamiwa na Waebrania katika kitabu cha Yoshua ilikuja kumaanisha ardhi katika pande zote za mto Yordani. Ardhi ya Kanaani ilikuwa na maili 100 pwani ya ardhi a na urefu wake ulikuwa kama maili 180 katika urefu na upana wake ulitofautiana kutoka maili 20 mpaka maili 120.

**12:6 "Shekemu"** Jina (BDB 1014) linamaanisha "ncha ya bega." Jiji hili liko kati ya Mlima Ebali na Mlima Gerizimu. Ni maeneo ya matukio ya Nyakati kadhaa: (1) baraka na laana ya agano (kama vile Kumb. 11:29-30; Josh. 8:30-35); (2) huduma ya uhuisho wa agano (kama vile Josh. 24); (3) eneo la kukutania kati ya Rehoboamu (mwana wa Suleimani) na Yeroboamu (kiongozi wa kazi wa Kaskazini) baaada ya kifo cha Suleimani, ambacho kilipelekea kugawanyika kati ya Yuda na Israeli (922 K.K).

◙**"Mwaloni wa More"** More inamaanisha mwalimu (BDB 435). Miti iliweka alama ya maeneo ya watu wa ki-semitiki. Hii ilikuwa inawezekana kuwa eneo la madhabahu ya Wakanaani au miungu (kama vile Mwanzo 35:4; Kumb. 11:30; Waamuzi 9:37). Mti ni terafini (BDB 18, "mti mkuu"), yawezekana ni mwaloni (kama vile LXX). Chanzo kizuri cha taarifa juu ya mimea na wanyama waliotajwa katika Biblia ni UBS', *Fauna and Flora of the Bible*, toleo la pili.

◙**"Wakanaani walikuwako katika nchi"** Hii inaonekana kwa wafasiri wengi, hata Ibn Ezra, kama nyongeza za baadae, lakini inaonekana katika ufahamu wa Mwanzo 9, ikimaanisha kwamba ardhi/nchi ilikuwa imekaliwa na uzao wa Kanaani.

## MADA MAALUM: WAKAZI WA ISRAELI WALIOISHI PALESTINA

A. Kuna orodha nyingi ya watu.
   1. Mwanzo 15:19-21 (10)

a. Wakeni
b. Wakenizi
c. Wakadmoni
d. Wahiti
e.Waperizi
f. Warefai
g.Waamori
h. Wakaanani
i. Wagirgashi
j. Wayebusi

2. Kutoka 3:17 (6)

a. Wakaanani
b.Wahiti
c. Waamori
d. Waperizi
e. Wahivi
f.Wayebusi

3. Kutoka 23:28 (3)

a. Wahivi
b. Wahiti
c.Wahiti

4. Kumbu kumbu la Torati 7:1 (7)

a. Wahiti
b.Wagirgashi
c.Waamori
d. Wakaanani
e. Waperizi
f. Wahivi
g.Wayebusi

5. Yoshua 24:11 (7)

a. Waamori
b. Waperizi
c. Wakaanani
d. Wahiti
e. Wagirgashi
f. Wahivi
g. Wayebusi

B. Asili ya majina haya haijulikani kwa sababu ya kukosa vielelezo vya kihistoria. Mwanzo 10:15-19 inajumuisha mengi kati yao kama inavyohusiana na Mwana wa Hamu.

C. Maelezo mafupi ya watu hawa waliotajwa

1. Wakeni
— BDB 884, KB 1098
— wasio Waisrael
— jina linahusiana na "mfua chuma" au "mhunzi," ambalo lingalirejelea kazi ya kufua bati au muziki (kama vile Mwa. 4:19-22)
— lilihusianishwa na eneo la Mlima Sinai Kaskazini mwa Hebron
— jina lilihusiana na Yethro, Mkwewe Musa (kama vile Amu. 1:16; 4:11)

2. Wakenizi
— BDB 889, KB 1114
— nduguze Wayahudi
— ukoo wa Edom (kama vile Mwa. 15:19)
— waliishi huko Negebu
— yumkini wakaishilia Uyahudi (kama vile Hes. 32:12; Yos. 14:6,14)

3. Wakadmoni
— BDB 870 II, KB 1071 II
— hawakuwa Waisrael, yumkini kizazi cha Ishmael (kama vile Mwa. 25:15)
— jina linahusiana na "mtu wa Mashariki"
— waliishi huko Negebu
— yumkini wanahusiana na "watu wa Mashariki" (kama vile Ayu. 1:3)

4. Wahiti
— BDB 366, KB 363
— hawakuwa Waisrael
— kizazi cha Sethi
— walitokea ufalme wa Anatolia (Asia Ndogo, Uturuki)

| | | |
|---|---|---|
| | | — walikuwepo mwanzoni kabisa huko Kaanani (kama vile Mwanzo 23; Yos. 11:3) |
| 5. | Waperizi | — BDB 827, KB 965<br>— hawakuwa Waisrael, yumkini Hurrians<br>— waliishi kwenye maeneo ya misitu ya Uyahudi( kama vile Mwa. 34:30; Amu. 1:4; 16:10) |
| 6. | Refaimu | — BDB 952, KB 1274<br>—hawakuwa Waisrael, yumkini majitu (kama vile Mwa. 14:5; Hes. 33:33; Kumb. 2:10-11,20)<br>— waliishi kwenye kingo za Mto Yordani (kama vile Mwa. 15:20; Yos. 12:4; 13:12; Kumb.2:8-11,20; 3:13) au Kingo za Magharibi (kama vile Yos. 15:8; 17:15; 2 Sam. 5:18,22; 23:13;1 Nya. 20:4)<br>—kizazi cha wapiganaji |
| 7. | Waamori | — BDB 57, KB 67<br>— kundi la watu wa Kisemitiki toka Hamu (kama vile Mwa. 10:16)<br>— wakawa wenye cheo kikuu kwa kizazi cha Wakaanani (kama vile Mwa. 15:16; Kumb. 1:7; Jos. 10:5; 24:15; 2 Sam. 21:2)<br>— jina laweza kumaanisha "watu wa Magharibi"<br>— ISBE, juzuu. 1, uk. 119, inasema neno linamaanisha<br>a. kizazi cha Wapalestina kiujumla<br>b. idadi ya watu wa nchi ya milima waliopingwa na watu wa uwanda wa Pwani<br>c. kikundi cha watu maalum wakiwa na Mfalme wao |
| 8. | Wakaanani | — BDB 489, KB 485<br>— toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:15)<br>— wakawa wenye cheo kikubwa kwa kabila zote za Wakaanani Magharibi mwa Yordani<br>— maana ya Kaanani haijulikani, yumkini "mfanya biashara" au "rangi ya hudhurungi"<br>— kama kikundi cha watu walioishi kando ya uwanda wa Pwani (kama vile Hes. 13:29) |
| 9. | Wagirgashi | — BDB 173, KB 202<br>— toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:16) au kiwastani "toka mwana wa [yaani., nchi ya] Wakaanani," ISBE, juzuu. 2, uk. 1232) |
| 10. | Wayebusi | — BDB 101, KB 382<br>— toka Hamu (kama vile Mwa. 10:16)<br>— toka Mji wa Wayebusi/Salemu/Yerusalem (kama vile Yos. 15:63; Yos. 19:10)<br>— Ezek. 16:3,45 inadai kilikuwa kizazi mchanganyiko toka kwa Waamori na Wahiti |
| 11. | Wahivi | — BDB 295, KB 297<br>— toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:17)<br>— ikatafasiriwa na maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) kama Waamori (kama vile Mwa. 34:2; 36:20-30; Yos. 9:7)<br>— yumkini toka kwenye neno la Kiebrania "pango," kwa hiyo, waishio mapangoni<br>—waliishi katika uwanda wa juu wa Lebanon (kama vile Yos. 11:3; Amu. 3:3). katika 2 Sam. 24:6-7 imewaorodhesha mbele ya Tiro na Sidoni |

**12:7 "BWANA akatokea"** Hiki ni KITENZI kilichozoeleka "kuona" (BDB 906) kikitumika katika namna maalumu (yaani muonekano wa kimwili unaoonekana wa ki-mungu, kama vile. 12:7 [mara mbili]; 17:1; 18:1; 26:2,24; 35:1,9; 48:3). Katika mstari wa 1 YHWH anazungumza na Abramu, lakini hapa anatokeza! Mara kwa mara YHWH anatokea katika muundo wa "malaika wa BWANA."

## MADA MAALUM: MALAIKA WA BWANA (BDB 521 kutengeneza BDB 217)

Ni dhahiri kwamba Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kimwili katika muundo wa mwanadamu kwenye Agano la Kale. Swali juu ya Utatu Mtakatifu linakuja, mtu gani miongoni mwa Utatu aliyeikamilisha kazi hii. Kwa kuwa Mungu Baba (YHWH) na Roho Wake wamedumu katika hali ya kutokuwa katika mwili, inaonekana kuwepo na uwezekano wa kwamba udhihirisho huu wa kibinadamu ni Masihi aliyekuwepo kabla ya kuuvaa mwili.

Ili kufafanua ugumu anaokabiliana nao mtu katika kujaribu kutambua udhihirisho wa Mungu katika hali ya kimwili ya mfanano wa kimalaika orodha ifuatayo ina ufafanuzi.

1. yeye malaika wa Bwana kama malaika (mara kwa mara "malaika wake", "malaika," "yule malaika," hata "nguzo")
   a. Mwa. 24:7,40
   b. Kut. 23:20-23; 32:34
   c. Nah. 22:22
   d. Fal. 5:23
   e. 2 Sam. 24:16
   f. 1 Nya. 21:15-30
   g. Zek. 1:12-13
2. Malaika wa Bwana kujidhihirisha katika hali ya kimwili
   a. Mwa. 16:7-13; 18:1-33; 22:11,15; 31:11,13; 48:15-16
   b. Kut. 3:2,4; 14:19 (13:21)
   c. Fal. 2:15; 6:22-24; 13:3-23
   d. Hos. 12:3-4
   e. Zek. 3:1-5
   f. Mdo. 7:30, 35, 38

Ni muktadha tu unaoweza kutofautisha kati ya mbadala hizi mbili

◙**"Nitaupa uzao wako nchi hii"** Hii ilikuwa ahadi kubwa kwa uzao wa Ibrahimu (kibayana "uzao," kama vile 13:15; 15:18), lakini Paulo aliona umoja "nzao" ikimaanisha Masihi (kama vile Gal. 3:16).

◙**"hivyo akajenga madhabahu pale"** Madhabahu hizi zilikuwa njia ya kukumbuka matukio maalumu au kutokewa (yaani 8:20; 13:18; 22:9; 26:25; 33:20; 35:7; Kut. 17:15; 24:4; Josh. 8:30; Waamuzi 6:24; 21:4; I Sam. 7:17; 14:35; II Sam. 24:25). Sadaka ilikuwa ni njia ya kuelezea njia inayoonekana kwa namna ya uwepo wa Mungu, kujali na upaji wake. Sadaka inayoonekana ilifanyika isiyoonekana katika moshi na kupanda kwa Mungu.

**12:8 "Betheli"** Hii inamaanisha "nyumba ya Mungu" (BDB 110). Kutoka 28:19 tunajifunza kwamba jiji hili kwa asili lilikuwa likiitwa Luzi mpaka siku ya Yakobo. Hili neno la baadaye na tungo ya mwisho ya mstari wa 6 inamaanisha kwamba simulizi hii iliwekewa kumbukumbu baadaye na inawezekana kuwepo kwa kipindi cha desturi za masimulizi ya kinywa. Muda kamili, mtu na mbinu za utungaji wa vitabu vya Agano Kale haujulikani. Angalia Utangulizi kwa Mwanzo, juzuu ya 1A, D. 1. 18

◙**"akaliitia jina la BWANA"** Mtu anapolinganisha mstari huu na 4:26 pamoja na Kut. 6:7, kunakuwa kunaonekana mkanganyiko. Hata hivyo, yawezekana jina kiasili lilitumika bila ufahamu wa umuhimu wa agano Lake Kamili. Tungo hii inamaanisha kuabudu/mazingira ya ibada (Kama vile 4:26; 12:8; 13:4; 21:33; 26:25).

## MADA MAALUM: "JINA" LA YHWH

Matumizi ya "jina" kama neno mbadala wa YHWH Yeye mwenyewe ni usambamba wa Kut. 23:20-33 matumizi ya "malaika," anayesemekana kuwa "Jina langu li ndani Yake." Huu mbadala pia unaweza kuonekana katika matumizi ya "utukufu Wake" (mfano Yohana 1:14; 17:22: Angalia Mungu anaelezewa kama mwanadamu).

Majaribio yote ni kulainisha tabia yake binafsi ya kupewa sifa za kibinadamu ya uwepo wa YHWH (kama vile Kut. 3:13-16; 6:3). YHWH hakika anazungumzwa juu ya namna ya kibinadamu, lakini pia ilijulikana kama alikuwepo kiroho katika uumbaji wote (kama vile I Wafalme 8:27; Zab. 139:7-16; Yer. 23:24; Mdo. 7:49 ananukuu Isa. 66:1).

Kuna mifano kadhaa ya "jina" ikiwakilisha maana ya uungu wa YHWH na uwepo wake binafsi.

1. Kumb. 12:5; II Sam. 7:13; I Wafalme 9:3; 11:36
2. Kumb. 28:58
3. Zab. 5:11; 7:17; 9:10; 33:21; 68:4; 91:14; 103:1; 105:3; 145:21
4. Isa. 48:9; 56:6
5. Ezek. 20:44; 36:21; 39:
6. Amosi 2:7
7. Yoh. 17:6,11,26

Dhana ya "kuita" (yaani kuabudu) jina la YHWH linaonekana mwanzoni katika Mwanzo.

1. 4:26, uzao wa Sethi
2. 12:8, Ibrahimu
3. 13:4, Ibrahimu
4. 16:13, Hajiri
5. 21:33, Ibrahimu
6. 26:25, Isaka

na katika Kutoka:

1. 5:22-23, inaongea katika jina Lako
2. 9:16, tangaza jina langu katika dunia yote (kama vile Rum. 9:17)
3. 20:7, usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako (kama vile Law. 19:12; Kumb. 5:11; 6:13; 10:20)
4. 20:24, ambapo nitasababisha jina langu kukumbukwa (kama vile Kumb. 12:5; 26:2)
5. 23:20-21, malaika ("kwakuwa jina langu li ndani yake")
6. 34:5-7, Musa anaita (au "kuliitia") jina la Bwana. Hili ni kati ya maandiko machache kwamba yanayoelezea tabia ya YHWH (kama vile Neh. 9:17; Zab. 103:8; Yoeli 2:13)

Kumfahamu mtu kwa jina kunamaanisha ukaribu (kama vile Kut. 33:12); Musa analijua jina la YHWH na katika 33:17, YHWH analijua jina la Musa. Huu ni muktadha ambapo Musa anataka kuona utukufu wa Mungu (kama vile mstari wa 18), lakini Mungu anaruhusu yaya kuona "Wema Wake" (mstari wa 19), ambao ni sambamba na "jina" (mstari wa 19). Waisraeli wanatakiwa kuharibu "majina" ya miungu ya Kanaani (kama vile Kumb. 12:3) kumuita Yeye (kama vile Kumb. 6:13; 10:20; 26:2) katika mahali maalumu Anasababisha jina lake kukaa/kudumu (kama vile Kut. 20:24; Kumb. 12:5,11,21; 14:23,24; 16:2,6,11; 26:2).

YHWH anakusudi la kiulimwengu kuhusisha jina lake

◙ **"Ai"** Hii ilimaanisha "lundo la mawe" (BDB 743) lilikuwa ni jiji, au yawezekana mabaki ya jiji, karibu na Betheli.

**12:9 "akasafiri"** Hii kibayana ilimaanisha "kuvuta/kuchomoa vigingi vya hema" (BDB 652, KB 704, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Inaaksi maisha ya ufugaji wa kuhamahama ya Ibrahimu, kama inavyokuwa "kupigilia hema lake" katika mstari wa 8.

◙**"Negebu"** Hii inamaanisha "kusini" (BDB 616, kama vile 13:1,3). Sio jangwa, lakini malisho yenye majani kidogo kwa nyakati Fulani za mwaka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:10-16**

[10] Bas**i kulikuwa njaa katika nchi ile; Abramu akashuka Misri, akae huko kwa muda maana njaa ilikuwa nzito**

**katika nchi. [11] Ikawa alipokuwa karibu kuingia Misri, akamwambia Sarai mkewe, Tazama, najua ya kuwa u mwanamke mzuri wa uso; [12] basi itakuwa, Wamisri watakapokuona watasema, Huyu ni mkewe; kisha wataniua mimi na wewe watakuacha hai. [13] Tafadhali useme, wewe u ndugu yangu, iwe heri kwangu kwa ajili yako, na nafsi yangu iishi kwa ajili yako. [14] Basi ikawa Abramu alipofika Misri, Wamisri wakamwona huyo mwanamke ya kwamba yeye ni mzuri sana. [15] Wakuu wa Farao wakamwona, nao wakamsifu kwa Farao; basi yule mwanamke akachukuliwa nyumbani mwa Farao. [16] Naye akamtendea Abramu mema kwa ajili yake; naye alikuwa na kondoo na ng'ombe, na punda waume, na watumwa, na wajakazi, na punda wake, na ngamia.**

**12:10 "njaa"** Hii kidhahiri ni "tumbo tupu" (BDB 944). Mungu aliijaribu imani ya Ibrahimu. Akashindwa (kama vile mistari ya 12-13)! Biblia inaonesha wanadamu, ni sugu na. Ibrahimu sio maalumu kihivyo; YHWH ndio maalumu!

**12:11** Wake za Makuhani wa kiume walikuwa wazuri (kama vile 12:11; 24:16; 26:7), lakini walikuwa wanawake walio tasa. YHWH alionesha nguvu zake, uwepo na kusudi kwa kuruhusu kila mmoja wao kuzaa mzao. Hii ilikuwa ni njia ya kuonesha kwamba alikuwa anashughulikia historia ya Israeli, sio vizazi vya binadamu au kupanga.

**12:12 "wataniua mimi"** Mungu alikuwa amemuhaidi kumfanya kuwa taifa kubwa lakini hapa anajaribu kujilinda yeye mwenyewe kwa gharama hata ya kumpoteza mkewe. Katika sura ya 20 alirudia tendo lake na sura ya 26 mwanawe akafanya kitu hicho hicho

## MADA MAALUM: SHETANI AKIJARIBU KUZUIA UZAO WA KIMASIHI KATIKA KITABU CHA MWANZO

A. Uasi wa Kaini, Mwanzo 4
B. Kuchanganywa kwa uzao wa binadamu na malaika, Mwanzo 6
C. Uasi wa Mnara wa Babeli, Mwanzo 11
D. Ibramu anamtoa Sarai kwa Farao, Mwanzo 12
E. Kuzaliwa kwa Ishmaeli kwa Hajiri (mtumishi wa Sarai), Mwanzo 16
F. Abramu anamtoa Sarai kwa Abimeleki, Mwanzo 20
G. Sadaka ya Isaka, Mwanzo 22
H. Mashindano kati ya Esau na Yakobo, Mwanzo 25, 32
I. Isaka anamtoa mke wake kwa Abimeleki, Mwanzo 26
J. Utapeli na mashindano ya Labani, Mwanzo 29-31
K. Yakobo anajiunga na Shekemu, Mwanzo 34
L. Mashindano kati ya watoto wa Yakobo, Mwanzo 37
M. Kukoswa imani kwa Yuda na uasherati unaohusiana na Tamari, Mwanzo 38

**12:13 "tafadhali useme kuwa wewe ni dada yangu"** Hii inaonekana geni kwetu lakini (1) walikuwa ndugu wasio kuwa wa damu kaka na dada (yaani baba mmoja, kama vile 20:12) na (2) kutoka katika Vibao vya Nuzi tunajifunza kwamba desturi hii ya kuoa ndani ya familia ilikuwa imezoeleka katika jamii ya Hurri ya juu au (3) zaidi kuwaita wake "dada" ilikuwa imezoeleka (kama katika Misri na Wimbo uliobora 4:9,10,12; 5:1,2).

**12:15 "Farao"** Cheo hiki (BDB 829) kinatumika na wafalme wa Misri kutoka katika utawala wa kinasaba wa kumi na nane na kuendelea. Asili ya neno la Kimisri "nyumba kuu."

**12:16 "akampatia"** Mali za Ibrahimu zote hazikutoka kwa Farao (kama vile 12:5b).

◙ Ingawa kondoo na mifugo, pamoja na punda ilikuwa mifugo iliyozoeleka na chanzo cha utajili katika ulimwengu wa kale (Abramu alipewa mahari kwa ajili ya Sarai), ngamia hawakuwa wakifugwa kwa upana mpaka baadaye (yaani mwishoni mwa Milenia ya pili k.k.). Kuna baadhi ya ushahidi wa kiekolojia kwa ngamia wanaofugwa

mwanzoni mwa milenia ya pili K.K. katika Mesopotamia, lakini ni kwa daraja la waliosoma tu (angalia R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, ukurasa wa 311. Pia angalia katika mstari huu kwamba watumwa na watumishi wanaorodheshwa pamoja na mali (kama vile 20:14; 26:14; 30:43; 32:5)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:17-20**

**17 Lakini Bwana akampiga Farao na nyumba yake mapigo makuu, kwa ajili ya Sarai, mkewe Abramu. 18 Ndipo Farao akamwita Abramu, akasema, N'nini hili ulilonitendea? Mbona hukuniambia ya kuwa huyo ni mkeo? 19 Mbona ulisema, Huyo ni umbu langu, hata nikamtwaa kuwa mke wangu? Basi sasa, huyo mke wako umchukue, uende zako. 20 Farao akawaagiza watu kwa ajili yake, wakampeleka njiani, na mkewe, na kila alichokuwa nacho.**

**12:17 "mapigo makuu"** Mapigo haya inavyoonekana yalikuwa yakihusishwa na ulinzi wa Sarai. Katika Mwanzo 20:18 Inamaanisha "tumbo la uzazi lililofungwa" kwa wake wa Abimeleki. KITENZI "kupiga" (BDB 619, KB 668, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ni mzizi mmoja na "mapigo" (BDB 619), ambalo lililkuwa njia ya kisarufi ya kuongezeka.

◙**"kwa ajili ya Sarai"** Hii ni "kwa maneno ya." Rashi anasema kwamba alimwamuru malaika kumlinda yeye mwenyewe. Inavyoonekana anamjulisha Farao juu ya hali (kama vile mstari wa 18).

**12:18** Mapigo kibayana yanahusiana na ulinzi wa kimwili/kimapenzi wa Sarai. Swali ni kwa namna gani Farao alifahamu juu ya sababu ya mapigo.

1. YHWH alimfunulia
2. Wanajimu na wenye hekima wa Misri (kama vile Kut. 7:11,22; 8:7)?
3. Sarai yeye mwenyewe

Huu unaweza kuwa mfano mwingine, kama Danieli 4 au Magi ya Agano Jipya, ambapo Mungu anazungumza na wasio Wayahudi kufunuliwa kusudi lake.

**12:19-20** Kuondoka kwa Ibrahimu Misri hakukuwa ni ombi bali amri.

1. "chukua" – BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "nenda" – BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. "Farao akaamuru watu wake" – BDB 845, KB 1010, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. "akamtoa nje" – BDB 1018, KB 1511, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini agano ni muhimu sana? Je nani anajumuishwa ndani yake? Toa masharti yake.
2. Je Ibrahimu kwa haraka alitimiza sehemu yake? Je neema ya Mungu inaonekana vipi katika sura hii?
3. Je Tera alikuwa amekufa wakati Ibrahimu alipoondoka Harani?
4. Je Mungu alimjaribu namna gani katika sura hii? Je alifanikiwa?

# MWANZO 13

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Abramu na Lutu | Abramu Anairithi Kanaani | Abramu na Lutu | Abramu na Lutu | Abramu na |
| 13:1 | 13:1-4 | | 13:1-4 | 13:1-4 |
| 13:2-7 | | 13:2-7 | | |
| | 13:5-13 | | 13:5-7 | 13:5-9 |
| 13:8-13 | | 13:8-13 | 13:8-9 | |
| | | | 13:10-13 | 13:10-13 |
| | | | Abramu anahamia Hebroni | |
| 13:14-18 | 13:14-18 | 13:14-18 | 13:14-18 | 13:18 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 13:1**
[1] **Abramu akapanda kutoka Misri, yeye, na mkewe, na kila alichokuwa nacho, na Lutu pamoja naye, mpaka kusini.**

**13:1 Abramu akapanda kutoka Misri**. Jina Negebu. linamaanisha maeneo kavu ya kusini mwa Kanaani. Yeye alikuwa amehamia katika eneo hili hili mapema sana (kama vile 12:9) na alirudi katika eneo hili tena katika 20:1. Pia hili ni eneo aliloishi Isaka (kama vile 24:62).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 13:2-7**
**[2] Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu. [3] Akaendelea kusafiri kutoka kusini mpaka Betheli, mahali pale palipokuwapo hema yake kwanza kati ya Betheli na Ai; [4] napo ndipo palipokuwa na madhabahu aliyofanya hapo kwanza; naye Abramu akaliitia jina la Bwana hapo. [5] Na Lutu aliyesafiri pamoja na Abramu, yeye naye alikuwa na makundi ya ng'ombe na kondoo, na hema. [6] Na ile nchi haikuwatosha, ili wakae pamoja; maana mali zao zilikuwa nyingi, hata wasiweze kukaa pamoja. [7] Kukawako ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abramu, na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile Wakanaani na Waperizi walikuwa wakikaa katika nchi.**

**13:2** Abramu alikuwa mtu tajiri. Kitabu cha Mwanzo kinaeleza vyanzo viwili vya utajiri huu.
1. umiliki wake kutoka Uru, 12:5
2. ulimbikizaji wake wa mali kutoka Misri, 12:16

Katika Mashariki ya Karibu ya Kale kulikuwa na njia kadhaa za kujilimbikizia mali zilizokusanywa.
1. vyuma vya thamani
2. dhahabu
3. mavazi
4. vyakula vya aina mbalimbali
5. ufugaji

**13:4 "Abramu akaliitia jina la Bwana hapo"** Kifungu hiki kinafafanua aina ya kipekee ya muundo wa ibada, huenda muundo huu ulihusisha dhabihu ya mnyama (kama vile Kut. 20:24). Muundo huu kwa mara ya kwanza unatumika katika 4:26, lakini unaonekana tena katika 12:8; 13:4;21:33; 26:25. Tazama Mada Maalum katika 12:8. Kwa sababu ya ufanano wa I Nya. 16:8; Zab. 105:1; 116:17; na Isa. 12:4, kuliitia jina pia kulihusisha tendo la "kusifu" au "kutoa shukrani" kwa YHWH.

Hili "jina" (BDB 1027) liliwakilisha uwepo binafsi wa Mungu wa agano. Umuhimu wake kamili hautafahamika hadi Kutoka 3:13-16. Kama jina *Elohim* lilivyowakilisha "Muumbaji," jina la YHWH liliwakilisha kufanya agano, kwa upekee, kuwepo, Mungu wa Sethi na Shemu mwenye ahadi. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 12:1.
Abramu alirudi katika madhabahu yake ya kwana katika Kanaani (kama vile 12:8).

**13:6** Nchi hii iliyokuwa kusini mwa Kanaani haikupata mvua ya kutosha kwa mwaka kuruhusu majani asilia kustawi. Ilichukua heka nyingi sana kukidhi mahitaji ya kundi moja. Mara nyingi kuanzia Aprili hadi Septemba kilikuwa kipindi cha kutosha kustawisha majani, lakini katika Octoba hadi Marchi umati wa watu ulilazimika kuhamia maeneo yenye majani mengi.

**13:7 "Wakanaani na Waperizi"** Hili neno "Wakanaani" ni neno la jumla la makazi ya Palestine, kama ilivyo kwa "Waamori" Baadhi wameiona taofauti katika majina haya ya aina moja: (1) Mperizi anaweza kumaanisha "mwanakijiji," ambapo (2) Mkanaani anarejelea mkazi wa mji uliozungushiwa ukuta. Hii ni sehemu pekee ambayo makundi haya mawili yameorodheshwa kama makazi ya Palestina pekee. Angalia Mada Maalum katika 12:6. Kwa maelezo kamili kuhusu "Wakanaani" tazama katika 12:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13:8-13**
**[8] Abramu akamwambia Lutu, Basi, usiwepo ugomvi, nakusihi, kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu. [9] Je! Nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi; ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume; ukienda upande wa kuume, nitakwenda upande wa kushoto. [10] Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya Bwana, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari. [11] Basi Lutu akajichagulia Bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatengana wao kwa wao. [12] Abramu akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile Bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma. [13] Lakini watu wa Sodoma walikuwa wabaya, wenye kufanya dhambi nyingi sana juu ya Bwana**

**13:8-9 "usiwepo ugomvi"** Kuna mlolongo wa miundo ya kisarufi ambayo inaeleza mazungumzo haya.

1. usiwepo ugomvi (BDB 937) – BDB 224, KB 243, *Qal* HALI YENYE MASHARTI, mst. 8
2. ujitenge nami – BDB 825, KB 962, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, mst. 9
3. nitakwenda upande wa kuume – BDB 412, KB 415, *Hiphil* YA KITENZI AMRISHI
4. nitakwenda upande wa kushoto – BDB 970, KB 1332, *Hiphil* YA KITENZI AMRISHI

Inashangaza kwamba Abramu (mtu mzee na mwnye mali nyingi) alimwacha Lutu achague, kwa sababu nchi ya Kanaani ilikuwa imechaguliwa na YHWH kama zawadi ya kipekee kwa Abramu. YHWH aliutumia uchoyo wa Lutu kumtia shauku ya kuuchagua upande wa mashariki ya Yordani. Ni baada tu ya Lutu kuondoka, na Abramu alikaa ndani ya Kanaani ndipo YHWH alipomtokea.

**13:8 "ndugu"** Hapa neno hili (BDB 26) linatumika katika maana ya jamaa (kama vile. 14:14,16; 29:12,15).

**13:10 "Lutu akainua macho yake, akaliona"**Lutu alijichagulia bonde hili kwa kuyaangalia maslahi yake mwenyewe. Uovu (kama vile mst. 13) wa eneo hili haukumtia hofu.

◙ **"kabla Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora"** Hapa kuna maoni mengine ya kiuhariri kutokana na tukio hili la kale. Mtu na wakati halisi ambao maelezo haya yalichukuliwa hauijulikani, lakini inaonekana kuwa mmoja wa makuhani waliokuwa wakitumika kama waandishi na wana wasifu wa Musa (yaani, aliyechukua kumbukumbu ya kifo chake [Kutoka 34] na kutoa maoni juu yake, kama ilivyo katika Hes. 12:3).

◙ **"kama bustani ya Bwana, kama nchi ya Misri"** Rashi (mwalimu wa Kiyunani wa Nyakati za Kati) anasema nchi hiyo ilikuwa na miti kama ile ya Edeni na mbogamboga kama zile za Misri. Hapa maelezo ya kimzaha yanaeleza bustani ya Edeni kama sehemu ya hukumu, ndivyo ilivyo, Bonde la Yordani!

◙ **"Soari"** Soari (BDB 858) ni moja ya mji ulio katika Bonde la Yordani (kama vile mst. 10), kusini mwa Bahari ya Chumvi, ambapo maelezo ya jina lake yanapatikana katika Mwa. 19:20-22, ambapo ni neno la kimzaha juu ya "dogo" (BDB 859 I). Hii ilikuwa eneo la jangwa lenye miti na chemchemi za maji (kama vile Josephus, *Jewish Wars* 4.8.4).

Kuna miji kadhaa iliyo katika eneo hili: (1) Sodoma; (2) Gomora; (3) Admah; (4) Zeboiim; na (5) Soari/Bela. Kwa pamoja yaliitwa "miji ya uwazi." Yote lakini Soari iliharibiwa na Mungu (kama vile Kut. 29:23).

**13:13** Idadi kubwa ya watu wa Sodoma inaelezwa katika njia hasi.

1. uovu – BDB 948, kama vile. 2:9; 3:22; 6:5; 8:21; 37:33; 38:7
2. wenye dhambi – BDB 308, kama vile Hes. 16:38; 32:14
3. dhidi ya Bwana
4. uovu uliozidi

Hata hivyo, andiko halifafanui ni kwa namna gani. Maelezo ya sura ya 19 yanatufungulia mlango wa kuujua uovu wao. Hesabu1 na 2 ni uelezeaji wa wazo moja kwa kutumia maneno mawili kwa kutumia viunganishi (hendiadys), ambazo mara kwa mara huunganishwa katika tafsiri kama "watenda uovu."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13: 14-18**

**[14] Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi; [15] maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. [16] Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, uzao wako nao utahesabika. [17] Ondoka, ukatembee katika nchi hii katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo. [18] Basi Abramu akajongeza hema yake, akaja akakaa kwenye mialoni ya Mamre, nayo ni miti iliyoko Hebroni, akamjengea Bwana madhabahu huko.**

**13:14 "Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu"** Huenda hili lilikamilisha agizo la 12:1. Abramu alienenda kwa ufunuo ("inua sasa macho yako," BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YENYE MASHARTI; "tazama," BDB 906, KB 1157, *Qal* SHURUTISHI) ; Lutu kwa maslahi yake binafsi (kama vile mst. 10).

**13:15 "nchi hii yote. . . milele"** Vitu viwili lazima vikumbukwe katika usemi huu: (1) Agano la Mungu mara nyingi ni la kimasharti kwa mwitikio wa imani ya mwanadamu (yaani, Kumb. 11:31-32; 28:36,63-68; 30:19-20) na (2) na neno la Kiebrania "milele" (*'olam*) lazima lifasiriwe katika muktadha huu (tazama NIDOTTE, juzuu. 4, kr. 1252-1253). Mara nyingi hili halimaanishi "milele" katika maana ya sasa ya neno hili la Kiingereza. Tazama Mada Maalum: Milele ikifuatiwa na Mada Maalum : Agano.

Hiki ndicho kiini cha jambo hili linalohusu Wayahudi kuwa na dai la kibiblia katika Palestina ya sasa. Navutiwa na

1. *Israel in Prophecy* na William Hendricksen
2. *Whose Promised Land? The Continuing Crisis Over Israel and Palestine*
   na Colin Chapman

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu mmoja wa kweli anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2) wito wa Abramu(kama vile Mwanzo 12)
2. agano pamoja na Abramu (kama vile Mwanzo 15)
3. utunzaji wake na ahadi kwa Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Kumbukumbu la Torati 27-29)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya". Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18 na Ezek. 36:27-38.). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na lile Jipya. Malengo ya haya yote ni sawa: (1) urejesho wa ushirika uliopotea katika Mwanzo 3 na (2) uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu.

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utoshelevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na

imani (mwanzoni na kuendelea). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo, Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, bali ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika kitabu cha Waebrania.

## MADA MAALUMU: MILELE (*'OLAM*)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, םלוע (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 345). Haya yanatumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na muktadha). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

A. vitu vya kale
   1. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
   2. mahari, Isa. 58:12; 61:4
   3. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
   4. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
   5. muda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
B. muda/ wakati ujao
   1. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
   2. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
   3. uwepo endelevu
      1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
      2) mbinguni, Zab. 148:5
   4. uwepo wa Mungu
      1) Mwa. 21:33
      2) Kut. 15:18
      3) Kumb. 32:40
      4) Zab. 93:2
      5) Isa. 40:28
      6) Yer. 10:10
      7) Dan. 12:7
   5. agano
      1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
      2) Kut. 31:16
      3) Ufu. 24:8
      4) Hes. 18:19
      5) II Sam. 23:5
      6) Zab. 105:10
      7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
      8) Yer. 32:40; 50:5
   6. Agano maalumu na Daudi
      1) II Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
      2) I Fal. 2:33,45; 9:5
      3) II Nya. 13:5
      4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
      5) Isa. 9:7; 55:3
   7. Masihi wa Mungu
      1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4

2) Isa. 9:6

8. Sheria za Mungu
    1) Kut. 29:28; 30:21
    2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
    3) Hes. 18:8,11,19
    4) Zab. 119:89,160
9. ahadi za Mungu
    1) II Sam. 7:13,16,25; 22:51
    2) 1 Fal. 9:5
    3) Zab. 18:50
    4) Isa. 40:8
10. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
    1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
    2) Kut. 32:13
    3) I Nya. 16:17
11. Sikukuu za ahadi
    1) Kut. 12:14,17,24
    2) Ufu. 23:14,21,41
    3) Hes. 10:8
12. umilele, kudumu milele
    1) 1 Fal. 8:13
    2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
    3) Isa. 26:4; 45:17
    4) Dan. 9:24
13. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
    1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
    2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
    3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
    4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
    5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
    6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
    7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
    8) baliki jina lake, Zab. 145:1

C. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
    a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
    b. Zab. 90:2 (Mungu Mwenyewe)
    c. Zab. 103:17 (huruma za Bwana)

Kumbuka, muktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la Kale (angalia mada maalum: unabii agano la Kale la mambo yajayo).

**13:16 "Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi"** Hapa hii ni ahadi ya kistiari (kama vile 15:5; 22:17; 26:4; 28:14; Kut. 32:13; Hes. 23:10) ya mwana, familia, kabila, na taifa kubwa (YHWH pia anahaidi kumbariki Ishmaeli, kama vile 16:10; 17:20). Ahadi hii si ya kupitia kwa Lutu; aliondoka! Abramu aliiamini ahadi hii kama vile Mwa. 15:6) na Paulo anaitumia ahadi hii kama msingi wa uthibitisho wake wa neema kupitia imani katika Rum. 4:3 na Gal. 3:6.

Katika kitabu cha Mwanzo Abramu anazipokea ahadi nyingi kutoka kwa YHWH.

1. ardhi – 12:1-2; 13:14-15; 15:7,18; 17:8

2. uzao/vizazi – 12:2; 13:16;15:5,18; 17:2,4-7,16,19; 22:17
3. agano – 17:7,19,21
4. baraka za kipekee za mataifa yote kupitia yeye – 12:3; 18:18; 22:18; 26:4; 28:14

Hata hivyo, hizi si ahadi za kimaagizo. Kuna msistizo unaohusu utii na matendo yaliyo upande wake, 12:1; 13:17; 17:1,23;18:19; 22:16-18; 26:4-5 (tazama *Dictionary of Biblical Imagery*,uk. 3). Abramu halianzishi hili, bali ilimpasa kutikia kwa usahihi!

**13:17** YHWH anamwagiza Abramu kukiangalia kipawa chake kwa upya.

1. "inuka" au "ondoka" – BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI (ni ya kinahau, tazama maelezo hapa chini)
2. "ukatembee" – BDB 229, KB 246, *Hithpael* KAULI SHURUTISHI (huenda ni hitiji la kisheria kwa ajili ya kuimiliki ardhi)

Toleo la UBS la *Handbook on Genesis* inatengeneza hoja nzuri inayohusu neno "inuka" linapotumika katika muungano wa maana nyingine."

"Neno inuka halimaanishi kwamba Abramu alikuwa amekaa au alikuwa amejilaza wakati alipoamrishwa kutembea. Katika Kiebrania hili neno linafanya kazi kwa namna ya kimubalagha pale linapojitokeza kama neno lenye masharti likifuatiwa na sharti lingine, likiashiria kwamba masharti ni muhimu na ya kwamba mtu analazimika kulifanya tendo kwa wakati huo huo baada ya kupewa masharti hayo. Kwa mfano mwingine katika Mwanzo tazama 19:15; 21:18; 28:2" (uk. 304).

◙ **"nitakupa wewe"**Tazama maelezo katika mst. 15.

**13:18 "mialoni ya Mamre"** Hii miti iliyowakifishwa (BDB 18) ni mawazo yaliyokuwa yakirudiwa rudiwa katika Israeli ya kale (WINGI katika MT, lakini UMOJA katika Agano la Kale la Kiebrania na Kishamu).

1. mti mkubwa wa huko More – 12:6; Kut. 11:30
2. mti mkubwa wa huko Mamre – 13:18;14:13; 18:1 (kama vile Josephus, Antiq. 1.10.4)
3. mti mkubwa wa huko Shekemu – 35:4; Amuzi. 9:6
4. mti mkubwa wa huko Saananimu – Yos. 19:33; Amu. 4:11
5. mti mkubwa wa huko Ofra – Amu. 6:11,19
6. mti mkubwa wa huko Tabori – I Sam. 10:3 (hapa hakuna madhabahu iliyotajwa)
7. BDB 18 inahusianishwa na BDB 781 katika Mwa. 18:1,4,8. BDB 781 ndiyo mti/miti ya kipekee) ya Mwanzo 2-3 inaitwa (kama vile 2:9,16,17; 3:1,2,3,6,8,11,12,17,22,24)

◙ **"Hebroni"** Katika kipindi hiki eneo hili lilijulikana kama Kiriath-arba (kama vile 23:2; 35:27), hili ndilo jambo linaloonyesha kwamba maelezo haya yaliandikwa kipindi cha mwanzo baada ya jina hili kubadilishwa na Waisraeli waliouvamia mji huu.

◙ **"akamjengea Bwana madhabahu huko"** Hii madhabahu mpya (mara nyingi madhbahu yalijengwa katika maeneo yaliyotumika kufanyia ibada huko Kanaani ya awali) ndiyo dhamira ya mapumziko ya Abramu ya mara kwa mara katika Kanaani (kama vile 12:7; 13:18; 22:9). Hizi madhabahu huenda zilihusisha dhabihu za wanyama, ambazo zilikuwa sifa za kipekee za kumwabudu YHWH.

1. Habili – 4:4
2. Nuhu – 8:20
3. Abramu – 13:18; 15:12-21
4. Isaya - 26:25
5. Yakobo - 33:20; 35:7
6. Ayubu - Ayubu 1:5

Dhabihu ya wanyama inaendelea katika kitabu cha Kutoka (kama vile Kutoka 12) na ilikuzwa katika agano la Musa (Mambo ya Walawi 1-7,16).

# MWANZO 14

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Vita ya wafalme | Lutu kutekwa Na kuokolewa | muungano wa wafalme wanne | Ibrahimu anamuokoa Lutu | Kampeni ya wafalme wanne |
| 14:1-12 | 14:1-4 | 14:1-12 | 14:1-7 | 14:1-12 |
| | 14:5-12 | | | |
| | | | 14:8-12 | |
| 14:13-16 | 14:13-16 | 14:13-16 | 14:13-16 | 14:13-16 |
| Ahadi ya Mungu Kwa Ibrahimu | | | Melkizedeki anambariki Abramu | Melkizedeki |
| 14:17-24 | 14:17 | 14:17-20 | 14:17-20 | 14:17-19 |
| | Ibrahimu na Melkizedeki | | | (19) |
| | 14:18-20 | | | |
| (19-20) | (19-20) | (19-20) | | |
| | | | | 14:20 |
| | 14:21-24 | | 14:21 | 14:21-24 |
| | | | 14:22-24 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:1-12**

**[1] Ikawa siku za Amrafeli mfalme wa Shinari, na Arioko mfalme wa Elasari, na Kedorlaoma mfalme wa Elamu**
**na Tidali mfalme wa Goimu, [2] walifanya vita na Bera mfalme wa Sodoma na Birsha mfalme wa Gomora, na**
**Shinabu mfalme wa Adma, na Shemeberi mfalme wa Seboimu, na mfalme wa Bela, ndio Soari. [3] Hawa wote**
**wakakutana panapo bonde la Sidimu, kwenye Bahari ya Chumvi. [4] Miaka kumi na miwili walimtumikia**
**Kedorlaoma, hata mwaka wa kumi na tatu wakaasi. [5] Na mwaka wa kumi na nne akaja Kedorlaoma na**
**wafalme waliokuwa pamoja naye, wakawapiga Warefai katika Ashteroth-karnaimu, na Wazuzi katika Hamu,**
**na Waemi katika Shawe-kiryathaimu, [6] na Wahori katika mlima wao Seiri, mpaka Elparani iliyo karibu na**

**jangwa. [7] Kisha wakarudi wakaja mpaka Enmisfati, ndio Kadeshi, wakapiga nchi yote ya Waamaleki, na Waamori waliokaa Hasason-tamari. [8] Mfalme wa Sodoma, na mfalme wa Gomora, na mfalme wa Adma, na mfalme wa Seboimu, na mfalme wa Bela, ndio Soari, wakatoka wakapanga vita panapo bonde la Sidimu; [9] wapigane na Kedorlaoma mfalme wa Elamu, na Tidali mfalme wa Goimu, na Amrafeli mfalme wa Shinari, na Arioko mfalme wa Elasari, wafalme wanne juu ya wale watano. [10] Na bonde la Sidimu lilikuwa limejaa mashimo ya lami. Nao wafalme wa Sodoma na Gomora wakakimbia, wakaanguka huko, nao waliosalia wakakimbia milimani. [11] Wakachukua mali zote za Sodoma na Gomora na vyakula vyao vyote, wakaenda zao. [12] Wakamtwaa Lutu, mwana wa nduguye Abramu, aliyekaa huko Sodoma, na mali yake, wakaenda zao.**

**14:1-12** Matukio yaliyoandikwa hapa hayajulikani katika historia ya sasa, kama majina ya Wafalme. Kumekuwa na kutokuelewana kukubwa kuhusu majina haya. Inawezekana kwamba jozi ya maandiko yanayohusiana ya chambeo na "Maandiko ya Kedorlaoma " yanaandika tukio hili hili kwasababu ya ufanano wa majina matatu ya wafalme kati ya manne, lakini hili pia halina uhakika. Hivyo tunajuaje?

1. Kuna "ushahidi wa ki-akiolojia wa ustaarabu uliokua (Shaba ya Kati ya I) katika kando ya mto Yordani, Negebu na Sinai kwa muda huu ambao ulianguka ghafla" (ZPEB, juzuu ya 1, ukurasa wa 785). Vita hivi vinashabihiana na ushahidi wa sasa.
2. Majeshi yalitembea kwa umbali mrefu wakati wa kipindi hiki (yaani Milenia ya pili K.K) kupata marupurupu na uongozi.

Mfano mmoja kuonesha hali ya nchi ya mkanganyiko ambao unazunguka tukio hili unajumuisha "mfalme wa Arioki wa Elasari," ambalo linaweza kumaanisha

1. Arioko, mfalme wa mji wa Larsa (Akkadian), ambalo liko kati ya Babeli au Ashuru
2. Upatanisho wa Armenia (Elasari ni Muameni kwa ajili ya Armenia)
3. Kappadokia (kutoka Mwanzo mwa Maandiko yaliyo katika Agano la Kale na katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani ya magombo ya mabaki ya Bahari ya chumvi)
4. Jiji kati ya Kakemishi na Harani (katika maandiko ya Mari)

Mkanganyiko u wazi. Majina haya hayajazoeleka kwenye vyanzo vyovyote vile. Herufi za majina zinabadilika kutoka katika lugha moja kwenda ingine. Ni vyema kusubiri mpaka historia zaidi iliyoandikwa ijulikane kutoka katika kipindi hiki na kupata sehemu husika inayohusiana na matukio haya. Wafalme sharti waanze kuishi kipindi kimoja na kutokea kipindi cha Ibrahimu (karne ya 19 au 18 K.K). Lakini ngoja niharakishe kutaja kwamba majina yanashabihiana na nchi (majimbo ambayo yanahusiana nayo, Derek Kidner, *Genesis*, ukurasa wa 30).

1. Amrafeli – mtindo wa Wasemiti
2. Arioko– mtindo wa Wahurri
3. Kedorlaoma – mtindo wa Elamu
4. Tidali – mtindo wa Wahiti

**14:2** Majiji yanayotajwa (Sodoma, Gomora, Adma, Zeboiim, na Bela/Zoari) ni majiji yaliyo kusini mwa Araba, leo ni katika ukanda uliofunikwa na ncha ya kusini mwa Bahari ya Chumvi.

◙**"Bera. . .Birsha"** Biblia ya Kujifunzia ya Kiyahudi inasema majina haya mawili ni ya kiishara "uovu" (BDB 948) na "ubaya" (BDB 957, ukurasa wa 34, pia angalia Derek Kidner, *Genesis*, ukurasa wa 130). Hii haithibitishwi na BDB. Inaweza ikawa ya kimsingi katika sehemu yake kuelezea kwamba masimulizi yake sio ya kihistoria. Majina ya wafalme hayana uhakika kutokana na historia.

**14:3 “bonde la Sidimu”** Eneo hili linapatikana tu katika sura hii, mistari ya 3, 8. Fasiri za kale zilitumia muktadha wa haraka (mstari wa 10) kufasiri kama Bonde la Ufa la Yordani, ambapo mabaki ya bidhaa ya petroli yalikuwa yanaonekana juu ya uso wa nchi. Hii yawezekana eneo kwasasa limefunikwa na sehemu ya kusini ya Bahari ya Chumvi.

**14:4** Mstari huu unatwambia sababu kwa “miji ya uwandani” kuasi (BDB 597, KB 632, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU) dhidi ya mabwana wa Mesopotamia. Katika mwitikio Kedorlaoma alitoa mafunzo kadhaa wafalme wa Tao la Ustawi (Fertile Crescent) kuungana naye katika mapambano.

**14:5-7** Derek Kidner (*Genesis*, Tyndale OT Commentaries, ukurasa wa 131) anafikiri mistari ya wa 5-7, yawezekana mistari ya 1-11, inaweza kuwa ilitokana na nyaraka za kihistoria (Kumbukumbu ya kifalme ya kampeni za kivita) zinazoelezea kushindwa kwa “majiji ya uwandani” na washirika wao wa maeneo yao ya karibu. Mimi pia ninafikiria kwamba hii ni mbadala unaowezekana. Ni “tofauti” kutoka katika sura zinazozunguka.

**14:5 “Warefai ……Wazuzi …..Waemi”**

## MADA MAALUMU: MANENO YATUMIKAYO KWA MASHUJAA/MAKUNDI YA WATU WAREFU/WENYE NGUVU

Watu hawa wakubwa/warefu/wenye nguvu wanaitwa kwa majina mbali mbali

1. *Wanefili* (majitu,BDB 658, KB 709) - Mwa. 6:4; (angalia Mada Maalum: Wana wa Mungu katika Mwanzo 6; Hes. 13:33
2. *Warefai* (huenda BDB 952 II, KB 1274) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:11,20; 3:11,13; Yosh. 12:4; 13:12; II Sam. 21:16,18,20,22; I Nya. 20:4,6,8
3. *Wazuzi* (BDB 273), *Wazuzi* (BDB 265) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:20
4. *Waemi* (BDB 34) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:10-11
5. *Wana wa Anaki* (wana wa *Anaki*, BDB 778 I) - Hes. 13:33; Kumb. 1:28; 2:10-11,21; 9:2; Yosh. 11:21-22; 14:12,15; 15:14; Amu. 1:20

Angalia namna Mwanzo 14:5 ilivyotaja wanaume watatu wakubwa wa haya makundi (kama vile LXX, Vulgate). Neno *Warefai* pia linatumika kwa viumbe walioko kule kwenye shimo *sheol* (kama vile Ayubu 26:5; Zab. 88:10-11; Isa. 26:14,19).

◙ **“Ashterothi”** Hii (BDB 800) ni moja ya majina ya mungu wa kike wa Kanaani anayeunganishwa na *Ba’al*.

## MADA MAALUMU: IBADA YA USTAWI WA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE

I. Sababu ya

A. Wanadamu wa kale walianza kama wawindaji walioishi sehemu moja, lakini maisha ya kuhamahama yaliimarika, hitaji kwa ajili ya mazao na mifugo.
B. Wakazi wa Mashariki ya Karibu ya kale walikuwa hatarini kukabiliana na nguvu ya asili. Kadiri ustaarabu ulivyokua kuzunguka maeneo ya vyanzo vikubwa vya maji safi, walikuwa wategemezi kwa utaratibu wa kila siku wa majira.
C. Nguvu za asili ikawa miungu iliyotakiwa kujazwa na kuongozwa/kuendeshwa.

II. Wapi na kwanini

A. Dini za kuabudu kuzaa ilikua katika
   1. Misri (Nile)
   2. Mesopotamia (Hedekeli na Frati)
   3. Kanaani (Yordani)
B. Kuna ufanano wa msingi kati ya dini za uzao za Mashariki ya Karibu ya kale.
C. Majira yanayobadilika na yasiyofikirika na hali ya hewa ilisababisha ukuaji wa hadithi za

kishujaa kwa kutumia analojia ya kibinadamu /kiungu kama msingi wa maisha katika ulimwengu war oho na duniani.

III. Nani na namna gani
   A. Nani (miungu ya kiume na kike)
      1. Misri
         a. Isis (wa kike)
         b. Osiris (wa kiume)
      2. Mesopotamia
         a. Ishtar/Inanna (wa kike)
         b. Tammuz/Dumuzi (wa kiume)
      3. Kanaani
         a. Ba'al (wa kiume)
         b. Ashera, Astarte, Anathi (wa kike)
   B. Kila moja ya jozi hizi zilikuwa hadithi za kimiujiza katika namna inayofanana
      1. Mmoja anafariki
      2. mwingine anarejesha
      3. Utaratibu wa kufa na kuinuka kwa miungu kunaiga mzunguko wa kila mwaka wa asili
   C. Uigaji wa kimiujiza uliona muunganiko wa ujamiiana wa kibinadamu (yaani ndoa za miungu) kama njia ya kuhakikisha ustawi wa mazao, mifugo na watu.

IV. Waisraeli
   A. Watu wa YHWH walionywa (yaani Mambo ya Walawi na Kumbukumbu la Torati) kukwepa ibada za ustawi (haswa za Kanaani).
   B. Dini/ibada hizi zilikuwa maarufu kwasababu ya uchawi wa wanadamu na chagizo la nyongeza la tendo la ndoa
   C. Ibada ya sanamu ilishirikisha Baraka ya uzima kutaftwa katika njia za ishetani badala ya imani binafsi na tumaini kwa YHWH.

V. Masomo yanayopendekezwa
   A. W. F. Albright, *Archaeology and the Religion of Israel*
   B. J. H. Breasted, *Development of Religion and Thought in Ancient Egypt*
   C. James G. Frazer
      1. *Adonis, Attis, Osiris*
      2. *Folklore in the Old Testament*
      3. *The Worship of Nature*
   D. C. H. Gordon, *Before the Bible*
   E. S. N. Kramer, *Mythologies of the Ancient World*

**14:6 "Wahori"** Angalia Mada maalum katika 12:6.

◙**"Elparani"** Hili sio jina la jumla kwa ajili ya uungu (yaani *El*) likiwekewa viambishi awali. Ni kifupisho cha "terafini" (kama vile LXX, yaani mti mkubwa).

**14:7 "Enmisfati (ambayo ni Kadeshi)"** Neno "En" (BDB 745) linamaanisha "chemichemi" na ni sehemu ya jina la maeneo kadhaa katika Agano la Kale. "Mispati" (BDB 1048) linamaanisha "hukumu," "haki," au "maamuzi," ambalo linaashiria matukio ya Hesabu 13. Hapa ni mahali pekee panapotukia jina hili katika Biblia. Mabano yanatambulisha pamoja na lenyewe chemichemi Kaskazini mwa jangwa la Sinai lililo maarufu sana wakati wa kipindi cha Kutangatanga Jangwani (kama vile Hes. 13:26; 20). Kadeshi pia umetajwa katika Mwanzo 16:14, 20:1,14, na Hes. 13:26; 20:1,14, baadaye iliitwa "Kadeshi Barnea" (kama vile Hes. 32:8). Inavyoonekana huu ni mfano mwingine wa mhariri au mwandishi aliyeongeza taarifa (1) kutoka katika kipindi au (2) kama maelezo ya ziada ya ufafanuzi kwa maandiko yaliyopo au desturi za masimulizi ya kinywa/fasihi simulizi (kama vile Mistari ya 2,8,17).

◙ **"Wa Amaleki"** Kundi hili linaweza kuwa uzao kutoka kwa Essau (kama vile Mwanzo 36:15-16), aliyefanyika kama ishara ya uovu kwa Israeli kwasababu ya kuteka sehemu zisizo na ulinzi za nyuma ya uhamiaji wa Israeli (kama vile Kut. 17:8-16; Kumb. 25:17-19).

◙**"Waamori"** Angalia Mada Maalumu katika 12:6.

◙**"Hasason-tamari"** Kutoka II Nyakati. 20:2 hii inatajwa kama En-gedi, chanzo cha kipekee cha maji safi upande wa magharibi mwa Bahari ya Chumvi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:13-16**
**13 Mtu mmoja aliyeponyoka akaenda, akampasha habari Abramu Mwebrania; naye amekaa panapo mialoni ya Mamre, yule Mwamori, ndugu ya Eshkoli, na ndugu ya Aneri, na hao walikuwa wamepatana na Abramu. 14 Abramu aliposikia ya kwamba nduguye ametekwa mateka, akawapa silaha vijana wake, waliozaliwa katika nyumba yake, watu mia tatu na kumi na wanane, akawafuata mpaka Dani. 15 Akajipanga apigane nao usiku, yeye na watumwa wake, akawapiga, akawafukuza mpaka Hoba, ulioko upande wa kushoto wa Dameski. 16 Naye akarudisha mali zote, akamrudisha na Lutu nduguye na mali zake, na wanawake pia, na watu.**

**14:13 "Abramu Mwebrania"** Neno la "Kiebrania" (BDB 720) linaweza kutokana na

1. Aneri – uzao wa Shemu (kama vile 10:21) na Shela (kama vile 10:24). Jina linamaanisha "zaidi" (kama vile LXX) au "ukanda unaopita" (BDB 719). Ikiwa neno hili linamaanisha kundi la watu (kama vile 39:14), mfano mwingine wa kosa la kikronolojia unaoelezea uhariri wa baadaye au uandishi ulioboresha andiko.
2. Habiru – jina kwa wahamiaji wa-Semiti ya Milenia ya pili K.K; wa-Akkadia kwa ajili ya Waebrania (ABD, juzuu ya 3, ukurasa wa 6); jina lenyewe linamaanisha "wakimbizi."

Neno hili mara kwa mara huelezea Waisraeli mpaka wageni. Sura ya 14 ni ya kipekee katika matukio yaliyoandikwa ya maisha ya Abramu.

1. matumizi ya "Kiebrania" (BDB 720 I)
2. ikiunganishwa na jiji la Yerusalemu (Salemu)
3. matumizi ya cheo/wadhifa/sifa "Mungu Mkuu aliyetukuka" (kama vile 14:18,19,20,22)

**14:14** Inashangaza kwamba nguzu ya 318 (kujumlisha washirika) ingeweza kushinda jeshi lililounganishwa la wafalme wanne wa Tao la Ustawi (Fertile Crescent) (huu ni muujiza wa imani). Kushindwa huku kunamaanisha kufunua uwepo na nguvu ya YHWH pamoja na Ibrahimu (kama mistari ya 17-24 na 15:1 inavyoonesha vizuri). Hii ndiyo sababu tukio hili linaandikwa! Pia matumizi ya Abramu ya cheo cha "Melkizedeki" kunatambua shughuli za YHWH kupita/zaidi ya agano la Abramu. Wengineo (yaani Ayubu, Elihu) pia alijua na kumwabudu YHWH, lakini kwa jina tofauti (yaani *El Elyon*). Wito wa Abramu haukuwa tendo lenye ubaguzi, lakini njia ya kufunua YHWH kwa mataifa yote.

◙**"watu wenye mafunzo"** Ingawa huu ni muktadha wa kijeshi, neno hili (BDB 335) linamaanisha mafunzo ya kuchunga au mafunzo ya kichungaji. Kipengele cha kijeshi kinaweza kupatikana katika KITENZI "aliongoza" (BDB 937, KB 1227, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU), ambayo inaweza kuaksi mzizi wa lugha ya Akkadia, "kupigisha gwaride jeshi," ambayo inafuatia Vitabu vitano vya Musa vya Kisamaria na Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani.

◙ **"mpaka Dani"** Hii ni jambo lingine la jina la baadaye linalotumiwa. Dani (jiji) linamaanisha uhamiaji wa kabila la Dani kutoka katika eneo la Wafilisti kwenda mbali kaskazini katika Yoshua 19:40-48 na Waamuzi 18. Kidhahiri mhariri wa baadaye au mwandishi anafanya kuboresha!

**14:15** Toleo la UBS la *Handbook on Genesis* linatoa maoni mazuri hapa. "14:15 inaonesha 'kwamba Abramu hamkurejesha Lutu wakati wa usiku kwa kuvamia Dani, lakini baadaye tu katika Hobah" (ukurasa wa 319).

Mji huu/ukanda wa "Hobah" (BDB 295) ni kaskazini mwa Dameski na inatajwa hapa tu katika Biblia. Wafalme wavamizi na Abramu pamoja na washirika wake walisafiri umbali mrefu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:17-24**

**[17] Abramu aliporudi kutoka kumpiga Kedorlaoma na wale wafalme waliokuwa pamoja naye, mfalme wa Sodoma akatoka amlaki katika bonde la Shawe, nalo ni Bonde la Mfalme. [18] Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana. [19] Akambariki, akasema, Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi. [20] Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako. Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote. [21] Mfalme wa Sodoma akamwambia Abramu, Nipe mimi hao watu, na hizo mali uchukue wewe. [22] Abramu akamwambia mfalme wa Sodoma, Nimeinua mkono wangu kwa Bwana, Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi, [23] ya kuwa sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu wala cho chote kilicho chako, usije ukasema, Nimemtajirisha Abramu; [24] isipokuwa hivyo walivyokula vijana, na sehemu za watu waliokwenda nami, yaani, Aneri, na Eshkoli, na Mamre; na watwae wao sehemu zao.**

**14:17 "mfalme wa Sodoma"** Kwa hakika ni namna gani "mfalme wa Sodoma" anahusiana na mfalme wa Salemu hakuna uhakika. (Mstari wa 17 Unachukua migawanyiko ya mabaki ya vita vinavyoendelezwa katika mstari wa 21-24). Inanishangaza kwamba hata anatajwa (yaani Shemeberi, mstari wa 2) hata pia anatajwa. Inavyoonekana (1) alikuwa mshauri wa kiroho wa mfalme wa Sodoma au (2) hii ni muktadha unaounganisha matukio mawili tofauti. Salemu sio mji mmojawapo wa miji ya uwandani ambayo ilivamiwa (kama vile mstari wa 1-2). Kutokea mstari wa 23 Abramu alitaka wanted YHWH apokee sifa zote kwa ajili ya utajiri wake (kama vile mstari wa 20b) na hakumwamini kiukamilifu mfalme wa Sodoma.

◙ **"bonde la Shawe, nalo ni Bonde la Mfalme"** Neno "Shawe" (BDB 1001) linamaanisha "kuwa nyororo" (BDB 1000) na hapa yaweza kumaanisha uwanda. "Bonde la Mfalme" pia linatajwa katika II Sam. 18:18 na linaonekana kuwa bonde karibu na Salemu. Mahali lilipo hapajulikana (japo wengine wanafikiri ni Bonde la Kidroni), kama walivyo watu wengi na sehemu nyingi katika sura hii.

**14:18 "Melkizedeki"** Jina linamaanisha "mfalme wa haki" au "mfalme wangu wa haki" (BDB 575, sawasawa na Josh. 10:1; Zedeki inaweza kuhusiana na mungu wa anga wa Kanaani, Zedeki). Jina (Melkizedeki) linatokea tu hapa katika Zab. 110:4 katika Agano la Kale. Kifungu cha Zaburi ya 110 kilisababisha jamii ya magombo ya vitu vya majini kutegemea Masihi.

1. wa kifalme kutoka katika kabila la Yuda
2. wa kikuhani atokaye kabila la Walawi

Kitabu cha Waebrania cha Agano Jipya (yaani sura ya 7) kinatumia kuhani/mfalme wa Kanaani kama aina ya ukuhani mkuu.

1. uzao wake hautolewi
2. Abramu anatoa zaka kwake (mstari wa 20, ishara ya kukubaliwa na wakubwa)
3. yeye ni kiongozi wa jiji baaye linalokuwa Yerusalemu
4. yeye ni kuhani (sio kawaida kwa kipindi hiki, baba alifanyika kuhani kwa ajili ya familia, kama vile 31:54; Ayubu 1) kwa Mungu Aliye Mkuu (*El Elyon*, אלעליונ, kama vile mstari wa 19,20)

Kwa namna ya elimu ya utafsiri wa maandiko ya kiualimu wa kiyahudi waandishi wa Waebrania wanamtumia yeye kama aina/ishara ya kuhani bora kuliko Haruni.

◙ ***"Salemu"*** Mji maalumu ambao YHWH alichagua kwa ajili ya Jina lake kutamalaki unaendana na majina kadhaa katika Agano la Kale.

1. Salemu – jina la Kikanaani la mwanzo
2. Yebusi – jina la Kikanaani katika siku za Yoshua
3. Yerusalemu – ya siku za Daudi (angalia usambamba katika Zab. 76:2)

◙***"mkate na mvinyo"*** Hii ilikuwa kwa ajili ya Abramu na wengineo wote. Hii ilikuwa njia ya kumaanisha mahitaji muhimu ya maisha (kama vile Zab. 104:15). Wanaweza kuwa walikuwa na umuhimu wa kidini (yaani agano la chakula cha amani), lakini hii haina uhakika kutoka katika maandiko. Sio kivuli cha Meza ya Bwana. Kuwa mwangalifu na aina zisizofunuliwa na waandishi wa Agano Jipya waliovuviwa!

◙***"mvinyo"***

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHUSU KILEO NA ULEVI

I. Maneno ya Kibiblia
  A. Agano la Kale
    1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
    2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
    3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya," BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
    4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi huu unaongezwa katika ndni yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).
  B. Agano Jipya
    1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
    2. *Neos oinos* (divai mpya) – neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
    3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

II. Matumizi ya Kibiblia
  A. Agano la Kale
    1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
    2. Divai ni sehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
    3. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2;Mit. 31:6-7).
    4. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnon i– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amos 4).
    5. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
    6. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
    7. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).

1. Kipindi cha uwazi kati ya Agano laKale na Agano Jipya
2. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
3. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa yalevyayo yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya
1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima moja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Ulevi huleta majuto (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi
1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.
3. Waamini katika baadhi ya tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka iliyokusudiwa
1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote.
2. Mwanadamu amezitumia vibaya karama za Mungu kwa kuzifanyia kazi nje ya mipaka ya Mungu aliyoikusudia.

Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (kama vile Rum. 14:14,20)

**14:19-20** Tafsiri nyingi za Kiingereza zinawekea alama mistari hii kama ushairi.

**14:19 “Abramu na abarikiwe”** Hiki ni KITENZI kilekile (BDB 138, KB 159) kinachopatikana mara tatu katika Mwanzo 12:3. Maana yake ya kimsingi ni “kupiga magoti” au “kubariki.”

◙**“Mungu Mkuu”** Abramu, Melkizedeki, na Ayubu wote walimjua Mungu wa uumbaji kwa majina tofauti.
1. Abramu – YHWH
2. Melkizedeki – *El Elyon*
3. Ayubu– *Elohim*, *El*

Angalia Mada Maalumu katika 12:1.

◙ **“Mmiliki wa mbingu na nchi”** KITENZI (BDB 888, KB 1111, *Qal* KAULI ENDELEVU, kama vile mstari wa 22) inamaanisha “kumiliki” au “kufanya” (yawezekana kutoka katika mizizi ya konsonanti zinazofanana). Lugha hii ya kithiolojia imezoeleka katika dini za Mashariki ya Karibu (yaani mashairi ya kikanaani ya Ugaritiki); Ilikuwa ni njia ya kutambua mungu mkuu (inavyofanyiwa kazi na YHWH katika Zab. 115:15; 121:2; 124:8; 134:3; 146:6).

**14:20 “sehemu ya kumi ya vyote”** Huku ni kutajwa kwa mara ya kwanza kwa dhana ya kimahesabu ambayo inakua katika fungu la kumi katika Mambo ya Walawi (angalia Mada Maalumu inayofuata). Hii ni ishara juu ya upande wa Abramu kama njia ya kumshukuru YHWH kwa ajili ya ushindi na kutambua kwamba hakuwa mshindi! Kwa kutoa hili kwa Melkizedeki alikuwa anamtambua yeye kama mmoja aliyemjua kwa ukweli na kumtumia Mungu huyohuyo aliyemuita yeye kutoka Uri (kama vile mstari wa 22)

## MADA MAALUM: ZAKA KATIKA UTUNGAJI WA SHERIA YA MUSA

A. Maandiko ya rejea
   1. Kwa makuhani na Madhabahu kuu
      a. Law. 27:30-32
      b. Kumb. 12:6-7, 11, 17, 14:22-26
      c. Hes. 18:21-24
      d. Neh. 12:44
      e. Mal. 3:8, 10
   2. Kwa makuhani wa maeneo yao
      a. Kumb. 12:12; 14:27; 26:12-15
      b. Hes. 18:25-29 (Walawi lazima watoe zaka kwa madhabahu kuu)
      c. Neh. 10:37,38
   3. Kwa ajili ya maskini wa maeneo yao
      a. Kumb. 14:28-29
      b. Neh. 12:44

B. Mifano ya utoaji zaka unaotangulia utungwaji wa sheria ya Musa
   1. Mwanzo 14:20, Ibrahimu mpaka Melkizedeki (Ebr. 7:2-9
   2. Mwanzo 28:22, Yakobo mpaka YHWH

C. Zaka za Israeli zilitumika kusaidia madhabahu kuu lakini kila mwaka wa tatu zaka ya kitaifa ilielekezwa kwa maskiniwa maeneo husika.

Kibinafsi ninaamini "utoaji wa zaka" ni dhana ya Agano la Kale. Sifikirii kuwa ni kanuni ya Agano Jipya. Mjadala bora na wa pekee kuhusu utaratibu wa utoaji wa watu wa Mataifa waaminio unaandikwa katika II Wakorintho 8-9, inayoshughulikia zawadi ya wakati mmoja ya makanisa ya Mataifa kwa kanisa la Yerusalemu.

## MADA MAALUMU: UTOAJI WA ZAKA

Agano Jipya lina rejea chache kuhusu utoaji wa zaka. Siamini kuwa Agano Jipya linafundisha kuhusu utoaji wa Zaka kwasababu mazingira haya yote yako dhidi ya "utaftaji makosa" wa sheria za kiyahudi na kujihesabia haki( yaani Mt. 23:13-36). Ninaamini miongozo ya Agano Jipya kwa ajili ya kutoa mara kwa mara (ikiwa kupo kwa aina yoyote) kunapatikana katika II Wakorintho 8 na 9 (yaani ikirejea zawadi ya mara moja ya makanisa ya Mataifa kwenda kwa maskini wa kanisa mama la Yerusalemu), ambayo inakwenda zaidi ya kulipa zaka! Ikiwa Myahudi aliye na taarifa za Agano la Kale alikuwa ameamriwa kutoa asilimia kumi mpaka thelathini (kuna mbili, yawezekana tatu, aina za zaka zinazotakikana katika Agano la Kale: angalia Mada Maalumu: Zaka katika utungaji wa sheria ya Musa), hivyo wakristo lazima watoe sana zaidi na sio hata kuchukua muda wa kujadiliana kuhusu zaka!

Waamini wa Agano Jipya lazima wawe waangalifu juu ya kugeuza Ukristo katika utaratibu uliojikita katika utendaji wa kisheria (Christian Talmud). Shauku yao ya kumpendezesha Mungu iwasababishe wao kujaribu kutafuta miongozo kwenye kila eneo la maisha. Hatahivyo, kithiolojia ni hatari kuvuta kanuni za agano la kale ambazo hazijathibitishwa tena katika Agano Jipya (yaani Baraza la Yerusalemu la Mdo. 15) na kuzifanya kigezo cha kimafundisho ya madhehebu, na haswa wakati zinapokuwa zinadaiwa (na wahubiri wa kisasa) kuwa sababu ya machafuko au ahadi za utajiri (kama vile Malaki 3).

Hiii hapa ni nukuu nzuri kutoka kwa Frank Stagg, *New Testament Theology*, kurasa za 292-293:

"Agano Jipya kwa mara moja halitambulishi utoaji wa zaka katika neema ya kutoa. Utoaji wa zaka unatajwa mara tatu tu katika Agano Jipya:

1. Kuwakemea Mafarisayo kwa kwa kupuuzia haki, rehema na imani wakati wakijali kwa sana juu ya utoaji wa zaka mpaka wa mazao ya bustani (Mt. 23:23; Luka 11:42);
2. Katika kufunua Farisayo mwenye majivuno ambaye 'alikuwa akijiombea,' akijivuna kuwa alikuwa akifunga mara mbili kwa wiki na kutolea zaka kila mali zake (Luka 18:12);
3. katika kubishania hoja ya ukuu wa Melkizedeki, na hivyo wa Kristo, kwa Walawi (Ebr. 7:6-9).

"Ni wazi kwamba Yesu alikubaliana na utoaji zaka kama sehemu ya mfumo wa hekalu, kama katika kanuni na desturi za jumla za Hekalu na Sinagogi alizoziunga mkono, lakini hauna dalili kwamba alifanya lazima sehemu yoyote ya desturi za hekaluni juu ya wafuasi wake. Zaka kwa sehemu kuu zilikuwa za mazao, hapo kabla zililiwa katika madhabahu na yule anayetoa zaka na baadaye kuliwa na makuhani. Zaka kama inavyoanzishwa baadaye katika Agano la Kale ingeweza kubebwa nje tu katika mfumo wa kidini uliojengwa kuzunguka mfumo mzima wa dhabihu za wanyama."

"Wakristo wengi wanaona zaka kama mpango sawa na unaotekelezeka kwa ajili ya utoaji. Ikiwa haitofanywa kuwa jambo la lazima au mfumu wa kisheria, inaweza kuthibitishwa kuwa mpango mzuri. Hatahivyo mtu anaweza asidai kihaki kwamba utoaji wa zaka unafundishwa katika Agano Jipya. Unatambuliwa kama utaratibu wa kuangaliwa sahihi wa Kiyahudi (Mt. 23:23; Luka 11:42), lakini hauwi wa lazima juu ya Wakristo. Kusema ukweli, sasa haiwezekani kwa Wayahudi au Wakristo kutoa zaka katika namna ya Agano la Kale. Kutoa zaka leo kwa kufifia tu kunafanana na taratibu za kiibada zilizokuwa zikifanyika juu ya mfumo wa kidhabihu za Wayahudi."

Stagg anahitimisha:

"Wakati mengi yanaweza kusemwa kwa kuuchukua utoaji wa zaka kama kutoa kwa hiari kama kipimo cha utoaji wa mtu bila kwa mkao wa kulazimisha juu ya wengine kama matakwa ya Kikristo, ni wazi katika kufanya taratibu hizi kwamba mtu habebi utaratibu wa Agano la Kale. Wakati mtu anafanya kitu Fulani kidogo anakuwa anahusianisha na taratibu za utoaji wa Ahgano la Kale, ambayo ilikuwa ni kodi kusaidia hekalu na mfumo wa makuhani, jamii na mfumo wa kidini ambao haupo tena. Zaka zilikuwa ni lazima katika dini ya Kiyahudi kama kodi mpaka uharibifu wa Hekalu katika mwaka wa 70 B.K, lakini hawafunganishi hivyo kwa Wakristo.

"Hii sio kukosoa utoaji wa zaka lakini ni kufafanua uhusiano wake kwa Agano Jipya. Ni kukataa kwamba Agano Jipya linasaidia ulazima, kuwekeana sheria, nia ya kutengeneza faida na maelewano ya kimatoleo ambavyo mara kwa mara vinaweka tabia ya ukataji rufaa wa utoaji zaka siku za leo. Kama mfumo huru, utoaji zaka unasaidia mengi; lakini lazima ukombolewe kwa neema ikiwa unataka uwe wa kikristo. Kuomba kwamba 'unafanya kazi' ni kufanyika kuwa majaribio ya kinadharia ya kivitendo ya kiulimwengu. 'Kusumbukiwa' sana huo sio ukristo. Utoaji zaka, ikiwa unataka uwe wa kupendeza, lazima uwe katika mizizi ya neema na upendo wa Mungu."

**4:21** Mtu anaweza kushangaa ikiwa "zaka" ya mstari wa 20 ni sehemu ya mjadala baki wa mstari wa 21. Kuna mkanganyiko katika muktadha.

1. Mistari ya 17, 21-24 inahusiana na mfalme wa Sodoma na mabaki
2. Mistari ya 18-20 inahusiana na zaka za mabaki kwa mfalme wa Salemu

**14:22** Tazama namna gani Abramu analinganisha majina na uungu.

1. YHWH
2. *El Elyon* hivyo na kuwatambua kama wao kama mmojawapo wa uungu

**14:23 “sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu wala cho chote kilicho chako”** Lugha hii ya kisitiari ni ya aina yake (kama vile NIDOTTE, vol. 3, ukurasa 120) ya Mashariki ya karibu ya kale (kama vile Mwanzo 23). Ni nahau kwa ajili ya “kutochukua kitu” Mavazi yalikuwa moja ya mabaki ya vita. Abramu alitaka kuweka wazi kabisa kikamilifu, hakuwa anaingia au hakuwahi kuwa katika uhusiano wa kiagano pamoja na mfalme wa Sodoma.

**14:24** Hii ni orodha ya majirani wa Abramu waliomsaidia katika vita na ambao walistahili wapewe/wapate mabaki.

# MWANZO 15

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Abramu anaahidiwa Mwana | Agano la Mungu na Abramu | Agano la Abrahamu na Sara | Agano la Mungu na Abramu | Ahadi ya Kiungu na agano |
| 15:1-11 | 15:1-11 | 15:1-6 | 15:1 | 15:1 |
| (1) | | | | (1) |
| | | | 15:2-3 | 15:2-6 |
| | | | 15:4-5 | |
| | | | 15:6 | |
| | | 15:7-11 | 15:7 | 15:7-11 |
| | | | 15:8 | |
| | | | 15:9-11 | |
| 15:12-16 | 15:12-16 | 15:12-16 | 15:12-16 | 15:12-16 |
| 15:17-21 | 15:17-21 | 15:17-21 | 15:17-21 | 15:17-21 |
| (18) | (18) | | | (18) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibilia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.K

## HISTORIA YA NYUMA

A. Sura ya 15 ni mlolongo wa majaribu na masharti ambayo Mungu alimpa Ibrahamu kwenye sura ya 12 mpaka 22 (kama vile 12:1-3; 14:12-14; 15:1-18; 17:1-5; 22:16-18). Sura ya 15 inaelezea matendo ya YHWH katika sura ya 14. YHWH alikuwa ushindi wa Abramu. Tumaini la Abramu liko katika ahadi ya YHWH, iliotolewa mwanzoni katika sura ya 12, lakini ikarudiwa mara nyingi (kama vile sura ya 12, 15, 17, 18, 22).

B. Inafurahisha kutambua kwamba tamko la agano katika sura ya 12 na 17 zimeelezea masharti, wakati sura ya 15 na 22 kwa wazi hazina masharti. Mambo yote ya mwanadamu yanayoshughulikiwa na Mungu yanatokana na huruma, na tabia zake zisizobadilika na upendo wake aliouanzisha, ingawa, Mungu pia amekusudia kuwa mwanadamu aliye mtengeneza kwa sura yake lazima aitikie kwenye pendo lake kwa toba, imani, utii, na ustahimilivu. Masharti haya ni ya muhimu, sio tu katika kitabu cha Mwanzo, bali katika Biblia nzima.

C. Ni muhimu kuwa tunaona kote Mungu alipokuwa akishughulika na Abramu kwamba neema yake, wala sio faida ya mwanadamu,bidii, au utajili, imesisitizwa tena na tena. Dhima hii ikaja kuwa kitovu cha wazo la kitabu cha Mwanzo. Hata hivyo, wito muhimu wa imani na ushirika ulikokuwa ukihitajika na Abramu pia ulisisitizwa (kama vile 22:16,18)! Paulo alitumia hili kama kielelezo cha Mungu kushughulika na mwanadamu mwenye dhambi. Ukweli halisi ni kwamba angali/atafanya kwa mshangao mkubwa!

D. Sura hizi za ufunguzi za kitabu cha Mwanzo ni za muhimu katika uelewa wa ulimwengu wetu na mahitaji yetu ya kiroho. Mwanzo 1-3 inaweka vipindi kwa ajili ya hali ya binadamu.
   1. Alimtengeneza kwa sura ya Mungu kwa ajili ya ushirika (1:26-27)
   2. Akaasi dhidi ya uongozi wa Mungu (3:1-7)
   3. Mbali na gharama za uasi wa mwanadamu (3:8-20)
   4. Ahadi ya Mungu ya ukombozi (3:15)

   Kiukweli kila kitu tokea Mwanzo 3 mpaka ufunuo 20 ni matengenezo ya Mungu kuhusu gharama ya dhambi ya Adamu na Hawa. Mbingu zimeelezewa katika Ufunuo 21-22 kama urejesho wa bustani ya Edeni. Sura ya ufunguzi ya kitabu cha Mwanzo inaelezea binadamu wote.
   1. Adamu
   2. Nuhu
   3. Abramu (kama vile 12:3; Mdo. 3:25; Gal. 3:8) Mungu alimchagua mtu mmoja ili kuwachagua watu wote! Uchaguzi wa Mungu hujumuisha ahadi (yaani agano lisilo na masharti) pamoja na mwitikio (yaani., agano lenye masharti). Maisha ya Abramu yanaonyesha athari za dhambi na neema. Anashughulika na utii na imani. Kutokana na mgongano huu, wote wameitwa (Abram ni kielelezo cha imani/dhambi/mashaka/kuamini, kama vile Warumi 4; Wagalatia 3).

E. Mstari wa 6 ni wa muhimu kwenye thiolojia ya Agano Jipya. Unaonekana kuwa hoja au hitimisho la habari nzima ya Abramu. Alikuwa Musa au wazee wa kale waliohitimisha hili (yaani Yakobo)? Suala si kwamba ni nani, lini, au namna gani maandiko yalitokea, bali ni ukweli wa Mungu au mtizamo wa mwanadamu? Hapa ndipo penye madhanio ya mamlaka (yaani., uvuvio) yanapoingia. Mara zote watu wenye dhambi ndio hutafuta kuwepo kwa Mungu na baadaye kutafuta habari zaidi kuhusu Yeye katika maandiko. Habari za maandiko ni kwa ajili yetu wale ambao hatujawahi kumwona Yeye! Huleta msingi na chanzo cha imani chenye kutafuta kuelewa. Maisha ya Abramu ni kielelezo cha waamini wote(watakatifu wa agano la kale na watakatifu wa agano jipya). Unaposhughulika na simulizi za kihistoria, mtu lazima aendelee kuuliza, "kwa nini hizi kumbukumbu (angalia Fee and Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 15:1-11**
**[1]Baada ya mambo hayo neno la Bwana likamjia Abramu katika njozi, likinena, Usiogope, Abramu, Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana. [2]Abramu akasema, Ee Bwana MUNGU, utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto, na atakayeimiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdameski? [3]Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu. [4]Nalo neno la Bwana likamjia likinena, Huyu hatakurithi, bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi. [5]Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. [6]Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki. [7]Kisha akamwambia, Mimi ni Bwana, niliyekuleta kutoka Uru wa Wakaldayo nikupe nchi hii ili uirithi. [8]Akasema, Ee Bwana MUNGU, nipateje kujua ya kwamba nitairithi? [9]Akamwambia, Unipatie ndama wa miaka mitatu, na mbuzi mke wa miaka mitatu, na kondoo mume wa miaka mitatu, na hua, na mwana njiwa. [10]Akampatia hao wote, akawapasua vipande viwili, akaweka kila kipande kuelekea mwenzake, ila ndege hakuwapasua. [11]Hata tai walipotua juu ya mizoga Abramu akawafukuza.**

**15:1** Ni vigumu kuelewa ni wakati gani wa kutafasiri andiko kama lugha ya mjazo au ushairi. Alama tu ya kimaandiko ni "mapigo ya wimbo" (yaaani., vifungu vyenye lafudhi), lakini haya ni maendeleo ya sasa. Mstari wa 1 umetafasiriwa kama ushairi katika matolea ya NASB, JPSOA, NJB, NIV, lakini kama mjazo wa lugha katika matoleo ya NKJV, NRSV, TEV, na REB. Utata huu wenye kufanana unaonekana katika 14:19-20.

Kifungu “baada ya mambo haya” ni chenye utata na cha kujirudia (kama vile 22:1; 22:20; 39:7; 40:1; 48:1). Simulizi za mtu zimeunganishwa pamoja kwenye kitabu cha Mwanzo katika muundo wa kihistoria wa Mashariki, na sio Magharibi ya sasa, katika utaratibu wa muda. Angalia makala: Uandishi wa Historia ya Agano la Kale Ukilinganisha na Tamaduni za Kisasa za Mashariki ya Karibu.
Hili ni moja kati ya (kama vile mst.4) matukio katika kitabu cha Mwanzo wa hiki kifungu kilichozoeleka (yaani., “Neno la Mungu likaniijia …….” Kama vile mst.4), ambacho kinapatikana kwa manabii wote. Kinasisitiza kuwa YHWH alimwelezea Ibrahamu, inavyoonekana kwa namna ya kuweza kusikika (BDB 55). Kwa namna habari ilivyo inaonyesha ilikuwa ni maono ya usiku. Angalia ujumbe katika 15:1c Hapa chini.
Abramu anachaguliwa kama mtu mwenye kuyapokea maono ya ki-Ungu. Kanuni za kiutangulizi ni za kawaida kwenye nyaraka za manabii, lakini adimu kabla yao. Hata Abramu aliitwa “nabii” (BDB 611) katika 20:7. Manabii waliyaandika maandiko. Mara zote imekuwa nadharia yangu kuwa Musa mwandishi mmoja na pekee wa sehemu za mwanzo wa kitabu cha Mwanzo, bali alikuwa ni muunganishaji/mhariri. Sanamu katika Mwanzo 1-2 ni za huko Mesopotamia, na sio Misri. Hakuna maneno ya ki-Misri yaliyokopwa yanaonekana mpaka kwenye maisha ya Yusufu. Nafikiri Yusufu alitumia mapokeo ya kusimuliwa kwa mdomo au ya kuandikwa yakiandikwa enzi za Abramu (yaani., wazee wa umri mkubwa). Alikuwa ni mwenye kuyakusanya pamoja maandiko na kuyahariri kwa muda mrefu wa historia ya awali. Waandishi wa kibinadamu wanatumia tamaduni zao na misamiati, lakini ujumbe ni wa kutoka kwa Mungu (yaani., uvuvio).

◙**“Bwana”** Neno YHWH ni muundo wa KITENZI cha Kiebrania, cha neno “kuwa” (kama vile Kut. 3:14). Kinaonekana kusisitiza kuwa Mungu wa milele, pekee aliyepo. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanadai kuwa pindi Mungu anaelezewa kuwa YHWH, inazungumzia kuhusu huruma na akiongelewa kama *Elohim* wanazungumzia kuhusu uwezo wake kama muumba. Napenda hii nadharia zaidi kuliko nadharia ya“JEDP” chanzo cha ukosoaji, ambayo ilikuwa maarufu sana katika karne ya 18 - 20. Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 12:1.

◙ **“katika maono”** Hii inadokeza kuwa ilikuwa ni usiku, ambapo pia inaungwa mkono na mst. wa 5. maudhui ya sura ya 15, hasa mstari wa 12, haijulikani kama maono haya yalikuja usiku mmoja au kama yaliendelea kwa siku mbili (yaani., maono mara mbili, mistari ya 1-6,7-21). Neno “maono”(BDB 303) linalopatikana hapa ni tofauti na lile “likanijia”(BDB 906) linalopatikana katika 12:7. Neno hili hapa ni adimu, linapatikana tu katika sura 3 za Biblia, Mwa. 15:1; Hes. 24:4, 16; na Ezek. 13:7.

Toleo la NIDOTTE, juzuu ya 4, uk. 354, lina muhtasari unaofurahisha wa namna YHWH anajidhihirisha Mwenyewe katika kitabu cha Mwanzo.
1. Kwa maneno (BDB 55) – 12:1-3; 13:14-17; 21:12-13; 22:1-2
2. Kwa maono – 15:1-6 (BDB 303); 46:2-4 (BDB 909 I)
3. Kwa ndoto – 20:3-7 (BDB 538); 28:12-15 (BDB 321); 31:10-13 (BDB 321), 24 (BDB 538)
4. Mungu kumtokea mtu, (hasa “kumtokea,” BDB 906) – 12:7; 17:1; 18:1; 26:2,24; 35:1,9; 48:3
5. Kwa malaika wa YHWH (angalia Mada Maalum katika 12:7) – 16:7-13; 21:17-19; 22:11-12,15-18; 31:11

Njia zinatofautiana , lakini mafunuo anzilishi ya Uungu yanamkabiri mwanadamu, sio kwa niaba ya watu

◙ **“usihofu, Abram”** KITENZI hiki (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU kimetumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO) inajirudia katika Mwanzo (kama vile 15:1; 21:17; 26:24; 46:3). YHWH anajua dhambi imesababisha mioyo yetu kuogopa (kumhofu Yeye, kuogopa maisha, kuogopana sisi wenyewe). Kinatumika mara ya kwanza katika Mwanzo. 3:10 kwa Adamu na Hawa kumhofu Mungu baada ya kutenda dhambi. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa hofu hii inahusiana na sura ya 14, hasa (1) hofu ya vita; (2) hofu ya kisasi kwa taifa husika hasa baada ya kumuua mfalme; au (3) hofu ya Mungu kwa sababu amechukua maisha ya mwanadamu. Hata hivyo, kutokana na muktadha wa sura ya 12 mpaka 15 inawezekana kuwa hofu imehusianishwa na hali endelevu ya Abram ya kutokuwa na mtoto.

◙ **“Mimi ni ngao yako”** Hili neno “ngao”(BDB 171) ni neno la kijeshi likitenda kazi kama sitiari kwa ajili ya “mlinzi” au “mtoaji” (kama vile Zab. 3:3; 28:7; 33:20; 84:9; na 91:4). Neno “ngao”kiuasilia linahusiana na neno

"kombolewa" (BDB 171, kama vile 14:20). Kwa ajili ya maelezo mazuri ya neno "ngao" angalia Kumb. 33:29. Napendelea tafasiri ya Luther juu ya toleo la New American Standard Bible kwa vile linadokeza kuwa "ngao" na "thawabu" ni vya Mungu mwenyewe—"Mimi ni ngao yako na thawabu yako" (kama vile toleo la NKJV). Hakuna KITENZI kilichoongelewa katika kifungu hiki.

◙ **"Thawabu yako itakuwa kubwa"** Abramu amekuwa akijaribiwa kwa ajili ya shauku wa kuwa na utajiri na kuiharibu katika 13:8- 13 na 14:21-24 na alikataa fursa ya mali. Mungu amekwisha kuahidi katika sura ya 12 kwa vyote uzao na ardhi. Hata hivyo, katika mwendelezo wa kuthibitisha ahadi za Mungu , Mungu mwenyewe ndiye mmiliki mkubwa wa Abramu (kama alivyokuwa kwa Walawi Hes. 18:20; Kumbukumbu 10:9).

**15:2 "Oh Bwana Mungu"** Hii ni mara ya kwanza kuwa muunganikano wa haya majina ya ki-Ungu yanaonekana pamoja katika Biblia. Linatokea katika kitabu cha Mwanzo na mst. 8. Kiuhalisia "*Adonai* ni YHWH." Tuweza kuyaona majina haya katika Kumb. 10:17. Neno *Adonai* ( "Bwana wangu," linatumika katika fasihi za Wakanani, na sio lugha zingine za Kisemiti) linaonekana kufanana kwa karibu na neno *Kurios* katika Agano Jipya, ambalo linadokeza "bwana," "mme," "mmiliki," au "Bwana." Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 12:1. Kuna majina mbalimbali ya Uungu ambayo yanajumuisha majina mawili. Hata hivyo,

1. YHWH *Elohim* – Mwanzo 2:4
2. *Adonai* YHWH – Mwanzo 15:2

Ingawa mara mara nyingi hutafasiliwa kwa namna ile ile katika Kiingereza, yanatofautiana katika maana na msisitizo.

◙ **"utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto "** Hoja muhimu ya Abramu ilikuwa ni kuendelea kutokuwa na mtoto. Uhusika wake uliegamia juu ya ahadi ya awali katika 12:1-3. Watu wa kale waliliona suala la kutokuwa na mtoto kama laana toka kwa Mungu, na bado Mungu alikuwa akimthibitisha Abramu kama mpokeaji wa fadhila maalum. Abramu alikuwa akitafuta udhihirisho wa wazi wa hizo fadhila alizoahidiwa.

◙ Neno "kutokuwa na mtoto" (BDB 792) ni neno adimu. Limetumika mara nne tu.

1. Kuhusu Abramu (na sio Sarai) – Mwa. 15:2
2. Kama adhabu kwa ajili ya kujamiiana – Law. 20:20,21
3. Kiujumla Yehoakimu aliposhindwa kumweka mmoja wa wanae kwenye kiti cha ufalme – Yer. 22:30

◙ **"na atakayeimiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdameski"** Kuna mchezo juu ya neno adimu la Kiebrania "mrithi" (משק, ambalo laweza kumaanisha "kupata" au "kumiliki" (BDB 606, NIDOTTE, juzuu 2, uk. 971) na neno "Dameski" (דמשק, BDB 199). Linatamkwa vile vile katika lugha ya Kiebrania. Baadhi wanaliona hili kama lenye kufanana na uasili wa mila ya Kihuri yaliopatikana katika vigae vya Nuzi katika karne ya pili K.K. baadhi wanafikiri kuwa "Eliezeri" (BDB 451), ambalo linamaanisha "Mungu ni msaada,"ni mtumishi aliyetajwa katika 24:2. Neno (BDB 606) linalotafasiliwa "mrithi" ni neno adimu. KITENZI cha kawaida kwa ajili ya neno "mrithi" (BDB 439, KB 441) kinapatikana katika mistari ya 4,5 (mara mbili), 7,8. Yote yanamaanisha "kuchukua umiliki wa." Kifungu hiki kimeelezewa kwa mst.3.

**15:3 "tazama, hakunipa uzao"** Abramu, kwa namna ya kujirudia, inaonyesha shauku aliokuwa nayo. Abramu ni mfano mzuri wa imani uliochanganyikana na mashaka. Abramu alimwamini Mungu, lakini hii haijalishi kuwa hakuwa na maswali kuhusu baadhi ya ahadi zake. Mungu hamchukii mwenye maswali mwaminifu! Mungu angalimleta kupitia mfururizo wa majaribu mpaka pale Abramu atambue kuwa umiliki wake mkubwa ulikuwa Mungu mwenyewe (hasa sura ya 22).

**15:4 "bali atakayetoka katika viuno vyako"** Lazima ikumbukwe kuwa bado ni miaka ishirini na tano inayokuja. Hadai haswa kuwa mtoto atatoka kwa Abramu, lakini haimaanishi kuwa atatoka kwa Sarai. Hii ndio sababu ya matatizo yanayopatikana katika sura ya 16. Kifungu kilichotafasiliwa "kutoka katika viuno vyako" kiuhalisia ni "katika viungo vyako." Neno hili (BDB 588) linatumika kwa maana mbalimbali.

1. Utumbo mdogo – II Sam. 20:10; II Nya. 21:15

2. Tombo – Ayubu 20:14; Ezek. 3:3; 7:19; Yona 1:17; 2:1; II Sam. 7:12; 16:11
3. Viungo vya uzazi
    a. Vya kiume – Mwa. 15:4
    b. Vya kike – Isa. 49:1 4. Mahali halisi pa mihemko ya mwanadamu – Wimbo ulio bora 5:4,14; Isa. 16:11; 63:15; Yer. 4:19; 31:20; Wimb. 2:11

**15:5 "Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu"** Mungu anamweleza Abramu kwa matamko mawili.

1. Angalia – BDB 613, KB 661, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. Hesabu – BDB 707, KB 765, *Qal* KAULI SHURUTISHI baraka za mungu ni nyingi na tele (kama vile 12:2; 17:2).

Mungu anatumia sitiari mbalimbali ambazo Abramu angalikuwa akizijua kuelezea utele wa uzao wake.

1. mavumbi (kama vile Mwa. 13:16; 28:14; Hes. 23:10)
2. nyota (kama vile Mwa. 15:5; 22:17; 26:4)
3. mchanga (kama vile Mwa. 22:17 na 32:12) kutokana na ahadi ya 12:3 na dhana ya "ufalme wa kikuhani" (kama vile Kut. 19:5-6) kwa unabii wa kiulimwengu wa Isaya (kama vile 42:6; 49:6; 51:4), familia ya Ibrahamu ingalikuwa kubwa zaidi kuliko yeyote aliyeifikilia. Ingalijumuisha wa mataifa wanaoamini. (kama vile Luka 2:32; Mdo 13:47; 26:23; Rum. 2:28-29; 4; Gal. 3:7-9,29).

**15:6 "akamwamini Bwana"** Hii sio kumaanisha kuwa Abramu hakuamini tena katika sura ya 12, kwa vile aliondoka Uru na kumfuata Mungu. Lakini, neno"akamwamini" (BDB 52, KB 63, *Hiphil* KAULI TIMILIFU, ambayo inaonyesha maisha ya imani, sio tu kwa tendo hili) ni kutoka kwenye mzizi wa neno אמן, pale tunapopata neno "amina." Mzizi wa neno unamaanisha "kuwa imara" au "kumtegemea." Ibrahamu aliweka imani yake kamili katika ahadi ya Mungu kuwa angalipata uzao. Kilikuwa ni kitendo cha imani pasipo kuangalia (kama vile 22:16,18; Ebr. 11:1). Abramu alimbeba Mungu katika neno lake, kwa imani, pasipo kuhitaji ishara ya kuonekana. Hili haswa ni la muhimu kwa sababu hii ikaja kuwa ndio msingi wa hoja ya Paulo ya kuakifishwa kwa neema kupitia imani inayopatikana katika Warumi 4 na Wagalatia 3. Pia Paulo ulitumia Hab. 2:4 katika Rum. 1:17; Gal.3:11 na mwandishi wa Ebr. 10:38. Inaonekana kuwa kiini cha neno ni "Ibrahamu kumtegemea YHWH na sio yeye mwenyewe."katika sehemu yote ya kitabu cha Mwanzo inasisitizwa tena na tena kuwa ni Mungu mwenyewe mwanzilishi wa upendo, na sio rasilimali za mwanadamu, zinazohitajika kwa ajili ya wokovu. Neno "akamwamini"linaweza kutafasiliwa kwa maneno matatu ya Kiingereza: kusadiki, kuamini na imani (kama vile Kut. 4:5,31; Kumb. 1:32; II Nya. 20:20; Isa. 43:10, linahusiana na Masihi katika Isa. 28:16 na linarejelea kutokuamini katika Hes. 14:11; 20:12; Kumb. 9:23; II Fal. 17:14; Zab. 78:22). Inaonekana kuwa kiini cha neno linalopatikana katika Agano la Kale "imani" au "kuamini," ambalo haliangazii kwetu, bali katika uaminifu wa Mungu na ahadi zake. Tambua Abraham aliamini

1. katika Bwana(uhusiano binafsi)
2. katika neno lake(ufunuo wa neno)

yamekuwa ya msaada kwangu kuainisha imani ya kibiblia kama

1. imani ndani ya mtu(YHWH/Kristo)
2. imani ndani ya ukweli kuhusu mtu huyo(Biblia)
3. kuishi maisha yanayofanana na mtu huyo(utii wa agano la kale/ufanano wa Kristo)

yote matatu ni ya muhimu, sio ya kiuchaguzi!

## MADA MAALUM: KUAMINI, TUMAINI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE.

I. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

A. Watu binafsi na jamii

B. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

A. Ibrahim na uzao wake

B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

II. Asili kuu iliyotumika

A. ןמא (BDB 52, KB 63)

1. KITENZI

a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)

b. Shina la neno *niphal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu

1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14

2) Kwa vitu, Isa. 22:23

3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5

c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini

1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6

2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)

3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24

4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9

5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16

6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12

2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)

3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno "amina" katika agano la kale na agano jipya.

B. תמא (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli

1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1

2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8

3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16

C. הנומא (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu

1. Katika mikono, Kut. 17:12

2. Katika muda, Isa. 33:6

3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2

4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale

A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).

B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (ןמא).

1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.

2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa

a) Rum. 9:33 "aibisha" au "katisha tamaa"

b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu

3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale

A. Petro anaunganisha
1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
3. Zab. 118:22 – 1 Pet. 2:7 (jiwe lililokataliwa)

B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama "jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe" toka
1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
2. Isa. 61:6; 66:21
3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1 Petro. 2:5,9)

1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii

A. Utumiaji wake

Neno "akaamini" linatokana na neno la Kiyunani *pisteuō* ambalo pia laweza kutafasiliwa " kuamini," "sadiki," au "imani." Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili "kuamini" unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. *eis* inamaanisha "ndani ya" muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
   a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
   b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
   c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
   d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
   e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
   f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
   g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mk 1:15; Mdo 5:14
3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti*, likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
   a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
   b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
   c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
   d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
   e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
   f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)

g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

V. Hitimisho

A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
3. Utii
4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)

B. Imani ya Kibiblia ni
1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya” inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!
Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

◙ **“akamwesabia jambo hili kuwa haki”** Neno “kumuhesabia” (BDB 362, KB 359, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU) laweza kumaanisha “kuhesabia” au “kumfikiria.”linatumiwa mara nyingi na makuhani katika kuhusiana na dhabihu ( Law. 7:18; 17:4; na Hes. 18:27). Kama mtu akileta dhabihu kwa kuhani, dhabihu ilihesabiwa kwa niaba yake mwenyewe. Mungu alimwesabia Abramu haki, hivyo kumkubali moja kwa moja.

◙ **“kama mwenye haki”** Neno hili (BDB 842) mwanzoni lilimaanisha “futi kamba” na kwa hiyo likaja kuwa likirejea kipimo cha kawaida. Mungu mwenyewe ndio kipimo kamili, kwa hiyo, mengi ya maneno ya Kiebrania na Kiyunani kwa ajili ya “dhambi”yanamaanisha kuchepuka toka kwenye kipimo cha haki ya Mungu. Neno hili limeendelea katika maana yake.

1. Kumaanisha asili ya uadilifu wa Mungu kama unavyoweza kuonekana wazi katika manabii wa karne ya nane
2. Likaja kumaanisha msaada wa Mungu kwa wasio na msaada (kama vile Zab. 10:16-18 na 72:12). Dhana hii imeendelea kujengeka hata katika siku za Yesu kwa utoaji sadaka kwa wasiojiweza (kama vile Mt. 6:1)
3. Utumiaji mkubwa wa mwisho wa neno hili “haki” linatumika kwa wokovu wa kiroho. Hili limeonekana katika Isaya 40-55 na utumiaji wa Paulo katika Agano Jipya. Paulo anaongea kuhusu haki yetu kwa Mungu inayotokana haswa na pendo la Mungu na mwitikio wetu wa imani katika Rum. 4:3 na Gal. 3:6
4. Tunaweza kuona mwendelezo wa kulitumia neno hili katika Yak. 2:14-16

Hapa neno limetumika si kwa maana ya “kutotenda dhambi,” bali kwamba kuamini kwa Abramu katika ahadi za YHWH zimefungua mlango kwa ajili ya mwendelezo wa uhusiano wa imani. Hili halikuwa tendo la kwanza (au la mwisho) la Abramu la kuendelea kumwamini YHWH. Mapokezi ya Abramu kwenye ahadi za YHWH ziliruhusu ushirika wa ndani kuendelea kuwepo na kudumu.

## MADA MAALUM: HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (KITENZI, BDB 842, KB 1003; NOMINO JINSI YA KIUME, BDB 841, KB 1004; NOMINO JINSI YA KIKE, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kisitiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

A. <u>kutangaza</u> haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
B. <u>kwa kutoa haki</u> huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
C. <u>kumtoa</u> Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
D. <u>kurejesha</u> ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

A. Toba
B. Imani
C. Utii kwenye stadi ya maisha

D. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

lli kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
    a. Warumi 3:26
    b. 2 Wathesalonike 1:5-6
    c. 2 Timotheo 4:8
    d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
    a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    b. Mathayo 27:19
    c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
    a. Mambo ya Walawi 19:2
    b. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki

a. Warumi 3:21-31
b. Warumi 4
c. Warumi 5:6-11
d. Wagalatia 3:6-14
e. Iliyotolewa na Mungu
    a. Warumi 3:24; 6:23
    b. 1 Wakorintho 1:30
    c. Waefeso 2:8-9
f. Iliyopokelewa kwa imani
    a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
    b. 2 Wakorintho 5:7,21
g. kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11

5. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
    c. Waefeso 1:4; 2:10
    d. 1 Timotheo 6:11
    e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    f. 1 Yohana3:7
    g. 1 Petro 2:24
6. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
    a. Matendo 17:31
    b. 2 Timotheo 4:8
7. Kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11
8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi wake wawe watakatifu
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi2:13; 5:1-5; 6:1-23
    c. Waefeso 1:4; 2:10
    d. 1 Timotheo 6:11
    e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    f. 1 Yohana 3:7
    g. 1 Petro 2:24
9. Mungu atauhukumu ulimwengu kwa haki
    a. Matendo 17:31
    b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni tabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

A. agizo la Mungu
B. zawadi ya Mungu
C. tendo la Kristo

D. ni maisha yapaswayo kuishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

A. injili ni mtu (msisitizo wa Kanisa la Mashariki na ufuasi wa Calvin)
B. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msisitizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

**15:7 "Mimi ni Bwana"** Huyu ni YHWH, ni jina maalum la agano kwa ajili ya Uungu. Angalia Mada Maalum katika 12:1.

◙ **"niliyekuleta toka katika Uru wa Wakaldayo"** Kuna baadhi ya vitu vya kutokukubaliana kuhusu mahali sahihi ambapo Mungu aliongea na Abramu. Huenda ilikuwa Uru au Harani. Linganisha Mwa. 11:31-12:1 na Neh. 9:7 na Mdo. 7:2. Baadhi hata wanadai kusema kuwa Mungu aliongea na Tera, baba yake Abramu, huko Uru na Abramu huko Harani, lakini nafikiri huu sio uelewa sahihi. Ni hakika inawezekana kuwa maono yalikuja pote akiwa Uru na Harani. Pia, kwa mantiki hii, ningependa kutaja kwa usahihi kitabu cha Mwanzo na Kumbukumbu la Torati vinapofaa kwenye tamaduni za karne ya pili K.K, hasa hasa kanuni za mkataba wa Wahiti/Suzereine. Hizi nyaraka za kihistoria, pamoja na vigae vya Nuzi na Mari, zimetuonyesha ni kwa namna gani zinafaa kitamaduni katika kur. Za 2,17,57 na 16:2 zikiwepo katika siku zao. Uhalisi wa matukio ya wazee wa kale umethibitishwa wazi kwa upatikanaji wa mambo ya kale. Kama ilivyo katika sura hizi za mwanzo wa kitabu cha Mwanzo, majina ya miji ya mwanzo na nchi yametumika. Jina Wakaldayo halitumiki kwa ajili ya watu wa Mesopotamia (yaani Babeli ya Kusini) mpaka karne ya sita K.K.. Waandishi wa Uyahudi walifundishwa huko Misri, ambapo waandishi walijisikia huru kuyafanya maandiko kuwa ya kisasa kwa jinsi walivyoendele kuyadurufu. (haikuwa hivyo kwa waandishi wa Mesopotamia).

**15:8 "nipateje kujua ya kwamba nitairithi"** Abramu, ambaye imani yake imehesabiwa kama haki katika mst.6, sasa anaelezea hitaji lake kwa ajili ya kuthibitishwa (kama vila kur. za 2-3). Hili ni la muhimu kithiolojia. Mungu alikumkubali Abramu, sio kwa ajili ya imani yake thabiti, bali kwa sababu ya pendo thabiti la Mungu. Hata alipokuwa katikati ya mashaka bado Mungu alimwamini na, hata sisi pia,(kama vila Yn. 20:24-29). Abramu alikuwa akitumikia kusudi la kithiolojia (yaani kielelezo cha ukombozi).

**15:9** Abramu anaamriwa (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kuleta wanyama mbali mbali kwa ajili ya kutoa dhabihu.

1. Ndama wa miaka mitatu
2. Mbuzi mke wa miaka mitatu
3. Kondoo mme wa miaka mitatu

4. Na hua
5. Na mwana njiwa

Sababu haswa kwa ajili ya hawa wanyama maalum haijulikani. Wametajwa baadaye kwenye utungaji sheria wa Musa, ambapo wangemaanisha kuwa na umuhimu wa kitamaduni ambao sisi hatuujui kikamilifu. Katika mst. 10 walipasuliwa vipande viwili na kila kimoja kikimwelekea mwenzake, isipokuwa kwa wale ndege. Hii ilikuwa ni desturi ya kitamaduni kwa ajili ya "kuchinja" agano ( angalia Mada Maalum katika 13:14, kama vile Yer. 34:18). Baadhi wamefikiria kuwa kifo cha mnyama ilikuwa ni njia ya kuonya washiriki wa agano kile kingeliwatokea kama watavunja maagano. Hata hivyo, hili halijulikani.

**15:11 "Hata Tai walipotua juu ya mizoga"** Pamekuwepo na mijadala mingi kati ya watoa maoni kuhusu kwa nini mst. 11 uliwekwa kwenye kumbukumbu. Baadhi ya nadharia ni kuwa

1. Ni alama ya mashaka ya Abramu
2. Ni alama ya maadui wa Israel (kama vila Ezek. 17:37,12)
3. Ilimchukua muda Mungu kujidhihilisha mwenyewe na hii ni ishara ya habari ya uhalisia wa matukio (yaani., uwepo wa wanyama waliokufa kulisababisha ndege wala nyama waonekane)

Kwangu mimi, kwa vile sina hofu juu ya istiari na uanishi ambao haujatajwa haswa katika Agano Jipya,kipengere namba 3 kinaonekana kuwa cha uchaguzi wa kufaa. Kumbuka matoleo haya yalikuwa hayachomwi. Hii ilikuwa sherehe ya agano, na sio dhabihu.

◙ **"na Abramu akawafukuza"** Inashangaza kwamba KITENZI cha Kiebrania cha neno "akawafukuza" (BDB 674, KB 728, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU) kinapaswa kutumika hapa. Sitiari hii mara nyingi ilikuwa ikitumiwa na Mungu (kama vile Zab. 147:18; Isa. 40:7), lakini ni kwa vipi hili linahusiana na kitendo cha Abramu haijulikani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 15:12-16**
**[12]Na jua lilipokuwa likichwa usingizi mzito ulimshika Abramu, hofu ya giza kuu ikamwangukia. [13]Bwana akamwambia Abramu, Ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne. [14] Hata na taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi. [15]Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani, utazikwa katika uzee mwema. [16]Na kizazi cha nne kitarudi hapa, maana haujatimia uovu wa Waamori bado.**

**15:12 "Na jua lilipokuwa likichwa"** Hii inadokeza kuwa siku mpya ilikuwa ikianza (kama vile Mwa. 1:5). Kujua kwa uhakika ni kwa muda gani haya maono yalidumu haijulikani, bali yaweza kuchukua siku mbili na mchana mmoja (angalia kumbukumbu katika mst. 1c).

◙ **"usingizi mzito ulimshika Abramu"** Hiki ni kama kile kifungu cha Kiebrania (BDB 922) kilichotumika kuhusu usingizi mzito uliomshika Adamu wakati Mungu alipochukua ubavu mmoja kumtengeneza Hawa(kama vile. Mwa. 2:21). KITENZI kinadokeza usingizi wa Kimungu uliomshika katika maandalizi kwa ajili ya maono (kama vile Ayubu 4:13; 33:15).

◙

**NASB "hofu ya giza"**
**NKJV "wasiwasi wa giza"**
**NRSV "giza la kutisha"**
**TEV "kitisho na hofu"**
**NJB "woga mwingi"**

Neno "hofu" (BDB 33, KB 41) linamaanisha wasiwasi,kitisho, hofu, woga. Mara nyingi linatumika katika vifungu vya ushairi wa hofu ya Mungu.

1. Kwa maadui-Kut. 15:16; 23:27
2. Kwa Ayubu – 9:34; 13:21

3. Kwa Israeli– Kumb. 32:25; Zab. 88:16

Neno "giza" (חשכה, BDB 365, KB 362 na mzizi unaoelekeana חשך) vinahusiana na

1. Giza la ulimwenguni – Mwa. 1:2
2. Moja ya mapigo ya kipindi cha wana wa Israeli kutoka Misri – Kut. 10:21
3. Kifo/jehanamu– Zab. 139:7-12
4. maafa – Ayubu 15:22-30; 20:26; Isa. 8:22; 50:10
5. Kujificha kwa Mungu – Zab. 18:11
6. Kukosekana kwa maono – Mika 3:6

Tena pamekuwepo na tafsiri mbalimbali za kifungu hiki.

1. Kuwa ingawa ahadi za Mungu zilikuwa za ajabu lakini zingalichukua muda mrefu, ngumu kuzitimiliza
2. Mara nyingi wanadamu hudhoofishwa kimwili baada ya maono ya Mungu juu ya mambo ya mbeleni; hili ni kweli kwa Danieli na wengi wa manabii
3. Kuwa Mungu alikuwa anamkaribia, ambacho ni kitu cha kuogopesha mara nyingi (kama vile Ayubu 4:12-21)

**15:13 "ujue ya kwamba, uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo ya kwao"** Kifungu "ujue hakika" ni matokeo ya muunganiko wa KITENZI JINA HALISI na KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 393, KB 390), "kujua," ambapo ni namna ya njia ya kisarufi kuonyesha msisitizo. YHWH anamjibu swali la Abramu la mst. 8. Bado kuna mpambano wa imani/mashaka ndani ya Abramu! Hili halimuumizi Mungu! Tambua kuwa nchi ya Misri haikutajwa kwa uwazi. Neno "wageni"linamaanisha "wapiti njia" (BDB 158) au mtu mwenye haki kidogo kwa sababu hajawa rasmi raia wa taifa. YHWH anatabiri uzoefu wa Wamisri. Imani ndani ya Mungu haimaanishi ni maisha rahisi! Ahadi za Mungu zinachelewa na mara nyingi kutoeleweka, lakini bado imani huendelea kudumu.

◙**"watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne"** Pamekuwepo na utofauti kati ya mstari huu, ambao umetajwa katika Mdo.7:6 kwenye mahubiri ya Stefano, na Kutoka 12:40, uliotaja namba 430 na kunukuliwa na Paulo katika Gal. 3:17. Tafasiri ya maaandiko ya kale ya Kiebrania na Torati ya Kisamaria inachukulia kipindi cha miaka 430 kama ni kupita kwa wazee wa kale kote katika nchi za Kaanani na Misri. Yawezekana kuwa namba 400 ni namba ya ujumla. Waalimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa kiliendelea toka kuzaliwa kwa Isaka mpaka kipindi cha wana wa Israeli kutoka Misri. Lazima ieleweke kuwa mst. 6 unataja kizazi cha nne na, kutokana na hesabu zetu, ambapo ni wazi namna kipindi hiki kilivyodumu.

**15:14 "Hata na taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi"** Huu ni utimilisho kamili kwenye Kut. 3:22 na 12:35-56. Umiliki huu unajumuisha dhahabu, fedha, shaba na vito vya thamani vilivyotumika kutengeneza hema la kukutanikia pamoja na samani zake (kama vile Kutoka 25-40). Andiko hili haliwezi kutumika kudai kuwa imani huzaa mali nyingi. Mwanzoni ustawi wa mali nyingi, ilikuwa ni namna ya kuyavuta mataifa kwa YHWH. Hata hivyo, mtazamo haukuwa kwenye utajili, bali ni katika uhusiano wa imani. Mmoja wa watoa maoni wangu ninaempenda, Gordon Fee, mtu mwenye haiba kubwa, akatangaza utumiaji wa maandiko yaliyo hakikiwa kama haya kuhubiri injili juu ya"afya, mali, utajili."kijitabu chake kinaleta ushawishi (i.e., *The Disease of the Health and Wealth Gospels*)

**15:15 "Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani"** Neno la Kiebrania "amani" (BDB 1022) linadokeza mvutano wa maisha na Mungu (angalia Mada Maalum ifuatayo). Mungu alimwahidi Ibrahimu kuwa ataishi kwa kuvuna, katika umri wa uzee na kufa kifo cha upole. Pia pana swali la kile kinachomaanishwa "utakwenda kwa baba zako." Kwa uhakika hii ni nukuu ya *Sheol* (kama vile Kumb. 32:50), lakini baadhi wanashangaa ikiwa inamaanisha kuwa familia zilizoko huko *sheol* (kuzimu) ziko pamoja. Hili laweza kusomeka kivinginevyo kwa vile wazazi wa Abramu hawakuwa wafuasi wa YHWH na, kwahiyo, wawezakuwa sehemu nyingine ya jehanamu au kuzimu. Wengi hatujui kuhusu maisha baada ya kifo na maneno ya Kibiblia kuhusu kuzimu, jehanamu, shimo la giza, na kwa namna panavyohusiana na kwingine kwa hali ya kawaida.

## MADA MAALUMU: WAFU WAKO WAPI? *(SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS*

I. Agano la Kale

A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol)* (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)

B. Tabia za shimoni (*sheol*)

1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
7. panahusiana na *utelekezaj*i (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa*. . .*Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*,Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya

A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)

B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheo*l)

1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luka 10:15; 16:23-24
4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Luk 16:23

C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)

1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Luk. 23:43
2. Sehemu ya waovu iitwayo “kwenye vifungo vya giza”,iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa “shimoni” Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3

*D. Gehenna*

1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, “bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalemu). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna

a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk. 9:43
b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
d. panafanana na *Sheol,* Mt. 5:29-30; 18:9
e. Panaainisha waovu kama “wana wa Jehanamu” Mt. 23:15
f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk. 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol),* kuzimu(*hades)* na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa
1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

A. Agano jipya halifundishi juu ya “zinaa ya nafsi,” ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
2. Ibrahamu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk. 12:26-27; Luk 16:23
3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26
3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea

tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemo (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia
   A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*
   B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

## MADA MAALUMU: AMANI(*Shalom*) [AGANO LA KALE]

Neno la Kiebrania *shalom* (BDB 1022, KB 1532) ni la kawaida katika asili ya Kisemiti.

A. Lugha ya Akkadia
   1. Kutokudhurika
   2. Kuishi vizuri
   3. Kuwa katika hali nzuri
B. Ugariti (Wakaanani)
   1. Kutodhurika
   2. Kuwa mzima
C. Kiarabu
   1. Kuwa mwenye afya
   2. Kuwa katika hali ya amani
D. Kiarama
   1. Kuwa mkamilifu
   2. Kufikia mwisho/kuhitimisha
   3. Kuhitmisha amani
   4. Kubaki pasipo kudhuriwa
E. Vidokezo vya Kiebrania
   1. Kuwa mtimilifu
   2. Mwenye kusikika
   3. Kustawi
   4. amani

Siku hizi neno *shalom* ni neno la salamu na maelezo ya kutakiana heri. Bado linamaanisha kukosekana kwa uovu na uwepo wa mema (yaani., kutosheka na maisha). Inamaanisha hali ya akili ya usalama na utosherevu. Tambua namna Agano la Kale linavyozungumzia juu ya "agano la amani" (kama vile Hes. 25:12; Ezek. 34:25; 37:26; pia kumbuka Mwa. 26:29,31; Yosh. 9:15). Lazima litendeke (kama vile Zab. 34:14; Rum. 14:19). AB, juzuu. 5, uk. 206, inasema, "amani," "ukweli," na "haki" zinafanana na dhana ya Kiebrania (kama vile Zak. 8:16-19). YHWH anaitwa "Bwana wa amani" (kama vile Amu. 6:24; Rum. 16:20; 2 Kor. 13:11; Fil. 4:9; 1 The. 5:23). Masihi ataitwa "Mfalme wa Amani" (kama vile Isa. 9:5). Siku mpya wakati amani, ukweli, na haki itakuwa wazi kwa uzoefu wa mwanadamu (kama vile Isa. 60:17; 66:12,22). "uzuri" wa Mwanzo 1:31 tena ni uwezekana, ahadi (yaani., "mbingu mpya na nchi mpya").

**15:16 "maana haujatimia uovu wa Waamori bado"** Hili linaonyesha kuwa Mungu alikuwa anaendelea kujaribu kuleta uzao wa Wakaanani wa nchi ya ahadi kwake mwenyewe. Melchizedeki alikuwa Mkaanani. Baada ya fursa za kutosha na muda ndipo Mungu atawahukumu na kuwaondoa. Hiki sio kitendo cha upendeleo dhidi ya Wayahudi, kwa vile wakichukuliana na utaratibu wa Wakaanani, pia wataondolewa katika nchi ya ahadi (yaani., Waashuru na wale waliokimbilia Babeli).Waamori na Wakaanani wote wanatumika kama njia yakurejea makabila yote ya Kaanani. Kwa maana hili andiko ni kivuli cha magomvi yatakayotokea pale Israel itakapoichukua nchi, lakini yenyewe ndiyo ilishindwa na ibada za sanamu za Wakaanani. Ubashiri huu unafanana na Mwa. 9:20-27,

hasa mst. 25. Ni Hamu ndiye alitenda dhambi, lakini mwanae Kaanani ndiye aliye laaniwa. Tamaduni za Kikaanani ni tatizo. Nyingi kati zao, kama si zote, ya taratibu katika tarati zinahusianishwa na tamaduni za Wakaanani na ibada. Israel ilitakiwa kuwa ya tofauti! Israeli ilitakiwa kumdhihirisha YHWH! Namna hili lilivyoingia kwenye andiko la kitabu cha Mwanzo ni kuwa

1. Huenda Mungu alikuwa akiwaandaa kwenye matukio yajayo
2. Mwandishi wa baadaye aliongeza hizi hoja kusisitiza siku zake

Kama kumbukumbu, ninapotaja mwandishi wa mwanzo au mhariri hii haimaanishi kuushushia hadhi "uvuvio." Ninadhania Roho aliwaongoza waandishi wote, wahariri, watoa habari na wakusanyaji habari! Mwandishi wa kweli wa andiko ni Mungu. Haswa namna gani, lini, na nani mhusika wa kihistoria (alipomtembelea kwenye historia).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 15: 17-21**
**[17] Ikawa, jua lilipokuchwa likawa giza, tazama, tanuru ya moshi na mwenge unaowaka ulipita kati ya vile vipande vya nyama. [18]Siku ile Bwana akafanya agano na Abramu, akasema, Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto Frati, [19]Mkeni, na Mkenizi, na Mkadmoni, [20]na Mhiti, na Mperizi, na Mrefai, [21] na Mwamori, na Mkanaani, na Mgirgashi, na Myebusi.**

**15:17 "tazama, tanuru ya moshi na mwenge unaowaka ulipita kati ya vile vipande vya nyama"** YHWH alimtokea Abramu kwa namna ambavyo angelimtambua kitamaduni. Tanuru la moshi linaonekana kuwa

1. Namna ya YHWH kuficha sura yake (yaani wingu la utukufu la *Shekinah* kipindi cha wana wa Israeli wakitoka Misri)
2. Alama ya Uungu inayotoa ulinzi Kwenye laana ya vigae vya lugha ya Akkadi
3. Alama ya vyote hukumu na ulinzi (kama vile Zak. 12:6)
4. Huko Mesopotamia namna hii ya uwekaji wa alama uliwakilisha usafi wa ki-Ungu.

Ndani ya tanuru kulikuweko na moto. Mungu mara nyingi anahusiana na moto, sio tu kwenye habari za kibiblia, bali pia katika nadharia ya ufuasi wa Zorostrer. Mimi pekee naamini kuwa hili tanuru linahusiana na ukweli kwamba mengi ya maagano yamethibitishwa kwa agano la chakula na hili tanuru linatambulisha chakula hicho. Pia, ni muhimu kithiolojia kutambua kuwa Abramu hakupita kati ya vile vipande vya nyama; Mungu tu ndiye anaweza kupita. Huu ni mfano mwingine kwamba agano linatoka kwenye vyanzo vya Mungu na sio bidii za mwanadamu, thamani, na utajili. Hili lilikuwa ni agano alilolianzisha Mungu na kulitenda (kama vile II Sam. 7:8-16; Zab. 89:20-37)

## MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

A. Chanya
   1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
   2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Math 25:1-13)
   3. Hupikia (kama vile. Kutoka 12:8; Isay 44:15:16; Yohana 21:9)
   4. Husafisha (kama vile. Hes. 31:22-23; Mith. 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
   5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa. 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Ezek. 1:27; Waebrania 12:29)
   6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 1. 18:24)
   7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile Mdo. 2:3)
   8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)

B. Hasi
   1. Huunguza (kama vile. Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7
   2. Huangamiza (kama vile Mwa. 19:24; Walawi 10:1-2)
   3. Hasira (kama vile. Hes 21:28; Isay 10:16; Zek 123:6)

4. Adhabu (kama vile. Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17
5. Ishara za uongo za matukio ya siku ya mwisho (kama vile.Ufunuo 13:13)

C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.
1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos 8:5; Sefania 3:8)
2. Humimina moto (kama vile Nah 1:6)
3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mith. 25:41; Yuda aya ya 7)
4. Hukumu ya matukio ya siku ya mwisho (kama vile.Math 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; Thes 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu 8:7; 16:8; 20:14-15)

D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru
1. Mwa. 15:17
2. Kutoka 3:2
3. Kutoka 19:18
4. Zaburi 18:7-15; 29:7
5. Ezek 1:4, 27; 10:2
6. Ebr. 1:7; 12:29

E. Kama sitiari nyingi katika Biblia (yaan., kichocheo, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

**15:18 "Siku ile Bwana akafanya agano na Abramu"** Istilahi "kufanya" kiuhalisia linamaanisha "kukata" (BDB 503, KB 500, *Qal* KAULI TIMILIFU). Hii istilahi kukata kiasili haihusiani na neno kwenye mst. 10 (BDB 144, KB 167), lakini linakuwa kipimo, sitiari ya Kibiblia kwa ajili ya "kufanya agano."

## MADA MAALUM: AGANO LILILOAHIDIWA KWA MABABA WA IMANI

Huu uhusiano wa ahadi maalumu ya agano la mwanzo ulifanyika kwa

1. Ibrahimu, Mwa. 12:1-3
   a. Ardhi, Mwa. 12:7; 13:4-15; 15:18-21
   b. Watu, Mwa. 13:16; 15:4-5; 17:2-6; 22:18
   c. Baraka kwa ulimwengu, Mwa. 18:18; 22:18
2. Isaka, Mwa. 26:2-4
   a. Ardhi
   b. Watu
   c. Kuubariki ulimwengu
3. Yakobo, Mwa. 28:2-4,13; 35:9-12; 48:3-4
   a. Ardhi
   b. Watu
4. Taifa la Israeli (nchi ), Kut. 3:8,17; 6:8; 13:5; 33:1-3; Kumb. 1:7-8,35; 4:31; 9:3; 11:25; 31:7; Yosh. 1:6

◙ **"agano"** "Agano" (BDB 136) likajakuwa wazo kuu la fasihi ya kibiblia. Linaongelea kiujumla kwenye ahadi na ulazima juu ya vyote Mungu na mwanadamu. Kuna uambatani wa kipekee wa dhana yenye masharti na isio na masharti ya agano katika zama za kibiblia. Je agano ni la kimasharti au lisilo na masharti? Ndiyo! Inaonekana kuwa pendo la Mungu lisilo na masharti linategemea juu ya imani ya mwanadamu na wajibu wa toba (kama vile 15:6; Warumi 4; Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Hili linaonekana kiasi fulani ni la kimafumbo, lakini ni namna ya njia za Mungu kutenda na mwanadamu mwenye dhambi. Angalia Mada Maalum: Agano katika 13:14.

◙ **"kutoka katika Mto wa Misri"** Mara nyingi, hili linarejelea Mto Nile, lakini katika muktadha wa ahadi za kibiblia za mipaka ya nchi ya ahadi, lazima inamaanisha"wadi El-arish" (kama vile Hes. 34:5 na Yosh. 15:4). Vipimo vya nchi

ya ahadi kwa kiasi vilitimizwa katika zile siku za Daudi, lakini vikakamilika katika zile siku za Sulemani (kama vile I Fal. 4:21).

**15:19-21** Tunapata hapa orodha kumi ya kabila zinazotengeneza idadi ya Wakaanani. Wakati mwingine idadi ya haya makabila hutofautiana: (1) Yoshua 24:11 ina makabila 7; (2) Kutoka 3:17 ina makabila 6; na (3) Kutoka 23:28 linaorodhesha makabila 3 . Namba halisi haijulikani, lakini ni dhahiri kuwa istilahi Waamori," ambalo linamaanisha "watu wa milimani," au istilahi "Wakaanani," lenye kumaanisha "watu wa uwanda wa chini," ikaja kuwa istilahi iliungana kwa ajili ya makabila yote. Angalia Mada Maalum: Waisraeli wa mwanzo walioishi Palestina katika 12:6

**15:20 "Mhiti"** Toka katika kitabu cha Mwanzo 10:15 tunaona kuwa watu hawa walitoka huko Heth (BDB 366). Baadaye wakatengeneza ngome kuu katikati ya Uturuki.

◙ **"Mrefai"** Hawa wanaonekana kuwa viumbe warefu (BDB 952, kama vile Yosh. 12:4; 17:15; I Nya. 20:4) kama wale *wana wa Anaki* (kama vile Kumb. 2:11 na 3:11) na yumkini *Manefili* (kama vile Mwanzo 6 and Hes. 13:33). Angalia Mada Maalum katika 14:5.

**15:21 "Myebusi"** Hawa walikuwa ni wakazi wa Yerusalemu ambao hawakushindwa mpaka siku za Daudi (BDB 101, kama vile Amu. 1:21; 19:11; II Sam. 5:6 na kuendelea).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Elezea na kufafanua kwa maneno yako mwenyewe umuhimu wa maneno yaliyotumika katika Mwa. 15:6. Husianisha hili na Warumi 4 na Wagalatia 3
2. Kwa nini watu wengi wanaistiarisha Mwa. 15:11?
3. Nini umuhimu wa Mungu kumtokea Ibrahimu kama tanuru la moshi na mianga (Mwa. 15:17)? .
4. Kwanini Makabila ya Kanaani yanaorodheshwa tofauti (kama vile 15:19-21)?

# MWANZO 16

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Sarai na Hajiri | Hajiri na Ishmaeli | Kuzaliwa kwa Ishmaeli | Hajiri na Ishmaeli | kuzaliwa kwa Ishmaeli |
| 16:1-6 | 16:1-3 | 16:1-6 | 16:1-4 | 16:1-2 |
| | | | | 16:3-6 |
| | 16:4-6 | | | |
| | | | 16:5 | |
| | | | 16:6 | |
| 16:7-14 | 16:7-14 | 16:7-14 | 16:7-18a | 16:7-12 |
| | | | 16:8b | |
| | | | 16:9-12 | |
| (11-12) | (11-12) | (11-12) | | (11-12) |
| | | | 16:13-14 | 16:13-14 |
| 16:15-16 | 16:15-16 | 16:15-16 | 16:15-16 | 16:15-16 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:1-6**

**[1] Basi Sarai mkewe Abramu hakumzalia mwana, naye alikuwa na mjakazi, Mmisri, jina lake Hajiri. [2] Sarai akamwambia Abramu, Basi sasa, Bwana amenifunga tumbo nisizae, umwingilie mjakazi wangu labda nitapata uzao kwa yeye. Abramu akaisikiliza sauti ya Sarai. [3] Sarai mkewe Abramu akamtwaa Hajiri Mmisri mjakazi wake, baada ya kukaa Abramu katika nchi ya Kanaani miaka kumi, akampa Abramu mumewe, awe mkewe. [4] Basi akamwingilia Hajiri, naye akapata mimba. Naye alipoona ya kwamba amepata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake. [5] Sarai akamwambia Abramu, Ubaya ulionipata na uwe juu yako; nimekupa mjakazi wangu kifuani mwako, naye alipoona kwamba amepata mimba, mimi nimekuwa duni machoni pake. Bwana na ahukumu kati ya mimi na wewe. [6] Naye Abramu akamwambia Sarai, Tazama, mjakazi wako yu mkononi mwako, mtendee lililo jema machoni pako. Sarai akamtesa, naye akakimbia kutoka mbele yake.**

**16:1 "alikuwa na mjakazi, Mmisri, jina lake Hajiri"** Jina la Hajiri lilimaanisha "kukimbia" (BDB 212). Hii ni tabia yake (kama vile mistari ya 6, 8). Alikuwa ni Mmisri ambaye yawezekana alinunuliwa kwa ajili ya Sarai walipokuwa Misri (kama vile Mwanzo 12:10-20).

**16:2 "Bwana amenifunga tumbo nisizae"** Ni dhahiri kwamba wenza walikuwa wameshajadili kabla mafunuo ya YHWH na pia kucheleweshwa katika kutimilizwa. Inavyoonekana walianza kupanga namna gani "watamsaidia" Mungu kutimiliza ahadi zake!

Muundo wa KITENZI "kuzuia" (BDB 783, KB 870, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) unaashiria kitendo. Sarai lazima alikuwa amefikiria kwamba alikuwa tasa wa kudumu.

Kwa namna fulani Sarai anamlaumu YHWH kwa kuendelea kwake kuwa tasa (kama vile 20:18). Kucheleweshwa kulikuwa ni mpango wa Mungu kukuza imani yao katika kumtumainia na kujifunua kwake mwenyewe kiukamilifu kwa vizazi vijavyo. Waaminio wote wanahangaika na kukamilishiwa kwa muda wa matukio yaliyoahidiwa ki-Ungu.

◙ **"umwingilie mjakazi wangu"** KITENZI (BDB 97, KB 112) ni *Qal* KAULI SHURUTISHI kinatumika katika namna ya ombi (kama vile 30:3). KITENZI mara kwa mara kinatumia tafsida ya ukaribu wa kujamiiana (kama vile Mwanzo 6:4; 16:2; 19:34; 30:3; 38:8,9; 39:14; Kumb. 22:13; 25:5; II Sam. 11:4; 12:24; 16:21-22; 20:3; Mith. 6:29).

◙**"labda nitapata uzao kwa yeye"** Hii inafanana sana na ubamba wa ubao wenye maandiko wa Nuzi ambao unaelezea desturi za wahuri za Milenia ya pili K.K. Mtoto wa Hajiri angekuwa kisheria mtoto wa Sarai na mrithi wa Abramu.

◙ **"Abramu akaisikiliza sauti ya Sarai"** Hii inakaribiana na usambamba wa tatizo la Mwanzo 3 (haswa mstari wa 17). Abramu alijaribiwa kufanya kitu fulani ambacho yawezekana alikuwa amekwisha kushawishiwa kukifanya hata hivyo KITENZI kidhahiri "kusikia" (BDB 1033, KB 1570) katika NJEO YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambacho kinamaanisha tendo linalojirudia. Hali ya uaminifu ya uumbaji wa asili inapotea, na kuwa hali ya kushangaza kwenda katika juhudi za "kumsaidia" Mungu!

**16:3 "baada ya kukaa Abramu katika nchi ya Kanaani miaka kumi"** Ni muhimu kwamba angalau miaka kumi imepita toka Mungu azungumze na Abramu katika sura ya 15. Abramu alikuwa anaendelea kutumainia, lakini alikuwa akijaribu kufikiria njia zingine ambazo zingeweza kumsaidia Mungu. Hii tena ni Mungu kumuonyesha Abramu kibayana kwamba ilikuwa ni rasilimali zake ambazo mwisho wa siku zingeleta ahadi. Kipengele hiki kinatumika kama istiari na Paulo katika Gal. 4:21-31.

◙ **"awe mkewe"** Hajiri kiukweli ni suria wake. Ingawa neno la Kiebrania "mke" linatumika hapa, Ni wazi kwamba yeye sio mke, lakini suria (yaani mwenza wa kingono aliye na haki kidogo zenye ukomo).

**16:4 "bibi yake alikuwa duni machoni pake"** KITENZI (BDB 886, KB 1103, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inaweza kumaanisha

1. kuwa mwepesi
2. ghafla
3. kutokuwa muhimu (kama vile I Sam. 2:30; Job 40:4)

Shina la neno *Hiphil* linaashiria hali ya kutokukubaliana (kama vile II Sam. 19:43; Isa. 23:9; Ezek. 22:7). Katika Kiebrania ilifikiriwa kuwa na heshima au uzito unaolinganishwa "kuwa mwepesi."

**16:5** Maajabu ya mahusiano kati ya mtu na mtu ni dhahiri. Sarai alianzisha mpango huu na sasa anasumbuka na matokeo yake. Kama ilivyo mara nyingi katika masimulizi ya Kibiblia, msomaji hapewi historia yote ya yale mazungumzo baina yao yaliyohusiana na matukio. Abramu inawezekana zaidi mwanzoni aliweza kujihusisha. Katika kufasiri masimulizi ya kibiblia ya kihistoria, wasomaji lazima wajiulize weyewe "kwanini kuandikwa hiki?"

Abramu na Sarai lazima wajifunze kwamba utendaji wa mwanadamu sio ufunguo/msingi kuelekea katika mahusiano na Mungu; imani, utii na ustahimivu ndivyo msingi.

Inawezekana kwamba kile kilichoandikwa kwenye huu mstari ni nahau ya kisheria. Sarai anazungumza katika namna kama anadai haki zake za kisheria katika hali ya kuwa katika utumwa ila kwa namna ya majivuno (yaani Utaratibu wa-Hammurabi na ubamba wa madini wenye maandiko ya Wa-Nuzi). Kila kitu alichokifanya kilikuwa kinakubalika kidesturi na kisheria, lakini mtazamo wa Hajiri haukuwa unakubaliwa. Abramu kama kichwa cha nyumba alikuwa anawajibika.

◙**"Bwana na ahukumu kati ya mimi na wewe"** KITENZI (BDB 1047, KB 1622) ni *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU kinachotumika katika namna ya KITENZI AMRISHI. Hakika anachokitaka YHWH akitende bado ni tata. Inavyoonekana ni kuwa natafta vikwazo vya ki-Ungu kwa ajili ya hisia alizonazo za kukataliwa au kuthibitishwa kwa vitendo anavyopanga dhidi ya Hajiri. Hatahivyo tungo inaonesha mvutano unaoendelea kati ya Abramu na Sarai.

**16:6** Hii inaonekana kwa namna fulani kama ukatili kwetu, lakini lazima tutoe hukumu kwa namna ya ufahamu wa siku zake na wala si kwa namna ya siku zetu. Hii inashabihiana kwa dhati na Vibao vya maandiko ya Nuzi na kanuni na taratibu wa-Hammurabi katika namna ya kushughulikia masuria.

Tena kwa njia kadhaa usambamba huu wa Mwanzo 3:11-13 inatoa masimulizi. Abramu anahamisha majukumu yake kutoka kwake kama kiongozi wa familia kwenda kwa Sarai. Wanadamu huwa wanatabia ya kukimbia majukumu na kuwa na udhuru mwingi!

◙**"Sarai akamtesa"** KITENZI (BDB 776 III, KB 853) ni *Piel* shina linalomaanisha kuwa mnyenyekevu au kumtendea vibaya (kama vile 31:50; Kut. 22:21,22 [mara mbili katika muundo wa ndani]; Ayubu 30:11). Mtazamo wa Hajiri haufanyi matendo ya Sarai yawe sahihi. Wanadamu wenye asili ya dhambi. Imani komavu yaweza kuleta suluhisho la tatizo hili.

Inawezekana kwamba mara baada ya Hajiri kubeba ujauzito Sarai alirudi katika huduma yake na kumwondoa yeye kama mwenzi wa kujamiina kutoka kwa Abramu.

◙**"akakimbia kutoka mbele yake"** Mtumwa kukimbia lilikuwa jambo nyeti lenye madhara makubwa. Hii inafanana sana na Mwanzo 21:8-21. Mistari ifuatayo inaonesha upendo na kujali kwa YHWH, hata kwa Suria Hajiri na mwanawe. Upendo wa YHWH hauishii kwenye familia ya Abramu (yaani Melkizedeki, Ayubu).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:7-14**

**[7] Malaika wa Bwana akamwona kwenye chemchemi ya maji katika jangwa, chemchemi iliyoko katika njia ya kuendea Shuri. [8] Akamwambia, Hajiri, wewe mjakazi wa Sarai, unatoka wapi, nawe unakwenda wapi? Akanena, Nakimbia mimi kutoka mbele ya bibi yangu Sarai. [9] Malaika wa Bwana akamwambia, Rudi kwa bibi yako, ukanyenyekee chini ya mikono yake. [10] Malaika wa Bwana akamwambia, Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyokuwa mwingi. [11] Malaika wa Bwana akamwambia, Tazama! Wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ishmaeli, maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako. [12] Naye atakuwa kama punda-mwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake, naye atakaa mbele yao ndugu zake wote. [13] Akaliita jina la Bwana aliyesema naye, Wewe U Mungu uonaye, kwani alisema, Hata hapa nimemwona yeye anionaye? [14] Kwa hiyo kisima kile kiliitwa Beer-lahai-roi.Tazama,kiko kati ya kadeshi na beredi.**

**16:7 "Malaika wa Bwana"** Huu umaarufu unaonekana kuwa kuupa sifa ya ubinadamu uwepo binafsi wa Mungu. Angalia Mada Maalumu katika 12:7.

◙**"chemchemi iliyoko katika njia ya kuendea Shuri"** Hatufahamu mahali pa uhakika pa kijiografia kunakozungumzwa hapa, lakini inawezekana ni kusini mwa Beersheba njiani kuelekea Misri. Hajiri anaenda nyumbani.

**16:8** Mistari kama hii (yaani 3:9,11; 4:9,10), ambayo inaandika Mungu au wawakilishi wake kuuliza maswali, imekuwa sehemu ya hoja za kithiolojia za "Imani ya Mungu mmoja kama mtawala wa dunia ya Wazi," ambayo inachukua maswali haya kibayana na kuyafanya madhanio ya kithiolojia kwamba Mungu hafahamu

1. hatima/ubaadaye
2. matendo ya kihistoria ya watu

Sikubaliani na Falsafa ya Kiyunani (yaani sifa za Mungu zilizokuzwa kifalsafa), wala sikatai kwamba historia ya masimulizi ya Mwanzo, lakini ninaeleza kwamba ni nyaraka za kifasihi zitumiazo lugha za kimafumbo (kama vile lugha zote za wanadamu zinavyofanya). Suala kubwa hapa ni kusudi la maswali katika Biblia. Je yanaaksi kukosa maarifa upande wa Mungu au Mungu kufanya kazi ya kukuza uelewa ndani ya wanadamu? Kuna maandiko mengi mengine ambayo yanaelezea maarifa ya watu na matukio ya siku zijazo kwa ajili yangu kujiskia huru na Imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala ya Wazi kama kitu chochote lakini thiolojia iliyofanyiwa kazi tena ya A. N. North (yaani Wazo la Kimchakato).

**16:9** Malaika anampatia amri mbili.

1. rudi – BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. nyenyekea – BDB 776 III, KB 853, *Hithpael* KAULI SHURUTISHI

Ujumbe huu unamaanisha kwamba ni mapenzi ya YHWH kwamba mtoto wa Hajiri akue chini ya ushawishi wa Abramu (yaani maarifa ya YHWH).

◙**"ukanyenyekee"** Hii ni KITENZI kilekile kilichofasiriwa "akamtesa" (BDB 776 III, KB 853) katika mstari wa 6 na NOMINO inatumika katika mstari wa 11, "mateso" (BDB 777). Haaidi kubadilisha mazingira ya Sarai lakini anaahidi kumbariki mtoto wa kiume (yaani Ishmaeli).

**16:10-12** Mwitikio wa malaika wa Bwana kwa Hajiri ni sawa sawa na mwitikio wa Mungu kwa Abramu katika 15:5. Baadhi ya ahadi kubwa zinafanywa juu ya mtoto, na pia mwili wake na tabia zake za kiakili na ufahamu. Hajiri anakuwa na furaha tela kwamba YHWH angeweza kumjali yeye.

**16:10 "Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyokuwa mwingi"** Ahadi hii imerudiwa kwa Abramu kuhusu Ishmaeli katika 17:20.

KITENZI kimeshadidiwa kwa muunganiko wa KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 915, KB 1176, vyote *Hiphil*). Kukutana na maarifa ya kutumaini katika maneno ya YHWH kunaleta baraka! Katika namna Hajiri anavyoitikia kwa Uungu katika namna ileile ya Abramu. Wala hata haulizi maswali (au angalau hayapo yaliyoandikwa) kama Abramu afanyavyo. Mara hizi zote mbili zinahusisha Baraka zilizohaidiwa za mtoto, lakini bado ni ufunuo wa nyakati ngumu. Mwanzo 15:6 ni sehemu ya wokovu kwa Abramu. Hajiri kwa hakika aliitikia kwa namna hiyo hiyo! Kwangu mimi, ambaye upendeleo nauona kama mpango wa milele wa ukombozi, Mungu kumkubali Hajiri na Ishamaeli ni ushuhuda wenye nguvu kwa kusudi lake la ukombozi zaidi ya Israeli (angalia Mada Maalumu katika 12:3). Katika namna huu ni mfano "mataifa" yakikaribishwa kwa jinsi hiyo hiyo kama Abramu—kwa imani ambayo inazalisha utii. Kuna vidokezo kadhaa vya Agizo kuu la Agano la Kale! Mapigo ya Moyo wa Mungu kwa ajili ya ulimwengu yalipotea, ushirika uliokatizwa lazima urejeshwe! Maono ya kiulimwengu ya Isaya, hadithi ya Yona, na Agano Jipya zimejaa kweli hizi.

**16:11-12** Toleo la NASB linachapa mistari ya 11-12 kama ushairi (kama vile 12:1-3; 14:19-20; 15:1,18; 17:1-2,4-5). Mstari wa 12 unaelezea ni aina gani ya mwanaume angekuwa.

**16:11 “utazaa mwana”** Hii sio taarifa mpya (kama vile mstari wa 4), lakini kwamba mtoto atakuwa wa kiume hilo ndilo jipya.

◙**“Ishmaeli”** Jina linamaanisha “*El* amesikia” au “ikiwezekana *El* asikie” (BDB 1035, KB 447). Katika tungo iliyotangulia malaika anasema “YHWH amesikia,” ambayo kidhahiri inamaanisha “alisikia” (BDB 1033). Tazama kwamba Mtoto hapewi jina na baba yake, lakini na Mungu (kama vile Mt. 1:21,25; Luka 1:31,35; 2:21).

**16:12 “punda-mwitu kati ya watu”** Mzizi huu (BDB 825) unamaanisha

1. Lugha ya Akkadia – Mwana punda
2. Kiashuru – Mwana punda pori
3. Kiarabu – Farasi mwitu
4. Kiebrania – Farasi mwitu au Farasi ( *Anchor Bible Commentary* on Genesis, ukurasa wa 118)

Lakini kuwa na tahadhari kwamba hii haikuwa kauli ya kushusha hadhi katika Mashariki ya Karibu ya kale. Wanyama hawa walitumika kwa ajili ya dhabihu huko Mesopotamia. Walikuwa wakiheshimika sana na kuthaminiwa. Inaashiria hali yake ya kutanga tanga (yaani kiongozi wa wafugaji). Ishmaeli atapenda uhuru wake na ataishi maisha ya kiufugaji. Mistari miwili ifuatayo ya kishairi inaelezea uwepo wa hali hii ya kifugaji (kujitegemea, kutoamini yoyote, kutotengeneza ushirika).

◙

**NASB “ataishi mashariki mwa ndugu zake wote”**
**NKJV “na yeye atakaa mahali walipo ndugu zake wengine wote”**
**NRSV “na ataishi kidhaifu kati ya jamaa zake wote”**
**TEV “ataishi mbali na ndugu zake wote”**
**NJB “ataishi maisha yake katika uasi mbele za ndugu zake”**

Tungo hii, “kuelekea mashariki,” inaonekana kuwa na asili mbili: (1) kuelekea mashariki ya (kibayana “kabla ya kukutana na,” BDB 815) na (2) “katika uasi/ufidhuli wa.” Asili zote mbili zinaonekana kuhusiana katika muktadha huu na kuelezea hakika kabila la Bedouin la Mashariki ya Kati.

**16:13-14** Tungo “Mungu (*El*) aonaye” zinahusiana na jina kwa ajili ya kisima ambacho kinapatikana katika mstari wa 14. Katika sehemu hizi za Mwanzo Mungu anaitwa kwa majina mengi. Kwa kutazama majina haya yote, tunashangazwa kwa upendo wa Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (na hapa kuna mwanamke mtumwa wa Kimisri).

**16:13 “Hata hapa nimemwona yeye anionaye na kuendelea kuwa hai?”** Ilieleweka vibaya katika Mashariki ya Karibu kwamba kumwona Mungu kulifuatiwa na kifo (kama vile Mwanzo 32:30 na Kutoka 33:20). Hajiri anashtushwa kwamba Mungu (yaani malaika wa Bwana) angemwendea na kuja karibu na kwamba angemuona Yeye na aendelee kuishi. Ni ngumu katika muktadha wa kujua kama

1. Alishangazwa kuona udhihirisho wa kimwili wa uungu (yaani niliona uungu)
2. alishangazwa kwamba Mungu alimuuona yeye na akaja kwake kwa kutiwa moyo na kujali kiasi kile (Mungu aliniona mimi)

Mimi nafikiria #2 inashabihiana vyema na muktadha na baadaye jina la kisima katika mstari wa 14. *Anchor Bible Commentary* on Genesis inasema kwamba jina linaoneshwa katika toleo la MT katika namna ambayo haijazoeleka kuruhusu uwezekano wote wa namna mbili (ukurasa 110).

Hii ni sehemu pekee katika Agano la Kale ambapo mtu anatoa jina kwa Mungu. Siku zote Mungu anajifunua mwenyewe kwa kutoa muunganiko wa jina (yaani *El* fulani, YHWH fulani, *Elohim* fulani). Pia tambua kwamba

kutoa majina huku kwa kipekee kulifanywa na binti wa kitumwa mwenye mateso wa kimisri. YHWH anamtafta na kumkabili. Upendo wake ni wa ajabu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:15-16**

**[15] Hajiri akamzalia Abramu mwana wa kiume; Abramu akamwita jina lake Ishmaeli, yule mwanawe, ambaye Hajiri alimzaa. [16] Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka themanini na sita, hapo Hajiri alipomzalia Abramu Ishmaeli.**

**16:15-16** Musa anaendelea kumfahamisha msomaji juu ya umri wa Abramu ili kwamba tuweze kufuatilia maisha yake katika namna ya matukio yenye mfuatano, ambayo yanafanyika muhimu katika ahadi za Mungu juu ya mtoto maalumu pamoja na Sarai katika umri wake wa uzee.

**16:15** Biblia haijaandika swali wala kusita kwa upande wa Hajiri kuhusu ahadi ya YHWH, kama inavyotokea kwa Abramu

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kweli gani kuu za kithiolojia zinazowasilishwa katika sura za 15 na 16?
2. Orodhesha rejea ambazo Mungu anatengeneza agano na Ibrahimu. Je ahadi zake ni zenye mashariti/vigezo au zisizo na mashariti/vigezo? Je hii ina maanisha nini kwetu?
3. Malaika wa Bwana ni nani? Kwanini?
4. Kwanini kuna onekana kuwa na umuhimu sana wa Mungu kwenda kumtafta Hajiri na mtoto wake?

# MWANZO 17

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Ibrahimu na agano la tohara | Ishara za agano | Agano la kudumu | Tohara, ishara ya agano | Agano na tohara |
| 17:1-8 (1-5) | 17:1-8 | 17:1-8 | 17:1-6 | 17:1-3a |
| | | | | 17:3b-8 |
| | | | 17:7-8 | |
| 17:9-14 | 17:9-14 | 17:9-14 | 17:9-14 | 17:9-14 |
| 17:15-22 | 17:15-22 | 17:15-22 | 17:15-16 | 17:15-22 |
| | | | 17:17-18 | |
| | | | 17:19-22 | |
| 17:23-27 | 17:23-27 | 17:23-27 | 17:23-27 | 17:23-27 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.K

## HISTORIA YA NYUMA

A. Mwanzo 17 ni uthibitisho wa tena wa agano uliofanywa katika Mwanzo 15 ambao ulitajwa katika Mwanzo 12.
B. Ilichukua takribani miaka kumi na minne tangu kuahidiwa mwana katika Mwanzo 15. Mwanzo 17 inatengeneza hatua kwa ajili ya Mungu kutimiliza mpango wake kwa Abramu kupia Sarai.
C. Sura hii ni mwendelezo wa masihala ulioegama juu ya majina binafsi yalihusishwa. Majina yalikuwa ni kitu cha muhimu kwa Waebrania (yaani 16:11-12). Kwenye kipindi muhimu katika maisha yao, mara nyingi waliyabadili majina yao kuonyesha kile kinachotokea maishani mwao.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 17:1-8**
**1 Abramu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, Bwana akamtokea Abramu, akamwambia, Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu, ukawe mkamilifu. 2 Nami nitafanya agano langu kati ya mimi na wewe, nami**

**nitakuzidisha sana sana. [3]Abramu akaanguka kifudifudi. Mungu akamwambia, akasema, [4]Mimi, agano langu nimefanya nawe, nawe utakuwa baba wa mataifa mengi, [5]wala jina lako hutaitwa tena Abramu, lakini jina lako litakuwa Ibrahimu, kwani nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi. [6]Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana, nami nitakufanya kuwa mataifa, na wafalme watatoka kwako. [7]Agano langu nitalifanya imara kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako. [8] Nami nitakupa wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni, nchi yote ya Kanaani, kuwa milki ya milele; nami nitakuwa Mungu wao.**

**17:1-5** Toleo la NASB linaligawa hili katika sehemu mbili za ushairi, 1b-2; 4-5, lakini matoleo ya NKJV, NRSV, TEV, NJB, na JPSOA hayagawi.

**17:1 "miaka tisini na kenda"** Kitabu cha Mwanzo kinaweka kumbukumbu ya miaka ya Abramu mara kwa mara ili kuleta utaratibu wa kupanga matukio ya kufanya hija ya imani yake.

1. Akiwa na miaka 75 , 12:4 – maono ya kwanza ya YHWH juu yake
2. Akiwa na miaka 86 , 16:16 – anamzaa Ishmaeli
3. Akiwa na miaka 99 , 17:1 – maono ya tatu ya YHWH juu yake
4. Akiwa na miaka 100 (hesabu ya jumla), 17:17 – umri katika sura ya 17
5. Akiwa na miaka 99 , 17:24 –alipotahiriwa
6. Akiwa na miaka 100 , 21:5 –anamzaa Isaka
7. Miaka kamili haijulikani , 24:1 – "umri unasonga"
8. Akiwa na miaka 175 , 25:7 – anafariki

◙ **"Bwana"** "YHWH" ni jina la agano kwa ajili ya Mungu lililotumika katika Kut. 3:14. Linatumika hapa tu katika sura hii. Linaonekana kutumika awali kabisa katika uzao wa Sethi (kama vile 4:26; na mara nyingi na wazee wa umri). Hata hivyo, toka Kut.6:3 tunaambiwa kuwa wazee wa umri walimwita *El Shaddai*, na sio YHWH. Yawezekana walimwita YHWH, lakini hakujua umuhimu kamili wa jina mpaka pale alipojitokeza kwa Musa katika kichaka cha moto. Angalia Mada Maalum katika 12:1.

◙ **"Bwana akamtokea Abramu na kusema"** Mungu alimtokea Abramu mara nyingi (yaani., 12:7; 18:1), lakini ilikuwa yapata miaka kumi na mitatu tangu kumbukumbu ya mwisho kuwekwa. Dhahili, YHWH alikuwa akiijaribu imani ya Abramu.

◙ **"Mimi ni Mungu Mwenyezi"** Wadhifa wa jina "Mungu Mwenyezi" ni *El Shaddai*. Asili ya neno la istilahi hii (BDB 994) haijulikani. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa linamaanisha "mwenye kujitosheleza." Tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania na toleo la Kilatini linafuata uelewa huu kwa kulitafsiri "Mungu (*El*) Mwenyezi."Inavyoonekana hili lilikuwa ni jina la kiukuu wa familia kwa ajili ya Mungu (kama vile Kut. 6:3). Limetumika mara sita katika kitabu cha Mwanzo na mara thelathini na moja katika kitabu cha Ayubu. Albright anadai kuwa linatokana na mzizi wa lugha ya Akkadi ambao waweza kumaanisha Mlima au jabari (kama vile Zab. 18:1, 2). Kama istilahi inamaanisha , "Mungu wa milima" kama maana ya kweli, hivyo lazima liaksi hadithi za kubuni za Wakaanani (kama vile Isa. 14:13; Ezek. 28:2) au dini ya huko Babeli (yaani ziggurats iliyojengwa juu ya milima iliyotengenezwa na wanadamu, kama vile Mwanzo 11) pale walipo iabudu miungu yao. Kivyovyote vile kusudi la mwanzo lingemaanisha, mwanzoni kabisa mwa Kutoka 19-20 mtazamo bado utaelekea kwa Mungu wa Mlima Sinai (kama vile Amu. 5:5). Angalia Mada Maalum katika 12:1.

◙ **"uende mbele yangu"** Hii ni moja kati ya amri mbili za YHWH kwa Abramu.

1. Uende – BDB 229, KB 246, *Hithpael* KAULI SHURUTUTISHI
2. Ukawe mkamilifu – BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI SHURUTUTISHI

YHWH alikuwa akitafuta ushirika na Abramu kama alivyokuwa na Adamu, Enoko, na Nuhu. Kifungu "uende mbele yangu" kinaashiria ushirika binafsi; wa ndani, maisha na imani ya kitofauti! Huu ni msisitizo juu ya uhusiano wa imani ya stadi ya maisha ambao ni mlinganyo wa tamko la kisheria la kuhesabiwa haki kwa njia ya neema kupitia imani inayoonekana katika 15:6. Katika agano jipya Paulo na Yakobo wanaiunganisha hii misisitizo kwa pamoja ya

maisha yanayo mfanana Yesu (kama vile Warumi 4 na Yakobo 2). Tambua kuwa stadi ya maisha ni sharti kwa ajili ya agano (kama vile mst. 9). Maagano yote ya Agano la Kale sio yenye masharti juu ya Mungu na yana masharti juu ya wajibu wa mwanadamu. Istilahi ile ile (BDB 229, KB 246), uende, imetumika kwa Henoko (kama vile Mwa. 5:24), na Nuhu (kama vile Mwa. 6:9) imani katika stadi ya maisha.

◙ **"Ukawe mkamilifu"** Huu mzizi wa Kiebrania (KITENZI, BDB 1070, NOMINO 1070, miundo ya VIVUMISHI viwili, 1070 & 1071) inaashiria "kwa moyo wake wote," "mkamilifu," "thabiti," "mwaminifu," na "pasipo na hatia." Lilitumika kwa

1. Nuhu – Mwa. 6:9
2. Abramu – Mwa. 17:1 (amri)
3. Abimeleki – Mwa. 20:5-6
4. Yakobo – Mwa. 25:27 (mara nyingi hutafasiliwa "mpole" or "mnyenyekevu")
5. Ayubu – Ayubu 1:1,8; 2:3
6. Israeli – Kumb. 18:13
7. Daudi – II Sam. 22:24; Zab. 18:23,25,32
8. YHWH – Kumb.32:4; II Sam. 22:31; Zab. 18:30

Inamaanisha mnyama aliye safi, ni uwasilishaji kamili wa aina yake, ambao ulikubalika kwa ajili ya dhabihu (yaani Kut. 12:5; 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; 4:3,23,28,32).

## MADA MAALUM: ASIYE NA HATIA, ASIYE NA KOSA, WALA MAWAA

A. Maelezo ya ufunguzi
   1. Hii dhana kithiolojia inaelezea asili ya mwanadamu (yaani., Mwanzo 1, bustani ya Edeni)
   2. Dhambi na uasi umekwisha haribu mazingira haya ya ushirika kamili (yaani Mwanzo 3)
   3. Wanadamu (wa kiume na wa kike) wanatamani urejesho wa ushirika na Mungu kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wake Mungu (yaani Mwa. 1:26-27)
   4. Mungu ameshughulika na dhambi ya mwanadamu kwa njia kadhaa kwa kutumia
      a. Watu wa Mungu (yaani Ibrahimu, Musa, Isaya)
      b. mtindo wa utoaji dhabihu (yaani Walawi 1-7)
      c. Mifano ya ki-Mungu (yaani Nuhu, Ayubu)
   5. Hatimaye Mungu anamtoa Masihi
      a. Kama ufunuo kamili wake mwenyewe (kama vile Yn. 1:1-14; Kol. 1:13-17; Ebr. 1:2-3)
      b. Kama dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
   6. Wakristo waliumbwa pasipo lawama
      a. Rasmi kupitia haki ya Kristo iliyowekwa ndani yetu (kama vile. Rum. 4:3,6,8,11,22,23,24; Yakobo 2:23)
      b. Kwa mwendelezo wa kazi ya Roho (Yn 16:8-1)
      c. Lengo la Ukristo ni kufanana kama Kristo (kama vile. Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tit. 2:14; 1 Pet. 1:15), ambao katika ukweli, ni urejesho wa taswira ya Mungu iliyopotea katika anguko la Adamu na Hawa.
   7. Mbinguni ndio urejesho wa ushirika kamili wa Bustani ya Edeni. Mbinguni ndiko Yerusalem Mpya inayotegemewa kuja nje ya uwepo wa Mungu (kama vile Ufu.21:2) kwenye ardhi iliyotakaswa (kama vile 2 Pet. 3:10). Biblia ilianza na kuishia kwenye maudhui yale yale ya:
      a. Ushirika binafsi wa ndani na Mungu
      b. Ndani ya muundo wa bustani (Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)
      c. Kwa maelezo ya kinabii, uwepo na urafiki wa wanyama (kama vile Isa. 11:6-9)

B. Agano la Kale
   1. Kuna maneno mengi ya Kiebrania ya aina tofauti ambayo yanachukua dhana nzima ya utimilifu, pasipo lawama, pasipo hatia ambayo yangalikuwa vigumu kuyataja na kuonyesha namna yahusianavyo
   2. Maneno makuu yanayochukua dhana nzima ya utimilifu, kutokuwa na kosa, au kutokuwa na hatia

(kutokana na Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kur. 94-99) ni:
   a. *shalom* (BDB 1022, KB 1532 )
   b. *thamam* (BDB 1070, KB 1743)
   c. *calah* (BDB 478, KB 476)
3. Tafsiri ya maandiko ya Kiyunani (yaani Biblia ya kanisa la mwanzo) inazitafsiri dhana hizi za Kiebrania kwa maneno ya lugha ya kawaida ya Koine yaliyotumika katika Agano Jipya (angalia C hapa chini)
4. Dhana muhimu imejikita kwenye mtindo wa utoaji dhabihu
   a. *amōmos* (kama vile Kut. 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; Hes. 6:14)
   b. *amiantos* and *aspilus* pia yana vidokezo vya kimadhehebu

C. Agano Jipya
1. Dhana ya kisheria
   a. Kidokezo cha sheria cha kimadhehebu ya Kiebrania kimetafasiriwa kwa neno *amōmos* (BDB 1071, kama vile Efe. 5:27; Flp. 2:15; 1 Pet. 1:19)
   b. Vidokezo vya sheria za Kiyunani (kama vile. 1 Kor. 1:8; Kol. 1:22)
2. Kristo yule asiye na dhambi, lawama, hatia (*amōmos*, kama vile. Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19)
3. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kumfuata Yeye (*amōmos*, kama vile. Efe. 1:4; 5:27; Fil. 2:15; Kol. 1:22; 2 Pet. 3:14; Yuda 1:24; Ufu. 14:5)
4. Dhana hii pia inatumiwa na viongozi wa kanisa
   a. *anegklētos*, "pasipo mashitaka" (kama vile. 1 Tim. 3:10; Tit. 1:6-7)
   b. *anepilemptos*, "zaidi ya shutuma" au "hapana nafsi ya lawama" (kama vile. 1 Tim. 3:2; 5:7; 6:14; Tit 2:8)
5. Dhana ya "kutokuwa najisi" (*amiantos*) imetumika kwa
   a. Kwa Kristo mwenyewe (kama vile. Ebr. 7:26)
   b. Urithi wa Wakristo (kama vile. 1 Pet. 1:4)
6. Dhana ya "ujumla" au "kusikika" *(holoklēria*) (kama vile. Mdo. 3:16; 1 The. 5:23; Yakobo 1:4)
7. Dhana ya kuwa "pasipo kosa," "kutokuwa na hatia" linaelezewa kwa *amemptos* (kama vile. Lk 1:6; Flp. 2:15; 3:6; 1 The. 2:10; 3:13; 5:23)
8. Dhana ya "kutokuwa kwenye lawama" linaelezewa kwa *amōmētos* (kama vile. 2 Pet. 3:14)
9. Dhana ya "kuwa safi," "pasipo doa" mara nyingi zimetumika katika sura zenye moja ya maneno ya hapo juu (kama vile. 1 Tim. 6:14; Yakobo 1:27; 1 Pet. 1:19; 2 Pet. 3:14)

D. Idadi ya maneno katika Kiebrania na Kiyunani yanayoelezea dhana hii yanaonyesha umuhimu wake. Mungu ametupatia mahitaji yetu kupitia Kristo na sasa anatuita kuwa kama Yeye.
Waamini kinafasi
, kihukumu wametangazwa kuwa "sawa" "wenye haki" "wasio na lawama" kwa kazi ya Kristo. Sasa waamini wanatakiwa kumiliki nafasi yao. "Tembeeni katika nuru kama Yeye alivyo nuruni" (kama vile. 1 Yn 1:7). "tembeeni kwa thamani ya mwito wenu" (kama vile Efe. 4:1,17; 5:2,15). Yesu ameirejesha taswira ya Mungu. Ushirika wa ndani sasa ni dhahiri, lakini kumbukeni Mungu anahitaji watu wanaoaksi tabia yake, kama Mwana wake alivyofanya, kwa ulimwengu uliopotea (yaani., mataifa). Hatukuitiwa chochote bali utakatifu (kama vile. Mt. 5:20,48; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:13-16). Utakatifu wa Mungu, sio tu kisheria, bali namna uishivyo!

**17:2 "Nami nitafanya"** Ahadi ya YHWH ni
1. "kulifanya" agano lake – BDB 678, KB 733, *Qal* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO; hiki ni KITENZI cha kawaida chenye vidokezo vingi. KITENZI kama hicho kimetumika kwenye ahadi ya YHWH ya "kuwapa" nchi uzao wa Abramu katika 12:7; 13:15; 15:7,18 na malalamiko ya Abramu kuwa YHWH hakuwahi "kumpa" yeye watoto 15:3. Kumbuka namna vile neno limetafasiliwa katika sura ya 17.

| | **NASB** | **NIV** |
|---|---|---|
| a. | Anaanzisha, mst. 2 | Anathibitisha, mst. 2 |
| b. | Anafanya, mst. 5 | Anafanya, mst. 5 |
| c. | Anafanya, mst. 6 | Anafanya, mst. 6 |

d. Anatoa, mst. 8 | Anatoa, mst. 8
e. Anatoa, mst. 16 | Anatoa, mst, 16
f. Anafanya, mst. 20 | Anafanya, mst. 20

2. “anazidisha” – BDB 915, KB 1176, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU iliyotumika kwa maaana ya KITENZI CHENYE KUSIHI (yaani .,uzao mwingi)
3. Nchi imetajwa katika mstari wa 8

◙ **“Agano kati Yangu na wewe”** Agano ndio wazo kuu la Agano la Kale. YHWH alimwijia Abramu katika hali ya neema, lakini alitakiwa kuwajibika, sio tu katika ile imani ya mwanzo, bali pia katika maisha ya imani. Kuna haki za kiushirika na uwajibikaji. Agano la Kale sio kati ya walio sawa, bali linatengeneza kipengere cha kitamaduni kwa ajili ya mikataba ya Wahiti/watu wa Mfereji wa Suezi ya mwaka 2000 K.K. Agano hili linatimiza vigezo katika mst.7

◙**“Nami nitakuzidisha sana sana”** Hili limekuwa wazo kawaida la ahadi ya YHWH kwa Abramu katika umri wake wa uzee akiwa na mkewe aliyekuwa mgumba (kama vile Mwa. 12:2; 15:2-5; 13:16; 17:6). Likaja kuwa ndio msingi wa kubadili jina lake. Kwa ukumbusho tu, huu ulikuwa ndio mpango wa Mungu wa mwanzo kwa ajili ya miundo ya maisha (kama vile Mwanzo 1 na Isaya 60).

**17:3 “Abramu akaanguka kifudifudi”** Hii ilikuwa ni ishara ya kutoa heshima na unyenyekevu kwa ajili ya Mungu (kama vile 18:2), lakini kumbuka 17:17.

◙ **“Mungud”** *Elohim* ni jina la kawaida kwa ajili ya Mungu huko Mashariki ya Karibu, likisimama juu ya mzizi wa neno *El*. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa lilisisitiza uweza wa Mungu na uthibiti wa asili kama muumbaji, wakati YHWH akisisitiza neema yake na ukombozi. Hii inaonekana kuwa nadharia nzuri zaidi kuliko ile ya ukosoaji (JEDP). Angalia Mada Maalum katika 12:1.

**17:4 “na utakuwa ni baba wa mataifa mengi”** Tambua kuwa mataifa mengi zaidi ya Israeli yaliyojumuishwa katika uzao wa Ibrahimu (kama vile 35:11; 48:4,19). Hili linatengeneza hatua kwa ajili ya uelewa wa Agano Jipya wa Ibrahimu kuwa baba wa wale wote wenye imani (kama vile Rum. 2:28-29; Gal. 3:1 na kuendelea).

**17:5 “Abramu”** Jina lake litabadilika na kuwa “Ibrahimu,” likimaanisha “baba wa walio wengi.” Hii sio asili ya neno la kisayansi, bali ni asili ya neno halisi linalojulikana lenye kuainisha hizi sura za awali kitabu cha Mwanzo. Wengi wamesema kuwa “Ibrahimu”anasimamia kwenye ahadi katika 12:2.

**17:7 “Nitalifanya”** KITENZI hiki (BDB 877, KB 1086, *Hiphil* KAULI TIMILIFU) katika shina la neno *Hiphil* linatumika na kiapo kuhakikisha utimilifu wake (kama vile 6:18; 17:19; Kut. 6:4; Law. 26:9; Ezek. 16:62). YHWH Mwenyewe atakuja ili kuzitimiliza ahadi zake.

◙ **“ni agano la milele”** Neno la Kiebrania *’olam* (BDB 761) ni kutokana na mzizi wa neno wenye kumaanisha “kujificha.”sio muhimu kumaanisha “milele na milele” (yaani kur. 8,13,19), bali ni lazima litafsiliwe katika muktadha. Angalia Mada Maaalum katika 13:14.

**17:8 “Nami nitakupa wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni ”** Hii ni moja ya ahadi ya YHWH (kama vile 12:7; 13:15, 17; na 15:18) na baadaye kwa Yakobo katika 48:4.

◙ **“Nitakuwa Mungu kwao”** Hii ikaja kuwa ni lugha maalum ya agano (kama vile., Kut. 6:7; 29:45; Law. 26:12,45; Hes. 15:41; Yer. 7:23; 11:4; 24:7; 30:22; 31:1,33). YHWH kiupekee, kwa maana ya pamoja, alimchagua Abramu na uzao wake kumwakilisha Yeye kwa mataifa (kama vile Kumb. 7:6; 14:2; 29:12-13). YHWH anayapenda mataifa kupitia yeye.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):17:9-14**
**[9]Mungu akamwambia Ibrahimu, Nawe ulishike agano langu, wewe na uzao wako kwa vizazi vyao baada yako. [10] Hili ndilo agano langu utakalolishika, kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, Kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa. [11] Mtatahiriwa nyama ya magovi yenu, na jambo hilo litakuwa ishara ya agano kati ya mimi na ninyi. [12] Mtoto wa siku nane atatahiriwa kwenu, kila mwanamume katika vizazi vyenu, mzaliwa nyumbani, na mnunuliwa kwa fedha, kila mgeni asiyekuwa wa uzao wako. [13] Mzaliwa nyumbani mwako, na mnunuliwa kwa fedha yako, lazima atahiriwe; na agano langu litakuwa katika mwili wenu, kuwa agano la milele. [14] Na mwanamume mwenye govi asiyetahiriwa nyama ya govi lake, mtu yule atatengwa na watu wake; amelivunja agano langu.**

**17:9 "nawe ulishike agano langu"** KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) kinajirudia katika 17:10. Kumbuka kuwa agano lilikuwa ni la kimasharti kwa kwa mujibu wa imani ya Ibrahimu, kwa namna yote mwanzoni na hata katika maisha yake yote. Ukweli huu unaweza kuonekana vizuri katika 26:5; Kut. 12:24; 13:10; 15:26; 19:5; 20:6; 23:17; Law. 18:4,5,26,30; 19:19,37; 20:8,22; 22:31; 25:18; 26:3; Kumb. 4:2,6,9,23,40; 5:1,29; 6:2,3,12,17,25; 7:9,12; 8:1,2,6,11; 10:13; 11:1,8,22, n.k. utii ni wa muhimu, na si suala la uchaguzi!

**17:10 "atatahiriwa"** Tohara (BDB 557 II) haikuwa ni kanuni ya kawaida katika nchi za Mashariki ya karibu ya kale. Watu wote waliozunguka maeneo hayo waliwatahiri watoto wao katika umri wa ujana isipokuwa Waashuru, watu wa Babeli, Wahivi, Wahori wa Palestina ya kati na (watu wa Aegea) ambao walivamia Pwani ya kusini mwa Palestina katika mwaka wa 1200's K.K. (kama vile Yer. 9:25-26). Hata hivyo, tohara ilikuwa na kusudi la kidini kwa Waisraeli. Siku zote ilikuwa ni alama ya nje yenye kuonyesha imani ya ndani (kama vile Kumb. 10:16; Yer. 4:4; 9:26; Rum.
2:28-29; Kol. 2:11-13).

**17:12-14** Jamii zingine na watu tofauti na Waisraeli walijumuishwa kwenye agano ikiwa walikuwa na utii kwenye mapenzi ya Mungu (kama vile Kut. 12:44; 20:10). Hiki ni kipimo cha Agano la Kale kwa ajili ya imani ya wale wenye kumiliki kaya kama inavyoonekana katika Agano Jipya (kama vile Mdo. 10:2; 11:14; 16:15,31-34; 18:8)

**17:12** Neno "tohara" (BDB 557 II) limetajwa mara nyingi katika sura hii.

1. mst. 10 – *Niphal* KITENZIJINA HALISI
2. mst. 11 – *Niphal* TIMILIFU
3. mst. 12 – *Niphal* ISIO TIMILIFU
4. mst. 13 – *Niphal* KITENZIJINA HALISI (muunganikano wa KITENZI KISICHO TIMILIFU na KITENZIJINA HALISI kinaimarisha kitendo, "hakika yawapasa kutahiriwa")
5. mst. 24 – *Niphal* KITENZIJINA UNGANISHI
6. mst. 25 – *Niphal* KITENZIJINA UNGANISHI
7. mst. 26 – *Niphal* TIMILIFU
8. mst. 27 – *Niphal* TIMILIFU

YHWH alichukua utendaji wa kitamaduni wa kawaida, na kubadili utaratibu wao wa muda wa kuanza na kuutumia kama alama ya kuonekana kwa watu wake wa kipekee. Hii haikuwa kwa maana ya usafi bali ni kwa kusudi la kidini.

**17:14 "mtu yule atatengwa na watu wake"** Hiki ni KITENZI kile kile kilichotumika katika kifungu "kujitenga na agano" (ni shina la neno *Qal*, kama vile 15:10). Katika shina la neno *Niphal* kinamaanisha adhabu ya kifo (kama vile Kut. 12:15,19; 30:33,38; 31:14; Law. 7:20,21,25,27; 17:4,9,14; 18:29; 19:8; 20:17,18; 22:3; 23:29; Hes. 9:13; 15:30,31; 19:13,20; angalia kumbukumbu katika toleo la NIDOTTE, juzuu ya 3, uk. 431). Kutokutii kulikuwa na matokeo mabaya. Kuliathiri matumizi ya "agano la milele" kwa watu binafsi.
Kuna baadhi ya wasomi wanaopendelea kukiona KITENZI hiki kama kinavyomaanisha kuvunja ushirika au kutengwa kwenye jamii badala ya kifo. Majadiliano ya wasoni bado yangali yakiendelea juu ya hoja hii.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 17:15-21**
**[15]Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara.[16] Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake. [17]Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa? [18]Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. [19] Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake. [20]Na kwa habari za Ishmaeli nimekusikia, nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu. [21]Bali agano langu nitalifanya imara kwa Isaka, ambaye Sara atakuzalia majira kama haya mwaka ujao.**

**17:15 "Sarai, jina lake litakuwa Sara"** Majina yote yanamaanisha kitu kile kile, lakini moja ni la muda mrefu. Baadhi wanafikiri mzizi wa neno ni "malkia" (BDB 979 I, KB 1354 I, Sara - KB 1354 II) kutokana na KITENZI "kutawala,"lakini pia yawezekana ni kutoka katika mzizi wa neno "kupambana," ambalo laweza kuwa ni zuri kwa sababu ya uhusiano wa mzizi wa neno "Israeli" (kama vile 32:28, BDB 975 I), ambalo linatoka kwenye mzizi wa neno "pambana"(KB 1354 I).

Sara, mtazamo wa mazingira ya nyuma

1. alikuwa ni mke wa Ibrahimu
2. alikuwa mgumba, Mwa. 11:29-30
3. alikuwa ni dada yake, Mwa. 20:12
4. alikuwa ni mzuri wa sura, Mwa. 12:10-13; limedokezwa katika 20:1-7
5. alikuwa ni binti mwenye wivu, Mwa. 16; 21:8-21
6. alicheka, kama Ibrahimu alivyofanya (Mwa. 17:17), kwenye ahadi za Mungu, Mwa. 18:12-15
7. Alikufa akiwa na miaka 127 na akazikwa huko Hebroni kwenye pango la Makpela, Mwa. 23:2-20
8. Ametumika kwenye istiari akiwa na Hajiri, Gal. 4:21-31
9. Amechuliwa kuwa kama mfano kwa wanawake, I Pet. 3:1-6

**17:16 "tena nitakupa Mwana kwake"** Imechukua takribani miaka kumi na mitatu tangu itolewe ahadi. Ishamaili alizaliwa kupitia Hajiri, lakini haukua uzao ulioahidiwa kulianzisha agano. Ibrahimu alimwamini Mungu katika 15:6 (Rum. 4:3), lakini ilichukua muda mrefu mpaka pale agano likaja kutimilizwa.

◙ **"nitambariki"** Matoleo ya Biblia ya Kilatini na Kishamu, yote yana jinsi ya kiume yanayomrejerea Isaka, lakini maelezo yanafanana nay ale aliyopewa Abramu.

◙ **"naye atakuwa mama wa mataifa, na Wafalme wa makabila watatoka kwake"** Tena angalia msisitizo zaidi juu ya Waisraeli. (kama vile mstari wa 6).

**17:17** YHWH anamjaribu Ibrahimu tena. Baada ya miaka yote hii (yaani., 13) bado anaendelea kuamini (kama vile 15:6) atapata mtoto (mwanaume, mrithi)? Ibrahimu "anacheka" (17:17); Sara "anacheka" (18:12,13,15). Hili linamaanisha nini?

1. Furaha ya kuitimiliza ahadi (kama vile 21:6)
2. Ishara za mashaka (kama vile 19:14)

Paulo, katika Rum. 4:19, inalenga juu ya imani ya Ibrahimu, lakini ilikuwa ni imani endelevu baada ya kujaribiwa au ni imani ya mwanzo inayojaribu kusaidia kuitimiliza baada ya kumchukua Hajiri? Hawa hawakuwa watu wakamilifu. Hakuna watu "wakamilifu!"Mungu hahitaji imani timilifu! Mlengo kwenye kitabu cha Mwanzo ni uaminifu wa YHWH, na sio Abramu, au Sara!
Kumbuka utofauti kati ya kitendo cha nje cha Ibrahimu, "akaanguka kifudifudi," lakini mrejesho wa ndani "akacheka"! ni Mungu tu ndiye awezae kuviona vyote.

**17:18** Hili laweza kuwa ni jaribio "kumsaidia" Mungu kuitimiza ahadi yake (kama Hajiri) au lakini yaweza kuwa ni mwonekano wa pendo halisi la Ibrahimu kwa Ishmaeli. Calvin anadai kuwa hii ilikuwa ni kukosekana kwa imani juu ya upande wa Ibrahimu na kuutumia mstari huu kwa maana iliyo hasi.

◙**"Ishmael"** Ishmaeli (BDB 1035) ni mwana wa Hajiri, mjakazi wa sara. Jina lake linaonekana kumaanisha "Mungu anajibu" na yawezakuwa ni mchezo kwa maombi ya Ibrahimu na Hajiri. Ishmaeli ni baba wa kabila za waarabu (kama vile 16:10-12).

**17:19 "utamwita jina lake Isaka"** Majina yote ya wazee wa kale yanabadilika pale tu walipoanza ushirika na YHWH isipokuwa Isaka. Hii ni kwa sababu jina hili alipewa na Mungu tokea mwanzo. "Isaka" (BDB 850) ni jina lenye masikhala juu ya neno "akacheka" (BDB 850). Hili limeelezewa katika 21:6. Kutokuamini kwa Sara kukabadilika na kuwa "kicheko"na furaha!

◙ **"agano la milele"** Hili ni neno linalofanana na la Kiebrania *'olam* (kama vile kur. 6, 8). Inamaanisha "kwa kipindi cha mbele kisichojulikana," na sio "milele na milele." Angalia Mada Maalum katika13:14.

**17:20** Angalia Mwanzo 25:12-18, ambapo uzao wa Ishmaeli unaelezewa.

**17:21** Huu ni utimilizo wa ahadi ya agano la Mungu unapoanza katika Mwanzo 12

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 17:22-27**
**[22]Mungu akaacha kusema naye, akapanda kutoka kwa Ibrahimu. [23] Ibrahimu akamtwaa Ishmaeli mwanawe, na wote waliozaliwa nyumbani mwake, na wote walionunuliwa kwa fedha yake, wanaume wote wa watu wa nyumba ya Ibrahimu, akawatahiri nyama ya magovi yao siku ile ile, kama Mungu alivyomwambia. [24] Naye Ibrahimu alikuwa mwenye umri wa miaka tisini na kenda alipotahiriwa nyama ya govi lake. [25] Na Ishmaeli mwanawe alikuwa mtu wa miaka kumi na mitatu, alipotahiriwa nyama ya govi lake. [26] Siku ile ile akatahiriwa Ibrahimu na Ishmaeli mwanawe. [27] Na watu wote wa nyumba yake, wazaliwa nyumbani, na wanunuliwa kwa fedha katika mkono wa mgeni, wakatahiriwa pamoja naye.**

**17:22 "Mungu akapanda"** Mungu alitenda kulinganisha na jinsi watu wa kipindi hicho walimtegemea atende (kama vile 11:5; 35:13). Kwa watu wa ki-Magharibi ya sasa kifungu hiki kinamaanisha kupanda, lakini yawezakuwa ni nahau kwa ajili ya "kuondoka ghafla."

**17:23 "siku ile ile, kama Mungu alivyomwambia"** Hii inaaksi utii wa Ibrahimu (kama vile 12:4; 22:3).

**17:25 "na Ishmaeli mwanae alikuwa na miaka kumi na mitatu alipotahiriwa nyama ya govi lake"** Tohara bado ni kanuni pindi vijana wanapopevuka kwa Waarabu, wanalolitenda pindi wakifikisha miaka kumi na mitatu. Hili yumkini linaaksi habari za Kibiblia. Inastahili kukumbukwa kuwa Waisraeli waliwatahili watoto wao wakiwa na siku nane, ambayo ilikuwa ni ishara ya ushirika wa agano, na sio ishara ya imani binafsi (madhehebu ya leo hutumia ufanano huu kwa ubatizo wa watoto wachanga). Imani lazima iingie na kuiacha ikae ili agano lijulikane kwa mtu .

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa vipi Mwanzo 17 inahusianishwa na Mwanzo 12 na 15?
2. Ni kwa nini majina ya mababa wa imani yalibadilishwa?
3. je agano la kale lilikuwa la masharti au lisilo na masharti?

4. elezea maana ya agano na wajibu wake.
5. ni kwa vipi tohara ilihusiana au kutohusiana na mataifa yale yanayoizunguka?

# MWANZO 18

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Kuzaliwa kwa Isaka | Mwana wa Ahadi | Ziara ya Bwana kwa Ibrahimu na Sara | Mwana anahaidiwa Ibrahimu | Kivuli cha huko Mamre |
| 18:1-8 | 18:1-8 | 18:1-8 | 18:1-5a | 18:1-5 |
| | | | 18:5b | |
| | | | 18:6-8 | 18:6-8 |
| 18:9-15 | 18:9-15 | 18:9-15 | 18:9a | 18:9-15 |
| | | | 18:9b | |
| | | | 18:10a | |
| | | | 18:10b-12 | |
| | | | 18:14-14 | |
| | | | 18:15a | |
| | | | 18:15b | |
| | Ibrahimu Anasihi Kuhusu Sodoma | Maombi ya Ibrahimu kuhusu Sodoma na Gomora | Ibrahimu Anaomba msamaha juu ya Sodoma na Gomara | Ibrahimu Anasihi juu ya Sodoma |
| 18:16-21 | 18:16-21 | 18:16-21 | 18:16-19 | 18:16-21 |
| | | | 18:20-21 | |
| 18:16-33 | 18:22-33 | 18:22-33 | 18:22-25 | 18:22-26 |
| | | | 18:26 | |
| | | | 18:27-28a | 18:27-29 |
| | | | 18:28b | |
| | | | 18:29a | |
| | | | 18:29b | |
| | | | 18:30a | 18:30-32 |
| | | | 18:30b | |
| | | | 18:31a | |
| | | | 18:31b | |
| | | | 18:32a | |
| | | | 18:32b-33 | |
| | | | | 18:33 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya yapili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Hiki kipengele cha lugha ya kibinadamu kumwelezea Mungu (chenye kumzunguzia Mungu katika lugha ya kibinadamu). Hii aina ya mfumo wa kifasihi mara kwa mara unawatia hofu watoa maoni wa Kiyahudi. Hata hivyo, kwa wengi wetu walio ndani ya Kanisa, huu ni mwili wa awali wa Kristo ambaye kimwonekano unadhihirisha tendo halisi la Mungu (kama vile "Malaika wa Bwana" katika 12:7).

B. Kitabu cha Mwanzo 18-19 kinatupatia ukweli halisi wa pande zote za asili ya Mungu : upendo na hukumu. Hizi sifa hazionekani tu ndani ya Mungu, bali zinaweza kuhamishiwa (1) kwa watu wake wanaoliaksi pendo lake na (2) kwa watu wa Sodoma wanaoiaksi tabia ya yule Mwovu na, hivyo,wanao uzoefu wa ghadhabu ya Mungu.

C. Haijulikani ni kwa dhana gani katika sura ya 18 kuwa Ibrahimu aliwatambua wageni watatu kuwa kama kiumbe wa kiroho. Mengi ya hiki kilichoandikwa kimebobea katika utamaduni.
   1. Aliinama mbele ya watu wa nchi (kama vile Mwa. 23:7; 33:6-7; 42:6; 43:26)
   2. aliwaosha miguu yao (kama vile 19:2; 24:32; 43:24)
   3. aliwapa chakula (kama vile mst. 5)
   4. alisimama huku wakiwa wanakula (kama vile mst. 8)
   5. aliwaita *Adonai*, lakini katika maana ya "Bwana" (kama vile mst. 3)

Kwa upande mwingine wa shilingi kunaonekana kuwepo ishara kwamba huyu alielewa mapema sana kwamba hawa walikuwa na asili ya nguvu ya kiroho.
1. alikimbia mbio na kuwalaki (kama vile mst. 2,6, na 7), tendo ambalo halikuwa la kawaida kwa mwanaume ambaye ni mkuu wa familia katika kipindi cha joto
2. mlo aliouandaa ulikuwa mzito sana (kama vile mst. 6)
3. kisha akachukua ndama kutoka kundini, kitu ambacho hakikuwa cha kawaida (kama vile mst.7)

Ni wazi kuwa kutokea mstari wa 9 kwamba alimtambua Bwana kama kiumbe aliyekaa ndani ya mmoja wa wageni hawa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 18:1-8**

**[1] Bwana akamtokea Ibrahimu karibu na mialoni ya Mamre, alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari. [2] Akainua macho yake akaona, alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari. Naye alipowaona alipiga mbio kuwalaki kutoka mlangoni pa hema, akainama mpaka**

**nchi, [3]akasema, Bwana wangu, kama nimeona fadhili machoni pako nakuomba usinipite sasa mimi mtumwa wako. [4] Na yaletwe basi maji kidogo mkanawe miguu, mkapumzike chini ya mti huu. [5]Nami nitaleta chakula kidogo, mkaburudishe moyo, baadaye mwendelee, iwapo mmemjia mtumwa wenu. Wakasema, Haya, fanya kama ulivyosema. [6]Basi Ibrahimu akaenda hima hemani kwa Sara, akasema, Himiza vipimo vitatu vya unga safi, uukande, ufanye mikate. [7]Ibrahimu akapiga mbio kwenda kundini, akaleta ndama wa ng'ombe aliye laini, mzuri, akampa mtumishi, naye akahimiza kuiandaa. [8] Akatwaa siagi na maziwa, na ndama aliyoiandaa, akawaandikia mbele yao, akasimama karibu nao chini ya mti, nao wakala.**

**18:1 "Bwana akamtokea"** Hiki KITENZI "akamtokea " (BDB 906, KB 1157, *Niphal* KAULI ISIO TIMILIFU) kinatumika mara kadhaa katika kitabu cha mwanzo (kama vile 12:7 [mara mbili]; 17:1; 18:1; 26:2,24; 35:1,9). Hiki kinadokeza udhihirisho wa mwonekano binafsi. Kwa kuwa YHWH ni roho ya milele, huu mwonekano wa kimaumbile ni vigumu kuufafanua.

Inanivutia kwamba walimu wa Kiyunani wanasema kwamba sura ya 18 inahusianishwa moja kwa moja na sura ya 17 na kusudi la ziara ya Bwana ilikuwa ni kuona kama Ibrahimu amepona kutokana na maumivu ya kutahiriwa kwake. Likiwa kama jambo la ukweli, walimu wa sheria za Kiyahudi wanatambua kuwa hawa wageni wote watatu walikuwa malaika ambao kwa upekee walimwakilisha Bwana. Wanaeleza kwamba (1) malaika mmoja alikuja kwa ajili ya kumpasha habari Sara juu kubeba mimba kwake (2) mwingine alikuja kwa ajili ya kumponya Ibrahimu; na (3) mwingine alikuja kwa ajili ya kuiangamiza Sodoma.

**MADA MAALUM : MUNGU ANAELEZWA KAMA MWANADAMU (LUGHA YA KIBINADAMU)**

I. Aina hii ya lugha (yaani, Uungu unaelezwa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
   A. Viungo vya mwili
      1. macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zek. 4:10
      2. mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
      3. viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15;26:8
      4. masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; II Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
      5. uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
      6. vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
      7. sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
      8. miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
      9. umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
      10. malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
      1. kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
      2. kutembea (yaani sauti ya) - Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
      3. kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
      4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
      5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
      6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
   C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
      1. majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
      2. hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
      3. wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
      4. karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
   D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
      1. Baba

a. wa Israeli- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
b. wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
c. sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17

2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha Mwenyewe kwa viumbe vya kibinadamu. Hakuna msamiati mwingine kuliko ule wa kuanguka, manaeno ya kidunia. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni roho!
B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha Mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (baba, mama, mzazi, mpendwa)
C. Ingawa ni muhimu, Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kutoka 20; Kumbukumbu 5)
D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-3). Ujumbe wa Mungu ukafanyika Neno la Mungu (kama vile Yohana 1:1-8).

II. Kwa majadala wa kimhutasari, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura ya 10, "Anthropomorphism," in *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kr. 152-154

◙“**karibu na mialoni ya Mamre**” Sehemu hii inatajwa katika 13:18 na 14:13. Ni muhimu sana kwetu kutambua umuhimu wa miti iliyo katika maeneo ya nusu jangwa. Miti hii ilionekana kuwa na maana takatifu kwa sababu iliwakilisha uwepo wa maji chini ya ardhini. Pia miti hii ilitoa kivuli ambacho, katika eneo hili la ulimwengu, inaweza kumaanisha tofauti ya nyuzi joto 60. Katika ukweli huu huenda haukuwa mwaloni, bali ni miti ya mipira (kama vile UBS, *Helps For Translators, Fauna and Flora of the Bible*, kr. 154-155). Walimu wa Kiyunani wanadai kuwa huu haukuwa mti mmoja bali shamba la miti, jambo ambalo linaweza kuwa la kweli.

◙“**alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari**” Jambo hili ni la kiuhalisia sana kulingana na utamaduni wa siku hizo, kwa kipindi hicho cha jua kali, hema lilitakiwa kuwa wazi muda wote. Watu walikuwa wakipumzika kwa utulivu katika kipindi hicho ili kuepuka mguso wa jua.

**18:2“alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari”** Tunajifunza kutokana na 19:1 kwamba wawili kati yao walikuwa malaika (kama vile Ebr. 13:2).

◙ **“akainama mpaka nchi”** Hili linaweza kuonekana kama

1. aina ya salamu iliyojikita katamaduni (kama vile 23:7; 33:6-7; 43:28)
2. tendo la kiunyenyekevu (wageni wa ki- Ungu, yaani, 19:1; au YHWH Mwenyewe, 24:26,48,52)
3. ni tendo la uchaji (Ibrahamu alikuwa mhamiaji katika nchi ya kigeni, Tazama Tambuzi za Ndani za Kimuktadha, C)

**18:3 “Bwana wangu”** Hizi ni konsonanti za neno *Adonai* (אדני, BDB 10). Kiini cha neno kinatuambia kwamba wasomi wa maandiko ya Kimosoreti waliamini kuwa majina haya yalisimama badala ya mtu fulani (yaani, #3 hapa chini). Huu wadhifa umewekwa bayana katika njia tatu mbalimbali : (1) ya kwanza kama “Mkuu” au “Mtawala”; (2) ya pili ni WINGI wa muundo huu, mara nyingi ni kwa wafalme ama mabwana; na (3) njia ya tatu ni kumaanisha Uungu (yaani, hapa),האדין . Tazama Mada Maalum katika 12:1.

◙ **“kama nimeona fadhili machoni pako”** Hii ni nanna ya kawaida ya kusalimiana (kama vile 30:27).

◙ Mistari ya 3-5 ni mtiriko wa upole lakini ni maombi yenye umuhimu.

1. Kusihi waingie ndani kwa ajili ya kupumzika kidogo (BDB 716, KB 778, *Qal* ya KAULI ISIO TIMILIFU inatumika katika maana ya MASHARTI), mst. 3.
2. Kusihi maji yaletwe (BDB 542, KB 534, *Hophal* ya KAULI ISIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya MASHARTI) kunawa (BDB 934, KB 1220, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI) miguu yao, mst. 4
3. Kusihi kwa ajili ya mapumziko chini ya mti, sehemu iliyokuwa imeheshimishwa ("safi," BDB 1043, KB 1612, *Niphal* ya KAULI SHURUTISHI), mst. 4
4. Kusihi wamruhusu Ibrahimu kuandaa na kuleta chakula (BDB 542, KB 534, *Qal* KITENZI CHA KUSIHI), mst. 5
5. Kusihi iwepo faraja endelevu (BDB 703, KB 761, *Qal* HALI SHURUTISHI), mst. 5

**18:4"mkapumzike chini ya mti huu"** Katika siku hizi hili neno "kupumzika" lina maana ya kujiandaa kwa ajili ya kupata chakula. Mara nyingi ni wakati wa ushirika wa vyakula uliopangwa. Vyakula ilikuwa njia ya kukazia ushirika na makubaliano.

**18:5"nitaleta chakula kidogo"** Huu ulikuwa usemi wa kimasihara mtu alipolinganisha kipimo cha mkate aliutengeneza Sara katika mst. 6, ambao lazima utakuwa na kwati zipatazo 33.

◙ **"iwapo mmemjia mtumwa wenu"** Hiki ni kifungu cha nahau ya Kiebrania ambacho kinaonekana kumaanisha kwamba hata hatua hii, Ibrahimu anaonekana kuelewa kwamba ujio huu haukuwa wa kawaida haukuwa wa bahati mbaya, au pasipo makusudi. Kutokana na mst. 9 naamini kwamba kusudi la ujio huu lilikuwa ni kuiongeza imani ya Sara na pia kumwezesha Ibrahimu kuielewa nafasi yake ya maombi yake ya kusihi kama huduma, ambayo itakuwa muhimu kwa Wakuu wote wa familia hasa akina baba.

**18:6** Ibrahimu kwenda haraka (KITENZI kimetumika mara tatu katika mist. 6, 7) kumwagiza mkewe kuandaa chakula kwa ajili ya wageni. Jambo hili lingekuwa na muda fulani muhimu.

1. uandae kwa haraka, BDB 554, KB 553, *Piel* KAULI SHURUTISHI
2. ukande, BDB 534, KB 525, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. fanya mikate, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI

◙ **"vipimo vitatu"** Neno hili "*se'ah*" (BDB 684), ambavyo ni sawa na efa 1/3.

## MADA MAALUM: UZANI NA VIPIMO VYA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE (USOMAJI WA VIPIMO)

Uzani na vipimo vilivyotumika katika masuala ya biashara vilikuwa ni vya muhimu katika uchumi wa kilimo hapo kale. Biblia inawasihi Waisrael kuwa wasiwe na upendeleo kwenye mambo yao wanayoyafanya na wengine (kama vile Law. 19:35-36; Kumb. 25:13-16; Mith. 11:1; 16:11; 20:10). Tatizo kubwa lilikuwa sio tu uaminifu, bali kutokuwepo na istilahi zilizo sawa na muundo uliotumika huko Palestina. Inaonekana kuwa palikuwepo jozi mbili za uzani; moja "nyepesi" na nyingine "nzito" kwa kila idadi (angalia *The Interpreter's Dictionary of the Bible,* juzuu ya 4, uk. 831). Pia muundo wa desimali (ulioegamia kwenye sehemu ya 10) wa Misri umekuwa ukijumuishwa na sehemu ya 6 huko Mesopotamia.

Wingi wa "vipimo" na "idadi"vilivyotumika vilitokana na sehemu ya mwili wa mwanadamu, wanyama, mizigo, vibebeo vya wakulima, hakuna hata kimoja kilichokuwa sawia. Kwa hiyo, chati hapa chini ni makadilio tu na ya majaribio. Njia rahisi ya kuonyesha uzani na vipimo iko katika jedwali la kimahusiano

I. Maneno ya ujazo yanayotumika mara nyingi

A. Vipimo vya vitu vikavu
   1. Homeri (BDB 330, yumkini "mzigo wa punda," BDB 331), mf., Law. 27:16; Hosea 3:2
   2. Lateki (AU lethech, BDB 547, yumkini inadokeza katika Hosea 3:2)
   3. Efa (BDB 35), mf., Kut. 16:36; Law. 19:36; Ezek. 45:10-11,13,24
   4. Se'ah (BDB 684), mf., Mwa. 18:6; 1 Sam. 25:18; 1 Fal. 18:32; 2 Fal. 7:1,16,18
   5. Homeri (BDB 771 II, yumkini "mganda" [safu ya mbegu zilizoanguka], BDB 771 I), mf., Kut. 16:16,22,36; Law. 23:10-15
   6. Hini (BDB 798, "sehemu ya kumi" ya efa), mf., Kut. 29:40; Law. 14:21; Hes. 15:4; 28:5,13
   7. Kibaba ( BDB 866), kama vile 2 Fal. 6:25

B. Vipimo vya vimiminika
   1. Kori (BDB 499), mf., Ezek. 45:14 (inaweza kuwa kipimi cha vitu vikavu, kama vile II Nya. 2:10; 27:5)
   2. Bathi (BDB 144 II), mf., I Fal. 7:26,38; II Nya. 2:10; 4:5; Isa. 5:10; Ezek. 45:10-11,14
   3. Hini (BDB 228), mf., Kut. 29:40; Law. 19:36; Ezek. 45:24
   4. Logi (BDB 528), kama vile Law. 14:10,12,15,21,24

C. Chati (iliyochukuliwa toka kwa Roland deVaux, *Ancient Israel*, juzuu. 1, uk. 201 na *Encyclopedia Judaica*, juzuu. 16, uk. 379)

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Homeri (kikavu) =Kori kimiminika au kikavu | 1 | | | | | | |
| Efa (kavu) =bathi (kimiminika) | 10 | 1 | | | | | |
| Se’ah (kikavu) | 30 | 3 | 1 | | | | |
| Hini (kimiminika) | 60 | 6 | 2 | 1 | | | |
| Homeri (kikavu) | 100 | 10 | - | - | 1 | | |
| Kibaba (kikavu) | 180 | 18 | 6 | 3 | - | 1 | |
| Logi (kimiminika) | 720 | 72 | 24 | 12 | - | 4 | 1 |

II. Istilahi za uzani zinazotumika mara kwa mara

A. Uzani wa aina tatu unaotumika mara nyingi ni talanta, shekeli, na gera.
   1. Kipimo kikubwa katika Agano la Kale ni taranta. Toka Kutoka 38:25-26 tunajifunza kuwa taranta moja ni sawa na shekeli 3,000 (yaani., “uzani wa jumla,” BDB 503)
   2. Neno shekel (BDB 1053, “uzani”) hutumia mara nyingi kama inavyodhaniwa, lakini hakijaelezewa katika andiko. Kuna thamani mbali mbali za shekeli zilizotajwa katika Agano la Kale.
      a. "kipimo cha kibiashara" (toleo la NASB la Mwa. 23:16)
      b. "shekeli ya madhabahuni" (toleo la NASB la Kut. 30:13)
      c. "kwa uzani wa Mfalme" (toleo la NASB la II Sam. 14:26), pia uliitwa "uzani wa Kifalme" kwenye mafunjo ya Elephantine.
   3. Gera (BDB 176 II) ilithaminiwa na shekeli 20 (kama vile Kut. 30:13; Law. 27:25; Hes. 3:47; 18:16; Ezek. 45:12). Uwiano ulitofautiana toka Mesopotamia hadi Misri. Israeli ilifuatisha uthaminishaji uliokuwa ukitumika huko Kaanani (Ugariti)
   4. Mina (BDB 584) inathaminishwa na shekeli 50 au 60. Neno hili linapatikana hasa katika vile vitabu vya Agano la Kale (yaani Ezek. 45:12; Ezra 2:69; Neh. 7:71-72). Ezekieli ilitumia uwiano wa 1 ya 60, wakati Wakaanani walitumia uwiano wa 1 ya 50.
   5. Beka (BDB 132, "nusu ya shekeli," kama vile Mwa. 24:22) imetumika mara mbili katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 24:22; Kut. 38:26) na inathaminishwa na nusu shekeli. Jina lake linamaanisha "kugawanya."

B. Chati
   1. Imesimamia juu ya Vitabu vitano vya Torati

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Taranta | 1 | | | | |
| Mina | 60 | 1 | | | |
| Shekel | 3,000 | 50 | 1 | | |
| Beka | 6,000 | 100 | 2 | 1 | |
| Gera | 60,000 | 1,000 | 20 | 10 | 1 |

2. Ikisimamia juu ya Ezekieli

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Taranta | 1 | | | | |
| Mina | 60 | 1 | | | |
| Shekeli | 3,600 | 60 | 1 | | |
| Beka | 7,200 | 120 | 2 | 1 | |
| Gera | 72,000 | 1,200 | 20 | 10 | 1 |

**18:7-8 Mistari 6-8** inaeleza mlo wa gharama na uliotengenezwa kwa uangalifu. Ibrahimu aliwapa wageni hawa kizuri alichokuwa nacho! Hawa walikuwa wageni muhimu!

**18:8 " akasimama karibu nao chini ya mti, nao wakala**" Philo, Josephus, na Targum wa Yonathani wanalitafsri hili kama "walionekana wakila," lakini miongoni mwetu wanaoukubali ufunuo wa Agano Jipya wanaona kwamba hata Yesu alikula (kama vile Luka 24:41-43) baada ya kutukuzwa Kwake, tendo ambalo lilisababisha ulaji wa chakula kupitia Uungu si kwa kukosa uwezekano. Waandishi wa Kiyahudi wanao huzuni sana kuhusiana na semi hizi za lugha za kibinadamu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 18: 9-15**

**[9] Wakamwambia, Yu wapi Sara mkeo? Akasema, Yumo hemani. [10] Akamwambia, Hakika nitakurudia wakati huu huu mwakani, na tazama, Sara mkeo atapata mwana wa kiume. Sara akasikia mlangoni pa hema iliyokuwapo nyuma yake. [11] Basi Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, na umri wao mkubwa, na Sara alikuwa amekoma katika desturi ya wanawake. [12] Kwa hiyo Sara akacheka moyoni mwake, akisema, Niwapo mkongwe, nitapata furaha, na bwana wangu mzee? [13]Bwana akamwambia Ibrahimu, Mbona Sara amecheka akisema, Mimi kweli nitazaa mwana, nami ni mzee? [14]Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume. [15]Akakana Sara, akisema, Sikucheka, maana aliogopa. Naye akasema, Sivyo, umecheka.**

**18:9 "Yu wapi Sara mkeo"** Hawa walilifahamu jina lake! Kumuuliza mwanamume juu ya jina la mkewe lingekuwa tendo lisilo la kawaida katika utamaduni wa siku zile. Hili lilionyesha ukaribu ambao ulimgusa Ibrahimu moja kwa moja.

**18:10 "nitakurudia wakati huu"** Hiki ni KITENZIJINA HALISI na KAULI ISIO TIMILIFU ya neno hili hili la Kiebrania (BDB 996, KB 1427), ambalo linachochea nguvu ya KITENZI, "hakika nitarudi."

◙ **"wakati huu huu mwakani, na tazama, Sara mkeo atapata mwana wa kiume"** Hakika hili ni neno ambalo Mungu alikuwa amempa Ibrahimu katika 17:15-21, lakini katika muktadha huu pia hili ni neno la Sara.
Kifungu cha NASB "kwa wakati huu mwaka ujao," si andiko sahihi la Masoreti, ambalo lina kifungu "katika wakati wa kuhuishwa" (BDB 311 I, 3, yaani, chipuka). Hili linarudiwa katika mst. 14, lakini likiwa na kifungu kilichoongezwa, "katika kuchaguliwa" (BDB 417). Kifungu hiki kinaongezwa ili kueleza kwamba kipindi kitakuwa muda wa miezi tisa, si mwaka mzima (kama vile II Fal. 4:16-17).

**18:11** Haya ni maoni kutoka kwa msimuliaji (yaani, mwandishi) wa baadaye aliyevuviwa. Uvuvio ni suala la imani. Waamini wanashawishiwa kwamba mwandishi wa kweli wa Maandiko ya ki-Kanuni alikuwa Roho Mtakatifu. Hatua halisi na mpangilio wa matoleo ya mwisho ya Maandiko haujulikani.

**18:12"Sara akacheka moyoni mwake, akisema**" Ibrahimu alicheka katika 17:17. Sara alicheka kwa sababu hakuamini kwamba yeye na Ibrahimu, wote walikuwa wazee, ingewezekanaje kuwa na mtoto. Hapa maneno yake yanatumiwa na mwandishi wa I Pet. 3:6 kuonyesha unyenyekevu kwa Ibrahimu. Kwa uwazi kabisa alikuwa ameshavuka kipindi cha hedhi na maisha yao ya tendo la ndoa yalikuwa yamestishwa kitambo. Kma tunavyojifunza, kwa uweza wa Mungu, si kwamba Sara pekee alikuwa na uwezo wa kuchukua mimba, lakini alikuwa na uwezo wa kuzalisha watoto wengine

**18:13 "Bwana akamwambia Ibrahimu Mbona Sara amecheka**'" Mmoja wa wageni anatambuliwa kama YHWH Mwenyewe. Bwana alizungumza na Ibrahimu kwa sababu siku hiyo isingekuwa vema kuzungumza na Sara moja kwa moja. Ukweli wa Mungu kushughulika na imani ya Sara unaweza kuonekana katika Waebrania 11:11. Tunauona ubinadamu wa Sara katika ukanaji wa kucheka kwake (kama vile mst. 15). Baadaye, Mungu alimpa jina mwana aliyehaidiwa kwa mfumo wa neno "kicheko," kama tunavyoona katika 21:3, 6, 7. Tambua kwamba ilipita miaka ishirini na mitano tangu Mungu alipomwahidi Ibrahimu juu ya kupata mtoto katika sura ya 12.

◙ **"akisema**" YHWH kuzijua kila fikra za Sara ni jambo linaloonyesha maarifa Yake na kuwa mwaminifu katika ahadi Yake.

**18:14 "Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana"** maarifa ya YHWH yanaunganishwa na kudura zake (kama vile Yer. 32:17,27; Mt. 19:26). YHWH anazidi kuijenga na kuimarisha imani/tumaini la Ibrahimu na Sara katika Yeye! YHWH ni mkweli wa neno Lake! Yeye ni Mungu azungumzaye na kutenda! Hapa neno hili linatafsiriwa kama "gumu" (BDB 810, KB 928) lilomaanisha "la pekee," "tendo la Mungu la kustaajabisha." Tambua matumizi yake katika Kut. 15:11; Zab. 77:14; 78:12; 88:10; 119:129; 139:6; na Isa. 9:6; 25:1; 29:14;Dan. 12:6.

Inasisimua kuona namna wanawake wa awali waliokuwa wake za wakuu, hawa wote hawakuwa na uwezo wa kuwa na watoto pasipo msaada wa Bwana. Hii ilikuwa njia ya kuonyesha uweza Wake, kusudi, na mpango wa milele. Hizi ni kweli zinazoelekea kuzungumzia juu ya kuzaliwa kwa Masihi wa uzao wa Daudi. YHWH anao mpango wa ukombozi wa milele, mtu, na uzao wa karibu ambao anauimarisha na kuulinda!

◙ **"kwa muhula wake**" Angalia katika mst. 10.

**18:15** Ibrahimu na Sara hawakuwa watu waliokamilika. Hakuna aliye mkamilifu! Wote wanaonyesha ishara za Anguko (yaani Mwanzo 3). Wote ni michanganyiko ya imani na walakini!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 18: 16-21**

**16 Kisha watu hao wakaondoka huko wakaelekeza nyuso zao Sodoma. Ibrahimu akaenda pamoja nao awasindikize. 17 Bwana akanena, Je! Nimfiche Ibrahimu jambo nilifanyalo, 18akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari, na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa? 19Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, wafanye haki na hukumu, ili kwamba Bwana naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake. 20Bwana akasema, Kwa kuwa kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana, 21basi, nitashuka sasa nione kama wanayotenda ni kiasi cha kilio kilichonijia; na kama sivyo, nitajua.**

**18:16 "Kisha watu hao wakaondoka huko wakaelekeza nyuso zao Sodoma"** Jerome anatwambia kwamba kulikuwa na eneo ambalo haliko mbali kutoka Hebroni au angeweza kuiona Bahari ya Chumvi, huenda ni pamoja na miji iliyo uwanda wa pwani. Wasomi wengi wa mambo ya kale wanadhani kwamba miji hii tambarare ilikuwa kusini mwa ukingo wa Bahari ya Chumvi.

**18:17-19** Kifungu hiki kinaonekana kuwa cha mazungumzo ya aina moja kwa upande wa YHWH au huenda alizungumza kwa upole ili Ibrahimu aweze kusikia na kuutambua uhusiano wake wa kipekee kwa Bwana. Huu ndiyo mwanzo wa Ibrahimu kuitwa,"rafiki wa Mungu" (kama vile II Nya. 20:7; Isa. 41:8; Yakobo 2:23). Aina hii hii ya huu ukweli inafunuliwa na Yesu kwa Wanafunzi wake katika Yohana 15:15.

YHWH anayafunua matendo Yake ya papo kwa papo yaliyolenga wakati ujao (yaani, hukumu ya miji ya uwanda wa pwani, kama vile sura ya 19) ili kumtia moyo Ibrahimu kuhusu ahadi yake ya mwana kupitia Sara. Mtririko wa uzao wa Ibrahimu ungeliweza kuwa chombo cha YHWH cha kuyaleta mataifa Kwake na kuurejesha ushirika wa karibu wa Edeni.

Ibrahimu anaonyeshwa kama nabii (kama vile 20:7). YHWH anajifunua katika upekee na katika njia ya utabiri kwa manabii (yaani, Amosi 3:7), ambao unaonyesha kuwa Yeye yu ndani ya mpangilio wa wakati na matukio na pia ni mtu azungumzaye ukweli.

Mstari 18 ni rejeo lililo dhahiri la mwanzo asilia wa ahadi ile katika 12:1-3.

**18:18 "akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari"** Hiki KITENZI ni KITENZIJINA HALISI na ni KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU katoka mzizi ule ule (BDB 224, KB 243) ambao unadokeza uweza au, ahadi yenye uhakika.

◙ **"na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa"** Kuna mjadala fulani uanaozungumzia kuwa kwa vyo vyote kifungu hiki kitafsiriwe katika muundo wa KAULI TENDEWA ama YENYE KUJIREJEA (yaani, *Niphal* Shina la neno). Kifungu hiki kinaonekana kutokea katika miundo miwili ndani ya kipengele hiki cha kitabu cha Mwanzo. Hata hivyo, kifungu hiki kinatuhakikishia juu ya asili ya upendo wa Mungu kwa ulimwengu. Kama tutajibariki wenyewe kwa kumwita Mungu wa Ibrahimu, au kama Mungu wa Ibrahimu atatubariki moja kwa moja kupitia Ibrahimu (yaani, mtiririko wa Masihi na dhana ya uthibitisho itokanayo na neema kupitia imani, kama vile 15:6) si sababu ya uhakika (kama vile 12:3; 22:18; 28:14; Matendo ya Mitume 3:25; Gal. 3:8).

Tambua maana ya kiulimwengu ya sitiari hii na mst. wa 25. Ibrahimu alielewa ya kwamba YHWH hakuwa mwenyeji wa mahali pale, Mungu wa familia, bali Mungu wa dunia yote. Mtu hustaajabu pale dhana hii ya kitheolojia ianziapo kwa Ibrahimu. Mwanzoni (yaani sura ya 13) maana kamili ya toleo hili lisingekuwa imetambuliwa, lakini kwa kiasi fulani ndivyo zilivyokuwa (yaani Mungu mmoja wa kwanza).

**18:19 "Kwa maana nimemjua**" Hili ni neno la Kiebrania "kujua" (BDB 393, KB 390, *Qal* YA KAULI TIMILIFU), ambalo linatumika katika Mwa. 4:1; 19:5,8; Hes. 31:18 kuonyesha "uhusiano binafsi wa karibu." Pia neno hili linaweza kueleweka katika maana ya dhanio la awali, lakini huenda afadhali hapa, "kujali" (kama vile Kut. 2:25; Kumb. 2:7; 33:9; Hosea 13:5).

## MADA MAALUM: KUJUA (kama ilivyoelezewa kutoka Kumbukumbu la Torati)

Neno la Kiebrania "kujua"(yada, BDB 393, KB 390) lina maana kadhaa (mazingira ya kimaana) katika shina la neno *Qal*.

1. Kuelewa mema na mabaya - Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yona 4:11
2. Kujua kwa kuelewa - Kumb. 9:2,3,6; 18:21
3. Kujua kupitia mazoea - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Yos. 23:14
4. Kufikiri - Kumb. 4:39; 11:2; 29:16
5. kujua kibinafsi
    a. Mtu - Mwa. 29:5; Kut. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9, Yer. 1:5
    b. mungu -Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
    c. YHWH - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
    d. Kujamiiana - Mwa. 4:1,17,25; 24:16; 38:26
6. ujuzi wa kujifunza - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. Kuwa mwenye hekima - Kumb. 29:4; Mit. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. maarifa ya Mungu

a. kwa Musa - Kumb. 34:10
b. kwa Israeli- Kumb. 31:21

kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya kibiblia ni ushirika wa ndani, wa kila siku, unaokua pamoja na Mungu (angalia Mada Maalum: *Koinōnia*). Sio sheria pekee au maisha ya kiadilifu pekee. Ni imani binafsi ya kiushirika. Hii ndio sababu Paulo alitumia nyumba ya mshirika katika Efe.5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa.

◙ **"ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana"** Tambua maana hii yenye kueleza kwamba Ibrahimu atakuwa na mtoto na mtoto huyo ataifuatisha imani yake kwa uzao wake (kama vile Kumb. 4:9; 6:7). Pia tambua masharti ya utii, ambayo hakika ni sehemu ya majukumu ya agano (kama vile 17:1), si kwa upande wa Ibrahimu pekee, bali ni kwa vizazi vyote vya imani vinavyotakiwa kulifuatisha hili. Bwana huwataka watu waifuatishe tabia Yake kwa mataifa. Hili neno "njia ya Bwana" linasisimua kwa sababu linazungumzia maisha ya imani (kama vile Waamuzi 2:22; Zab. 119:1). Hili ndilo jina la kwanza lililotumiwa na kanisa la mwanzo (kama vile Matendo ya Mitume 9:2; 18:25-26; 19:9, 23; 22:4;24:14,22; Yohana 14:6).

◙ **"wafanye haki na hukumu"** Haya maneno mawili (BDB 842 na 1048) mara nyingi yanatumika kwa pamoja. Haya yanaeleza juu ya maisha ya pendo kwa Mungu, jirani, na jumuiya, ambayo kwa uwazi kabisa yametajwa katika Amri Kumi za Kutoka 20 na Kumbukumbu la Torati 5. Tambua agizo la maisha lililo maanishwa katika mtiririko wa sifa ya Mungu iliyofunuliwa (kama vile 17:1).

**18:20 "Bwana akasema, Kwa kuwa kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana"** Hili neno"kilio" (BDB 277) ni neno la kimasihara linalofanana sana na neno la Kiebrania ambalo linamaanisha "fedheha" (BDB 277). Maelezo haya haya ya hukumu ya Sodoma na Gomora yamenukuliwa katika Mwanzo 19 na Yuda mstari 7. Tambua jinsi dhambi ya Sodoma ilivyo.

1. kubwa – BDB 912 I, KB 1174, *Qal* YA KAULI TIMILIFU
2. iliyozidi sana (BDB 547) mbaya sana – BDB 457, KB 455, *Qal* YA KAULI TIMILIFU

Dhambi zao "alipaza sauti" kwa YHWH kwa ajili ya hukumu! inawezekana kwamba Lutu na familia yake ndio waliokuwa wakiomba (kama vile mst. 23) au malaika walinzi, au hata sitiari ya dhambi zenyewe. YHWH anautambua ukubwa wa dhambi ya mwanadamu (kama vile 6:5-6,11-12,13b; 15:16; Zab. 14:1-3).18:21 "Nitashuka" Hiki kifungu cha lugha ya kibinadamu kinauzungumzia uwepo binafsi wa YHWH juu ya

1. hukumu, hapa na Mwa. 11:5,7
2. msaada, Kut. 3:8

Hili halipaswi kutumika katika kuyakanganya maarifa ya YHWH ya matukio ya sasa (yaani, "Imani iliyo wazi ya kuwepo kwa Mungu mmoja"). Hii ni lugha ya kistiari ya mashariki. Pia fahamu kwamba hii ni njia ambayo YHWH aliitumia kuwa na hao malaika wawili ("watu"). Yeye alilijua lililokuwa la kweli kwa sababu ya (1) Yeye alivyo (2) na kile ambacho malaika walikabiliana nacho. Kuna kutokujulikana kati ya UMOJA na WINGI wa "watu" hawa watatu (kama vile 18:1-2).

Hiki ni kifungu chenye umuhimu ambacho kinaonyesha kwamba huyu ni Mungu mwenye haki, japokuwa ni mjuzi wa yote, huchunguza kwa upekee kabla ya kutenda hukumu. Kifungu hiki kilitumiwa na waalimu wa sheria za Kiyunani kusema kwamba hii ilipaswa kuwa sifa ya mahakimu walio katika Israeli (kama vile Mwa. 11:5; Kut. 3:8).

◙ **"kama sivyo, nitajua"** Hiki ni kifungu kingine cha lugha ya kibinadamu chenye kuifafanua haki ya Mungu (kama vile Kut. 2:25). Kuna MASHARTI kadhaa yanayohusiana na YHWH katika mstari huu.
Nitashuka – BDB 432, KB 434,

1. *Qal* YENYE MASHARTI
2. Nione – BDB 906, KB 1157, *Qal* ISIO TIMILIFU inatumika katika maana YENYE MASHARTI
3. Nitajua – BDB 393, KB 390, *Qal* YENYE MASHARTI

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 18:22-33**

**[22]Basi wale watu wakatoka huko wakaelekea Sodoma; lakini Ibrahimu alikuwa akali akisimama mbele za Bwana. [23] Ibrahimu akakaribia, akasema, Je! Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu? [24]Huenda wakawapo wenye haki hamsini katika mji, utaharibu, wala hutauacha mji kwa ajili ya hao hamsini wenye haki waliomo?**
**[25]Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; Mhukumu ulimwengu wote asitende haki? [26] Bwana akasema, Nikiona katika Sodoma wenye haki hamsini mjini, nitapaacha mahali pote kwa ajili yao. [27]Ibrahimu akajibu, akasema, Basi, nimeshika kusema na Bwana, nami ni mavumbi na majivu tu. [28] Huenda wakapunguka watano katika wale hamsini wenye haki, je! Utaharibu mji wote kwa kupungua watano? Akasema, Sitauharibu, nikiona humo arobaini na watano. [29] Akazidi tena kusema naye, akinena, Huenda wakaonekana humo arobaini? Akasema, Sitafanya kwa ajili ya hao arobaini. [30] Akasema, Bwana asiwe na hasira, nami nitasema, Huenda wakaonekana huko thelathini? Akasema, Sitafanya, nikiona humo thelathini. [31]Akasema, Tazama, nimeshika kusema na Bwana, huenda wakaonekana huko ishirini? Akasema, Sitaharibu kwa ajili ya hao ishirini. [32] Akasema, Bwana asiwe na hasira, nami nitasema mara hii tu, Huenda wakaonekana huko kumi? Akasema, Sitaharibu kwa ajili ya hao kumi. [33]Basi Bwana alipokwisha kuzungumza na Ibrahimu, akaenda zake; Ibrahimu naye akarudi mahali pake.**

**18:22"watu"** Kulikuwa na wageni watatu waliojitokeza kuwa wawakilishi wa kimwili wa ulimwengu wa roho: (1) malaika wawili waliotajwa hapa (kama vile 19:1) na (2) YHWH aliyeendelea kukaa na Ibrahimu.

◙**" lakini Ibrahimu alikuwa akali akisimama mbele za Bwana"** Hii ni moja ya maeneo machache ambayo wasomi wa lugha ya Kimasoreti walibadailisha andiko la Kiebrania kwa sababu walifikiri kwamba andiko hili halikuwa sahihi katika hali yake ya sasa. Kiuhalisia hili lilikuwa neno "ya kwamba YHWH alisimama mbele ya Ibrahimu." Agano la kale la Kiebrania linaakisi maandiko ya Kimasoreti.

**18:23"Ibrahimu akakaribia, akasema"** Mara nyingi hili lilitumika katika maombi na dhabihu. IleTargum Jonathan anakitafsri kifungu hiki kama "na Ibrahimu akaomba," kifungu ambacho kinaweza kuwa sahihi. Hiki kifungu (na muktadha) kinaonyesha ushirika wa ajabu kati ya Ibrahimu na YHWH.

◙**"Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu"** Kifungu hiki kinaonyesha ufahamu wa Ibrahimu kuhusu asili na sifa ya YHWH (yaani, "Mhukumu ulimwengu wote asitende haki? " mst. 25). Kwa hakika YHWH alikuwa na ufahamu wa hali iliyokuwepo, lakini alitaka Ibrahimu kuulewa uhusuano wa kipekee uliokuwepo kati yake na Yeye, na umuhimu wa maombi ya kusihi kwa niaba ya wengine, ambayo kwa hakika aliyatumia kwa Abimaleki kama itakavyoonekana katika 20:7, 17. Nafikiri kwa namna hii Ibrahimu lazima alikuwa amefikiri mema kumhusu Lutu na familia yake kule Sodoma, lakini pia kuhusu mst. 18!

**18:26** Mstari huu ni mfano wa asili ya ushirika wa utamaduni wa Kiebrania.

1. Kwa namna ya ukanushaji
    a. Adamu na Hawa walitenda dhambi na vyote vilivyoumbwa vilikumbwa na matokeo ya dhambi hiyo.
    b. Akani alifanya dhambi (kama vile Yoshua 7) na jeshi la Israeli wakashindwa katika mapigano (wengine wakafa).
2. Kwa uhalisia
    a. Watu wenye haki walikuwa na mvuto juu ya matendo ya Mungu hadi mji mzima wa Sodoma (na miji mingine iliyokuwa uwandani).

b. Mtu mmoja mwenye haki angeweza kuighairisha hukumu ya Mungu juu ya Yerusalemu (kama vile Yer. 5:1).
c. Dhambi ya Adamu iliiuathiri uuumbaji wote. Maisha na kifo cha Yesu kilileta matokeo kwa uumbaji wote (kama vile Rum. 5:12-21).

Dhana hii iliyo msingi wa kithiolojia ndiyo msingi wa ufafanuzi, agano mbadala la Isaya 53. Kifo cha Mtu asiye na hatia chaweza kuleta msamaha (kama vile Mambo ya Walawi 1-7; Yohana 1:29; II Kor. 5:21).

**18:27 "Bwana"** Hili ni neno lenye kumaanisha *Adonai*, neno hili limewekwa wazi katika njia hii ili kuuzungumzia Uungu. Tazama Mada Maalum katika 12:1.

◙ **"nami ni mavumbi na majivu tu"** Kwa uwazi hili ni dokezo la Mwanzo 3 ambapo wanadamu hutoka mavumbini na hurudi mavumbini. Ibrahimu alizifahamu desturi zinazohuusu uumbaji! Hata hivyo, kifungu hiki kilikuwa nahau ya ki-semitiki ya siku hizo (yaani Ayubu, Matumizi ya sasa ya Ibrahimu ya kifungu hiki katika Ayubu 30:19;42:6).

**18:32 "Huenda wakaonekana huko kumi?"** Sababu halisi ya Ibrahimu kuishia katika idadi ya watu 10 haujulikani. Hii inaweza kurejelea juu ya (1) Lutu na familia yake ama (2) katika ukweli kwamba Ibrahimu hakutaka kuweka mpaka wa hukumu iliyojikita katika kumweka kando Lutu na familia yake.

# MWANZO 19

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Mwisho wa Sodoma | kumomonyoka kwa maadili ya Sodoma Na Gomora | kuharibiwa kwa Sodoma na Gomora | Hali ya dhambi ya Sodoma | kuharibiwa kwa Sodoma |
| 19:1-11 | 19:1-3 | 19:1-11 | 19:1-2a | 19:1-3 |
| | | | 19:2b | |
| | | | 19:3 | |
| | | | 19:4-5 | 19:4-5 |
| | | | 19:6-8 | 19:6-11 |
| | | | 19:9-11 | |
| | Sodoma na Gomora Inaharibiwa | | Lutu anaondoka Sodoma | |
| 19:12-14 | 19:12-14 | 19:12-14 | 19:12-13 | 19:12-14 |
| | | | 19:14 | |
| 19:15-22 | 19:15-22 | 19:15-23 | 19:15-17 | 19:15-16 |
| | | | | 19:17-22 |
| | | | 19:18-20 | |
| | | | 19:21-22a | |
| | | | 19:22b | |
| | | | Kuharibiwa kwa Sodoma Na Gomora | |
| 19:23-26 | 19:23-26 | | 19:23-26 | 19:23-26 |
| | | 19:24-26 | | |
| 19:27-28 | 19:27-28 | 19:27-28 | 19:27-29 | 19:27-28 |
| 19:29 | 19:29 | 19:29 | | 19:29 |
| Lutu Anajidhalilisha | Uzao wa Lutu | | Asili ya Wamoabu na Waamoni | Asili ya Wamoabu na Waamoni |
| 19:30-38 | 19:30-35 | 19:30-38 | 19:30-33 | 19:30 |
| | | | | 19:31-38 |
| | | | 19:34-38 | |
| | 19:36-38 | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:1-11**

**[1] Basi, wale malaika wawili wakaja Sodoma jioni; na Lutu alikuwa amekaa mlangoni pa Sodoma. Lutu**
**akawaona akaondoka akaenda kuwalaki, akainama kifudifudi. [2] Akasema, Bwana zangu, karibuni nawasihi**
**mwingie nyumbani mwa mtumwa wenu, mkalale, mkanawe miguu yenu, hata asubuhi mwondoke na**
**mapema mkaende zenu. Wakasema, Sivyo, lakini tutakaa uwanjani usiku kucha. [3] Akawasihi sana, nao**
**wakaja, wakaingia nyumbani mwake. Akawafanyia karamu, akawapikia mikate isiyochachwa nao wakala. [4]**
**Hata kabla hawajalala, watu wa mji, wenyeji wa Sodoma, wakaizunguka nyumba, vijana kwa wazee, watu**
**wote waliotoka pande zote. [5] Wakamwita Lutu, wakamwambia, Wa wapi wale watu waliokuja kwako usiku**
**huu? Uwatoe kwetu, tupate kuwajua. [6] Lutu akawatokea mlangoni, akafunga mlango nyuma yake. [7]**
**Akasema, Basi, nawasihi, ndugu zangu, msitende vibaya hivi. [8] Tazama, ninao binti wawili ambao hawajajua**
**mtu mume, nawasihi nitawatolea kwenu mkawafanyie vilivyo vyema machoni penu, ila watu hawa**
**msiwatende neno, kwa kuwa wamekuja chini ya dari yangu. [9] Wakasema Ondoka hapa! Kisha wakanena,**
**Mtu huyu mmoja amekuja kwetu kuketi hali ya ugeni; naye kumbe, anataka kuhukumu! Basi tutakutenda**
**wewe vibaya kuliko hawa. Wakamsonga sana huyo mtu, huyo Lutu, wakakaribia wauvunje mlango. [10] Lakini**
**wale watu wakanyosha mikono yao, wakamwingiza Lutu kwao nyumbani, wakaufunga mlango. [11] Kisha**
**wakawapiga hao watu walioko mlangoni kwa upofu, wadogo kwa wakubwa, hata wakachoka kwa kuutafuta**
**mlango.**

**19:1 "malaika wawili wakaja Sodoma jioni"** Walikuwa wamemwacha Ibrahimu na YHWH juu ya mlima wakitazama kutoka juu Bahari ya Chumvi wakati wa jioni na kuwasili umbali wa maili 40 kwa dakika chache – ni malaika!!! Wako katika maumbo ya kibinadamu, mazungumzo yao, walivyovaa kama ilivyo dhahiri kutoka 18:2,22; 19:10,12,16. Sikuzote huwa wanatokea kama wanaume isipokuwa yawezekana katika Zak. 5:9.

◙**"na Lutu alikuwa amekaa mlangoni pa Sodoma"** Tunaweza kuona kitu fulani cha mwendelezo wa uovu wa Lutu kwa namna kwamba

1. Katika 13:11 anasemekana kuhamia katika uwanda wa Sodoma na Gomora
2. Mchungaji wa mifugo ya kuhamahama amehamia katika mji. Inavyoonekana ni kwamba amefanyika mmoja wa wazee wa mji ambapo inadokezwa katika kifungu "katika lango la"
3. katika mstari wa 3 ni wazi anaelewa juu ya shughuli za kisenge za wakazi ambazo inawezekana aliona mara kadhaa
4. katika mstari wa 7 anaenda mbali kuwaita "ndugu zangu"
5. Baadaye anaonekana kama hayuko tayari kuondoka katika mji na mali zake anazozimiliki.

Mungu atusaidie—Lutu anaonekana kujaribu kuwabadilisha (mstari wa 9) lakini kama mara kwa mara ilivyotokea, ushawishi wao wa uovu ulimuathiri yeye, mke wake na binti zake!

Kama Ibrahimu alikuwa amefanya, Lutu pia iliinuka kuwasalimia na kushuka chini. Kama ishara hizi ni ishara za kitamaduni (ambalo linawezekana) au kutambua asili yao haina uhakika.

**19:2 "karibuni nawasihi mwingie nyumbani mwa mtumwa wenu, mkalale, mkanawe miguu yenu"** Lutu anaonekana kuwa ni mtu pekee wakuwahutubia na kuzungumza na wageni hawa bila kutambua kuwa walikuwa malaika alitaka kuwalinda kutoka katika wakazi wa mji huu. Hii inaweza kuonekana katika kuwabembeleza kwake kwa nguvu katika mstari wa 3. Mwitikio wa malaika wawili ni nahau ya kisemitiki kwa njia ya kidesturi kusema "ndio," lakini bila kusihi fulani.

KAULI SHURUTISHI tatu hizi (zinazoelezea shauku ya Lutu) zinafunua ishara za ukarimu wa kimashariki.

1. geuza chini – BDB 693, KB 747, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. kukaa usiku kucha (kifasihi nyumba ya wageni) – BDB 533, KB 529, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. kuosha – BDB 934, KB 1220, *Qal* KAULI SHURUTISHI

Kuongezea katika hili aliwaandalia karamu/sherehe kwa ajili yao (kama vile mstari wa 3). Ni wazi malaika hawa na uwakilishi wao wa mwili wa YHWH (yawezekana Malaika wa Bwana) waliweza na walikula chakula, kama alivyofanya Yesu aliyefufuka (kama vile Yohana 21).

◙ **"tutakaa uwanjani usiku kucha"** Hii lazima ilikuwa taratibu za kawaida kwa ajili ya wageni. Lakini Lutu alijua madhara yake. Yawezekana aliwahi kuona ikitokea kabla!

**19:3 "Akawasihi sana"** KITENZI hiki (BDB 823, KB 954, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatumika mara mbili katika mstari huu.

1. Katika mstari wa 9 maana yake ya wazi ya kuwaondoa au kuwashinikiza inatumika kwa wanaume wa Sodoma.
2. Hapa ni matumizi ya ki-istiari ya "kusihi" yanatumika (kama vile Waamuzi. 19:7; II Wafalme. 2:17; 5:23). KIELEZI "kwa nguvu" (BDB 547) inazidisha ombi.

◙**"akawapikia mikate isiyochachwa"** Walimu wanasema kwamba hii ilikuwa Pasaka, hivyo Isaka alizaliwa siku ya Pasaka (mwaka unaofuata). Hatahivyo, hii inaonekana kusomeka sana katika tungo, "mikate isiyochachwa." Mapema katika siku za Ibrahimu alikuwa anapika mikate ambayo haikuwa imechacha. Inavyoonekana watumishi wa Lutu au familia waliandaa chakula haraka (kama vile Waamuzi 6:19).

**19:4 "watu wa mji, wenyeji wa Sodoma, wakaizunguka nyumba, vijana kwa wazee, watu wote waliotoka pande zote."** Hii inamaanisha kwamba kila mtu mmoja katika mji, wazee kwa kwa vijana walikuwa wamefanyika wasenge au kwa namna fulani wenye jinsia mbili. Kama Mungu alivyomwambia Ibrahimu kuwapa mafunzo watoto wake, 18:19, Tunaona sehemu hasi ya hiki kadiri watu wa Sodoma wanavyowafundisha watoto wao katika uovu. Huu ni mfano mzuri wa dhambi za wababa zikirithishwa kwa watoto wao wa kiume (kama vile Kumb. 5:9-10).

Tungo ya mwisho inafasiriwa "kutoka katika eneo" (kama vile toleo la NASB na NKJV) linavyobainisha kifasihi "mpaka mtu wa mwisho" (BDB 892). Neno linatumiwa kwa vitu kati (mfano 47:21). Maovu ya Sodoma kwamba malaika (yaani YHWH) alikuwa ametaja katika 18:20-21 ilikuwa kweli. Kulikuwa hata hakuna watu kumi wenye haki (kama vile 18:32).

## MADA MAALUM: KUJAMIIANA KWA JINSIA MOJA

Kuna shinikizo kubwa la desturi za kisasa kukubaliana na kujamiiana kwa jinsia moja kama mtindo wa maisha sahihi na mbadala.
Biblia inalaani kitendo hiki kama mtindo wa maisha wenye uharibifu, nje ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya uumbaji wake.

1. inavunja amri ya Mwanzo 1 juu ya kuzaa na kuongezeka
2. Inaweka bayana tabia za ibada za kipagani na desturi (kama vile Mambo ya Walawi 18:22; 20:13; Rum. 1:26-27; na Yuda 7)
3. Inafunua uhuru wa kibinafsi kujitenga mbali na Mungu(kama vile 1 Kor. 6:9-10)

Hatahivyo kabla sijaachana na mada hii ngoja nielezee upendo wa Mungu na msamaha kwa wanadamu wote waasi. Wakristo hawana haki ya kuwa na chuki kuu wala kujivuna juu ya dhambi hii, haswa wakati I wazi kwamba sisi sote tunatenda dhambi. Maombi, kujaliana, ushuhuda na huruma vinafanya kazi zaidi katika eneo

hili kuliko kushutumiana kwa ukali. Neno la Mungu na Roho wake watafanya kazi ya kulaani na kuhukumu ikiwa tutawaruhusu. Dhambi zote za zinaa, sio tu hii ni chukizo mbele za Mungu na zinatupeleka katika hukumu. Hali ya kutamani kujamiina ni zawadi na kipawa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ustawi wa mwanadamu, furaha na jamii imara. Lakini hamu hii yenye nguvu na iliyotolewa na Mungu mara kwa mara inageuzwa kuelekea katika ubinafsi na kujitaftia maslahi yake yenyewe, maisha ya "zaidi-kwa ajili yangu-kwa gharama yoyote" (kama vile Rum. 8:1-8; Gal. 6:7-8).

Mara kwa mara watu wanasema, "Mungu aliniumba hivi."Ni kweli kwamba bado hatujui chanzo cha usenge (yaani kijenetiki au kijamii) lakini vyovyote, Biblia lazima utuongoze juu ya chaguzi zetu; Chaguzi zina matokeo. Maandiko yana vipaumbele juu ya hisia au upendeleo binafsi. Sisi ni jamii ya kiimani tunaoongozwa kwa ufunuo wa kiungu na sio uhuru au haki za mtu mmoja mmoja.

Neno la kuhitimisha kama kiongozi wa kanisa sifahamu kwamba asilimia mashindano ya Wakristo juu ya suala hili. Tatizo sio ile hulka ila tendo. Baadhi ya wanafunzi wa kihuduma katika chuo changu wanahangaika na mambo mengine ya kingono (yana nguvu sana katika hatua hii ya maisha). Wale wanaochagua kuweka mipaka katika shauku zao (yaani kujizuia) katika eneo hili (yaani matamanio ya kingono) hakika ndio watu sahihi kwa ajili ya nafasi za huduma. Hili pia ni hivyo hivyo kweli kwa wale wanaohangaika na kujamiiana kwa jinsia moja. Suala la msingi hapa ni tendo na sio wazo. Kwanini baadhi wanavutwa kwa wengine wa jinsi moja bado ni fumbo. Kuna uchaguzi katika eneo hili (kama ilivyo katika maeneo mengine). Tunawajibika kwa chaguzi zetu!

Mungu anawapenda watu na kutamani afya zao za kudumu na ustawi kwa wale wote waliofanywa kwa sura na mfano wake (Mwanzo 1:26-27; angalia Mada Maalumu: Kujamiiana kwa Jinsia moja). Yale mambo/matendo ambayo yanamuharibu afya ya mtu na furaha na pia jamii lazima yakemewe na kulaaniwa. Mungu anataka kutuona tukiwa katika ubora wetu! Sisi tunataka kutimizwa kwa matakwa yetu haraka haraka! Mungu aturehemu sisi sote.

**19:5 "Wa wapi wale watu waliokuja kwako usiku huu? Uwatoe kwetu, tupate kuwajua"** Matakwa yao ni

1. watoeni nje – BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. kuwa na mahusiano na – BDB 393, KB 390, *Qal* HALI YA KUSIHI

Josephus katika kitabu chake *Antiquities of the Jews* 1:11:3, Inasema kwamba malaika walikuwa viumbe wazuri na waliwashawishi wana wa wanadamu wa Sodoma. Biblia mara kwa mara inazungumza juu ya dhambi ya kujamiiana kwa jinsia moja ambayo inavyoonekana ilikuwa kawaida katika Kanaani (kama vile Mambo ya Walawi 18:22; 20:13). Ilikuwa kawaida katika ufalme wa Rumi siku za Paulo (kama vile Rum. 1:26, 27; I Kor. 6:9; I Tim. 1:10).

Tungo ya Kiebrania, "kuwa na mahusiano nao," kifasihi ni "kuwajua" (BDB 393, KB 390), ambayo inazungumza juu ya "uhusano wa karibu wa kibinafsi." Ubakaji huu wa kibasha wa kikundi ungewezekana kuua wageni. Ni wazi mstari wa 9 kwamba hii ingewatokea pia mabinti wa Lutu na hata Lutu. Baadhi ya Wafasiri wanaona kwamba kitendo cha Lutu kutoa mabinti zake kwa makundi ya watu kama jambo lililosababisha wao kupunguza na kupoteza heshima kwa baba yao.

**19:7 "msitende vibaya"** KITENZI hiki (BDB 949, KB 1269, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, hapa kinatumika katika namna ya KITENZI AMRISHI) katika hii *Hiphil* shina linaweza kumaanisha

1. msiwaumize – mfano 43:6; Kut. 5:22-23; Josh. 24:20; Isa. 11:9
2. msifanye uovu – mfano I Sam. 12:25; Yer. 4:22; 13:23

Inaonekana Lutu anawatuhumu watu juu ya kusudio ovu (kama vile mstari wa 9). Anafanyika kama kioo cha kimaadili kwa vurugu za kingono zilizokusudiwa ambazo zinazunguka uovu wa aina mbili.

1. kuvuja ukarimu
2. upotovu wa kingono

**19:8 "Tazama, ninao binti wawili"** Lutu anajielezea mwenyewe kwa genge kwa mapendekezo matatu.

1. niruhusu niwalete kwenu (binti zake wawili) – BDB 422, KB 425, *Hiphil* HALI YA KUSIHI
2. Muwafanyie chochote mnachotaka – BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. msiwafanyie chochote watu hawa – BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI.

Wageni hawa walikuwa wamekuja kwa minajiri ya "kupata hifadhi chini ya dari langu" (kifasihi, "kivuli," BDB 853). Neno hili hili linatumika kwa "chini ya uvuli wa mbawa za Mungu," ambayo ni sitiari kwa ajili ya ulinzi na kujali (kama vile Hes. 14:9; Zab. 17:8; 36:7; 57:1; 63:7). Lutu alikuwa analazimika kuwapa ulinzi wageni wake kwa gharama yoyote!

Hii imeelezewa kwa namna nyingi lakini inaendelea kubaki fumbo juu ya nia za Lutu.

1. Ilikuwa ni shauku yake kuu kulinda wageni wake (ukarimu wa asili ya nchi za Mashariki)
2. Alifahamu kuwa genge hili halikuwa linahitaji wanawake
3. Alikuwa akitumaini wakwe zake, ambao walikuwa katika umati wa watu, wangeweza kuzuia genge katika hatua hii. Masimulizi haya ni sawa sawa na Waamuzi 19:24.

**19:9 "Ondoka hapa"** KITENZI (BDB 620, KB 670, *Qal* KAULI SHURUTISHI) siku zote inafasiriwa "kuja karibu" (mfano Mambo ya Walawi 21:21; II Wafalme 4:27); kipekee hapa inaashiria "toka katika njia yetu" kadiri walivyoendelea mbele.

◙**"naye kumbe, anataka kuhukumu"** Hii ni tungo yenye mkazo (yaani KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na KITENZIJINA HALISI cha mzizi uleule wa kiebrania). Matendo ya wanaume hawa yanastahili hukumu (kama vile mstari wa 13). Taarifa hizi zinaelezewa katika 18:20-24. Hii inaweza kuwa chanzo cha II Pet. 2:7-8, ambacho kinachomuita Lutu mwenye haki.

◙ **"Basi tutakutenda wewe vibaya kuliko hawa"** Walipendekeza kumuudhi (Hiki ni KITENZI kilekile kama mstari wa 7) Lutu na familia yake walikuwa kama wageni.

**19:11 "wakawapiga hao watu walioko mlangoni kwa upofu"** Hili ni neno la kiebrania (BDB 645, KB 697, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ikimaanisha zaidi ya upofu wa muda (KITENZI kinatokea mara mbili tu katika Agano la Kale, kama vile II Wafalme. 6:18). Iben Ezra anasema kwamba inamaanisha "upofu wa macho na akili," ambao unaonekana kushabihiana na mstari wa baadaye ambao unasema waliendelea kuzunguka zunguka wakitafuta njia ya mlango kama vile wamechanganyikiwa (mfano Kut. 3:20). Upofu hapa (BDB 703) unatofautiana na Mambo ya Walawi 22:22; Kumb. 28:28 (BDB 734). Hii inaashiria "kufanywa upofu kwa kwa kutumia mwanga mkali."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:12-14**

**[12] Basi wale watu wakamwambia Lutu, Je! Unaye mtu hapa zaidi? Mkwe, wanao, na binti zako, na wo wote ulio nao katika mji, uwatoe katika mahali hapa; [13] maana tutapaharibu sisi mahali hapa, kwa kuwa kilio chake kimezidi mbele za Bwana; naye Bwana ametupeleka tupaharibu. [14] Lutu akatoka akasema na wakweze, waliowaposa binti zake, akasema, Ondokeni mtoke katika mahali hapa kwa sababu Bwana atauharibu mji huu. Lakini akawa kama achezaye machoni pa wakweze.**

**19:12 "Je! Unaye mtu hapa zaidi"** Hii si taarifa zaidi ya malaika kama ilivyo kwa Lutu kuona hakuwa na mfungamano hasa na Sodoma!

**19:13-14 "Bwana ametupeleka tupaharibu…… Bwana atauharibu mji huu"** Uwepo wa malaika aharibuye unaweza kuonekana katika mapigo kumi ya Misri, lakini mamlaka ya kilele ni YHWH nyuma ya shughuli za malaika. Mara tatu katika mistari hii miwili ya neno la kiebrania "haribu" (BDB 1007, KB 1469) linatumika.

1. mst. 13 – "haribu" – *Hiphil* KAULI ENDELEVU
2. mst. 14 – "haribu" – *Piel* KITENZIJINA HALISI (kama vile mstari wa 29)
3. mst. 14 – "haribu" – *Hiphil* KAULI ENDELEVU (kama vile 18:28)

Neno kimsingi linamaanisha "kufanya uharibifu" lakini linatumika katika namna ya kuharibu (kama vile 6:17; 9:15; 13:10; II Sam. 24:16). Huu ni mzizi sawa na uliotumika kuelezea malaika wa "mauti" katika Kut. 12:23 (tazama I Nyakati. 21:15; Isa. 54:16; Yer. 22:7).

**19:14 "akatoka akasema na wakweze"** Baadhi wanafikiri kuwa yumkini mabinti za Lutu walikuwa tayari wamekwisha kuolewa (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU, kama vile Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani na Kiaramaiki), lakini wengine kwamba walikuwa wamechumbiwa tu (kama vile Josephus, the Vulgate, Rashi, na TEV). Inaonekana kwangu kutokana na muktadha kwa asilimia 100% Lutu alikuwa na mabinti wawili tu na walikuwa bado hawajaolewa, waliishi nyumbani tu lakini inaendelea kuwa na uwezekano kwamba alikuwa na mabinti wengine wawili ambao wenyewe walikuwa wamechukuliwa na maisha ya Sodoma na hawakuwa tayari kuacha.

Lutu alijaribu kuwahamasishwa vijana hawa kuondoka.

1. juu (kifasihi inuka) – BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. ondoka (kifasihi nenda) – BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI SHURUTISHI

◙ **"kama achezaye"** KITENZI hiki (BDB 850, KB 1019, *Piel* KAULI ENDELEVU) kina visawe kadhaa.

1. kitendo cha kujamiiana – Mwa. 26:8
2. kubeza – Mwa. 21:9
3. kuchezea (inafanana na #1) – Mwa. 39:14,1
4. kucheza (inahusiana na #1) – Kut. 32:6
5. kufurahisha – Waamuzi 16:25

Mzizi huu huu unatumika kwa kicheko cha Ibrahimu na Sara kwa ahadi ya YHWH ya mtoto kwa msimu wa kuchipua unaofuata (kama vile 17:17; 18:12).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:15-22**

**[15] Hata alfajiri ndipo malaika wakamhimiza Lutu, wakisema, Ondoka, mtwae mkeo na binti zako wawili waliopo hapa, usipotee katika maovu ya mji huu. [16] Akakawia-kawia; nao wale watu wakamshika mkono, na mkono wa mkewe, na mkono wa binti zake wawili, kwa jinsi Bwana alivyomhurumia, wakamtoa wakamweka nje ya mji. [17] Ikawa walipomtoa nje, mmoja alisema, Jiponye nafsi yako usitazame nyuma, wala usisimame katika hilo bonde po pote; ujiponye mlimani, usije ukapotea. [18] Lutu akawaambia, Sivyo, bwana wangu! [19] Tazama, mtumwa wako ameona kibali machoni pako, nawe umezidisha rehema zako ulizonifanyia kwa kuponya nafsi yangu, nami siwezi kukimbilia mlimani nisipatwe na yale mabaya, nikafa. [20] Basi mji huu u karibu, niukimbilie, nao ni mdogo, nijiponye sasa huko, sio mdogo huu? Na nafsi yangu**

**itaishi.[21] Akamwambia, Tazama, nimekukubali hata kwa neno hili, kwamba sitauangamiza mji huo uliounena. [22] Hima, ujiponye huko, maana siwezi kufanya neno lo lote, hata uingiapo humo. Kwa hiyo jina la mji ule likaitwa Soari.**

**19:15** Hata ilipofika alfajiri malaika waliweka mkazo.

1. juu (kifasihi inuka) – muundo sawia wa mstari wa 14
2. kuchukua– BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI

Katika mistari ya 16-22 hali ya kujali ya malaika na ulinzi unaenelea.

◙**"usipotee katika maovu ya mji huu"** Hili ni neno la kawaida kwa hukumu ya ki-Ungu (kama vile 18:23,24; 19:15,17; Hes. 16:26; I Sam. 12:25).

**19:16 "Akakawia-kawia"** KITENZI hiki (BDB 554, KB 552, *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inatumika mara kadhaa katika Agano la Kale na kumaanisha "kukawia" au "kuchelewa." Kwanini hakutajwi sababu za kusitasita kwa Lutu. Mtu anaweza kudhania, lakini inadhihirisha kukosa imani katika ujumbe wa malaika. Maonyo ya mstari wa 17 inamaanisha hali ya upande wa Lutu kutotaka kuacha maisha yake ya Sodoma au yawezekana milki zake za kimwili (yaani mali zake za nyumbani, watumwa, vitu vya thamani, mifugo). Kumbuka Lutu alichagua sehemu bora ya ardhi kwa ajili yake mwenyewe (kama vile 13:10).

◙ **"kwa jinsi Bwana alivyomhurumia"** NOMINO ya Kiebrania (BDB 328) inapatikana hapa tu katika Isa. 63:9, ambayo inaashiria pia agano la upendo la YHWH huruma, rehema na neema juu ya watu wake. Kujali kwake kimaalumu kunahusiana na ahadi zake kwa wazee wa familia (Ibrahimu, Isaka, na Yakobo). KITENZI (ingawa hakijawahi kutokea katika Zaburi) limetumika juu ya agano la upendo la YHWH (kama vile II Nyakati 36:15; Yoeli 2:18; Mal. 3:17 [mara mbili], lakini tazama utofautiano wakati wanapotenda dhambi katika II Nyakati 36:17; Ezek. 5:11; 7:4,9; 8:18; 9:5,10)!

**19:17 "Jiponye nafsi yako"** KITENZI "kimbia" (מטל, BDB 572, KB 589, *Niphal* KAULI SHURUTISHI) inatumika mara tano katika muktadha huu (kama vile 19:17 [mara mbili], 19,20,22). Ni mzaha kwenye jina "Lutu" (לוט, BDB 532).

◙ **"usitazame nyuma, wala usisimame katika hilo bonde po pote"** Malaika wanatoa mikazo ya nguvu.

1. kimbia uponye maisha yako – BDB 572, KB 589, *Niphal* KAULI SHURUTISHI
2. usitazame nyuma – BDB 613, KB 661, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotimiwa katika namna ya KITENZI AMRISHI (tazama janga la mstari wa 26, inavyoonekana ilikuwa ngumu kwa Lutu na familia yake kuyaacha maisha yao kuondolewa Sodoma)
3. usikae popote katika bonde – BDB 763, KB 840, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya KITENZI AMRISHI
4. kimbilia milimani – muundo huo huo kama #1

"Popote katika bonde" kifasihi linamaanisha "miji mitano." Hii ilimaanisha miji mikubwa mitano katika uwanda ya Yordani: Sodom, Gomora, Adma, Zeboiim, na Zoari, ambayo inaitwa Bela (kama vile Mwanzo 14:2).

**19:19** Mstari huu unaonesha kitu juu ya haiba ya Lutu. Hakika kwa nini alikuwa na hofu juu ya milima haijulikani (isipokuwa ni umbali kidogo tu kutoka hapo), lakini inaonesha na kufuanua kukosa kwao tumaini kwa utoshelevu na ulinzi unaoendelea wa YHWH (kifasihi "kibali machoni pako," kama vile 6:8; 32:5; 34:11).

◙
**NASB** **"wema"**

**NKJV "rehema"**
**NRSV "huruma"**

Hii ni Nomino *hesed* (BDB 338) ya Kiebrania ya Agano maalumu.

## MADA MAALUMU: WEMA (*HESED*)

Neno hili (BDB 338 I, KB 336 II) lina maeneo mapana ya maana.

A. Lilitumika katika kuwaunganisha wanadamu
   1. Wema kwa wenzetu (mf. 1 Sam. 20:14; 2 Sam. 16:17; 2 Nya. 24:22; Ayubu 6:14; Zab. 141:5; Mit. 19:22; 20:6)
   2. wema kwa maskini na wahitaji (mf. Mika 6:8)
   3. upendo wa Israeli kumuelekea YHWH (kama vile Yer. 2:2; Hos. 6:4,6)
   4. uzuri wa muda wa maua ya kondeni (kama vile Isa. 40:6)

B. Lilitumika kuhusiana na Mungu
   1. uaminifu wa agano na upendo
      a. " ukombozi kutoka katika maadui na taabu" (mf. Mwa. 19:19; 39:21; Kut. 15:13; Zab. 31:16; 32:10; 33:18,22; 36:7,10; 42:8; 44:26; 66:20; 85:7; 90:14; 94:18; 107:8,15,21,31; 109:21-22; 143:8,12; Yer. 31:3; Ezr. 7:28; 9:9)
      b. "katika ulinzi wa maisha kutoka katika kifo" (mf. Ayubu 10:12; Zab. 6:4-5; 86:13)
      c. "katika wepesi wa maisha ya kiroho" (mf. Zab. 119:41,76,88,124,149,159)
      d. "katika ukombozi wa kutoka dhambini" (kama vile Zab. 25:7; 51:1; 130:7-8)
      e. "katika kutunza maagano" (mf. Kum. 7:9,12; 2 Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4; Mik. 7:20)
   2. kuzielezea sifa za Mungu (mf. Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoeli 2:13; Yona 4:2; Mika 7:20)
   3. wema wa Mungu
      a. "utele" (mf. Hes.14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:5; 103:8; 145:8; Yoeli 2:13; Yer. 4:2)
      b. "ukuu katika kiwango chake" (mf. Kut. 20:6; Kum. 5:10; 7:9)
      c. "umilele" (mf. 1 Nya. 16:34,41; 2 Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136:1-26; 138:8; Yer. 33:11)
      d. Kama ngome (mf. Zab. 59:17)
      e. ilihusiana na nguvu za Mungu (mf. Zab. 62:11c-12a)
   4. matendo ya wema (mf. 2 Nya. 6:42; Zab. 89:2; Isa. 55:3; 63:7; Omb. 3:22)

Neno hili linatafsiriwa kwa njia nyingi mbalimbali katika tafsiri za Kiingereza. Nafikiri muhtasari bora wa maana yaliyo katika ufupisho yangelikuwa "hakuna kamba iliyounganisha uaminifu wa agano la Ki-Mungu" neno hili ni sambamba na neno la Agano Jipya "upendo" (*agapaō*). Mungu ni mwaminifu na mwenye upendo kwa sababu ya Yeye alivyo!

**19:20 "Tafadhali niache nitoroke "** Hii ni HALI YA KUSIHI (BDB 572, KB 589, *Niphal* HALI YA KUSIHI), ambayo inaelezea "tafadhali, niache" ya NASB.

KITENZI kinachofuata (BDB 310, KB 309) "kutoroka" (kifasihi "kuishi") ni *Qal* KITENZI AMRISHI.

**19:21 "Tazama, nimekukubali hata kwa neno hili"** Hii kifasihi ni nahau ya kiebrania "inua uso" (KITENZI, BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU ikiwa na "sura," BDB 815). Inatoka katika ulimwengu wa kimahakama. Ikiwa hakimu "aliinua uso" wa mtuhumiwa kuona alikuwa nani, utoaji wake wa haki ungeweza kuwa umewekwa hatarini (kama vile Mambo ya Walawi 19:15; Zab. 82:2; Mith. 18:5). Hakimu lazima awe mtu asiyependelea watu.
Lutu akiwa na hofu kwamba asingeweza kupona huko juu mlimani, alimuomba Bela (Zoari, BDB 858, mzizi unamaana "kutokuwa muhimu/thamani"), ambayo inamaanisha "kidogo" (BDB 859 I), "kubakizwa." Malaika cha kushangaza wakamkubalia na ombi lake (inaonekana kwa namna ya malaika watatu waliwakilisha uwepo wa

YHWH mwenyewe binafsi). Mji huu ulikuwa mkubwa vya kutosha ili kuwa na mfalme kama inavyoandikwa katika 14:2. Hii inaweza kuwa kithiolojia ni njia nyingine ya kuonesha nguvu ya utetezi (yaani Ibrahimu katika 18:22-33).

**19:22** Tena Malaika wanamwamuru Lutu.

1. harakisha – BDB 554, KB 553, *Piel* KAULI SHURUTISHI (kinyume cha mstari wa 16a)
2. toroka – BDB 572, KB 589, *Niphal* KAULI SHURUTISHI (kama vile 19:17 [mara mbili], 19,20), hapa tu katika Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati

◙**"maana siwezi kufanya neno lo lote"** Malaika waharibuo wako chini ya mamlaka kumuokoa na kumbakiza Lutu na familia yake. Hii inaaksi aidha

1. Neema ya YHWH
2. nguvu ya maombi ya utetezi (yaani 18:22 na kuendelea)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:23-26**

**[23] Jua lilikuwa limechomoza juu ya nchi Lutu alipoingia Soari. [24] Ndipo Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana. [25] Akaangusha miji hiyo na Bonde lote, na wote waliokaa katika miji hiyo, na yote yaliyomea katika nchi ile. [26] Lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi.**

**19:24 "Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni"** Inaonekana kama sio kawaida kwa neno "YHWH" linatumika mara mbili hapa. Wafasiri wa Kiyahudi wanaliita neno kwa wingi wa mfalme, wakati wafasiri wa kikristo wanaona kitu fulani cha Utatu hapa. Kusema ukweli Baraza la Sirmium lilitoa maoni yake juu ya huu mstari huu kama ifuatavyo, "Mungu mwana alishusha chini mvua kutoka kwa Mungu Baba." Tunajifunza kutoka 14:10 juu ya uwepo wa mashimo ya lami katika mji huu na inavyoonekana, kwa namna fulani kupitia miale au kunyesha kwa mvua (kama vile Ezek. 38:22; Luka 17:29; Ufunuo. 14:10; 19:20; 20:10), Mungu alisababisha ukanda wote kuchochea na kuuwasha kwa moto na kulipuka (kama vile Yuda 7).

Tena tazama kulindwa kwa kiungu kwa Zoari. Hii ni sawa na Gosheni kulindwa kutoka kwenya mapigo kumi.

Moto siku zote ulihusianishwa na hukumu ya kusafisha ya YHWH. Angalia Mada Maalu katika 15:17. 103

**19:25 "Akaangusha miji hiyo"** Hili ni neno la Kiebrania "kupindua" (BDB 245, KB 253, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFUI) likimaanisha kupindua juu chini na hivyo kuharibu. Kuharibiwa kwa Sodoma kunatumika katika maandiko yote kuashiria hukumu ya (kama vile 29:23; Isa. 13:19; Yer. 49:18; 50:40; Amosi 4:11). Uharibifu huu ulikuwa ni hukumu binafsi ya YHWH. Angefanya vivyo hivyo kwa desturi za Kikanaani ambayo Yoshua angekabiliana nayo katika utawala wa Kanaani.

**19:26** Wasomaji hawana uhakika na kitu gani kilitokea hapa, lakini ni wazi kuwa moyo wa mke wa Lutu ulikuwa bado uko Sodoma na alipata malipo yake (kama vile Luka 17:32). Alifanyika kumbukumbu ya kukosa utii! Sio tu kwamba mke wa Lutu aliathiriwa na muda wao katika Sodoma, ambavyo ni dhahiri iko wazi kutoka mistari ya 30-38.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:27-28**

**[27] Ibrahimu akatoka asubuhi kwenda mahali aliposimama mbele za Bwana, [28] naye akatazama upande wa Sodoma na Gomora na nchi yote ya hilo Bonde, akaona, na tazama, moshi wa nchi ukapanda, kama moshi wa tanuru.**

**19:27** "**kwenda mahali aliposimama mbele za Bwana**" Hii ni nahau kwa kuwa katika uwepo wa Mungu (kama vile 18:22; Mambo ya Walawi 9:5; Kumb. 10:8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:29**

**[29] Ikawa Mungu alipoiharibu miji ya Bondeni, Mungu akamkumbuka Ibrahimu, akamtoa Lutu katika maangamizi alipoiangamiza miji hiyo aliyokaa Lutu.**

**19:29 "Mungu akamkumbuka Ibrahimu, akamtoa Lutu katika maangamizi** "Tambua kwamba Lutu aliachwa na kusazwa kwasababu ya maombezi ya Ibrahimu, mmiliki wa ahadi za agano (kama vile Kut. 2:24). Mstari huu unasisisitiza ukuu wa Ibrahimu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:30-38**

**[30] Lutu akapanda kutoka Soari akakaa mlimani, na binti zake wawili pamoja naye, kwa sababu aliogopa**
**kukaa katika Soari. Akakaa katika pango, yeye na binti zake wawili. [31] Yule mkubwa akamwambia mdogo,**
**Baba yetu ni mzee, wala hakuna mtu mume katika nchi atuingilie kama ilivyo desturi ya dunia yote. [32] Haya,**
**na tumnyweshe baba yetu mvinyo, tukalale naye, ili tumhifadhie baba yetu uzao. [33] Wakamnywesha baba**
**yao mvinyo usiku ule, akaondoka huyo mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala**
**alipoondoka. [34] Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo, Tazama, nimelala jana na baba yangu,**
**tumnyweshe mvinyo tena usiku huu, ukaingie ukalale naye. [35] Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku**
**ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. [36] Basi hao binti**
**wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao. [37] Yule mkubwa akazaa mwana, akamwita jina lake**
**Moabu; huyo ndiye baba wa Wamoabi, hata leo. [38] Na yule mdogo naye akazaa mwana akamwita jina lake**
**Benami; huyo ndiye baba wa Waamoni hata leo.**

**19:30-38** Mistari hii ni maelezo ya asili ya Wamoabu na Waamoni.

**19:30 "kwa sababu aliogopa kukaa katika Soari"** Kuna uwezekano wa aina mbili kuhusiana na mstari huu: (1) alipuuzia ahadi maalumu ya malaika ya mstari wa 21 au (2) aliona namna uovu wa watu mji huu pia na alikuwa na hofu kwamba hukumu ya Mungu ingekuwa dhahili kuwaangukia wao. Aliende eneo lile lile aliyosema katika mstari wa 19 kwamba aliogopa!

**19:31** Mabinti wanaonesha kukosa tumaini kule kule katika utoshevu wa YHWH Kama ilivyo kwa baba yao. Wanaonekana kuwa wamesahau

1. Ukombozi wa Mungu kupitia Ibrahimu katika sura ya 14
2. Ukombozi wa Mungu kupitia malaika katika sura ya 19

**19:32** Mabinti waliandaa mpango wa kutunza familia yao.

1. kuja – BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI (kama vile mstari wa 34)
2. tumfanye baba yetu anywe mvinyo – BDB 1052, KB 1639, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI katika namna HALI YA KUSIHI (kama vile mstari wa 34)
3. Tuache tulale pamoja naye – BDB 1011, KB 1486, *Qal* HALI YA KUSIHI (mstari wa 34 KAULI SHURUTISHI)

Mstari wa 34 unarudia matendo haya ya kujamiiana kwa maharimu.

**19:36** Mtu anaweza kushangaa ikiwa wote walipata mimba siku ya kwanza au kwamba haya yalikuwa matukio yaliyorudiwa.

**19:37 "Wamoabu"** Maana maarufu lakini isiyo na maana ya kiufundi iliyojikita katika sauti zinazofanana "kutoka kwa baba yangu" (BDB 555), ambayo inaonesha uhusiano wa kujamiiana baina ya maharimu. Mtoto huyu baadaye alikuwa baba wa Wamoabi waliosababisha matatizo makubwa ya namna hiyo kwa ajili ya Waisraeli, na bado walikuwa ndugu (kama vile Kumb. 2:9).

**19:38 "Benami. . .wana wa-Amoni"** Benami anaonekana kumaanisha "mwana wa watu wangu" (kama vile Tafsiri ya Agano la kale la Kiyunani, Jerome, na Augustine). Wana wa Amoni (BDB 769) baadaye ilisababisha matatizo lukuki kwa taifa la Israeli (kama vile Kumb 2:19). Kumomonyoka kwa mistari ya 30-38 kulionekana aidha kama (1) alama ya kushindwa kimaadili au (2) majivuno ambayo yalisababisha kuendelea kuweka uzao wa makabila na familia bila michangavyo ya makabila mengine. Majina yote mawili ni ya kebehi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kweli gani kuu zinazowasilishwa katika sura ya 18 na 19?
2. Kwanini YHWH anatokea pamoja na malaika? Nini kusudi (au makusudi) ya ugeni wao?
3. Nini neno *Adon* linamaanisha na kuhusisha?
4. Orodhesha mmomonyoko wa taratibu wa Lutu katika sura hizi.

# MWANZO 20

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Udanganyifu wa Ibrahimu | Ibrahimu na Abimaleki | Ibrahimu na Sara Gerari | Ibrahimu na Sara | Ibrahimu huko Gerari |
| 20:1-7 | 20:1-7 | 20:1-7 | 20:1-3 | 20:1-7 |
| | | | 20:4-5 | |
| | | | 20:6-7 | |
| 20:8-18 | 20:8-13 | 20:8-18 | 20:8-10 | 20:8-13 |
| | | | 20:11-13 | |
| | 20:14-16 | | 20:14-16 | 20:14-18 |
| | 20:17-18 | | 20:17-18 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## MAELEZO YA NYUMA

A. Inastaajabisha kwa uwazi wa ahadi za sura ya 18 kwamba Ibrahimu angaliangukia kwenye utafutaji binafsi, hatua ya hofu kama alivyokuwa katika 12. Huu ni ubunifu mwingine kifasihi na wa kipekee unaonyesha kwamba kwa ukamilifu ahadi ipo juu ya Mungu na si juu ya mwanadamu.
   Hebu fikiri kidogo juu ya matatizo yote yaliyohusiana na ahadi ya mwana na vizazi vya Ibrahimu.
   1. mke tasa
   2. mke aliyetwaliwa na Farao (Mwanzo 12)
   3. mke aliyetwaliwa na Abimeleki (Mwanzo 20)
   4. dhabihu ya Isaka (Mwanzo 22)

Ilimpasa Ibrahimu kuzishikilia ahadi za YHWH katikati ya mambo yasiyozuilika. Ibrahimu “alimwamini” Mungu (Mwa. 15:6)!

B. Sura hii inatufunulia kwamba kulikuwa na wenye haki wengi huko Kanaani katika siku za Ibrahimu.
   1. Melkizedeki wa mji wa Salemu
   2. Abimeleki, mfalme wa Wafilisti

   Kifungu hiki kinaweza kueleza ni kwa nini, katika unabii wa Ibrahimu katika Mwa. 15:13-16, dhambi ya Mwamori (jina la jumla la watu wa KanaanI) haikukamilika. Katika sura hizi Abimaleki anaonekana kuwa juu kiroho kwa Ibrahimu!

C. Umuhimu wa maombi ya Ibrahimu ya kumsihi YHWH kwa niaba ya Abimeleki yanaonyesha nafasi ya pekee na upendeleo wa Ibrahimu kama mtu wa YHWH aliyechaguliwa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 20 :1-7**

**1 Ibrahimu akaondoka huko kwenda nchi ya kusini, akakaa kati ya Kadeshi na Shuri, naye akatembea katika Gerari. 2 Ibrahimu akamnena Sara mkewe, Huyu ni ndugu yangu. Basi Abimeleki mfalme wa Gerari akapeleka watu akamtwaa Sara. 3 Lakini Mungu akamjia Abimeleki katika ndoto ya usiku, akamwambia, Umekuwa mfu wewe kwa sababu ya mwanamke huyu uliyemtwaa, maana ni mkewe mtu. 4 Basi Abimeleki alikuwa hakumkaribia, akasema, Ee Bwana, Je! Utaua hata taifa lenye haki? 5 Je! Hakuniambia mwenyewe, Huyu ni ndugu yangu? Na mwanamke mwenyewe naye alisema, Huyu ni ndugu yangu. Kwa ukamilifu wa moyo wangu, na kwa kuwa safi mikono yangu, nimefanya hivi. 6 Mungu akamwambia katika ndoto, Nami nimejua ya kwamba kwa ukamilifu wa moyo wako umefanya hivi, ndipo nami nikakuzuia usinitendee dhambi, kwa hiyo sikukuacha umguse. 7 Basi sasa umrudishe mwanamke kwa mtu huyo, maana yeye ni nabii, naye atakuombea, upate kuishi. Bali usipomrudisha, fahamu ya kwamba kwa hakika utakufa wewe na watu wote ulio nao.**

**20:1 “Ibrahimu akaondoka huko”**Ibrahimu aliyaacha makazi yake katika mialoni ya Mamre (kama vile 18:1) au Hebroni (kama vile 13:18). Ibrahimu aliishi maisha ya kuhamahama, kama alivyofanya Ayubu (hali ya muda ule ule).

◙ **“nchi ya kusini”** Kifungu hiki kinarejelea juu ya “nchi ya kusini” (BDB 616), ambayo ilikuwa nusu jangwa, ukiwemo mji wa Beer sheba kuelekea kusini. Eneo hili hili linatajwa katika 13:1.Wazee, Ibrahimu, na Isaka waliishi katika eneo hili kwa muda mrefu.

◙ **“Kadeshi”** Huu mwaloni pia ulijulikana kama Kadesh-barnea (kama vile 14:7; 16:14), ambao ni maili zipatazo 50 kusini mwa Beer sheba. Inataia shauku kwamba hili neno Kadeshi (BDB 873 II, linalomaanisha “uliyowafikishwa”) linahusiana na neno la Kiebrania “takatifu,” ambalo ni *Kadosh* (BDB 871).

◙ **“Shuri”** Hili neno (BDB 1004 III) linamaanisha “ukuta,” huenda unarejelea juu ya mtiririko wa ngome za ki-Misri (kama vile I Sam. 15:7; 27:8). Neno hili linarejelewa katika 16:7 kama mahali ambapo Malaika wa Bwana alizungumza na Hajiri. Hatufahamu ni wapi eneo hili lipo kijiiografia, lakini kwa namna iliyo dhahiri ni eneo la kusini mwa Beersheba barabara ya kuelekea Misri (kama vile 18:25).

◙ **“naye akatembea katika Gerari”** Kwa uwazi kabisa kuna hatua mbili za uhamaji zilizoandikwa hapa**,** Gerari iko kusini mwa *Kadesh.* KITENZI cha kwanza kilicho katika mst. 1 “akatembea” (BDB 652, KB 704) kiuhalisia linamanisha “kung’oa vigingi vya hema,” lakini huyu, “alikaa kwa muda” (BDB 157, KB 184), hili linamaanisha muda mrefu (kama vile 12:10; 21:23-24; 26:3; 32:6; 35:27;47:4). Hili lilikuwa eneo ambalo baadaye lilishikiliwa na

Wafilisti (kama vile 10:19). Tunajifunza kutoka katika historia ya kale kwamba eneo hili lilikuwa karibu na Gaza, moja ya miji mikuu ya Wafilipi.

**20:2 "Huyu ni ndugu yangu"** Hiki ni kitu kile kile kilichotokea katika 12:17-18 kwa Farao huko Misri. Hiki pia kilitokea kwa Isaka na Rebeka katika 26:1 na kuendelea. Maelezo pekee tuliyonayo kuhusiana na hili ni mst. 13, ambapo lilionekana kuwa tendo la kawaida kwa Ibrahimu na Sara baada ya kuondoka Uru wa Wakaldayo. Inawezekana kwamba kweli walikukuwa nusu ndugu (kama vile 12), lakini pia inawezekana kwamba Ibrahimu alimtwaa katika sherehe ambayo tumeisoma katika vigae vya Nuzi ambavyo vinaeleza utamaduni wa Kihuri.

◙ **"Abimeleki mfalme wa Gerari akapeleka watu akamtwaa Sara"** Je Hili linamaanisha kwamba kimwonekano bado Sara alikuwa anavutia? Kwa ujumla hili linawezekana, tukijikita katika 12:14. Wengine wanasema kwamba Mungu aliurudisha mwili wake katika ujana ili kumwezesha kubeba mimba na ya kwamba alikuwa mzuri tena. Watoa maoni wengine wamedhani kwamba, kwa kuwa alikuwa na miaka takriban tisini, hii ilikuwa njia ya kiutamaduni ya kulikazia agano la urafiki kati ya Ibrahimu na Abimaleki.

**20:3 "Mungu akamjia Abimeleki katika ndoto"** Abimeleki (BDB 4) ni jina la mtawala, kama Farao, Kaizari, au Zari. Kwa uwazi jina hili linamaanisha "baba ni mfalme" au "mfalme ni baba yangu." Tunaliona jina la jumla kwa wafalme wa Wafisti linalopatikana katika utangulizi wa Zaburi ya 34.

Ile dhana kwamba Mungu alimtokea katika ndoto, kama alivyofanya kwa Labani katika 31:34, inaonyesha kitu fulani cha uhusiano wa mtu huyu na Mungu. Kwa upekee hili linaweza kuonekana pale ambapo anamuita Mungu *Adonai* (mstari wa 4) na pia inaonyesha kwamba tayari angekuwa na uelewa fulani kuhusu Mungu wa agano (YHWH), kama alivyofanya Melkizedeki (Mwanzo 14), mtu mwingine ambaye hakuwa na agano.

**20:4-6** Hapa tunaona majadiliano kati ya Mungu na Abimeleki ambapo Abimeleki anamkumbusha Mungu kwamba alilitenda jambo hili pasipo hatia, pasipokujua ukweli wo wote. Sitiari iliyopo katika mst. 5, "kwa kuwa mikono yangu i safi"(MUUNDO WA MANENO BDB 667 na BDB 496), inarejelea nahau ya Kiebrania ya mikono iliyo wazi yaani, "hakuna kilicho fichika." Hii inafanana na "katika ukweli wa moyo wangu" (MUUNDO WA MANENO BDB 1070 na BDB 523, kama vile I Fal. 9:4; Zab. 7:8; 101:2). Katika mst. 6 Mungu anasema kwamba amemzuia asitende dhambi (kama vile I Sam. 25:39; Ayubu 33:18; pia elewa Zab. 19:13).

Kwa uthibitisho ulio dhahiri hili linarejelea juu ya aina fulani ya ugonjwa ambao ulimpata Abimaleki na watu wa nyumbani mwake (kama vile mist. 17-18;12:17). Nafikiri kwamba ni muhimu kuona kwamba kwa hakika Mungu alihusika katika ulimwengu wake katika kuwajali mtu asiye wa agano. Pia hili linaweza kuonekana katika kushughulika kwake juu ya Hajiri na Ishmaeli. Hili lazima liwe tumaini kuu kwa viumbe vyote vya kibinadamu (kama vile Eze. 18:23,32; Yohana 3:16; Rum. 11:32; I Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11;II Pet. 3:9; I Yohana 2:1; 4:14).

**20:4 "Bwana,Utaua hata taifa lenye haki?** Aya hii inaonyesha uelewa wa haki ya Mungu, uelewa ambao Ibrahimu alikuwa nao katika 18:23. Kwa uwazi kabisa wafalme walikiona kifo chake kama mwanzo wa uharibifu wa kabila lote (pigo, kama vile mst. 17). Anadai (kwa kutumia neno "wasio na hatia" au "wenye haki," BDB 843) kwamba hakumtenda Sara tendo lo lote la kiuzinifu na ya kwamba alitenda nje ya ufahamu wake, si dhambi iliyojulikana. Kutokana na mstari huu ni dhahiri kwamba uzinzi ulifikiliwa kama ukiukaji mbaya wa maadili ya Mungu hata katika historia ya kipindi hiki cha kale (kama vile Mwa. 12:17-19; 26:7-11) kwa sababu uliathiri haki za kiurithi.

## MADA MAALUM : UJINSIA WA MWANADAMU

I. Maelezo ya Utangulizi
   A. Wakristo wamevutiwa sana na uyakinishaji wa Kiyunani, ambao wote umeufanya mwili wa mwanadamu kuwa tendo la kawaida la uovu. Biblia inakiri juu ya uzuri wa uumbaji wa kimwili (kama vile Mwa. 1:31), lakini inatambua matokeo ya uasi wa mwanadamu (kama vile Mwa. 3). Siku moja laana hii itaondolewa! (kama vile Rum. 8:18-22).

B. Wanaume kwa wanawake ni wazo la Mungu! Ujinsia wa mwanadamu ni sehemu ya uumbaji wa Mungu na mpango kwa mwanadamu aliyeumbwa kwa sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27). Kujamiianaa si kitu tukifanyacho; ni kama tulivyo. Kila eneo la fikra na maisha yetu linaathiriwa na kujikita katika kujamiiana, kama inavyotafsiriwa na tamaduni.

II. Mitazamo ya Kibilia (mifano iliyoteuliwa)
   A. Kutoka kitabu cha Mwanzo
      1. Kuna uhusiano asilia kati ya wanaume na wanawake (kama vile Mwa. 1:26-27; angalia neno la kujifunza "msaidizi" katika Mwa. 1:18 mtandaoni.
      2. Watoto walikuwa agizo toka kwa Mungu (yaani, Mwa. 1:28; 9:1,7).
      3. Uumbaji wote unakubalika kama "mzuri sana" katika Mwa. 1:31, likiwemo tendo la kujamiiana kwa mwanadamu.
      4. Wanawake si kinyume, bali ni ukamilifu, kwa wanaume (yaani, Mwa. 2:18).
      5. Uasi wa Hawa na Adamu wa kufunguliwa macho umetuathiri sisi sote na ulimwengu wetu, ikiwemo namna ya kujamiiana (kama vile Mwa. 3:7,16; Rum. 5:12-21).
   B. Upendo wa kimwili unakubaliwa katika Maandiko, hata baada ya Anguko.
      1. Mithali 5:15-23 inakiri juu ya kuwepo maisha ya wawili na hata tendo la kujamiiana
      2. Mhubiri 9:7-9, furahia maisha yako katika yote namna zote uwezavyo
      3. Wimbo Ulio Bora ni ukubalifu wa mapenzi ya mwili
      4. Mungu ni roho ya milele pasipo mwili, bado "Yeye" anatumia stiari za kujamiiana ya mwanadamu kujieleza Mwenyewe (yaani, Hosea 1-3; 11)

III. Mipaka iliyowekwa na Mungu kwa ajili ya kueleza ujinsia wa Mwnadamu
   A. Ndoa
      1. kama desturi iliyo katika Agano la Kale na Agano Jipya
      2. ilitumika kama mfano wa "maisha ya kujazwa na Roho," Efe. 5:15-6:9
      3. 1 Wakorintho 7:3-5, kujamiiana ni zaidi ya kuzaliana
         a. mwili ni mali ya Mungu, 1 Kor. 6:19-20
         b. mwili ni mali ya mke/mme mmoja, 1 Kor. 7:4
   C. Ujinsia wa Mwanadamu unatumika kutoa kielelezo cha Mungu na pendo lake.
      1. Wagalatia 3:28, ufupisho wa zama mpya, injili na mapana yake katika pande zote zinaonekana na sawa.
      2. Waefeso 5:21-31, nyumbani mwa Mkristo huwa mfano wa mahusiano kati ya Kristo na Kanisa lake (kama Hosea 1-3 ilivyotumika, katika Hosea ndoa ni kama njia ya kueleza upendo wa Mungu kwa Israeli)
   D. Mungu anajieleza kama mke na mme.
      1. mme, aliyezoeleka
         a. Baba, Kumb. 1:31; 32:5; Zab. 103:13; Isa. 63:16; 64:8; Yer. 3:4,19; 31:9; Hos. 11:1; Mal. 3:17
         b. mme, Hos. 11:3-4
      2. mke
         a. Mwa. 1:2, Roho ya Mungu ilitulia juu ya vilindi vya maji
         b. Mwa 17:1, Neno *El Shaddai* linaweza kuwa na maana nyinginezo (yaani, mzizi wa Kiarabu)
         c. Kumb. 32:18, Mungu kama ndege jike
         d. Kut. 19:4, Mungu kama tai jike
         e. Isa. 49:14-15; 66:9-13, Mungu analinganishwa na mama anyonyeshaye

IV. Upotofu wa mwanadamu juu ya ujinsia wa mwanadamu ulioumbwa na Mungu
   A. Kabla ya ndoa (uasherati) na baaada ya ndoa (uzinzi)

B. Badhi ya maandiko yaliyochaguliwa

1. 1 Kor. 6:15-20
2. Gal. 5:19-21
3. Ebr. 13:4

C. Kujamiiana (katika vyote, fikra na tendo, kama vile Mt. 5:27-28) inaweza kuwa kibali cha watu kuitumia kama utosherevu binafsi.

D. Taraka
1. Mara nyingi hii ni nyongeza bora ya pili
2. Hii iliruhusiwa katika Agano la Kale, Kumb. 24:1-4, lakini ilizuiliwa na Yesu, Mt. 5:27-32; 19:3-12.
*3.* sikiliza mafundisho yaliyo katika mfumo wa sauti ulioko mtandaoni "*Controversial and Difficult Texts" #2130 na 2131*

E. Kujamiiana kwa jinsia moja (angalia Mada Maalum : Kujamiiana kwa jinsia moja)

1. Kamwe si mapenzi ya Mungu
   a. Law. 20:13
   b. Rum. 1:26-27
   c. 1 Kor. 6:9-11
2. Hii ni mbaya kwa sababu ni maisha ya dhambi, lakini ni mbaya sana kuliko maisha mengine ya dhambi ya ngono (uzinzi au uasherati au shauku). Hii ni dhambi isiyosameheka" (ambayo ni kutokuamini).
3. Wanadamu walioanguka wanaweka bidii katika ujinsia. Hili lina nguvu, bado linaendelea, shauku iliyo ovu, hulka, na ghadhabu lazima iwe juu yetu kila siku!
4. Waamini wengi walikuwa wakijihusisha na tendo hili la kujamiiana kwa jinsia moja katika mahekalu ya wapagani wa kikahaba, lakini baada ya wokovu hawakuwa watumwa tena wa tendo hili hata kidogo, 1 Kor. 6:9,11

V. Maelezo ya Kuhitisha
   A. Ujinsia ni mpango wa Mungu kwa ajili ya ukamilifu wa kuuongeza ulimwengu
   B. Ujinsia ni kwa ajili ya muda tu, si wa milele, Mt. 22:30; Marko 12:25; Luka 20:34-36.
   C. Ujinsia umeathiriwa na Anguko. Kila mmoja wetu kwa uhaliasia ni mhuhusika wa hili, ni wa mtu binafsi.
   D. Ujinsia unamaanisha kutusaidia sisi kama watu waliokombolewa kujichunga zaidi (muhuri wa tunda la Roho katika Gal. 5:23).
   E. Wakristo wanalistahimili jukumu la kwanza la kuzisaidia nyumba zao, jamii, na mataifa walishighulika na hili lilio na nguvu na jambo la uovu. Hii ni juhudi au ngazi ya juu. Sisi ni mifano ya neema ya ki-Ungu. Elimu bora inayoihusu kujamiiana ni wazazi wanaopendana wao wenyewe!

   F. Zinaa inaweza kuwa ya kustaajabisha au ya kutisha. Hii ilimaanisha
      1. kuijaza nchi
      2. kuwaunganisha watu wawili
      3. kuunda familia na jamii
      4. kufurahisha

**20:7** Hii miundo ya MANENO ina urahisi katika ujumbe huu uliotoka kwa Mungu kwenda kwa Abimaleki kupitia ndoto.

1. kumrejesha mke wa mtu," BDB 996, KB 1427, *Hiphil* SHURUTISHI, katika namna inayovutia, hiki ni KITENZI kile kile kinachotumika mara nyingi sana katika Agano la Kale kwa maana ya "kutubu"
2. "naye atakuombea" BDB 813, KB 933, *Qal* ISIO TIMILIFU (huenda kauli hii ilitumika katika maana ya MASHARTI). Elewa msamaha wa Mungu ulifuatana na maombi ya kusihi yaliyofanywa na Ibrahimu (kwa muda mrefu kama ilivyo katika Ayubu 42:8). Tendo hili linaonyesha umuhimu wa dhamana ya Ibrahimu iliyo ya kipekee!
3. "upate kuishi," BDB 310, KB 309, *Qal* SHURUTISHI
4. "Bali usipomrudisha," *Hiphil* ENDELEVU (angalia #1)
5. "fahamu," BDB 393, KB 390, *Qal* SHURUTISHI
6. "hakika utakufa," the KITENZIJINA HALISI NA KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi huo huo (BDB 559,KB 562) kinadokeza uweza. Dhambi inahusiana na "mauti" (2:17; Kut. 10:17;Hes. 18:22).

◙ **"yeye ni nabii"** Haya ni matumizi ya kwanza ya neno hili katika Biblia na yenye kutokea katika kitabu cha Mwanzo. Hili neno "nabii" (BDB 611) linamrejelea mtu anayepokea na kutoa ufunuo wa Mungu (kama vile Hes. 12:6). Hata hivyo, katika muktadha huu neno hili linaonekana kuhusiana na maombi ya kusihi (kama vile mist. 7, 17). Jambo hili linawezekana kwa sababu ya marejeo mengine ya kibiblia (kama vile I Sam. 7:5, 12:19, 23; Ayubu 42:8; Jer. 7:16; 11:14; 14:11; 27:18). Wengine wanasema kwamba neno hili linarejelea juu ya ufunuo wa maamuzi ya Mungu kwa watoto wake (kama vile 18:19).

## MADA MAALUM: UNABII WA AGANO LA KALE

. UTANGULIZI
- A. Maelezo ya Ufunguzi
  1. Jamii ya waaminio haikubaliani kuhusu namna ya kufasiriri unabii. Baadhi ya kweli zingine zimehimarishwa kama sehemu ya imani halisi kwa karne zote, lakini si hii.
  2. Kuna hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale zilizoelezwa vizuri
     - a. Kabla ya utawala wa wafalme na malkia
       - (1) Watu binafsi walioitwa manabii
         - (a) Ibrahimu - Mwa. 20:7
         - (b) Musa – Hes. 12:6-8; Kumb. 18:15; 34:10
         - (c) Haruni – Kut. 7:1 (msemaji wa Musa)
         - (d) Miriamu – Kut. 15:20
         - (e) Medadi na Eldadi Hes. 11:24-30
         - (f) Debora – Amu. 4:4
         - (g) Wasiotajwa – Amu. 6:7-10
         - (h) Samweli – 1 Sam. 3:20
       - (2) marejeleo kuhusu manabii kama kundi – Kumb. 13:1-5; 18:20-22
       - (3) Kundi la manabii au waongozaji 1 Sam. 10:5-13; 19:20; 1 Fal. 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Fal. 2:3, 7; 4:1 , 38; 5:22; 6:1, nk.
       - (4) Masihi aliyeitwa nabii – Kumb. 18:15-18
     - b. Utawala wa kifalme usioandikwa (ulijishughulisha na mfalme):
       - (1) Gadi – 1 Sam. 22:5; 2 Sam:24:11; Nya. 29:29
       - (2) Nathani – 2 Sam. 7:2; 12:25; 1 Fal. 1:22
       - (3) Ahija – 1 Fal. 11:29
       - (4) Yehu – 1 Fal. 16:1, 7, 12
       - (5) wasiotajwa 1 Fal. 18:4, 13; 20:13, 22
       - (6) Eliya – 1 Fal. 18-2 Fal. 2

(7) Mika – 1 Fal. 22
(8) Elisha- 2 Fal. 2:9, 12-13

c. Manabii wa sasa walioandikwa (wanatumikia taifa na mfalme): Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

B. Maneno ya Kibiblia.

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Sam. 9:9 Marejereo yenyewe yanaonesha mabadiliko kuelekea neno nabi Ro'eh linatokana na neno la jumla "kuona." Mtu huyu alielewa njia za Mungu na mipango na alikuwa akiona kuhusu kuelewa kusudio la mapenzi ya Mungu kwa jambo fulani.
2. *Hozeh* = "muonaji" (BDB 302, KB 3011), 2 Sam 24:11. Kimsingi ni neno sawa na *Ro'eh*. Linatokana na neno adimu "kuona." Muundo uliobadilishwa unatumika mara nyingi sana kurejea juu ya linatumika kuwarejelea manabii. (yaani "kutazama").
3. *Nabi'* = "nabii" (BDB 611, KB 661), sawa na KITENZI cha Lugha ya Mesopotamia ya Kale *Nabu* = "kuita" na Kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neno la kawaida sana katika Agano la Kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili na maana yake halisi haifahamiki vizuri lakini "kuita" kwa sasa inaonekana ndiyo sahihi. Bila shaka uelewa wa uhakika unatokana na maelezo ya Musa kuhusu YHWH na uhusiano wa Musa na Farao kupitia kwa Aruni (kama vile Kut. 4:10-16; 7:1 Kumb. 5:5). Nabii ni yule mtu ambaye huzungumza na Mungu kwa ajili ya watu Wake (Amosi 3:8; Yer. 1:7, 17; Ezek. 3:4).
4. Maneno yote matatu yanatumika katika huduma ya nabii katika 1Nya. 29:29; Samweli- *Ro'eh*; Nathani – *Nabi*' na Gadi - *Hozeh*.
5. Fungu *'ish ha – 'elohim,* "Mwana wa Mungu," pia ni neno pana kwa mtu yule anayezungumza na Mungu. Limetumika takribani mara 76 katika Agano la Kale kwa maana ya "nabii."
6. Neno "nabii" ni Kiyunani kwa asili yake. Linatokana: (1) *pro* = "kabla" au "kwa ajili ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza"

. MAANA YA UNABII

A. Neno "nabii" lina elimu-maana pana katika Kiebrania kuliko kiingereza vitabu vya kihistoria vya Yoshua mpaka wafalme (isipokuwa Ruthu) imeandikwa na Wayahudi kama "manabii wa mwanzo" wote wawili Ibrahimu (Mwa. 20:7 Zab. 105:15) na Musa (Kumb. 18:18) wametambuliwa kama manabii (pia Miriamu, Kut. 15:20). Kwa hiyo kuwa makini na maelezo ya kiingereza yanayobashiri
B. "kutoa unabii kwaweza kuelezewa kama kuielewa historia inayokubaliana na maana ya maneno yanayohusika ki-Uungu, yenye kusudi la ki-Ungu, na ushiriki wa ki-Ungu." *Interpreter's Dictionary of the Bible*, vol. 3, ukurasa wa 896
C. Nabii sio mwana falsafa wala mwana theolojia, bali ni mtu mpatanishi wa agano ambaye huchukua neno la Mungu kulipeleka kwa watu wake ili kuyatengeneza maisha yao ya mbele kwa kurekebisha maisha waliyonayo sasa" Nabii na unabii, *Encyclopedia judaica* juzuu 13 ukurasa wa 1152.

. KUSUDI LA UNABII

A. Unabii ni njia ya Mungu ya kuongea na watu wake, kuwapa mwongozo katika mipango yao mipya na matumaini katika udhibiti wake juu ya maisha yao na matukio ya ulimwengu. Ujumbe wao kimsingi ulikuwa wa kiushirikiano. Ulikusudia kukemea, kuhamasisha, kusababisha imani na toba na kuwajulisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Kuwafanya watu wa Mungu kuwa waaminifu kwenye maagano ya Mungu. Kwa hili yapaswa kuongezewa kuwa daima inatumika kubainisha wazi uchaguzi wa Mungu na msemaji wake (Kumb. 13:1-3; 18:20; 22). Hii ingalirejea juu ya Masihi.
B. Daima nabii anachukulia mgogoro wa kihistoria na kithiolojia nyakati zake na kuuendeleza katika muundo wa siku za kiama. mtazamo huu wa siku za mwisho wa historia si wa kawaida katika Israeli na maaana yake ya uteuzi wa kiungu na ahadi za maagano.
C. Ofisi ya nabii inaonekana kuweka usawa (Yer.18:18) na kujitwalia ofisi ya kuhani mkuu kama njia ya

kujua mapenzi ya Mungu. Urimu na Thumamu wanazidi kuingia katika ujumbe wa mdomo toka kwa mnenaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kutoweka katika Israeli baada ya malaki. Haionekani tena mpaka miaka 400 baadaye ikisemwa na Yohana mbatizaji. Haijulikani ni kwa namna gani kipawa cha Agano Jipya cha "unabii"kinahusishwa na agano la kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Kor. 12:10; 28-29; 14:29, 32,37; Efe. 4:11) sio wadhihilishaji wa ufunuo mpya au maandiko, bali wanenaji wa mambo yajayo ya mapenzi ya Mungu katika hali ya Agano.

D. Unabii sio hasa utabiri kiasili. Utabiri ni njia mojawapo ya kuthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, lakini itambuliwe kuwa "chini ya 2% ya unabii wa Agano la Kale ni wa ki-Umasihi. Chini ya 5% hasa inaelezea enzi mpya ya patano. "chini ya 1% inahusu matukio ambayo bado hayajatokea."(Fee and Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).

E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati kuhani anawakilisha watu kwa Mungu. Huu ni usemi wa jumla. Kulikuwepo na wenye dharura kama Habakuki, ambaye alijitetea kwa Mungu.

F. Sababu inayosababisha kutowaelewa manabii ni kwamba hatujui ni vipi vitabu vyao viliandikwa. Havina mfuatano mzuri. Vinaonekana kuwa na mrejea lakini sio mara zote kile mtu angekitarajia. Mara zote havina muundo wa kihistoria ulioko wazi, muda muafaka, au mgawanyo wa wazi kati ya mafanikio. Vitabu hivi ni vigumu:
   1. Kusoma katika mkao mmoja
   2. Kuchambua ki mada au mada kwa mada
   3. Kutambua kiini cha ukweli au kusudio la manabii katika kile kipindi.

. TABIA ZA UNABII

A. Katika Agano la Kale kunaonekana kuwepo na mwendelezo wa dhana ya "Nabii" na "unabii." katika Israeli ya mwanzo kulianzishwa ushirika wa manabii, ukiongozwa na kiongozi mwenye haiba kubwa kama Eliya au Elisha. Wakati mwingine kifungu "wana wa manabii" kilitumika kumaanisha kundi hili (2 Falme 2). manabii walikuwa wanaainishwa na upeo wa hisia ( 1 Sam. 10:10-13; 19: 18-24).

B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita haraka sana kuingia katika kipindi cha nabii mmoja mmoja. palikuwepo na wale manabii (wa ukweli na wa uongo) waliotambuliwa na mfalme na waliishi katika nyumba ya mfalme (Gad na, Nathan). Pia, palikuwa na wale waliokuwa wanajitegemea, wakati mwingine hawakuhusiana na jamii ya watu wa Israel wenye hadhi (Amosi). Wakijumuisha wote wanaume na wanawake (2 Fal. 22:14)

C. Nabii daima alikuwa muonaji wa nyakati zijazo, kwa sharti la mwitikio wa mtu mmoja. Daima wajibu wa nabii ulikuwa kuweka wazi mpango wa Mungu kwa watu wote kuhusu uumbaji wake usioathiriwa na mwitikio wa Mwanadamu. Mpango wa kiama kwa watu wote ni wa kipekee kati ya manabii wa kake wa Mashariki. Utabiri na itii wa agano ni pacha ya ujumbe wa kinabii (kama vile Fee na Stuart, uk. 150). Hii inaonesha kuwa manabii kimsingi walikuwa na mtazamo wa pamoja. Kwa kawaida walihudumia taifa japo sio taifa pekee bali na mengine.

D. Mambo mengi ya kinabii yaliwasilishwa kwa mdomo. Baadaye yaliwekwa pamoja kwa namna ya dhamira, mfuatano, au mpangilio mwingine wa fasihi za Mashariki ambazo zimepotea kwetu. Kwa sababu ilikuwa kwa njia za simulizi hazikupangiliwa kama maandiko yaliyoandikwa. Hii inasababisha kuwepo na ugumu wa kukisoma kitabu chote moja kwa moja na kuwepo ugumu wa kuelewa pasipo muundo maalumu wa kihistoria.

E. Manabii wanatumia mipangilio kadhaa kufikisha ujumbe wao.
   1. Mazingira ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake katika mahakama, daima ni suala la talaka ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwa kutokuwa mwaminifu (Hosea 4; mica 6).
   2. Maombolezo ya msiba –kipimo halisi cha aina ya ujumbe huu na tabia yake ni "huzuni" iliyoondolewa kama kitendo maalumu(Isaya 5; Habakuki2).
   3. Tamko la Agano la Baraka- asili ya kimasharti ya agano limesisitizwa na madhara yake yote, hasi na chanya, yametajwa kwa ajili ya siku za mbeleni (Kumb 27:28).

. MIONGOZO INAYOSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

A. Tafuta kusudio la awali la nabii (mwandishi) kwa kutambua muundo wa kihistoria wa kitabu na uelewa wa kifasihi wa kila kitabu. Bila shaka kitahusu Waisraeli kuvunja agano la Musa kwa namna Fulani.
B. Soma na kutafsili unabii wote, na sio sehemu tu, elezea kwa mhutasari kama ulivyo ujumbe. Tazama namna unavyohusiana na habari iliyopo. Jaribu kuelezea kwa muhtasari kitabu chote.
C. Chukua tafasili ya fasihi ya habari hadi kitu fulani katika andiko lenyewe likupeleke kwenye matumizi ya kitamathari; kasha weka lugha ya kitamathari katika nadharia.
D. Chambua vitendo vyenye alama katika uwazi wa mpangilio wa kihistoria na aya zinazofanana. Kumbuka hili kuwa fasihi za mashariki ya mbali sio fasihi za magharibi au zile za kisasa.
E. Zingatia utabiri wako kwa makini.
    1. Je unajitenga na siku zile za mwandishi?
    2. Je ni wapi baadaye unatekelezwa katika historia ya Israeli?
    3. Je bado ni matukio yajayo?
    4. Unanahitajika kukamilishwa sasa au siku zijazo?
    5. Ruhusu waandishi wa biblia, sio wa sasa, kuongoza majibu yako.
F. Jambo maalumu
    1. Je utabiri umewezeshwa na mwitikio wenye masharti?
    2. Je ni kwa yupi unabii huu umeelekezwa (na kwa nini?)
    3. Kuna uwezekano, wa kibiblia au kihistoria, kwa utekelezwaji wa pamoja?
    4. Waandishi wa Agano Jipya, wakiwa chini ya uvuvio, walikuwa na uwezo kumuona masihi sehemu mbalimbali katika Agano la Kale ambazo hazikudhihilishwa kwetu. hili halina uhakika, wanaonekana kutumia mfumo wa kugawanya vitu. Kwa vile sisi hatukuvuviwa bora tuwaachie wenyewe.

. VITABU VITAKAVYOKUSAIDIA

A. *A Guide to Biblical Prophecy* cha Carl E. Amending and W. ward Basque
B. *How to read the Bible for All its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
C. *My servants the Prophets* cha Edward J. Young
D. *Plowshares and Pluning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Profecy and Apocalyptic* cha D. Brent Sandy
E. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, vol. 4, pp. 1067-1078
F. *The Language and Imagery of the Bible cha* G.B Caird

◙ **"wewe na watu wote ulio nao"** Tena tunao umuhimu wa kuwa na ushirika, ambao ni wa kawaida katika Agano la Kale (kama vile 17:27; 19:12). Katika hali iliyo dhahiri hatulioni jambo binafsi hadi kufikia Ezekieli 18 na Yeremia 31:31-34, ambayo itabainisha Agano Jipya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 20:8-18**

***8*** **Abimeleki akaamka asubuhi na mapema, akawaita watumwa wake wote, akawaambia maneno hayo yote**
**masikioni mwao, nao watu hao wakaogopa sana.** ***9*** **Kisha Abimeleki akamwita Ibrahimu, akamwambia,**
**Umetutenda nini? Nimekukosa nini, hata ukaleta juu yangu na juu ya ufalme wangu dhambi kuu? Umenitenda**
**matendo yasiyotendeka.** ***10*** **Abimeleki akamwambia Ibrahimu, Umeona nini hata ukatenda jambo hili?** ***11***
**Ibrahimu akasema, Kwa sababu naliona, Yakini hapana hofu ya Mungu mahali hapa, nao wataniua kwa ajili ya**
**mke wangu.** ***12*** **Naye kweli ni ndugu yangu, binti wa baba yangu ila siye mwana wa mama yangu, ndipo akawa**
**mke wangu.** ***13*** **Ikawa hapo Mungu aliponisafirisha kutoka nyumba ya baba yangu, nikamwambia, Hii ndiyo**
**fadhili yako, utakayonifanyia. Kila mahali tuingiapo, useme, Huyu ni ndugu yangu.** ***14*** **Basi Abimeleki akatwaa**
**kondoo, na ng'ombe, na watumwa, na wajakazi, akampa Ibrahimu, akamrudishia Sara mkewe.** ***15*** **Abimeleki**

**akasema, Nchi yangu iko mbele yako, kaa upendapo. [16] Naye akamwambia Sara, Tazama! Nimempa ndugu yako fedha elfu, itakuwa kifunika macho kwako mbele ya wote walio pamoja nawe, nawe utakuwa na haki mbele ya watu wote. [17] Ibrahimu akamwomba Mungu, Mungu akamponya Abimeleki, na mkewe, na wajakazi wake, nao wakazaa wana. [18] Maana Bwana alikuwa ameyafunga matumbo ya watu wa nyumbani mwa Abimeleki, wasizae, kwa ajili ya Sara mkewe Ibrahimu.**

**20:8 "akaamka asubuhi na mapema"** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye umuhimu na uharaka (kama vile 21:14; 22:3) wa kuitikia juu ya matakwa ya Mungu yalioelezwa.

◙ **"nao watu hao wakaogopa sana"** Si imani ya Abimaleki tu ambayo inaonekana katika mist. 4-6, bali hata imani ya watu wote wa nyumbani mwake inaelezwa katika mstari huu. Kifungu hiki kinaufanya usemi wa Ibrahimu ulio katika mstari wa 11a kuwa wa kimasihara.

**20:9-10** Kupitia mtiririko wa maswali matatu kwa uhalisia Abimeleki kwa uhalisia anaonyesha kutomtenda Ibrahimu neno lo lote, kama alivyofanya Farao hapo awali katika sura ya 12.

**20:10 "Umeona"** Wengine wanaliona hili kama ono la kinabii, lakini wasomi walio wengi wanalichukulia hili kumaanisha "Umeona nini kwa wakati uliopita ambacho kimekusababisha kutenda hivi?"

**20:11-12** Ibrahimu anatoa maelezo ya aina tatu yanayohusu sababu iliyomfanya kutenda hivi. Maelezo ya aina hizo zote kwa kiasi fulani yalionekana kutokuwa sahihi. Hii ni kwa sababu ya woga au mauti pia hili linanukuliwa katika 12:12 na kutokea kwa Isaka katika 26:7.

**20:13"aliponisafirisha"** Katika lugha ya Kiingereza kwa namna fulani tunaona kwamba huyu anamaanisha kwamba ni usababishi wa Mungu uliomfanya kutenda namna hii. Hili linatukumbusha juu ya Adamu alivyomlalamikia Mungu (kama vile Mwa. 3:12). Hata hivyo, haijulikani kama tunaweza kulielewa jambo hili kwa jinsi hii. Kinachojulikana ni kwamba hili jina *Elohim*, ambalo linatumika hapa, linafuatiwa na KITENZI CHA WINGI (BDB 1073, KB 1766, *Hiphil* KILICHO TIMILIFU), ambacho kinatumika sana katika namna isiyo ya kawaida pindi ikiurejelea Uungu wa Mungu Mmoja wa Waisraeli. Wengine wanasema kwamba huyu anafadhaika kwa sababu ya ukaribu wa Abimeleki na miungu wengine (S. R. Driver). Hata hivyo, Abimeleki anaonekana kufahamishwa juu ya Mungu mmoja pia. Waalimu wa sheria za Kiyunani wanasema kuwa kifungu hiki kiko katika hali ya WINGI, japo ni adimu, si cha kawaida pindi kimrejeleapo Mungu (kama vile 1:26; 11:7; 35:7; II Sam. 7:23). Mara nyingi Kanisa huutafsiri WINGI huu wa Agano la Kale kama muundo wa kwanza wa mafundisho ya Utatu.

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
    1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
    2. Yohana 14:26
B. Matendo ya Mitume - Mdo. 2:32-33, 38-39
C. Paulo
    1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
    2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
    3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
    4. Gal. 4:4-6
    5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
    6. 1 The. 1:2-5

7. 2 The. 2:13
8. Tit. 3:4-6

D. Petro – 1 Pet. 1:2
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
   1. Jina *Elohim* liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
   2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
B. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
   1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
   2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
   3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   4. Zakaria 3:1-2
C. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
D. Mungu (YHWH) na Masihi (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
E. Masihi na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
F. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Konstantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho)

◙ **"Hii ndiyo fadhili yako, utakayonifanyia. Kila mahali tuingiapo"** Kifungu hiki kinaonekana kuonyesha kwamba Ibrahimu na Sara alikuwa amefanya makubaliano kuhusu ndugu huyu na dada alifanya ujanja toka wakati ule walipotoka Uru ya Wakaldayo.

**20:14** Kwa uahalisia kifungu hiki kinarudia kile alichokifanya Farao kwa Ibrahimu katika 12:16.

Hizi ndizo jozi zilizowasababisha wasomi wa magharibi kumuuliza mwandishi mmojawapo wa Vitabu Vitano vya Kwanza vya Biblia. Majina tofauti ya Uungu na jozi hizi ziliwasababisha kutoa nadharia za waandishi kadhaa/wahariri (angalia mjadala wa Dr. Utley wa utangulizi huu [Uandishi] wa utoaji wa maoni juu ya kitabu cha Mwanzo 1-11, unaopatikana bure mtandaoni katika www. freebiblecommentary.org). Pia tambua mjadala mzuri ulio mfupi katika *Hard Sayings of the Bible*, kr. 118-120.

**20:16 "fedha elfu"** Tafsri zilizo nyingi zina kubali kwamba hili neno "shekeli" linatakiwa kuonekana hapa kwa sababu lilikuwa neno la kawaida lilitumika katika "uzito wa thamani ya chuma" katika Mashariki ya Karibu ya Kale (angalia Mada Maalum katika 18:6). Kuna maandiko mengine kadhaa ambapo yanayodhaniwa lakini hayakuelezwa (kama vile Mwa. 37:28; Jdgs. 17:2,3,4,10).

◙
**NASB, NKJV, "kifunika macho kwako"**
**NRSV "itakayo kutoa katika lawama"**
**TEV "ya kwamba hauna hatia"**
**NJB "umesamehewa kwa ukamilifu"**

Haijulikani kama kuna zawadi nyingine za siri zilizotolewa na Abimeleki, moja kwa Ibrahimu (mst. 14) na moja kwa Sara (mst. 16), ama zawadi moja, thamani ya kifedha ambayo imeelezwa katika mstari huu. Kibinafsi naamini kwamba kuna zawadi mbili tofuti. Hiki kifungu,"kifunika macho kwako" kiuhalisia ni "kwa ajili ya kukufunika macho" (MUUNDO WA MANENO BDB 492 & 744), ambacho ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha kwamba Sara hakuwa na hatia hata kidogo na alizawadiwa ili kuondoa aibu.

**20:17 "Mungu akamponya Abimeleki**" Kwa uhalisia hatufahamu ni ugonjwa gani ambao ulikuwa umempata Abimaleki na watu wa nyumbani mwake, lakini ugonjwa huu ulisababisha ugumu wa kuzaliwa watoto. Kwa uwazi kabisa hii ilikuwa njia moja ambayo Mungu aliitumia kumzuia Abimaleki asiwe na uhusiano na Sara. Pia, kutokana na mist. 17 na 18, tunaona kwamba utasa ulifikiliwa kama laana ya ki-Ungu. Hii ni moja ya sababu aliyokuwa nayo katika wakati mgumu wa kuyaaamini maneno ya Mungu ya neema wakati Sara alipokuwa tasa.

**20:18 "Bwana alikuwa ameyafunga matumbo"** Hiki ni KITENZIJINA HALISI na KITENZI TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 783 & 870), ambacho huchochea tendo la KITENZI.

Kifungu hiki kinaonekana katika sura ya 20 ambapo jina la agano la Uungu, YHWH, linatumika. Katika muktadha (mst. 17) unafanana na *Elohim*. Vitabu Vitano vya Kisamaria na baadhi ya machapisho ya Agano la Kale la Kiebrania yana jina *Elohim.*

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Ibrahimu alimtambulisha Sara kama ndugu yake?
2. Ni kwa namna gani unalielezea hili lililofanyika kwa Sara mara mbili na mara moja kwa Rebeka?
3. Kwa nini ulinzi wa Sara ni wa muhimu sana kithiolojia?

# MWANZO 21

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Isaka anazaliwa | Isaka anazaliwa | Isaka na Ishmaeli | Kuzaliwa kwa Isaka | Kuzaliwa kwa Isaka |
| 21:1-7 | 21:1-7 | 21:1-7 | 21:1-7 | 21:1-7 |
| | | | | (6-7) |
| | Hajiri na Ishmaeli Wanaondoka | | | Kuondoka kwa Hajiri na Ishmaeli |
| 21:8 | 21:8-14 | 21:8-14 | 21:1-8 | 21:8-14a |
| Sara anakwenda Kinyume na Hajiri | | | Hajiri na Ishmaeli wanapelekwa mbali | |
| 21:9-14 | | | 21:9-13 | |
| | | | 21:14-16 | 21:14b-16 |
| 21:15-19 | 21:15-21 | 21:15-19 | | |
| | | | 21:17-21 | 21:17-19 |
| 21:20-21 | | 21:20-21 | | 21: 20-21 |
| Agano pamoja na Abimaleki | Agano pamoja na Abimaleki | Majadiliano ya Ibrahimu na Abimaleki | Makaubaliano kati ya Ibrahimu na Abimaleki | Abrahamu na Abimaleki huko Beer-sheba |
| 21:22-26 | 21:22-34 | 21:25-24 | 21:25-23 | 21:22-24 |
| | | | 21:24 | |
| | | 21:25:34 | 21:25-29 | 21:25-31 |
| 21:27-34 | | | | |
| | | | 21:30-34 | 21:32-34 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21:1-7**

**[1] Bwana akamjia Sara kama alivyonena, na Bwana akamfanyia kama alivyosema. [2] Sara akapata mimba akamzalia Ibrahimu mwana wa kiume katika uzee wake, kwa muhula alioambiwa na Mungu. [3] Ibrahimu akamwita jina lake Isaka, yule mwana aliyezaliwa, ambaye Sara alimzalia. [4] Ibrahimu akamtahiri Isaka mwanawe, alipokuwa mwenye siku nane, kama Mungu alivyomwamuru. [5] Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa miaka mia, alipozaliwa mwana wake Isaka. [6] Sara akasema, Mungu amenifanyia kicheko; kila asikiaye atacheka pamoja nami. [7] Akasema, N'nani angemwambia Ibrahimu, Sara atanyonyesha wana? Maana nimemzalia mwana katika uzee wake.**

◙
**21:1**
**NASB "Bwana akamjia Sara"**
**NKJV "kisha Bwana akamwendea Sara"**
**NRSV "Bwana akashughulika na Sara"**
**TEV "Bwana akambariki Sara"**
**NJB "Bwana Mungu akamtunza Sara kama alivyosema"**

Jina YHWH limerudiwa mara mbili kwa ajili ya msistizo. Mtoto huyu alikuwa kwa uwezo Wake! Hiki KITENZI kiuhalisia ni "akamjia"(BDB 823, KB 955, *Qal* TIMILIFU). Mara nyingi kitenzi hiki kinatumika kumaanisha Mungu yu karibu kwa ajili ya Baraka ama hukumu. Katika maana chanya mtu aweza kuielewa Mwa. 15:24-25 na Kut. 13:19. Hata hivyo, lazima ieleweke kwamba neno hili mara nyingi linatumika katika maana ya hukumu.

◙ **"akamfanyia kama alivyosema**" Kifungu hiki kwa upekee kinaonekana kurejelea Mwanzo 18:10-15. Sara anamzaa (mst. 2; Ebr.11:11 ) mwana wa pekee wa ahadi iliyodokezwa katika ahadi za Mungu kwa Ibrahimu katika sura za 12, 15, na 17.

**21:2 "kwa muhula alioambiwa"** Kifungu hiki kwa upekee kinarejelea 17:21 na 18:10,14. Naamini kwamba hii inarejerea kipindi cha miezi tisa ya kubeba ujauzito.

**21:3 "Isaka"** Jina lake lilitolewa katika 17:19, 21. Hili lilitokana na neno "mchekaji" (BDB 850) na linahusiana na kicheko cha Ibrahimu katika 17:17na kicheko cha Sara katika 18:15.

**21:4 "Ibrahimu akamtahiri Isaka"** Hii ilikuwa ishara ya ahadi iliyoagizwa na YHWH. Hii ilikuwa ikifanyika wakati mtoto alipokuwa na umri wa miaka minane kama Mungu alivyoagiza (kama vile 17:9-14).Kutokana na Mwa. 17:25, Warabu waliliendeleza zoezi la kuwatahiri watoto katika umri wa miaka minane, katika mtiririko wa tohara ya Ishmaeli. Watu wote wa Mashariki ya Karibu ya Kale waliwatahiri watoto wao, lakini kwa umri tofauti na kwa sababu tofauti. Ni Wafilipi na Wahiti peke walikuwa hawatairiwi (yaani sura ya 34).

**21:5** Tena , Umri wa Ibrahimu (kama vile 17:17) unaonyeshwa ili kuonyesha Neema ya Mungu katika ahadi Yake, si nguvu au juhudi za mwanadamu.

**21:6** Kuna neno la kimasikhala juu ya

1. Umri wa Ibrahimu na umri wa Sara ulitia shaka kuhusu wokovu wa Bwana katika 17:17 na 18:12 kwa kicheko
2. Mtoto aliitwa "kicheko"

3. Kicheko kilikuwa ni ishara ya furaha ya nje ya Sara, hatimaye kuwa na mwana wake mwenyewe na watu wakampongeza kwa kucheka naye
4. mchekaji anatumika katika namna iliyo hasi katika mst. 9 ambapo Hajiri anakuwa na mtazamo tofauti kumhusu Isaka

**21:7 "Sara atanyonyesha wana"** Hili neno "wana" ni WINGI. Kiebrania pia kina wingi usiotarajiwa. Lazima hii iwe njia ya kuonyesha (1) mambo yajayo katika jozi (macho, masikio, mikono) na (2) uweza (yaani, WINGI WA KIFALME).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21:8-14**

**[8] Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya; Ibrahimu akafanya karamu kuu siku ile Isaka alipoachishwa kunyonya. [9] Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. [10] Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. [11] Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. [12] Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa. [13] Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyu naye ni uzao wako. [14] Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba.**

**21:8 "Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya**, **Ibrahimu akafanya karamu kuu**" Tunaelewa kutokana na fasihi ya siku zile kwamba kulikuwa na utaratibu wa kufanya karamu iliyofanyika wakati wa kumwachisha mtoto kunyonya (yaani, kiasi cha kuhakikisha kwamba angeishi). Kuachishwa huku kungekuwa katika umri wa miaka miwili au mitatu (kama vile II Mak. 7:27).

**21:9 "Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri**, **ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka"** Toleo la NKJV lina neno "dharau," ambapo Tafsri za NRSV na TEV zina neno "kejeli." Agano la Kale la Kiebrania linaoneza kifungu "akichaze na mwanae." Hili neno la Kiebrania linamanisha "mchekaji" (BDB 850), lakini katika shina la neno *Piel* (KB 1019) neno hili linaweza kumaanisha "kutania ama masihara" (kama vile 19:14; Kut. 32:6; Amu. 16:23), lakini kwa sababu ya Gal. 4:29, na kwa sababu ya dhihaka za Hajiri katika 16:4,5, huenda hili linamaanisha "kudhihaki" au "kuleta upinzani." Walimu wa Kiyunani wanainukuu II Sam. 2:14na Mit. 26:19 kama mifano ya matumizi hasi ya neno hili.

**21:10 "Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe"** KITENZI hiki *Piel* ni neno jingine (BDB 176, KB 204) na ni KAULI SHURUTISHI (kama vile Gal. 4:30). Kulingana na vigae vya Nuzi, hili lilikuwa tendo haramu. Hata hivyo, kutokana na kumbukumbu za awali za kisheria ziitwazo "*Lipit-ishtar"* kwa vyo vyote kushiriki urithi ama kuwapa uhuru wao ilikuwa njia ya kisheria kuwahudumia watoto wa nje ya ndoa.

**21:11** Ibrahimu alimpenda Ishmaeli (kama vile 17:18), kama afanyavyo YHWH (kama vile 17:20; 21:3,18,20). Ibrahimu alishindwa kutoa dai hili kwamba Sara hakuwa sahihi na huenda pia alikuwa amekosea (kama vile Hes. 11:10; I Sam. 1:8).

**21:12** Mungu alimpa Ibrahimu masharti mawili.
1. "Neno hili lisiwe baya machoni pako," BDB 949, KB 1269, *Qal* KAULI SHURUTISHI inatumika katika maana ya KUSHURUTISHA. Hiki KITENZI kinatumika katika mst. 11 kuelezea mwitikio wa Ibrahimu wa ombi la Sara (amri).
2. "sikiliza sauti yake," BDB 1033, KB 1570, *Qal* SHUTUTISHI "sikia").

◙ **"Kila akuambialo Sara"** Katika kifungu hiki inamaanisha kwamba Mungu alikubaliana na hali ya makadirio haya. Hili halimaanishi kwamba mtazamo wa Sara ulikuwa sahihi. Hata hivyo, kwa upande mwingine, hatuifahamu hali kwa ukamilifu. Labda, yu kama Rebeka (baadae katika sura ya 27), alikuwa akijaribu kuilinda ahadi ya agano.

**21:13 "maana huyu naye ni uzao wako"** Mungu alimbariki Ishmaeli kwa sababu ya babaye, Ibrahimu. Maisha yake yanaelezwa katika unabii katika 16:11-12. Uhusiano wa Ishmaeli kwa Ibrahimu ulikuwa chanzo cha Baraka zake kama alivyokuwa Lutu katika 19:29.

**21:14 "kiriba cha maji"** Neno hili (MUUNDO WA SENTENSI BDB 332 na BDB 565) linapatikana katika sura hii pekee katika Agano la Kale (kama vile mst. 14,15,19). Hili linarejelea juu ya ngozi ya kondoo au tumbo la kondoo, ililoshonwa kwa namna ya kuwekea maji. assess

◙ **"akimtwika begani pake"** Agano la Kale la Kiebrania na toleo la ki-Shamu linakitafsri kifungu hiki kwa namna hii kwamba, pia walimweka Ishmaeli mgongoni mwake. Kutokana na muktadha inaonekana kwamba Ishmaeli lazima alikuwa na umri kati ya 15 na 17, alikuwa mzito sana kubebwa na mamaye, hivyo, huenda hii ni nahau ya kujiandaa na safari.

◙ **"akapotea katika jangwa la Beer-sheba**" Tazama mstari wa 31

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21:15-19**

**[15] Yale maji yakaisha katika kiriba, akamlaza kijana chini ya kijiti kimoja. [16] Akaenda akakaa akimkabili, mbali naye kadiri ya mtupo wa mshale; maana alisema, Nisimwone kijana akifa; naye akakaa akimkabili, akapaza sauti yake, akalia. [17] Mungu akasikia sauti ya kijana. Malaika wa Mungu akamwita Hajiri kutoka mbinguni, akamwambia, Una nini, Hajiri? Usiogope, maana Mungu amesikia sauti ya kijana huko aliko. [18] Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa. [19] Mungu akamfumbua macho, naye akaona kisima cha maji; akaenda akakijaza kiriba maji, akamnywesha kijana**.

◙
**21:15**
**NASB, TEV "akamlaza"**
**NKJV "akamweka"**
**NRSV "akamrusha"**
**NJB "akamwacha"**

Hili neno (BDB 1020) linadokeza kuacha (Kut. 1:22; Isa. 71:9; Yer. 38:6,9; Eze.16:5), ambako kunapelekea mauti**.**

**21:16 "mbali"** Hiki KITENZI adimu (BDB 377, KB 373, *Polel* ENDELEVU) kinapatikana hapa katika kitabu cha agano la Kale.

◙ **"akapaza sauti yake, akalia"** Kuna baadhi ya mkanganyiko katika andiko lililo hapa kwa sababu Malaika wa Bwana alisema kuwa amemsikia kijana akilia na ni sauti ya mwanamke pekee inayotajwa. Hata hivyo, yatupasa kukumbuka kwamba huu ni ufupisho tu wa hali na tendo zima halikuwekwa humu. Malaika wa Bwana akamwambia tena Hajiri kama alivyofanya katika l6:6 na kuendelea jambo ambalo linaonyesha upendo wa Mungu kwa wale waliokuwa na uhusiano pembeni na Ibrahimu .

**21:17-18** Mungu anamwambia Hajiri.
1. "Una nini?" (hakuna KITENZI)
2. "Usiogope," BDB 431, KB 432, *Qal* ISIO TIMILIFU inatumika kama KAULI YENYE KUSIHI, kama vile yenye mzizi sawa katika15:1; 26:24;46:3

3. “Ondoka,” BDB 877, KB 1086, *Qal* YENYE MASHARTI
4. “ukamwinue kijana,” BDB 669, KB 724, *Qal* YENYE MASHARTI
5. “ukamshike mkononi mwako,” BDB 304, KB 302, *Hiphil* YENYE MASHARTI, jambo hili linamaanisha tendo la kumjali, kumstawisha.

**21:17** Pia tambua jinsi gani *Elohim* na Malaika wa Bwana wanavyotolewa ufafanuzi (yaani, wanazungumza toka mbinguni), hata hivyo walikuwa na umbali (kama vile Kut. 3:2; 4). Tazama Mada Maalum: Malaika wa Bwana katika 12:7.

◙ **“maana Mungu amesikia”** Hili neno la kimzaha la jina la Ishmaeli (kama vile 16:11). Hiki KITENZI “amesikia” (BDB 1033),“Ishmaeli” (BDB 1035), na “Mungu amesikia” yote haya yanatoka katika mzizi ule ule.

**21:18 “kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa”** Hiki KITENZI (BDB 962, KB 1321, *Qal* YENYE MASHARTI) kinamaanisha “kuweka utaratibu” au “kuweka sehemu fulani,” kama vile 21:13; 46:3. Hiki si KITENZI kile kile (BDB 793, KB 889, *Qal* CHENYE MASHARTI kilichotumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUSIHI) kilichotumika katika ahadi ya HWH kwa Ibrahimu katika 12:2 ama 18:18 (BDB 224, KB 243, kama *Qal* KITENZIJINA HALISI).

**21:19** Mtu anashangaa kama mst. 19 ni muujiza wa wenye kuonekana kwa macho ama ni utoaji wa maji ya chanzo cha maji kilichokuwepo.Neneo hili hili linatumika katika Mwa. 3:5 na II Fal. 6:15-19.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21: 20-21**

[20] **Mungu akawa pamoja na huyo kijana, naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde.**
[21] **Akakaa katika jangwa la Parani; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri.**

**21:20** Hii sitiari “Mungu akawa pamoja na” pia inatumika juu ya Yakobo (Mwa. 28:15) na Yusufu (Mwa. 39:2,3,21). Hii inaeleza juu ya mapenzi binafsi ya YHWH na uwepo wake (elewa 21:22). Ishmaeli alishiriki katika Baraka za Ibrahimu!

**21:2 “mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri”** Ni wazi kuwa hili lilimaanisha kuwa tendo hili lilipaswa kufanywa na baba, lakini katika namna hii Hajiri alimchagulia mke Ishmaeli kutoka kwa watu wake mwenyewe.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21: 22-26**

[22] **Ikawa wakati ule Abimeleki, na Fikoli mkuu wa jeshi lake, wakamwambia Ibrahimu, wakinena, Mungu yu pamoja nawe katika yote unayotenda.**
[23] **Basi sasa uniapie kwa Mungu, ya kuwa hutanitenda hila, wala mwanangu, wala mjukuu wangu, lakini kwa kadiri ya fadhili niliyokutendea utanitendea mimi, na nchi hii ambayo umetembea ndani yake.**
[24] **Ibrahimu akasema, Nitaapa.**
[25] **Kisha Ibrahimu akamlaumu Abimeleki kwa sababu ya kisima cha maji ambacho watumwa wa Abimeleki wamekinyang'anya.**
[26] **Abimeleki akasema, Mimi sijui ni nani aliyetenda neno hili, wala hukuniambia, wala sikusikia habari hii ila leo tu**.

**21:22 “Abimeki na Fikoli”** Haya majina mawili yanayofanana yanatajwa katika Mwa. 26:26 katika uhusiano na Isaka na matatizo ya jambo hili yanafanana sana na ya huko Beer-sheba. Haya majina ni majina ya jumla ya mfalme na kiongozi mkuu, watu hawa kwa ukweli waliishi kipindi kirefu, ama kumekuwa na mkanganyiko katika andiko la Kiebrania la kitabu cha Mwanzo (yaani, wahariri).

◙ **“Mungu yu pamoja nawe katika yote unayotenda”** Hili halikusemwa juu ya Ibrahimu, bali pia juu ya Isaka (kama vile Mwa. 26:28).

**21:25 "Kisha Ibrahimu akamlaumu Abimeleki"** Hapa neno linaonekana kuwa "karipia" (BDB 406, KB 410, *Hiphil* KITENZI TIMILIFU). Mgogoro juu ya visima ulikuwa wa kawaida katika maeneo haya ya eneo la nusu jangwa. Jibu la Abimeleki linaonyesha kwamba bado alikuwa hajalitambua tatizo na bado alihitaji kufafanua agano pamoja na Ibrahimu ("kuapa," BDB 989, KB 1396, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, mst. 23).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21: 27-34**

**[27] Ibrahimu akatwaa kondoo na ng'ombe akampa Abimeleki, na hao wawili wakafanya mapatano. [28] Ibrahimu akaweka wana kondoo wa kike saba peke yao. [29] Abimeleki akamwambia Ibrahimu, Hawa wana kondoo wa kike saba, uliowaweka peke yao, maana yake nini? [30] Akasema, Hawa wana kondoo wa kike saba utawapokea mkononi mwangu, wawe ushuhuda ya kuwa ni mimi niliyekichimba kisima hiki. [31] Kwa hiyo akapaita mahali pale Beer-sheba, kwa sababu waliapa huko wote wawili. [32] Basi wakafanya mapatano huko Beer-sheba. Abimeleki, na Fikoli mkuu wa jeshi lake, wakaondoka wakarudi hata nchi ya Wafilisti. [33] Ibrahimu akapanda mkwaju huko Beer-sheba, akaliitia huko jina la Bwana Mungu wa milele. [34] Ibrahimu akakaa hali ya ugeni katika nchi ya Wafilisti siku nyingi.**

**21:27 "hao wawili wakafanya mapatano"** Kwa udhihirisho kabisa, wanyama wa mst. 27 walikuwa wakichinjwa nusu kwa nusu ili kufanya agano (angalia Mada Maalum: Agano katika 13:14).

**21:28 "wana kondoo wa kike saba"** Ni dhahiri kwamba hili ni kundi lililotengwa kutoka katika mst. 27, kwa uwazi kabisa liko katika uhusiano na Beer-sheba. Hili jina "Beer-sheba" linatokana na asili mbili : (l) "visima saba," 21:28 au (2) "ukubwa wa ahadi" katika 26:33 ("saba" [BDB 987] na "kuapa" [BDB 989] ni sawa katika Waebrania).

**21:32"Wafilisti"** Watoa maoni wengi wanatoa hoja kwamba kwa wakati huo Wafilisti walikuwa hawajaingia katika nchi hii kwa idadi kubwa. Ijapokuwa hili ni la kweli kabisa, asili ya watu hawa wa Aegean wenye kupigana vita inaonyesha kwamba walikuwa katika eneo hili kwa idadi ndogo kabla ya karne 12 K.K. kutokana na hili ndipo walipoishi hapa baada ya kuzuiwa kuingia Misri. Pia inawezekana kwamba hili ni kosa la mambo ya kale.

**21:33 "akapanda mkwaju"** Jambo hili liliashiria mambo mawili.

1. Kuwepo kwa maji chini ya ardhi ambayo mara nyingi yalihusiana na sehemu zilizowakifishwa (Mungu alimpa maji Hajiri, Ishmaeli, na pia Ibrahimu).
2. Ibrahmu, mhamajihamaji, aliyekuwa na mpango wa kukaa hapa kwa kipindi kirefu.

◙ **"akaliitia huko jina la Bwana"** Hili ni jina la agano la Uungu, YHWH (BDB 42). Jambo hili linamaanisha muundo wa kuabudu (kama vile 4:26; 12:8). Hili ni sawa na lile alilolifanya Nuhu katika Mwa. 8:20.

◙ **"Mungu wa milele"** Hili jina Mungu linapatikana hapa pekee. Jina hili linaundwa na maneno ya Kiebrania *El* (BDB 42) na*'olam* (BDB 761). Hili neno *El* limeunganishwa na majina mengine kadhaa katika vipengele vya kale vya kitabu cha Mwanzo ili kuonyesha asili ya Mungu: (1) *El Shaddai* (BDB 42 na 994), 17:1; 43:14 na kitabu cha Kutoka 3; (2) *El Elyon* (BDB 42 na 751 II), 14:18-24; (3) *El Roi* (BDB 42 na 909), 16:13; (4) *El Bethel* (BDB 42 na 110),31:13; 35:7. *El* lilikuwa jina la Mungu la jumla katika Mashariki ya Karibu ya Kale (tazama Mada Maalum katika 12:1).

Jina *'olam* (BDB 761) linamanisha "kilichofichika" na kwa vyovyote linarejelea wakati uliopita au ujao. Hili linatumika katika maana ya "milele," lakini maana hii kwa upekee lazima ibainishwe kutokana na muktadha (tazama Mada Maalum katika 13:14).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Sura ya 20 ni maoni hasi kuhusu Ibrahimu?
2. Abimeleki pia alimfahamu Adonai?
3. Kwa nini Abimeleki alimtwaa Sara kama mkewe wakati alikuwa mkongwe sana na ambaye alijieleza kama "mwanamke mwenye kuhangaika" (kama vile 18:12)?
4. Je! Neno "nabii" linamaanisha nini na ni kwa namna gani Ibrahimu anaendena na sifa ya wadhifa huu?
5. Orodhesha sababu tatu ambazo Ibrahimu alizitoa katika mist. ya 11-13 za kujaribu kumdanganya Abimaleki.
6. Kwa nini Sara alidai Hajiri na Ishmaeli waondoke?

# MWANZO 22

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Matoleo ya Isaka | imani ya Ibrahimu Inathibitika | kujaribiwa kwa Ibrahimu | Mungu anamwamuru Ibrahimu kumtoa Isaka | sadaka ya Ibrahimu |
| 22:1-8 | 22:1-2 | 22:1-8 | 22:1 | 22:1-2 |
| | | | 22:2 | |
| | 22:3-8 | | 22:3-5 | 22:3-5 |
| | | | 22:6-7a | 22:6-8 |
| | | | 22:7b | |
| | | | 22:7c | |
| | | | 22:8 | |
| 22:9-14 | 22:9-14 | 22:9-14 | 22:9-11a | 22:9-10 |
| | | | 22:11b | 22:11-14 |
| | | | 22:12 | |
| | | | 22:13-14 | |
| 22:15-19 | 22:15-19 | 22:15-19 | 22:15-19 | 22:15-18 |
| | | | | 22:19 |
| | Familia ya Nahori | Uzao wa kaka wa Ibrahimu, Nahori | Uzao wa Nahori | Uzao wa Nahori |
| 22:20-24 | 22:20-24 | 22:20-24 | 22:20-24 | 22:20-24 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 22:1-8**

**[1] Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi**
**hapa. [2] Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi**
**ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. [3] Ibrahimu**
**akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na**
**Mungu. [4] Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali. [5] Ibrahimu akawaambia**

**vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena. [6] Basi Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake, wakaenda wote wawili pamoja. [7] Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? [8] Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.**

**22:1 "Mungu"** Hili ni neno la Kiebrania *Elohim.* Hili ni moja la jina lililozoeleka la majina ya Mungu ambalo linapatikana katika kitabu cha Mwanzo. Hatuna uhakika na asili yake, lakini kwasababu ya mzaha wa maneno yanayopatikana katika Mwanzo 31:29, Inaonekana kuhusiana na tungo "jitie nguvu." Taaluma ya ukosoaji ya karne ya 18 na 19 imetumia maneno kama *Elohim* na YHWH, yanayopatikana katika sehemu mbali mbali za sura za kitabu cha Mwanzo, kupendekeza hati ya madhanio ya vyanzo kadhaa. Hata hivyo walimu wa kiyahudi wanasema kwamba utofauti kati ya majina haya unapatikana katika tabia ya Mungu ambayo inawakilishwa. *Elohim* inawakilisha nguvu ya Mungu na kujali kama Muumbaji, wakati YHWH inawakilisha rehema za agano la Mungu. Mimi nafikiria maelezo ya kiualimu ni ya kupewa upendeleo.

◙ **"Ibrahimu anajaribiwa"**

## MADA MAALUMU: MUNGU HUWAJARIBU WATU WAKE (AGANO LA KALE)

Neno "jaribu" (BDB 650, KB 702, *Piel* kauli ya wakati uliopo; Mwa. 22:1) ambalo linatumika katika namna ya "kufanya jaribio." Linatumika katika namna ya kumleta mtu katika sehemu ambapo wanatambua na kufanyia kazi vipaumbele vyao walivyojiwekea wenyewe. Ni wazi kutoka Mwanzo 12 mpaka 22 kwamba Mungu anampatia Ibrahimu mfululizo wa mazingira (walimu wa kiyahudi wanasema ni kumi) ili aweke shabaha ya upendo wake na tumaini katika Mungu na Mungu tu (yawezekana pia Ayubu). Majaribu haya hayakuwa sana kwa ajili ya Mungu, lakini kwa ajili ya Ibrahimu na uelewa wake kwa Mungu aliyemuita kutoka Uru ya Wakaldayo. Ibrahimu anaamriwa aache familia yake, nyumba, marafiki, urithi, desturi na hata maisha yake ya baadaye (mwana wake aliyehaidiwa katika Mwanzo 22) kumfuata Mungu kwa Imani. Mungu anawajaribu watoto wake wote katika eneo la vipaumbele vyao (kama vile Mt. 4: na kuendelea; Ebr. 5:8; 12:5-13).

Mungu anajaribu (BDB 650) ili aweze kujua (BDB 393; angalia Mada Maalumu: Kujua). Israeli mara kwa mara walimjaribu Mungu kwa kutotii kwao na Mungu alithibitisha kuwa kweli kwa neno lake. Sasa Mungu atawapa Israeli na watu wake nafasi ya kuonesha uaminifu wao unaotajwa na imani.

1. Mungu aliwajaribu watu wake kwa pamoja
   a. Kutoka 15:25; 16:4; 20:20
   b. Kumbu kumbu la Torati 8:2,16; 13:3
   c. Waamuzi 2:22; 3:1,4
2. Mungu aliwajaribu Waisraeli mmoja mmoja
   a. Ibrahimu, Mwanzo 22:1-12
   b. Hezekia, 2 Nyakati 32:31
3. Waandishi wa Zaburi wanalia kwa Mungu kuwajaribu ili aondoe uchafu uliojificha (kama vile Zab. 26:2; 139:23)
4. Watu wa Mungu wa Agano Jipya pia wanajaribiwa, kama ilivyokuwa kwa Yesu (Mathayo 4; Luka 4; Ebr. 5:8). Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani kwa Kujaribiwa na Visawe Vyake.

◙**"akamwambia"** Sura hii ni mfuatano wa mazungumzo kati ya mtu na mtu. Tazama mara ambazo "akasema/akamwambia" (BDB 55, KB 65) zinatumika, kufasiriwa katika njia kadhaa.

1. Mstari wa 1, mbili
2. Mstari wa 2, mbili
3. Mstari wa 3, moja
4. Mstari wa 5, moja
5. Mstari wa 7, nne
6. Mstari wa 8, moja
7. Mstari wa 9, moja
8. Mstari wa 11, mbili
9. Mstari wa 12, moja
10. Mstari wa 14, moja
11. Mstari wa 16, moja
12. Mstari wa 20, moja

◙**"Ibrahimu"** Mungu alibadilisha jina lake kutoka Abramu, ambalo linamaanisha "baba aliyetukuzwa," kuwa Ibrahimu, linalomaanisha "baba wa mataifa/wa wengi." Mungu anataka kumuuliza swali Ibrahimu kufanya kitu fulani ambacho kinaweza kuhatarisha jina lake la sasa! Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani inaweka mara mbili hotuba ya Mungu kwa Ibrahimu, lakini maandiko ya Kiebrania yana moja tu "Ibrahimu" katika mstari wa 1, wakati ina mara mbili katika mstari wa 11.

◙ **"Mimi hapa"** Hii ni nahau ya kiebrania juu ya upatikanaji (kama vile mstari wa 11; Kut. 3:4; I Sam. 3:4; Isa. 6:8).

**22:2** Tazama mfululizo wa amri zinazotolewa kwa Ibrahimu juu ya Isaka.

1. "mchukue mwanao sasa," BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "Nenda katika nchi ya Moria," BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI (inafurahisha kuona kwamba hiki KITENZI katika muundo huu kinapatikana hapa tu na Mwanzo 12:1, ambacho kinaunganisha majaribu haya mawili kama ahadi na kutimilizwa [pia tazama 18 na 12:3])
3. "mtoe yeye hapa," BDB 748, KB 828, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

◙ **"Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka"** Hii inaonekana kuwa mfufulizo wa tungo yenye makusudi inayomrejerea hasa Isaka kama mwana maalumu wa ahadi. Pia tazama mwana wa "pekee" (BDB 402) (kama vile mistari ya 2,12,16). Ishmaeli hakuwa mwana wa ahadi na alikuwa amekwisha fukuzwa mbali! Tumaini lote la Ibrahimu kwa ajili ya uzao liko ndani ya kijana huyu wa kiume na YHWH anamuelekeza amtoe kama dhabihu!

◙ **"mpaka nchi ya Moria"** Neno hili (BDB 599) limefasiriwa katika njia nyingi.

1. Toleo la Kilatini na Vitabu vitano vya Musa vya Kisamaria vina "maono"
2. Toleo la Targums linafasiri hii kama "kuabudu"
3. Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani "kuu"
4. Toleo la Kishamu lina "ya Waamoni"
5. baadhi ya wanazuoni wanalifasiri kama "kuoneshwa na YHWH"
6. wengineo "wateule"
7. bado wengine "sehemu ya kutokezea"

Inaonekana kwamba "mahali/sehemu ya kutokezea" inaweza kuwa fasiri njema zaidi yenye uwezekano iliyojikita katika matumizi mengine ya neno hili katika II Nyakati. 3:1, ambayo yanataja kwamba Hekalu lilijengwa juu ya mlima Moria, mahali ambapo Mungu alimtokea Daudi. Hii inaweza aidha kumaanisha II Sam. 24:16 au zaidi yawezekana, I Nyakati 21:18-30. Kutajwa kwa sadaka ya Isaka ya Ibrahimu katika muktadha huo aidha umeondolewa kwasababu ilikuwa inajulikana sana au haikuwa inajulikana kwa mwandishi wa 1 Nyakati. Pia Moria inaonekana kufanana na mji wa Melkizedeki, Salemu (14:18), baadaye ukaitwa Yebusi ambao ulifanyika Yerusalemu.

◙ **"sadaka ya kuteketezwa"** Hili ni neno la Kiebrania "maangamizi makuu" inayomaanisha "sadaka ya kuteketezwa moja kwa moja" (BDB 750). Sio tu kwamba ilijumuisha ibada za kuchinja Koromeo lake. Ni amri gani hii ya kushangaza kutoka kwa Mungu aliyemuhaidi mtoto wa kiume na kumsababisha yeye kumpeleka Ishmaeli

mbali! Ibrahimu lazima amtumaini Mungu bila uelewa sawa sawa na Hesabu 21 tukio linaloelezewa katika Yohana 3:14.

**22:3 "Ibrahimu akaondoka alfajiri"** Tazama kwamba hakuna kusitasita au kuuliza uliza upande wa Ibrahimu kulikoandikwa, lakini ni usiku mbaya kiasi gani aliokuwa nao. Ikiwa huku kuondolewa au ishara ya ukuaji wa imani ya Ibrahimu haina uhakika. Ibrahimu kwa hakika sio mkamilifu, lakini ukuu wa tumaini lake katika Mungu unaweza kuonekana katika masimulizi haya. Haya yalikuwa mazingira ya jaribu la tumaini.

**22:4 "Siku ya tatu"** Umbali kati ya Beersheba na Mlima Moria ni kama mwendo wa siku mbili na nusu lakini kwa farasi na vitu vingine, ingeweza kuwa imechukua zaidi.

**22:5** Tazama amri kwa watumwa wake na maelezo ya kusudio lake.

1. "kaa hapa," BDB 442, KB 444, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "mimi na kijana tutakwenda mbele zaidi," BDB 229, KB 246, *Qal* HALI YA KUSIHI
3. "tutaabudu," BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* HALI YA KUSIHI
4. "tutarudi kwenu," BDB 996, KB 1427, *Qal* HALI YA KUSIHI

◙**"tukaabudu, na kuwarudia tena"** Imani ya Ibrahimu katika Mungu ni thabiti kwamba Ebr. 11:17-19 inadhania kwamba Isaka atafufuliwa kutoka kwa wafu na ikiwezekana kwa ajili ya kumsindikiza Ibrahimu kurudi nyumbani kwao. Hii iko sambamba na ahadi ya Mungu iliyotangulia kwa Ibrahimu katika 21:12 kwamba Ibrahimu angekuwa na uzao kupitia Isaka. Ingawa Ibrahimu hakuelewa ni kwa namna gani au ni kwanini, ni hakika alijua na kuelewa kwamba Mungu ana uweza.

**22:6 "Basi Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe;"** Kuna uambatani mwingi kati ya nini kinatokea kwa Isaka na nini kinatokea baadaye kwa Yesu. Kibinafsi nafadhaika kuhusu istiari yoyote na muainisho ambao hautajwi kibayana katika Agano Jipya kwasababu ya kiasi gani limekuwa likitumiwa vibaya na wafasiri kwa nyakati zote za maisha ya kanisa. Kuna maelezo ya kiuwazi kati ya Isaka na Yesu. Kitu ambacho Mungu asingeruhusu Ibrahimu kufanya kwa Isaka, Alikifanya yeye mwenyewe kwa Mwanawe wa Pekee. Nafikiria tunaweza kuelewa kitu fulani juu ya uzito wa upendo wa Mungu wakati tunapohisi kwa upendo na imani ya Ibrahimu.

◙ **"akatwaa moto na kisu mkononi mwake"** Ikiwa moto huu unamaanisha makaa yaliyobaki kutokana na kambi ya kuota moto wa jana yake au kimkoba kidogo cha mawe na muwako haijulikani. Kisu ni neno kwa ajili ya "kisu cha mchinjaji" (BDB 38), kisu kikubwa sana ambacho kilikuwa kinatumika kwa ajili ya kupikia (kama vile Waamuzi 19:29; Mithali. 30:14).

**22:7 "lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?"** Swali la Isaka lazima liliukata moyo wa Ibrahimu, ambapo Ibrahimu anaelezea imani yake kwa Mungu kwa uzuri katika mstari wa 8. Ule ukweli kwamba Isaka alikuwa anauelewa juu ya sadaka inaonesha kwamba mfumo wa kidhabihu unatangulia kabla ya utungwaji wa Sheria ya Musa. Hii inaweza kuonekana (1) kwa Kaini na Habili (Mwanzo 4); (2) kwa Nuhu (Mwanzo 8:20); na (3) kwa Ayubu (Ayubu 1:5).

**22:8 "Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka"** Tungo "Mungu atajitwalia" baadaye inakuwa jina kwa ajili ya Mungu katika mstari wa 14 ("YHWH," BDB 217 na "kuona," BDB 906). Tumeona namna gani ilivyozoeleka kwa matendo ya Mungu kupelekea katika jina jipya kuelezea tabia yake na matendo yake. Neno la Kiebrania "atajipatia" hakika ni "tutaona/tutaliangalia hilo" (BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU), lakini ilikuja kutumika katika maana ya kiutaalamu (Yule aonaye ni Yule atakayetoa).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 22:9-14**

[9] **Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni,**

**kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni. [10] Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. [11] Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. [12] Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. [13] Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. [14] Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire,kama watu wasemavyo hata leo,Katika mlima wa BWANA itapatikana.**

**22:9 "Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu"** Tunaona kitu fulani, sio tu imani kubwa ya Ibrahimu, lakini imani kubwa ya Isaka. Inavyoonekana Isaka alikuwa na umri wa kutosha wa kuweza kubeba kuni mpaka juu ya mlima na alikuwa na uwezo wa kupinga kukamatwa na kufungwa kamba. Ninao uhakika kwamba tukio hili lilisababisha masaa ya mjadala wa kidini baadaye kati ya Ibrahimu na Isaka.

KITENZI "mfunge" (BDB 785, KB 873, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO KAMILIFU) kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale. Mzizi ule ule (BDB 785) unamaanisha kuinamishwa na kugeuzwa. Hivyo inadhaniwa ni kugeuza na kukunja mnyama wa kudhabihu ilikuwa ni namna ya kuweza kufunga miguu yake kwa pamoja.

**22:10 "Ibrahimu akanyosha mkono wake"** Hii inavyoonekana inamaanisha matendo ya kiibada ya kuchinja koromeo la mnyama anayetolewa dhabihu.

**22:11 "Ndipo malaika wa Bwana"** Hii ni wazi tunaposoma mistari ya 11 na12 kwa pamoja kwamba huyu "malaika wa BWANA" ni kumpa Mungu sifa za kibinadamu (kama vile Mwanzo 16:7-13; 18:1; 19:1; 21:17, 19; 22:11-15; 31:11, 13; 32:24, 30; 48:15-16; Kut. 3:2, 4; 13:21; 14:19; Waamuzi 6:12, 14; na Zek. 3:1, 2). Lakini, tazama katika mstari wa 12 malaika anamaanisha "Mungu." Ni vigumu kukubali hali ya mkazo ya kuabudu Mungu mmoja (yaani "Roho" katika Mwanzo 1:2; "Na tu…." Katika Mwanzo 1:26; 3:22; 11:7; "Malaika wa BWANA juu" na pia tambua na "BWANA amwambia Bwana wangu" katika Zab. 110:1). Namna gani mambo haya yote yanaingiliana ni siri/ajabu. Wakristo hukiri, pamoja na Wayahudi, hali ya kuabudu Mungu mmoja inaelezewa katika Kumb. 6:4. Angalia Mada Maalumu: Utatu katika 20:13.

**22:12** Kuna amri hasi mbili

1. "usiinue mkono wako juu ya kijana," BDB 1018, KB 1511, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini ikitumika katika namna ya KITENZI AMRISHI
2. "usimfanyie chochote," BDB 793, KB 889, *Qal* KITENZI AMRISHI

KAULI ZA WAKATI TIMILIFU zifuatazo zinaonesha kwamba YHWH ameridhishwa kikamilifu na tumaini na imani ya Ibrahimu kwake.

1. "kwakuwa sasa najua," BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. "kwakuwa haukunizuilia mwanao," BDB 362, KB 359, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Tungo  za kujirudia rudia zinazommaanisha Isaka zinapatikana katika mstari wa 2 na kurudiwa katika mstari wa 12 (kama vile mstari wa 16).

Hili neno kuhusu "sasa najua." Je hii inaweka maswali juu ya uweza wa YHWH kuelewa kitu kabla hakijatokea au hii ni njia tu ya kifasihi ya kuonesha uthibitishwaji wa imani ya Ibrahimu? Naielewa kwa namna ya pili. Siko na utulivu juu ya imani kwamba Mungu yupo na ni muumba na mtawala wa dunia ya Wazi.

◙

**NASB, NKJV**

| | |
|---|---|
| **NRSV, NJB** | **"hofu"** |
| **TEV** | **"heshima"** |
| **Peshitta** | **"adhama"** |
| **REB** | **"mtu mwenye hofu ya Mungu"** |

Neno hili (BDB 431) linatokea mara kwa mara katika Agano la Kale. Linaweza kumaanisha "hofu" (kama vile Mwanzo 3:10; 18:15; 20:8; 28:17; 32:7; 42:35; 43:18), lakini kwa muktadha fulani "heshima," "adhama," au "tukuza" wakati wa kuelezea mtazamo wa mwanadamu juu ya uungu. Tazama maandiko yafuatayo: Mwanzo 42:18; Kut. 1:17; 9:30; 18:21; Law. 19:14,32; 25:17,36,43; Kumb. 6:2,24; 10:12,20; 14:23; 17:19; 25:18; 28:58; 31:12-13; Zab. 33:8. Hii "hofu" inatakiwa itoke wakati wa kuabudu na utii. Ni mtindo wa maisha ya kimahusiano, na sio jozi za matukio yaliyojitenga, maeneo, matamko, au sheria. Utii utiririke kutoka katika heshima na upendo, sio hofu na ulipizaji visasi. Kutotii kimsingi ni kinyume na upendo, lakini pia kama sheria! Uhusiano wa mtu na Mungu lazima ufanyike kuwa kipaumbele kwenye maisha! Ile "Ibrahimu alimwamini Mungu" (Mwanzo 15:6) imekwisha kuoneshwa katika maisha!

◙

**22:13**

| | |
|---|---|
| **NASB, RSV** | **"nyuma yake kondoo dume"** |
| **NKJV** | **"na tazama nyuma yake kuna kondoo dume"** |
| **NRSV, TEV** | **"kondoo dume"** |

Kuna utofautiano wa maandiko ya kiebrania katika hatua hii. Toleo la MT lina KIELEZI "nyuma" (אחו BDB 29), lakini baadhi ya maandiko ya Kiebrania na vitabu vitano vya Musa vya Kisamaria, Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani, na Peshitta yana "moja" (אחד BDB 25), inafasiriwa kama " kondoo dume".

◙**"badala ya mwanawe"** Mungu hakuuliza Ibrahimu kutoa sadaka ya kondoo dume, lakini Ibrahimu kwa niaba yake yeye mwenyewe na shukrani, alimtolea kwa Mungu juu ya mlima na kwamba siku moja ingekuwa mahali/pahala pa Hekalu la Suleimani. Hii inaweza kuwa muundo wa kuanzisha dhabihu kama tendo mbadala ambalo baadaye linakuzwa, sio tu katika Utungaji wa sheria ya Musa lakini pia kiukubwa kupita vyote, dhabihu ya Kristo (kama vile Isaya 53 na Yohana 1:29; kitabu cha Waebrania; I Pet. 1:18-19; Ufu. 5:11-14).

**22:14 "kama ilivyo hata leo"** Hii inaweza kuwa alama ya kifasihi ya mhariri wa baadaye. Inawezekana ilikuwa hata Musa, au mwandishi wa kikuhani wa Musa. Mimi binafsi ninafikiria kwamba zidi ya Mwanzo mpaka kwa siku za Yusufu, kutoka uongozi wa mababa wa iamani kwa njia ya mdomo au desturi zilizoandikwa.

◙**"Ibrahimu akapaita mahali hapo BWANA atatoa"** Hii inaonekana kujikita juu ya tendo la Mungu na jibu la Ibrahimu kwa Isaka katika mstari wa 8.

◙**"Katika mlima wa BWANA itapatikana"** Hii inaonekana kuwa kivuli cha mbele cha mahali kwa tungo "mahali Mungu atasababisha jina lake kukaa" (kama vile Kumb. 12:5,11,21; 14:23,24; 16:2,6,11, n.k. Kiasili hii inamaanisha hema, lakini ilikuja kumaanisha hekalu juu ya mlima Moria).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 22:15-19**

**[15] Malaika wa Bwana akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni [16] akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema Bwana, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee, [17] katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; [18] na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu. [19] Basi Ibrahimu akawarudia vijana wake, wakaondoka, wakaenda zao pamoja mpaka Beer-sheba; Ibrahimu akakaa huko Beer-sheba.**

**22:16 "Nimeapa kwa nafsi yangu"** Huu ni wakati pekee katika kitabu cha Mwanzo ambapo Mungu anaapa kwa nafsi yake Yeye mwenyewe kuhusiana na agano. Hapa panakuwa mahali pakubwa pa kithiolojia katika Ebr. 6:13-18. Tambua kwamba ni ahadi isiyokuwa na masharti wala kigezo kilichojikita katika upendo wa Mungu, lakini ni mwitikio kwa tendo kubwa la imani la Ibrahimu (yaani "kwakuwa umeitii sauti yangu," mstari wa 18). Asili ya masharti/kutokuwa na masharti ya maagano ya Biblia kunaonekana kuhusiana na upendo wa Mungu usio na mashharti lakini mwitikio wa kimasharti wa mwandamu.

**22:17 "katika kubariki nitakubariki"** Kuna miundo miwili ya kisarufi ambayo inaashiria mkazo katika mstari huu.

1. Hili neno *Piel* KITENZIJINA HALISI na *Piel* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi uleule, "bariki" (BDB 138, KB 159), hivyo inafasiriwa "Nitakubariki sana."
2. Hili neno *Hiphil* KITENZIJINA HALISI na *Hiphil* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi ule ule, "kuongezeka" au "kufanya wengi" (BDB 915, KB 1176), hivyo kufasiriwa"Nitakubariki na kuuzidisha uzao wako."

Hii inaonekana kurudi mwanzoni mwa ahadi kwa Ibrahimu katika sura ya 12 (kama ilivyokuwa katika uumbaji wa kwanza), ahadi ya uzao na ya nchi. Agano Jipya linasisistiza ahadi ya uzao na linadhoofisha msisitizo wa ahadi ya nchi.

◙ **"nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani;"** Hizi ni sitiari mbili kati ya kadhaa zilizotumika kuelezea asili ya wingi wa uzao wa Ibrahimu (kama vile vumbi, Mwanzo 13:16; 28:14; Hes. 23:10; Nyota, Mwanzo 15:5; 26:4; na mchanga, Mwanzo 32:12).

◙ **"na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao"** Lango linawakilisha Ulinzi wa miji ya kale wenye kuta. Kuingia katika lango la mji wa mtu ilimaanisha kuteka mji wake. Hivyo hii ni sitiari kwa ajili ya ushindi wa jeshi wa uzao wa Ibrahimu dhidi ya wale wote ambao wangelikuwa kinyume nao. Sitiari hii hii inatumika katika Agano Jipya katika Mathayo 16 kuwa "malango ya kuzimu hayataliweza kanisa."

Kutoka kwa Manabii tunajua kwamba hata ahadi hizi zina vigezo vya utii wa Israeli, kama walivyokuwa kwa utii wa Ibrahimu (kama vile 15:6; 22:16,18). Ahadi za YHWH zimebatilishwa kwa kukosa utii kwa kuendelea na kuabudu sanamu kwa Israeli. Lazima tukumbuke kwamba shabaha ya msingi katika maandiko ni tabia ya Mungu ba uaminifu wake. Hatahivyo lazima pia isemwe kwamba shauku yake ni kwamba watu wake waaksi tabia yake kwa ulimwengu usioamini (yaani mataifa) ili waweze kumuendea Yeye!

**22:18 "na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia"** Mambo ya kisarufi na kithiolojia yanahusishwa ni namna gani kufasiri *Niphal* na *Hithpael* KAULI ZA WAKATI TIMILIFU za KITENZI "bariki" (BDB 138, KB 159) ambayo inaonekana kuwa sambamba

1. Mwanzo 12:3, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. Mwanzo 18:18, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. Mwanzo 22:18, *Hithpael* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
4. Mwanzo 26:4, *Hithpael* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
5. Mwanzo 28:14, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Hili shina la neno *Niphal* siku zote ni KAULI TENDWA (KITENZI hiki kinatokea tu katika maandiko ya Mwanzo KAULI TENDWA), lakini kinaweza kufanya kazi kama KAULI REJEREA au HALI YA KUTENDEANA. Hii *Hithpael* shina ni KAULI REJEREA au HALI YA KUTENDEANA (kama vike Kumb. 29:19; Zab. 72:17; Isa. 65:16 [mara mbili]; Yer. 4:2).

Agano Jipya kudondoa ahadi hii muhimu ni KAULI TENDWA. Angalia Mdo. 3:25 na Gal. 3:8. Swali lina husiana na mamlaka ya kimishionari ya Israeli kuwa "ufalme wa kikuhani" kwa ajili ya mataifa (kama vile Kut. 19:5-6). Ingawa

hii haitajwi bila utata mpaka manabii wa karne ya kumi nane, inadhaniwa na kuelezewa kwa haya maandiko ya Mwanzo.

Kwa namna moja Israeli ilitakiwa kutoa taarifa kuhusu Mungu (kupitia kuangalia mtindo wao wa maisha wa sheria ya Musa). Mataifa yalitakiwa kufikia kilele cha kuitikia na kutumaini uaminifu wa YHWH (kama Ibrahimu alivyofanya, kama vile Mwanzo 15:6; Rum. 4:3; Gal. 3:6; Yakobo 2:23). Lazima watambue na kuitikia kwa ufunuo uliotolewa na YHWH kwa na kupitia Israeli. Ikiwa Israeli isingelitii, badala ya kushuhudia utele na pia jamii iliyo imara, mataifa yote yaliona tu upande wa hukumu ya YHWH. Israeli imeshindwa katika mamlaka yake ya kimishionari na imetoa kwa kanisa (yaani "Agizo Kuu," Mt. 28:19- 20; Luka 24:47; Mdo 1:8)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 22:20-24**

**[20] Ikawa baada ya mambo hayo, Ibrahimu akaambiwa ya kwamba, Tazama, Milka naye amemzalia Nahori ndugu yako wana; [21] Usi, mzaliwa wa kwanza wake, na Buzi nduguye, na Kemueli, baba wa Aramu; [22] na Kesedi, na Hazo, na Pildashi, na Yidlafu, na Bethueli. [23] Bethueli akamzaa Rebeka; hao wanane Milka alimzalia Nahori ndugu wa Ibrahimu. [24] Na suria wake Reuma naye alizaa Teba na Gahamu na Tahashi na Maaka.**

**22:20-24** Huu uzao wa familia unaonekana kwa namna fulani kuwa katika hali isiyo ya kawaida, lakini kwa kusema kweli sio muhimu katika kujenga msingi kwa ajili ya mchumba wa baadaye wa Isaka, Rebeka, atakayetajwa katika mstari wa 23.

**22:23 "Bethueli"** Hili jina linamaanisha "mtu wa Mungu" (BDB 143 I).

◙ **"Rebeka"** Inawezekana kwamba asili ya kiebrania ya jina hili (BDB 918) linamaanisha "kumfunga mnyama" na baadaye kuja kumaanisha "mahali pa kufungia" au linapotumika juu ya mwanamke "mtu awekaye mtego." Walimu wa kiyahudi wanaona hili kama maana ya uzuri wa Rebeka kwamba ulikuwa unatega na kushawishi na "aliufunga" upendo wa Isaka.

**22:24 "Reuma"** Neno hili (BDB 910) lina maana mbili zinazowezekana: (1) "kuinuliwa," ambalo linamaanisha kuwa sawa kwakuwa alikuzwa kutoka katika hali ya utumwa mpaka kuwa suria au (2) "lulu" au "marijani," ambayo inaonekana kuwa ufanano wa karibu na neno la kiebrania.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je ni kweli kuwa Mungu anawajaribu watoto Wake? Ikiwa ndivyo, kwanini?
2. Nini maana ya neno "Moria" na iko mahali gani hasa?
3. Kwanini Mungu alimuuliza Ibrahimu kutoa mwana wa ahadi?
4. Kwanini mistari ya 20-24 inajumuishwa katika kifungu hiki cha habari?

# MWANZO 23

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Kifo na mazishi ya Sara | Kifo na mazishi ya Sara | Ibrahim anunua shamba la kuzikia familia | Sara afariki na Ibrahim anunua Shamba la Kuzikia | Mahala pa kuzikia |
| 23:1-16 | 23:1-16 | 23:1-16 | 23:1-2 | 23:1-2 |
| | | | 23:3-4 | 23:3-6 |
| | | | 23:5-6 | |
| | | | 23:7-9 | 23:7-11 |
| | | | 23:10-11 | |
| | | | 23:12-13 | 23:12-16 |
| | | | 23:14-16 | |
| 23:17-20 | 23:17-20 | 23:17-20 | 23:17-18 | 23:17-20 |
| | | | 23:19-20 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO NASB (LILILOBORESHWA ) 23:1-16**

**1 Basi umri wake Sara ulikuwa miaka mia na ishirini na saba ndio umri wake Sara. 2 Sara akafa katika Kiriath-**

**arba, ndio Hebroni, katika nchi ya Kanaani. Ibrahimu akaja kumlilia Sara na kumwombolezea. [3] Akaondoka Ibrahimu kutoka mbele ya maiti wake, akasema na wazawa wa Hethi, akinena, [4] Mimi ni mgeni, ninatembea kwenu; nipeni mahali pa kuzikia kwenu, pawe pangu, nimzike maiti wangu atoke mbele yangu. [5] Wazawa wa Hethi wakamjibu Ibrahimu, wakamwambia, [6] Utusikie, Ee bwana, ndiwe mtu mkuu sana kwetu, uzike maiti wako katika kaburi lile utakalochagua katika makaburi yetu. Hapana mtu kwetu atakayekuzuilia kaburi lake, usizike maiti wako. [7] Ibrahimu akaondoka, akainama mbele ya watu wa nchi, mbele ya hao wazawa wa Hethi. [8] Naye akazungumza nao, akisema, Ikiwa nia yenu nimzike maiti wangu atoke mbele yangu, mnisikie, mkaniombee kwa Efroni bin Sohari, [9] ili kwamba anipe pango ya Makpela, iliyo katika mpaka wa shamba lake, na anipe kwa kima kilicho kamili, katikati yenu, iwe milki yangu ya kuzikia. [10] Basi Efroni alikuwa akiketi kati ya wazawa wa Hethi. Efroni Mhiti akamjibu Ibrahimu, na wazawa wa Hethi wanasikiliza, hata watu wote waingiao mlango wa mji wake, akisema, [11] Sivyo, bwana wangu, unisikilize. Lile shamba nakupa, na pango iliyomo nakupa; mbele ya wana wa watu wangu nakupa, uzike maiti wako. [12] Ibrahimu akainama mbele ya watu wa nchi. [13] Akamwambia Efroni, na watu wa nchi wanasikiliza, akisema, Tafadhali unisikilize; nitatoa kima cha shamba, nawe ukipokee kwangu, nami nitamzika humo maiti wangu. [14] Efroni akamjibu Ibrahimu, akamwambia, [15] Bwana wangu, unisikilize. Sehemu ya nchi, ambayo thamani yake ni shekeli za fedha mia nne, n'nini hii baina yako na yangu? Basi uzike maiti wako. [16] Ibrahimu akakubali maneno ya Efroni. Ibrahimu akampimia Efroni ile fedha aliyotaja masikioni mwa wazawa wa Hethi, shekeli za fedha mia nne za namna inayotumika na wenye biashara**

**23:1** Waalimu wa Kiyahudi wanasema kwamba Ibrahim aliporudi nyumbani na kumweleza Sara mambo aliyotenda,Sara alilia kwa sauti kuu na kufa. Kifo chake kimeandikwa kwenye sura ya 23. Kwa vyovyote hii ni kweli au sio kweli,Bila shaka tunaweza kuona kuwa waalimu wa kiyahudi waliipata wapi tafasiri yao

**23:2 "Kiriath-arba"** Jina hili (BDB 900) Linatokana na

1. "Kiriath" lenye maana ya "mji"
2. "Arba"
   a. kwa kawaida linatafasiriwa "mji wa nne"(mfano,Anaki na watoto wake wa kiume watatu au vijiji vinne kwa pamoja)
   b. lenye asili ya uvamizi (BDB 70)
   c. jina la mtu mmojawapo wa wana wa anaki,Joshua 14:15,15:13,21:11,

Angalia Mada Maalum: Majitu 14:5.

◙ **"Ibrahimu akaja kumlilia Sara na kumwombolezea."**Jambo moja la ajabu haya maombolezo yalichukua muda gani na mwishowe wakakubaliana na wenyeji. Mwili wa Sara ungeharibika mapema kwenye hali ya joto. (Angalia sura ya kifo taratibu za mazishi" in *Ancient Israel: Social Institutions* Juzuu 1 cha Roland de Vaux, kr. 56- 61) Leo katika Israeli (Ambapo hawatii dawa ili isioze)Ni lazima maiti azikwe ndani ya masaa ishirini na nne

**23:3-**13 Kinachofuatia kupitia kwenye ukurasa uliobakia ni mazungumzo(Akitumia kulasimisha na mtoza ushuru wa kawaida anayestahili) kati ya wakaazi wenyeji jirani na Hebron na Ibrahim.

1. "nipeni " mst. 3, BDB 678, KB 733, *Qal* SHURUTISHI kwa maana ya ombi
2. "Shamba la kuzikia"mst 3(Kumiliki eneo la kuzikia), BDB 868, KB 1064, *Qal* HALI YA KUSIHI
3. "Utusikie" mst 6 BDB 1033, KB 1570, *Qal* SHURUTISHI (Ilitumiwa na wana wa Hethi kwa Ibrahim)
4. "Uzike maiti wako "mst. 6, BDB 868, KB 1064, *Qal* SHURUTISHI (Hiki sio ambacho Ibrahim alipenda kufanya,yaani ..,kumzika Sara kwenye ardhi zao.)
5. "mnisikie", mst 8 Lakini Ibrahimu akazungumza nao.
6. "Karibia" (au kusihi), mst. 8, BDB 803, KB 910, *Qal* SHURUTISHI (kama ombi)

7. “Anipe”” mst. 9, BDB 678, KB 733”
    a. *Qal* KAULI AMRISHI
    b. *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU iliyotumika katika maana AMRISHI (Efroni anakubali katika mst. 11 [ *Qal* KAULI ZA WAKATI TIMILIFU tatu], Lakini hii haikuwa zawadi halisi ya bure,ni sehemu kidogo ya makubaliano yaliyotarajiwa;ni msingi unaoonyesha mauziano ya baadae.)
8. “unisikilize**”** mst 11 (Efroni akizungumza na Ibrahim na kumpa pango na shamba )
9. “Uzike” mst 11,
10. “wanasikiliza **“** mst 13,(Ibraham akanena na Efroni)
11. “unisikilize “ mst 15 (Efroni akinena na Ibrahim kuhusu bei ya shamba ambapo wanakubaliana kwa gharama iliyo sahihi,na hii ni gharama kubwa)

mazungumzo haya yanaonekana kama yaliyobuniwa au kukaririshwa kwetu,lakini huu ni utaratibu uliotegemewa na jamii ya wakanaani miaka elfu mbili k.k.

**23:3 “Wazawa wa Hethi ”** Jina Hethi (**חת**, BDB 366) ni la zamani la ukoo wa wahiti (**חתי**, BDB 366, kama vile. Mwa. 10:15; I Nyak. 1:13). Tazama Mada Maalumu: Wazawa wa Israeli walioishi Palestina katika 12:6.

**23:4 “Mimi ni mgeni, Ninatembea “** Maneno haya mawili yana vidokezo tofauti,lakini hapa yamkini maelezo yenye tungo mbili zilizo pamoja

1. “Mgeni” (BDB 158) inadokeza mkazi wa kigeni, kama vile Mwanzo 15:13, Kut. 22:21, Law. 19:34, Kumb. 10:19; 23:8.
2. “Mtembezi” (BDB 444) ni mgeni anayepita asiyekua na haki,Law 22:10;25:40.

Kwa kadiri iwezekanavyo ni vigumu kuwa pamoja,Inadokeza mtu mmoja kuingia eneo lisilo la makazi,Lakini sio ardhi yake. Tazama makala ya “*Resident Aliens*” katika *Ancient Israel: Social Institutions*, juzuu. 1, cha Roland deVaux, kur. 74-76.

**23:6 “Ndiwe mtu mkuu”** Neno lililotafasiri “Mkuu” ni neno *elohimu* (BDB 43) ,ambalo linatumika kama;

1. Mungu
2. Hakimu
3. Malaika
4. Hapa anatoa nguvu,Mahali maalum,Kiongozi wa familia ,

Tafsiri ya neno “Mkuu” inatokana na asili ya maana ya *el* (BDB 421,kama vile Nyak. 12:22, Zab. 68:15,Yona 3:3,) Baadhi ya watoa maoni wanataka kutafasiri kama “Mwana wa mfalme wa Mungu”

Neno lililotafasiriwa “Mwana” lina maana “aliyeinuliwa juu” NASB inalitafasiri kama;

1. ”Mwana wa mfalme” kwenye kitabu cha Mwanzo 17:20; 25:16; 34:2.
2. ”Kiongozi” kwenye kitabu cha Kutoka 16:22; Hes. 1:16 , 44; 2:3; Yoshua 22:32.
3. ”Mtawala” kwenye kitabu cha Kutoka 22:28; 34:31; 35:27; 1 wafalm 11:34.
4. ”Shehe” kwenye kitabu cha Yoshua 13:21.
   Kwa makubaliano haya ya juu ni hekima yenye utii.Wahiti hawakufanya makubaliano ya kidini.

**23:9 “Pango ya Makpela”** Hili lilionekana kuwa ni pango (Sehemu ya kuzikia) lililokuwa kwenye wilaya ya Makpela,mbali kutoka mkoa wa Hebroni kuelekea Mamre. (kama vile. 13:18; 14:13; 18:1).

Uzao wa familia ya Ibrahimu walizikwa hapa.

1. Sara, 23:19
2. Ibrahim, 25:9
3. Isaka, 35:29
4. Rebeka na Leah, 49:31
5. Yakobo, 50:13

**23:10 "Mlango wa mji"** Hapa ni mahala ambapo viongozi walikutana kwa ajili ya ushirika,biashara,na mambo ya kihalali.

◙**"Wahiti"** Angalia mada ya 12:6.

**23:15 "Shekeli"**Angalia mada maalumu: Uzani na Vipimo Vilivyotumika Mashariki ya Karibu ya Kale na Juzuu ya 18:6

**ANDIKO NASB (LILILOBORESHWA ) 23: 17-20**

*17* **Mungu akaiweka katika anga la mbingu, itie nuru juu ya nchi** *18* **na kuutawala mchana na usiku na kutenga nuru na giza; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.** *19* **Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne.**
*20* **Mungu akasema, Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu.**

**23:17 "Vyote viliyakinishwa "** KITENZI **(**BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) Hii ina maana kuinuka au kusimama juu. Ilikuja kufuatia mapatano halali yaliyofanyika. Ibrahimu sasa anamiliki ardhi ya Palestina au kanaani kihalali. Ibrahimu hakuwa mtembezi tena na mgeni.

# MWANZO 24

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inayofuata MT)** |
| Mwari wa Isaka | Mwari wa Isaka | Kumtafuta mke kwa ajili ya Isaka | Mke kwa ajili ya Isaka | Kuoa kwa Isaka |
| 24:1-9 | 24:1-9 | 24:1-9 | 24:1-4 | 24:1-9 |
| | | | 24:5 | |
| 24:10-14 Rebeka Anachaguliwa | 24:10-14 | 24:10-4 | 24:10-14 | 24:10-14 |
| 24:15-21 | 24:22-28 | 24:15-21 | 24:15-17 | 24:15-21 |
| | | | 24:18-21 | |
| 24:22-27 | 24:22-28 | 24:22-27 | 24:22-23 | 24:22-27 |
| | | | 24:24-25 | |
| | | | 24:26-27 | |
| 24:28-41 | | 24:28-33 | 24:28-31 | 24:28:32 |
| | 24:29-31 | | | |
| | 24:32-41 | | 24:32-33a | |
| | | | 24:33b | 24:33-49 |
| | | 24:34-41 | 24:32-33a | |
| | | 24:34-41 | 24:34-41 | |
| 24:42-44 | 24:42-44 | 24:42-44 | 24:42-42 | |
| 24:45-49 | 24:45-49 | 24:45-49 | | |
| 24:50-51 | 24:50-51 | 24:50-51 | 24:50-53 | 24:50-53 |
| | (60) | (60) | | |
| 24:52-61 | | | | |
| (60) | | | 24:54 | 24:54-61 |

| | |
|---|---|
| | (60) |
| | 24:54 |
| | 24:55 |
| | 24:56 |
| | 24:57-58a |
| | 24:58b |
| | 24:59-61 (60) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24: 9**

**[1] Basi Ibrahimu alikuwa mzee mwenye miaka mingi, na Bwana alikuwa amembariki Ibrahimu katika vitu vyote. [2] Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake, aliyetawala vitu vyake vyote, Tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu, [3] nami nitakuapisha kwa Bwana, Mungu wa mbingu, na Mungu wa nchi, kwamba hutamtwalia mwanangu mke katika binti za Wakanaani ambao nakaa kati yao; [4] bali enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu, ukamtwalie mwanangu Isaka mke. [5] Yule mtumishi akamwambia, Labda yule mwanamke hatakubali kufuatana nami mpaka nchi hii, je! Nimrudishe mwanao mpaka nchi ulikotoka? [6] Ibrahimu akamwambia, Ujihadhari, usimrudishe mwanangu huko. [7] Bwana, Mungu wa mbingu, aliyenitoa katika nyumba ya babangu, na kusema nami katika nchi niliyozaliwa, aliniapia akisema, Nitawapa uzao wako nchi hii; yeye atampeleka malaika wake mbele yako, nawe utamtwalia mwanangu mke tokea huko.**

**24:1"Basi Ibrahimu alikuwa mzee mwenye miaka mingi**" Mtu anapolinganisha Mwa. 25:20, ambayo inasema kwamba Isaka alikuwa amemuoa Rebeka akiwa na umri wa miaka arobaini, pamoja na Mwa. 21:5, ambayo inasema kwamba Ibrahimu alikuwa na miaka 100 alipozaliwa Isaka, pia inaonekana kwamba Ibrahimu alikuwa na miaka 140 mwanzoni mwa sura ya 24. Huyu aliishi yapata miaka 175 (kama vile Mwa. 25:7).

◙ **“na Bwana alikuwa amembariki Ibrahimu katika vitu vyote”** Angalia orodha kamili ya hizi baraka katika mst. 35.

**24:2 “Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake, aliyetawala vitu vyake vyote”** Hiki KIVUMISHI “mzee” (BDB 278, kinatokana na NOMINO “ndevu”) kinaweza kumaanisha mtu mwenye mamlaka, si lazima awe mzee sana kwa umri wake (kama vile Mwa. 50:7; Isa. 3:2). Watoa maoni wengi wanadhani kwamba mtumishi huyu mwaminifu ni Eliezeri wa Dameski, aliyetajwa katika Mwa. 15:2. Ile dhana ya kwamba kumtafutia Isaka inaonyesha asili yake ya kutokuwa na ubinafsi sanjali na haki za kumiliki. Kama ilivyo kawaida huyu ni moja ya wacha- Mungu, wazuri, na mfuasi mwenye matendo ya uaminifu miongoni mwa wale waliotajwa katika Biblia.

◙ **“Tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu**” Hiki KITENZI “kutia” (BDB 962, KB 1321, *Qal* KAULI SHURUTISHI) ni agizo muhimu la kiutamaduni linalohusiana na kula kiapo cha mst.3 (“kuapa,” BDB 989, KB 1396, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO).
Hili tendo la kipekee la kiutamaduni linatajwa hapa tu katika Mwa. 47:29. Kumekuwa na nadharia kadhaa zinazozungumzia kusudi lake halisi.

1. Kwa sababu paja ni ishara ya vizazi vya mwanadamu (BDB 437,1,b, kama vile Mwa. 46:26; Kut.1:5; Amu. 8:30), hili linaweza kurejelea juu ya viungo vya uzazi. Ikiwa hili ni la kweli, linaonekana kurejelea juu ya tohara, ambayo ni ishara ya agano la YHWH (kama vile mst. 3). Hii ndiyo njia iliyotumiwa na katika toleo la Targum la Jonathan na Rashi katika kuufasiri mstari huu.
2. Iliidhinishwa kwamba neno hili linarejelea juu ya vizazi na hivyo, Jerome, Augustine, na Luther wote wanasema kwamba neno hili linarejelea juu ya hatima ya uzao wa Ibrahimu, Masihi.
3. Wengine wanaliona neno hili kuwa linarejelea juu ya ubwana wa Ibrahimu kwa mtawala huyu wa pekee aliyepewa kazi muhimu ya kutafuta mke kwa ajili ya Isaka (kama vile Aben Ezra na Calvin).
4. Hii inaweza kuakisi juu ya madhara ya kiapo cha laana ya kitamaduni kinapokiukwa.

**24:3 “nitakuapisha kwa Bwana, Mungu wa mbingu, na Mungu wa nchi”** Kumekuwa na mijadala ya aina mbalimbali miongoni mwa watoa maoni kama Ibrahimu alikuwa akimwabudu Mungu mmoja au alikiri vyote viwili (mtu aliyemwabudu Mungu mmoja pekee, lakini hakanushi kuwepo kwa miungu wengine). Kwa sababu ya vifungu kama hivi, Naamini kwamba Ibrahimu alikuwa akimwabudu Mungu mmoja. Wasomi wengi wanadhani kwamba kumwabudu Mungu mmoja kwa ukamilifu, katika maana ya kifalsafa, hakuimarishwa hadi walipotokeza Manabii katika karne ya 8.

◙ **“hutamtwalia mwanangu mke katika binti za Wakanaani”** Huenda ni kwa sababu ya unabii wa Mwa. 15:13-16 au Mwa. 9:25-27 (pia Kut. 34:15-16 na Kut. 7:3-6). Ibrahimu alikuwa amekutana na wacha- Mungu wengi ambao walikwa Wakanaani.

1. Waamori waliotajwa katika 14;13
2. Melkisedeki, aliyetajwa katika 14:18
3. Abimeleki, aliyetajwa katika sura 20.

Hili linaonyesha kwamba hatma ya ufukara wa Mwamori bado ulikuwa haujafikia kikomo kwa wakati huu katika kistoria yake.

**24:4 “enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu”** Kifungu hiki kinaonekana kurejelea juu ya nchi ya kusini ya Wakaldayo na nyumba ya Nahari aliyetajwa katika 11:27-31.

**24:5“Labda yule mwanamke hatakubali kufuatana nami mpaka nchi hii,”** Kwa uwazi kabisa, mtumishi huyu alihusika katika mahitaji muhimu ambayo Ibrahimu alikuwa ameyaweka katika matakwa yake. Ibrahimu alihusika katika kuhakikisha Isaka anapata mwanamke ambaye (1) atakuwa na hiari yake, wa imani, wa kuishi na nyumba yake, kama yeye alivyoishi na nyumba yake na (2) aliyemjua YHWH, Mungu wao.

◙ **"je! Nimrudishe mwanao mpaka nchi ulikotoka"** Mstari 5 ni swali la mkazo la *Hiphil* KITENZIJINA HALISI na *Hiphil* KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi unaofanana, BDB 996, KB 1427) lilioulizwa na mtumishi na mst. 6 ni amri ya mkazo ("angalia hii usimchukue," a *Niphal* KITENZI SHURUTISHI [BDB 1036, KB 1581] kikifuatiwa na *Hiphil* KISICHO TIMILIFU [BDB 996, KB 1427] ya KITENZI kinachofanana kilichotumiwa na Ibrahimu katika mst. 5) kwamba Isaka harudi katika nchi aliyozaliwa Ibrahimu. Kuna sababu mbili tu: (1) hawa bado walikuwa wakiabudu miungu au (2) Ahadi za Mungu kwa upekee zilihusiana na Kanaani (kama vile mst. 7; Ebr. 11:15; Mwa. 12:7; 13:15;15:18).

**24:7 "yeye atampeleka malaika wake mbele yako"** Malaika wa YHWH mara nyingi alizungumza na kuteenda ili kuyatimiza mapenzi ya YHWH. Huyu anatajwa mara kadhaa katika Mwanzo (kama vile 16:7; 21:17; 22:11; pia angalia Kut. 23:20,23). Angalia mada maalum katika 12:7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24 : 10-14**

**[10] Kisha huyo mtumishi akatwaa ngamia kumi katika ngamia za bwana wake akaenda zake, maana mali zote za bwana wake zilikuwa mkononi mwake, akaondoka, akaja mpaka Mesopotamia, mpaka mji wa Nahori.**
**[11] Akawapigisha magoti ngamia nje ya mji karibu na kisima cha maji wakati wa jioni, wakati ambapo wanawake wanakwenda kuteka maji. [12] Naye akasema, Ee Bwana, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, nakuomba mambo yangu uyajalie yawe heri leo, ukamfadhili bwana wangu Ibrahimu. [13] Tazama! Nimesimama karibu na kisima cha maji, na binti za watu wa mjini wanatoka kuteka maji, [14] basi na iwe hivi; yule msichana nitakayemwambia, Tua mtungi wako, nakuomba, ninywe; naye akasema, Unywe, nami nitawanywesha na ngamia zako pia; basi huyu na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako Isaka; na kwa hayo nitajua ya kuwa umemfadhili bwana wangu.**

**24:10 "Kisha huyo mtumishi akatwaa ngamia kumi "** Kumekuwa na mijadala mbali mbali miongoni mwa wanahistoria kuhusu tarehe ambayo ngamia hawa walianza kufugwa. Ni kweli kabisa kwamba hawa hawakutumika kwa upana kwa sababu za kibiashara (yaani, wanamsafara) hadi 1200 K.K., lakini hawa wanaoneka kufugwa sana hapa awali kwa matumizi ya binafsi.

◙ **"Mesopotamia"** Hili neno la Kiebrania "Aram-na-harain" (BDB 74 na 625, kama vile Kut. 23:4), ambalo linaonekana kumaanisha "linahusiana na mito miwili huko Syria ya sasa." Kifungu hiki kinairejelea kusini ya kati ya Mesopotamia.

◙ **"mji wa Nahori"** Nahori (BDB 637, maana yake haijulikani) ni jina la Tera, baba yake na Ibrahimu (kama vile Mwa. 11:22,23,24,25; I Nya. 1:26). Pia ni jina la mmoja wa wana wa Tera (Mwa.11:26,27,29). Kwa uwazi kabisa, Ibrahimu anamwambia mtumishi wake kurudi katika mji ambao nduguye Nahori anaishi (Mwa. 22:20-24). Huu umekuwa ukijulikana kwa jina jingine, huenda hata nchi ya kusini ya Wakaldayo, Nyumbani halisi kwa Ibrahimu au eneo lingine ambalo watu wa nyumbabi kwao walihamia, Harani (kama vile Mwa. 11:31). Maelezo ya Toleo la NIV Study Bible yanautaja mji huu kwa jina la Nahorappears katika vigae vya mfinyanzi vinavyopatikana huko Mari (uk. 41). Katika maana hii "Harani" inarejelea juu ya wilaya, si mji ulio kusini kati huko Mesopotamia.

**24:12 "Naye akasema**, '**Ee Bwana, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu,**'" Hili si oni la kushusha hadhi ya imani ya mtumishi huyu, bali ni utambuzi wa chanzo cha ahdi ya agano (kama vile mst. 26). Maombi yake yaliambatana na mambo mawili.

1. "kujalia" ( "sababisha kutokea"), BDB 899, KB 1137, *Hiphil* KITENZI SHURUTISHI
2. "heri," BDB 793, KB 889, *Qal* KITENZI SHURUTISHI.

Hili neno "fadhiri" ni agano lenye nguvu la NOMINO חסד ((kama vile 19:19; 20:13; 21:23;24:12,14,27,49; 32:10; 39:21; 40:14; 47:29). Angalia Mada Maalum katika 19:19. Huyu mtumishi kwa hakika alikuwa akizungumzia juu ya ombi la Agano la Ibrahimu.

**24:12**,**16** Sifa kadhaa za Rebeka zinaelezwa.

1. na kwa nguvu zako unijalie, mst. 12 (ombi la mtumishi wa Ibrahimu)
2. mzuri sana, mst. 16
3. bikra, mst. 16
4. mkarimu, mist. 18-25

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 24: 15-21**

***15*** **Ikawa, kabla hajaisha kunena, tazama, Rebeka anatokea, binti wa Bethueli mwana wa Milka, mkewe Nahori, ndugu wa Ibrahimu, naye ana mtungi begani pake.** ***16*** **Naye yule msichana alikuwa mzuri sana uso wake, bikira, wala mwanamume hajamjua bado; akashuka kisimani, akajaza mtungi wake, akapanda.** ***17*** **Ndipo yule mtumishi akapiga mbio kwenda kumlaki, akasema, Tafadhali unipe maji kidogo katika mtungi wako ninywe.** ***18*** **Naye akasema, Unywe, bwana wangu, akafanya haraka, akatua mtungi wake mkononi mwake, akamnywesha.** ***19*** **Hata alipokwisha kumnywesha akasema, Na ngamia zako nitawatekea, hata watakapokwisha kunywa.** ***20*** **Akafanya haraka, akamwaga maji ya mtungi wake katika birika, akapiga mbio kisimani ateke, akawatekea ngamia zake wote.** ***21*** **Basi yule mtu akamkazia macho, akanyamaza, ili ajue kwamba Bwana ameifanikisha safari yake ama sivyo.**

**24:15 "Rebeka anatokea, binti wa Bethueli mwana wa Milka"** Nyumba hii ilitajwa katika Mwa. 22:20-24. Jina la babaye, Bethueli, linamaanisha "mtu wa Mungu" (BDB 143 I), ambalo linaweza kuonyesha asili ya kiroho ya nyumba hii. Pia ni muhimu kwamba mtiririko wa nyumba hii ulitokana na Milka, mke mwema, na si suria la Nahori, Reuma.

◙ **"ana mtungi begani pake"** Hii ni moja ya hoja ambayo inaonyesha habari kuhusu historia.Wanawake wa huko Misri walibeba mitungi vichwani mwao, lakini huko Mesopotamia hawa walibeba mitungi mabegani mwao.

**24:17 "Tafadhali unipe maji kidogo katika mtungi wako ninywe"** Hii ni *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (BDB 167, KB 196). Hii inaenda sambamba na ombi lake mst. 14.

**24:18 "Unywe"** Hii ni *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 1059, KB 1667), ombi lake la mwongozo wa kumpata mke mwema.

**24:19-20 "ngamia zako nitawatekea"** Hii ilikuwa sehemu ya maombi ya mtumishi yalio katika mst. 14. YHWH alimpa Rebeka mwongozo wa kipekee. Tendo hili linalozungumzia sehemu ya Rebeka linaweza kuwa limehusisha wakati fulani na nguvu za ngamia kumi waliokuwa na kiu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24 :22-27**

***22*** **Ikawa, ngamia walipokwisha kunywa, yule mtu akatwaa pete ya dhahabu, uzani wake ulikuwa nusu shekeli, na vikuku viwili kwa mikono yake, uzani wake ulikuwa shekeli kumi za dhahabu,** ***23*** **akasema, U binti wa nani wewe? Tafadhali uniambie. Je! Iko nafasi katika nyumba ya baba yako tupate mahali pa kukaa kwa muda?** ***24*** **Akasema, Mimi ni binti wa Bethueli mwana wa Milka, aliyemzalia Nahori.** ***25*** **Tena akamwambia, Kwetu kuna majani na malisho ya kutosha, na mahali pa kukaa wageni.** ***26*** **Yule mtu akainama akamsujudu Bwana.** ***27*** **Akasema, Na atukuzwe Bwana, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, ambaye hakuacha rehema zake na kweli yake kwa bwana wangu. Bwana akaniongoza mimi nami njiani hata nyumba ya nduguze bwana wangu.**

**24:22 "yule mtu akatwaa pete ya dhahabu, uzani wake ulikuwa nusu shekeli, na vikuku viwili kwa mikono yake, uzani wake ulikuwa shekeli kumi za dhahabu"** Pete hii ya dhahabu inarejelea juu ya chanda cha pua (kama vile

mst. 47 na vitabu vitano vya Kisamaria.). Fikiria kwamba chanda cha pua cha nusu shekeli kingesababisha pua kuinama (kama vile Mit. 11:22; Isa. 3:21; Eze. 16:12).

◙
**24:27**
**NASB "rehema"**
**NKJV "huruma"**
**NRS "pendo la milele"**
**Peshitta "neema"**

Hili ni neno la Kiebrania *hesed* (BDB 338, angalia Mada Maalum katika 19:19), ambalo linamaanisha "wema" au "uaminifu wa agano." Hili limetajwa mara kwa mara katika uhusiano na kazi ya Mungu kwa watu wake waliochaguliwa. Hili linatumika

1. kumwokoa mtu kutoka kwa adui zake
2. kumwokoa mtu toka kifoni
3. kumrejesha mtu katika Neno la Mungu (kama vile Zaburi 109:26; 119:41, 76, 88, 124, 149, 159)
4. kusamehe dhambi (kama vile Zab. 25:7; 51:1)
5. kulitunza agano (kama vile Kumb. 7:9, 12; I Fal. 8:23; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4)
6. kuueleza ukamilifu na umilele wa pendo la Mungu na uhusiano wake (kama vile I Nya. 16:34,41; II Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 103:17; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136: na kuendelea; 138:8)

◙
**NASB, NKJV,**
**Peshitta "ukweli"**
**NRSV "uaminifu"**
**NJB "uaminifu wa pendo"**

Huu ni umuhimu mwingine wa neno, "ukweli," (BDB 54) ambalo mara nyingi huonekana katika kiunganishi na neno "rehema." Asili yake halisi ilimaanisha "thabiti" au "kuwa na hakika" na lililotokea, hivyo, kuzungumzia juu ya "uaminifu." Usawa wa Kiyunani wa neno hili analolitumia Paulo kuainisha uthibitisho kwa neema kupitia imani katika Warumi 4 na Wagalatia 3, ukinukuliwa kutoka katika Habakuki 2:4 (kumbuka waandishi wa kitabu cha Agano Jipya walikuwa wanafikra za Kiebrania walioandika katika lahaja ya lugha ya Koine ya Kiyunani, angalia Mada Maalum: Amini katika 15:6). Mara nyingi maneno haya hutokea kwa pamoja (kama vile Zab. 25:10; 40:11; 57:3; 61:7; 85:10; 89:14; 115:1).

◙ **"Bwana akaniongoza mimi "** Hiki KITENZI (BDB 634, KB 685, *Qal* cha WAKATI TIMILIFU) kinaeleza uhusiano wa Mungu na mwongozo wake kwa wale wanao mtumainia (kama vile Zab. 5:8; 27:11; 139:24; Isa. 58:11).

◙ **"njiani"** Hili neno (BDB 202) linaeleza maisha ya imani katika Mungu (kama vile Amu. 2:22; Zab. 119:1). Hii nahau ya Agano la Kale ilikuja kuwa jina kwa kanisa la kwanza la ki- Kristo (yaani, "Njia," kama vile Matendo ya Mitume 9:2; 18:25, 26; 19:9, 23; 22:4; 24:14, 22; na pengine Yohana 14:6).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24 :28-41**

**[28] Basi yule msichana akapiga mbio, akawaambia watu wa nyumba ya mama yake mambo hayo. [29] Na Rebeka alikuwa na kaka, jina lake Labani. Labani akatoka mbio kumwendea yule mtu kisimani. [30] Ikawa, alipoiona ile pete, na vikuku mikononi mwa nduguye, akasikia maneno ya Rebeka nduguye, akisema, Hivyo ndivyo alivyoniambia mtu huyo, basi akamjia mtu yule, na tazama, amesimama karibu na ngamia kisimani. [31] Akasema, Karibu, wewe uliyebarikiwa na Bwana, mbona unasimama nje? Kwa maana nimeiweka nyumba tayari, na nafasi kwa ngamia. [32] Na mtu yule akaingia katika nyumba, akawafungua ngamia; naye akatoa majani na malisho kwa ngamia, na maji ya kuoshea miguu yake, na miguu ya watu waliokuwa pamoja**

**naye.**
[33] **Akaandaliwa chakula, lakini akasema, Sili mpaka niseme kwanza maneno yangu. Akamwambia, Haya,**
**sema.** [34] **Akasema, Mimi ni mtumwa wa Ibrahimu,** [35] **na Bwana amembarikia sana bwana wangu, amekuwa mtu mkuu; amempa kondoo, na ng'ombe, na fedha, na dhahabu, na watumwa, na wajakazi, na ngamia, na**
**punda.** [36] **Naye Sara, mkewe bwana wangu, akamzalia bwana wangu mwana wa kiume, katika uzee wake;**
**naye amempa yote aliyo nayo.** [37] **Kisha bwana wangu akaniapisha akisema, Usimtwalie mwanangu mke wa**
**binti za Wakanaani, ambao nakaa katika nchi yao.** [38] **Ila uende mpaka nyumbani kwa babangu, na kwa jamaa**
**zangu, ukamtwalie mwanangu mke.** [39] **Nikamwambia bwana wangu, Labda huyo mwanamke hatafuatana**
**nami.** [40] **Akaniambia, Bwana, ambaye naenenda machoni pake, atapeleka malaika wake pamoja nawe, atafanikisha njia yako; nawe umtwalie mwanangu mke katika jamaa zangu, na wa nyumba ya**
**babangu.** [41] **Ndipo utafunguliwa kiapo changu hapo utakapowafikilia jamaa zangu; nao wasipokupa msichana huyo, utafunguliwa kiapo changu.**

**24:29 "Labani"** Vyanzo vya Sheria za Kiyahudi vina mtazamo hasi juu ya Labani, hivyo, walimu wa sheria za Kiyunani wanautafsri mst. 30 kwa kusema kwamba alikwenda nje ili kukutana na mtumishi wakati alipoona dhahabu aliyopewa dada yake. Hata hivyo, mst. 30 pia unaitaja nyumba ya Ibrahimu, ambayo ni sababu nyingine muhimu ya masilahi ya Labani. Labani ni mtu mgumu kumwelewa katika Maandiko kwa sababu katika mst. 31 anatumia neno "YHWH," lakini katika Mwa. 31:53 huyu anaonekana kuwa mwabudu sanamu na mwabudu miungu wengi na kumaanisha kwamba kuna mungu mwingine wa Nahori.

**24:32-33** Wengi walilitarajia kwamba matendo ya kiutamaduni yanafanywa na mtumwa wa Ibrahimu na Labani/watumwa wa Labani.

1. kushusha mizigo iliyokuwa juu ya ngamia
2. kuwapa ngamia chakula
3. kuwapa maji watumwa walioambatana naye "mtumwa" kuwaosha miguu yao
4. akawalisha wote

**24:34-41** Kipengele hiki kinayarudia maneno ya Ibrahimu kwa mtumwa wake ambayo yamenukuliwa hapo awali katika sura hii.

**24:36 "Naye Sara, mkewe bwana wangu, akamzalia bwana wangu mwana wa kiume, katika uzee wake"** Kwa uwazi kabisa habari hii ilisimuliwa kwa ajili ya kuzisisimua fikra za nyumba hii juu ya umri wa Isaka. Isaka alikuwa mwana wa Ibrahimu, ambapo Rebeka alikuwa mjukuu wa Nahori.

**24:41 "kiapo"** Katika sehemu ya kwanza ya sura hii Ibrahimu alimsihi mtumwa wake kula kiapo (BDB 46). Mfumo wa neno lililotumika hapa katika mst. 41 pia unamaanisha "laana," ambayo inaonyesha asili ya msistizo wa ombi la Ibrahimu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24:42-44**

[42] **Nami nikaja leo kisimani, nikasema, Ee Bwana, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, ukinifanikishia sasa**
**njia yangu niendayo mimi,** [43] **tazama! Nimesimama karibu na kisima cha maji; basi na iwe hivi, msichana**
**ajaye kuteka maji, nikamwambia, Nipe, nakuomba, maji kidogo katika mtungi wako ninywe,** [44] **naye**
**akaniambia, Unywe wewe, na ngamia zako pia nitawatekea, huyo na awe ndiye mke Bwana aliyemwekea mwana wa bwana wangu.**

**24:43 "msichana"** Inatia shauku kwamba Rebeka aliitwa bikra katika mst. 16, "bethula" (BDB 143), ambapo katika mst. 43 anaitwa msicha, "alma" (BDB 761). Watafsiri wa Agano la Kale la Kiyunani wanalitafasiri neno "alma"

kama “bikra” katika Isa. 7:14 na katika mstari huu, inaonekana kwamba maneno haya , kiutamaduni, yalimaanisha kitu kile kile, ingawa neno “bethula” kwa uhalisia linamaanisha “bikra” na neno “alma” linamanisha “msichana mdogo mwenye umri wa kuolewa” ambaye alidhaniwa kuwa anafaa kuolewa.

**24:42-48** Haya ni marudio ya mjadala uliopita katika mist. 11-27.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24: 45-49**

**[45] Hata kabla sijaisha kusema moyoni mwangu, tazama! Rebeka akatokea, na mtungi begani mwake. Akashuka kisimani akateka. Nami nikamwambia, Tafadhali nipe maji ninywe. [46] Akafanya haraka akatua mtungi wake chini, akanena, Unywe, na ngamia zako nitawanywesha pia; basi nikanywa, akawanywesha na ngamia nao. [47] Kisha nikamwuliza nikasema, U binti wa nani wewe? Naye akasema, Mimi ni binti Bethueli, mwana wa Nahori, Milka aliyemzalia. Nami nikamtia hazama puani mwake na vikuku mikononi mwake. [48] Nikainama, nikamsujudia Bwana, nikamtukuza Bwana, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, aliyeniongoza njiani, nimtwalie mwana wa bwana wangu binti wa ndugu yake. [49] Basi, kama mnataka kumfanyia rehema na kweli bwana wangu, niambieni kama sivyo, niambieni; ili nigeuke upande wa kuume au wa kushoto.**

**24:49** Mtumishi alitaka jibu toka kwa Labani. Je! Atatenda kama Ibrahimu kwa wema na kweli?
Ikiwa hahitaji kuendelea na makubaliano ya ndoa mtumishi ataondoka (sitiari, “Ninaweza kurudi mkono wa kuume au kushoto”) na kujaribu kwingine. Mstari huu una KAULI SHURUTISHI TATU.

1. “niambie,” BDB 616, KB 665, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. “nijue,” ni KITENZI sawa kilichorudiwa
3. “kwamba naweza kurudi,” BDB 815, KB 937, *Qal* KAULI SHURUTISHI iliyotumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUSIHI.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24 : 50-51**

*[50]* **Ndipo Labani na Bethueli wakajibu wakasema, Neno hili limetoka kwa Bwana, wala sisi hatuwezi kukuambia neno jema wala baya.** *[51]* **Tazama, huyo Rebeka yuko mbele yako, umchukue, ukaende zako awe mke wa mwana wa bwana wako, kama alivyosema Bwana.**

**24:50** “**Ndipo Labani na Bethueli wakajibu wakasema**, ‘**Neno hili limetoka kwa Bwana, wala sisi hatuwezi kukuambia neno jema wala baya**’” Si jambo la kawaida kwamba Labani, ndugu, kutajwa kabla ya Bethueli, baba. Tumejifunza kutoka katika vigae vya Nuzi kwamba mara nyingi ndugu alifuata kanuni za ndoa kupitia makubaliano. Kifungu cha mwisho cha mstari huu kina ugumu mkubwa wa kueleweka kwa watoa maoni wengi. Hii inaonekana kuwa nahau ya Kiebrania au “YHWH akizungumza, sisi twaweza kuzungumza nini?” (kama vile mst. 51c).
Inashangaza kwamba Bethueli anatajwa katika mst. 50, lakini si katika mist. 53,55. Wengi wanadhanai kwamba huyu lazima kwa wakati huu alikuwa amekwisha kufa. Huenda jibu la Labani lililo katika mst. 50 linamweleza yeye kama yeye na Bethueli bila kuwepo babaye. Inawezekana kwamba ndugu ndiyo waliokuwa wakikubaliana juu ya kuolewa kwa dada zao.

**24:51** Kuna masharti kadhaa katika kuyakubali maelezo aliyoyatoa Yule mtumwa kwa mara nyingine kuhusu sababu iliyomleta na ombi lake la kupewa jibu la haraka (mst. 49).

1. “mchukue,” BDB 542, KB 534, *Qal* SHURUTISHI
2. “ukaende zako,” BDB 229, KB 246, *Qal* YENYE MASHARTI
3. “awe mke,” BDB 224, KB 243, *Qal* ya maelezo yenye AMRI, Rebeka haulizwi kuhusu matendo yake katika mst. 28, bali anaulizwa katika mist. 57-58, tendo ambalo linaonekana kuwa la ishara ya unyenyekevu kwa sababu mahari ilikuwa imekwisha tolewa katika mst. 53.

Kumbuka Biblia inatupatia ufupisho wa kile kilichosemwa na kile kilichotokea, lakini tunaamini ya kuwa Roho ndiye aliyetoa mwongozo wa ufupisho huu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24:52-61**
***52*** **Ikawa mtumishi wa Ibrahimu aliposikia maneno yao, akainama hata nchi mbele za Bwana.** ***53*** **Kisha huyo mtumishi akatoa vyombo vya fedha, na vyombo vya dhahabu, na mavazi, akampa Rebeka; na vitu vya thamani akampa nduguye na mamaye pia.** ***54*** **Wakala wakanywa, yeye na watu waliokuwa pamoja naye, nao wakakaa usiku. Wakaondoka asubuhi, naye akasema, Nipeni ruhusa niende kwa bwana wangu.** ***55*** **Ndugu yake na mama yake wakasema, Msichana na akae kwetu kama siku kumi, zisipungue, baadaye aende.** ***56*** **Naye akawaambia, Msinikawilishe, mradi Bwana amefanikisha njia yangu; nipeni ruhusa niende kwa bwana wangu.** ***57*** **Wakasema, Na tumwite huyo msichana, tumwulize mwenyewe.** ***58*** **Wakamwita Rebeka wakamwuliza, Je! Utakwenda na mtu huyu? Akasema, Nitakwenda.** ***59*** **Ndipo wakampeleka Rebeka ndugu yao, na yaya wake, na mtumishi wa Ibrahimu, na watu wake.** ***60*** **Wakambarikia Rebeka, wakamwambia, Ndugu yetu, uwe wewe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi, na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao.** ***61*** **Rebeka akaondoka na vijakazi wake, nao wakapanda juu ya ngamia, wakamfuata yule mtu. Naye huyo mtumishi akamchukua Rebeka akaenda zake.**

**24:52 "akainama hata nchi mbele za Bwana"** Hii ni mara ya tatu ambapo mtumishi huyu anaomba hadharani, akionyesha imani na shukrani zake kwa Bwana. Hii ndiyo sifa ya kweli ya kibiblia ishangazayo.

**24:53** Katika ulimwengu wa Kale mali ilikusanywa kupitia

1. uzito wa vyuma vya thamani
2. vito
3. mavazi ya gharama
4. vyakula vya aina mbalimbali
5. ardhi
6. ufugaji

Tambua kuwa mtumishi huyu alilileta vitu kadhaa kati ya hivi, ambavyo vingesafirishwa kwa urahisi.

1. vyombo vya fedha
2. vyombo vya dhahabu
3. mavazi
4. na vitu vya thamani

Ibrahimu alikuwa mtu tajiri. Kuwa na mtu mwingine ilikuwa sehemu ya watu wa nyumbani mwake (yaani, mke wa Isaka) ilikuwa heshima kubwa sana.

**24:54** Kwa kufahamu umuhimu uliokuwa katika mlo kwa niaba ya kufikia hatima ya makubaliano au kuimarisha maagano ya urafiki, mlo huu ungeweza kuwa wa muhimu sana kuliko sherehe.

**24:55"siku kumi, zisipungue"** Vitabu vitano vya mwanzo vya Kisamaria vina neno "mwezi."

**24:56** Mtumishi alihitaji kuondoka kwa haraka. Huyu alitaka kuikamilisha kazi yake haraka iwezekanavyo.

1. "nipeni ruhusa niende kwa bwana wangu," mst. 54, BDB 1018, KB 1511, *Piel* SHURUTISHI
2. "msinikawilishe," mst. 56, BDB 29, KB 34, *Piel* ISIYO TIMILIFU inatumika katika maana AMRISHI
3. "niruhusuni niende," sawa na #1
4. "ya kwamba niruhusuni niende kwa bwana wangu," BDB 229, KB 246, *Qal* ya KITENZI CHENYE KUSIHI

**24:58 "Wakamwita Rebeka wakamwuliza, Je! Utakwenda na mtu huyu?' Akasema, Nitakwenda'"** Tunajifunza kutoka katika vigae vya Nuzi kwamba ridhaa ya msichana ilihitajika. "Nitakwenda" ni *Qal* ya KAULI YA KUSIHI (BDB 981, KB 1371).

**24:59 "yaya wake"** Tunajifunza kutokana na Mwa. 35:8 kwamba jina lake lilikuwa "Debora" na aliishi kwa muda mrefu na alimtumika Rebeka. Hili neno "yaya" (BDB 413, KB 416, *Hiphil* HALI ENDELEVU) linatokana na KITENZI "kunyonya"(BDB 413), hili linaweza kuwa la kifasihi au stiari la msaidizi wa mtu. Kutokana na mst. 61 tujajifunza kwamba kulikuwa na watumishi wengine.

**24:60** Hii gharama ya ushairi huu mzuri ni sawa na maneno ya Mungu ambayo yamenukuliwa katika Mwa. 22:17. Walimuomba Mungu kwa niaba ya vizazi vingi na ushindi wa kijeshi.

**23:61** Hapo awali ngamia walitumika kubeba mahari na zawadi kwa ajili ya Rebeka, kwa namna nyingine walitumika kumbeba Rebeka, watumishi wake, na vitu vyao.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24: 62-67**

**[62] Basi Isaka alikuwa amekuja kwa njia ya Beer-lahai-roi, maana alikaa katika nchi ya kusini. [63] Isaka akatoka ili kutafakari kondeni wakati wa jioni; akainua macho yake, akaona, kuna ngamia wanakuja. [64] Rebeka akainua macho, naye alipomwona Isaka, alishuka juu ya ngamia. [65] Akamwambia mtumishi, Ni nani mtu huyu ajaye kondeni kutulaki? Mtumishi akasema, Huyu ndiye bwana wangu. Basi akatwaa shela yake akajifunika. [66] Yule mtumishi akamwambia Isaka mambo yote aliyoyatenda. [67] Isaka akamwingiza Rebeka katika hema ya mama yake, Sara, akamtwaa Rebeka, akawa mkewe, akampenda; Isaka akafarijika kwa ajili ya kufa kwa mamake.**

**24:62 "**Beer- lahai-roi**"** Hili lilikuwa neno ambalo lilimaanisha "Mtu mwenye afya njema aishiye kwa kuniona" (TUNGO BDB 97 na BDB 91). Hili ni jina la chemchemi ambayo malaika wa Bwana alimwonyesha Hajiri katika Mwa. 16:14.

◙
**24:63**
**NASB, NKJV "kutafakari"**
**NRSV, TEV,**
**NJB, JPSOA "tembea"**

Hili ni neno nadra la Kiebrania (BDB 1001 I au BDB 962) lililotumika katika Maandiko ya Kiebrania. Nadharia mbalimbali zinazohusiana na maana yake ni:

1. kwa kufuata Agano la Kale la Kiebrania na Toleo la Kilatini, hili linamaanisha "kufikiri." Kuna neno linalofana sana katika Kiebrania ambalo linamaanisha "kutafakari" (BDB 967, kama vile Zab. 105:2; 119:15, 23).
2. hili neno linaweza kumaanisha "mtu kutembea mwenyewe huku na huko akiwa kimya" kama Hajiri alivyofanya katika eneo hili hili (sura ya 16).
3. Toleo la Targum la Onkelos inalitafsri neno hili kama "kuomba." Hii nafasi ya tatu ya uchaguzi inafuatiwa na Vitabu Vitano vya mwanzo vya Kisamaria, Kimchi, Rashi na Luther.

**24:64 "alishuka"** Kiuhalisia neno hili linamaanisha "kuanguka" (BDB 656, KB 709, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) Kiutamaduni hili lilikuwa sahihi na kwa wanawake ilikuwa kawaida yao kuanguka toka juu ya mnyama pale waonapo wanaume.

**24:65 "akatwaa shela yake akajifunika"** Hii ilikuwa ishara ya (1) ya heshima kwa Isaka; (2) ndoa kwa Isaka; au (3) ya kwamba alikuwa hajaolewa.

**24:67** "**Isaka akamwingiza Rebeka katika hema ya mama yake, Sara"** Huyu alikuwa wa muhimu kwa sababu Sara alikuwa amekufa miaka mitatu iliyopita na Isaka alikuwa bado akiomboleza. Uzuri na heshima ya hema ya Sara ilikuwa njia ya kumkaribisha mke mtarajiwa kwa namna ya kustaajabisha.

◙ **"Isaka akafarijika kwa ajili ya kufa kwa mamake"** Mstari huu unaonekana kumaanisha kwamba Isaka bado alikuwa akiendelea kuomboleza juu ya kifo cha mamaye na hili linaweza kuiathiri njia ile tunayoitumia kulifasiri neno "kutafakari" katika mst. 63.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Ibrahimu hakumtaka Isaka kumuoa Mkanaani?
2. Je! Imani ya mtumishi huyu inaonekana kwa namna gani au haionekani katika sura hii?
3. Je! mtu aweza kuzungumza nini juu ya mwonekano wa Labani kutoka mistari ya 29 na kuendelea?
4. Ni umuhimu gani wa Rebeka kuitwa bikra katika mstari wa 16 na msichana wa kwanza katika mstari wa 43?
5. Ni kwa nanmna gani faraja ya Isaka na Rebeka inaonekana kuakisiwa kwa kila mtu katika mistari ya 61-67?

# MWANZO 25

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Kifo cha Ibrahimu | Ibrahimu na Ketura | kifo cha Ibrahimu | uzao mwingine wa Ibrahimu | uzao wa Ketura |
| 25:1-6 | 25:1-6 | 25:1-6 | 25:1-4 | 25:1-4 |
| | | | 25:5-6 | 25:5-6 |
| | Kifo na maziko ya Ibrahimu | | kifo na maziko ya Ibrahimu | kifo cha Ibrahimu |
| 25:7-11 | 25:7-11 | 25:7-11 | 25:7-11 | 25:7-11 |
| Uzao wa Ishmaeli | Familia za Ishmaeli na Isaka | | uzao wa Ishmaeli | uzao wa Ishmaeli |
| 25:12-18 | 25:12-18 | 25:12-18 | 25:12-18 | 25:12-16 |
| | | | | 25:17 |
| | | | | 25:18 |
| Wana wa Isaka | | mvutano kati ya Yakobo (Israeli) na Esau (Edomu) | kuzaliwa kwa Esau na Yakobo | Kuzaliwa kwa Esau na Yakobo |
| 25:19-26 (23) | 25:19-26 (23) | 25:19-26 (23) | 25:19-23 (23) | 25:19a |
| | | | | 25:19b-23 (23) |
| | | | 25:24-26 | 25:24-28 |
| | | | Esau anauza haki zake Kama mzaliwa wa Kwanza | |
| 25:27-34 | 25:27-28 | 25:27-28 | 25:27-28 | |
| | Esau anauza haki yake | | | Esau anaachia haki Yake ya uzaliwa |
| | 25:29-34 | 25:29-34 | 25:29-30 | 25:29-34 |
| | | | 25:31 | |
| | | | 25:32 | |
| | | | 25:33a | |
| | | | 25:33b-34 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:1-6**
**[1] Ibrahimu alioa mke mwingine jina lake akiitwa Ketura. [2] Akamzalia Zimrani, na Yokshani, na Medani, na Midiani, na Ishbaki, na Sua. [3] Yokshani akamzaa Sheba, na Dedani; na wana wa Dedani walikuwa Waashuri na Waletushi, na Waleumi. [4] Na wana wa Midiani walikuwa, Efa, na Eferi, na Hanoki, na Abida, na Eldaa. Hao wote walikuwa ni wana wa Ketura. [5] Ibrahimu akampa Isaka yote aliyokuwa nayo. [6] Lakini wana wa masuria aliokuwa nao Ibrahimu, Ibrahimu akawapa zawadi, naye akawaondoa katika mahali alipokaa Isaka mwanawe, wakati wa uhai wake, waende pande za mashariki, mpaka nchi ya Kedemu.**

**25:1 "Ibrahimu alioa mke mwingine jina lake akiitwa Ketura"** Desturi za Kiyahudi zinasema hili lilikuwa ni jina lingine la Hajiri (kama vile mstari wa 12), lakini wingi wa neno "suria" (BDB 811) unapatikana katika mstari wa 6 unaonekana kwenda kinyume kuhusu hili. Luther anadhania kuwa Ibrahimu labda alifanya hivi ili kutimiza Mwanzo 17:4. Haijulikani ikiwa Ibrahimu alimuoa Ketura baada au kabla ya kifo cha Sara. Mfuatano wa matukio ni moja ya sifa na alama ya maandiko ya kihistoria ya magharibi kuliko mashariki, maandiko ya kihistoria ya mashariki. Jina Ketura (BDB 882) linamaana "aliyepakwa marashi" au "aliyefungiwa katika moshi wa ubani!"

**25:2 "Akamzalia"** Huu ni mfululizo wa makabbila ya kiarabu yaliyothabiti kweli kweli. Linalojulikana zaidi ni Wa-Midiani (kama vile Mwanzo 36:35; 37:28; Kut. 2:15,16; 3:1; 18:1; Hes. 25:15; 31:3,8,9; Waamuzi 6-8). Jedwali bora kabisa la makabila haya ya kiarabu inaweza kupatikana katika Fasiri ya Mwanzo ya Leupold (commentary on Genesis, vol. 2, ukurasa wa 690).

**25:4 "Na wana wa Midiani walikuwa"** Mstari wa 4 unaorodhesha watoto wa makabila haya mashuhuri zaidi. Tunasikia juu ya kabila hili la baadaye la baba mkwe wake na Musa, Yethro, aliyekuwa wa kabila la wa-Kanaani au wa-Midiani.

**25:6 "Lakini wana wa masuria"** I Nyakati 1:32 pia inamuita Ketura suria.

◙**"naye akawaondoa katika mahali alipokaa Isaka mwanawe, wakati wa uhai wake, waende pande za mashariki,"** Kama Ibrahimu mapema alivyokuwa amemtoa mtoto wa Hajiri Ishmaeli aende zake mbali (kuelekea Misri), sasa anawafukuza tena watoto wa kiume wa Ketura mbali (kuelekea mashariki mwa Kanaani). Tunajua kutokana na Ubamba wa maandiko ya Nuzi, ambayo yanaelezea mila za wa-Hurri, kwamba hii ilikuwa njia inayokubalika kisheria kwa baba kuchagua mrithi wa mali na kushughulikia watoto wa suria wasio wa kisheria kwa asilimia mia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25: 7-11**
**[7] Hizi ndizo siku za miaka ya maisha ya Ibrahimu alizoishi, miaka mia, na sabini na mitano. [8] Ibrahimu akafariki, naye akafa katika uzee mwema, mzee sana, ameshiba siku, akakusanyika kwa watu wake. [9] Isaka na Ishmaeli wanawe wakamzika katika pango ya Makpela, katika shamba la Efroni bin Sohari Mhiti, lielekealo Mamre. [10] Katika lile shamba alilolinunua Ibrahimu kwa wazawa Hethi, huko ndiko alikozikwa Ibrahimu na Sara mkewe. [11] Ikawa, baada ya kufa kwake Ibrahimu, Mungu akambariki Isaka mwanawe. Naye Isaka akakaa karibu ya Beer-lahai-roi.**

**25:7 "Hizi ndizo siku za miaka ya maisha ya Ibrahimu"** Umri wa maisha ya Ibrahimu ni miaka 175, ambao ulikuwa unaonekana kama umri mzuri.

**25:8 "Ibrahimu akafariki, naye akafa katika uzee mwema, mzee sana, ameshiba siku"** Tungo hii hii inatumika kumuelezea Ishmaeli katika 25:17, Isaka katika 35:29, na Yakobo katika 49:33. Huku kulikuwa ni kutimilizwa kwa ahadi ya YHWH katika 15:15. kifo hakikuwa kitu cha kuogopwa, bali kutegemewa mwishoni mwa maisha marefu (kama vile Ayubu 42:17; I Nyakati 23:1; 29:28; II Nyakati 24:15).

◙**"akakusanyika kwa watu wake"** Kwakuwa Ibrahimu kifasihi hakuzikwa pamoja na familia yake ya kiukoo (kama vile mstari wa 9), Hii lazima inamaanisha mtazamo wa maisha yao baada ya maisha ya hapa duniani. Hii ni tungo inayojirudia rudia katika Mwanzo (kama vile 25:8,17; 35:29; 49:29,33). Kwa namna fulani kulikuwa na uwepo wa ufahamu baada ya kifo ambao ulijumuisha marafiki na familia. Ufahamu wa ufunuo fulani ni mwangaza kuliko unaozimika katika Agano la Kale kuhusiana na eneo hili (tazama Zaburi 16:9-11; Ayubu 19:25-27; Isa. 26:19; Dan. 12:2-3). Angalia *Hard Sayings of the Bible*, ukurasa wa 127-129. Tunajifunza kutoka Ebr. 11:13-16 kwamba Ibrahimu alikuwa anautazamia mji ambao mjenzi wake na mtengenezaji wake ni Mungu.

Angalia Mada Maalumu: Wafu wako wapi? katika 15:15.

**25:9 "Isaka na Ishmaeli wanawe wakamzika"** Ni muhimu kwamba Isaka na Ishmaeli walikuwa kwa namna Fulani wameungana katika maziko ya baba yao. Ishmaeli alikuwa amefukuzwa katika 21:14, lakini inavyoonekana mahusiano yalikuwa yamerejeshwa katika maziko ya baba yao. Kitu hicho hicho kinatokea kwa Esau na Yakobo katika msiba wa Isaka (kama vile Mwanzo 35:29.).

◙**"pango ya Makpela"** Tunajifunza kwamba hapa mahali pa kuzikia palikuwa pamenunuliwa na Ibrahimu (kama vile Mwanzo 23:17- 18) kwa ajili ya Sara. Itaweza kuchukua ndugu wengine wa familia za wazee wa miji.

**25:11 "Naye Isaka akakaa karibu ya Beer-lahai-roi"** Eneo hili (BDB 91) linatajwa kwa kumuunganisha Hajiri (kama vile Mwanzo 16:14; 24:62). Inavyoonekana lilikuwa kusini tu mwa Beersheba katika barabara kubwa ya kuelekea Misri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:12-18**
**12 Hivi ndivyo vizazi vya Ishmaeli, mwana wa Ibrahimu, ambaye Hajiri, Mmisri, mjakazi wa Sara, alimzalia Ibrahimu. 13 Na haya ndiyo majina ya wana wa Ishmaeli, kwa majina yao, na kwa vizazi vyao. Mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, ni Nebayothi, na Kedari, na Abdeeli, na Mibsamu, 14 na Mishma, na Duma, na Masa, 15 na Hadadi, na Tema, na Yeturi, na Nafishi, na Kedema. 16 Hao ndio wana wa Ishmaeli, na hayo ni majina yao, katika miji yao, na katika vituo vyao, maseyidi kumi na wawili kwa kufuata jamaa zao. 17 Na hii ndiyo miaka ya maisha ya Ishmaeli, miaka mia na thelathini na saba. Akakata roho, akafa, akakusanyika kwa watu wake. 18 Wakakaa toka Havila mpaka Shuri, unaoelekea Misri, kwa njia ya kwenda Ashuru. Akakaa katikati ya ndugu zake wote.**

**25:12 "Hivi ndivyo vizazi vya"** Hii ni tungo ya kitabia ya kitabu cha Mwanzo, imetumika mara kadhaa kukigawa kitabu katika historia za maisha za watu kadhaa tofauti tofauti. Wale ambao kwa bahati tu wameunganishwa na agano walipewa nafasi kidogo zaidi (yaani Ishmaeli) kuliko wale ambao kipekee waliitwa kubeba ahadi ya uzao ya masihi ajaye (kama vile Mwanzo 5:1; 6:9; 10:1; 11:10,27; 25:12,19; 36:1,9; 37:2).

**25:13 "Kedari"** Hili ni kabila tawala la Ishmaeli (BDB 871, kama vile Isa. 21:16-17; 42:11; Yer. 2:10; 49:28; Zab. 120:5). Makabila ya Ishamaili yanaonekana kuwa mahali pa mashariki na kusini mwa makabila ya wana wa Ketura.

**25:15 “Tema”** Hii ni chemichemi katika kaskazini mashariki mwa Arabia ambayo baadaye ilifanyika shabaha ya mungu mwezi wa kike, *Zin.* Angalia Mada Maalumu katika 12:4. Neno “Tema” linamaana “jangwa” (BDB 1066).

**25:16 “maseyidi kumi na wawili”** Hii inaonekana kutimilizwa kwa Mwanzo 17:20. Hili ni neno la cheo cha heshima cha uongozi, ni kama neno la kisasa, Shehe kati ya makabila ya kiarabu. Hesabu ya namba “kumi na mbili” inaonekana kuwa namba ya kufaa na ya kupendeza ya watoto: Nahori ana watoto kumi na mbili (kama vile Mwanzo 22:20-24); Ishmaeli ana watawala wa makabila kumi na mbili (kama vile Mwanzo 17:20; 25:16); Esau ana makabila kumi na mbili (kama vile Mwanzo 36:15-19); hapa, na baadaye Yakobo atakuwa na watoto kumi na mbili (kama vile Mwanzo 35:22). Yawezekana ni hesabu ya uwakilisho wa mpangilio wa ushirika mzuri.

## MADA MAALUM: NAMBA KUMI NA MBILI

Kumi na mbili mara nyingi imekuwa kiishara namba ya shirika

A. Nje ya biblia
   1. Ishara kumi na mbili za zodiaki
   2. Miezi kumi na miwili ya mwaka
B. Katika Agano la Kale (BDB 1040 kuongeza 797)
   1. wana wa Yakobo (Makabila ya Kiyunani)
   2. waliotazamishwa kwenye
      a. Nguzo kumi na mbili za madhabahu katika Kut. 24:4
      b. Vito kumi na viwili juu ya kifua cha kuhani mkuu (ambayo vinasimama kwa niaba ya makabila) katika Kut. 28:21
      c. unga mwembamba wa mkate kimi na miwili katika sehemu takatifu ya kibanda katika Law. 24:5
      d. wapelelezi kumi na wawili waliotumwa huko Kanaani katika idadi ya kabila (mmoja kutoka katika kila kabila)
      e. fimbo kumi na mblili (viwango vya kikabila) katika uasi wa Kora katika Hes. 17:2
      f. mawe kumi na mawili ya Yoshua katika Yos. 4:3,9,20
      g. majimbo kumi na mawili ya kiutawala katika utawala wa Suleimani katika 1 Fal. 4:7
      h. mawe kumi na mawili ya madhabahu ya YHWH katika 1 Fal. 18:31
C. Katika Agano Jipya
   1. Mitume kumi na wawili waliochagulwa
   2. Vikapu kumi na iwili vya mikate (kimoja kwa kila Mtume) katika Mt. 14:20
   3. Viti kumi na viwili vya enzi ambapo Wanafunzi wa Agano Jipyala wamekaa (vinayorejea juu ya makabila 12 ya Israeli) katika Mt. 19:28
   4. majeshi kumi na mbili ya malaika wa kumsaidia Yesu katika Mt. 26:53
   5. Ishara ya Ufunuo
      a. Wazee 24 juu ya viti 24 4:4
      b. 144,000 (12 x 12,000) katika 7:4; 14:1,3
      c. nyota kumi na mbili juu ya taji la mwanamke katika 12:1
      d. malango kumi na mawili, malaika kumi na wawili wakiakisi makabila kumi na mawili katika 21:12
      e. Mawe kumi na mawili ya misingi ya Yerusalemu mpya na juu yao majina ya mitume kumi na mawili katika 21:14
      f. Mianzi kumi na mbili elfu katika 21:16 (kipimo cha mji mpya, Yerusalemu Mpya)
      g. kuta ni dhiraa 144 katika 21:17
      h. malango kumi na mawili ya lulu katika 21:21
      i. miti mipya katika Yerusalemu yenye aina aina kumi na mbili za tunda (moja kwa kila mwezi) katika 22:2

**25:17 "Akakata roho,"** Neno "akapumua" (kifasihi "akamaliza muda wake," גוע, BDB 157, KB 184, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Mwanzo 6:17; 7:21; 25:8,17; 35:29) inatumika mara kwa mara na zaidi katika Mwanzo, Hesabu, na maandiko ya kishairi. Maana yake ya msingi ni kuwa tupu (yaani kutoa pumzi kutoka katika mwili).

**25:18** Hili eneo lilikuwa linahusika na kusimamia njia za usafiri kutokea Misri mapaka Ashuru/Babeli. Ilikuwa sehemu sahihi kwa watu wa kuhama hama, walioishi kwenye mahema.

◙**"Akakaa katikati ya ndugu zake wote"** Tungo "katika uasi" (BDB 815-819) ina uwanja mpana kimaana. Maana yake ya kimsingi ni "uso," "uwepo," au kisitiari "kabla." Inatumika mapema katika mstari huu kumaanisha "juu dhidi ya" au "kinyume" eneo la kijiografia, lakini hapa linamaanisha upinzani kwa watu wengine.

Huku ni kutimilizwa kwa Mwanzo 16:12, ambayo inaelezea mtazamo wa Ishmaeli wa kutokuwa na ukarimu, kuhama hama na ndugu zake. Hii tungo inafasiriwa katika namna nyingi mbali mbali. Inawezekana kwamba hii inamaanisha kuvamia kijeshi dhidi ya ndugu walioko karibu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:19-26**
**[19] Na hivi ndivyo vizazi vya Isaka, mwana wa Ibrahimu. Ibrahimu alimzaa Isaka. [20] Isaka akawa mwenye miaka arobaini alipomtwaa Rebeka binti Bethueli, Mshami, wa Padan-aramu, ndugu wa Labani, Mshami, kuwa mke wake. [21] Isaka akamwomba Bwana kwa ajili ya mke wake, maana alikuwa tasa. Naye Bwana akamwitikia, na Rebeka mkewe akachukua mimba. [22] Watoto wakashindana tumboni mwake. Naye akasema, Ikiwa ni hivi, kuishi kwanifaa nini? Akaenda kumwuliza Bwana. [23] Bwana akamwambia, Mataifa mawili yamo tumboni mwako,Na kabila mbili za watu watafarakana tangu tumboni mwako.Kabila moja litakuwa hodari kuliko la pili,Na mkubwa atamtumikia mdogo. [24] Siku zake za kuzaa zilipotimia, tazama! Mapacha walikuwamo tumboni mwake. [25] Wa kwanza akatoka, naye alikuwa mwekundu mwili wote kama vazi la nywele. Wakamwita jina lake Esau. [26] Baadaye ndugu yake akatoka, na mkono wake unamshika Esau kisigino. Akaitwa jina lake Yakobo. Isaka alikuwa mwenye miaka sitini mkewe alipowazaa.**

**25:19 "hivi ndivyo vizazi vya Isaka"** Hii ni tabia ya tungo zilizojadiliwa katika mstari wa 12, lakini hapainahusiana na muweka agano na hivyo kupanuliwa sana.

◙**"mwana wa Ibrahimu. Ibrahimu alimzaa Isaka"** Huku ni kurudiwa kwa kauli kusiko kwa kawaida. Rashi anasema kwa kurudiwa huku mara mbili kulitumika kuondoa uvumi kuwa Isaka alikuwa mtoto wa Abimeleki (kwa tumbo la Sara). Walimu wa kiyahudi pia walisema kwamba Isaka alikuwa na mwonekano kama wa Ibrahimu ili kuondoa uvumi ambao ulikuwa umeanzishwa kwa tukio la Mwanzo 20:1-18.

**25:20 "Isaka akawa mwenye miaka arobaini alipomtwaa Rebeka"** Mtu anapolinganisha Mwazo 25:20 pamoja na mstari wa 26 Ni wazi kwamba Isaka alikuwa na miaka sitini wakati wa kuzaliwa kwa Yakobo.

◙ **"Bethueli, Mshami, wa Padan-aramu,"** Neno "Shamu" mara nyingi linafasiriwa kama "Armenia" (BDB 74). Inaonekana kuwa eneo la wilaya linalozungukwa na Harani. Paddan-aramu (BDB 804 and BDB 74) ikimaanisha "uwanda wa Aramu," ambalo linaashiria eneo lilelile "Aram-naharaimu" ya 24:10.

**25:21 "Isaka akamwomba Bwana kwa ajili ya mke wake, maana alikuwa tasa"** Kulikuwa na makusudi mawili ya kithiolojia ya wazee hawa wa miji kuwa hali ya utasa (BDB 785) wake zao: (1) kuonesha utoshelevu wa Mungu (2) kuonesha kwamba jambo hili halikutokea tu kwa juhudi za mwanadamu, lakini kwa neema na sio kwa kustahili. Walimu wa kiyahudi hutumia maandiko haya kuweka msisitizo juu ya nguvu ya maombezi.

**25:22 "Watoto wakashindana tumboni mwake"** KITENZI hiki cha nguvu (BDB 954, KB 1285, *Hithpolel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Kinafasiriwa (NIDOTTE, juzuu ya 3, 1191)

1. katika *Qal* shina kama kuponda, kuvunja, kutumia vibaya
2. katika *Niphal* shina kama kuweka ufa, kuvunja
3. katika *Hiphil* and *Piel* shina kama kuponda katika vipande vipande
4. katika *Polel* kama kutesa
5. katika *Hithpolel* kama kupondana

Hii ilikuwa ni kivuli kijacho cha mbeleni kinachohusiana na mstari wa 23.

◙**"naye akasema, 'Ikiwa ni hivi, kuishi kwanifaa nini?'"** Kumekuwa na majadala mkubwa juu ya tungo hii ya kinahau yenye utata (kifasihi "kwa nini hivi, mimi?"). Nadharia zilizopo ni:

1. Alikuwa anauliza kwanini amefanywa kuwa na ujauzito na Mungu alafu anapitishwa katika matatizo makali ya namna hiyo; Kwa wakati huu hakuwa anajua kuwa amebeba mapacha.
2. Ujauzito wake ulikuwa unamsababishi amaumizu makali saa na akawa anaduwaa kwa nini aliomba hata hali hii.
3. Alikuwa na hofu kwa ajili ya maisha yake katikati ya tatizo la ujauzito.
4. Aliogopa kwamba labda tatizo hili lingeweza kuendelea hata baada ya kuwa amejifungua. Ujauzito wenye matatizo ilikuwa ni ishara ya tatizo litakalotokea baadaye (kivuli cha baadaye).

◙**"Akaenda kumwuliza Bwana"** Hili pia limesababisha mjadala mkubwa kati ya wafasiri. Wanauliza alipokwenda na kwamba alimuuliza nani! Ni dhahiri kwamba maandiko hayakuandika hili. Wengine wanaeleza kwamba kulikuwa na mahali palipoandaliwa ambapo wazee wa Miji walienda kuabudu. Kumekuwa na madhanio mengi juu ya nani alimuuliza.

1. Luther anasema kuwa alimuuliza Shemu
2. Walimu wa sheria wanaserma kuwa alimuuliza Melkizedeki
3. wengine wanasema kuwa alimuuliza Ibrahimu
4. bado wengine wanaamini kwamba ilikuwa ni Isaka
5. yawezekana, ilikuwa ni maombi binafsi tu katika madhabahu ya nyumbani (yawezekana hata dhabihu)

Inawezekana kwamba andiko hili na 28:22 inamaanisha wahudhuriaji watakatifu katika maeneo ya ibada (yaani makuhani, Roland deVaux, *Ancient Israel*, vol. 2, ukurasa wa 345)

**25:23 "Bwana akamwambia,"** Hili ni neno muhimu sana la kiushairi kutoka kwa Bwana kwenda kwa Rebeka. Mungu alikuwa amekwisha ahidi watoto kwa Isaka (kama vile Mwanzo 17:19; 21:12). Unabii huu kibayana unasawiri ni nani mmojawapo kati ya watoto ambaye angeweza kubeba uzao wa familia. Hii inanukuliwa katika Rum. 9:10-12. Mtu anaweza kushangaa kwanini Isaka hakuonekana kufuata neno hili kutoka kwa Bwana, kwa maana iko wazi kuwa Rebeka alimshirikisha wakati alipojaribu kumfanya Esau kuwa mrithi katika sura za 26 na 27.

◙**"Na mkubwa atamtumikia mdogo"** Kama wake tasa wa wazee wa miji tungo hii inaonesha kwamba uzao uliohaidiwa hautakuja kwa namna ya kawaida kama wa-Semiti walivyo rithisha haki (kama vile Rum. 9:10-12).

**25:25 "Wa kwanza akatoka, naye alikuwa mwekundu"** Neno hili (*admoni*, BDB 10, "mwekundu") linahusiana na neno katika Mwanzo linalozungumza juu ya "vumbi" (BDB 9) ambalo Mungu alitumia kumuumbia mwanadamu (kama vile Mwanzo 2:7), ile "Adama," ambayo inavyoonekana ina mzizi wa wazo la "uwekundu" (BDB 10). Mzaha wa kimaneno unaendelea katika mstari wa 30, ambapo uji mwekundu (BDB 10) unaunganishwa kwa "Edomu" (BDB 10), ambalo kutokana na hilo tunapata taifa ambalo lingetoka kwa Esau.

◙**"kama vazi la nywele. Wakamwita jina lake Esau"** Neno "kuwa na nywele" (BDB 972) inakuwa na ufanano wa karibu sawa na neno "Seir" (BDB 973), ambalo ni jina la mwanzoni kwa ajili ya Edomu. Kuna mzaha wa mara mbili juu ya maneno "mwekundu" na "yenye nywele" na "Esau" na "Edomu."

Maelezo haya ya kiebrania juu ya mtoto kuwa mwekundu na mwenye nywele inaweza isilete kisawe kwa wasomaji wa kisasa. Hii haikumaanisha hata kidogo kuleta maana hasi. Neno "yenye nywele" (BDB 12) ilimaanisha vazi zuri lenye mwonekano wa kupendeza (mfano Josh. 7:21,24 au koti/vazi la kinabii (kama vile I Wafalme 19:13,19; II Wafalme 2:8,13,14).

**25:26 "Baadaye ndugu yake akatoka, na mkono wake unamshika Esau kisigino. Akaitwa jina lake Yakobo"** Jina Yakobo (BDB 784) lina husiano na "kisigino" (BDB 784). Kutoka Hosea 12:3 na kutokana na maneno ya Esau katika mwanzo 27:36 tunatambua kwamba jina Yakobo linakua kwenda katika "mchukua nafasi" au "mnyang'anyi" (kutoka katika KITENZI na KIVUMISHI, BDB 784). Haitokei mpaka mkabiliano pamoja na Mungu katika kijito Yaboki miaka ya baadaye kwamba jina hili litabadilishwa kuwa "Israeli" (kama vile Mwanzo 32:28) na kwa maana ya tabia yake.

◙**"Isaka alikuwa mwenye miaka sitini mkewe alipowazaa"** Inatakiwa izingatiwe kwamba alikuwa amekwisha subiri miaka ishirini baadaye, katika imani kwa mtoto huyu aliyehaidiwa. Mungu alikuwa anamjaribu Isaka kwa nama ileile aliyomjaribu Ibrahimu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:27-34**
**[27] Watoto wakakua, Esau alikuwa mtu ajuaye kuwinda wanyama, mtu wa nyikani, na Yakobo alikuwa mtu mtulivu, mwenye kukaa hemani. [28] Basi Isaka akampenda Esau, kwa sababu alikula mawindo yake, na Rebeka akampenda Yakobo. [29] Yakobo akapika chakula cha dengu. Esau akaja kutoka nyikani, naye alikuwa amechoka sana. [30] Esau akamwambia Yakobo, Tafadhali, unipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi. Kwa hiyo walimwita jina lake Edomu. [31] Yakobo akamwambia, Kwanza niuzie leo haki yako ya mzaliwa wa kwanza. [32] Esau akasema, Tazama, mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi? [33] Yakobo akamwambia, Uniapie kwanza. Naye akamwapia, akamwuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza. [34] Yakobo akampa Esau mkate na chakula cha dengu, naye akala, akanywa, kisha akaondoka, akaenda zake. Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza.**

**25:27 "Watoto wakakua, Esau alikuwa mtu ajuaye kuwinda wanyama, mtu wa nyikani, na Yakobo alikuwa mtu mtulivu, mwenye kukaa hemani."** Shabaha ya kifungu hiki cha habari ni kwamba walikuwa tofauti sana katika haiba zao. Esau aliridhika kuwa mbali na nyumbani; Yakobo aliridhika kuwa nyumbani. Yakobo ndiye aliyetimiza matarajio ya kawaida ya kuhamahama ya umbo la wazee wa mji.
Neno "kwa amani" (NKJV "upole"; NRSV na TEV "kwa ukimya") kwa ukweli ni "ukamilifu" (BDB 1020). Hapa inaonekana kumaanisha kiongozi wa kawaida, mkamilifu na mwenye kuhamahama. KIVUMISHI kilekile kinatumika kuelezea heshima ya Ayubu (kama vile 1:1,8; 2:3; 8:20; 9:20,21,22, pia tazama Zab. 37:37; Mithali 29:10).

**25:28 "Basi Isaka akampenda Esau, kwa sababu alikula mawindo yake"** Isaka alikuwa mpole, mtu mwenye amani na inawezekana kwamba mtoto wake wa kiume alikuwa vile ambavyo asingepaswa.Inashangaza kwamba Esau alikuwa kipenzi chake wakati kiuwazi alijua neno la kiungu kutoka Mwanzo 25:23.

◙**"lakini Rebeka akampenda Yakobo"** Hali ya ubaguzi na upendeleo inakwenda kusababisha machafuko na matatizo makubwa kama ambavyo huwa inasababisha. Lakini inaonekana kwamba Rebeka alikuwa anajaribu kuvumilia mpaka kwenye ahadi ya kiungu ya mstari wa 23.

**25:29** Mtu anaweza akashangaa ikiwa tukio hili lilikuwa limefikiriwa na kufanyiwa tafakari kwanza na kurudiwa. Je Yakobo alikuwa anasubiria fursa kama hii? Matumizi ya neno "kupika" (kifasihi "kuchemsha," BDB 267, KB 268,

*Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inaweza kuwa kidokezo. Mara kwa mara neno lilimaanisha kufikiria kabla kuwa na haki ambazo kisheria sio zao (NIDOTTE, vol. 1, ukurasa wa 1094).

Inavyoonekana mlo huu ulikuwa umeandaliwa umbali kutoka katika eneo la kambi. Mlo huu uliitwa

1. "mchemsho," mstari wa 29, BDB 268, sufuria la maharage lililochemshwa, kama vile II Wafalme 4:38
2. "mchemsho wa dengu," mstari wa 30, BDB 10
3. "mchemcho wa dengu," mstari wa 34, BDB 727, kama vile II Sam. 17:28; 23:11; Ezek. 4:9

**25:30 "Tafadhali, unipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi"** Hili ni neno lenye nguvu kwa "kula." Kifasihi lina maana "kubwia kwa pupa" (BDB 542, KB 533, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI). Hakika Esau hakuwa katika nafasi ya kufa na njaa, lakini alikuwa amechoka (BDB 746, kama vile Kumb. 25:18; Waamuzi 8:4-5). Hii ni moja ya dondoo ya kwanza kati ya kadhaa ambayo inamuonesha kuwa Esau hakuwa mtu mbaya, lakini mwenye akili za kidunia (angalia *Hard Sayings of the Bible*, ukurasa wa 347-348). Vitu vya imani na majukumu ya maisha ya nyumbani havikuwa vitu vya msingi vyenye tija kwake.

**25:31,33** Yakobo akasema, "Kwanza niuzie mimi haki ya uzaliwa wako wa kwanza. . .kwanza uniapie"

1. "niuzie," BDB 569, KB 581, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "niapie," BDB 989, KB 1396, *Niphal* KAULI SHURUTISHI

Ni wazi kuwa Yakobo alimshinda Esau penye udhaifu wake. Swali ni kwamba, je ilikuwa ni kwasababu ya (1) unabii (kama vile 25:23), (2) au ustawi wa familia, au (3) utashi na maslahi binafsi?

**25:32 "Tazama, mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi?"** Hii imefasiriwa kimsingi katika njia tatu tofauti: (1) utiaji chumvi; (2) kwamba ni kweli alikuwa anategemea kufa (BDB 559, KB 562, *Qal* KITENZI JINA) katika umri mdogo au (3) mfano mwingine wa kukosa kwake hali ya kujali mambo ya rohoni. Kutoka katika ubamba wa maandiko ya Nuzi ya kipindi hicho hicho tunaweza kuelewa kwamba kuhamisha haki ya uzaliwa wa kwanza ilikuwa inaweza kufanyika kisheria. Pia tunaona kwamba lazima ingeweza kuwa kutokea kunakofanana kwasababu imezuiliwa katika Kumb. 21:15-17. Baadaye, nafasi ya Reubeni itachukuliwa na Yuda. Yakobo inawezekana amekuwa akifuatilia katika namna isiyokuwa sahihi juu ya amri ya kiungu mstari wa 23. Ni vigumu kusoma ufahamu wa Yakobo katika masimulizi haya kwakuwa mara kwa mara anakutana na mtu mkweli lakini mwenye hila.

**25:34** Mstari huu unaoelezea matendo ya Esau inaweza kuwa njia ya kuelezea umoja wake na haiba yake ya kutokuwa karibu (kutojichanganya) na jamii.

1. "alikula," BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. "alikunywa," BDB 1059, KB 1667, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. "aliinuka," BDB877, KB 1086, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. "alikwenda katika njia yake," BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
5. "akaidharau haki yake ya uzaliwa," BDB 102, KB 117, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

◙**"Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza"** Kitenzi (BDB 102, KB 117, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inaashiria "kuona kama sio kitu" au hata "kuangalia kwa chuki." Walimu wa Kiyahudi wanamuelezea Esau kama mtu muovu sana. Waebrania 12:16 inamuonesha kama mtu ambaye hajakomaa kiroho. Aliichukulia maisha yake ya kiroho na maisha yake ya kifamilia kwa wepesi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Mstari wa 8 unasema nini juu ya mtazamo wa kale juu ya kifo?
2. Kwa nini wake mababa wa imani wengi ni tasa?
3. Kwanini mstari wa 23 ni muhimu sana?
4. Ipi ni asili maarufu iliyomo katika mstari wa 25?
5. Je tunaweza kujua nia  na tabia za kisaikolojia za Esau na Yakobo? HowKwa namna gani?
6. Orodhesha njia ambazo kitabu cha Waebrania kinafasiri masimulizi haya katika sura ya 11 na 12.

# MWANZO 26

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Isaka afanya makazi Gera | Isaka na Abimeleki | Habari kuhusu Isaka | Isaka aishi huko Gera | Isaka huko Gera |
| 26:1-5 | 26:1-5 | 26:1-5 | 26:1-5 | 26:1-6 |
| 26:6-11 | 26:6-11 | 26:6-11 | 26:6-9a | |
| | | | 26:9b | |
| | | | | 26:7-11 |
| | | | 26:10-11 | |
| 26:12-17 | 26:12-16 | 26:12-16 | 26:12-15 | 26:12-14 |
| | | | | Visima kati ya Gera na Beersheba |
| | | | | 26:15-18 |
| | | | 26:16-18 | |
| Ugomvi juu ya visima | 26:17-22 | 26:17-22 | | |
| 26:18-22 | | | | |
| | | | 26:19-20 | 26:19-22 |
| | | | 26:21-22 | |
| 26:23-25 | 26:23-25 | 26:23-25 | 26:23-25 | 26:23-24 |
| (24) | | | | (24) |
| | | | | 26:25 |
| Agano na Abimeleki | | | Makubaliano kati ya Isaka na Abimeleki | Ushirikiano na Abimeleki |
| 26:26-33 | 26:26-33 | 26:26-33 | 26:26-27 | 26:26-30 |
| | | | 26:28-31 | |
| | | | | 26:31-33 |
| | | | 26:32-33 | |
| | | | Wake wa Esau kutoka nchi ya kigeni | Wake wa Esau wa kabila la Wahiti |
| 26:34-35 | 26:34-35 | 26:34-35 | 26:34-35 | 26:34-35 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## MAELEZO YA NYUMA

A. Hii ndiyo sura pekee katika kitabu cha Mwanzo pale ambapo Isaka ndiyo mhusika mkuu.
B. Isaka anakuwa, katika sura hii, mtu pekee wa tofauti, anayeaminika na wa ki-Mungu. Sio mhusika wa moja kwa moja kama Ibrahimu na Yakobo, lakini mfuasi mwaminifu wa YHWH.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:1-5**
**1 Ikawa njaa katika nchi hiyo, mbali na njaa ile ya kwanza iliyokuwa siku za Ibrahimu. Isaka akamwendea Abimeleki, mfalme wa Wafilisti, huko Gerari. 2 Bwana akamtokea, akasema, Usishuke kwenda Misri, kaa katika nchi nitakayokuambia. 3 Kaa ugenini katika nchi hiyo, nami nitakuwa pamoja nawe, na kukubariki, maana nitakupa wewe na uzao wako nchi hizi zote. Nami nitakifanya imara kiapo nilichomwapia Ibrahimu baba yako. 4 Nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, nami nitawapa uzao wako nchi hizi zote, na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia. 5 Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu.**

**26:1 "Ikawa njaa katika nchi hiyo"** Hili linafanana na lile lililotokea katika Mwanzo 12:10 lililomlazimisha Ibrahimu kutoka katika nchi ya ahadi.

◙ **"Isaka akamwendea Abimeleki, Mfalme wa Wafilisti, huko Gerari"** Wafilisti walikuwa ni watu mamuluki toka katika kisiwa cha Aegean. Walijaribu kuivamia Misri, walitimuliwa na kukimbilia Kusini Magharibi mwa Pwani ya Palestina, yapata mwaka wa 1200 K.K. Kwa sababu jina la Abimeleki limetajwa mapema katika Mwanzo 21:22, hili lawezakuwa ni jina lililozoeleka kuonyesha Wafalme wote wa Kipalestina. Huu ni mfanano wa utumiaji wa Hadad huko Shamu na Farao huko Misri.

Hakika yawezekana kuwa,

1. Palikuwepo na wafanya biashara wa Kifilisti wa mwanzo huko Kaanani
2. Kundi la Wakaanani walioambatana na Wafilisti na jina hili limepitwa na wakati.
3. Wafilisti wameorodheshwa katika Mwanzo 10:6-20 wakitokea katika uzao wa Hamu na Wakaanani, na sio Yafethi (kisiwa cha Aegean). Yawezekana jina linamaanisha kwa makundi mbali mbali yaliyohusiana na Wapalestina/Wakaanani (toleo la NIDOTTE, juzuu ya 4, uk. 1049).

**26:2-3** Kujitokeza kwa YHWH mbele ya Isaka kuna maelekezo mbali mbali na ahadi.

1. "usishuke kwenda Misri," mst. 2, BDB 432, KB 434, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU iliyotumika kwa maana ya KITENZI AMRISHI
2. "kaa katika nchi nitakayokuambia," uk. 2, BDB 1014, KB 1496, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. "kaa ugenini katika nchi hiyo," uk. 3, BDB 157, KB 184, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. "nami nitakuwa pamoja nawe," uk. 3, BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI SHURUTISHI iliyotumika kwa maana ya KUSIHI
5. "nami nitakubariki," uk. 3, BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI SHURUTISHI iliyotumika kwa maana ya KUSIHI
6. "nitakupa nchi hizi zote," uk. 3, BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI SHURUTISHI iliyotumika kwa maana ya KUSIHI

**26:2 "na Bwana akamtokea, na kumwambia, usishuke kwenda Misri'"** Hili lingewezakuwa kwa sababu ya uzoefu wa Ibrahimu huko Misri au kwa sababu ya Isaka alihitaji kumwamini Mungu kwa ajili ya utoaji katika nchi ya ahadi.

**26:3 "nitakuwa nawe na kukubariki"** Huu tena ni uthibitisho, sio tu kwa ajili ya uwepo wa Mungu (kama vile 28:15; 31:3), bali Baraka zake na uthibitisho wa mara ya pili wa ahadi zake.

◙**"nami nitafanya imara kiapo nilicho mwapia baba yako Ibrahimu"** Hii ni rejeo kwa ahadi maalum za Mungu kwa Ibrahimu ambazo zinapatikana katika Mwanzo 12,15,17 na 22.

KITENZI "nitafanya" (BDB 877, KB 1086, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kimetumika mara kwa mara katika kitabu cha Mwanzo.

1. Kufanya au kuthibitisha agano, kama vile 6:18; 9:9,11; 17:7,19,21
2. Kutoa matokeo au kulithibitisha agano, 26:3 (Law. 26:9; Kumb. 8:18)

**26:4** Kunaonekana kuwepo kwa ahadi maalum tatu zilizotajwa:

(1) kuwepo na uzao tele; (2) ardhi (kama vile 12:7; 15:18-19; 17:7-8; 26:1-5; 28:10-15; 35:12); na (3) mataifa yote yatabarikiwa kutokana na Isaka na uzao wake.

◙**"kama nyota za mbinguni"** Hili lilikuwa limekwisha kutajwa awali kwa Ibrahimu katika Mwanzo 15:5 na 22:17. Sitiari zingine mbili zilizotumiwa na Mungu kuuelezea ustawi wake zilikuwa ni mchanga wa bahari na mavumbi ya nchi.

◙ **"nchi hizi zote"** Hii ilikuwa ni sehemu ya ahadi ya Ibrahimu (kama vile 12:7; 13:15; 15:18; 17:8).

◙ **"mataifa yote ya dunia yatabarikiwa"** Kifungu hiki kiuhalisia kinatafasiliwa "watajibariki." Kuna miundo miwili tofauti ya MANENO ya ahadi hii. Neno *Niphal* linapatikana katika Mwa. 12:3; 18:18; 28:14. Pia limenukuliwa katika Agano Jipya katika Mdo.3:25; Gal. 3:8. Mwanzo 26:4 ipo katika neno *Hithpael*, ambalo linapatikana tu hapa na katika Mwanzo 22:16-18 na kwa umakini linapaswa kutafasiliwa "watajibariki."kwa ukweli, kuna tofauti ndogo kati ya "watajibariki" na "watabarikiwa." Kwa namna ya ukweli tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania haitoi utofauti kati ya miuundo ya MANENO haya. Baraka kubwa, na za wazi ni kuwa kupitia Ibrahimu na wana wake Mungu alikuwa akitafuta kuubariki ulimwengu wote. Mungu alimchagua mtu ili achague taifa na ulimwengu wote. Lazima tutambue kuwa Wayahudi walichaguliwa, na sio kwa Baraka maalum, bali kama chombo kwa ajili ya mpango wa Baraka kuwaijia watu wote. Mara zote Israeli ilimaanisha kuwa ufalme wa makuhani (kama vile Kut. 19:5-6). Angalia Mada Maalum katika 12:3.

**26:5 "Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu"** Vitenzi viwili katika mstari huu vinasisitiza dhana ya kibinadamu ya agano (kama vile 12:1; 17:1,9-14; 22:16; 26:3-5).

1. "alisikia" ( "sikia kwa ajili ya kutenda"), BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU
2. "kuhifadhi," BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU

Yote yanaonyesha kitendo endelevu.

Kuna mvutano wa kweli (na wa kimakusudi) kati ya neema iliyohuru ya Mungu iliyotolewa kwa mwanadamu/taifa kuwaita watu wote/mataifa(kama vile kitendo kisicho na masharti kuhusu Mungu katika Mwa. 15:12-21) na utajwaji wa mara kwa mara wa utii (yaani., asili ya kimasharti ya ahadi za Mungu). Yote ni kweli! utendaji wa mwanadamu haumleti mwanadamu aliyeanguka kwenye ukubarifu wa ki-Mungu. Hata hivyo, pale tu tunapokabiliana naye, hatuwezi kuona athari, mabadiliko (kama vile Efe. 1:4; 2:8-9,10). Lengo la Mungu ni kuwa watu wa haki wapate kuyavuta mataifa kumwelekea Yeye. Hatari ni neema ya bure pasipo masharti na ustahili wa neema wenye masharti mengi. Agano jipya la Yer. 31:31-34 na Ezek. 36:22-38 linatuonyesha njia-moyo mpya, mawazo mapya, na roho mpya. Muundo wa nje wa Mungu ukajakuwa ndiyo mamlaka ya ndani.

Uorodheshaji wa "gharama" (BDB 1038), "amri" (BDB 846), "matamko" (BDB 349), na "sheria" (BDB 435) yanapatikana mahali hapa tu katika vitabu vya awali vya Mwanzo-Hesabu, lakini yanajitokeza mara nyingi katika

kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Angalia Mada Maalum:Maneno kwa ajili ya Mafunuo ya Mungu yakiendelea katika aya inayofuata.

Hili linaonekana kuwa dokezo la Mwa. 15:6. Kwa habari hii, imani ya Ibrahimu kwamba atakuwa na mtoto ilichukuliwa na Mungu kama kitendo cha imani na kufikiriwa ndani ya Ibrahimu kama mtu wa haki. Umuhimu wa sura hizi za Agano la Kale unatumika kama tegemezo la kithiolojia kwa Mtume Paulo kwa ajili ya mafundisho ya kumwesabia haki kwa neema kupitia imani, na kuelezewa vizuri katika Warumi 4 na Wagalatia 2-3. Neno “sheria”hapa ni mwanzo wa utumiaji wa neno “sheria za Musa” (BDB 435), ambalo ni neno la Kiebrania lenye kumaanisha “mafundisho” au “miongozo.” Neno hili likajakuwa ni cheo kwa ajili ya vitabu vitano vya mwanzo vya Musa.

Angalia urudiwaji wa KIWAKILISHI nomino cha kibinafsi!

## MADA MAALUM: ISTILAHI KWA AJILI YA UFUNUO WA MUNGU (Kwa kutumia KUMBUKUMBU LA TORATI na ZABURI)

I. “Amri ya Serikali,” BDB 349, “fanya kuwa sheria, tamko, au agizo”
   A. JINSI YA KIKE, חק (KB, 346) – Kumb. 4:1,5,6,8,14,40,45; 5:1; 6:1,24; 7:11; 11:32; 16:12; 17:19; 26:17; 27:10; Zaburi 2:7; 50:16; 81:4; 99:7; 105:10,45; 148:6
   B. JINSI YA KIUME, חקה (KB, 347) – Kumb. 6:2; 8:11; 10:13; 11:1; 28:15,45; 30:10,16; Zab. 89:31; 119:5,8,12,16,23,26,33,48, 54,64,68,71,80, 83,112,124,135, 145,155,171

II. “Sheria,” BDB 435, KB 1710, “maelekezo”
   -Kumb.1:5;4:44;17:11,18,19;27:3,8,26;28:58,61;29:21,29;30:10;31:9; Zaburi 1:2;19:7;78:10;94:12; 105:45;119:1,18,29,34,44,51,53,55,61,70,72,77,85,92,97,109,113,126,136,142,150,153,163,165,174

III. “Shuhuda”BDB 730,KB 790, “Sheria za ki-Ungu”
   A. WINGI עדה – kumb. 4:45; 6:17,20; Zab. 25:10; 78:56; 93:5; 99:7; 119:22,24,46,59,79,95,119,125,138, 146,152,167,16
   B. עדות au עדת – Zaburi 19:7; 78:5; 81:5; 119:2,14,31,36,88,99,111,129,144,157

IV. “Maagizo” BDB 824, KB 959, “Shitaka”
   - Zaburi19:8;103:18;111:7;119:4,15,27,40,45,56,63,69,78,87,93,94,100,104,110,128,134,141,159,168,173

V. “Amri” BDB 846, KB 622
   – Kumb. 4:2,40; 5:29; 6:1,2,17,25; 8:1,2,11; 10:13; 11:13; 15:5; 26:13,17; 30:11,16; Zab. 19:8; 119:6,10, 19,21,32,35,47,48, 60,66,73,86,96,98,115,127,131,143,151, 166,176

VI. “Hukumu/Maagizo, “ BDB 1048, KB 651, “maamuzi” au “haki”
   – Kumb. 1:17; 4:1,5,8,14,45; 7:12; 16:18; 30:16; 33:10,21; Zab. 10:5; 18:22; 19:9; 48:11; 89:30; 97:8; 105:5,7; 119:7,13,20,30,39,43,52,62, 75,84,102,106,120,137, 149,156,160,164; 147:19; 149:9

VII. “Njia zake” BDB 202, KB 231, Mwongozo wa YHWH kwa maisha ya watu wake
   – Kumb. 8:6; 10:12; 11:22,28; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16; 32:4; Zab. 119:3, 5,37,59

VIII. “Maneno yake”
   A. BDB 182, KB 211 – Kumb. 4:10,12,36; 9:10; 10:4; 17:19; 18:19; Zab. 119:9,16,17,25,28,42,43,49, 57,65,74, 81,89,101,105,107,114,130,139,147, 160,161,169
   B. BDB 57, KB 67
      1. "Neno" – Kumb. 33:9; Zaburi 119:11,67,103,162,170,172
      2. "Ahadi" – Zaburi 119:38,41,50,58,76,82,116,133,140,148,154
      3. "Amri" – Zaburi 119:158

Haya yote yanarejerea ufunuo maalum Wake Mungu kwa Israel. Kimsingi yanafanana. Angalia Mada Maaalum: Uvuvio.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 26: 6-11**

**[6] Isaka akakaa katika Gerari. [7] Watu wa mahali hapo wakamwuliza habari za mkewe. Akasema, Ni ndugu yangu huyu maana aliogopa kusema, Ni mke wangu, watu wa nchi wasije wakamwua kwa ajili ya Rebeka; kwa maana alikuwa mzuri wa uso. [8] Ikawa alipokuwa amekaa huko siku nyingi, Abimeleki, mfalme wa Wafilisti,**

**akachungulia dirishani, akamwona Isaka anacheza-cheza na Rebeka mkewe. [9] Abimeleki akamwita Isaka, akasema, Yakini huyu ni mkeo, mbona ulisema, Ni ndugu yangu huyu? Isaka akamwambia, Kwa sababu nalisema, Nisife kwa ajili yake. [10] Abimeleki akasema, Ni nini hii uliyotutendea? Labda mtu mmojawapo angalilala na mkeo bila kufikiri, nawe ungalitutia hatiani. [11] Basi Abimeleki akawaamuru watu wote, akisema, Amgusaye mtu huyu au mkewe lazima atauawa.**

**26:7 "Ni ndugu yangu huyu maana aliogopa kusema, ni mke wangu'"** Baadhi wanaliona hili kama kipengele cha kitamaduni kinachohusiana na vigae vya Nuzi, ambapo mtu alimwasili mkewe. Kama hivyo ndivyo ilivyo hivyo basi Isaka anasema ukweli. lakini, inaonekana kuwa Isaka anafuata nyayo za baba yake (kama vile Mwa. 12:13; 20:2, 12). Katika suala la Ibrahimu, huu ulikuwa ni ukweli nusu, lakini katika Isaka haijulikani kwa vile katika mstari huu (na mst.9) mwenendo wake unaainishwa na hofu yake binafsi. Inaonyesha ukosefu wa imani juu ya Isaka kwa vile Mungu aliahidi kuwa nae na kumlinda. Bado, katikati ya imani ya Isaka, kama aliyokuwa nayo Ibrahimu, Mungu alikuwa mwaminifu.

**26:8 "Isaka anacheza-cheza na Rebeka mkewe"** Istilahi hii "chezacheza" (BDB 850, KB 1019, *Piel* KAULI ENDELEVU) ni kutoka katika mzizi ule ule kama wa jina la Isaka,linalomaanisha "kucheka" au "kucheza" (BDB 850, kama vile Mwa. 17:17,19; 18:12; 21:6,9). Hapa lina kidokezo cha kujamiiana kama ilivyofanywa katika Mwa.39:17 na Kut. 32:6. Baadhi ya tafasiri zinalitumia neno "kupapasa."

**26:10 "na Abimeleki akasema"** Wote Abimeleki wa siku za Ibrahimu na Abimeleki wa siku za Isaka wanakabiliana kwa karibu sana kiheshima na kiuadilifu kuliko wazee wa kale. Hili laweza kumaanisha kuwa kwenye hatua ya historia Wakaanani walikuwa na kiwango Fulani cha kiroho.

**26:11** Ulinzi wa YHWH uko nyuma ya hili tamko!

Kifungu "hakika atakufa" kinaaksi *Qal* KITENZIJINA HALISI na *Hophal* KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 559, KB 562), ambapo ilikuwa ni njia ya kisarufi ya kuonyesha uimarishaji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 26:12-17**
**[12] Isaka akapanda mbegu katika nchi ile, akapata mwaka ule vipimo mia kwa kimoja, Bwana akambariki. [13] Na mtu huyu akawa mkuu, akazidi kusitawi, hata akawa mkuu sana. [14] Akawa na mali ya kondoo, na mali ya ng'ombe, na watumwa wengi. Hao Wafilisti wakamhusudu. [15] Na vile visima vyote walivyochimba watumwa wa baba yake, siku za Ibrahimu babaye, Wafilisti walikuwa wamevifukia, wakavijaza kifusi. [16] Abimeleki akamwambia Isaka, Utoke kwetu, maana wewe una nguvu sana kuliko sisi. [17] Basi Isaka akatoka huko akapiga kambi katika bonde la Gerari, akakaa huko.**

**26:12-14** Kumbuka baraka.
1. Akavuna vipimo mia kwa kimoja, mst. 12
2. Akatajirika na kuendelea kustawi mpaka akawa mkuu sana mst.13
3. Akawa na kundi la ng'ombe na kondoo wengi mst.14
4. Akawa na watumwa wengi mst. 14
   Hoja ya pili iliyoko #2 ni neno *Qal* KITENZIJINA HALISI na KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 229, KB 246), kinachoonyesha uimara.
   Hoja ya tatu iliyoko #2 ni KIVUMISHI na KITENZI cha mzizi ule ule (BDB 152, KB 178, *Qal* KAULI TIMILIFU).

**26:12 "Bwana akambariki"** Huu ni utambuzi wa kithiolojia wa moja kwa moja kwamba alikuwa ni Mungu na sio Isaka yule mkulima ambaye alikuwa chanzo cha baraka.

**26:14 "Wafilisti wakamhusudu"** Hiki ni KITENZI (BDB 888, KB 1109, *Piel* KISICHO TIMILIFU) "wakaona wivu."
1. Wakavifukia visima vya Ibrahimu, mst. 15
2. Wakamwodoa Isaka, mst. 16

Mali ya Isaka ilikusudiwa kuwasaidia Wafilisti kuja kwa YHWH, lakini badala yake ikasababishia wivu na hasira.

**26:15 "Wafilisti wakavifukia"** Kama Isaka alivyoendelea kukua, kwa idadi na utajiri, akawa chanzo cha hofu kwa Wafilisti. Wakaonyesha maumivu na hofu yao kwa kuvifukia visima vya Isaka. Wakitambua kuwa Isaka alikuwa mfugaji, ukosefu wa maji ungalimsababisha kukimbilia mbali. Kipengere hiki cha sura ya 26 kinatuonyesha uvumilivu na imani ya Isaka. Mengi kuhusu aina ya tabia yake inaweza kutambuliwa kwa namna anavyoshughulikia huu mvutano wa haki ya maji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:18-22**
**[18] Isaka akarudi akavichimbua vile visima vya maji walivyovichimba siku za Ibrahimu babaye; maana wale Wafilisti walikuwa wamevifukia baada ya kufa kwake Ibrahimu; naye akaviita majina kufuata majina alivyoviita babaye. [19] Watumwa wa Isaka wakachimba katika lile bonde, wakapata kisima cha maji yanayobubujika. [20] Wachungaji wa Gerari wakagombana na wachungaji wa Isaka wakisema, Maji haya ni yetu. Ndipo akakiita jina la kile kisima Eseki, kwa sababu waligombana naye. [21] Wakachimba kisima kingine, wakagombania na hicho tena. Akakiita jina lake Sitna. [22] Akaondoka huko akachimba kisima kingine, wala hicho hawakukigombania. Akakiita jina lake Rehobothi, akasema, Kwa kuwa sasa Bwana ametufanyia nafasi, nasi tutazidi katika nchi.**

**26:18 "akaviita majina kufuata majina alivyoviita babaye"** Hili kiwastani linaendelea kudumisha tamaduni ya kifamilia au lawezakuwa ni tendo la kidini linalohusiana na agano na babaye.

**26:20-22 "Eseki. . .Sitna. . .Rehobothi"** Huu ni mlolongo wa visima vitatu vilivyokuwa vikitumika kuonyesha kile kilichokuwa kikitokea kwenye mahusiano ya Isaka na jirani zake.

1. Kisima cha kwanza kinamaanisha "magomvi" (BDB 796)
2. Kisima cha pili kilimaanisha "uadui" (BDB 966 II)
3. Kisima cha tatu kilimaanisha "uwanda mpana" (BDB 932), ambayo ni nahau ya Kiebrania kumaanisha utulivu na amani na furaha.

**26:22 "kwa kuwa sasa Bwana ametufanyia nafasi, nasi tutazidi katika nchi"** Isaka alikuwa na watenda kazi ambao kwa urahisi wangekabiliana na Wafilisti, lakini alichagua kusubiri kwa imani, juu ya Mungu ambaye alimwahidi. Jina la kisima cha tatu na neno "chumba" yanafanana (BDB 932)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:23-25**
**[23] Akapanda kutoka hapo mpaka Beer-sheba. [24] Bwana akamtokea usiku uleule, akasema, Mimi ni Mungu wa Ibrahimu baba yako, usiogope, maana mimi ni pamoja nawe, nami nitakubarikia, na kuzidisha uzao wako kwa ajili ya Ibrahimu mtumishi wangu. [25] Akajenga madhabahu huko, akaliitia jina la Bwana. Akapiga hema yake huko, na watumwa wa Isaka wakachimba kisima huko.**

**26:23 "Akapanda kutoka hapo mpka Beersheba"** Hii ni sehemu ya eneo la kusini mwa nyika ya Yudea ambayo ilikuwa ni muhimu kwa wageni katika nchi ile walipopiga hema (kama vile Mwa. 22:19).

**26:24 "Bwana akamtokea usiku ule ule na kusema"** Hii ni mara ya pili YHWH anamtokea Isaka (kama vile mst. 2). Hapa alikuwa katika ndoto wakati wa usiku (kama vile 15:5,12; 21:12,14; 22:1-3; 26:24). Mengi ya maono katika kitabu cha Mwanzo yamechapishwa katika ushairi, kama ilivyo mst. 24 (kama vile 12:1-3; 15:1,18; 17:1-2,4-5; 35:10,11-12).

◘**"Mimi ni Mungu wa baba yako Ibrahimu"** Tambua namna neno YHWH na *Elohim* yanavyofanana (kama vile Mwa. 2:4). Hili ni rasmi na timilifu zaidi kuliko mst. 2. Yameundwa kimfanano wa mafunuo ya Mungu kwa Ibrahimu.

◙**“usiogope, maana Mimi ni pamoja nawe”** Ni ahadi namna gani iliyo kuu (pia kumbuka 15:1; 21:17; 46:3).

◙**“kwa ajili ya mtumishi wangu Ibrahimu”** Hiki ni cheo cha kiheshima kwa ajili ya Ibrahimu, Musa, Yoshua, na Daudi. Yawezakuwa ni chanzo cha kifungu cha nyaraka za Paulo, “mtumwa wa Kristo Yesu.”

**26:25** Hii sehemu binafsi ya mafunuo ya YHWH pakajakuwa ni mahali patakatifu. Madhabahu yalijengwa katika sehemu hizi na zikajakuwa ni sehemu za kuabudia, maombi, na dhabihu (kama vile 8:20; 12:7,8; 13:4,18; 22:9).

◙**“akachimba kisima”** Maji ni bidhaa ya thamani kwenye maeneo haya ya nusu jangwa. Isaka kwa utulivu alimsubiri YHWH kwa ajili ya msaada na maelekezo. Visima mbalimbali venye kufanikiwa vilivyotajwa katika muktadha huu vinaonyesha uwepo wa YHWH na Baraka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:26-33**
**[26] Ndipo Abimeleki akamwendea kutoka Gerari, pamoja na Ahuzathi rafiki yake, na Fikoli, jemadari wa jeshi lake.[27] Isaka akawauliza, Mbona mwanijia, nanyi mmenichukia, mkanifukuza kwenu? [28] Wakasema, Hakika tuliona ya kwamba Bwana alikuwa pamoja nawe; nasi tukasema, Na tuapiane, sisi na wewe, na kufanya mapatano nawe [29] ya kuwa hutatutenda mabaya, iwapo sisi hatukukugusa wewe, wala hatukukutendea ila mema, tukakuacha uende zako kwa amani; nawe sasa u mbarikiwa wa Bwana. [30] Basi akawafanyia karamu, nao wakala, wakanywa. [31] Wakaondoka asubuhi na mapema, wakaapiana wao kwa wao, kisha Isaka akawapa ruhusa, nao wakaenda zao kwa amani. [32] Ikawa siku ileile, watumwa wa Isaka wakaja wakampasha habari za kile kisima walichokuwa wamekichimba, wakamwambia, Tumeona maji. [33] Naye akakiita jina lake Shiba; kwa hiyo jina la mji huo ni Beer-sheba, hata leo.**

**26:26“Abimeleki. . .Fikoli”** Ingawa majina haya ni yale yale kama yaliyoko katika Mwa. 21:222, imechukua yapata miaka 75-80 na dhahiri haiwezi kurejea mtu yule yule. Toka kwenye utangulizi hadi Zaburi 34 inaonekana dhahiri kuwa hizi ni nyadhifa badala ya majina husika.

**26:27** Kwa wazi kabisa Isaka bado alisikia maumivu na aibu ya kufukuzwa!

**26:28 “hakika tuliona ya kwamba Bwana alikuwa pamoja nawe”** Kuna vipengere mbalimbali vya kisarufi vya mst. huu.

1. “hakika tuliona,” hiki ni KITENZIJINA HALISI *Qal* na KITENZI TIMILIFU*Qal* cha mzizi ule ule (BDB 906, KB 1157), unaomaanisha “ilikuwa hakika kwamba”
2. “nasi tuapiane,” BDB 224, KB 243, *Qal* KITENZI AMRISHI; Neno “kiapo” (BDB 46) linapatikana hapa tu na 24:41 (mara mbili), hata mst. 31 ni neno tofauti (BDB 989). Laweza kumaanisha kiapo au laana (mf., Hes. 5:21,23,27; Kumb. 29:12,14,19,20,21). Laweza kumaanisha “na mtu alaaniwe ikiwa hatatunza kiapo.”
3. “tufanye agano,” BDB 503, KB 500, *Qal* KAULI YA KUSIHI

Hili ni kusudi la kithiolojia la Baraka za wazee. Halikutolewa kwenye vitu halisia kwa wazi, lakini kuwaonyesha wengine uhusiano wao wa kipekee kwa YHWH (kama vile mst. 29c).

**26:30 “basi akawafanyia karamu”** Utaratibu wa kawaida wa kulifanya agano ulikuwa ni kuandaa chakula cha pamoja.

**26:32-33 “wamekichimba kisima . . .‘tumeona maji’. . .Shiba”** Kiuhalisia visima hivi vilikuwa na umuhimu wa kimwili na kiroho. Viliweka alama ya Baraka za Mungu katika maisha ya Isaka. Mstari wa 33 wawezakuwa asili ya neno pinzani kwa ajili ya jina Beersheba (yaani “akakiita jina,” BDB 988) katika Mwa. 21:31, ambapo jina laweza kutafasiliwa kama “kisima walichoapiana” au “visima saba.” Shiba yawezakuwa ni njia ya kurejerea “kiapo.” Maneno ya Kiebrania “saba” na “kuapa” yanafanana kiukaribu. Mara nyingi katika Agano la Kale asili ya maneno yanajulikana zaidi kuliko ya kiufundi na, kwa hiyo, yaweza kuwa na asili mbili zinazojulikana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26: 34-35**
**34 Esau alipokuwa mwenye miaka arobaini, akamwoa Yudithi, binti Beeri, Mhiti, na Basemathi, binti Eloni, Mhiti. 35 Roho zao Isaka na Rebeka zikajaa uchungu kwa ajili yao.**

**26:34-35** Hii mistari miwili kiukweli inatengeneza hatua kwa ajili ya sura ya 27, hasa mst. 46. Mwandishi anaviunganisha vipengele ndani ya habari hii ili kwamba baadaye viwe na umuhimu wa kithiolojia (yaani kwa vile Isaka na Rebeka walimtuma Yakobo arudi Harani kwa ajili ya kujipatia mwanamke)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Abimeleki wa Mwanzo 21 ni sawa na yule wa Mwanzo 26?
2. Wapi asili ya Palestina?
3. Kwa nini wote Ibrahimu na Isaka walidai kuwa wake zao walikuwa ni dada zao?
4. Ni nini kusudu la visima vingi kudokezwa katika sura hii?
5. Elezea haki za kale za sherehe ya agano na namna gani ziliweza kugonganisha ufunuo wa kibiblia?

# MWANZO 27

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Uongo wa Yakobo | Isaka anambariki Yakobo | Yakobo anamfanyia hila Esau juu ya Baraka yake | Isaka anambariki Yakobo | Yakobo anapata Baraka ya Isaka kwa udanganyifu |
| 27:1-4 | 27:1-4 | 27:1-4 | 27:1a | 27:1-4 |
| | | | 27:1b | |
| | | | 27:2-4 | |
| 27:1-7 | 27:5-17 | 27:5-17 | 27:5-10 | 27:5-10 |
| | | | 27:11-12 | 27:11-17 |
| | | | 27:13-17 | |
| 27:18-29 | 27:18-29 | 27:18-29 | 27:18a | 27:18-29 |
| (27b-29) | (27-29) | (27-29) | | (27b-29) |
| | | | 27:18b | |
| | | | 27:19 | |
| | | | 27:20a | |
| | | | 27:20b | |
| | | | 27:21-24a | |
| | | | 27:24b | |
| | | | 27:25-29 | |
| Baraka zilizoibiwa | kupoteza tumaini Kwa Esau | | Esau anaomba Baraka za Isaka | |
| 27;30-38 | 27:30-38 | 27:30-38 | 27:30-31 | 27:30-40 |
| | | | | (39-40a) |
| | | | 27:32 | |
| | | | 27:33 | |
| | | | 27:34 | |
| | | | 27:35 | |
| | | | 27:36 | |
| | | | 27:37 | |
| | | | 27:38-40 | |
| | | | (39-40) | |
| 27:39-40 | 27:39-40 | 27:39-40 | | |
| (39-40) | (39-40) | (39-40) | | |
| | Kukimbia kwa Yakobo kutoka kwa Esau (27:41-28:5) | | | |
| 27:41-45 | 27:41-46 | 27:41-45 | 27:41 | 27:41-45 |
| | | | 27:42-45 | |
| | | Kuondoka kwa Yakobo kwenda Aramu Na ndoto yake Betheli (27:46:-28:22) | Isaka anatuma Yakobo kwa Labani ( 27:46-28:5) | Isaka anamtuma Yakobo kwa Labani (27:46-28:5) |
| 27:46 | | 27:46-28:5 | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA

A. Mara kwa mara Wafasiri wameona sura hii. Kama yenye kushusha sana hadhi dhidi ya Rebeka na Yakobo Hatahivyo, katika ufahamu wa Mwanzo 25:23, ni Isaka na Esau wanaojaribu kuendesha ufunuo wa Mungu.

B. Esau haijalishi haki yake ya kuzaliwa na amekwisha iuza kwa Yakobo (kama vile Mwanzo 25:27-34). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anafunua nia za Esau katika Ebr. 12:16-17. Haki ya kuzaliwa ilikuwa imeunganishwa moja kwa moja kwa Baraka za baba wa imani (yaani nahau "ili kwamba roho yangu ikubariki," mistari ya 4,19,25,31). Esau anaonekana kutojali aidha kuhusu utabiri wa Rebeka au kwa adhabu yake yeye mwenyewe juu ya haki yake ya kuzaliwa katika Mwanzo 25. Ikiwa Isaka alikuwa amesahau ufunuo huu kwa Rebeka, ambao hakika angekuwa imeshirikishwa pamoja naye au aliupuuzia, haijulikani, lakini Yakobo, kiukweli sio "mjanja mjanja" ambayo mara kwa mara huwa inachukuliwa. Hii haimaanishai kuwa hana hali za udanganyifu, lakini sio sawa kumlaumu yeye kwa matatizo yote ya sura hii.

C. Sura hii ina amri zisizo za kawaida zinazohusiana na shauku ya Isaka kwa ajili ya mlo maalumu kabla ya kutoa Baraka za ubaba wa imani (yawezekana kwa Esau).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:1-4**

**[1] Ikawa Isaka alipokuwa mzee, na macho yake yamepofuka asione, akamwita Esau, mwanawe mkubwa, akamwambia, Mwanangu. Naye akamwitikia, Mimi hapa. [2] Akasema, Tazama, sasa mimi nimekuwa mzee, wala sijui siku ya kufa kwangu. [3] Basi, nakuomba, chukua mata yako, podo lako na upinde wako, ukaende nyikani uniwindie mawindo; [4] ukanifanyie chakula kitamu namna ile niipendayo, ukaniletee, ili nile; na roho yangu ikubariki, kabla sijafa.**

**27:1 "Ikawa Isaka alipokuwa mzee, na macho yake yamepofuka asione"** Matatizo ya macho lazima ilikuwa ndio ugonjwa ulioshamiri katika Mashariki ya Karibu ya kale (kama vile Yakobo katika Mwanzo 48:10; Eli katika I Sam. 3:2 na baadaye, Paulo katika Gal. 4:13-15; 6:11; II Kor. 12:7).

◙**"akamwita Esau, mwanawe mkubwa,"** Hii inaonesha (1) upendeleo wa Isaka kwa Esau (kama vile Mwanzo 25:28), ambalo litafanyika wazi kadiri sura inavyoendelea au (2) mategemeo ya kimila ya watu wa kale (yaani kifasihi "kuu," BDB 152, yaani katika zama, kama vile10:21; 44:12) nafasi ya pekee ya mwana katika familia.

**27:2 "Akasema, Tazama, sasa mimi nimekuwa mzee, wala sijui siku ya kufa kwangu."** Inafurahisha kujua kwamba Isaka, kama umri wa miaka 137 ana hofu juu ya kifo chake. Tunajifunza kutoka Mwanzo 35:28 kwamba aliishi kufikia mpaka umri wa miaka 180. Hali yake inaweza kuwa ilitokana na ukweli kwamba kaka yake Ishmaeli alikufa akiwa na umri wa miaka 137, inayoandikwa katika Mwanzo 25:17. Ikiwa ni kweli kwamba hesabu za umri

wa Isaka zilizofanywa na Martin Luther, miaka 137 inaweza kuwa sahihi, hivyo Isaka alikuwa akitenda sawa na mwitikio wake wa udhaifu wa mwili na sio ufunuo kutoka kwa Mungu. Kutoka katikambao za maandiko ya Nuzi kutoka katika eneo hili hili na muda tunajifunza kwamba "Mimi ni mzee" inawezekana ni nahau ya kisheria kwa uhamisho wa umma wa urithi wa haki kwenda kwa utawala wa mwana wake wa kiume.

**27:3,4** Kuna mfuatano wa KAULI SHURUTISHI zinazohusiana na mlo ulioombwa na Isaka kabla ya kuachia Baraka za ubaba wa imani. Hizi hapa ni amri/maombi ya Isaka.

1. "tafadhali chukua mavazi yako" ("kutetemeka," BDB 1068, hapa tu katika Agano la Kale na "upinde," BDB 905), mstari wa 3, BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "uende porini," mstari wa 3 BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. "niwindie," mstari wa 3, BDB 844, KB 1010, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. "niandalie chakula kinono," mstari wa 4, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. "uniletee mimi," mstari wa 4, BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
6. "ili nipate kukila," mstari wa4, BDB 37, KB 46, *Qal* HALI YENYE KUSIHI

**27:4 "ili roho yangu"** Hili ni neno *nephesh* (BDB 659, KB 711, kama vile mstari wa 25), ambalo linamaanisha chenye pumzi au kilicho na uhai. Linaweza kutumika juu ya mifugo (kama vile Mwanzo 1:24; 2:19) au wanadamu (kama vile Mwanzo 2:7). Wanadamu hawana nafsi (fikira za Wayunani), wao ni nafsi. Mwili wao wa nje ni mpaka wan je wa mwili/nafsi/roho.

◙**"ikubariki, kabla sijafa"** Angalia kusudio la chakula ilikuwa ni tukio kwa ajili ya kurithisha uongozi wa familia (yaani Baraka za ubaba wa imani). Dhana ya Kiebrania ya neno lililokwisha kuzungumzwa ilikuwa kwamba likishatolewa lisingeweza kurudishwa (kama vile mistari ya 33-38; Isa. 55:11). Isaka alidhani alikuwa anakufa (kama vile mstari wa 2), lakini aliishi miaka kadhaa zaidi. Isaka alikuwa mnufaika wa ahadi za kiagano kwenda kwa Ibrahimu. Lakini bado alikuwa kipofu na alidhani angekufa hivi karibuni. Ugonjwa wa mwili si ishara ya Mungu kutopendezewa, lakini kama matokeo ya kuishi katika ulimwengu ulioanguka (angalia kijitabu cha Gordon Fee, "The Disease of the Health, Wealth Gospel").

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:5-17**
**5 Na Rebeka akasikia, Isaka aliposema na Esau mwanawe. Basi Esau akaenda nyikani awinde mawindo,**
**ayalete. 6 Rebeka akamwambia Yakobo mwanawe, akisema, Angalia, nimemsikia baba yako akisema na**
**Esau, ndugu yako, akinena, 7 Niletee mawindo, ukanifanyie chakula kitamu ili nile, na kukubariki mbele za**
**Bwana kabla ya kufa kwangu.8 Basi, mwanangu, sikiliza sauti yangu kama nitakavyokuagiza. 9 Enenda sasa**
**kundini ukanitwalie wana-mbuzi wawili walio wema, nami nitawafanya chakula kitamu kwa baba yako,**
**namna ile aipendayo. 10 Kisha utampelekea baba yako, apate kula, ili akubariki kabla ya kufa kwake. 11**
**Yakobo akamwambia Rebeka mamaye, Esau ndugu yangu ni mtu mwenye malaika, na mimi ni mtu laini.12**
**Labda baba yangu atanipapasa, nami nitakuwa machoni pake kama mdanganyifu; nami nitaleta juu yangu**
**laana wala si mbaraka. 13 Mamaye akamwambia, Laana yako na iwe juu yangu, mwanangu, usikie sauti**
**yangu tu, enenda ukaniletee wana-mbuzi. 14 Akaenda, akawatwaa, akamletea mamaye. Mamaye akafanya**
**chakula kitamu namna ile aliyopenda babaye. 15 Kisha Rebeka akatwaa mavazi mazuri ya Esau mwanawe**
**mkubwa, aliyokuwa nayo nyumbani, akamvika Yakobo mwanawe mdogo. 16 Na ngozi za wana-mbuzi**
**akamvika mikononi, na katika ulaini wa shingo yake. 17 Naye akampa Yakobo mwanawe mikononi mwake**
**hicho chakula kitamu, na mkate alioufanya.**

**27:5 "Na Rebeka akasikia, Isaka aliposema"** Kiuwazi kuna tatizo la wivu na ujanja ujanja katika familia hii. Tunaweza kuona migogoro na mvutano kati ya Rebeka na Isaka na Yakobo na Esau. Inafurahisha ni kwa namna gani mara kwa mara Biblia inaandika matatizo ya kindoa na kifamilia kati ya mashujaa hawa wa Agano la Kale. Usikilizaji wa Rebeka katika hema unaweza kutafsiliwa aidha kama kuwa mmbea au kama kujaribu kwake kutimiliza ufunuo wa Mungu kwake katika Mwanzo 25:23. Katika uelewa wangu wa kifungu hiki cha habari nitaenda kumpa Yakobo na Rebeka faida ya mashaka kwakuwa inaonekana kama vileIsaka na Esau wanajaribu kuzunguka kwenye utabiri wa wazi wa Mungu.

**27:7** KAULI SHURUTISHI zinaaksi mistari ya 3 na 4.

◙ **"na kukubariki mbele za Bwana kabla ya kufa kwangu."** Ule ukweli kabisa kwamba jina la Mungu linatajwa (katika maandiko na Rebeka, sio Isaka, kama vile mstari wa 4) unaonesha umuhimu wa Baraka za ubaba wa imani. Ilikuwa karibia inachukuliwa kama kuwa na nguvu za kujitegemea na mara zinapotolewa zisingeweza kurudishwa tena. Ilikuwa muhimu sana kwasababu ya ahadi za Mungu kwa Ibrahimu na ahadi za baadaye zinazofuata kwa Isaka, Yakobo na wanawe kumi na wawili.

**27:8-9** Rebeka anaamua kumjaribu Isaka na kuzuia makusudio yake, hivyo anamwamuru Yakobo

1. kusikiliza/kusikia, mstari wa 8, BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. kwenda katika zizi la mifugo, mstari wa 9, BDB BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. kuleta/kuchagua wana wawili, mstari wa 9, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. Kwamba niweze kuandaa chakula kinono, mstari wa 9, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU inayotumika katika namna ya KUSIHI.

**27:9 "namna ile aipendayo"** Rebeka alijua namna ya kupika chakula akipendacho Isaka. Inavyoonekana hakuwa akipika mara kwa mara au asingeweza kukiomba kutoka kwa Esau.

**27:11 "Esau ndugu yangu ni mtu mwenye malaika,"** Angalia Mwanzo 25:25.

◙

**27:12**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"mdanganyaji"** |
| **NASB (Margin)** | **"mwenye kukebehi"** |
| **NARSV** | **"kukebehi"** |
| **TEV** | **"kudanganya"** |
| **NJB** | **"kudanganya"** |
| **LXX** | **"mwenye nia mbovu"** |

KITENZI cha kiebrania (BDB 1073, KB 1770, *Pilpel* KAULI ENDELEVU) katika shina hili (*Pilpel*) maana "kebehi" au "danganya," wakati katika shina *Hitpalpel* (kama vile II Nyakati 36:16) inaashiria "kukebehi" au "kutumia vibaya" (NIDOTTE, vol. 4, ukurasa wa 320). Neno hili linapatikana katika Agano la Kale katika haya maeneo mawili tu. Toleo la NIV linayafasiri kama "kufanya mbinu" na "kubeza" Mzizi huu hauusiani na jina la Yakobo katika 25:26 (BDB 784).

**27:13-17** Hii inaonesha mpango wa kina wa wote Rebeka na Yakobo katika matendo ya udanganyifu na ujanja ujanja.

**27:13 "Laana yako na iwe juu yangu"** Hakuna KITENZI katika toleo la MT. Rebeka alijua kungekuwa na madhara ya matokeo! Hivyo alimwambia Yakobo afanye kwa niaba yake.

1. tii (kifasihi. sikia), BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile mistari ya 5 (mara mbili),6,8,13,34,43
2. nenda, BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile mistari ya 5,9,13,14
3. chukua, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile mistari ya 9,13,14,15,35,36 (mara mbili),45,46

**27:15-17** Tazama matendo yasiyo ya uaminifu.

1. alichukua nguo za Esau zile zilizo bora (BDB 326) na akamvalisha Yakobo, mstari wa15
2. alivaa ngozi ya mbuzi katika mikono ya Yakobo na shingoni, mstari wa 16 (yawezekana kutoka kwa wanambuzi wawili waliochinjwa ili kuweza kupata mlo)
3. alimpatia Yakobo chakula kilichoandaliwa ampelekee Isaka, mstari wa 17

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:18-29**
**[18] Akaja kwa baba yake, akasema, Babangu. Akasema, Mimi hapa, U nani wewe, mwanangu? [19] Yakobo akamwambia babaye, Mimi ni Esau, mzaliwa wako wa kwanza, nimefanya kama ulivyoniambia. Ondoka, tafadhali, ukae kitako, ule mawindo yangu, ili roho yako inibariki. [20] Isaka akamwuliza mwanawe, Imekuwaje umepata upesi namna hii, mwanangu? Akasema, Kwa sababu Bwana, Mungu wako, amenifanikisha. [21] Isaka akamwambia Yakobo, Karibu, tafadhali, ili nikupapase, mwanangu, nione kwamba wewe ndiwe mwanangu Esau, ama siyo. [22] Basi Yakobo akamkaribia Isaka, babaye, naye akampapasa, akasema, Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau. [23] Wala hakumtambua, kwa maana mikono yake ilikuwa kama mikono ya Esau, ndugu yake, yenye malaika; basi akambariki. [24] Akamwuliza, Wewe ndiwe kweli mwanangu Esau? Akasema, Ndimi. 25 Akasema, Niletee karibu nami nipate kula mawindo ya mwanangu, ili roho yangu ikubariki. Akamsogezea karibu, naye akala; kisha akamletea mvinyo, akanywa. [26] Isaka, baba yake, akamwambia, Njoo karibu sasa, ukanibusu, mwanangu. [27] Akakaribia akambusu. Naye akasikia harufu ya mavazi yake, akambariki akasema, Tazama, harufu ya mwanangu Ni kama harufu ya shamba alilolibariki Bwana. [28] Mungu na akupe ya umande wa mbingu, Na ya manono ya nchi, Na wingi wa nafaka na mvinyo. [29] Mataifa na wakutumikie Na makabila wakusujudie, Uwe bwana wa ndugu zako, Na wana wa mama yako na wakusujudie. Atakayekulaani alaaniwe, Na atakayekubariki abarikiwe.**

**27:18-24** Huu ni mwanzo wa uongo kadhaa.
1. Wewe ni nani?, mstari wa 18, Mimi ni Esau, mstari wa 19
2. Umewezaje kuwpata mawindo kwa haraka hivyo na kupika kwa haraka?, mstari wa 20, Bwana alinisaidia, mstari wa 20
3. Wewe kweli ni Esau?, mstari wa 24, Mimi ndiye, mstari wa 24
4. mashaka ya Isaka yanaweza kuonekana katika mistari ya 21,24,27

**27:19** Yakobo anamuomba Isaka
1. ainuke, BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. akae, BDB 442, KB 444, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. ale, BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**27:20 "Kwa sababu Bwana, Mungu wako, amenifanikisha"** Wafasiri wengi wanaita hii kukufuru kwasababu Yakobo alidanganya kwa kutumia jina la Mungu. Lakini nafikiri Yakobo anamaanisha kwenye ukweli kwamba utabiri wa Mungu kuhusu yeye kupitia mama yake pamoja na kununuliwa kwake kwa haki ya uzaliwa kutoka kwa Esau ni matendo ya Mungu (yaani mtazamo mkubwa)!

**27:22-23** Rebeka lazima aliweka ngozi yua mwanambuzi kwa uangalifu katika mikono (vidole). Ni kwa namna gani aligundisha ngozi bado haijulikani. Inawezekana kwamba "mikono" hakika inamaanisha mikono ya Yakobo.

**27:25** Inavyoonekana Baraka hii maalumu ambayo ilihamisha uongozi wa familia ilikuwa kama agano na hivyo ilikuwa inaambatana na chakula. Kula na mtu na alafu kuwafanyia usaliti ilikuwa inaonekana kama kosa kubwa dhidi ya mwingine.

**27:26-27** Hili lilkuwa ni jaribu lingine. Kubusiana kwa kawaida ilikuwa salamu ya kukutana na kuagana, lakini hapa ilikuwa ni nafasi kwa Isaka kuwa karibu na Yakobo kumnusa na kushika mavazi yake. Esau lazima alikuwa na harufu yake ya aina yake iliyohusiana na shughuli zake za uwindaji.

**27:27-29** Isaka alimaanisha Baraka ya ubaba wa Imani kwa ajili ya Esau. Tazama kwamba inajumuisha Baraka za kiukulima (kama vile Kum. 33:28) pamoja na kuwa mababu wa familia. Utagundua baadhi ya vipengele vinavyohusiana na Baraka za Ibrahimu (yaani mstari wa 29).

**27:28 "umande wa mbingu,"** Mvua inakuja kwa nyakati Fulani tu katika Palestina (mvua za kwanza, kama vile Kumb. 11:14; Yoeli 2:23; mvua za baadaye, kama vile Kumb. 11:14; Yoeli 2:23). Kipindi kinachobaki cha kuvuna

kinatokana na maji ya umande. Hivyo, “umande” (BDB 378) inakuwa sitiari kwa ajili ya neema na utoshelevu wa Mungu (kama vile Kumb. 33:13, 28). Mistari ya 28 na 29 zina mfuatano wa KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU zinazotumika kama HALI ZENYE KUSIHI.

1. “Mungu na akupatia,” mst. 28, BDB 678, KB 733, *Qal* AULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inatumika katika namna ya HALI YA KUSIHI
2. “watu na wakakutumikie,” mstari wa 29, BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU inatumika katika namna ya HALI YA KUSIHI
3. “mataifa yakakuinamie,” mst. 29, BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI.
4. “utakuwa mkuu na bwana wa ndugu zako,” mst. 29, BDB 217, KB 241, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. “na wana wa mama yako wakuinamie,” mst. 29, sawa sawa na #3

**27:29** Hii kidhahiri ni ushairi wa Kiebrania ikiwa na usambamba wa ulinganifu. Inaelezea kweli inayopatikana katika Mwanzo 25:23, ambayo inaelezewa katika Agano la Ki-Ibrahimu katika Mwanzo 12:1-3. “mbarikiwa” (BDB 138, KB 159) na “laana” (BDB 76, KB 91) inawakilisha uwepo au kutokuwepo kwa utoshelevu wa ki-Mungu (kama vile Hes. 24:9; Kumb. 27:15-28:19). Katika namna iliyokuwa inaonekana kama ahadi ya agano.

◙ **“Na wana wa mama yako na wakusujudie”** Hii inakaribia kuwa na mwonekano wa kushushwa chini kimahesabu kwa Yakobo (Isaka alijua kuwa anazungumza na Esau)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:30-38**
**[30] Ikawa Isaka alipokwisha kumbariki Yakobo, na alipokuwa Yakobo ndiyo kwanza ametoka mbele ya Isaka, baba yake, mara Esau ndugu yake akaja kutoka katika kuwinda kwake. [31] Naye pia amefanya chakula kitamu akamletea babaye, akamwambia baba yake. Babangu na aondoke, ale mawindo ya mwanawe, ili roho yako inibariki. [32] Isaka, baba yake, akamwuliza, U nani wewe? Akasema, Mimi ni mwanao, Esau, mzaliwa wako wa kwanza.[33] Isaka akatetemeka tetemeko kuu sana, akasema, Ni nani basi yule aliyetwaa mawindo akaniletea? Nami nimekwisha kula kabla hujaja wewe, nikambariki; naam, naye atabarikiwa. [34] Esau aliposikia maneno ya babaye, akalia kilio kikubwa cha uchungu sana, akamwambia babaye, Nibariki na mimi, mimi nami, Ee babangu. [35] Akasema, Nduguyo amekuja kwa hila, akauchukua mbaraka wako. [36] Akasema, Je! Hakuitwa Yakobo kwa haki, maana amejitia mahali pangu mara mbili hizi? Alichukua haki yangu ya mzaliwa wa kwanza, na sasa amechukua mbaraka wangu. Akasema, Je! Hukuniwekea na mimi mbaraka? [37] Isaka akajibu, akamwambia Esau, Tazama, nimemfanya awe bwana wako, na ndugu zake wote nimempa kuwa watumishi wake; kwa nafaka na mvinyo nimemtegemeza, nami nikufanyie nini sasa, mwanangu? [38] Esau akamwambia babaye, Una mbaraka mmoja tu, babangu? Unibariki mimi, mimi nami, Ee babangu. Esau akapaza sauti yake, akalia.**

**27:30 “na alipokuwa Yakobo ndiyo kwanza ametoka mbele ya Isaka”** Tungo hii ni *Qal* KITENZI JINA HALISI na *Qal* KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU kutoka katika mzizi ule ule (BDB 422, KB 425). Hii ni tungo yenye kuonesha huruma ikiashiria kipindi kifupi cha muda kati ya kuondoka kwa Yakobo na kuwasili kwa Esau.

**27:31 “akamwambia baba yake”** Inafurahisha kwamba hali za tungo za Esau ni za vilevile kama zile zilizotumika na Yakobo katika mstari wa 19. Yawezekana Yakobo hata alimuigilizia mazungumzo ya kinahau ya kaka yake katika kujaribu kumrubuni baba yake. Hatahivyo inaweza kuwa maelezo ya kinahau ya kawaida.

**27:32** Ghafla Esau anajitambulisha mwenyewe kama “mzaliwa wa kwanza” (BDB 114). Hii haikuwahi kutokea kuwa kitu cha kujali sana kwa upande wake (angalia 25:29-34).

**27:33 “Isaka akatetemeka tetemeko kuu sana”** Katika Kiebrania KITENZI na KISHAMIRISHO CHENYE MASHTAKA (BDB 353, KB 350, kama vile Dan. 10:7) lazima ifasiliwe kama “alitetemeka kwa tetemeko kuu.” Ni uelewa wangu kwamba 175 ya andiko hili kwamba Isaka hatimaye anatambua kwamba amekuwa akipigana dhidi ya Mungu katika kujaribu kumbariki mzaliwa wake wa kwanza, Esau, na si kwamba tu ana hasira juu ya Yakobo. Inafurahisha kugundua kwamba hii ni njia nyingine ya Mungu kuonesha utawala wake juu ya agano kwa watoto wa uzaliwa wa

kwanza, ambao mara nyingi wangepokea ahadi ya baba, haifanyiki katika sura hizi zote za ufunguzi wa Mwanzo. Ni ya pili, au baadaye, watoto wanopokea Baraka ya ubaba wa imani.

◙ **"naam, naye atabarikiwa"** Tungo hii inaweza kueleweka aidha kama (1) kama dhidi ya historia ya nyuma ya nguvu ya neno lililokwisha kutamkwa ambalo mara baada ya kutolewa lisingeweza kurudishwa au (2) kama ukweli kwamba Isaka alitambua kwamba alikuwa anapigana dhidi ya Mungu (angalia dokezo lililotangulia).

**27:34 "akalia kilio kikubwa cha uchungu sana"** Tazama viashiria vya msisitizo.

1. Misamiati ya KISHAMIRISHO (BDB 858, KB 1042), "akalia kwa kilio kikubwa"
2. "sana," KIVUMISHI (BDB 152)
3. "kwa huzuni," KIVUMISHI (BDB 600 I)

◙**"Nibariki na mimi, mimi nami, Ee babangu.!"** Hii ni KAULI SHURUTISHI ya kwanza kati ya mbili *Piel* (BDB 138, KB 159, kama vile mstari wa 38). Waebrania 12:17 inatuonesha sisi kwamba Esau, ingawa alijuta kwamba alikuwa amekosa Baraka za utajiri, alikuwa anajuta kwa sababu mbaya.

**27:35-36 "Nduguyo amekuja kwa hila, akauchukua mbaraka wako"** Ni ukweli nusu tu kwamba Yakobo "mjanja mjanja," "mfikiaji wa juu" (BDB 784), na "muongo" (BDB 941) kwasababu (1) Esau aliuza haki yake mwenyewe ya uzaliwa (kama vile mstari wa 36 na Mwanzo. 25:27-34) na (2) Isaka alipuuzia ufunuo wa Mungu kwa Rebeka katika Mwanzo 25:23. Jina Yakobo linatolewa maana kama "mfikia mambo ya juu" au "mjanja mjanja" (BDB 139) katika Mwanzo 25:26.

**27:36 "mara mbili hizi"** Hii kidhahiri inamaanisha kwa Mwanzo. 25:27-31 na 27:18-29.

◙ **"haki yangu ya mzaliwa. . . mbaraka"** Kuna mzaha juu ya maneno ya Kiebrania yenye sauti ya mfanano: "haki ya uzaliwa" ni sawa na *bekhorah* (BDB 114), wakati "baraka" sawasawa na *berakhah* (BDB 139).

◙**"Je! Hukuniwekea na mimi mbaraka?"** Baraka ya ubaba wa imani ilikuwa inaeleweka. Kila kitu kinachojumuisha uongozi wa familia na ahadi za kiagano (kama vile mstari wa 37) zilitolewa kwa Yakobo na zisingeweza kurudishwa kwasababu ya dhana ya kiebrania juu ya nguvu ya neno linalozungumzwa baada katika jina la YHWH, hata kama Isaka alifanyiwa ujanja katika kulitoa!

**27:37** Esau hakufanywa kuwa mtu maskini. Alikuwa amebakiwa na moja ya tatu ya mali zote za Isaka, lakini asingekuwa mtawala wa mambo yanayohusu familia wala mzungumzaji wa familia.

**27:38 "akapaza sauti yake, akalia"** Hii ni nahau ya kiebrania ya kihisia kwa kuonesha hali ya majonzi (kama vile Mwanzo 21:16).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:39-40**
**39 Isaka, baba yake, akajibu, akamwambia, Angalia, penye manono ya nchi patakuwa makao yako,Na penye umande wa mbingu unaotoka juu. 40 Kwa upanga wako wewe utaishi, nawe utamtumikia nduguyo; Na itakuwa utakapoponyoka, Utalivunja kongwa lake katika shingo yako.**

**27:39-40** Hakuna sana Baraka za ubaba wa imani kama ilivyo kwenye ushairi wa kinabii, sambamba na Mwanzo 49. Kuna muwako wa uhuru katika mstari wa 40, mstari wa 3 na 4.

**27:40** Hii inaweza kuelezea historia ya taifa la Edomu ambalo linatoka kwa Esau (kama vile Mwanzo 36). Kwa historia yao zaidi walikuwa chini ya kutawaliwa (yaani nira, BDB 760, kama vile Law. 26:13; I Fal. 12:4) ya Wayahudi. Mfasiri, Leupold, anatafsiri hii kama "walikuwa siku zote wanajaribu kutoka katika kutawaliwa na Wayahudi." Hatahivyo, wengine wanaweza kutafsiri hili kama kumaanisha hatimaye walifanikiwa, ikiwa ni rejea kwa Herode (aliyekuwa akitokea Edomu) akitawala Palestina wakati wa Yesu (Luther).

◙

**NASB, NKJV,**
**NRSV, LXX "kuvunja"**
**NASB (margin) "kuchana"**
**TEV "kukung'uta"**
**NJB "kutoroka"**

Neno (BDB 923, KB 1194) ni neno nadra. Katika *Qal* shina (mfano Yer. 2:31) inamaanisha kuzunguka huru, lakini katika shina *Hiphil* linamaanisha kujichana mwenyewe kwa kujiachia (hapa tu na yawezekana Zab. 55:2).

## MADA MAALUM: EDOMU NA ISRAELI

A. Edomu ni taifa mashariki mwa bahari ya Chumvi, linalotokana na kaka yake na Yakobo (kama vile Mwanzo 25-28; 32-33). Edomu inamaania "wekundu" wakati Esau linamaanisha "mwenye nywele" (kama vile Mwanzo 25:25, 30).
B. Israeli aliamuriwa kuheshimu Edomu kwasababu walikuwa ni ndugu (kama vile Kumb. 23:7)
C. Israeli na Edomu walikuwa na matatizo yanayoendelea.
   1. Hes. 20:14-21
   2. Amu. 11:16-17
   3. 1 Sam. 14:47-48
   4. 2 Sam. 8:14
   5. 1 Fal. 11:14-22
   6. 2 Fal. 14:22; 16:5-6
   7. 2 Chr. 20:10-30; 21:8 na kuendelea
   8. Amosi 1:6, 9
D. Unabii dhidi ya Edomu.
   1. Isa. 34:5 na kuendelea; 63:1 na kuendelea
   2. Yer. 49:7-22
   3. Maombolezo 4:21-22
   4. Ezek. 25:12-14; 35:1-15; 36:2-6
   5. Amosi 1:11-12
E. Katika Obadia, Edomu alishutumiwa
   a. Majivuno yake, mistari ya 3-4
   b. katika ulinzi wa kijiografia
   c. katika ushirika wa kisiasa na nguvu za kijeshi
   d. katika mali za biashara
   e. katika hekima za kidesturi
2. Kuvunja kwake sheria huko Yuda, ndugu zake, Obadia mistari ya 10-14
   a. alifurahi juu ya kuanguka kwa Yerusalemu (Maombolezo 2:15-17; 4:21)
   b. walikataa kusaidia (Obadia mstari wa 11)
   c. kushiriki vyema kwa adui (Obadia mstari wa 14)
   d. walichukua mali za Yuda (Yer. 13:19)
3. kukataa kwake na kumpuuzia YHWH (Obadia mistari ya 16)
F. inaweza kuwa kiwakilishi (aina) kwa mataifa yote ambayo wanamwasi Mungu na watu wake, Obadia mistari ya 15-21 (kama vile Zaburi 2).
G. Uwezekano wa utimilizwaji wa unabii huu
   1. kuharibiwa kwa Edomu na Babeli ya kisasa takribani miaka 5 baada ya anguko la Yerusalemu mwaka 580 k.k.
   2. kuondolewa na kuhamishwa kwa Edomu kutoka Petra kulikofanywa na Waarabu wa Nabatean takribani miaka ya 550-449 k.k (kama vile Mal. 1:2-5). Edomu hatajwi katika orodha ya Nehemia ya maadui waliomzunguka, lakini anawekewa mbadala na makabila ya kiarabu. Edomu anahamia Negebu.

3. kushindwa kwa Edomu kulikofanywa na makamanda wa kijeshi wa  Alexander Antigonus mwaka 312 k.k (inaandikwa katika Diodorus Seculus)
4. kushindwa kwa Edomu katika Negebu kulikofanywa na Judah Maccabaeus takribani 175 k.k (kama vile I Maccabees 5.3,15; II Maccabees 10.15; Maandiko ya kale ya Josephus ya wayahudi 12.8.1; 13.9.1
5. Edomu analazimishwa akubali dini ya Kiyahudi kulikofanywa na John Hyrcanus mwaka 125 k.k. Sasa wanaitwa wa-Idumeans.
6. Kamanda wa Kirumi, Titus, kwa asilimia zote za ushawishi wa wa-Idumean  mwaka wa 70 b.k.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:41-45**
**[41] Esau akamchukia Yakobo kwa ajili ya ule mbaraka babaye aliombarikia. Esau akasema moyoni mwake, Siku za kumlilia baba yangu zinakaribia, ndipo nitakapomwua ndugu yangu Yakobo. [42] Rebeka akaarifiwa maneno ya Esau, mwanawe mkubwa. Akapeleka mtu kumwita Yakobo, mwanawe mdogo, akamwambia, Tazama, katika habari zako Esau, ndugu yako, anajifariji moyo wake, maana anakusudia kukuua. [43] Na sasa, mwanangu, sikia sauti yangu, uondoke, ukimbilie kwa Labani, ndugu yangu huko Harani; [44] ukae kwake siku chache, hata ghadhabu ya ndugu yako igeuke; [45] hata ikuondokee ghadhabu ya ndugu yako, akasahau uliyomtenda. Ndipo nitakapopeleka watu kukuchukua kutoka huko. Kwa nini nifiwe nanyi nyote wawili siku moja?**

**27:41** Tafsiri ya Agano la Kale linafasiri mstari huu kama tamanio la Ishmaeli kwa Isaka kufa (yaani Isaka alifikiri kwamba alikuwa anaenda kufa; hii ndio maana alitoa Baraka zake za ubaba wa imani kama vile mstari wa 2), lakini hii inaonekana kuwa nje ya kuktadha kabisa kabisa kwa asilimia zote. Esau anaonekana kwa hakika kumpenda Isaka.

**27:43** Mara Rebeka anaposikia juu ya mipango ya Esau kulipa kisasi kwa Yakobo anamwamrisha Yakobo kufanya hima.
1. "tii" (kifasihi, "sikiliza ili ufanyie kazi"), BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "inuka," BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. Kimbia (kifasihi. kwenda), BDB 137, KB 156, *Qal* KAULI SHURUTISHI

Alimtuma arudi kwa familia yake huko Harani. Safari ilikuwa na makusudi mawili.
1. kumuweka mbali kutoka kwa Esau na kuruhusu hasira ya Esau kushuka (kama vile mistari ya 44-45)
2. apate mke kutoka kwenye familia yake (kama vile mstari wa 46), sio kutoka kwa Wakanaani kama ambavyo Esau alikuwa amefanya (kama vile Mwanzo 26:34-35; 27:46)

**27:44-45** Huu ni mfululizo wa tungo za Rebeka ambazo zinzonekana kumaanisha kwamba atamuita Yakobo arudi nyumbani harakaharaka. Kusema ukweli, Yakobo alikaa zaidi ya miaka 20 na yawezekana hatowahi kumuona mama yake tena. Je hii sio kejeli kwamba japokuwa Yakobo alipokea vyote urithi na haki ya mzaliwa, alitakiwa akimbie kuokoa maisha yake na Esau alifurahia vyote kwa zaidi ya miaka 20. Namuhurumia Rebeka alilazimika kubaki na mzee, mtu mwenye ulemavu aliyemdanganya na mwana wa kiume mkubwa aliyejiona kasalitiwa.

**27:45 "Kwa nini nifiwe nanyi nyote wawili siku moja"** Hii inaweza kufasiliwa kwa namna mbili: (1) kwamba Esau angemuua Yakobo na alafu ndugu wake wa karibu angekua kama *go'el* na kumuua Esau (kama vile Mwanzo 9:6) au (2) kwamba Yakobo japo ni wa nyumbani, alikuwa shupavu mwenye nguvu jambo ambalo lilikuwa wazi kutokana na  maelezo ya majukumu yake ya kichungaji na Labani (kama vile Mwanzo 31:38-42), na baadaye mieleka yake na malaika (kama vile Mwanzo 32:24- 32), na yawezekana ndugu wawili wangeuana ikiwa wangepigana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27: 46**
**[46] Rebeka akamwambia Isaka, Rohoni mwangu sina raha kwa sababu ya hao binti za Hethi. Kama Yakobo akitwaa mke katika binti za Hethi, kama hawa binti za nchi, maisha yangu yatanifaidia nini?**

**27:46** Tena tunaona mbinu/ujanja wa Rebeka. Anatumia udhuru anaoupendekeza kwa kumtoaYakobo bila kutaja uchovu wake wa kimaisha (BDB 880 I) kwa Esau. Inavyoonekana sababu yake ilikuwa ya msingi kwasababu Isaka anaiheshimu (kama vile 28:1-2). Tunarejea katika Mwanzo 26:34, 35 kwamba Esau alikuwa ameoa Wakanaani wanawake wawili (Heth, BDB 366, kama vile 23:3,10; angalia mada Maalum: Wakazi wa Palestina kabla ya Waisraeli 12:6) .

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Sura hii ianaonekana kumtambua nani kama mtu mwenye nia na mbinu mbovu?
2. Ni kwa namna gani Mwanzo 25:23 inahusiana na sura hii?
3. Je Baraka za mababa wa imani zinahusisha nini)
4. Kwanini Rebeka anataka mwanae wa kiume aoe ndugu yake?

# MWANZO 28

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakobo anaondoka | Yakobo Anamkimbia Esau (27:41-28:5) | Yakobo anaondoka Harani na ndoto yake Betheli (27:46-28:22) | Isaka anamtuma Yakobo kwa Labani (27:46-28:5) | Isaka anamtuma Yakobo kwa Labani (27:46-28:5) |
| 28:1-5 | 28:1-5 (3-4) | | | |
| | Esau anamwoa Mahaleti | | Esau anaoa mke mwingine | Ndoa nyingine ya Esau |
| 28:6-9 | 28:6-9 | 28:6-9 | 28:6-9 | 28:6-9 |
| Ndoto Ya Yakobo | Yakobo anaapa Betheli | | Ndoto ya Yakobo Betheli | Ndoto ya Yakobo |
| 28:10-17 | 28:10-17 | 28:10-17 | 28:10-15 | 28:10-19 |
| | | | 28:16-17 | |
| 28:18-22 | 28:18-22 | 28:18-22 | 28:18-22 | |
| | | | | 28:20-22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28 :1-5**

**[1] Basi Isaka akamwita Yakobo, akambariki, akamwagiza akamwambia, Usitwae mke wa binti za Kanaani. [2] Ondoka, uende Padan-aramu, mpaka nyumba ya Bethueli baba ya mama yako, ukajitwalie huko mke katika binti za Labani, ndugu wa mama yako. [3] Na Mungu Mwenyezi, akubariki, akuzidishe, na kukuongeza, ili uwe mkutano wa makabila. [4] Akupe mbaraka wa Ibrahimu, wewe na uzao wako pamoja nawe, upate kuirithi nchi**

**ya kusafiri kwako, Mungu aliyompa Ibrahimu. [5] Basi Isaka akampeleka Yakobo, naye akaenda Padan-aramu, kwa Labani, mwana wa Bethueli, Mshami**

**28:1 "Basi Isaka akamwita Yakobo, akambariki"**Tafsiri ya sura hii msingi unatokana na mpango wa Rebeka kumfanyia hila Esau uliotekelezwa kwenye 27:46. Ni muhimu Isaka ambariki Yakobo wazi pasipo kudanganywa. Kwa uhalisia alitambua ya kwamba anapambana na chaguo la Mungu la kutaka Esau apokee Baraka. Hata hivyo, kwa muktadha "Baraka"hapa ni salaamu tu (mfano 47:7,10 na Ruth 2:4).

◙ **"Usitwae mke wa binti za Kanaani"**Haya ni maelezo ya wazi ambayo Ibrahim alimpa mtumishi wake amtafutie Isaka mke kwenye Mwa. 24:3-4.Hii ni lazima iwe habali ya kumwabudu YHWH. Ingawa Labani mwana wa Bethueli hakuwa mwabudu halisi wa YHWH (yaani *Teraphim*, kama vile 31:19,34,35),ni dhahili kuna baadhi ya namna ya kithiolojia ya kufahamika kwenye hii familia.

**28:2 Isaka** anampa Yakobo masharti kadhaa
1. "Ondoka," BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "uende," BD 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. "ukajitwalie," BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI

◙**"uende Padan-aramu "**Neno hili (BDB 804 na 74) baadae lilitumiwa kwa utawala wa Shamu (kama vile 25:20) na bado hapa linalejerezea maeneo ya Harani (yaani Mji au Wilaya ).

◙ **"mpaka nyumba ya Bethueli baba ya mama yako"** Tazama pia Mwa. 22:20-24 ; 24:15.

**28:3 "Na Mungu Mwenyezi, akubariki"** Hili ni jina la heshima *El Shaddai* (BDB 42 na 994, angalia sio kwenye 17:1). Hii ni heshima ya mkuu wa familia kwa Mungu (kama vile 17:1; 28:3; 35:11; 43:14; 48:3; na labda 49:25).Tunajifunza kutoka kitabu cha Kut 6:2-3 Kwamba hili ni jina la heshima au cheo ambacho wazee wa familia walitumia kwa ajili ya Mungu. Tazama Mada maalumu: Majina ya Uungu katika 12:1.

◙ **"ili uwe mkutano wa watu"** Hili ni neno la kwanza la kiebrania *Qahal* (BDB 874, kama vile Kumb. 5:22; 9:10; 10:4; 23:2-9; 31:30), Ambalo linatafsiliwa kwa tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania kama *ekklesia*. Waamini wa agano jipya hutumia neno hili kuelezea ushirika wao mpya wa agano la uamini. Ni njia yao ya kusema wanahisi kama mmojawapo wa watu Mungu wa agano la kale.

**28:3-4** Mistari hii ina kauli mbali mbali ZISIZO TIMILIFU zimetumika kwa maana ya AMRISHI.

1. Bariki mst. 3, BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU
2. Akuongeze mst . 3, BDB 826, KB 963, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU
3. Akuzidishe mst. 3, BDB 915, KB 1176, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU
4. Akupe wewe Baraka za Ibrahim mst . 4, BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU, kama vile 15:7,8

**28:4 "mbaraka wa Ibrahimu"** Huu ukaja kuwa ni kipimo cha kawaida kwa ajili ya ahadi ya ki-Ibrahimu (kama vile mst . 13; 12:7; 13:15,17; 15:7,8; 17:8; 26:3,4; Kut . 6:4)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28:6-9**
**[6] Esau akaona ya kwamba Isaka amembariki Yakobo na kumpeleka Padan-aramu, ili ajitwalie mke huko, na katika kumbariki akamwagiza, akasema, Usitwae mke wa binti za Kanaani, [7] na ya kuwa Yakobo amewatii babaye na mamaye, akaenda Padan-aramu. [8] Esau akaona ya kuwa binti za Kanaani hawakumpendeza Isaka, baba yake. [9] Basi Esau akaenda kwa Ishmaeli akamtwaa Mahalathi, binti Ishmaeli mwana wa Ibrahimu, ndugu wa Nebayothi, kuwa mkewe pamoja na wakeze aliokuwa nao**

**28:6 "Sasa Esau"** Tunaona tabia ya ndani kutoka kwa Esau mistari ya 6-9. Bado hataki kuwajibika, Lakini anatamani Baraka. Na tena anaonekana ni mwanaume ambae anatawaliwa na mambo ya kidunia. Na tayali alikuwa na wanawake ambao ni mabinti wa kanaani (kama vile Mwa. 26:34-35; 27:46; 28:8; 36:2) na akamwoa binti wa Ishimaeli ili kumfurahisha baba yake. Na jina la binti huyu aliitwa "Mahalathi" kwenye mst. 9, lakini hii inaitwa "Basemathi" kwenye Kut. 36:3.Na kwa wazi akawa anajaribu kupata Baraka kutoka kwa Isaka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28: 10-17**
**[10] Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani. [11] Akafika mahali fulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale pale. [12] Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake. [13] Na tazama, Bwana amesimama juu yake, akasema, Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako. [14] Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kaskazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa. [15] Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia. [16] Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, Kweli Bwana yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. [17] Naye akaogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni**.

**28:10 "Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani"** Hosea 12:12 Inasema alikuwa anamkimbia kaka yake (kama vile Mwa. 27:41-45).

**28:11**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB**
**LXX "na akafika mahali Fulani"**
**TEV "mpaka mahali patakatifu"**
**REB "mpaka katika madhabahu fulani"**

Hii kidogo inaonesha sio tungo ya kawaida (hasa "mahali," BDB 879) kwa mahali pasipo faa. Ina maanisha sehemu fulani ya milima katika nchi ya Efrahimu,karibu sana na mji wa Luzi. Mahali hapa palikuwa na muunganiko maalumu na Ibrahimu (kama vile Mwa. 12:8; 13:3-4).

**28:12 "ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni"** Neno ngazi (linapatikana agano la kale pekee) ni kwenye asili ya "kusimamisha kitu Fulani wima" (BDB 700, KB 757). Sehemu hii ilijulikana kwa mawe yaliyokuwa bapa. Badala ya ngazi hizi za kiasasa, ni wazi kuwa ngazi hizi zilipangwa kwa mawe makubwa makubwa. Yesu anatumia ngazi hizi za mawe kwenye kitabu cha Yoh 1:51 kujielezea yeye mwenyewe.

◙**"malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake"** Utaratibu unaonekana kupindishwa hapa, lakini huenda utaratibu huu wa kipekee ili kuonyesha umuhimu kwamba Mungu wa Agano wa Ibrahimu alikuwa tayari na Yakobo, na malaika zake tayali wanaongoza maisha yake kila siku.

◙
**28:13**
**NASB, NKJV,**
**RSV, Peshitta "BWANA amesimama juu yake"**
**NRSV, TEV,**
**JPSOA, NRSV "BWANA amesimama upande wake"**
**NJB, NASB (margin) "BWANA alisimama upande wake"**
**NIV "juu yake alisimama BWANA"**
**LXX "BWANA alisimama juu yake"**

Kitenzi (BDB 662, KB 714, *Niphal* WAKATI ENDELEVU) kina maana "simama".Muktadha au KIVUMISHI kinachoambatana lazima kielezee habari kamili . Hapa על chaweza kumaanisha "kwa" au "juu ya." Haya ni maelezo ya kutengeneza upya agano, la kwanza lilirasimishwa kwa Yakobo. Tungo "Mimi ni Mungu wa baba yako"ni heshima ya ukuu wa kifamilia. (yaani , 26:24; 28:13; 31:5,29,42,53; Kut . 3:6,15).

◙**"Nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako."** Hili lilinenwa kwanza kwa Ibrahimu (Mwa. 12:7; 13:15, 17; 15:7,8; 17:8), na kisha kwa Isaka (Mwa 26:3), na sasa kwa Yakobo .

**28:14 "kama mavumbi ya nchi"** YHWH aliahidi uzao mwingi usio hesabika kwa mababa wa imani (kama vile . 12:2; 13:16; 15:5; 16:10; 17:2,4-5). Katika maana hili lilikuwa ni utimilifu wa ahadi ya urithi, lakini zaidi-kwa warithi wengi. Kwetu sisi ambao ni wakristo tazama hili kwenye kitabu cha Gal. 3:14 na Rum 2:28-29; 8:15-17! Mwa. 3:15 ni ya uhakika kabisa.

◙**"na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa."** Huu ukweli mkuu wa kusudi la kuitwa kwa Ibrahimu ni kuleta wokovu kwa dunia nzima. (tazama H. H. Rowley, *The Missionary Message of the Old Testament*). Huu muundo halisi wa MANENO ni *Niphal kw*a kiebrania na inatafsiliwa "watabalikiwa". Kama inavyoonekana kwenye 12:3;18:18;Mdo. 3:25; Gal. 3:8. The *Hithpael* kama linavyoonekana kwenye Mwa. 26:4 na 22:16-18 na linatafsiliwa "watajibalikia wenyewe" Hizi ni njia mbili za kuiangalia Baraka ile ile. Mungu anaonyesha Baraka kupitia watu wake ambapo wengine waone na kutamani Baraka hizo. Hata hivyo inapatikana tu kwa kupitia ushirika na Mungu ambaye ni Mkuu wa familia (yaani YHWH).

◙**"kwa maana sitakuacha"** YHWH Hawezi kuacha kamwe ahadi yake/ watu (yaani Kumb. , 31:6,8; Yosh. 1:5;Ebr. 13:5).

◙ **"hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia"** Ni maneno ya kweli ya YHWH aliyoaahidi, tazama Kumb. 7:9 na Isa. 55:11.

◙
**28:16**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, REB** **"kwa hakika BWANA yuko mahali hapa"**
**TEV** **"BWANA yuko hapa"**
**JPSOA** **"kwa uhakika uwepo wa BWANA upo hapa"**

Kielezi "Hakika" "ukweli" (BDB 38,kama vile Kut. 2:14; I Sam. 15:32; Isa. 40:7; 45:15; Yer. 3:23 [mara mbili]; 4:10) inaonyesha mkazo zaidi.

◙**"wala mimi sikujua"** Ni dhahili Yakobo alihisi kuwa ameingia bila heshima kwenye aridhi takatifu, lakini hakujua kuwa ni takatifu kwa sababu haikuonekana kuwa si ya kawaida au tofauti. Hili ni wazo langu, kukana nadhalia ya watoa maoni wa zamani kwamba hili ni eneo takatifu la kanaani.

**28:17 "Naye akaogopa" M**tazamo ya Yakobo kwenye ndoto hii unaelezea kama "hofu" (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU). Anaelezea mahali kama "Panatisha" BDB 431, KB 432, *Niphal* KAULI ENDELEVU). Wanadamu wana/ana hofu ya kuona au uwepo wa Mungu Mtakatifu au kuongozwa na Roho (yaani Malaika ). Maneno ya Mungu kwa Musa kwenye kichaka kilichokuwa kinaungua kwenye Kut. 3:5 au taifa la Israeli kabla ya kufika Mlima Sinai Kut. 19.

◙ **Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni**. **"B**aadhi ya watoa maoni wanahisi hii tungo"lango la mbinguni" (BDB 1044 INAUNGANISHA 1029) na muktadha wa ngazi kufika mbinguni ni mawazo kumbukumbu ya kale ya dini za kibabeli (yaani the Ziggurats). Ingawa ni kweli kwamba hawa mawazo yanapatikana katika hadithi za kubuni za Wababeli, Hii haina maana kwamba ndio chanzo cha fikra za Yakobo.

Huu ni mkanganyiko wa sehemu ambapo Mungu na wanadamu hukutana. Hapa inaongezeka dhana ya malaika wa Mungu kupanda na kushuka inamaanisha kuhusisha mambo ya kila siku ya familia, hasa hasa agano la familia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28: 18-22**
**[18] Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe aliloliweka chini ya kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake. [19] Akaita jina la mahali pale Betheli; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu. [20] Yakobo akaweka nadhiri akisema, Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niiendeayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae; [21] nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo Bwana atakuwa Mungu wangu. [22] Na jiwe hili nililolisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu; na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.**

**8:18 "akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake "** Hii nguzo, kwa kiebrania *massebah* (BDB 663), ni kumbukumbu (kama vile 35:14) mahali ambapo Yakobo alikutana na Mungu. Na baadae ikaunganishwa na miungu ya ustawishaji na ikashutumiwa vikali na sheria zilizotungwa kwenye vitabu vitano vya kwanza vya agano la kale. (kwa mfano Kut. 23:24; 34:13; Kumb.16:22).

**28:19 "Akaita jina la mahali pale Betheli "** Hili linatokana na neno la kiebrania kwa ajili ya nyumba, *beth* (BDB 108), na kwa ujumla ni jina la Mungu kwa Mashariki ya kati, *El* (BDB 41). Inafahamika kwa Wakanaani kama Luz, lenye maana "mti wa mlozi" (BDB 531 II,kama vile 35:6; 48:3), lakini kutoka kwenye upeo huu wayahudi huita Betheli (yaani nyumba ya Mungu).

**28:20-22 "kama"** Hii inaonekana ni upungufu wa imani ya Yakobo, lakini ni kama alijaribu kuweka lugha bayana ya ahadi ya Mungu. Yawezekana zaidi kuwa kama SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani na alikuwa na uhakika ya kwamba alichosema Mungu ni kweli na kuweka neno hilo kwa ufahamu na kulishikilia. Katika upeo huu siko tayali kukanusha imani ya Yakobo kwa sababu ya hizi tungo tata.

Kumbuka masharti.
1. Kama Mungu atakuwa naye
2. Kama Mungu atamtunza/ atamwangalia (BDB 1036, KB 1581)
3. Kama Mungu atampa chakula
4. Kama Mungu atamvika
5. Kama atarudi salama kwenye nyumba ya baba yake

Kumbuka matendo aliyoahidi Yakobo.

1. Atapaimalisha mahali pa ndoto na kuliinua jiwe kama nyumba ya Mungu
2. Atamtolea zaka ("nitakutolea wewe sehemu ya kumi" KITENZIJINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIOTIMILIFU toka kwenye mzizi unaofanana [BDB 797, KB 894] kinaonyesha mkazo) Yakobo hakuuliza utajiri lakini riziki na uwepo wa Mungu na ulinzi kwenye safari yake.

**28:22 "nitakutolea wewe sehemu ya kumi"** Zaka kama tohara na sadaka ya kuteketezwa, ilikuwa ni muhimu sana hapo zamani zaidi ya sheria zilizotungwa kwenye vitabu vya mwanzo vya sheria. Tunaona huu Muktadha wa zaka kwenye Mwa. 14:20 na 28:22, zamani kabla Musa hajapokea sheria. Inaonekana ni alama kwamba vyote tulinavyonavyo ni vyake Mungu. Ajabu moja kubwa ni kwa nani ambae Yakobo angempa hii zaka . Hapakuwa na makuhani au mahali halisi palipotengwa na YHWH kwa ajili ya kuteketezea sadaka.

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Yakobo alibadili fikra zake kuhusu Yakobo kuwa mrithi wa ahadi wa  halali?
2. Kwa namna gani mkuu wa ukoo ulimfahamu Mungu?
3. Ni nini maana ya ngazi kugusa mbingu kwa ajili ya Yakobo, na baadae kwa Yesu?
4. Nguzo ni nini na kwa nini ilishutumiwa?
5. Mst wa 22 unasema nini kuhusu zaka?

# MWANZO 29

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakobo akutana Na Raheli | Yakobo anakuta na Raheli | Yakobo anafanikiwa Harani (29:1-31:55) | Yakobo anawasili nyumbani kwa Labani | Yakobo anawasili nyumbani kwa Labani |
| 29:1-3 | 29:1-3 | 29:1-3 | 29:1-3 | 29:1-8 |
| 29:4-8 | 29:4-8 | 29:4-8 | 29:4a | |
| | | | 29:4b | |
| | | | 29:5b | |
| | | | 29:6a | |
| | | | 29:6b | |
| | | | 29:7 | |
| | | | 29:8 | |
| 29:9-12 | 29:9-12 | 29:9-12 | 29:9-12a | 29:9-14a |
| | | | 29:12b-14 | |
| 29:13-14 | 29:13-14 | 29:13-14 | | Ndoa mbili za Yakobo |
| | Yakobo anamwoa Lea na Raheli | | Yakobo anamtumikia Labani kwa ajili ya Raheli na Lea | 29:14b-19 |
| 29:15-20 | 29:15-20 | 29:15-20 | 29:15-17 | |
| | | | 29:18 | |
| | | | 29:19-20 | |
| Udanganyifu wa Labani | | | | 29:20-30 |
| 29:21-30 | 29:21-30 | 29:21-30 | 29:21-25 | |
| | | | 29:26-27 | |
| | | | 29:28-30 | |
| | Wana wa Yakobo (29:31;30:24) | | Wana waliozaliwa kwa Yakobo (29:31-30:24) | Wana wa Yakobo (29:31-30:24) |
| 29:31-35 | 29:31-30:8 | 29:31-30:8 | 29:31-35 | 29:31-30:8 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:1-3**
[1] **Kisha Yakobo akashika njia yake, akafika nchi ya wana wa mashariki.** [2] **Naye akaangalia, na tazama, kiko kisima kondeni, na makundi matatu ya kondoo yamelala karibu nacho, kwa sababu katika kisima kile hunywesha makundi; na palikuwa na jiwe kubwa juu ya kinywa cha kisima.** [3] **Makundi yote hukusanyika huko, watu wakafingirisha hilo jiwe katika kinywa cha kisima wakawanywesha kondoo, na kulirudisha jiwe juu ya kinywa cha kisima mahali pake.**

**29:1 "Kisha Yakobo akashika njia yake "** Kwa uhalisia fungu hili la maneno linatafsiriwa "akaondoka" (BDB 669 na 919). Hii ni sehemu pekee ambapo lugha hii imeonekana kwenye agano la kale. Hii inaonyesha jambo la msisimko na makusudi ambalo Yakobo alihisi baada ya kukutana na Mungu hapo Betheli

◙ **"Akafika nchi ya wana wa mashariki."**Katika Amu.6:3 na 33 Hii inaonekana inalejerea kwenye makabila ya kiarabu (Kama vile Ayu 1:3; Isa. 11:14; Ezek. 25:4,10).Hata hivyo,hapa inaonekana kuelezea wakazi wa Harani (kama vile. Yer. 49:28).kwa kadri iwezekanavyo ,inaelezea makabila ya Kiarabu ya kaskazini kati ya Betheli na Harani ambapo Yakobo aliishi.

**29:2 "Naye akaangalia, na tazama, kiko kisima kondeni"** Na safari ikaishia hapo mst.2 Yakobo akatafuta kuwa karibu na Harani, Lakini halikuwa eneo lake sahihi. Kisimani ni mahala ambapo makundi ya kondoo hukutanika. Uwepo wa Mungu upo wazi pale unapokaa. Harani ni neno la muktadha katika sura ya 29-31.

◙ **"na palikuwa na jiwe kubwa juu ya kinywa cha kisima"** Huu ni utamaduni wa kawaida wa jamii hii ukiwa na maana ya (1) kuzuia mvukizo wa maji (2) maji kuwa safi daima au (3) kwa kusudi la ulinzi ( kutokuwa na ruhusa ya kutumia)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:4-8**
[4]**Yakobo akawauliza, Ndugu zangu, watu wa wapi ninyi? Wakasema, Tu wa Harani sisi.** [5] **Akawauliza, Je! Mnamjua Labani, mwana wa Nahori? Wakasema, Tunamjua.** [6] **Akawauliza, Je! Hajambo? Wakasema, Hajambo; tazama, Raheli binti yake anakuja na kondoo.** [7] **Akasema, Tazama, ukali mchana bado, wala sio wakati wa kukusanya wanyama; wanyweshéni kondoo, mwende kuwalisha.** [8] **Wakasema, Hatuwezi, hata yakusanyike makundi yote, watu wakafingirishe jiwe katika kinywa cha kisima, ndipo tunapowanywesha kondoo.**

**29:4 "Ndugu zangu "** Hili neno hutumika (BDB 26) kwa kusalimiana bila kutaja mahusiano ya familia husika. Siku hizi pia tunatumia salamu hii kwa washirika wa kikristo Amerika ya kusini.

Kwenye mst. 12 na 15 Neno limetumika kama jamaa,lakini kwa uhalisia sio tena "ndugu".Utambulisho huu wa familia unaitwa "mfupa wangu na nyama yangu" kwenye mst 14 (kama vile Mwa. 2:23).

**29:5 "Mnamjua Labani, mwana wa Nahori"**Hapa ni mfano mzuri ambapo neno "mwana" (BDB 119) kwa lugha ya kiebrania linaelezea "Baba" au "Babu". Bethueli ni baba yake Labani na Nahori ni babu yake ( kama vile Mwz.24:24,29).

**29:6"Je! Hajambo? Wakasema, Hajambo"** Hili neno *shalom* (BDB 1022). Tazama Mada maalumu ya 15:15.

◙**"Raheli binti yake anakuja na kondoo"** Kwa watumishi wa Mungu hakuna ulinganifu wa maisha (kama vile. 24:15; Kut. 2:16, Tazama. *The Christian's Secret of a Happy Life* by Hannah Whithall Smith). Kuna mkono wa Mungu usioonekana hapa, Kama ulivyokuwa na Yusufu katika Mwa. 37:15-17 (Pia katika kitabu cha Esta ambapo jina la Mungu halionekani kamwe lakini uwepo na uongozi wake ulikuwa dhahili).

**29:7 "Tazama, ukali mchana bado"**Yakobo alikuwa ni mchungaji na alijua atafanya zoezi gani dhidi ya wachungaji imara aliowakuta hapo kisimani(Maarifa hayo yatamshawishi na kuvutia Labani).Hii itamfanya yeye kuonyesha uwezo na nguvu zake(kama vile mst 10) kwa ajili ya Raheli! Kwa dhahili,alifanikiwa!Raheli alishikwa na mshangao mgeni huyu alipombusu (kama vile.mst. 11),lakini alifurahia zaidi baada ya Yakobo kumwambia kuwa yeye ni nani.Kitendo cha Yakobo kulia kilionyesha mwelekeo wa utamaduni wa watu wa kawaida wa kuonyesha hisia zao zaidi ya wenzi wao wa magharibi(kama vile mst 13).

Yakobo alivaa mavazi kama wachungaji wengine ambao walitumia mbinu ya kuonekana KUSHURUTISHWA kuwa dhaifu sana kwa kuwaangalia mara moja ungehoji maswali kuwahusu.

1. maji, BDB 1052, KB 1639, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. nenda, BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. marisho, BDB 944, KB 1258, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:9-12**
**[9]Hata alipokuwa akisema nao, Raheli akaja na kondoo za baba yake, maana aliwachunga. [10] Ikawa Yakobo alipomwona Raheli binti Labani, ndugu wa mamaye, na kondoo za Labani, ndugu wa mamaye, Yakobo akakaribia, na kulifingirisha lile jiwe litoke katika kinywa cha kisima, akawanywesha kondoo za Labani, ndugu wa mamaye. [11] Yakobo akambusu Raheli, akainua sauti yake akalia. [12] Yakobo akamwarifu Raheli ya kuwa yeye ni ndugu wa babaye, na ya kuwa ni mwana wa Rebeka. Basi akapiga mbio akampasha babaye habari**.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:13-14**
**[13] Ikawa Labani aliposikia habari za Yakobo, mwana wa nduguye, akaenda mbio amlaki, akamkumbatia, akambusu, akamleta nyumbani kwake. Naye akamwambia Labani maneno hayo yote. [14] Labani akamwambia, Ndiwe kweli mfupa wangu na nyama yangu. Naye akakaa kwake muda wa mwezi mmoja**

**29:13 Ikawa Labani aliposikia habari za Yakobo, mwana wa nduguye, akaenda mbio amlaki"** Waalimu wa sheria wanasema kuwa Labani alimkimbilia Yakobo kwa sababu alidhania kuwa ana vitu kama Eliazeri alivyomletea hapo kabla.(Mwa. 24:10) Hata hivyo, katika habari hii siwezi kutilia shaka nia yake. ukweli ni kwamba Labani alitoka nje kumtawala Yakobo,mtawala mwenye hila,lakini huu ni mpango wa Mungu juu ya kumkomaza Yakobo.

**29:14 "mwezi"** Ni neno (BDB 294) linalohusika na neno "mwezi" (BDB 294). Waebrania walitumia mwezi kama alama kwenye kalenda zao (yaani mwezi mpya,).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 29:15-20**
**[15] Labani akamwambia Yakobo, Kwa sababu wewe ni ndugu yangu, basi, je! Unitumikie bure? Niambie mshahara wako utakuwa nini? [16] Labani alikuwa na binti wawili, jina la mkubwa ni Lea, na jina la mdogo ni Raheli. [17] Naye Lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri uso. [18] Yakobo akampenda Raheli akasema, Nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo. [19] Labani akasema, Afadhali nikupe wewe kuliko mtu mwingine; kaa kwangu. [20] Yakobo akatumika miaka saba kwa kumpata Raheli. Ikawa machoni pake kama siku chache tu kwa vile alivyompenda.**

**29:15** Jambo hili ni gumu na linatatiza, lakini inaonekana kuwa Labani alijua kuwa Yakobo anampenda sana Raheli na akawa anatumia njia ya kumzungusha maana Yakobo hakuwa na mali hivyo hana budi kumtumikia. Yawezekana ule ujuzi wake wa kichungaji alikuwa nao.

**29:16 "Lea,"** Elimu ya asili ya jina lake (BDB 521, KB 513) ni cha mabishano: (1) Asili ya Akkadia "ng'ombe" (2) Asili ya kiarabu "nyati; au (3) "aliyechoka kuishi" (kutoka KITENZI, KB 512). Kutoka mst. 17 inaonekana Lea hakuwa na umbo la kuvutia kama alivyokua Raheli.

◙**"Raheli"** Jina lake lina maana ya "Kondoo jike" (BDB 932, KB 1216). Ni dhahili;watu wanao hamahama huwapa watoto wao majina ya wanyama.

◙

| | |
|---|---|
| **29:17** | |
| **NASB, RSV,** | |
| **JPSOA, NIV,** | |
| **LXX** | **"macho yalikuwa dhaifu"** |
| **NKJV** | **"macho yalikuwa laini"** |
| **NRSV** | **"macho yalikuwa kupendeza"** |
| **TEV, NJB** | **"macho ya kupendeza"** |
| **REB** | **"macho ya kufifia"** |
| **Peshitta** | **"macho ya kuvutia"** |

KIVUMISHI chenye (BDB 940, KB 1230) kinamaanisha

1. Asili ya kiebrania-laini, mwororo, mwembamba
2. Asili ya kiarabu-dhaifu, nyembamba, maskini

Tafasiri nyingi za kiingereza hutumia muktadha wa kiarabu kwa sababu ya maana ya asili ya jina.lakini ukurasa huu unajaribu kuonyesha sifa za wasichana wote.

◙ **"mzuri wa umbo, na mzuri uso"**KIVUMISHI (BDB 421) kimetumika mara mbili UUNDAJI wa aina mbili

1. BDB 421 na 1061 inamaanisha kutopendelea/mzuri wa umbo
2. BDB 421 na 909 inamaanisha kutopendelea/ mzuri kwa muonekano

Wanawake wote wa awali wa mababa wa imani walikuwa wazuri,wakuvutia (lakini tasa)

**29:18 "Yakobo akampenda Raheli . . . Nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo."**Hii ni ahadi ya hatari sana,zaidi sana kuliko Labani alivyouliza. Lakini alisisimka na kuchukua hatua kwa ajili yake.upendo wao wa kweli kati ya hawa wawili unaonekana mst . 19-20,30.

**29:19 "kaa kwangu"** Hii ni amri (BDB 442, KB 444, *Qal* KAULI SHURUTISHI), lakini kwa muktadha ni njia ya watu wanao hama hama kumkubalia Yakobo amtumikie Labani kwa miaka saba kama gharama ya bibi arusi.

**ANDIKO LA NABS (LILILOBORESWA) 29:21-30**

**[21] Yakobo akamwambia Labani, Nipe mke wangu, maana siku zangu zimetimia; niingie kwake. [22] Labani akakusanya watu wote wa mahali pale, akafanya karamu. [23] Ikawa wakati wa jioni akamtwaa Lea, binti yake, akamletea Yakobo, naye akaingia kwake. [24] Labani akampa Lea mjakazi wake Zilpa, awe mjakazi wake. [25] Ikawa, kulipokuwa asubuhi, kumbe! Ni Lea. Akamwambia Labani, Nini hii uliyonitenda? [26] Sikukutumikia kwa Raheli? Mbona umenidanganya? Labani akasema, Havitendeki hivi kwetu, kumtoa mdogo kabla ya mkubwa; [27] timiza siku zake saba, nasi tutakupa huyu naye kwa utumishi utakaonitumikia, miaka saba mingine. [28] Yakobo akafanya hivi, akatimiza siku zake saba. Naye akampa Raheli binti yake kuwa mkewe. [29] Labani akampa binti yake Raheli mjakazi wake Bilha, awe mjakazi wake. [30] Akaingia kwa Raheli naye, akampenda Raheli kuliko Lea, akatumika kwa ajili yake miaka saba mingine.**

**29:21 "Yakobo akamwambia Labani, Nipe mke wangu, maana siku zangu zimetimia; niingie kwake "** Ni dhahili, Labani hakuwa na haraka hata mwisho wa miaka saba,kumpa Yakobo binti yake.Hii ilionyesha tabia Fulani itakayo onekana kupitia mstari huu kuhusiana na mbinu za hila za Labani. Alikuwa anataka kujua mambo ya familia yake kwa haraka.

**29:23 "Yakobo akaingia kwake"** Kulikuwa na mashauliano zaidi juu ya Yakobo kwa nini,baada ya muda wote huu,hakumjua kwamba huyu ni Lea.Baadhi ya nadharia zinasema (1) Ilikuwa giza (yaan.,mst 23,"wakati wa jioni");

(2) Alikuwa amejifunika (kama vile.24:65);(3) Alikuwa amelewa(neno "karamu" [BDB 1059]kwenye mst . 22 ni kutoka kwenye asili ya "kunywa" [BDB 1059], inaonyesha sherehe za kienyeji ) Hii inanionyesha kwamba namba (3) inafaa kwa muktadha zaidi.

**29:24 "Labani akampa Lea mjakazi wake Zilpa, awe mjakazi wake "**Tunajifunza kutoka vigae vya Nuzi, ambapo inaelezea utamaduni wa Hurria kwa wakati mmoja(miaka elfu mbili kabla ya kristo),Hili ni jambo la kawaida .kwa kuwa binti alikuwa tasa,mjakazi angemzalia mwana badala yake(kama vile mst. 28-29; 30:3). Mstari wa 24 na 29 imetengwa na msimuliaji kutuandaa kwa ajili ya sura ya 30.

**29:25"kumbe! Ni Lea"** Ingawa tabia hii ilikuwa dhahili kutoka kwa Labani ni jambo ambalo lilitarajiwa, Inashangaza kuwa Lea hakusema chochote na hata Raheli nae hakusema jambo lolote. Lakini ni lazima kwenye siku hizi tuhukumu tamaduni zao sio za kwetu,Na kwa sababu ya ukosefu wa maandiko ulio dhahili tafsiri ya kisasa ni lazima isiwe ya kukisia.

**29:27 "timiza siku zake saba, nasi tutakupa huyu naye kwa utumishi utakaonitumikia, miaka saba mingine"** Hii wiki ya harusi ilikuwa ni ya kawida kwenye utamaduni huu (kama vile (Wam. 14:12,17). Pia inaaksi zaidi kwenye kitabu cha Tobiti 11:18. Dhana ya mwezi kugawanywa ndani ya wiki ni la kipee kibiblia (kama vile Mwa. 2:1, 2). Tendo la Labani lilitengeneza maombi yasiyo aminika ya kuwa Yakobo kumtumikia miaka saba zaidi kulionyesha tendo la ujasiri la mwanaume huyu.Yakobo alikutana na mchezo na sasa anatambua vile alivyofanyiwa hila (kama vile 27:35).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:31-35**
**[31] Bwana akaona ya kwamba Lea hakupendwa, naye akafungua tumbo lake; bali Raheli alikuwa hazai. [32] Lea akapata mimba akazaa mwana, akampa jina lake, Reubeni, maana alisema, Kwa kuwa Bwana ameona teso langu; sasa mume wangu atanipenda. [33] Akapata mimba tena akazaa mwana, akasema, Kwa kuwa Bwana amesikia ya kwamba mimi sikupendwa, amenipa na huyu; akamwita jina lake Simeoni. [34] Akapata mimba tena, akazaa mwana, akasema, Basi wakati huu mume wangu ataungana nami, kwa sababu nimemzalia wana watatu. Kwa hiyo akamwita jina lake Lawi. [35] Akapata mimba tena, akazaa mwana. Akasema, Mara hii nitamsifu Bwana; kwa hiyo akamwita jina lake Yuda; akaacha kuzaa**

**29:31 "hakupendwa"** Hii ni nahau ya kiebrania ambayo kwa uhalisia ni,"Chukia" (BDB 971, KB 1338, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU, kama vile mst. 33),lakini kwa sababu imetumika Kumb. 21:15; Mal. 1:2-3; Yoh. 12:25 na Luka 14:26, tunafahamu kwa kawaida nahau ya mlingano ambayo inatafsiriwa "hakupendwa " na sio atanipenda. Inaongelea kipaumbele.Yakobo alimpenda Raheli zaidi kuliko Lea.

**29:32 "Lea akapata mimba akazaa mwana, akampa jina lake, Reubeni"** Rabani (BDB 910, "tazama mwana" kutoka kitenzi "tazama", BDB 909) ni neno pendwa ambalo linatokana na neno la elimu ya asili ya "kuona" (BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI TIMILIFU, "kuona").

◙ Kuzaa mwana ni heshima kubwa. Lea alijihakikishia Yakobo angemfurahia kwa ufahamu na uangalifu zaidi.

**29:33 "Akapata mimba tena akazaa mwana......akamwita jina lake Simeoni "** Neno "Simeoni" (BDB 1035) ni neno pendwa ambalo linatokana na neno la kiebrania "amesikia " au "Bwana amesikia " (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI TIMILIFU).

**29:34 "Akapata mimba tena, akazaa mwana.......akamwita jina lake Lawi"** Jina hili (BDB 532 I) ni neno pendwa ambalo linatokana elimu ya asili kwa " ataungana" (BDB 530 I, KB 522, *Niphal* KAULI ISIOTIMILIFU). Lea alikuwa na hisia za ndani zaidi za mahusiano na Yakobo.

**29:35 "Akapata mimba tena akazaa mwana..........akamwita jina lake Yuda"** Huyu ni mwana ambaye Mungu alimchagua kutimiliza ahadi zake. Jina lake lina maana "nitamsifu" (BDB 397), ambalo lina maana" nitamsifu YHWH" (BDB 392, KB 389, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU). Jina lake likawa jina la kabila na baadae taifa, na baadae kwa wayahudi wote. Wana watatu wakubwa walikataliwa kwa sababu ya matendo yao yasiyofaa. Tena Mungu akampendelea kwa kumchagua mwanamke asiye pendwa kumleta masihi. Upinduaji huu wa tukio lililotarajiwa kwenye kitabu cha Mwanzo na kuonyesha YHWH anaongoza na kutawala.

# MWANZO 30

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Wana wa Yakobo | Watoto wa Yakobo (29:31-30:24) | Yakobo anafanikiwa Harani (29:1-31:55) | Watoto waliozaliwa kwa Yakobo (29:31-30:24) | Watoto wa Yakobo (29:31-30:24) |
| 30:1-13 | | | 30:1 | 29:31-30:8 |
| | | | 30:2 | |
| | | | 30:3-8 | |
| | 30:9-13 | 30:9-13 | 30:9-13 | 30:9-13 |
| 30:14-21 | 30:14-21 | | 30:14 | 30:14-21 |
| | | | 30:15a | |
| | | | 30:15b | |
| | | | 30:16 | |
| | | | 30:17-21 | |
| 30:22-24 | 30:22-24 | 20:22-24 | 30:22-24 | 30:22-24 |
| Mali za Yakobo | Makubaliano kati ya Yakobo na Labani | | Majadiliano ya Yakobo na Labani | Yakobo alivyopata utajiri |
| 30:25-36 | 30:25-36 | 30:25-36 | 30:25-26 | 30:25-31 |
| | | | 30:27-28 | |
| | | | 30:29-30 | |
| | | | 30:31a | |
| | | | 30:31b-33 | |
| | | | | 30:32-36 |
| | | | 30:34-36 | |
| 30:37-43 | 30:37-43 | 30:37-43 | 30:37-39 | 30:37-43 |
| | | | 30:40 | |
| | | | 30:41-43 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakinini mwongozo wakufuata kusudio la mwandish wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya yapili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:1-8**
**[1] Naye Raheli alipoona ya kuwa hamzalii Yakobo mwana, Raheli alimwonea ndugu yake wivu. Akamwambia Yakobo, Nipe wana; kama sivyo, nitakufa mimi. [2] Yakobo akamghadhibikia Raheli, akasema, Je! Mimi ni badala ya Mungu, aliyekuzuilia uzao wa mimba? [3] Akasema, Yuko mjakazi wangu, Bilha, uingie kwake ili kwamba azae juu ya magoti yangu, nami nipate uzao kwa yeye. [4] Basi akampa Bilha mjakazi wake kuwa mkewe. Yakobo akaingia kwake. [5] Naye Bilha akapata mimba, akamzalia Yakobo mwana. [6] Raheli akasema, Mungu amenipa haki yangu, naye amesikia sauti yangu, akanipa mwana. Kwa hiyo akamwita jina lake Dani. [7] Bilha, mjakazi wa Raheli, akapata mimba tena, akamzalia Yakobo mwana wa pili. [8] Raheli akasema, Kwa mashindano makuu nimeshindana na ndugu yangu, nikashinda. Akamwita jina lake Naftali**

**30:1 "alimwonea ndugu yake wivu "** Kiuhalisia hii ni kusema "alionyesha chuki usoni" (kutoka kwenye mzizi wa neno la kiarabu BDB 888, KB 1109, *Piel* KAULI ISIOTIMILIFU). Inavyoonekana aliamua kutomwonea wivu Yakobo ("Nipe wana"; BDB 396, KB 393, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU), ambaye hakumkubali hata kidogo (kama vile mst 2)utasa ulionekana ni kawaida kwa wake wa wakuu wa familia. Ukosefu wa subira wa Raheli umeonekana kwenye mst . 1, Pale Rebeka alipoomba kwa miaka zaidi ya ishirini.Baada Lea kupata watoto wane, Raheli aliona wivu, hasira na kukoswa subira.

**30:3 "Yuko mjakazi wangu, Bilha, uingie kwake ili kwamba azae juu ya magoti yangu,"** Hii ni nahau ya kitamaduni inayoonekana kumaanisha kitendo cha kupanga mtoto (kama vile Mwa. 48:12). Tunafahamu kutoka kwenye sheria zilizopangwa za Lipit-Ishtar, alama za siri toka kwenye sheria za Mesopotamia, bamba za maandiko ya Nuzi, bamba za maandiko ya Mali, na bamba za maandiko ya Alalakh kwamba hizi ni tamaduni halisia. Hatuwezi kuhukumu maadili ya desturi hizi kwa wakati wetu huu.Mkanganyiko wa Raheli unaweza kuonekana kutokana na amri kadhaa alizotao.

1. Uingie kwake, BDB 97, KB 112, *Qa/ K*AULI SHURUTISHI (maombi ya nguvu)
2. ili kwamba azae, BDB 408, KB 411, *Qa/* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI
3. nami nipate uzao kwa yeye, ( kifasihi Ninaweza kujengwa, BDB 124, KB 139, *Nipha/*KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU imetumika kwenye HALI YA KUSIHI

**30:5-6 "Naye Bilha akapata mimba, akamzalia Yakobo mwana.......Dani** Jina la "Dani" ni neno la kiebrania lenye maana "hakimu" (BDB 192). Binti atakayezaliwa kwenye mst. 21 ni wa muundo wa jinsi ya kike wa neno sawa na(Dina, BDB192)

◙
**30:8**
**NASB, NRSV "mapambano makuu"**
**NKJV "mapambano makubwa"**
**TEV "mapigano magumu"**
**NJB "vita vya maangamizi**
**LXX "kushindana"**

Tatizo ni kwamba toleo la MT lina neno "*elohim*," ambalo lingaliweza kumaanisha Raheli alipambana na Mungu au kutafsiriwa kama yenye kuelezea " Ukuu/mwenye uweza " na kuonekana kisitiari lenye kumaanisha pambano la mieleka na Lea. Yumkini inahusiana kote kiroho (Mungu) na kimwili (dadaye) akipambana na utasa wake (kama vile toleo la Kishamu).

◙**"Naftali"** Neno hili linahusiana na neno "mapambano" (kifasihi "kumenyana," BDB 836).Alikuwa anapambana na dada yake kwa ushindani na kwa maombi na Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:9-13**
**[9] Lea alipoona ya kuwa ameacha kuzaa, alimtwaa Zilpa, mjakazi wake, akampa Yakobo kuwa mkewe. [10] Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana. [11] Lea akasema, Bahati njema! Akamwita jina lake Gadi. [12] Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana wa pili. [13] Lea akasema, Ni heri mimi, maana wanawake wataniita heri. Akamwita jina lake Asheri.**

**30:9** Kulikuwa na mashindano ya kweli kati ya hawa wasichana/wanawake!

**30:10-11 "mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana........ Gadi "**Neno Gadi (BDB 151 III) linatokana na neno la kiebrania "Bahati" au "Bahati njema" (BDB 151 II).

Andiko la Kimasoreti lina neno "kwa bahati njema," lakini kumbukumbu za pambizo za wasomi wa andiko la Kimasoreti lina neno "bahati njema imewadia").inawezekana kwamba Gadi (גד, BDB 151 III) alitokana na

1. Kundi la askari, גדיד, BDB 151 I, NKJV (tanbihi kwenye toleo la NIV )
2. Bahati, גד, BDB 151 II, LXX, NASB, NRSV, TEV, JPSOA, NJB, REB, Peshitta
3. Furaha, LXX

**30:12 "Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana........Asheri"** Jina hili linahusiana na neno la kiebrania "furaha" (BDB 81).

**30:13 "Asheri"** Jina hili (BDB 81)linatokana na KITENZI "furaha" (BDB 80, KB 97 II, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU), lenye maana ya "kuwa na furaha" au "kubarikiwa"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:14-21**
**[14] Reubeni akaenda siku za mavuno ya ngano akaona tunguja kondeni, akazileta kwa Lea mamaye. Ndipo Raheli akamwambia Lea, Nipe mimi baadhi ya tunguja za mwanao. [15] Naye akamwambia, Je! Ni jambo dogo kuninyang'anya mume wangu; hata wataka kuzitwaa tunguja za mwanangu pia? Raheli akamwambia, Kwa hiyo atalala kwako usiku huu kwa tunguja za mwanao. [16] Yakobo akaja kutoka kondeni jioni, Lea akatoka kumlaki, akasema, Lazima uje kwangu, kwa sababu nimekuajiri, kwa tunguja za mwanangu; akalala kwake usiku ule. [17] Mungu akamsikia Lea, naye akapata mimba, akamzalia Yakobo mwana wa tano. [18] Lea akasema, Mungu amenipa ujira wangu, kwa sababu nimempa mume wangu mjakazi wangu. Akamwita jina lake Isakari. [19] Lea akapata mimba tena, akamzalia Yakobo mwana wa sita. [20] Lea akasema, Mungu amenipa mahari njema, sasa mume wangu atakaa nami, kwa kuwa nimemzalia wana sita. Akamwita jina lake Zabuloni. [21] Baadaye akazaa binti, akamwita jina lake Dina.**

**30:14 "Reubeni akaenda siku za mavuno ya ngano akaona tunguja kondeni, akazileta kwa Lea mamaye. Ndipo Raheli akamwambia Lea "** Tunguja (BDB 188) dawa ya kuamsha hisia ( za kiume/kike) kwa watu wa kale (kama vile Wimb . 7:13). Huenda matunda yake ya njano au mizizi yake ilifanana na mwanaume, ni mapokeo ya asili ya jamii hii. Raheli aliyataka haya na akatumai ya kuwa atapata mtoto wa kiume (tena agano la familia akijaribu kumsaidia Mungu). Mgogoro kati ya hawa dada wawili unakuja kuwa wazi na dhahili kwenye hili jambo. Kinachonishangaza mimi ni kwa namna gani Yakobo alitawaliwa kwa urahisi na migogoro ya wanawake hawa wawili waliokuwa na ugomvi kati yao ( kama vile mst . 15-16).

**30:16 "kwa sababu nimekuajiri "** Hiki ni KITENZIJINA HALISI na KITENZI TIMILIFU chenye kutoka kwenye mzizi ule ule wa neno (BDB 968, KB 1330), kinachomaanisha mkazo zaidi. Yakobo alikwisha tawaliwa na mapenzi ya wake zake wawili. Jina la Isakari (tazama chini) linaakisi huzuni ya mashindano haya.

**30:18 "Isakari"** Jina Isakari (יִשָּׂשכָר, BDB 441) linahusika na neno la kiebrania "Ujira" au "sifia" (שָׂכָר, BDB 969). Lea aliukodi upendo wa Yakobo kwa tunguja za Reubeni!

**30:19-20 "Lea akapata mimba tena, akamzalia Yakobo mwana wa sita...... Zabulon "** Neno Zabuloni (BDB 259) Ni mchezo wa maneno ya Kiebrania kwa ajili ya neno "zawadi" au "mahari" (BDB 256) na neno "kukaa" au "heshima" (BDB 269). Wake zake waliendelea kugombana juu ya upendo wake.

**30:21 "Baadaye akazaa binti, akamwita jina lake Dina"** Hii inaonyesha ni binti pekee aliyezaliwa kwenye hii familia. Ukweli kwamba ni mmoja tu aliyeitwa jina hili inatuonyesha kwamba yumkini palikuwepo na binti mmoja tu. Hata hivyo, angalia sura ya 37:35.Ingawa, nafasi ya Dina katika simulizi za baadaye zawezakuwa ndiyo sababu ya kulitaja jina hili moja la huyu binti.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:22-24**
**22 Mungu akamkumbuka Raheli; Mungu akamsikia, akamfungua tumbo. 23 Akapata mimba, akazaa mwana, akasema, Mungu ameondoa aibu yangu. 24 Akamwita jina lake Yusufu, akisema, Bwana aniongeze mwana mwingine.**

**30:22-24 "Mungu akamkumbuka Raheli; Mungu akamsikia, akamfungua tumbo" J**ina "Yusufu " (BDB 415) linahusiana na moja ya VITENZI viwili vya kiebrania.

1. "akamwondolea aibu" (BDB 62, KB 74, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile mst wa 23) au
2. "aniongezee" (BDB 414, KB 418, *Hiphil* KITENZI CHA HALI YA KUSIHI) akimuuliza Mungu juu ya mwana mwingine wa kiume( kama vile 35:17)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:25-36**
**25 Ikawa Raheli alipomzaa Yusufu, Yakobo akamwambia Labani, Nipe ruhusa niende kwetu, na kwenye nchi yangu. 26 Nipe wake zangu na watoto wangu, niliokutumikia, niende zangu, maana umejua utumishi wangu niliokutumikia. 27 Labani akamwambia, Iwapo nimeona fadhili machoni pako, kaa, maana nimetambua ya kwamba Bwana amenibariki kwa ajili yako. 28 Akasema, Sema mshahara wako utakao, nami nitatoa. 29 Akamwambia, Umejua jinsi nilivyokutumikia, na jinsi wanyama wako walivyokuwa kwangu. 30 Maana mali yako ilikuwa haba kabla sijaja, nayo imezidi kuwa nyingi, Bwana akakubariki kila nilikokwenda. Basi sasa, nitaangalia lini mambo ya nyumba yangu mwenyewe? 31 Akamwuliza, Nikupe nini? Yakobo akasema, Usinipe kitu; ukinifanyia neno hili, nitalisha wanyama wako tena na kuwalinda. 32 Nitapita katika wanyama wako wote leo, na kutoa huko kila mnyama aliye na madoadoa na marakaraka, na kila mnyama mweusi katika hao kondoo, na aliye na marakaraka na madoadoa katika mbuzi; nao watakuwa mshahara wangu. 33 Na haki yangu itanishuhudia katika siku zijazo, utakapokuja kwa habari ya mshahara wangu ulioko kwako. Kila asiye madoadoa au marakaraka katika mbuzi, au asiye mweusi katika kondoo, akionekana kwangu, itahesabiwa kuwa ameibiwa. 34 Labani akasema, Tazama, na iwe hivi kama usemavyo. 35 Basi akatoa siku ile mbuzi waume walio na milia na madoadoa, na mbuzi wake walio na madoadoa na marakaraka, kila aliye na doa jeupe, na kondoo wote waliokuwa weusi, akawatia mikononi mwa wanawe. 36 Akajitenga na Yakobo mwendo wa siku tatu; naye Yakobo akachunga wanyama wa Labani waliosalia**.

**30:25-26 "Nipe ruhusa niende kwetu, na kwenye nchi yangu."** Ni wazi kiutamaduni ilikuwa ni kawaida kwa Labani amtoe Yakobo aende zake badala ya Yakobo kuomba ruhusa ya kuondoka. Ni wazi alijaribu kuondoka mara nyingi na wakati wote kupata majibu yasiyo kubalika. Labani alitaka Yakobo aendelee kukaa kwa sababu alikuwa na manufaa kwake(kama vile mst 27).

Mstari wa 25 na 26 una lugha nzito.

1. "Nipe ruhusa niende,"mst. 25, BDB 1018, KB 1511, *Piel* KAULI SHURUTISHI
2. "kwenye nchi yangu," mst. 25, BDB 229, KB 246, *Qal* HALI YA KUSIHI
3. "nipe wake zangu na watoto wangu,"mst 26, BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI SHURUTISHI

4. “niende zangu ” BDB 229, KB 246, Qal HALI YA KUSIHI
KITENZI “ nilivyokutumikia” (BDB 712, KB 773) kimetumika mara mbili (kama vile mst 29), Ilionyesha mtazamo wa Yakobo kuwa amekwisha kumlipa Labani yote aliyokuwa anamdai (na zaidi mst 30)!

**30:27 “maana nimetambua ya kwamba Bwana amenibariki kwa ajili yako”** Neno “nimetambua” linatoka kwenye mzizi wa neno “kubeza” au “nong’ona” (BDB 638 II). Ni kujaribu kujua na kutawala yajayo kupitia namna ya kimwili mbali na kumtumaini YHWH. Ilihukumiwa kwenye Law.19:26; Hes.23:23-24; na Kumb. 18:10.
Ni vigumu kutambua kwa nini watu hawa wa kwanza kwenye kitabu cha Mwanzo walitumia vitu ambavyo baadae vilishutumiwa kwenye sheria ya vitabu vitano vya agano la kale.

1. Kusimamisha mawe
2. Uaguzi, hapa na 44:5,15 (Yusufu)
3. Uigaji wa kichawi (yaani fimbo ya mistari kutoa wanyama wenye mistari)
4. Kutumia tunguja kwa ajili ya kutungisha mimba
5. Vinyago vya kaya (*teraphim*)
6. Tohara za wapagani (kama ngao)

Kwenye siku hizi za mwanzo za YHWH, matukio ya zamani yaliathiriwa na tamaduni zao. Walisonga mbele kwa kung’ang’ania mno, zaidi wakikamilisha lengo la kuwa na mungu mmoja tu, lakini barabara ilikuwa ndefu mbele yao!

**30:28 “Akasema, Sema mshahara wako utakao, nami nitatoa”** Labani alitambua wazi kuwa mali zake zilitokana na Yakobo na alitaka kumzuia kwa gharama yoyote ile.
KITENZI cha neno “jina” (BDB 666, KB 718, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kina elimu maana pana. kwa kawaida ina maana “kutoboa” au “pekecha” Hapa inaonyesha Yakobo alitaja fidia yake ili aweze kubaki na Labani.
KITENZI cha pili cha neno “nipe” (BDB 678, KB 733, *Qal* HALI YA KUSIHI) kinamwashiria msomaji kuwa Labani alitambua uwepo na msaada wa Yakobo (kama vile mst 30). Labani lazima alitaka awe baba mkwe (kama vile 31:11-12). Na hata maandiko yanadokeza kuwa Yakobo anaonekana alimchukulia kama mtumishi aliyeajiliwa. (kama vile 31:14-16).

**30:30 “Bwana akakubariki kila nilikokwenda ” Y**akobo alitambua kuwa chanzo cha baraka za Labani ni yeye na pamoja na mahusiano yake na YHWH. Lakini, kama mst . 30 na kuendelea, inaonyesha kwamba pia Yakobo alitambua mahitaji ya kaya yake.

**30:31 “Akamwuliza, nikupe nini? Yakobo akasema, Usinipe kitu”** Yakobo alitambua kuwa chanzo cha baraka sio Labani lakini ni Mungu.

**30:32** Yakobo anajiandaa kuwaondoa wale wanyama wenye madoamadoa toka kwenye kundi la mbuzi na kondoo (BDB 378, KB 375, imetumika mara tano kwenye mst 32-35). Katika kundi la kondoo ni yule aliye mweusi na katika kundi la mbuzi ni yule aliye na madoadoa au marakamaraka. Wanyama hawa waliokuwa na rangi isiyo ya kawaida walikuwa wazuri mno. Hii kwa uwazi ndio sababu Yakobo kwa muda huu alimtambua Labani na yeye hakutaka maswali kuhusu nani alikuwa nani siku zijazo. (kama vile mst. 33).

**30:35-36 Basi akatoa siku ile mbuzi waume walio na milia na madoadoa, na mbuzi wake walio na madoadoa na marakaraka, kila aliye na doa jeupe, na kondoo wote waliokuwa weusi, akawatia mikononi mwa wanawe ” H**ivi ni vitu viwili vya maana sana katika ukurasa huu na kwenye mst . 36. Neno “yeye” katika mwanzo wa mst 35 kwa uwazi inamaanisha Labani. Hii ni kwa mara ya kwanza inawataja wana wake. Kwa dhahili, Labani anagawa kundi na kuwapa wanyama wa Yakobo kuwa chini ya ungalizi wa wanawe(Labani). Kutoka mst .36 tunaona kwamba

Labani anawapeleka wanyama wa Yakobo safari ya mwendo wa siku tatu ili wasizaane na wanyama wake. Hii ilimlazimu Yakobo kuwachunga wanyama wa Labani ili kujihakikishia baraka toka kwao. Ingawa vitu vyote vilikuwa upande wa Labani, lakini Mungu alikuwa na Yakobo. Mimi mwenyewe siwezi kuamini kuwa mbinu za Yakobo zilizotajwa kwenye mst . 37 na kuendelea ndio chanzo cha wanyama wa madoadoa na marakamaraka kuzidishwa kwa haraka, lakini ni Nguvu ya uwepo wa Mungu.

Rejeo la usomaji wa Biblia ya NIV linatetea kwamba mst. 35 ilifanywa kwa siri na Labani na wanawe ili kupunguza au kuondosha wanyama wote wa rangi isiyoyakawaida. Kama ni hivyo, basi madai ya Yakobo yalikuwa yanamaanisha uzao wa baadae. Niliposoma hii sikuona mst 35 kama ni muhimu kuwa na kidokezo hiki , lakini hainishangazi kujua asili ya Labani ya kutawala kwa hila.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:37-43**
**37 Yakobo akatwaa fito za mlubna mbichi, na mlozi, na mwaramoni, akazibambua maganda, mistari myeupe ionekane ndani ya hizo fito. 38 Akazisimamisha fito hizo alizozibambua katika mabirika ya kunyweshea maji, pale walipokuja wanyama wanywe; wakachukua mimba walipokuja kunywa. *39* Wanyama wakapata mimba mbele ya hizo fito, wakazaa wanyama walio na milia, na madoadoa, na marakaraka. *40* Na Yakobo akawatenga wana-kondoo, akazielekeza nyuso za makundi zielekee wale waliokuwa na milia, na kila aliyekuwa mweusi katika wanyama wa Labani. Akaweka kando wanyama wake mwenyewe, wala hakuwachanganya pamoja na wanyama wa Labani. 41 Ikawa kila walipopata mimba wanyama wenye nguvu, Yakobo akaziweka zile fito mbele ya macho ya hao wanyama katika mabirika ili kwamba wachukue mimba kati ya zile fito, 42 lakini wanyama walipodhoofika hakuziweka zile fito. Basi wale dhaifu walikuwa wa Labani, na wenye nguvu walikuwa wa Yakobo. 43 Kwa hiyo mtu huyo akazidi mno, akawa na wanyama wengi, na vijakazi, na watumwa, na ngamia, na punda.**

**30:37-43** Hii tena inaonekana kama familia ya ubaba wa imani inajaribu kumsaidia YHWH kutimiza ahadi zake! Ikiwa mbinu hii ilifanya kazi (yaani, kuwepo kwa kemikali kwenye mmea) au laah sio suala la kithiolojia, Yakobo mhadaaji, yuko bado katika kazi. Ni kweli kwamba ahadi za YHWH zinategemea matendo ya Yakobo?

**30:43** Makundi ya wanyama ya Yakobo na yalikua kwa miaka mingi (Labda mara sita zaidi baada ya kuwekwa chini ya uangalizi, kama vile 31:41).

## MASWALI YA MJADALA KWA SURA YA 29-30

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

1. Kwa nini Mungu aliruhusu mlaghai kama Labani kutawala kwa hila chombo chake kiteule, Yakobo?
2. Je, Yakobo alitaka kuwa na wake wengi?
3. Andika kila jina la hawa wana na utuambie sifa ya asili na historia ya maneno.

# MWANZO 31

| MIGAWANYO YA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakobo Anaondoka Kwa Siri | Yakobo Anakimbia toka kwa Labani | Mafanikio ya Yakobo huko Harani (29:1-31:55) | Yakobo Anakimbia toka kwa Labani | Usafiri wa Yakobo |
| 31:1-16 | 31:1-16 | 31:1-9 | 31: 1-3 | 31:1-13 |
| | | | 31:4-9 | |
| | | 31:10-16 | 31:10-13 | |
| | | | 31:14-16 | 31:14-16 |
| 31:17-21 | 31:17-21 | 31:17-18 | 31:17-21 | 31:17-21 |
| Labani Anamfuatilia Yakobo | Labani Anamfuatilia Yakobo | 31:19:-21 | Labani Anamfualia Yakobo | Labani Anamfuatilia Yakobo |
| 31:22-24 | 31: 22-24 | 31:22-24 | 31:22-25 | 31: 22-25 |
| 31:25-32 | 31:25-32 | 31:25-32 | | |
| | | | 31:26-30 | 31:26-30 |
| | | | 31:31-32 | 31: 31-35 |
| 31:32-35 | 31:32-35 | 31:33-35 | 31:33-35 | |
| 31:36-42 | 31:36-42 | 31:36-42 | 31:36-42 | 31:36-42 |
| Agano la huko Mispa | Agano la Labani pamoja na Yakobo | | Makubaliano kati ya Yakobo na Labani | Maapatano kati ya Yakobo Labani (31:43-32:3) |
| 31:43-55 | 31:43-50 | 31:43-50 | 31:43-44 | 31:43:44 |
| | | | 31:45-55 | 31:45-55 |
| | 31:51-55 | 31:51-54 | | |
| | | 31:55 | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA ) 31:1-16**
[1]**Basi Yakobo akasikia maneno ya wana wa Labani, wakisema, Yakobo amechukua mali yote ya baba yetu; na kwa mali ya baba yetu amepata fahari hii yote.** [2] **Yakobo akaona uso wa Labani, ya kuwa hakumtazama vema kama jana na juzi.** [3] **Bwana akamwambia Yakobo, Urudi mpaka nchi ya baba zako na kwa jamaa zako, nami nitakuwa pamoja nawe.** [4] **Yakobo akatuma watu, akawaita Raheli na Lea waje nyikani kwenye wanyama wake. Akawaambia,** [5] **Naona uso wa baba yenu, kwamba hanitazami vema kama jana na juzi. Lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami.** [6] **Nanyi mmejua ya kwamba kwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu.** [7] **Na baba yenu amenidanganya, akabadili mshahara wangu mara kumi; lakini Mungu hakumwacha kunidhuru.** [8] **Aliposema, Walio na madoadoa watakuwa mshahara wako, wanyama wote wakazaa madoadoa. Aliposema, Walio na milia watakuwa mshahara wako, ndipo wanyama wote wakazaa wenye milia.** [9] **Hivi Mungu akamnyang'anya mali yake baba yenu, na kunipa mimi.** [10] **Ikawa, wakati wale wanyama walipochukua mimba, naliinua macho yangu nikaona katika ndoto, na tazama, mabeberu waliowapanda hao wanyama walikuwa na milia, na madoadoa, na marakaraka.** [11] **Na malaika wa Mungu akaniambia katika ndoto, Yakobo! Nikasema, Mimi hapa.** [12] **Akasema, Inua, basi, macho yako, ukaone; mabeberu wote wanaopanda wanyama wana milia, na madoadoa, na marakaraka; maana nimeona yote aliyokutendea Labani.** [13] **Mimi ni Mungu wa Betheli, huko ulikotia mafuta nguzo, na kuniwekea nadhiri. Sasa ondoka, toka katika nchi hii, urudi mpaka nchi ile uliyozaliwa.** [14] **Raheli na Lea wakajibu, wakamwambia, Je! Imetubakia sehemu au urithi katika nyumba ya baba yetu?** [15] **Hakutufanya kama wageni, maana ametuuza, naye amekula fedha zetu kabisa?** [16] **Maana mali yote ambayo Mungu amemnyang'anya baba yetu, mali hiyo ndiyo yetu na ya wana wetu. Basi yo yote Mungu aliyokuambia, uyafanye.**

**31:1 "Basi Yakobo akasikia maneno ya wana wa Labani, wakisema"** Kwa hakika wana hawa walikuwa na umri gani haijulikani, lakini walikuwa na umri wa kutosha kufikia hatua ya kuchunga kundi la mifugo wao wenyewe (kama vile 30:35). Lazima miaka mingi itakuwa imepita tangu kutukia kwa matukio ya sura ya 30. Ni dhahiri kuwa walikuwa wakirudia mazungumzo waliyo yasikia nyumbani kwao. Pia waliyarudia mazungumzo haya hadharani, kitu ambacho kinaonyesha kwamba hawakuwa na woga iwapo Yakobo angewagundua. Japo malalamiko yao yalikuwa dhahiri, lakini hawakuwa na uhakikia (kama vile 30:30). Kabla ya Yakobo kuja, Labani hakuwa mwenye mali. YHWH alikuwa pamoja na Yakobo; Labani alibarikiwa kwa sababu ya ukaribu wake na Yakobo.

◙ **"mali"** Kiuhalisia neno hili ni "utukufu" (BDB 459, kama vile KJV). Neno la Kiebrania "utukufu" linamaanisha "uzito" au "ukubwa." Hili linaweza kutumika kwa neno "heshima," lakini hapa neno linaonekana kumaanisha "utele wa mambo yanayoonekana" (NKJV).

**31:2 "Yakobo akaona mtazamo wa Labani"** Labani alikuwa mtu mwenye hila. Japo alikuwa akimnyanyasa Yakobo, lakini alikuwa akimwonyesha furaha, lakini sasa uso wake ulikuwa umebadilika.

**31:3 "Bwana akamwambia Yakobo"** YHWH aliichukuwa nafasi yake kuhusu utambuzi wa Yakobo wa hali iliyo kinyume aliyoiona, ndipo alipomfunulia Yakobo kuwa ni wakati wake wa kwenda nyumbani ("rudi," BDB 996, KB 1427, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI). Alimkumbusha juu ya mambo aliyoyafanya Betheli kwa kifungu "Nitakuwa pamoja nawe," kwa miaka 20 hapo mwanzo (kama vile Mwa. 28:10-22, hasa mst. 15).

**31:4 "Yakobo akatuma watu, akawaita Raheli na Lea waje nyikani kwenye wanyama wake"** Raheli anatajwa kwanza kwa sababu ndiye mke aliyependwa sana. Hawa wanaitwa kwa siri, mkutano wa siri. Ni dhahiri kuwa hapo awali Yakobo hakuwahi kulijadili jambo hili pamoja na wake zake.

**31:5 “Mungu wa baba yangu”** Hii ni moja ya vifungu vilivyo katika sura ya 31 ambavyo vinaonyesha mwendelezo wa kihistoria wa agano la Mungu pamoja na vizazi vya nyumba ya Ibrahimu.

**31:6 “Nanyi mmejua ya kwamba kwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu”** Wake hawa walikuwa wamemtambua Yakobo kwa muda mrefu na ugumu wa shughuli alizokuwa akipewa na baba yao. Alimtumikia baba yao kwa kipindi cha miaka 14 kwa ajili yao na miaka 6 zaidi kwa ajili ya mifugo yake na watu wake mwenyewe.

**31: 7 “Na baba yenu amenidanganya, akabadili mshahara wangu mara kumi”** Hili neno “amenidanganya” (BDB 1068, KB 1739, *Hiphil* YA KAULI TIMILIFU) linatokana na mzizi wa Kiebrania unaomaanisha “kukatisha tamaa,” “kulaghai,” au “kuchezea.”
Hili neno “akabadilika” (BDB 322, KB 321) pia limedokezwa katika mst. 41. Ingawa hatuambiwi kikamilifu namna Labani alivyobadilisha ujira wake, kutokana na muktadha huu ni wazi kwamba ilimpasa Yakobo kuchukua wanyama wote walio na madoadoa, lakini wanyama wenye madoadoa walipozaa ndama wengi, Labani alianza kuyachukua makundi kadhaa kwa ajili ya faida yake. Alifanya mabadiliko kila wakati, Mungu aliyabariki makundi ya wanyama wa Yakobo yaliyobakia, aidha yalikuwa na madoa ama milia (kama vile mst. 8).

◙ **“mara kumi”** Usemi huu unaonekana kuwa idadi ya ujumla iliyotumika kama kukuza kitu, si mara kumi (iweni makini na fasihi ya magharibi).

◙ **“Mungu hakumwacha kunidhuru”** Yakobo, aliitambua nafasi yake mbele za Mungu, ambayo haikujikita katika unabii wa 25:23 tu, bali katika ono la kipekee lililo katika 28:10-22, huyu alikuwa na uelewa wa kithiolojia juu ya kile alichokuwa akikifanya. Labani pia alilifahamu hili (kama vile mst. 29).

**31:8** Mstari huu unaeleza kwa undani namna Labani alivyojaribu kubadilisha makubaliano yao. Hata hivyo, alibadilisha makubaliano haya kila wakati, Mungu aliubadilisha mzunguko wa joto la mbuzi na kondoo ili kumnufaisha Yakobo (kama vile mst. 9).

**31:9 “Mungu akamnyang'anya”** Hiki ni KITENZI (BDB 664, KB 717, *Hiphil* cha WAKATI USIO TIMILIFU), ambapo katika shina la *Hiphil* kinamaanisha “kutwaa,” kama vile mist. 9 na 16. Kitenzi hiki Kinamaanisha kuokoa kutokana na mashambulizi ya wanyama (kama vile I Sam. 17:34-35; Eze. 34:10; Amosi 3:12). Kadiri Labani alivyojichukulia haki ya mshahara wa Yakobo, na sasa Mungu alijitwalia kundi lake la wanyama na kumpa Yakobo. Mambo yanayoonyesha mabadiliko yanaelezwa katika mst. 12.

**31:10 “Ikawa, wakati wale wanyama walipochukua mimba”** Kifungu hiki kinaeleza maono endelevu kwamba Yakobo alikuwa akitumikia wanyama ambao baadaye wangekuwa wake. Hii haikuwa hila ya Yakobo ya kuifanikisha mbinu fulani (yaani, 30:37-43), bali neema ya Mungu, iliyosababisha sehemu ya kundi la wanyama wa Yakobo kuongezeka (kama vile mst. 9, na hasa mst. 12).

**31:11 “Malaika wa Mungu”** Tena, malaika wa Bwana ni utambulisho wa Uungu (yaani, Mwa. 16:7-13; 18:1; 19:1; 21:17, 19; 22:11-15; 31:11, 13; 32:24, 30; 48:15, 16; Kut. 3:2, 4; 13:21; 14:19; Amu. 6:12, 14; Zek. 3:1-2). Huyu anazungumza kwa niaba ya YHWH. Angalia Mada Maalum katika 12:7.

**31:13 “Mimi ni Mungu wa Betheli”** Kifungu hiki kinarejelea juu ya ono la Mungu kwa Yakobo ambalo limenakiliwa katika Mwa. 28:10-22. Mungu wa baba wa Yakobo na baabu yake (kama vile mst. 5) alizua maagizo mapya.

1. “inua,” BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “ondoka” (kifasihi. “nenda”), BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. “urudi,” BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**31:14** Wake za Yakobo walienenda pamoja naye kwa ukamilifu!

**31:15"Je! Imetubakia sehemu au urithi katika nyumba ya baba yetu? Hakutufanya kama wageni, maana ametuuza, naye amekula fedha zetu kabisa"** Hapa mabinti wawili wa Labani wanamlalamikia baba yao kwa sababu ya kutowatendea vema kwa upande wa taratibu za tamaduni za siku hizo (utamaduni wa Huri). Katika taratibu za Huri "Mohari" au "mahari ya mke" ilikuwa ikitunzwa, angalau kiasi fulani, kwa ajili ya binti. Hata hivyo, Labani alijitwalia mshahara wa Yakobo na aliutumia moja kwa moja. Mstari 15 unatuonyesha kuwa mabinti hawa waliutambua ulafi huu na kakataa kumpa mahari ndugu wa kiume wa Labani.
Kifungu hiki "amekula fedha zetu kabisa" ni KITENZIJINA HALISI na KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB37, KB 46), ambao unadokeza juu ya uweza.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31 : 17-21**
*17* **Ndipo Yakobo akaondoka, akapandisha wanawe na wakeze juu ya ngamia.** 18 **Akachukua wanyama wake wote, na mali yake yote aliyokuwa ameyapata, na wanyama aliowapata katika Padan-aramu, ili afike kwa Isaka babaye katika nchi ya Kanaani.** 19 **Basi Labani alikuwa amekwenda kuwakata manyoya kondoo zake, na Raheli akaviiba vinyago vya babaye.** 20 **Yakobo akamhadaa Labani, Mshami, kwa kuwa hakumwambia ya kwamba anakimbia.** 21 **Basi akakimbia yeye na yote aliyokuwa nayo; akaondoka akauvuka mto, akaelekeza uso wake kwenda mlima wa Gileadi.**

**31:17"Ndipo Yakobo akaondoka, akapandisha wanawe na wakeze juu ya ngamia"** Aina hii ya usafiri ilikuwa ya haraka sana na watu wa nyumba yake hawakuwa wenyeji sana kiasi cha kutumia usafiri wa ngamia.

**31:18"Akachukua wanyama wake wote"** Hili neno "akachukua" (BDB 624, KB 675) linadokeza juu ya uharaka ambao ulitumika kuwachukua wanyama hao. Kwa uwazi kabisa, walisafiri mchana na usiku ili kuepuka joto.

**31:19"Basi Labani alikuwa amekwenda kuwakata manyoya kondoo zake"** Msimu wa kukata manyoaya ni kipindi cha sherehe kubwa na cha kuunganisha familia upya (kama vile Mwa. 38:12; I Sam. 25:4 na I Sam. 13:23). Kutokuwepo kwa Yakobo kulikuwa kwa muhimu, ni jambo ambalo linaonyesha kutengana kwa uhusiano wao.

◙**"na Raheli akaviiba vinyago vya babaye"** Neno la Kiebrania "vinyago"ni *teraphim* (BDB 1076). Vinyago hivi bila shaka vilikuwa vikubwa sana (kama vile I Sam. 19:13), ama vidogo sana kiasi cha kubebeka kama mzigo juu ya ngamia wa Raheli (kama vile mst. 34). Kutokana na ubamba wa maandiko ya Nuzi tunaelewa kwamba vinyago hivi vilikuwa ishara za haki za urithi hivyo Raheli aliviiba kama ishara ya kuwa na uelewa juu ya matendo ya Labani yasiyo ya haki ukizingatia urithi wake ama kudai haki ya mwanae ya kurithi mali za Yakobo. Wengine wanasema kwamba huyu aliviiba ili Labani asitambue eneo walilokuwepo (yaani, Rashi, kama vile 30:27). Hivi vinyago vilitumika kwa ajili ya ubashiri (kama vile Zek. 10:2). Mara nyingi hivi vilitumika katika uhusiano na "vazi lililovaliwa na kuhani" (kama vile Amu. 17:5; 18:14-20 na Hos. 3:4). Hivi vinadaiwa kuwa kama ibada ya sanamu katika I Sam.15:23.

## MADA MAALUM: *TERAPHIM (*VINYAGO (BDB 1076, KB 1794))

Neno la Kiebrania (asili ya neno hili haijulikani) lenye kumaanisha "vinyago vya nyumbani" ni *teraphim* (BDB 1076, KB 1794). Yawezekana hivi vinyago vya nyumbani vilikuwa vikubwa sana (kama vile 1 Sam. 19:13,16), au vidogo sana, kwa ajili ya kwenda sawa na matandiko ya ngamia wa Raheli (kama vile Mwa. 31:34). Kutokana na ubamba wa maandiko ya Nuzi tunaelewa kwamba hivi vinyago vya nyumbani ilikuwa ishara ya haki za urithi, hivyo yawezekana Raheli aliviiba kama ishara ya kutambua matendo ya Labani yasiyo sahihi ukilinganisha na urithi wake au kwa ajili ya kudai urithi wa baadaye wa mmanae unaotokana na mali za Yakobo. Wengine wanasema kwamba Raheli aliviiba vinyago hivi ili Labani asitambue maeneo walipo (yaani, Rashi, kama vile Mwa. 30:27). Hivi vinyago vilitumika kwa ajili ya ubashiri (kama vile Zek. 10:2). Mara nyingi vilionekana katika uhusiano na "vazi la kuhani" (kama vile Amu. 17:5; 18:14-20; na Hos. 3:4). Hivi pia vilidaiwa kuwa kama ibada ya sanamu katika 1 Sam. 15:23.
Kutokana muungano wa sehemu mbalimbali za Agano la Kale ufafanuzi unaohusu vinyago hivi ni mgumu:

1. vinyago vya nyumbani vidogo na vyepesi, Mwa. 31:19,34,35
2. kinyago kikubwa chenye umbo kama binadamu, 1 Sam. 19:13,16
3. vinyago vilivyotumika majumbani, lakini pia katika nyumba za miungu, Amu. 17:5; 18:14,17,18; Hosea 3:4
4. pia vinyago vilitumika kutambua mambo yatakayotokea baadaye ama kama miungu/mungu
   a. vililaaniwa na kuhusianishwa na tendo la ubashiri, 1 Sam. 15:23
   b. vililaaniwa na kuhusianishwa na vyombo vya mawasiliano, roho za utambuzi, sanamu, 2 Fal. 23:24
   c. vililaaniwa na kuhusianishwa na ubashiri, kuitikisa mishale, na kuulizia terafi na maini ya kondoo, Eze. 21:21
   d. vililaaniwa na kuhusianishwa na wabashiri na manabii wa uongo, Zek. 10:2

◙
**31:20**
**NASB, TEV,**
**NRSV, NIV,**
**PESHITTA “Yakobo akamlaghai”**
**NKJV “aliiba”**
**RSV, NJB “alinyakua”**
**REB “alijitwalia”**
**JPSOA “alitunza kwa siri”**
**LXX “alificha jambo”**

Kwakuwa Raheli “aliviiba” vinyago vya nyumbani, Yakobo naye “aliuiba moyo” (BDB 170, KB 198, *Qal* KAULI SHURUTISHI) wa Labani, ambao ni wazi kuwa ni nahau ya udanganyifu

◙ **“Labani, Mshami”** Hilli neno “Mshami” linaweza kutafsriwa kama “Mwaramu” (BDB 74). Uhusiano halisi kati ya Labani kuitwa Mwaramu na Yakobo kuitwa vile vile katika Kumb. 26:5 haiujulikani. Kutokana na mfululizo wa vizazi vya Mwanzo 10 hawa wanaonekana kuwa mtiririko wa vizazai viwili tofauti, lakini mwingiliano wa kuoana uliwasababishia kutambuliwa kwa pamoja ama kutokana na maeneo ya kijiografia (yaani, Harani) ambapo Ibrahimu aliishi hapo awali.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:22-24**
**[22] Hata siku ya tatu Labani akaambiwa ya kwamba Yakobo amekimbia, [23] akatwaa ndugu zake pamoja naye, akamfuata mwendo wa siku saba. Akampata katika mlima wa Gileadi. [24] Mungu akamjia Labani, Mshami, katika ndoto ya usiku, akamwambia, Ujihadhari, usimwambie Yakobo neno la heri wala la shari.**

**31:22 “Hata siku ya tatu Labani akaambiwa ya kwamba Yakobo amekimbia”** Kutokana na Mwa. 30:36 tunajifunza kwamba kundi la wanyama wa Labani na Yakobo liliwekwa kando siku tatu kabla kwa ajili ya safari, hivyo nidhahiri kuwa mtumishi wa Labani alkimwona Yakobo akiondoka na kwenda kumwambia Labani upesi (BDB 616, KB 665, *Hophal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU).

**31:23 “katika mlima wa Gileadi”** Kumekuwa na baadhi ya mijadala kuhusu uwezekano wa mwendo mrefu aliotembea kwa muda mfupi. Hata hivyo, tunazungumza kuhusu kipindi cha siku kumi za mwendo wa nguvu. Haijulikani ni mwendo wa umbali gani, bila shaka ni kati ya maili 250 na 350 kwa sababu (1) hatufahamu eneo la shami ambalo wanyama wa Yakobo walikuwekwa na (2) hatuna uhakika wa mpaka wa mashariki ya Gileadi.
Labani alikuja kwa shauku kubwa ya kumdhuru watu hawa (kama vile mst. 29). Kutafuta kwake kunaelezwa kama “safari ya shari” (BDB 196, KB223, *Qal* KAULI YAWAKATI TIMILIFU) katika mst. 36.

**31:24 "Ujihadhari, usimwambie Yakobo neno la heri wala la shari"** Hii ni lahaja ya Kiebrania ("tujia hadhari, usimwambie Yakobo neno la heri wala la shari") ambayo kwa uwazi kabisa inamaanisha "mwache kabisa." Tena, Neema na ulinzi wa Mungu vinaonekana vema katika kumkomboa mkuu wa nyumba kwa mara nyingine.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:25-32**
[25] **Labani akamfikia Yakobo, na Yakobo alikuwa amepiga hema zake katika mlima, na Labani na ndugu zake wakapiga hema zao katika mlima wa Gileadi.** [26] **Labani akamwambia Yakobo, Umefanya nini? Umenihadaa, ukawachukua binti zangu kama mateka waliotwaliwa kwa upanga.** [27] **Mbona umekimbia kwa siri ukanihadaa, wala hukuniambia, nipate kuagana nawe uende zako kwa furaha, na nyimbo, na ngoma, na kinubi?** [28] **Wala hukuniacha niwabusu wanangu, na binti zangu; basi umetenda upumbavu.** [29] **Ninao uwezo mkononi mwangu wa kukufanyia madhara; lakini Mungu wa baba yako usiku huu ameniambia, akisema, Ujihadhari, usimwambie Yakobo neno la heri wala la shari.** [30] **Basi sasa, umetoka kwa sababu umetamani sana nyumba ya baba yako. Mbona basi umeiiba miungu yangu?** [31] **Yakobo akajibu, akamwambia Labani, Kwa sababu naliogopa, nikasema, Usije ukaninyang'anya binti zako kwa nguvu.** [32] **Awaye yote utakayemwona kuwa nayo miungu yako, yeye asiishi. Mbele ya ndugu zetu ukitambue kilicho chako kwangu, ukakichukue. Maana Yakobo hakujua ya kwamba Raheli ameiiba.**

**31:25 "Yakobo alikuwa amepiga hema"** Huu ni ufafanuzi wa kwanza wenye kueleza kuwa Yakobo alikuwa amepiga hema, hivyo ni dhahiri kuwa mwendo huu wa ghafla usingeweza kumpa mwanya wa kupumzika sehemu za karibu. Kwa uwazi kabisa, Yakobo na nyumba yake walihofia usalama wa maisha yao.

**31:26-30** Nakitafasiri kifungu hiki kama Labani, mlaghai, mtu mwenye kuunda mashtaka yasiyo sahihi kumhusu Yakobo. Mambo mengi ambayo Labani alikuwa akiyalalamikia hayakuwa ya msingi. Labani anaonekana kuweka mambo yake hadharani kwa manufaa ya jamaa zake (na Yakobo) ambao walikuwa wakimsikiliza na hatimaye wangemtenda Yakobo kama mwamuzi.

**31:27** Labani anaesema kuwa angemfanyia Yakobo sherehe. Yakobo anaikumbuka sherehe yaliyofanyiwa kipindi kilichopita (yaani, usiku wa harusi ya Lea)! Hakutaka zaidi "sherehe" za baba mkwe wake.

**31:28 "basi umetenda upumbavu"** Hili neno (BDB 698, KB 754, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) mara nyingi linatumika kwenye Biblia katika uhusiano na dhambi na hatia (kama vile I Sam. 13:13 katika uhusiano na Sauli, na II Sam. 24:10 katika uhusiano na Daudi). Kwa uwazi kabisa Labani alikuwa akilalamika juu ya usafiri wa Yakobo kuwa ni wa asili ya dhambi.

**31:29 "Ninao uwezo mkononi mwangu wa kukufanyia madhara; lakini Mungu wa baba yako usiku huu"** Hiki kifungu "mkonono mwangu" (BDB 42) kinahusiana katika namna ya asili ya neno na neno *El* (BDB 42) au *Elohim* (BDB 43). Huu ndiyo mstari pekee unaotupa dondoo kwamba asili ya msingi ya neno *El* inaweza kumaanisha "kuwa na nguvu." Mungu anamtahadharisha Labani katika ndoto kama alivyomtahadharisha Farao mwanzoni (kupitia pigo, kama vile 12:17, na baadhi ya ufunuo uliofuatia, lakini kwa hakika mengine hayakuchukuliwa kumbukumbu) na Abimaeleki (kama vile 20:3). YHWH anatazama na kulilinda agano la nyumba hii dhidi ya madhara /mashambulizi.

**31:30 "umetoka kwa sababu umetamani sana nyumba ya baba yako"** Hapa kuna miundo miwili iliyotiwa chumvi katika mstari huu uliuzungumzwa na Labani.

1. "umetoka," KITENZIJINA HALISI na KITENZI TIMILIFU kinachotokana na mzizi ule ule (BDB 229, KB246, "uende")
2. "umetamani sana," KITENZIJINA HALISI na KITENZI TIMILIFU kinachotokana na mzizi ule ule (BDB 493, KB 490)

Neno "umetamani sana" (BDB 493) linatokana na mzizi wa Kiebrania "kuangazwa," ambalo mara nyingi lilitumika kueleza juu ya chuma cha fedha (BDB 494). Hili lilikuwa neno lenye nguvu lenye kumaanisha "shauku." Labani

alilalamika juu ya kuondoka kwa Yakobo kwa sababu alikuwa hajiwezi kwa sababu ya maradhi, si kwa sababu ya msingi ambayo ni unyanyasaji wa Labani, ulaghai, uongo na mtazamo mbaya.

◙ **“Mbona basi umeiiba miungu yangu”** Rejea juu ya 31:19. Kwa uwazi kabisa hii miungu ya nyumbani ilikuwa ya kishirikina na yenye kuhusianishwa na urithi pamoja na mali na Labani alikuona kuodoka kwa Yakobo kama kuondoka na mali pamoja na kuwepo kwa upotevu wa urithi na mwelekeo wa kiroho kutokana na kuondoshwa kwa vinyago hivi (yaani, *teraphim*).

**31:31-32** Yakobo anayajibu maswali ya Labani kuanzia mst. 27, lakini si swali hili, kuanznia mst. 30b. Yakobo hakujua kama Raheli ameiba vinyago (mst. 19).

**31:32 Kwa udhihirisho kabisa Yakobo hakujua kama Raheli ameiba miungu hawa**. Mstari 32 unaakisi alama ya siri ya sheria ya Mesopotamia ya kale katika uhusiano na mtu aliyeiba, kwa vyo vyote kutoka katika hekalu, ama miungu ya mtu fulani. Walimu wa Kiyahudi wanasema (kama vile *Mwa. Rab.* 74.4) kwamba kifo cha Raheli kilichoandikwa katika Mwa. 35:16-18, wakati alipokuwa akimzaa Benjamini, kinahusiana na maneno ya Yakobo yaliyoandikwa katika mstari huu. Kwa uwazi kabisa hili neno la kisheria (yaani, “katika uwepo wa ndugu”).Hapa kuna USHURUTISHI wa aina mbili

1. kutambua (kifasihi “chunguza,” kama vile 37:32; 38:25), BDB 647 I, KB 699, *Hiphil* SHURUTISHI
2. kuchukua (maana nyingine, “ukakichukue”), BDB 542, KB 534, *Qal* SHURUTISHI

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:33-35**
**[33] Labani akaingia katika hema ya Yakobo, na hema ya Lea, na hema ya vijakazi wawili, wala hakuiona. Akatoka katika hema ya Lea, akaingia katika hema ya Raheli. [34] Basi Raheli alikuwa amevitwaa vile vinyago ameviweka katika matandiko ya ngamia, na kuvikalia. Labani akapapasa hema yote wala hakuviona. [35] Naye Raheli akamwambia babaye, Bwana wangu asikasirike kwa sababu siwezi kuinuka mbele yako, maana nimeshikwa na mambo ya kike. Akatafuta, wala hakuviona vile vinyago.**

**31:33 “Labani akaingia katika hema ya Yakobo, na hema ya Lea”**Kifungu hiki kinaonyesha maelezo ya kihistoria kuwa wanawake walikuwa wakiishi katika mahema yaliyojitenga.

**31:34 “katika matandiko ya ngamia”** Hili neno (BDB 468), linalopatikana hapa pekee, lingeweza kurejelea juu ya mkoba uliokuwa katika matandiko ama begi lililokuwa limetundikwa juu ya matandiko (TEV, REB).

◙ **“Labani akapapasa hema yote”** Hili neno “akapapasa” linamaanisha “kusaka kwa makini kwa kutumia mikono” (BDB 606, KB 653, *Piel* ya KAULI ISIO TIMILIFU). Mara nyingi njia hii inatumiwa na watu walio vipofu katika utambuzi wa mambo yaliyo giozani (kama vile Kumb. 28:29; Ayubu 5:14; 12:25).

**31:35 “maana nimeshikwa na mambo ya kike”** Kifungu hiki kinarejelea juu ya siku za hedhi (BDB 202 LINAUNDA NENO BDB 61). Kutoka na Law. 15:19 ni wazi kuwa kulikuwa na baadhi ya miiko ya kidesturi iliyokuwa imehusishwa na hili. Hata hivyo, haijulikani ni kwa jinsi gani tunaweza kuyahusianisha maagizo haya ya Mambo ya Walawi na utamaduni wa Labani na Yakobo, lakini kulikuwa na sababu yenye kushawishi ya kwamba kwa nini hakumtaka Raheli kuamka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:36-42**
**[36] Yakobo akakasirika, akagombana na Labani. Yakobo akajibu, akamwambia Labani, N'nini hatia yangu? Nayo ni nini dhambi yangu, hata ukanifuatia namna hii? [37] Umepapasa-papasa vyombo vyangu vyote; ni kitu gani ulichokiona cha nyumbani mwako? Kiweke hapa mbele ya ndugu zangu, na ndugu zako, wakaamue kati yetu. [38] Miaka hii ishirini nimekaa kwako; kondoo zako wala mbuzi zako wake hawakuharibu katika wanyama wako sikuwala. [39] Kilichoraruliwa na hayawani sikukuletea, mimi mwenyewe nimetwaa hasara yake, wewe umekidai katika mkono wangu, ikiwa kilichukuliwa mchana, au ikiwa kilichukuliwa usiku. [40] Hii ilikuwa hali**

**yangu; mchana jua likanipata, na baridi usiku, usingizi ukanitoka machoni mwangu. [41] Miaka hii ishirini nimekaa nyumbani mwako; nilikutumikia miaka kumi na minne kwa binti zako wawili, na miaka sita kwa wanyama wako, nawe umebadili mshahara wangu mara kumi. [42] Kama Mungu wa baba yangu, Mungu wa Ibrahimu na Hofu ya Isaka, hangalikuwa pamoja nami, hakika sasa ungalinifukuza mikono mitupu. Mateso yangu na kazi za mikono yangu Mungu ameziona, akakukemea usiku huu.**

**31:36 "Yakobo akakasirika "** KITENZI hiki (BDB 354, KB 351, *Qal* KISICHO TIMILIFU) kinamaanisha "kujeruhi" na kinadokeza hasira ya mwanadamu (kama vile 4:5,6; 30:2; 34:7; 39:19).

◙ **"akagombana na Labani"** Hiki KITENZI (BDB 936, KB 1224, *Qal* KISICHO TIMILIFU) kina maana za kisheria (kama vile mst. 37). Kwa nini Yakobo alishambuliwa na Labani mbele za ndugu, na sasa Yakobo anakabiliwa na maswali yenye kupima ufahamu.

1. "N'nini hatia yangu?" (mst. 36)
2. "nini dhambi yangu?" (mst. 36)
3. "ni kitu gani ulichokiona cha nyumbani mwako?" (mst. 37)

Katika maana halisi ndugu walianzisha mahakama ya wahamaji. Iliwapasa kufanya maamuzi ya ugomvi huu (mst. 37).

**31:38-42** Yakobo alijitetea juu ya ufundi wake wa kuchunga mifugo na umakini wake (mbele ya watu wake wa ukoo).

1. kondoo wala mbuzi zako hawakuharibu mimba
2. hakula waume katika wanyama wa Labani, hakuwala
3. alitwaa hasara kwa kile kilichoraruliwa na hayawani

Haya yote yanaendana na utamaduni wa siku zile ambao unaonyeshwa katika alama za siri za sheria ya Mesopotamia ya kale (ibara ya 266).

**31:42 "Kama Mungu wa baba yangu, Mungu wa Ibrahimu na Hofu ya Isaka"** Kifungu hiki "na Hofu ya Isaka**"**ni cha kipekee katika sura hii na kimetumika mara mbili (kama vile mst. 53). Hiki kinaweza kurejelea juu ya Uungu na ukuu aliouheshimu Isaka. Mtaalamu wa Kimarekani wa mambo ya kale, Albright, anasema kwamba hili neno"hofu" linahusiana na matumizi ya neno "ndugu" katika lugha mfanano (Kiaramu, Kiarabu, na Ugaritic) na linapaswa kutafsriwa kama "ndugu wa Isaka," njia nyingine ya kueleza "Mungu wa baba zangu." Hata hivyo, hili halina uyamkini.

◙ **"ungalinifukuza mikono mitupu"** Yakobo aliuelewa vema ulafi wa Labani na pia uwepo wa neema ya Mungu. Jambo hili linaonekana katika kifungu cha mwisho cha mst. wa 42, ambapo Yakobo anadokeza juu ya ndoto ya Labani ambayo imenukuliwa katika mist. 24 na 29. Mungu amekwisha kuhukumu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:43-55**
**[43] Labani akajibu, akamwambia Yakobo, Hao binti ni binti zangu, na wana ni wanangu, na wanyama ni wanyama wangu, na yote uyaonayo ni yangu; nami naweza kuwatendea nini leo binti zangu na wana wao waliowalea? [44] Haya! Na tufanye agano, mimi na wewe, liwe kwa ushahidi kati ya mimi na wewe. [45] Yakobo akatwaa jiwe akalisimamisha kama nguzo. [46] Yakobo akawaambia ndugu zake, Kusanyeni mawe. Wakatwaa mawe, wakafanya chungu, nao wakala huko karibu na ile chungu. [47] Labani aliiita Yegarsahadutha, lakini Yakobo aliiita Galedi. [48] Labani akasema, Chungu hii ni shahidi kati ya mimi na wewe hivi leo. Kwa hiyo likaitwa jina lake Galedi, [49] na Mispa, maana alisema, Mungu avizie kati ya mimi na wewe, wakati tusipoonana. [50] Ukiwatesa binti zangu, na ukitwaa wake zaidi ya binti zangu, wala hapana mtu pamoja nasi, tazama, Mungu ni shahidi kati ya mimi na wewe. [51] Labani akamwambia Yakobo, Tazama chungu hii utazame na nguzo niliyoitia kati ya mimi na wewe. [52] Chungu hii na iwe shahidi, na nguzo hii na iwe shahidi, ya kuwa mimi sitapita chungu hii kuja kwako, wala wewe hutapita chungu hii na nguzo hii uje kwangu, kwa madhara. [53] Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Nahori, Mungu wa baba yao, ahukumu kati yetu. [54] Yakobo akachinja**

**sadaka katika mlima, akawaita ndugu zake waje wale chakula, nao wakala chakula, wakakaa usiku kucha mlimani. [55] Labani akaondoka asubuhi na mapema, akawabusu wanawe na binti zake, akawabariki; kisha Labani akaenda zake, akarudi kwao.**

**31:43** Labani anajaribu kuyajibu malalamiko ya Yakobo.

**31:44"Haya! Na tufanye agano, mimi na wewe, liwe kwa ushahidi kati ya mimi na wewe "**Ingawa Labani alijitolea kwa ajili ya kufanya agano , Yakobo ndiye aliyeweka nguzo (mst. 45 [angalia 28:18], japo Labani anadai kulifanya hili katika mst. 51) na kuwaambia ndugu wakusanye mawe (mst. 46). Walikula chakula cha agano. Katika Agano la Kale mara nyingi vyakula vilihusiana na kufanya agano.
Mionekano ya kisarufi ya kifungu hiki ni

1. "njoo," BDB 229, KB 246, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. "na tufanye agano," BDB 503, KB 500, *Qal* HALI YA KUSIHI, (kifasihi. "kuondoa," angalia Mada Maalum katika 13:15)
3. "liwe kwa ushahidi," BDB 224, KB 243,*Qal* KAULI TIMILIFU, yenye kumaanisha kusitisha machafuko daima (kama vile mst. 52)

**31:47** Hapa kuna majina mawili. Jina la kwanza ni la Kiaramu (BDB 1094 LINAUNDA NENO BDB 1113) na la pili ni la Kiebrania (BDB 165). Kuna ufanano, unaorejelea juu ya rundo la mawe. Yakobo alipaita mahali pale "Galedi" (BDB 165, "nguzo ya ushahidi"), jina ambalo linahusiana na mahali walipokuwa wameweka makazi ya muda (yaani, "Gileadi," BDB 166, "chungu cha mawe" au "milima wa mawe").
Kumekuwa na mijadala ya aina mbalimbali kuhusiana na Kiaramu dhidi ya Kiebrania kama lugha/lahaja ya ukoo. Inaonekana kwamba Kiaramu kilizungumzwa huko Mesopotamia, nyumbani kwao Ibrahimu, lakini alipoenda Kanaani alichagua lahaja ya Kiaramu ambayo ilikuwa ikijulikana kama Kiebrania. Hili linatufanya kuwa na upeo wa isimu ya lugha hizi zilizokuwepo kwa wakati huo.

**31:49 "Mispa"** Hili neno "Mispa" (BDB 859) katika mst. 49 pia ni neno la Kiebrania ambalo linamzungumzia "mlinzi wa mnara" na neno hili linaelezwa hapa kumrejelea Mungu anayeshuhudia (BDB 859, KB 1044, *Qal* KITENZI AMRISHI, mzizi wenye kuhusiana na Mispa) kati watu hawa wawili. Jambo hili linatia shauku kwangu kwamba hakika Labani alichukua nafasi hii kufuta yote aliyomtenda Yakobo mbele ya ndugu zake, jambo ambalo kwa ujumla halikuwa sahihi. Mfano wa hili unaweza kuwa kutokuoa wake wengine. Ni Yakobo pekee aliyeonyesha kumjali Lea na Raheli, kama inavyoonekana katika mst. 31, na si Labani.

**31:53 "Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Nahori, Mungu wa baba yao, ahukumu kati yetu"** Hiki KITENZI kilichopo hapa ni WINGI (BDB 1047, KB 1622, *Qal* KISICHO CHA WAKATI TIMILIFU chenye kutumika katika maana YA KUSIHI ya WINGI), ambacho kinamaanisha kwamba Labani azungumza usemi wenye kumchanganya Mungu na miungu. Agano la Kale la Kiebrania hapa halifuati Toleo la MT (hili lina KITENZI CHA WINGI). Kitabu cha Mwanzo kinaonekana kumaanisha kwamba Ibrahimu akawa mchaji sana wa YHWH lakini si Nahori. Hili linaonekana kuwa dokezo la makubaliano yaliyofanywa katika majina ya nyumba za miungu mbalimbali. Lakini, tambua kwamba Yakobo aliapa kwa jina la Mungu pekee wa baba zake. YHWH ("Hofu ya Isaka").

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana

1. Katika sura hii nani anaonekana kuwa mtesaji/mjanja mjanja?
2. Orodhesha njia ambazo Labani alizitumia kumtenda Yakobo pasipo haki.
3. Orodhesha njia ambazo Yakobo alikuwa akizitenda kwa uaminifu.

4. Nini maana ya *teraphim* (mst. 19)? Nini ilikuwa kusudi lake?
5. Orodhesha malalamiko ya Labani katika mst. 26-30 na onyesha ni kwa namna gani yako sahihi au siyo sahihi.
6. Kwa nini Raheli aliviiba vinyago vya Labani?

# MWANZO 32

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Hofu ya Yakobo kwa Esau | Esau anakuja kukutana na Yakobo (32:1-33:20) | Yakobo kupatana na na Esau | Yakobo anajiandaa kukutana na Esau | Yakobo anajiandaa kukutana na Esau |
| 32:1-2 | 32:1-8 | 32:1-2 | 32:1-2 | |
| 32:3-5 | | 32:3-5 | 32:3-5 | |
| | | | | 32:4-7 |
| 32:6-8 | | 32:6-8 | 32:6-8 | |
| | | | | 32:8-14a |
| 32:9-12 | 32:9-12 | 32:9-12 | 32:9-12 | |
| 32:13-21 | 32:13-21 | 32:13-21 | 32:13-21 | |
| | | | | 32:14b-22 |
| | Kushindana na Mungu | | kushindana kwa Yakobo Penieli | Yakobo anashindana na Mungu |
| 32:22-23 | 32:22-23 | 32:22-23 | 32:22-24a | |
| Yakobo anashindana | | | | 32:23-25a |
| 32:24-32 | | | 32:24b-26a | |
| | | | | 32:25b-30 |
| | | | 32:26b | |
| | | | 32:27a | |
| | | | 32:28 | |
| | | | 32:29a | |
| | | | 32:29b | |
| | | | 32:30-32 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 32:1-2**
**[1]Yakobo akashika njia yake na malaika wa Mungu wakakutana naye. [2]Naye Yakobo alipowaona, alisema, Hili ni jeshi la Mungu. Akapaita mahali pale, Mahanaimu.**

**32:1**
**NASB**
**NRSV, TEV "wakakutana"**
**NJB, JPSOA "wakakabiliana"**

Hiki KITENZI (BDB 803, KB 910, cha *Qal* yaWAKATI USIO TIMILIF) kinadokeza juu ya nafasi ya kukutana (kama vile NIDOTTE, juzuu 3, uk.575, mf.Kut.23:4; Hes. 35:19,21; Yos. 2:16; I Sam. 10:5; Amosi 5:19). Mtu anashangaa ikiwa mstari huu mfupi na wenye utata unauhusiano nan a yule mshindana mweleka wa mst. ya22-32. Ni dhahiri kuwa mshindana mweleka alikuwa malaika ama kuimbe cha kiroho cha namna hiyo ambacho kilikuwa na nguvu (kutoka YHWH) kumbriki Yakobo na kulibadili jina lake. Tatizo linajikita katika

1. huu mstari wa ufunguzi wenye utata
2. mshindana mweleka kukosa uwezo wa kumwondoa Yakobo katika mapambano yaliyochukua muda mrefu

◙**"malaika wa Mungu"** Aliwaona malaika wa Mungu wakiondoka Kanaani (kama vile 28:12), na sasa katika kurudi kwake, malaika hawa walitokea tena (kama vile IIFal. 6:16-17; Zab. 34:7). Hawa waliwakilisha uwepo na ulinzi wa YHWH. Jambo hili lingemkumbusha juu ya maagizo aliyopewa na ahadi za Mungu za sura ya 28. Sura hii ni mchanganyiko wa hofu na tumaini. Yakobo alipambana na huu uchaguzi wa aina mbili!

◙**"wakakutana"**Hiki KITENZI (BDB 803, KB 910, cha *Qal*yaKAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha "kukutana" au "kukabiliana." Toleo la AnchorBible Commentary (uk. 254) linawahusianisha hawa malaika wawili na mst.ya24-32. Jambo hili halimruhusu mtu kuiona sura hii kamamwanzo na mwisho wa ki-Ungu.

**32:2 "kambi la Mungu"** Hili neno "kambi" (BDB 334) linamaanisha mahali pa kupiga kambi ama kupumzika kwa ajili ya safari. Neno hili pia linaweza kudokeza kambi ya kijeshi (kama vile Yos. 6:11,14; I Sam. 4:3,6,7; 17:53; II Fal. 7:16) ama jeshi (kama vile Ku.14:24). Hii ni moja ya maneno kadhaa ya kijeshi ya Kiebrania linalotafsiriwa kama "halaiki."

◙**"Mahanaim"** Hili neno kiuhalisia linamaanisha"kambi mbili" au "alaiki za aina mbili" (BDB 334, liko katika mundo wa uwili). Hizi kambi mbili zinaweza kurejelea

1. Labanina Yakobo
2. Malaika na Yakobo
3. Esau na Yakobo
4. Kundi la nyumba ya Yakobo lililogawanyika

Katika upande wa muktadha wa papo kwa papo, #2 inaendana vema. Katika upande wa muktadha ulio mpana, #4 inaendana na tabia ya Yakobo ya kujaribu kutumaini katika akili yake mwenyewe.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 32:3-5**
**[3]Basi, Yakobo akapeleka wajumbe mbele yake kwenda kwa Esau nduguye mpaka nchi ya Seiri katika nyika ya Edomu. [4]Akawaagiza akisema, Mwambieni hivi bwana wangu, Esau, Hivi ndivyo asemavyo mtumwa wako, Yakobo; Nimekaa ugenini kwa Labani, na kukawia huko hata sasa, [5]nami nina ng'ombe, na punda, na kondoo, na watumwa, na vijakazi; nami nimepeleka watu nimpashe bwana wangu habari, nipate neema machoni pako.**

**32:3 "wajumbe"** Katika maneno yote ya Kiebrania (BDB 521) na Kiyunani neno "wajumbe" (lenye mzizi sawa na na jina Malaki) linamaanisha "malaika." Walimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwamba Yakobo aliwatuma malaika kabla ya kukutana na Esau. Mzizi ule ule wa Kiebrania unatafsiriwa kama "malaika" katika mst. wa 1 na "wajumbe" katika mist. ya 3 na 6.

**32:4 "bwana wangu, Esau"**Hapa neno "bwana" linatumika wadhifa wa kumaanisha heshima (*Adon*) katika ujumbe wa Yakobo kwa Esau.

◙**"mtumwa wako" Hawa wajumbe walitakiwa kumtambulisha** Esau kama "Bwana" (BDB 10) na kumuita Yakobo "mtumwa " au"mtumishi" (BDB 713). Yakobo anaendelea kuwa na hofu (kama vile mist.ya 7,11) kwamba Esau bado ana kinyongo (kwa sababu ya kujitwalia Baraka za nyumba hiyo katika Mwanzo 27).

**32:5** Kwa ubayana kabisa ujumbe huu una makusudi mawili.
1. Yakobo amekuwa na mali
2. Anataka kumpa Esau sehemu ya mali yake kama zawadi (kama vile mist. ya 13-21)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 32:6-8**
**[6]Wale wajumbe wakarudi kwa Yakobo wakisema, Tulifika kwa ndugu yako, Esau, naye anakuja kukulaki, na watu mia nne pamoja naye. [7]Ndipo Yakobo akaogopa sana, na kufadhaika sana, akawagawanya watu waliopo pamoja naye, na kondoo, na ng'ombe, na ngamia, wawe matuo mawili. [8] Akasema, Akija Esau kwa kundi la kwanza, akalipiga, kundi litakalosalia litaokoka.**

**32:6 "watu mia nne pamoja naye"** Esau hakuujibu ujumbe wa Yakobo na alikuwa na watu 400. Jambo hili lilimtia hofu Yakobo (kama vile mst. wa 7).

**32:7** Tambua mwitikio wa akili ya Yakobo kutokana na habari hizi**.**
1. "hofu kubwa"
   a. hofu, BDB 431, KB 432, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*,*kama vile 3:10; 18:15; 43:18
   b. kubwa mno, KIELEZI, BDB 547
2. "alikuwa na mshtuko," BDB 864 I, KB 1058, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILFU, ambao kimsingi imaanisha "kuwa na mkakamao wa misuri," kama vile Ayubu 20:22; Isa. 49:19, lakini neno hili linatumika kistiari kumaanisha "roho yenye huzuni" (yaani, kuwa na uchungu), kama vile Amu.2:15; 10:9; II Sam. 13:2

**32:7-8** Yakobo anapanga mipango yenye uwezekano duni. Tena katika muktadha wa mst. wa1, jambo hili linaonekana kudokeza juu ya upungufu wa imani. Anafanya maombi katika mist.ya 9-12, lakini katika maana hii bado anaendelea kujaribu kuizatiti hatima yake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBOORESHWA) 32:9-12**
**[9] Yakobo akasema, Ee Mungu wa baba yangu Ibrahimu, na Mungu wa baba yangu Isaka, Bwana, uliyeniambia, Rudi uende mpaka nchi yako, na kwa jamaa zako, nami nitakutendea mema; [10]mimi sistahili hata kidogo hizo rehema zote na kweli yote uliyomfanyia mtumwa wako; maana nalivuka mto huo wa Yordani na fimbo yangu tu, na sasa nimekuwa matuo mawili. [11]Uniokoe sasa na mkono wa ndugu yangu, mkono wa Esau, maana mimi namwogopa, asije akanipiga, na mama pamoja na wana. [12]Nawe ulisema, Hakika nitakutendea mema, nami nitafanya uzao wako uwe kama mchanga wa bahari, usiohesabika kwa kuwa mwingi.**

**32:9** Tambua njia mbalimbali za kuurejelea Uungu.

1. "Ee Mungu (אלה, BDB 43) wa baba yangu Ibrahimu"
2. "Ee Mungu (sawasawa na hapo juu) wa baba yangu Isaka"
3. "Ee BWANA" (יהוה, BDB 217)

Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 12:1. Yote haya yanamjerejelea Mungu wa Ibrahimu (kama vile 12:1; 28:3-4) na ahadi zake kwa Yakobo katika 28:13-17.

◙**"uliyeniambia"** Kifungu hiki kinarejelea 31:13,29 na hatimaye kinarudi 28:15.

1. "Rudi," BDB 996, KB 1427, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 31:13
2. "nami nitakutendea mema," BDB 405, KB 408, *Hiphil* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO, kama vile mst. ya 10,13; 28:14

**32:10 "mimi sistahili"** Hili ni ungamo mhuhimukwa Yakobo (BDB 881, KB 1092, *Qal* ya KAULI TIMILIFU, ambalo linadokeza kutokuwa na umuhimu, kama vile II Sam. 7:19; I Nya. 17:17). Msistizo uko katika neema ya ulinzi wa agano la Mungu, na msisitizo upo katika agano la neema ya Mungu, ulinzi, uwezeshaji!

**NASB "mema"**
**NKJV "huruma"**
**NRSV, REB "wema**
**TEV "pendo la kujitolea"**
**NJB "pendo lenye uaminifu"**
**LXX "haki" au mwenye haki"**
**Peshitta "upendeleo"**

Neno linalotumika hapa ni *hesed* (BDB 338 I), ambalo linadokeza uaminifu wa agano. Angalia Mada Maalum katika 19:19.

◙
**NASB, NRSV**
**TEV "uaminifu"**
**NRSV, LXX,**
**Peshitta "ukweli"**
**NJB "uhakika"**
**REB "kweli"**

Hili neno la Kiebrania *emeth* (BDB 54), ambalo linadokeza uaminifu. Neno *Hesed* na*emeth* mara nyingi yanapatikana kwa pamoja katika Agano la Kale ili kutoa maelezo yanayomhusua Mungu. Angalia Mada Maalum katika 15:6.

**32:11 "Uniokoe "** Hili neno (BDB 664, KB 717, *Hiphil KAULI* SHURUTISHI) katika shina la neno *Hiphil* linamaanisha "kuchomoa" na kistiari "ondoa."

◙**"asije akanipiga"** Hili neno"akanipiga" (BDB 645, KB 697, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) katia shina la *Hiphil* linamaanisha kuangamiza nyumba nzima kwamakali ya upanga (kama vile 34:30). Yakobo alikuwa na hofu kuwa Esau angewaua watu wote wa nyumbani mwake.

**32:12** Yakobo anamkumbusha Mungu juu ya agano la ahadi zake za 28:14 na 22:17. Hili lilikuwa agano la mara kwa mara kwa wale waliokuwa wamebeba mamlaka ya kifamilia. Haya yalikuwa matokeo ya kuwapa mwana.

◙**"nitakutendea mema"** Kiuhalisia kifungu hiki ni"nitakutendea yaliyo mazuri." Kifungu hiki ni KITENZIJINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi huo huo (BDB 405, KB 408), ambao unadokeza uweza.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 32:13-21**
**[13]Akakaa huko usiku ule. Kisha akatwaa baadhi ya vitu alivyokuwa navyo, kuwa zawadi kwa Esau, nduguye;**
**[14]mbuzi wake mia mbili, na mbuzi waume ishirini, kondoo wake mia mbili, na kondoo waume ishirini;**
**[15] ngamia wanyonyeshao thelathini pamoja na wana wao, ng'ombe wake arobaini na mafahali kumi; punda wake ishirini na wana wao kumi. [16]Akawatia mkononi mwa watumwa wake, kila kundi peke yake. Naye akawaambia watumwa wake, Vukeni mbele yangu, mkaache nafasi kati ya kundi na kundi. [17]Akamwagiza yule wa kwanza akasema, Esau, ndugu yangu, akikukuta, na kukuuliza, akisema, Wewe u wa nani? Unakwenda wapi? Tena ni wa nani hawa walio mbele yako? [18]Basi, useme, Ni wa mtumwa wako, Yakobo, ni zawadi, aliyompelekea bwana wangu, Esau. Na tazama, yeye mwenyewe yuko nyuma yetu. [19]Akamwagiza tena wa pili, na wa tatu, wote waliofuata makundi, akisema, Hivi ndivyo mtakavyomwambia Esau, akiwakuta.**
**[20]Tena semeni, Tazama, mtumwa wako, Yakobo, yuko nyuma yetu. Maana alisema, Nitamsuluhisha kwa zawadi inayonitangulia, baadaye nitamwona uso wake; huenda atanikubali uso wangu. [21]Basi ile zawadi ikavuka mbele yake, naye mwenyewe akakaa usiku ule kambini**.

**32:20**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV, NRSV, REB PESHITA** | **"nitajionyesha kwake"** |
| **TEV** | **"nitamshindia"** |
| **NJB** | **"nitampatanisha"** |
| **JPSOA, LXX** | **"tuliza"** |

Hiki KITENZI (BDB 497, KB 493, *Piel* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO) ni KITENZI kinachotumika kwa ajili ya dhabihu ya damu ya utakaso (kama vile Mambo ya Walawi 4 na 16). Maana yake ya msingi ni "kufunika" au "kufanya upatanisho"

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV, NRSV, LXX** | **"atanikubali"** |
| **TEV** | **"atanisamehe"** |
| **NJB** | **"nitamwinamia"** |
| **JPSOA, LXX** | **"ananionyesha upendeleo"** |
| **REB** | **"atanipokea kwa upole"** |

Hiki KITENZI (BDB 669, KB 724, *Qal* cha KAULI YA WAKATI USIO TIMIILIFU) kinamaanisha "kwendana na." Hii ni nahau ya Kiebrania "kuuona" (kama vie Ayubu 42:8,9; Zab. 82:2; Mit. 18:5; Omb. 4:16). Katika muktadha wa kisheria neno kitenzi hiki kinarajelea juu ya kuhukumu kulingana na uso wa mshtakiwa, ambayo inahataharisha uhuru wake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 32:22-32**
**[22] Akaondoka usiku ule akawatwaa wakeze wawili, na vijakazi wake wawili, na wanawe kumi na mmoja, akavuka kivuko cha Yaboki. [23]Akawatwaa, akawavusha mto, akavusha na vyote alivyokuwa navyo. [24] Yakobo akakaa peke yake; na mtu mmoja akashindana naye mweleka hata alfajiri. [25]Naye alipoona ya kuwa**

**hamshindi, alimgusa panapo uvungu wa paja lake; ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye. [26] Akasema, Niache, niende, maana kunapambazuka. Akasema, Sikuachi, usiponibariki. [27]Akamwuliza, Jina lako n'nani? Akasema, Yakobo. [28]Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda. [29]Yakobo akamwuliza, akasema, Niambie, tafadhali, jina lako? Akasema, Kwa nini waniuliza jina langu? Akambariki huko. [30]Yakobo akapaita mahali pale, Penueli, maana alisema, Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka. [31]Jua likamzukia akivuka Penueli, akachechemea kwa sababu ya paja la mguu wake. [32]Kwa hiyo wana wa Israeli hawali ule mshipa ulio katika uvungu wa paja hata leo; maana alimgusa Yakobopanapo uvungu wa paja katika mshipa wa kiuno**.

**32:22 "akavuka kivuko"** Hili neno la Kiebrania "kuptia" (BDB 716, KB 778, *Qal ya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni mzizi sawa na "kivuko" (BDB 721, kama vile Yos. 2:7; Amu. 3:28; Isa. 16:2). Hii inadokeza kutembea karibu na katika kiwango hafifu.

◙**"Yaboki"** Mzizi huu unamaanisha"kutiririka" (BDB 132).Huu ulikuwa umechimba mtaro mrefu sana

**32:24 "na mtu mmoja akashindana naye mweleka"** Hapa neno "akashindana naye mweleka" (BDB 7, KB 9, *Niphal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU), Yaboki" (BDB 132), pamoja na "Yakobo" (BDB 784), yote yanasikika sawa pale yanapotamkwa. Hapa kiumbe kinaitwa "mtu" (BDB 35, *ish*, kama vile mst. wa 6), lakini muktadha unamaanisha kuwa huu ulikuwa udhihirisho wa kimwili wa Uungu (kama vile mist. ya 28,30; 18:1-2). Hata hivyo, mst. wa 26 unamaanisha baadhi ya mionekano fulani ya kimalaika.

Hii ni aina ya andiko la fasihi ya kimagharibi ambalo haliwezi kueleweka. Kifungu hiki kina yote vipengele vyote vya kiroho na kiishara. Dhana hii ilikuwa kwa ajili ya manufaaa ya Yakobo. Kwa hakika kifungu hiki hakielezi juu ya tabia za "mweleka" wa Mungu!!

YHWH limtokea Yakobo mara nyingi (kama vile 28:10-22; 32:22-31; 35:9-13; 46:2-4) na kwa kila wakati ni kwa sifa na mwonekano wa ahadi za Mungu ambazo zinasisitizwa. Kiini cha mazungumzo haya si Yakobo (au matendo yake), bali Mungu na agano la ahadi zake!

**32:25 "Naye alipoona ya kuwa hamshindi"** Toleo la *Jewish Study Bible*, uk. 67, linautaja utamaduni wa Kiyahudi wenye kusisimua (Mwa. Rab. 77.3) ambao unadai kwamba huyu alikuwa mlinzi wa Esau na huku kukabiliana naye tana kunasaidia kama onyo kwa wote wanaowapinga watu wa agano. Kifungu hiki kinajaribu kueleza kwa nini kiumbe wa kimalaika hawezi kumshinda kwa urahisi. Hata hivyo, malaika wa Esau aweza kulibadili jina la Yakobo kwa kumuita Israeli?! Kwa namna fulani hili likikuwa "lilikuwa jambo la ki- Mungu."

◙**"uvungu wa paja lake" Waalimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwa hili linarejelea"**Walimu wa sheria za Kiyahudi wanasemakuwa kifungu hikli kinarejeleavena ya pajana Uyahudi hii sehemu ya mwili wa myama hairuhusiwi kuliwa (kama vile mst. wa 32).

**32:26 "kunapambazuka"** Hiki kipindi cha siku kilijulikana kama kipindi pekee cha kazi ya Mungu (kama vile NIDOTTE, juzuu 4, uk. 85). Kipindi hiki mara nyingi ilitajwa katika simulizi za jadi za kale. Katika nuru ya hofu ya Kiebrania ya kumwona Mungu (kama vile 16:13; 32:30; Kut. 33:20), bila shaka pambazuko lingeweza kufunua utambulisho wa ki-Ungu wa mapambano ya Yakobo.

◙**"usiponibariki"** Huu haukuwa uwezo wa Ykobo wa kushindana mweleka ambao ungemfanya abarikiwe, bali ni mtazamo wake kung'ang'ania kumtegemea Mungu.

**32:27 "Jina lako nani"** Huu si ukosefu wa taarifa kwa mshindana mweleka wa kimalaika /wa ki- Ungu, bali ni ukumbusho kwa Yakobo juu ya tabia yake ya hila na werevu.

**32:28 "Israeli"** Hili hili badiliko la jina linaonekana kuwa kiini cha fasiri ya maelezo mazima. Jina Israeli linamaanisha "anaweza *El* atunze" (BDB 975) ama ikiwa ni KAULI AMRISHI "na *El* apambane" (kama vile Hosea 12:3-4). Hii haikuwa nguvu ya Yakobo, bali lilikuwa kusudi la Mungu. Jina la mtu huyu lilikuwa muhimu sana kwa Waebrania na lilidokeza sifa ya mtu.

Mbadala mwingine wa jina hili "Israeli" (ישראל, BDB 975) linatokana na ישׁרוב ("*Jeshurun*," BDB 449, kama vile Kumb.32:15; 33:5,26; Isa. 44:2), ambalo linamaanisha "mtu aliye wima."

## MADA MAALUM: ISRAELI (Jina)

I. Kwa mshangao maana ya jina haijulikani (BDB 975, KB 442).
   A. *El* kug'ag'ania
   B. Mwache *El* ag'ag'ane (KAULI AMRISHI)
   C. *El* Hulinda
   D. *Mwache El* na apambane
   E. *El* Achuchumilie
   F. Yule apambanaye na Mungu (neno la mzaha la Mwa. 32:28)
   G. Mwenye Kutegemewa (IDB, juzuu ya 2, uk. 765)
   H. Aliye fanikiwa
   I. Furaha

II. Matumizi katika Agano la Kale
   A. Jina la Yakobo (mbadilishaji, mshika kisigino, BDB 784, KB 872, kama vile Mwa. 25:26) linabadilishwa baada ya kushindana mweleka na mtu katika mto Yaboki (kama vile Mwa. 32:22-32; Kut. 32:13). Mara nyingi maana ya majina ya Kiebrania ayanatamkika kama lahaja, si kwa asili zake (kama vile Mwa. 32:28). "Israeli" likawa jina lake la kupewa (kama vile, Mwa. 35:10).
   B. Hili lilikuja kutumika kama jina la jumla kwa wana wote kumi na wawili wa Yakobo (mf. Mwa. 32:32; 49:16; Kut. 1:7; 4:22; 28:11; Kumb. 3:18; 10:6).
   C. Hili lilikuja kubeba wadhifa wa taifa lililoundwa kwa makabila kumi na mawili kabla ya kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile Mwa. 47:27; Kut. 4:22; 5:2) na baadaye (kama vile Kut. 1:1; 18:6; 33:10).
   D. Baada ya muungano wa utawala wa kifalme wa Sauli, Daudi, na Suleimani chini ya waliyatenga makabila Rehoboamu (kama vile 1 Fal. 12).
      1. tofauti inaanza hata kabla ya utenganishaji wa kiutawala (mf. II Sam. 3:10; 5:5; 20:1; 24:9; 1 Fal. 1:35; 4:20)
      2. hili linabeba wadhifa wa makabila ya kaskazini hadi kufikia kuanguka kwa Samaria hadi Ashuru katika 722 K.K. (kama vile 2 Wafalme 17).
   E. Hili linatumika kumaanisha Yuda katika maeneo machache (mf. Isaya 1; Mika 1:15-16).
   F. Baada ya kupelekwa utumwani Ashuru na Babeli kwa mara nyingiine jina hili lilikuwa jina la ujumla kwa vizazi vya Yakobo vilivyoishi katika Palestina (mf. Isa. 17:7,9; Yer. 2:4; 50:17,19).
   G. Hili lilitumika jumuisho la muundo wa kuwatofautisha makuhani (kama vile 1 Nya. 9:2; Ezra 10:25; Neh. 11:3).

◙**"umeshindaa na Mungu"** Huyu mshindana mweleka anaonekana kujitofautisha na Mungu, japo katika mst. wa 30 Yakobo anatambua kuwa alikuwa akishindana na Uungu.

**32:29 "Niambie, tafadhali, jina lako"** Katika Mashariki ya Karibu ya Kale hili jina la kiumbe cha kiroho lilindwa kwa ukaribu sana kwa sababu ya uwezekano wa kulitumia katika laana, viapo, na taratibu za kimila. Kwa hakika hili si jambo lililo katika maandiko ya kibiblia (kama vile Amu. 13:17-18). Katika maandiko ya kibiblia YHWH analifunua jina lake kwa watu wake (kama vile Kut.3:13-15). Hata hivyo, maana yake haitambuliwi mara kwa mara (linganisha Kut. 6:3 na Mwa. 4:26). Kama Waamuzi 13:18 inavyoeleza, hili jina "linastaajabisha" sana kwa wanadamu kulielewa.

**32:30 "Penieli"** Jina Penieli linamaanisha "uso wa Mungu" (BDB 819). Matamshi ya jina "Penueli" yanaweza kuwa kusababisha matamshi ya jina la mahali.
Kwa hakika jina hili linamaanisha Yakobo alifikiri kuwa uchaguzi wake ulikuwa wa YHWH, ambaye aweza kuuondoa uhai kwa haraka, bali huyaruhusu makubaliano ya muktadha kudokeza juu ya mapenzi yake ili yafanye kazi na kwa upande mwingine wa Yakobo. Huyu hakuwa kinyume, bali anawakilisha msaada na mwenye kubarikiwa.
Hakika haya ni maelezo ya kale yenye kutaabisha yenye vipengele visivyojulikana, kama ilivyo Kut. 4:24-26. Hii inaweza isiwe busara kuyatumia maandiko haya kwa mafundisho au matumizi. Haya yanabaki kamasiri na fasiri zake ni dhahanio tu za sasa!

**32:31 "akachechemea" Kwa vyo vyote vile hali hii ilikuwa ya kudumu** (utamaduni wa Kiyahudi ulio fuatia) ama ya muda tu, jambo hili halijulikani.

**32:32 "hata leo" Kifungu hiki ni uthibitisho wa kimaandiko wa mhariri aliyefuatia**. Mwiko wa kutokula sehemu hii ya mnyama ni wa sheria za kiyahudi, si wa kibiblia.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nani aliyeshindana mweleka?
   a. mtu (kama vile mst. wa 24)
   b. malaika (kama vile mst.wa 26, Hosea 12:3-4)
   c. Mungu katika muundo wa mwanadamu (kama vile mst. 30)
   d. Yesu (Martin Luther, akimfuatisha Justin)
2. Sehemu ya malaika wa mst. wa 1 ina kazi gani katika sura nyingine zilizobakia ?
3. Kwa nini makabilianao haya (yaani, pamoja na malaika na Esau) ni muhimu sana kwa Yakobo
4. Kwa nini jia lilibadilika?

# MWANZO 33

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Yakobo anaonana na Esau | Yakobo na Esau wanakutana | Yakobo na Esau wanapatana (32:1-33:20) | Yakobo na Esau wanakutana | Kukutana na Esau |
| 33:1-3 | 33:1-3 | 33:1-3 | 33:1-5a | 33:1-7 |
| 33:4-11 | 33:4-11 | 33:4-11 | | |
| 33:5b-7 | | | | |
| | | | 33:8a | 33:8-11 |
| | | | 33:8b | |
| | | | 33:9 | |
| | | | 33:10-11 | Makundi ya Yakobo Yanaambatana na Esau |
| 33:12-14 | 33:12-14 | 33:12-14 | 33:12 | 33:12-17 |
| | | | 33:13-14 | |
| 33:15-17 | 33:15-17 | 33:15-17 | 33:15a | |
| Yakobo anakaa Shekemu | Yakobo anafika kanaani | | 33:15b-17 | Yakobo anafika Shekemu |
| 33:18-20 | 33:18-20 | 33:18-20 | 33:18-20 | 33:18-20 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Ukurasa huu unaambatana na mijadala mingi (kumbuka tafasiri ya toleo la TEV). Neno "sema" (BDB 55, KB 65) limetuka mara kumi.

Utaratibu wa mjadala huu una amri/maombi mbalimbali

1. "uliyo nayo na yawe yako,"mst. 9, BDB 224, KB 243, *Qal* KITENZI AMRISHI
2. ."Pokea, tafadhali, mbaraka wangu," mst 11 BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. "Twende zetu, tusafiri ,"mst . 12, BDB 652, KB 704, *Qal* HALI YA KUSIHI

4-5. "Twende zetu, tusafiri," (Mara mbili), mst 12, BDB 229, KB 246, *Qal* HALI YA KUSIHI

6. "Tafadhali bwana wangu na apite mbele ya mtumwa wake ,"mst . 14, BDB 716, KB 778, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI
7. "nami nitawaongoza polepole kwa kadiri ya mwendo wa wanyama walio mbele yangu,"mst . 14, BDB 624, KB 675, *Hithpael* HALI YA KUSIHI
8. "Nikuachie, basi, baadhi ya watu walio pamoja nami "mst . 15, BDb 426, KB 427, Hiphil HALI YA KUSIHI
9. Na nione kibali tu machoni pa bwana wangu,"mst . 15, BDB 592, KB 619, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye HALI YA KUSIHI

B. Yakobo aliikabili hofu yake .

1. Labani
2. Malaika mpambanaji
3. Esau

C. Yakobo anarudi kwenye nchi ya ahadi (kanaan).Unatimia ufunuo ulioahidiwa kule Betheli.Agano alililoahidiwa kwa Ibrahimu na uzao wake linaendelea. (yaani, mpango na mkakati wa wokovu wa milele)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:1-3**
**1 Yakobo akainua macho yake, akaona, na tazama, Esau anakuja na watu mia nne pamoja naye.**
**Akawagawanyia Lea, na Raheli, na wale vijakazi wawili, wana wao. 2 Akawaweka hao vijakazi na wana wao**
**mbele, na Lea na wanawe nyuma yao, na Raheli na Yusufu mwisho. 3 Akapita mwenyewe mbele yao,**
**akainama mpaka nchi mara saba, hata alipomkaribia ndugu yake.**

**33:2** Tambua tofauti inayoonyeshwa kwenye hii famlilia.Wanawake wasio na umuhimu na watoto wanatangulia mbele kwanza, wale anaowapendelea wanafuatia mwishoni (yaani Raheli na Yusufu). Vitu vilibadilika kwenye moyo wa Yakobo, hata hivyo, alitangulia mbele yao wote (kama vile mst. 3).Kama wangeuwawa, yeye (Yakobo) angeuwawa kwanza. Bado alikua na mikakati, lakini alimwamini YHWH's uwepo wake na ahadi ya kulindwa.

**33:3 "akainama mpaka nchi "** Hiki KITENZI (BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) Kimerudiwa mara nne.

1. Yakobo akainama mbele ya Esau,mst . 3
2. vijakazi na wana wao wakainama mbele ya Esau, mst 6
3. Lea na wanawe wakainama mbele ya Esau, mst. 7
4. Raheli na wanawe wakainama mbele ya Esau, mst. 7

◙**"mara saba"** Hili ni tendo la kuonyesha utii (yaani nyaraka za Tel El Amarna, karne ya 14 kabla ya kristo.).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:4-11**
**4Esau akaja mbio kumlaki, akamkumbatia, na kumwangukia shingoni, akambusu; nao wakalia.**
**5Akainua macho yake, akawaona wale wanawake na watoto, akauliza, Ni nani hawa walio pamoja nawe?**
**Akasema, Ni watoto Mungu aliompa mtumwa wako kwa neema yake. 6Ndipo wale vijakazi, na wana wao,**

**wakakaribia wakainama. [7]Lea naye, na wanawe, wakakaribia wakainama. Baadaye Yusufu na Raheli wakakaribia, wakainama. [8]Akasema, Kundi hili lote nililolikuta, maana yake ni nini? Akasema, Kunipatia kibali machoni pa bwana wangu. [9]Esau akasema, Ninayo tele, ndugu yangu, uliyo nayo na yawe yako. [10]Yakobo akasema, Sivyo; kama nimekubalika machoni pako tafadhali upokee zawadi yangu mkononi mwangu, iwapo nimeona uso wako kama kuona uso wa Mungu, ukapendezwa nami. [11]Pokea, tafadhali, mbaraka wangu, ulioletewa, kwa sababu Mungu amenineemesha, na kwa sababu ninavyo hivi vyote Akamshurutisha, naye akapokea.**

**33:4 "Esau akaja mbio kumlaki, akamkumbatia, na kumwangukia shingoni, akambusu; nao wakalia"**Hizi zote ni ishara za salamu za furaha.
1. "akaja mbio," BDB 930, KB 1207, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. "akamkumbatia," BDB 287, KB 287, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. "Kumwangukia shingoni," BDB 656, KB 709, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 45:14; 46:29
4. "akambusu," BDB 676, KB 730, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (Hii inakosekana kwenye LXX (tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani) na kuwekewa kwenye andiko la Kimasoreti (MT) kama toleo jingine),kama vile . 45:15; 48:10; 50:1
5. "wakalia," BDB 13, KB 129, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (Kwenye Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania) na matoleo ya TEV, REB kuna maneno " wote wakalia ," lakini kwa uhalisia , " akalia," kama vile NJB, AB, uk. 258)

**33:5** Esau akamuuliza Yakobo juu ya makundi ya wanawake na watoto wao walioambatana nae. Ilikuwa si jambo la kawaida kwa mwanaume kuwa na wanawake wawili na vijakazi wawili na watoto wao kila mmoja au kama sivyo Esau asingeuliza. Kumbukumbu ya hisia ya Esau katika jambo hili haikuandikwa.

**33:8** Esau akamuuliza Yakobo juu ya kundi hili lote (yaani wanyama ) ambalo Yakobo alikuwa amelituma litangulie mbele ya familia yake (kama vile . 32:13-21).

**33:9 "ndugu yangu,"** Usomaji wa toleo la NASB (uk. 51) Inaleta maana nzuri zaidi inapoelezea kwamba Esau anamuita Yakobo "ndugu yangu," lakini Yakobo anamuita Esau "bwana wangu." Yakobo labda alikuwa (1) binadamu mwenye hekima au (2) alijawa na hofu kubwa .

Zawadi ni ni jambo la kipekee kwa kwa wakati muafaka. Kukataa zawadi kwenye utamaduni huu inaonyesha ni uhusiano wa kulazimisha (yaani James M. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, uk. 41).Kama Esau angekataa kupokea zawadi hii, ingezidisha hofu kuu kwa Yakobo! Esau hakuzihitaji zawadi hizi, lakini kuzipokea zawadi hizi ni kama alama ya kumpokea kaka yake.

**33:10** Yakobo anamsihi Esau kukubali kupokea zawadi yake kwasababu Esau amekubali kumpokea (kama vile mst. 14) ingeenda sambamba na fadhila za Mungu juu yake ("kama kuona uso wa Mungu") mbele zake. Huu yaweza kuwa siri iliyofichwa inayodokezwa kwenye sura ya 25:23.

**33:11** Yakobo alifahamu kuwa chanzo cha Baraka za mali zake ni agano lake na Mungu (yaani "amenineemesha" BDB 335, KB 334, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile mst. 5; 43:29).

◙**"zawadi"** Hii (BDB 139) hasa ni "mbaraka" ni neno lililotumika kuelezea namna Yakobo alivyomdanganya Esau kwenye Sura ya 27. Sio kwa bahati mbaya ya kwamba Yakobo alipenda kumbariki kaka yake kwa kumpa zawadi (hasa baraka). Kwa busara alikuwa amekusudia kumpa zawadi maana alimhadaa hapo mwanzoni.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:12-14**
**[12]Kisha Esau akamwambia, Twende zetu, tusafiri, nami nitakutangulia. [13]Akamjibu, Bwana wangu anajua ya kuwa watoto ni wachanga, tena kondoo na ng'ombe nilio nao wanyonyesha. Hao wanyama wakiharakishwa siku moja, watakufa wote. [14]Tafadhali bwana wangu na apite mbele ya mtumwa wake; nami nitawaongoza polepole kwa kadiri ya mwendo wa wanyama walio mbele yangu, na kwa kadiri ya mwendo wa watoto, hata**

**nitakapofika kwa bwana wangu huko Seiri.**

**33:13** Jambo moja la kushangaza kama njia hii aliyoitumia Yakobo ya kumfanya Esau ahisi ni mkubwa zaidi, kumwomba haraka kuwa hatasafiri pamoja nae kwenda Seiri. Watoto wake hawakuwa "dhaifu"na makundi ya wanyama tayari yalishasafiri umbali mrefu. Je bado Yakobo alikuwa ni mwongo aliye mfanyia hila Esau?

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:15-17**
[15]**Esau akasema, Nikuachie, basi, baadhi ya watu walio pamoja nami. Akasema, Pana haja gani? Na nione kibali tu machoni pa bwana wangu.** [16]**Basi Esau akarudi siku ile ile akishika njia yake mpaka Seiri.** [17]**Yakobo akaendelea mpaka Sukothi. Akajijengea nyumba, akawafanyia makundi yake vibanda. Kwa hiyo jina la mahali pale pakaitwa Sukothi**

**33:15 "watu"** Neno hili ni *goi* (BDB 766 I), ambalo kwa kawaida lina kidokezo hasi chenye kumaanisha ulimwengu, Lakini hapa kimetumika kama watu wa Esau kwenye Kut. 33:13 kikimaanisha watu wa Mungu. Muktadha, muktadha, muktadhaunakusudia maana ya neno, Sio msamiati! Maneno yana maana pekee katika sentensi; sentensi ina maana pekee katika aya/ubeti au shairi;na hii ina maana kubwa sana na hasa katika umoja. Kuwa makini na ufafanuzi wa neno "weka" au "kiufundi"!

**33:17 "Sukothi"** Neno hili (BDB 697) lina maana ya "vibanda" Yakobo alijijengea makazi kwa ajili yake mwenyewe, lakini hii iliitwa "nyumba" (BDB 108), lakini angalia mst . 19. Pia alijenga "vibanda" (BDB 697, yaani vibanda vilivyotokana na matawi ya mti) kwa ajili ya wanyama wake.

Hakuna uhakika kama kulikuwa na vijiji kwenye maeneo haya kabla Yakobo hajaweka kambi. Baadae likaja kuwa jina la mji (kama vile Amu. 8:5).Mji huu Sukothi si sawa na ule unaopatikana jirani na mto delta huko Misri (kama vile Kut. 12:7;Hes . 33:5).Huu ni mji ambao uko mashariki mwa Yordani ( yaani toleo la MacMillan Bible Atlas,uk. 22).

Jambo moja zaidi, Yakobo inaonekana hakumfata Esau Mlima Seiri, lakini akasafiri kwenda Sukothi, ambako siyo njia ya kuelekea Seiri/Edomu. Na akajenga hata nyumba! Haijulikani kama maandiko yanatueleza kwamba (1) Hii ilikuwa nia au (2) Yakobo hakuwa na budi tena ya kutembelea Seiri. Ninarejelea uchaguzi wa #2. Nataka niamini ya kuwa ni kweli Yakobo alikuwa amebadilika, hakuwa tena mtu ambae amejaa hila, hadaa, mwongo

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:18-20**
[18]**Yakobo akaja kwa amani mpaka mji wa Shekemu, ulio katika nchi ya Kanaani, alipokuja kutoka Padan-aramu; akapiga kambi mbele ya huo mji.** [19]**kaAinunua sehemu ya nchi, alipopiga hema yake, kwa mkono wa wana wa Hamori, baba wa Shekemu, kwa vipande mia vya fedha.** [20]**Akajenga huko madhabahu, akaiita, El-elohe-Israeli**

**33:18 "Shekemu"**Jina linaweza kumaanisha
1. jina la mtu,mst. 18,19; 34:2;Hes. 26:31;Yosh. 17:2; 24:32; Amu. 9:28
2. Mandhari ya mji kati ya Mlima Ebali na Mlima Gerazimu. Ni asili moja (BDB 1014 I) yenye maana"bega" au "jembe."
3. Mji ,Yosh. 20:7; 21:21; 24:1; Amu. 8:31

Kwa mara ya kwanza unatajwa katika Mwa . 12:6 ukihusianishwa na Abramu na sasa tena unahusianishwa na Yakobo (kama vile. 37:14).

Hakuna muunganiko ulio wazi kati ya mst . 17na mst. 18. Haikuandikwa ni kwa muda gani Yakobo alikaa Sukothi. Panaonekana kuwepo na matukio mawili tofauti na muda yalipoandikwa hayana uhusiano wa wazi.Kutoka kujenga nyumba hadi kununua aridhi inaonyesha kudokeza kutoka katika makazi ya muda mfupi hadi makazi ya kudumu. Tatizo moja ni kwamba kwenye mst . 18 inaonyesha mara tu baada ya Yakobo kufika akitokea Padani-aramu (eneo linalozunguka Harani) Yakobo alinunua ardhi.

Aliambiwa arudi Betheli, lakini alisimama kwa muda mfupi kisha akabaki. Kwa nini haikuzungumzwa kwenye maandiko!

**33:19 "Akainunua sehemu ya nchi, alipopiga hema yake**"Kitendo cha kununua eneo kinamaanisha ukaaji au kiwastani ni kuonyesha ni mkazi halali.

◙**"Hamori, "J**ina hili lina maana ya "punda" (BDB 331 II). Katika ulimwengu wa kale punda walifikiliwa kuwa ni wanyama watakatifu. Tunalifahamu hili sio tu kutoka bamba za Mari, lakini pia kutokana na (1) wapandao punda mwenye thamani ( kama vile Amu. 5:10) na (2)Mfalme wa Israeli alipanda juu ya punda maalumu kwa ajili ya kuapishwa (yaani., I Fal. 1:33).

◙**"kwa vipande mia vya fedha"** Hili ni neno zuri mno kwa kiebrania, קשיטה, *qesitah* (BDB 903). Ni uzito wa chuma usiofahamika (kama vile.Yosh. 24:32;Ayub 42:11), Labda kwa (1) gharama ya mwanakondoo (LXX) au (2) uzito (mina) wa chuma katika umbo lake (au kupiga muhuri) wa mwanakondoo.

**33:20 "Akajenga huko madhababu"** Mpango huu wa mahali, muda,na namna ya kuabudu. Iliruhusu maombi na sadaka za kuteketezwa kwa YHWH (kama vile . 8:20; 12:7-8; 13:18; 22:9; 26:25). Huu ni ni utimilifu wa ahadi ya YHWH' kwenye kitabu cha Mwa. 28:15!

◙**"El-Elohe-Israeli"** Uundaji huu unafanywa na

1. *El*, BDB 42,kama vile Kut 34:6; tazama Mada Maalumu 12:1
2. *Elohe*, BDB 43, kama vile Kumb. 32:15,17; Zab. 18:32
3. Israeli, tazama Mada Maalumu 32:28

Maandiko ya kale ya Kiebrania yanatafsiri kama "Mungu wa Israeli" Toleo la Jewish Study Bible, ikitumia tafasiri ya JPSOA kwenye tanbihi yake ya maandiko, ina neno "*El*, Mungu wa Israeli" (uk. 69).

# MWANZO 34

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Udanganyifu wa Wana wa Yakobo | Tukio la Dina | Shekemu Kumdhlilisha Dina | Ubakwaji wa Dina | Ubakwaji wa Dina |
| 34:1-7 | 34:1-4 | 34:1-4 | 34:1-4 | 34:1-5 |
| | | 34:5-7 | 34:5-10 | Mungano wa Kuoana na Washekemu |
| | | | | 34:6-12 |
| 34:8-12 | 34:8:12 | 34:8:12 | | |
| 34:13-17 | 34:13-17 | 34:13-17 | 34:13-17 | 34:13-19 |
| 34:18-24 | 34:18-24 | 34: 18-24 | 34:18-24 | |
| | | | | 34:20-31 |
| | | | | Mbinu za kisasi cha Simeoni na Lawi |
| 34:25-31 | 34:25-31 | 34:25-31 | 34:25-29 | 34:25-29 |
| | | | 34:30 | 34:30-31 |
| | | | 34:31 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ilimpasa Yakobo kukabiliana na hofu yake na majaribu.
   1. Labani
   2. Esau
   3. Mwingiliano wa kuoana na Wakanaani
   4. Ghasia za Wakanaani

B. Yakobo bado ni mtu mwenye hofu.
   1. alimdanganya Esau na hakumfuata Seiri
   2. hakwenda Betheli (kama alivyoambiwa na Mungu)
   3. anajaribiwa kuoana na watu wa nchi hiyo kwa manufaa yao binafsi
   4. ana hofu juu ya malipizi ya Wakanaani

C. Jina la Mungu halionekani katika sura hii (inaweza kuwa ni kwa kusudi fulani)!

D. Bila shaka inawezekana kwamba sura hii imehusishwa katika sura hii
   1. kama ulinganisha wa ubora wa sura ya 17
   2. kama njia ya kuonyesha sababu ya Yuda kuwa mlolongo wa Masihi na si mtiririko wa wana watatu.

Sura ya 34 itawaondoa Simeoni na Lawi kama mbadala unaowezekana (kama vile Mwa. 49:5-7)

Kumbuka "simulizi za kihistoria" lazima ufasiriwe katika upana wa vipengele vya kimuktadha. (Angalia Makala inayohusu Simulizi za Agano la Kale katika ukurasa wa xvii.)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA ) 34:1-7**
**1 Basi Dina, binti Lea, ambaye Lea alimzalia Yakobo, akatoka kuwaona binti za nchi.**
**2 Shekemu, mwana wa Hamori, Mhivi, mkuu wa nchi, akamwona akamtwaa, akalala naye, akambikiri.**
**3 Moyo wake ukaambatana na Dina binti Yakobo, akampenda huyu msichana, akasema na huyu msichana kwa maneno mazuri.**
**4 Shekemu akamwambia Hamori, babaye, akasema, Unipatie msichana huyu awe mke wangu.**
**5 Basi Yakobo akasikia ya kwamba amembikiri Dina, binti yake. Na wanawe walikuwako pamoja na wanyama wake nyikani. Yakobo akanyamaza, hata walipokuja.**
**6 Akatoka Hamori, babaye Shekemu, kumwendea Yakobo, aseme naye.**
**7 Wanawe Yakobo waliposikia hayo, wakaja kutoka nyikani; nao wakasikitika sana, wakakasirika mno, kwa sababu amefanya upumbavu katika Israeli kwa kulala na binti Yakobo, neno lisilojuzu kutendeka.**

**34:1 "Dina, binti Lea"** Kipindi kirefu kilipita kati ya Mwanzo 33 na Mwa 34. Watoto wamekwisha kua sasa. Dina ndiye binti pekee anayetajwa katika uzao wa Yakobo (kama vile 30:21). Bila shaka kulikuwa na mabinti wengine (kama vile 37:35), lakini Dina ndiye anayetajwa tu kwa sababu ya kiini chake cha mjadala wa sura hii. Jina lake liko katika muundo wa jinsia ya kike ya neno "hukumu" au "ushahidi" (BDB 192), ambalo ni jina la wana wa Yakobo (kama vile 30:6) na baadaye kuwa moja ya makabila, Dani.

◙
**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB** **"kuwatembelea"**
**NKJV, LXX,**
**Peshitta** **"kuwaona"**

Hiki KITENZI "kuwaona" (BDB 906, KB 1157, *Qal* TUNGO YA KITENZIJINA) kinaweza kueleweka katika namna mbalimbali (kwa maelezo yaliyo dhahiri alikwenda peke yake).
   1. kuwatambua, kujifunza kutoka kwao na kuyaona maisha yao

2. kuwatembelea marafiki zake, Yako alikuwa ameishi maeneo yale kwa miaka kadhaa
3. ni mzaha wa mst. wa 2, “Shekemu akamwona” (KITENZI kile kile)

**34:2 “Shekemu”** Huyu ni mwana wa mfalme wa kabila la mahali pale. Hamori ni mkuu au kiongozi wa kikabila kwa wakati. Huyu mwana wa mfalme aliitwa jina hili baada ya kuua kwa mji huu. Ili kuifahamu maana ya jina hili, angalia 33:18.
Inawezekana kwamba kisarufi kuutwaa “ukuu” (BDB 672 I), jambo linamaanisha “mtu aliyeinuliwa,” kama ilivyo rejea ya Hamori (angalia *Handbook on Genesis* na Reyburn na Fry, USB, uk. 786).

◙ **“Mhivi”** Agano la Kale la Kiebrania linalitafsri neno hili kama Mhori (kama vile Mwa. 34:2; Yos. 9:7). Ni dhahiri kwamba hawa walikuwa hawajatahiriwa, kundi la watu wasio wa Kisemiti ambalo lazima litambuliwe kama na wa-Huri. Makundi mawili pekee ya watu waliokuwa hawajatahiriwa katika Israeli kwa nyakati zile za kale yalikuwa ya Wafisti, ambao walikuwa wahamiaji wa wanajeshi wastaafu wa Aegean, na hawa wa-Hurri. Makabila yote ya Wakanaani yalikuwa yakifanya tohara. Angalia Mada Maalum katika 12:6.

◙ **“akamtwaa, akalala naye”** Hii ni mbinu ya kiuandishi (VITENZI viwili vyenye kuelezea tendo moja). Katika siku zile hili linashtua sana, lakini Katika Mashariki ya Karibu ya Kale mwana wa mfalme alikuwa na haki. Njia za utafutaji mwanamke katika kipindi hiki na katika maeneo haya zilikuwa tofauti sana na ukilinganisha njia za sasa (yaani, Kut. 22:16-17; Kumb. 21:10-14; 22:28-29). Utamaduni wa kiukoo ulihusu haki za wanaume na kwa uchache sana kuhusu uhuru na hisia wanawake. Kuna VITENZI kadhaa ambavyo vinadokeza tendo la kujamiiana.
1. akalala naye, BDB 1011, KB 1486, kama vile Mwa.19:32; 26:10; 30:15; 39:7; Law. 18:22
2. akamtwaa, BDB 897, KB 1132, kama vile Mwa. 20:4; Law. 18:6,14,19; 20:16
3. akamwingilia, BDB 97, KB 112, kama vile Mwa. 19:31; 29:21,23,30; 30:3,4,16; 38:8,9,16; 39:14
4. akamjua, BDB 393, KB 390, kama vile Mwa. 4:1,17,25; 19:5,8; 24:16; 38:26; Hes. 31:17,18,35; Amu. 19:22,25; 21:12

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV,** | |
| **JPSOA** | **“kwa nguvu”** |
| **NKJV, REB** | **“akamwingilia”** |
| **TEV** | **“akambaka”** |
| **NJB** | **“akalazimisha kulala naye”** |
| **LXX** | **“akamdhalilisha”** |
| **Peshitta** | **“akamnajisi”** |

Hiki KITENZI (BDB 776, KB 853, *Piel* cha WAKATI USIO TIMILIFU) katika shina la *Piel* kinamaanisha “kudhalilisha” katika maana ya kujamiina na mtu pasipo matakwa yake (yaani, kubaka, kama vile Kumb. 21:14; 22:24,29; Amu. 19:24; 20:5; II Sam. 13:12,14,22,32; Eze.22:10,11). 34:3 “Moyo wake ukaambatana na Dina” Ingawa kijana huyu na heshima kuliko watu wote wa numbani mwa babaye (kama vile 19), bado anaendelea kufanya tendo la kidhalilishaji kwa Dina. Ni dhahiri kuwa huu ulikuwa udhalilishaji kwa huyu mhamiaji na watu wa nyumbani kwa Dina. Hisia za Shekemu kwa Dina zimerudiwa katika namna tatu.
1. “Moyo wake ukaambatana na Dina” (kifasihi. “moyo wake ukapasuka kwa ajili yake”), BDB 179, KB 209, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU kama vile I Fal. 11:2
2. “akampenda huyu msichana,” BDB 12, KB 17, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU; neno “msichana” (BDB 655) linadokeza binti, lakini mwenye umri wa kuelewa, kijana
3. “akasema na huyu msichana kwa maneno mazuri” (kifasihi. “akazungumza na moyo wa huyu msichana”), BDB 180, KB 210, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 50:21; Amu. 19:3; Ruthu 2:13
4. “Roho ya Shekemu, mwanangu, inamtamani binti yenu,” mst. wa 8, BDB 365 I, KB 362, *Qal ya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 21:11
5. “maana amependezewa na binti Yakobo,” mst. 19, BDB 342, KB 339, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

◙ “**huyu msichana**” Katika sura hii Dina anaelezwa kwa maneno kadahaa na tofauti tofauti.

1. binti, mst. wa 1, BDB 123 I (mara kadhaa)
2. msichana, mst. wa 3, BDB 655, kama vile mst wa 12
3. msichana, mst. wa 4, BDB 409, kama vile Yoeli 3:3; Zek. 8:5 (neno hili linatumika kwa wanawake hawa pekee mara tatu, kutokana na mzizi “zaa,” “sababibishiwa”)
4. umbu, mst. wa 13, BDB 27, kama vile mist. wa 14,27,31

**34:4 “Shekemu akamwambia Hamori, babaye, akasema, ‘Unipatie msichana huyu awe mke wangu**’”
Jambo hili linaendana na utamaduni wa wazazi kupanga utaratibu wa ndoa za watoto wao. Lakini tambua kwamba kijana alianza kwa kutoa ombi (BDB 542, KB 534, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI). Tatizo lilikuwa ni upumbavu wa Shekemu wa kuanza kwa dhalilisho la kiuzinifu (kama vile mst. wa 7).

**34:5**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, LXX,**
**JPSOA “amembikiri”**
**TEV “amefedhehesha”**
**NJB, REB “amemchafua”**

Hiki KITENZI (BDB 379, KB 375, *Piel* cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinadokeza kitu kile kinachoonekana kutokuwa safi kulingana na sheria ya Mungu (kama vile Law. 18:24-30). Hapa kitenzi hiki kinadokeza uchafu wa kiuzinifu (kama vile Eze. 18:6,11,15; 22:11; 23:17;33:26). Dina alibakwa na Mkanaani asiyetahiriwa.

◙ **“Yakobo akanyamaza”** Sababu yake haikuelezwa. Inaweza kuwa

1. jaribu la kutumia wakati huu kwa ajili ya manufaa yake binafsi (kama vile mst. wa 6,30).
2. kuwangoja wanae na watumwa wake wachukue maamuzi yake wenyewe
3. ya kwamba ndugu zake walikuwa na “neno la kuzungumza” kuhusiana na tukio hili

**34:7** Ndugu wa Dina walikasirika mno.

1. “nao wakasikitika sana,” BDB 780, KB 864, *Hithpael* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Mwa. 6:6
2. “walikasirika mno,” BDB 354, KB 351, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Mwa. 4:5,6; 31:36; 39:19.
3. “amefanya upumbavu,” BDB 615, yaani, jambo lisilo na maana na alitenda kinyume na taratibu za maadili ya Yakobo na utamaduni wa dini yake, kama vile Kumb. 22:21; Amu. 19:23; 20:6; II Sam. 13:12 (hii NOMINO inamaanisha “mpumbavu”)

◙ **“katika Israeli”** Huku ni kutumia neno hili katika maana inayofuata. Katika kifungu hiki neno hili linarejelea sheria za taifa la Israeli. Hii ni ishara ya kimuktadha ya mhakiki wa baadaye, mlinganishaji, ama mwandishi (kama vile Kumb. 22:21; Yos. 7:15; Amu. 19:23;20:10).
Baadhi ya watoa maoni wanajaribu kukiweka KUHUSISHI hiki (BDB 88-91) kimaanishe “kwa,” lakini kinamaanisha “katika”

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 34:8-12**
[8] **Hamori akasema nao, akinena, Roho ya Shekemu, mwanangu, inamtamani binti yenu, tafadhalini, mpeni amwoe.** [9] **Mkaoane na sisi, mtupe sisi binti zenu, nanyi mkatwae binti zetu.** [10] **Nanyi mtakaa nasi, na nchi hii itakuwa mbele yenu; kaeni, na kufanya biashara humo, mkapate mali humo.** [11] **Shekemu akamwambia babaye yule msichana na nduguze, Na nikubalike machoni penu, na mtakavyoniambia nitatoa.** [12] **Mjapoongeza sana mahari na zawadi, nitatoa kadiri ya mtakavyoniambia, lakini mnipe huyu msichana, awe mke wangu.**

**34:8 "nao"** Neno ili linawarejelea ndugu wote wa na Dina wale wa baba yake. Baba yake Shekemu anajaribu kuituliza hasira na ile maana mbaya ya fedheheha. Mstari wa 11 unaonyesha kwamba Yakobo anazungumziwa pia.

**34:9 "Mkaoane"** Huu ulikuwa utamaduni wa nyumba ya Ibrahimu (kama vile Mwa. 24:3) au Isaka (kama vile Mwa. 28:1,8). Sasa Yakobo anajaribiwa.

**34:10 "na nchi hii itakuwa mbele yenu"** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha kuingia na kusafiri bure ndani ya nchi hiyo (kama vile Mwa. 13:9; 20:15).
Tambua wingi wa ahadi zilizohaidiwa kwa Yakobo na nyumba yake ikiwa wangeikubali ndoa hii.

1. "nanyi mtakaa nasi," mst. wa 10
2. "na nchi hii itakuwa mbele yenu," mst. wa 10
3. "na kufanya biashara humo, mst. wa 10 ("biashara" huenda neno hili linamaanisha "kusafiri bure katika nchi hii" katika muktadha huu, kama vile 42:34; NJB, lakini mzizi huu huu unaweza kumaanisha "wafanya biashara," kama vile. 23:16; I Fal. 10:28-29)
4. "mkapate mali humo," mst. wa 10
5. "mtakavyoniambia nitatoa," mst. wa 11
6. "Mjapoongeza sana mahari na zawadi," mst. wa 12

Katika maana nyingine, iweni mmoja wetu! Ilimpasa Yakobo kwenda Betheli. Alibaki karibu na Shekemu (mji) kwa muda mrefu. Na sasa hili dhalilisho na maumivu ikawa gharama ya kutii kwake.

**34:12 "mahari na zawadi"** Kifungu hIki kinarejelea mapambo ya bibi harusi au *mohar* ya Kiebrania (BDB 555). Hili haikuwa na maana ya kumpata mwanamwali, bali fidia ya kumpoteza msaidizi (kama vile Kut. 22:16-17; I Sam. 18:25). Mahari hii mara nyingi ilitunzwa ikiwa kwa ajili ya mwanamke ikiwa atafiwa na mwanamme ama kwa mahitaji ya baadaye (kama vile Mwa.31:15 ambapo binti za Labani wanalalamika kwamba baba yao alikula fedha zao).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 34: 13-17**
**13 Wana wa Yakobo wakawajibu Shekemu na Hamori babaye, kwa hila, maana amemharibu Dina, umbu lao, 14 wakawaambia, Hatuwezi kufanya neno hili, tumpe umbu letu mtu asiyetahiriwa; ingekuwa aibu kwetu. 15 Lakini kwa sharti hii tu tutapatana nanyi; mkiwa kama sisi, akitahiriwa kila mwanamume wenu, *16* ndipo tutawapa ninyi binti yetu, na sisi tutatwaa binti zenu tutakaa pamoja nanyi, nasi tutakuwa watu wamoja. *17* Lakini kama hamtusikii na kutahiriwa, basi tutamtwaa umbu letu, nasi tutakwenda zetu.**

**34:13**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa hila"** |
| **NKJV** | **"walizungumza kwa ulaghai"** |
| **NRSV, Peshitta** | **"wakajibu. . .kwa ulaghai"** |
| **TE** | **"katika namana ya ulaghai"** |
| **NJB** | **"wakajibu kwa udanganyifu"** |
| **LXX** | **"udanganyifu"** |
| **JPSOA** | **"wakazungunza kwa ujanja"** |

Hii NOMINO "hila" (BDB 941) inamaanisha undumilakuwili. Hii ilitumiwa na Isaka kuhusu njama iliyokuwa ikifanywa juu ya Yakobo katika Mwa. 27:35. Mzizi huu huu unatumika kueleza juu ya njama za Labani kwa Yakobo kumhusu Lea katika Mwa. 29:25. Hii tabia ya Yakobo ilibaki ndani ya nyumba yake.

**34:14-17"hamtusikii na kutahiriwa"** Tohara ilikuwa ishara ya agano la YHWH (kama vile Mwa. 17:9-14). Hapa, ndugu za Dina wanalitumia jambo hili kimwili kuliko maana yake ya kiroho. Hawa walikuwa na shauku za kimadhabahu. Lazimisho la Shekemu za kiudhalilishaji sasa linatumika kama msamaha wa lazimisho la

kiudhalilizaji kwa kabila zima! Aina hii ya kisasi hasa ndiyo sheria ya Kiebrania "Jicho kwa jicho" (kama vile Kut. 21:24; Law. 24:20) iliyomaanisha kusitisha.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 34: 18-24**
[18] **Maneno yao yakawa mema machoni pa Hamori, na machoni pa Shekemu, mwana wa Hamori.** [19] **Na yule kijana hakukawia kulifanya neno lile, maana amependezewa na binti Yakobo, naye alikuwa mwenye heshima kuliko wote nyumbani mwa babaye.** [20] **Hamori, na Shekemu mwanawe, wakaja langoni pa mji wao, wakasema na watu wa mji wao, wakinena,** [21] **Watu hawa wana amani nasi, basi na wakae katika nchi, na kufanya biashara humo; kwa maana nchi ni kubwa, yawatosha; na tuwatwae binti zao kuwa wake zetu, na binti zetu tuwape wao.** [22] **Lakini kwa sharti hiyo moja tu watapatana nasi wakae wote kwetu, tuwe watu wamoja, kama tukitahiriwa kila mwanamume, kama hawa walivyotahiriwa.** [23] **Je! Kondoo zao, na mali zao, na wanyama wao wote hawatakuwa mali zetu? Basi na tupatane nao tu, nao watakaa kwetu.** [24] **Wakawasikia Hamori na Shekemu mwanawe, wote watokao katika lango la mji wake. Wakatahiriwa kila mwanamume, wote watokao katika lango la mji wake**.

**34:19** Mstari huu unaorodhesha mambo matatu ambayo Shekemu aliyafanya ili kupata ukubalifu ndani ya nyumba ya Yakobo (1) hakuchelewa; (2) alipendezwa na binti Yakobo; na (3) alihatarisha hadhi na heshima yake kwa kuiweka rehani.

**34:20 "wakaja langoni pa mji wao"** Lango lilikuwa sehemu ya lilikuwa ni kwa ajili ya eneo la taifa hilo, jamii, na kwa ajili ya utawala wa maisha ya jamii. Akaomba rufani kwa watu hawa (yaani, wale waliokuwa wamekwisha kufikia umri wa kupigana) katika misingi ya kulipa fidia (kama vile mst. 23).

**34:21** VITENZI vyote vine vilivyo katika mstari huu ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika klatika maana ameishi (yaani, "na tuwatwae . . .").

**34:23** Washekemu waliiona ishara hii (yaani, tohara) kama sehemu ya kuongeza nguvu na utajiri wa kabila lao. Watu wa agano hawakukua, lakini kabila la Wakanaani ndivyo lilivyokuwa!

**34:24** Vyema! Huu ni umiliki mkuu. Tohara kwa vijana inama maumivu nan i hatari (yaani) zile hatua zake. Haya yote yalikuwa ni kwaajili ya kumruhusu mkuu kumuoa mwanamke wa kigeni aliyempenda (yaani, neno mkuu ndilo neno haliosi). Ni vigumu kwa wanamagharibi wa sasa kuufahamu uaratibu wa utawala wa makabila ya  na kutoa heshima kwa viongozi wa makabila hayo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 34:25-31**
[25] **Ikawa siku ya tatu, walipokuwa wakiumwa sana, wana wawili wa Yakobo, Simeoni na Lawi, nduguze Dina, wakatwaa kila mtu upanga wake, wakaujia mji kwa ujasiri, wakawaua waume wote.** [26] **Wakawaua Hamori, na Shekemu mwanawe, kwa makali ya upanga, wakamtwaa Dina katika nyumba ya Shekemu, wakatoka.** [27] **Wana wa Yakobo wakawajilia hao waliouawa, wakauteka nyara mji kwa sababu wamemharibu umbu lao.** [28] **Wakachukua kondoo zao, na ng'ombe zao, na punda zao, na vitu vilivyokuwamo mjini, navyo vilivyokuwako kondeni.** [29] **Wakatwaa na mali zao zote, na watoto wao wote, na wake zao, na vyote vilivyokuwamo nyumbani mwao wakavichukua mateka.** [30] **Yakobo akawaambia Simeoni na Lawi, Mmenitaabisha, kunifanya ninuke vibaya kati ya watu wa nchi hii, Wakanaani na Waperizi; na mimi, kwa kuwa watu wangu ni haba, watanikusanyikia, na kunipiga, nami nitaangamizwa, mimi na nyumba yangu.** [31] **Nao wakasema, Je! Ni vema amtendee umbu letu kama kahaba?**

**34:25"Ikawa siku ya tatu**. . . **Simeoni na Lawi, nduguze Dina"** Watu waliokuwa wametahiriwa wangelisikia maumivu zaidi siku ya tatu baada ya tohara.  Wana wa Lea wa ipi na wa tatu walilifahamu jambo hili na kuchukulia kama faida ya kuwaua kwa makali ya upanga wamaume wote, na kuchukua mali zote walizozimiliki wanawake na watoto. Baadaye, katika Mwa. 49:5-7, jambo hili litakuwa msingi wa unabii dhidi ya haya makabila mawili

yaliyokuwa na wazo la utawala ndani ya nyumba ya Yakobo.  Hata hili liaelezwa kama sababu ya Lawi kutomiliki uajili pamoja na makabila mengine, bali atatengwa pamoja na makabila mengine.

**34:26"wakamtwaa Dina katika nyumba ya Shekemu"** Huu ulikuwa utamaduni wa kiukoo. Kiongozi hakutazisikiliza hisia ama uchaguzi wa Dina hata kidogo. Mtu anashangaa

1. kama msichana huyu aliishi ndani nya nyumba ya Shekemu kwa hiari yake ama alilazimishwa
2. kama hakurudi nyumbani kamwe na simulizi lake kusikika ama alisindimkizwa na watu wa nyumbani kwao katika mst. wa 1.
3. kama kama aliyafahamu fika matokeo ya agano la uwezekano wa kuolewa kwake kwa Wakanaani

**34:27**
**NASB** **"Wana wa Yakobo"**
**LXX, Peshitta** **"lakini wana wa Yakobo"**
**TEV, NJB,**
**REB** **"wana wengine wa Yakobo"**

Toleo la NASB linafuatisha toleo la MT, lakini matoleo ya kale yanakitafsiri kifungu hiki hivyo ili kuwahusisha wana wote wa Yakobo katika unyanganyi, lakini si katika mauaji.  Kungekuwa na tuhuma nyingi za mauaji zilizowazunguka hasa kwa hawa nawa wawili na wangetumika kama kielelezo.

**34:28-29** Mapigano ya wao kwa wao katika nyakati za kale ni ya kuogopesha sana kwa jamii za sasa, hii ni kutokana na namna watu hao walivyofanya mambao katika namna ya machafuko na namna walivyotenda matendo ya kiunyang'anyi.  Wanawake na watoto walionekana kama vitu vya kumilikiwa na hawakuhusishwa katika jamii mpya (hivi ndivyo Dina alivyochukuliwa).

**34:30-31** Yakobo anaonekana  kuwa na hisia za woga zaidi kutokana na mambo hayo kulikokumwamini Mungu. Mungu aliahidi kumlinda na kuwa pamoja naye,  lakini anaonekana kuonyesha hisia zake zilizojikita katika uweza wake mwingi, na si ahadi (kama vile 28:15).
Kama Rebeka na Yakobo walivyotumiwa na Mungu kumlazimisha Isaka kufanya jambo lililotabiriwa(kama vile Mwa. 25:23), ndivyo ilivyokuwa kwa wana wa Yakobo sasa, WANA wa Yakobo wanamlazimisha Yakobo kufanya jambo la haki (yaani, kutooana na Wakanaani na ile safari ya Betheli).  Uelekeo huu unaonekana tena katika Amu. 8:33-35.
Mungu anafanya mambo katika namna ya kushangaza ili kutimiza makusudi yake ndani ya nyumba ya Ibrahimu!!!

**34:30**
**NASB, NRSV,**
**JPSOA,** **"chukizo"**
**NKJV** **"karaka"**
**NJB, REB** **"harufu mbaya"**
**LXX** **"uovu"**
**Peshitta** **"haribu sifa yangu"**

Hii *Hiphil* TUNGO KITENZIJINA (BDB 92, KB 107) inamanisha kusababisha kunuka (kama vile Kut. 16:24; Zab.38:5). Hii imetumika kistiari kumaanisha kukataliwa na watu wa katika Kut. 5:21; I Sam. 27:12; na hapa.

◙ "Wakanaani na Waperizi" Tazama Mada Maalum katika 12:6.

# MWANZO 35

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakobo anaenda Betheli | Yakobo anarudi Betheli | safari ya Yakobo kutoka Shekemu Hadi Mamre | Mungu anambariki Yakobo huko Betheli | Yakobo huko Betheli |
| 35:1-4 | 35:1-4 | 35:1-4 | 35:1 | 35:1 |
| 35:2-4 | 35:2-5 | | | |
| 35:5-8 | 35:5-7 | 35:5-8 | 35:5-8 | |
| Yakobo anaitwa Israeli | 35:8 | | | 35:6-8 |
| 35:9-15 | 35:9-15 | 35:9-15 | 35:9-15 | 35:9-10 |
| (10) | | | | |
| (11-12) | | | | |
| | | | | 35:11-13 |
| | | | | 35:14-15 |
| | Kifo cha Raheli | | kifo cha Raheli | kuzaliwa kwa Benyamini Kifo cha Raheli |
| 35:16-21 | 35:16-20 | 35:16-21 | 35:16-18 | 35:16-20 |
| | | | 35:19-21 | kujamiiana kwa maharimu Wa Rubeni |
| | 35:21-22 | | Wana wa Yakobo | 35:21-22a |
| 35:22a | | 35:22a | 35:22a | |
| Wana wa Israeli | | | | Wana kumi na mbili wa Yakobo |
| 35:22b-26 | Wana kumi na mbili Wa Yakobo | 35:22b-26 | 35:22b-26 | 35:22b-26 |
| | 35:23-26 | | | |
| | Kifo cha Isaka | | Kifo cha Isaka | kifo cha Isaka |
| 35:27 | 35:27-29 | 35:27-29 | 35:27-29 | 35:27-29 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Mungu anamwamuru Yakobo
   1. inuka, BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI

   2. nenda, BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI
   3. ishi (kifasihi. kuishi), BDB 442, KB 444, *Qal* KAULI SHURUTISHI
   4. tengeneza madhabahu, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHIna baadaye katika mstari wa 11
   5. zaeni, BDB 826, KB 963, *Qal* KAULI SHURUTISHI
   6. mkaongezeke, BDB 915, KB 1176, *Qal* KAULI SHURUTISHI; amri zote hizi mbili zina aksi amri za Mungu
      a. kwa wanyama,Mwanzo 1:28
      b. kwa kumaanisha Adamu na Hawa
      c. kwa Nuhu, Mwanzo. 9:1,7
      d. kwa Ibrahimu kwa namna mbali mbali
      e. na sasa kwa Yakobo

B. Yakobo anaiamrisha familia yake kujiandaa
   1. wekeni mbali miungu migeni, BDB 693, KB 747, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
   2. jitakaseni, BDB 372, KB 369, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
   3. badilisheni mavazi yenu, BDB 322, KB 321, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
   4. tuinuke, BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI YENYE HALI YA KUSIHI, kama vile mstari wa 1
   5. twendeni, BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFUimetumika katika namna ya HALI YA KUSIHI, kama vile mstari wa 1

C. WakatiYakobo hatimaye alikuwa mtii na kuja Betheli YHWH inasemekana alizungumza naye tena, mistari ya 9-1

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:1-4**
**1 Mungu akamwambia Yakobo, Ondoka, panda uende Betheli, ukakae huko; ukamfanyie Mungu madhabahu huko; yeye aliyekutokea ulipomkimbia Esau, ndugu yako. 2Yakobo akawaambia watu wa nyumbani mwake, na wote waliokuwa pamoja naye, Ondoeni miungu migeni iliyoko kwenu, mjisafishe mkabadili nguo zenu. 3Tuondoke, tupande kwenda Betheli, nami nitamfanyia Mungu madhabahu huko; yeye aliyenisikia siku ya shida yangu, akawa pamoja nami katika njia yote niliyoiendea. 4Nao wakampa Yakobo miungu migeni yote iliyokuwa mikononi mwao, na pete zilizokuwa masikioni mwao, naye Yakobo akazificha chini ya mwaloni ulioko Shekemu.**

**35:1 "Mungu akamwambia Yakobo, 'panda uende Betheli'"** Makutano ya kwanza ya Yakobo na YHWH ilikuwa eneo hili, kama vile Mwanzo 28:18-22; 35:14. Anajiita yeye Mwenyewe "Mungu wa Betheli" na anamwambia Yakobo kurudi Kanaani katika Mwanzo 31:13.231.
Ile "ondoka" KITENZI (BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI) inaweza kueleweka katika namna mbili.
1. Betheli ilikuwa kusini, lakini ilikuwa katika uwanda wa juu kulinganisha na Shekemu.
2. VITENZI mara nyingi vinatumika juu ya kwenda hekaluni (yaani sehemu takatifu). Betheli inawezekana kuwa iliwakilisha ukaribu wa kiupendo na Mungu.

◙**"ukamfanyie madhabahu"** Neno "madhabahu" (BDB 258) linamaanisha sehemu ya machinjio.Mababa wa Imani walitengeneza madhabahu nyingi sana.
1. Nuhu juu ya mlima Ararat, Mwanzo 8:20
2. Ibrahimu
   a. pale Shekemu, Mwanzo 12:7
   b. pale Betheli, Mwanzo 12:8
   c. pale Hebroni, Mwanzo 13:18
   d. pale Moria, Mwanzo 22:9
3. Isaka pale Beersheba, Mwanzo 26:25

4. Yakobo
    a. pale Shekemu, Mwanzo 33:20
    b. Betheli, Mwanzo 35:7

Ni wazi utoaji wa dhabihu ulitangulia agano la Musa

**35:2 "miungu migeni iliyoko kwenu"** Neno "miungu" (herufi ndogo ya "m" WINGI) ni sawasawa na neno*Elohim* (herufi kubwa"Mungu") katika mstari wa 1. Muktadha lazima uamue ufasiri wa neno hili. Angalia Mada Maalum katika 12:1.

Mstari huu unafurahisha sana kwa namna unavyoonyesha maandalizi muhimu ya kiroho kwa ajili ya kufanya upya ahadi za agano. Hii miungu ya kigeni inaweza kufa ilimaanisha (1) *teraphim (vinyago)*ya Mwanzo 31:19,30; (2) miungu mingine iliyoletwa kutoka Harani na watu wa nyumba yake; au (3) miungu iliyochukuliwa kutoka Shekemu na iliyofanywa kwa vyuma (thamani ya kiuchumi na kifedha), iliyotengenezwa kwa ufundi mkubwa (ascetic thamani). Hii inafanana na kufanywa upya kwa Josh. 24:14,23 (kama vile I Sam.7:3).

Inafurahisha sana kwamba maandalizi ya kiroho (the VERBKITENZI "kutakasa" [BDB 372, KB 369] ni*Hiphil*KAULI SHURUTISHI; hii haikuwa mbadala; haya ni matumizi pekee ya KITENZI hiki katika Mwanzo, lakini inakuwa kawaida iliyozoeleka katika Mambo ya Walawi), na ilikuwa inawakilishwa na kuoga na kubadilisha kwa mavazi (kama vile Kutoka 19:10; Hes. 8:7,21; 19:19).Hivyo uwakilishi huu wa kimweili wa nje ulikusudiwa kuaksi maandalizi ya ndani ya kiroho ya familia yote ya Yakobo. Doa la kuchinjwa kwa Shekemu lilikuwa zito sana kwao.

**35:3 "Tuondoke, tupande kwenda Betheli, nami nitamfanyia Mungu madhabahu huko"** Yakobo anarudi katika eneo ambalo kwa mara ya kwanza alikutana na Mungu (kama vile Mwanzo 28:18-22). Kwa wakati huu mahusiano yake na YHWH mtu anaweza akashangaa kama ni mwamini wa imani kwa Mungu mmoja (Mungu mmoja na mmoja tu) au mwamini wa Mungu kwake tu (Mungu mmoja kwa ajili yangu tu na familia yangu).

**35:4 "miungu migeni"** Hii inaweza kumaanisha "miungu wa nyumbani kwetu" (*teraphim*, kama vile 31:19,30,34; Waamuzi 17:5;I Sam. 19:13; Hosea 3:4, angalia Mada Maalum katika 31:19),ambayo inaashiria ibada ya watu wa kale. Inawezekana kabisa kwa hakika kwamba Yakobo na familia yake yote (yaani wafanyakazi wake, kama vile mstari wa 6b) walikuwa waabudu miungu wengi na walikuwa wameleta viwakilishi au vitu vinavyowakilisha miungu pamoja nao.

◙**"na pete zilizokuwa masikioni mwao"** Inavyoonekana hizi zilikuwa aina fulani ya hirizi za miujiza ambazo zilikuwa zikihusiana na kuabudu miungu (kama vile Hos. 2:13)

◙
**NASB, NKJV**
**NRSV** **"kuficha"**
**TEV, NJB**
**JPSOA, REB** **"kuzika"**

KITENZI (BDB 380, KB 377, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO MKAMILIFU) inaweza kumaanisha "kuficha," "kuweka mbali pasipofikika kirahisi," au "kufukia" (kama vileAyubu 40:13).Alikuwa anawaficha mbali na nani? Hii ilikuwa ishara ya mapumziko ya usafi pamoja na matendo ya kidini ya familia yake mpya iliyokua kutoka Harani.

◙**"chini ya mwaloni"** "Mwaloni" ni fasiri kutoka Tafsiri ya Agano la kale la Kiyunani (kama vile Peshitta; angalia dokezo katika UBS, *Fauna andFlora of the Bible*, ukurasa wa 154-155). Kiebrania kina*terebinth* (BDB 18).Miti

inaonekana kuwa ilikuwa na umuhimu mkubwa sana katika Agano la Kale, mara kwa mara ikihusiuanishwa na maeneo matakatifu (kama vile Mwanzo, 12:6; 13:18; 14:13; 18:1; Kumbu. 11:30;Yosh. 24:26; Waamuzi. 9:6,37).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA) 35:5-8**
**[5]Wakashika njia, hofu ya Mungu ikaishika miji iliyowazunguka, wala hawakuwafuata wana wa Yakobo. [6]Basi Yakobo akafika Luzu, ulio katika nchi ya Kanaani, ndio Betheli, yeye na watu wote waliokuwa pamoja naye. [7]Akajenga huko madhabahu, akapaita mahali pale, El-Betheli; kwa sababu huko Mungu alimtokea, hapo alipomkimbia ndugu yake. [8] Akafa Debora mlezi wa Rebeka, akazikwa chini ya Betheli, chini ya mwaloni; na jina lake likaitwa Alon-bakuthi.**

**35:5 "hofu ya Mungu ikaishika miji iliyowazunguka"** Mzizi wa msingi wa neno"hofu" ni חת;( (BDB 369, K 363, kama vile 9:2; Ayubu 41:25); pia חתת( katika Ayubu 6:21. Mzizi wa msingi wa konsonanti mbili unamaanisha "kuvunja vunja" (kama vile I Sam. 2:4) au"kuvunjika moyo" (kama vile Yer. 10:2; 46:5). Muundo katika mstari huu ni חתח na inatokea hapa tu.
Japokuwa neno halitumiki katika maandiko ya Ushindi inaonekana kuashiria kitu fulani cha taswira ya"vita vitakatifu" (kifasihi "hofu ya Mungu," kama vile Kutoka 15:16; 23:27; Yosh. 10:10). Katika Mashariki ya Karibu ya Kale ya Kampeni za kijeshi zilifanywa katika jina la uungu wa taifa (kama vile Mwanzo 34). Mungu alikuwa pamoja na Yakobo katika namna ya kimaalum kwa njia inayotambulikana!

Inawezekana kwamba *elohim* inatumika katika namna ya kuelezea "hofu kuu," kama ilivyo katika 23:6 (kama vile NASB, REB).

**35:6 "Luzu"** Tunajua kutoka Mwanzo 28:19 kwamba Mungu alikutana naYHWH nje tu ya mji wa Kikanaani na akapataja mahali pale kuwa "Betheli." Kipindi hiki chote hiki cha Wakanaani wangeuita mji huu "Luzu" (BDB 531 II, ikiwa na maana "mti wa mlozi") na Wayahudi wangeuita kwa jina la mahali ambapo Yakobo kwa mara ya kwanza alikutana na YHWH, "Betheli," ikiwa na maana "nyumba ya Mungu" (BDB 110).

**35:7**Angalia dokezo katika 26:25.

◙
**NASB, NRSV** **"El-Betheli"**
**NKJV, NJB**
**JPSOA** **"El-Betheli"**
**TEV** **"Mungu wa Betheli"**

Mababa wa imani walitoa majina ya sehemu ambazo walitokewa na Mungu. Eneo hili karibu na Luzu ilikuwa mahali ambapo YHWH kwa mara ya kwanza alikutana na Yakobo. Analikumbuka vizuri sana! Hivyo analiita tena jina "*El*wa nyumba ya *El*" (Betheli) kwasababu ya malaika (kama vile Ayubu 1:6; Zab. 8:5 au rejea kwa baraza la kimalaika, kama vile Mwanzo 1:26; I Wafalme. 22:19) ascending and descending and YHWH wakipanda na kushuka na YHWH akiwa amesimama juu/pembeni ya ngazi.

◙**"Mungu alimtokea"** Jina kwa ajili ya "Mungu" ni*Elohim*, ambalo ni WINGI. Mara nyingi wakati jina linapotumika juu ya Mungu mmoja na KITENZI ni UMOJA, lakini hapa ni WINGI (BDB 162, KB 191, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU yenye WINGI). Hii inaweza kuwa (ABD, vol. 1, ukurasa wa 270) kwasababu ya Mwanzo 28:12*Elohim* linatumika katika muunganiko pamoja na malaika wa Mungu. Kutokea huku kwa *Elohim* na WINGI wa KITENZI ni nadra.
Inawezekana pia kwamba NJEO YA WAKATI TIMILIFU na KITENZI chenye WINGI kinaashiria ufunuo kamili.

**35:8 "Akafa Debora mlezi wa Rebeka"** Maelezo haya yanaashiria ushuhuda wa macho/chanzo cha kisasa! Debora alikuwa mtumishi mwaminifu sana kutokea Mwanzo 24:59. Anaweza kuwa alikuwa mwenye umri mkubwa sana. Tambua kwamba anazikwa chini (BDB 1065) ya mwaloni; tena eneo lililo takatifu.Jina la sehemu liliitwa "mwalononi wa maombolezo" (BDB 47 and 113).

◙**"chini. . .chini ya"** Maneno haya (BDB 1065) yanahitajika kuelezewa kwasababu ya utata wao katika lugha ya kingereza.

1. chini Betheli, inaashiria sehemu ya chini ya kiurefu kuliko madhabahu yenyewe
2. chini, inamaanisha chini ya matawi, sio chini ya shina

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:9-15**
**[9]Mungu akamtokea Yakobo tena, aliporudi kutoka Padan-aramu akambariki. [10]Mungu akamwambia, Jina lako ni Yakobo; hutaitwa tena Yakobo, lakini Israeli litakuwa jina lako. Akamwita jina lake, Israeli. [11]Mungu akamwambia, Mimi ni Mungu Mwenyezi, uzidi ukaongezeke. Taifa na kundi la mataifa watatoka kwako, na wafalme watatoka viunoni mwako. [12]Na nchi hii niliyowapa Ibrahimu na Isaka nitakupa wewe, na uzao wako baada yako nitawapa nchi hiyo. [13]Mungu akakwea juu kutoka kwake mahali hapo aliposema naye. [14]Yakobo akasimamisha nguzo mahali aliposema naye, nguzo ya mawe, akamimina juu yake sadaka ya kinywaji, akamimina mafuta juu yake. [15]Yakobo akapaita mahali pale, Mungu aliposema naye, Betheli.**

**35:9-12** Huku kufanywa upya kwa agano na kujitoa kunafanana sana na Mwanzo 28:13-15. Muda wa kukutana huku na Mungu hakuko wazi sana. Inaonekana kama kurejeshwa nyuma sana katika 32:28-32 au YHWH kuthibitishwa upya kwa mabadiliko ya jina kutoka Yakobo kwenda Israeli.

**35:10 "Yakobo. . .Israeli"** Toleo la NASB linafasiri mstari wa 10 na mistari ya 11-12 kama ushairi. Hii inashabihiana na marudio ya mstari wa 10 na inaufanano wa ushairi wa udhihirisho wa Mungu wa Mwanzo 12:1-3; 15:1; na 17:1-5.

Inashangaza kwamba hatuna uhakika kwa habari ya maana (asili) ya jina "Israeli" Angalia Mada Maalum katika 32:28.

**35:11 "Mimi ni Mungu mwenye nguvu"** Hii ni ambatani ya kiebrania*El Shaddai* (BDB 42 na 994). Tunajifunza kutokea Kutoka 6:2-3 kwamba ilikuwa jina lililozoeleka katika Mwanzo (kama vile17:1; 28:3; 35:11; 43:14; 48:3). Inaonekana kuuundwa na neno *El* (BDB 42), ambalo ni jinala jumla kwa Mungu katika Mashariki ya Karibu ya kale, yawezekana kutoka katika mzizi kwa ajili ya "kuwa imara" au "mwenye nguvu," na neno*Shaddai* (שדי, BDB 994), ambalo limeunganishwa na matiti ya mwanamke (BDB 994, kama vile Mwanzo 49:25). Fasiri nyingine inayowezekana ni ile "Mwenye utoshelevu wote" au ile ya walimu wa Kiyahudi "mwenye kujitosheleza mwenyewe," ingawa katika Hes. 24:4,16, inafasiriwa na toleo la NASB kama "mwenye uweza wote." Linatumika mara kwa mara katika vyanzo visivyo vya Ki-Isaeli kama vile Ayubu na Balaamu. Cheo hiki mara kwa mara kinaunganishwa na Baraka za Mungu (kama vile Mwanzo. 17:1; 28:3; 35:11; 48:3-4). Angalia Mada maalumu katika 12:1.
Katika Kumb. 32:17 Mzizi unaofanana (שד, BDB 993) inafasiriwa kama "pepo" (neno la kukopwa kutoka lugha ya kishamu).

◙**"Zaeni Mkaongezeke"** Angalia madokezo katika 17:1 na 28:3. Hii imekuwa mamlaka ya Mungu kutokea Mwanzo 1 (kwa wanyama, wanadamu, na sasa kwa familia yake maalumu ya kiagano).

◙**"Taifa na kundi la mataifa"** Kidhahiri hii inarejerea uzao wa Yakobo (kama vile 48:4), lakini pia kwa kundi kubwa pana (yaani "wale walioumbwa kwa sura na mfano wa Mungu," Mwanzo 1:26-27).

1. Ahadi za Mungu za Mwanzo. 3:15
2. Maana ya wito wa Mungu kwa Ibrahimu katika Mwanzo. 12:3

3. Vyeo vya Mungu kwa Waisraeli na kusudi lake katika Kutoka. 19:5-6
4. Maana ya jumla ya Isaya ya "mataifa" kuhusuishwa
5. Maneno ya mwisho ya Yesu kwa kanisa katika Mt. 28:19-20 na kurudiwa katika Luka 24:47 na Mdo. 1:8
6. Mahubiri katika Mdo na barua za Paulo
7. Maelezo yaliyowazi ya Wagalatia 3 na kitabu cha Waebrania kuhusu kusudi la Agano la Kale

Tungo hii ni ya maelezo ya kupunguza nguvu ya kimakusudi yenye umuhimu mkubwa wa kithiolojia!

◙**"kwako watatoka wafalme"** Tungo hii inaweza kuonekana katika namna mbili.
1. usambamba wa kifasihi "kundi la mataifa"
2. njia ya kumaanisha kwenye agano na Ibrahimu (kama vile 17:6,16)

Yakobo ni kianzilishi cha "makabila," lakini Ibrahimu mwanzilishi wa "wafalme."

**35:12** Huu ni uthibitisho mpya wa ahadi ya awali (kama vile 13:15; 26:3; 28:13). Ahadi hizi za YHWH zilikuwa kwa ajili ya familia na mfuatano wa vizazi! Baadhi walikuwa wenye nguvu na wenye rohoni zaidi ya wengine.Hii haikuwa ahadi kwa "wapendwao sana," bali ahadi ya kutimiza kusudi la ukombozi la milele la Mungu wa uumbaji ambao katika sura yake wanadamu wote wameumbwa (kama vile Mwanzo 1:26-27)! Ni ahadi ya uanadamu ulioanguka (kama vile Mwanzo 3:15) kuwakomboa wao! Mungu alimchagua mmoja ili awe amechagua wote!

**35:13 "Mungu akakwea juu kutoka kwake"** KITENZI "kwenda juu" (BDB 748, KB 828) kina upana mkubwa wa kimaana ("nenda juu," "kupaa," "kupanda," "kuchomoza," "kudhabihu," "kurudi," "kusindikiza," na mengineyo. Hii hapa ni maelezo ya mtawanyiko wa Mungu kumuacha mtu (kama vile 17:22). Watu wa kale waliamini Mungu na mbingu vilikuwa"juu" na hukumu "chini." Moshi wa dhabihu ulipanda juu kwa Mungu (kama vile 8:20; 22:2,13). Mungu alizungungumza kutokea kwenye mlima/mbinguni (kama vile Kutoka 19-20). Malaika wa Mungu walipaa na kushuka katika 28:12.

Sasa kwamba watu wa sasa wanajua juu ya ukuu wa uumbaji wa mwilini, wafasiri wengi wanaamini kwamba njia bora ya kumaanisha sehemu ya Mungu ni kati ya kivipimo kuliko kuelea angani. Mbingu kimsingi ni mtu/nafsi, sehemu sio jambo la umuhimu kabisa.

◙**"mahali pale alipokuwa amezungumza naye"** Hii tungo kwa hakika inarudiwa katika mstari wa 14. Hii ni aina ya marudio ambayo yanaonekana kama makosa ya kawaida ya kiuandishi (mbinu ya kiuandishi ya kurudia rudia).

**35:14 "Yakobo akaweka nguzo"** Hiki ndicho alichokifanya kwa asili pale Betheli (kama vile Mwanzo28:18, 19, 22). Pia tambua kwamba katika mstari wa 20 wa sura hii atainua nguzo juu ya kaburi la Raheli. Nguzo hizi ziliashiria sehemu ya matukio muhimu.

◙**"akamimina. . .alimimina"** Kuna VITENZI viwili tofauti vilivyotumika.
1. cha kwanza, BDB 650, KB 703, *Hiphil* kauli ya wakati usiotimilifu, inamaanisha sadaka ya kinywaji (BDB 651)
2. ya pili, BDB 427, KB 428, *Qal* kauli ya wakati usio timilifu, ikimaanisha mafuta ya mzeituni (BDB 1032, kama vile 28:18) ikitumika, Kutoka 29:7; Mambo ya Walawi 8:12

**35:15** Yakobo kutoa majina kwa eneo hili la ufunuo linawekwa katika kumbukumbu mara tatu. Baadhi wanaona hili kama waandishi tofauti (J.E.D.P.), lakini nafikiri ni sawasawa na kumbukumbu kuongoka kwa Paulo mara tyatu katika Matendo ya Mitume. Ilikuwa tukio kubwa la kithiolojia. YHWH alijifunua mwenyewe kwa Yakobo/Israeli!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:16-21**
**16Wakasafiri kutoka Betheli, hata ukabaki mwendo wa kitambo tu kufika Efrathi, Raheli akashikwa na utungu**

**wa kuzaa, na utungu wake ulikuwa mzito. [17]Ikawa alipokuwa anashikwa sana na utungu, mzalisha akamwambia, Usiogope, maana sasa utamzaa mwanamume mwingine. [18]Ikawa hapo katika kutoa roho yake, maana alikufa, akamwita jina lake Benoni, lakini babaye alimwita Benyamini. [19]Akafa Raheli, akazikwa katika njia ya Efrathi, ndio Bethlehemu. [20]Yakobo akasimamisha nguzo juu ya kaburi lake, ndiyo nguzo ya kaburi la Raheli hata leo. [21]Kisha akasafiri Israeli akapiga hema yake upande wa pili wa mnara wa Ederi.**

**35:16 "Efrathi"** Hii ni njia nyingine ya kuelezea Bethlehemu katika Yuda (kama vile Mika 5:2). Kulikuwa na Bethlehemu nyingine, lakini Efrathi ilikuwa njia ya kuashiria mtuatakayewekwa karibu na Yerusalemu, ambao baadaye utakuwa jiji la Daudi, eneo la kuzaliwa kwa Masihi.

◙**"na utungu wake ulikuwa mzito"** KITENZI hiki (BDB 904, KB 1151) katika shina*Piel* kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale.
Familia iliyochaguliwa iliteseka na ilikuwa na magonjwa (kama vile 27:1) kama watu wale wengine waliathiriwa na anguko. Mungu huingilia kati kuweka uhakika wa kuishi kwao, lakini sio faraja yao na urahisi (angalia Gordon Fee, *The Disease of the Health, Wealth Gospel*).

**35:17 "usiogope"** KITENZI (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI) hii kwa namna Fulani inashangaza. Mtu angeweza kufikiri alikuwa anafikiria juu ya kifo chake mwenyewe, lakini katika muktadha kuzaa kiafya kwa mwanawe wa kiume kulikuwa ndiyo kipaumbele (kama vile I Sam. 4:20). Hii inaonekana kutimiliza ombi alilotoa kwa Mungu katika 30:24.

**35:18 "katika kutoa roho yake"** "nafsi" ni neno la Kiebrania *nephish* (BDB 659). Lazima tuwe makini kwamba tusichanganye Falsafa ya Kiyunani pamoja na Maandiko ya Kiebrania. Agano la Kale halisemi kwamba tunayo nafsi lakini linasema sisi ni nafsi (kama vile Mwanzo Gen. 2:7). Neno "nafsi" linatoka katika neno la ki-Akkadia *napishtu*, ambalo linaashiria sehemu ya kupumulia au koromeo (kama vile Zaburi 69:2). Upekee wa kibinadamu haupo katika ukweli kwamba wana *nephish*, kwa maana katika sehemu za mwanzo za Mwanzo za sehemu ya Mwanzo wanyama pia walikuwa na *nephish* (kama vile 1:21, 24; 2:19; Law. 11:46; 24:18). Hii ni nahau ya Kiebrania tu ambayo kwamba maisha ya kimwili ya mtu duniani yanaisha pale pumzi inapokata.

◙**"akamwita jina lake Benoni, lakini babaye alimwita Benyamini"** Jina lake analopewa na Rebeka lilimaanisha "mwana wa huzuni" (BDB 122), hata hivyo Yakobo alilibadilisha kuwa "mwana wa mkono wangu wa kulia" (BDB 122). Hii ilikuwa sehemu ya ujuzi, heshima, na msaada. Tunajifunza kutoka katika mabamba ya vibao vya maandiko vya Mari "mwana wa kusini" (yaani mahali pa kuzaliwa, Kanaani).

**35:19 "(ndio Bethlehemu)"** Hapa yawezekana kulikuwa na kuingizwa kwa baadaye kwa uhariri wa kiuandishi (majina ya maeneo 35:6,27; 36:1 na tungo "mpaka leo hii" katika 35:20). Japokuwa mimi binafsi nashikilia kwenye uandishi wa Musa kwa sehemu kubwa ya Torati, lakini pia naamini kuna mikono mingine ya kiuandishi kadhaa kama ilivyo pia masimulizi ya njia ya mdomo na yaliyoandikwa kutoka kwa mababa wa imani ambayo yalitumiwa na Musa. Wahariri wengine yawezekana kuwa walijumuishwa: Yoshua, Samweli, mwandishi wa kitabu cha Wafalme, Ezra, Yeremia, na/au makuhani.

**35:21 "mnara wa Ederi"** Jina lake ni "Migdali-ederi." Migdali (BDB 153) ikimaanisha mnara na inatumika katika muunganiko na maeneo kadhaa (yaani Yosh. 15:37; 19:38). Hii hapa ipo karibu na Bethlehemu (kama vile Mika 4:8). Ederi (BDB 727) ikimaanisha mifugo au kundi la mifugo. Hili lundo la mawe lililoinuliwa lingetumika kama sehemu nzuri ya kutazamia katika kulinda kundi la mifugo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:22a**
**[22]Ikawa Israeli alipokuwa akikaa katika nchi ile, Reubeni akaenda akalala na Bilha, suria wa babaye;**

**35:22 "Reubeni akaenda akalala na Bilha, suria wa babaye"** Hili tendo kama lisiloonekana sawa ni kwa namna Fulani linahusiana na mategemeo ya haki za kurithi (yaani I Wafalme 2:13-25). Rubeni alikuwa anajaribu kumlazimisha mkono wa babaye katika kumtaja kama kiongozi wa ukoo. Kama ilivyotokea, alishutumiwa na kukataliwa kwasababu ya tukio hili (kama vile Mwanzo 49:3-4; I Nyakati. 5:1). Kama vile Mungu alivyokuwa amefanya kazi mapenzi yake ya kipekee kupitia wanawake tasa wa mababa wa imani, katika Mwanzo aoneshe mapenzi yake ya kipekee kwa kumruhusu mtoto wa kiume wa Lea kuwa katika uuzao wa Masihi (yaani Yuda).

◙**"Israeli akasikia"** Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, "jambo hili lililonekana kumtia huzuni mbele yake" (kama vile matoleo ya TEV, NAB). Hii haitokei katika MT. Hatuna uhakika ikiwa tafsiri ya LXX ililiongezea au ilikuwa ni sehemu ya mwanzoni mwa maandiko ya Kiebrania.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:22b-26**
**[22b]Israeli akasikia habari. Basi hao wana wa Yakobo walikuwa kumi na wawili. [23]Wana wa Lea ni Reubeni, mzaliwa wa kwanza wa Yakobo, na Simeoni, na Lawi, na Yuda, na Isakari, na Zabuloni. [24]Wana wa Raheli, ni Yusufu na Benyamini. [25]Wana wa Bilha, kijakazi wa Raheli, ni Dani na Naftali. [26]Wana wa Zilpa, kijakazi wa Lea, ni Gadi na Asheri. Hawa ndio wana wa Yakobo aliozaliwa katika Padan-aramu.**

◙**"Basi hao wana wa Yakobo walikuwa kumi na wawili"** Asili maarufu inayohusiana na majina haya pia yanasaidia baadhi ya uelewa kwamba inaweza kutambuliwa katika nabaa za Mwanzo 49.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:27**
**[27]Yakobo akaja kwa Isaka, babaye, huko Mamre, mji wa Arba, ndio Hebroni, walipokaa ugenini Ibrahimu na Isaka.**

**35:27 "Yakobo akaja kwa Isaka, babaye, huko Mamre"** Hili lilikuwa eneo lingine la mwaloni (kama vile Mwanzo 13:18; 14:13; na 18:1). Kipengele cha muda hakijulikani. Je Yakobo alisubiri wakati wote huu baada ya kurudi Kanaani kumtembelea baba yake?! Hii yawezekana ni mbinu ya kurejea nyuma kwa matukio ya kihistoria.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:28-29**
**[28]Siku za Isaka zilikuwa miaka mia na themanini. [29]Naye Isaka akakata roho, akafa, akakusanyika kwa watu wake, ni mzee, ameshiba siku. Esau na Yakobo, wanawe, wakamzika**

**35:29"Isaka akakata roho, akafa"** Isaka lazima alikuwa ameishi muda mrefu katika hali ngumu ya kuteketea (kama vile 27:1). Yakobo alikuwa ameondoka zaidi ya miaka ishirini na baba yake alikuwa ametegemea kufa muda mfupi baada yay eye kuondoka. Hii inaonesha kuwamba japokuwa Mababa wa Imani walikuwa na Baraka za Mungu, lakini bado alikuwa amepitia hali mbaya na udhaifu mwingi wa kimwili na magonjwa kwa muda mrefu wa maisha yake.

◙**"Esau na Yakobo, wanawe, wakamzika"** Kama vile Ishmaeli na Isaka walivyolazimika kurudi kumzika Ibrahimu hivyo pia watoto hawa wa kiume Esau na Yakobo walikuwa pamoja kwa ajili ya maziko ya baba yao. Hii inavyoonekana ilikuwa tukio la muhimu la kiutamaduni.

◙**"akakusanyika kwa watu wake,"** KITENZI (BDB 62, KB 74, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ikimaanisha "kukusanya" au "kuondoa." ni nahau kwa kuunganishwa na familia ya watu tuliowapenda baada ya kifo (yaani 25:8,17; 35:29; 49:29,33; Hes. 20:24,26; 27:13; 31:2; Kumb. 32:50). Ufunuo wa Agano la Kale kuhusu maisha baada ya kifo ni kwa muhtasari na umejaa utata (isipokuwa kwa sehemu kadhaa katika Ayubu na Zaburi juu ya ufufuo).

Inaweza kuashiria

1. nahau kwa ajili ya kifo cha amani
2. nahau kwa ajili ya maziko katika kaburi la familia
3. nahau kwa kuunganishwa na wapendwa wetu waliokufa(yaani ukiri wa uwepo binafsi baada ya kifo). Angalia *Hard Sayings of the Bible*, ukurasa wa 127-129.
4. nahau ya kusubiri waliokufa tuliowapenda mpaka hapo Mungu atakapowafufua katika wafu (kama vile Ayubu 14:14-15; 19:25-27; Zab. 16:10; 49:15; 86:13; Ezekiel 37; Dan. 12:2-3; Hosea 13:14). Andiko kamilifu la Agano Jipya lingekuwa 1 Wakorintho 15.

**35:29 "ni mzee, ameshiba siku"** Hii ni nahau ya maisha marefu. Kifo kilichukuliwa kama mwisho wa asili wa maisha ya kiubinadamu. Maisha marefu yalichukuliwa kama baraka. Kifo kilikuwa ni rafiki kwa waamini wazee (na bado iko hivyo)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yakobo alisafiri tu mpaka Shekemu na hakwenda mpaka Betheli?
2. Wahivi ni watu gani?
3. Je uzinzi siku zote lilikuwa kosa baya zaidi au hiyo ilianza na utungwaji wa sheria ya Musa?
4. Kwanini Rubeni, Simeoni na Lawi walikataliwa kuwa viongozi mababa wa kifamilia?
5. Yakobo anamaanisha miungu gani ya kigeni katika 35:2?
6. Je pete za masikioni zinawakilisha nini katika 35:4?
7. Kwanini miti ilichukuliwa kuwa maeneo matakatifu kwa wakazi hawa wa kuhamahama wa jangwani?
8. Kwanini Yakobo aliinua nguzo katika maeneo maalumu nanyakati katika maisha yake? Kwanini hili baadaye linashutumiwa?
9. Je sisi tunayo nafsi au sisi ni nafsi? Kwanini?

# MWANZO 36

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Esau ahama | Familia ya Esau | Orodha ya Waedomu | Kizazi cha Esau | Wake na watoto wa Esau huko Kaanani |
| 36:1 | 36:1-8 | 36:1-5 | 36:1-5 | 36:1-5 |
| 36:2-5 | | | | Kuhama kwa Esau |
| 36:6-8 | | 36:6-8 | 36:6-8 | 36:6-8 |
| Kizazi cha Esau | | | | Kizazi cha Esau huko Seiri |
| 36:9-14 | 36:9-14 | 36:9-14 | 36:9-13a | 36:9 |
| | | | | 36:10 |
| | | | | 36:11-12 |
| | | | 36:13b | 36:13 |
| | | | 36:14 | 36:14 |
| | Machifu wa Edomu | | | Watemi wa Edomu |
| 36:15-19 | 36:15-16 | 36:15-19 | 36:15-16 | 36:15-16 |
| | 36:17 | | 36:17 | 36:17 |
| | 36:18-19 | | 36:18-19 | 36:18 |
| | | | | 36:19 |
| | Wana wa Seiri | | Kizazi cha Seiri | Kizazi cha Seiri ambao ni Wahori |
| 36:20-30 | 36:20-30 | 36:20-30 | 36:20-21 | 36:20-28 |
| | | | 36:22 | |
| | | | 36:23 | |
| | | | 36:24-26 | |
| | | | 36:27 | |
| | | | 36:28 | |
| | | | 36:29-30 | 36:29-30 |
| | Wafalme wa Edomu | | Wafalme wa Edomu | Wafalme wa Edomu |
| 36:31-39 | 36:31-39 | 36:31-39 | 36:31-39 | 36:31-39 |
| | Machifu wa Esau | | | Watemi wa Edomu |
| 36:40-43 | 36:40-43 | 36:40-43 | 36:40-43 | 36:40-37:1 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (**angalia ukurasa wa xxiv**)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## KUJIFUNZA HISTORIA YA NYUMA - Uhusiano wa Israel na kizazi cha Esau (yaani Edomu)

A. Israeli ilihitaji kuwa na urafiki maalum dhidi ya Edomu kwa vile walihusiana
   1. Hesabu 20:14
   2. Kumb. 23:7,8
B. Kuna matatizo mengi kati ya Israel na Edomu kwa muda wa miaka mingi
   1. Hesabu 20:14-21
   2. Waamuzi 11:16-17
   3. I Samuel 14:47-48
   4. II Samuel 8:14
   5. I Wafalme 11:14-25
   6. II Wafalme 14:22; 16:5, 6
   7. II Nyakati 20:10-30; 21:8-15
   8. Amos 1:6, 9

C. Kuna nabii mbalimbali zilizo kinyume na Edomu
   1. Isaya 34:5 na kuendelea ; 63:1 na kuendelea
   2. Yeremia 49:7-22; Wimbo ulio Bora 4:21, 22
   3. Ezekiel 25:12na kuendelea; 35:1 na kuendelea; 36:2-6
   4. Amos 1:11, 12
   5. Obadia

D. Sura ya 36 ni unasaba wa Esau, ambao unaonekana kuaksi unabii wa Mwa. 27:39-40. Ni dhahiri toka kwenye kifungu kinachojirudia ("hizi ndio kumbukumbu za vizazi vya. . .") kinachopatikana katika 36:1 kwamba Musa alitumia hawa wahusika wa Agano la Kale kama njia ya ya kuigawa habari yake (yaani., Mwanzo) ya mwanzo wa watu wa Kiebrania (kama vile 2:4; 5:1; 6:9; 10:1; 11:10,27; 25:12, 9; 36:1,9; 37:2). Wale wote walio sehemu ya ukoo wa Kimasihi hupokea nafasi zaidi na usikivu.

E. Maelezo sahihi ya sura hii yangaliweza kuwa
   1. Mistari ya 2-9 ni kuhusu watoto wa Esau huko Kaanani
   2. Mistari ya 10-14 ni kuhusu wajukuu wa Esau huko Seiri
   3. Mistari ya 15-19 na 40-43 ni kuhusu watemi wa taifa la Edomu
   4. Mistari ya 20-30 inaorodhesha watawala wazawa katika eneo hili
   5. Mistari ya 31-39 ni wafalme wa baadaye wa Edomu (orodha mfanano inatokea katika I Nya. 1:35-54)
   6. Mistari ya 40-43 ni majina ya uzao wa machifu toka kwa Esau

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:1**
**[1]Hivi ndivyo vizazi vya Esau, ndiye Edomu.**

**36:1 "hivi ndivyo vizazi vya"** Kifungu hiki chenye kujirudia (yumkini ni wasifu wa mwandishi) inatia alama mgawanyo wa kitabu cha Mwanzo (kama vile 2:4; 5:1; 6:9; 10:1; 11:10, 27; 25:12, 19; 36:1, 9; 37:2). Hakuna KITENZI katika kifungu hiki.

◙ **"Esau (ndiye, Edomu)"** Msisitizo huu juu ya asili ya watu wa Edomu unahusiana huko nyuma na nduguye Yakobo, Esau, ni mada inayojirudia katika sura hii nzima (kama vile 8, 9, 19, 43. Uhusiano wa Esau na Edomu unaelezewa hasa hasa katika Mwanzo 25:25, 30).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:2-5**
**[2] Esau alitwaa binti za Kanaani, kuwa wakeze; Ada, binti Eloni, Mhiti, na Oholibama, binti Ana, binti Sibeoni, Mhivi; [3] na Basemathi, binti Ishmaeli, nduguye Nebayothi. [4] Ada akamzalia Esau Elifazi; na Basemathi alizaa Reueli. [5] Oholibama alizaa Yeushi, na Yalamu, na Kora. Hao ndio wana wa Esau aliozaliwa katika nchi ya Kanaani.**

**36:2 "Esau alitwaa binti za Kaanani, kuwa wakeze"** Majina ya wake wa Esau ambao ni Wakaanani yameandikwa katika sehemu tatu tofauti: Mwa. 26:34, 35; 28:8; na 36:2 na kuendelea. Hata hivyo, tatizo linajitokeza pale habari hii inapotofautiana juu ya majina ya hawa wakeze. Utofauti huu umeelezewa katika njia tofauti : (1) kwamba hawakuwa wake watatu, bali wane na (2) kwamba hawa wanawake walikuwa na majina zaidi ya moja. Inaonekana wazi toka katika andiko kuwa Esau kwa kiasi Fulani alikuwa na wake wawili toka Kaanani na binti mmoja wa Ishimaeli.

◙ **"Ada, binti Eloni, Mhiti"** Katika Mwa. 26:34 binti Elono, Mhiti anaitwa Basemathi (BDB 142). Inaonekana ni kitu kisicho cha kawaida kuwa jina kama lile lile linatumika kwa binti wa Ishmaeli katika Mwanzo. 36:3. Rashi anasema kuwa hili lingeweza kuwa ni jina lililozoeleka kwa wanawake kwa vile inawezekana linahusiana na neno kwa ajili ya vitu vyenye kutoa manukato (BDB 141). Utamaduni wa Kiyahudi wenye kuwa na upendelea dhidi ya Esau unathibitisha kuwa jina lake linahusiana na ubani ulichomwa kwenye ibada za sanamu, kwa hiyo, na kumfanya kuwa mtu anayeabudu sanamu.

Neno "Wahiti" (BDB 366) limetumika katika makundi matatu tofauti kwenye Agano la Kale

1. Wakazi wa mwanzo wa Asia ndogo ya kati iliyoitwa Wahatia (yaani waliongea kihati) katika karne ya tatu K.K. Hawakuwa Wasemiti wala wapiga mieleka wa huko Ulaya.
2. Wapiga mieleka wa ulaya walivamia katika karne ya pili K.K. waliotengeneza ngome imara.
3. Uzao wa Hethi (Mwanzo 10:15; 23:3,5,7,10,16,20; 25:10; 27:46; 49:32). Wameorodheshwa kama moja ya makabila kumi yaliyokaa huko Kaanani.

Uandikaji wa makundi matatu tofauti kwa kutumia jina moja ulisababisha mkanganyiko mkubwa.

◙ **"Oholibama"** Jina hili linamaanisha "hema la juu" (BDB 14), hata hivyo, majina haya yote yanajadilika kama ilivyo uhusiano wake kiasili. Mzizi ule ule wa neno unaweza kumaanisha "mti," "mshubiri,""ng'aa" au "kuwa safi."Toka Mwanzo 26:34-35 binti yule yule inavyoonekana aliitwa Yudithi (kama Esau alikuwa na wake watatu). Rashi anasema kuwa Esau alibadili jina lake na kumwita Yudithi (BDB 397 II), pale aliposema jina linamaanisha "Myahudi"(KIVUMISHI, BDB 397 I). Hii inaonyesha kuwa aliachana na ibada zake za sanamu na kwa hiyo, amufurahishe babaye (yaani Isaka). Si kitu cha kawaida kwa jina lile lile kuonekana tena katika mstari wa 41 wa sura ile ile kumaanisha mtu. Bado liko katika muundo wa JINSI YA KIKE, kitu ambacho kinaonyesha kuwa pamekuwepo na mwingiliano wa neno la Kiebrania katika sura hii. Utofauti wa unasaba ni wa kawaida katika Biblia kwa sababu ya (1) ugumu wa kuweka kumbukumbu ya majina marefu pasipo kukosea herufi na (2) ugumu

wa kuyaandika majina toka lugha moja hadi nyingine. Tambua namna majina yanavyobadilika katika 1 Nya. 1:35-54.

◙ **"binti Sibeoni, Mhivi"** Andiko la Kimasoreti lina neno "binti wa," hata hivyo, fasihi ya Kisamaria., tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania, na tafasiri ya Kishami ina neno "mwana."ni wazi kutoka kwenye muktadha na mstari wa 24 kuwa tunaongea kuhusu binti.

Sibeoni anaitwa Mhivi. Kama hili ni kweli kwamba huyu binti anahusiana na yule aliyeandikwa katika sura yenye kuhusiana na Mhiti (BDB 366), Mhivi (BDB 295), na Mhori (BDB 360 II, kama vile mst. 20; 14:6). Mara zote neno "Wahori"(kama vile mst. 20) linatumika kwa ajili ya wale Wahori wasio Wasemiti (ZPBE, juzuu ya 3, kur. Za 228-229), lakini inavyoonekana neno linaweza kumaanisha kundi la Wasemiti ambao walikuwa wachimba madini au watu walioishi kwenye mapango (BDB 359, KB 339, shimo"). Ushahidi wa hili ni kuwa majina yao yote ni ya Kisemiti, na sio ya Kihori.

**36:3"Basemathi"** Binti anaitwa "Mahalathi," lenye kumaanisha "kusamehe" (BDB 142) katika Mwa. 28:9. Inafurahisha kuona kuwa katika torati ya Kisamaria jina lake linabadilika toka Basemathi (Mwa. 36:3,4,10) kwenda Mahalathi. Hii inaonyesha kwamba, mwanzoni kabisa, wasomi walitambua matatizo ya haya majina (yaani., mtu anakuwa na majina mawili, jina maarufu, mbadala wa majina). Yapaswa ikumbukwe kuwa Esau alimwoa mmoja wa binti wa Ishmaeli ili amufuarahishe babaye na mamaye.

◙ **"nduguye Neyabothi"** Inadhaniwa kuwa Ishmaeli alikuwa amekufa katika kipindi hiki na kwamba nduguye alisimama katika nafasi yake kumwoza mbali na hii ndiyo sababu ya jina lake kujumuishwa kwenye andiko. Pia inawezekana, kwa sababu hili linatokea mara nyingi (yaani., ndugu wa kiume anasimama kama mwakilishi wa masuala ya familia , Labani, Simeoni/Lawi, hata Abramu anadai kuwa nduguye na Sarai), kwamba hili laweza kuaksi tamaduni za Mashariki ya Karibu ya Kale. Baadhi wamedhani ni kwa sababu ya umuliki wa majina ya kike katika unasaba huu kuwa kulikuwa na tabia ya uwepo wa muundo wa utawala wa mwanamke katika jamii katika kabila hizi za Kiarabu, lakini katika hoja hii uwekaji wa kumbukumbu za kihistoria haujulikani.

**36:4-5** Hii ni orodha ya baadhi ya makabila makuu ya Esau ambayo baadaye yaliendelea kuwemo katika orodha ya watemi katika sura hii. Sura hii inaweza kugawika ikisimamia juu ya dhima ya huu unasaba.

1. mst. 2-9 ni watoto wa Esau huko Kaanani
2. mst. 10-14 ni wajukuu wa Esau huko Seiri
3. mst. 15-19 na 40-43 ni watemi wa taifa la Edomu
4. mst. 20-30 unaorodhesha watawala wazawa kwenye eneo hilo
5. mst. 31-39 tawala wa baadaye wa Edomu
6. mst. 40-43 ni majina ya machifu wa uzao wa Esau

Orodha mfanano inaonekana katika 1 Nya.1:35-54.

**36:5 "Kora"** Kiwastani nimechagua moja ya majina yanayotumika kwa nyakati mbili tofauti ili kuonyesha tatizo la uelewa halisi wa uhusiano ulioelezewa katika unasaba huu. Inadaiwa na baadhi kuwa kuna majina tofauti ya "Kora" yaliyoorodheshwa; moja hapa katika mst. 5 na jingine katika mst. 16. Rashi anasema kuwa yanahusiana kwa maelezo kwamba mtu yule yule ndiye alimchukua mke wa babaye. Hii inaonyesha upendeleo wa Wayahudi dhidi ya Esau. Tafsiri ya waalimu wa dini ya Kiyahudi wa sura hii ni kinyume na inadhaniwa kujamiiana kusiko elezeka kwa watu walio karibu kuoana na matatizo ya familia katika uzao wa Esau. Hili laweza kuwa kweli, lakini halikuelezewa kwenye andiko na uelewa ulio kinyume unaweza kufikiwa tu kwa madhanio yaliyo na upendeleo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:6-8**
**[6] Esau akawatwaa wakeze, na wanawe, na binti zake, na watu wote wa nyumbani mwake, na ng'ombe zake, na wanyama wake wote, na mali yake yote, aliyoyapata katika nchi ya Kanaani; akaenda mpaka nchi iliyo mbali na Yakobo nduguye. [7] Maana mali yao yalikuwa mengi wasiweze kukaa pamoja, wala haikuweza nchi ya kusafiri kwao kuwachukua, kwa sababu ya wanyama wao. [8] Esau akakaa katika mlima Seiri, Esau ndiye Edomu.**

**36:6 "Esau akawatwaa wakeze, na wanawe. . .na akaenda mpaka nchi iliyo mbali na Yakobo nduguye"** Sababu ya utengano huu umetajwa katika sura ya 36 kama hitaji kwa ajili la malisho zaidi (mst.7). ingawa kithiolojia, inaonekana kuhusianishwa na ukweli kwamba Yakobo ndiye alikuwa mrithi wa kweli (yaani., wa baraka za Isaka)

**36:8 "Esau akakaa katika Mlima Seiri; Esau ndiye Edomu"** Inawezekana kuwa kipindi cha kutokuwepo kwa Yakobo, Esau aliirudisha mifugo yake toka Mlima Seiri hadi Kaanani kwa nyakati tofauti na habari hii inaelezea kuwa alikaa huko Seiri (kama vile 32:3). Hata hivyo, hili halijulikani. Mlima Seiri likajakuwa jina la kimila kwa ajili ya taifa la Edomu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:9-14**
**[9] Hivi ni vizazi vya Esau, baba ya Edomu katika mlima Seiri. [10] Haya ndiyo majina ya wana wa Esau; Elifazi, mwana wa Ada mkewe Esau. Reuli, mwana wa Basemathi, mkewe Esau. [11] Na wana wa Elifazi, ni Temani na Omari, na Sefo, na Gatamu, na Kenazi. [12] Na Timna alikuwa suria wa Elifazi, mwana wa Esau; naye akamzalia Elifazi Amaleki. Hao ndio wana wa Ada, mkewe Esau. [13] Na hawa ni wana wa Reueli, Nahathi, na Zera, na Shama na Miza. Hao walikuwa wana wa Basemathi, mkewe Esau. [14] Na hawa ni wana wa Oholibama, binti Ana, binti Sibeoni, mkewe Esau; akamzalia Esau, Yeushi, na Yalamu, na Kora.**

**36:10 "Haya ndiyo majina ya wana wa Esau"** Ni dhahiri toka kwenye orodha iliyorudiwa ya wana wa Esau kuwa sura hii imegawanyika katika aina mbali mbali tofauti za nayaraka za kiunasaba (angalia kumbukumbu toka aya ya 36:4-5)

**36:11 "wana wa Elifazi"** Kumekuwepo na majadiliano mengi ikiwa huyu ni yule yule Elifazi aliyeko katika kitabu cha Ayubu. Pameonekana kuwepo na kuaminika kwenye hili kwa sababu ya nchi ya Uzi (yaani., mwana aliyeitwa Uzi) ametajwa katika mstari wa 28. Taifa la Edomu lilikuwa maarufu kwa ajili wanajimu, hasa toka kwenye Mji wa Temani. Shuhuda hizi mbili zinailenga Edomu kama nchi ya makaazi ya Ayubu. Ikiwa Elifazi ni yule yule "rafiki" ndiyo haijulikani.

**36:12 "Timna alikuwa suria wa Elifazi . .naye akamzalia Elifazi Amaleki"** Kipekee ameelezewa dhahiri kama suria kwa sababu ni mama wa adui mkubwa wa Mwisraeli aliyeitwa "Amaleki" (kama vile Kut. 17; Kumb. 25:17,19; I Samuel 15). Ilimaanisha kuwa ni maelezo ya kumshushia heshima mtu kwa sababu huyu alikuwa ni mtoto pekee wa suria aliyetajwa katika orodha hii ya unasaba.

**36:14 "hawa ni wana wa Oholibama, mkewe Esau"** Pamekuwepo na majadiliano mengi kwa nini wana wa huyu mwanamke wametajwa pamoja na wajukuu. Baadhi wanasema hii ni kuwarejesha watoto kwenye daraja la wajukuu, yaani kuliko kuleta hoja zenye kuumiza kwa wana wa huyu mwanamke. Yumkini inaelekea kwenye haki za kurithi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:15-19**
**[15] Hawa ndio majumbe wao wana wa Esau; wana wa Elifazi, mzaliwa wa kwanza wa Esau; jumbe Temani, jumbe Omari, jumbe Sefo, jumbe Kenazi, [16] jumbe Kora, jumbe Gatamu, jumbe Amaleki. Hao ndio majumbe, waliotoka kwa Elifazi katika nchi ya Edomu. Hao ni wana wa Ada. [17] Na hawa ni wana wa Reueli, mwanawe Esau; jumbe Nahathi, jumbe Zera, jumbe Shama, jumbe Miza. Hao ndio majumbe waliotoka kwa Reueli katika nchi ya Edomu. Hao ni wana wa Basemathi, mkewe Esau. [18] Na hawa ni wana wa Oholibama, mkewe Esau; jumbe Yeushi, jumbe Yalamu, jumbe Kora. Hao ndio majumbe waliotoka kwa Oholibama, binti Ana, mkewe Esau. [19] Hao ni wana wa Esau, na hao ndio majumbe wao; naye Esau ndiye Edomu.**

**36:15-19** Hii ni orodha ya viongozi wa kikabila waliotoka kwa Esau. Neno "kizazi" (BDB 49 II) ni neno la Kiebrania kwa ajili ya neno "elfu" (BDB 48 II), ambalo linatumika kwa ajili

1. familia au sehemu ya ukoo, Yosh. 22:14; Amu. 6:15; I Sam. 23:23; Zak. 9:7

2. sehemu ya kijeshi, Kut. 18:21,25; Kumb. 1:15
3. kiuhalisia ni elfu moja, Mwa. 20:16; Kut. 32:28
4. kama kiwakilisho, Mwa. 24:60; Kut. 20:6 (Kumb. 7:9; Yer. 32:18)
5. lugha ya Ugariti (lugha mfanano na Kisemiti), consonanti zile zile za neno *alluph*,lenye kumaanisha "mtemi" (kama vile Mwa. 36:15). Hili lingalimaanisha kuwa kwa ajili ya andiko la Hes. 1:39 palikuwepo na watemi 60 na wanaume 62,700 toka uzao wa Dani. Tatizo linakuja pale panapokuwepo watemi wengi kwa ajili ya idadi ya watu kwa baadhi ya makabila.

Wingi wa matatizo mengi yaliyopo ya idadi katika agano la kale yanaweza kuelezewa na kushindwa kwetu kuwa na uhakika wa tafasiri ya baadhi ya maneno ya Kiebrania. Wengi wa wana wa Esau wametajwa katika orodha hii ya watemi, ambapo inaonyesha ni jinsi gani familia ilichukua uongozi wa eneo hili kijiografia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:20-30**
**[20] Hawa ni wana wa Seiri, Mhori, wenyeji wa nchi ile; Lotani, na Shobali, na Sibeoni, na Ana, [21] na Dishoni, na Eseri, na Dishani. Hao ndio majumbe waliotoka katika Wahori, wana wa Seiri, katika nchi ya Edomu. [22] Na wana wa Lotani, ni Hori, na Hemamu; na umbu lake Lotani ni Timna. [23] Na hawa ni wana wa Shobali, Alvani, na Manahathi, na Ebali, na Shefo, na Onamu. [24] Na hawa ni wana wa Sibeoni, Aya, na Ana; ni yule Ana aliyeona chemchemi za maji ya moto katika jangwa, alipokuwa akichunga punda za Sibeoni babaye. [25] Na hawa ni wana wa Ana, Dishoni, na Oholibama, binti Ana. [26] Na hawa ni wana wa Dishoni, Hemdani, na Eshbani, na Ithrani, na Kerani. [27] Na hawa ni wana wa Eseri, Bilhani, na Zaawani, na Akani. [28] Na hawa ni wana wa Dishani, Usi, na Arani. [29] Hawa ndio majumbe waliotoka katika Wahori; jumbe Lotani, jumbe Shobali, jumbe Sibeoni, jumbe Ana, [30] jumbe Dishoni, jumbe Eseri jumbe Dishani. Hao ndio majumbe waliotoka katika Wahori, kwa habari za majumbe yao, katika nchi ya Seiri.**

**36:20 "Hawa ni wana wa Seiri, Mhori, mwenyeji wa nchi ile"** Toka Kumb. 2:12 tunajifunza kuwa wana wa Esau waliwaondoa wenyeji wa Edomu kama wana wa Yakobo walivyo waondoa wenyeji wa nchi ya Kaanani. Hata hivyo, pia tunaona kuwa palikuwepo na mwingiliano wa ndoa kati ya makundi haya mawili. Haijulikani kama mwingiliano huu wa kuoana ulikuwa ni matokeo ya awali kwenye muunganikano wa makabila haya au yalikuwa ni matokeo ya kuwashinda watu hawa na kuchukua wake zao kama mateka.

**36:24 "Hawa ni wana wa Sibeoni. . .aliyeona chemichemi za maji ya moto katika jangwa, alipokuwa akichunga punda za Sibeoni babaye"** Neno la Kiebrania linatafasiri "chemichemi za maji moto" (BDB 411) ni gumu kulielezea. Nataka kulitumiwa kama mfano kwenye baadhi ya ugumu tunaokabiliano nao katika kujaribu kuielewa sehemu ya Agano la Kale, hasa sehemu zile zilizoelezewa kwa maneno ambayo ni nadra kutumika.

1. Neno linatumika hapa tu katika Biblia ya Kiebrania
2. Katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebraniain limenukuliwa kwa maneno matupu, na sio kutafasiliwa.
3. Katika toleo la Kilatini limetafasiliwa kama "chemichemi ya maji ya moto" (kama vile REB), ambacho tunajua ni kitu kilichopo katika maeneo hayo
4. Baadhi ya tafasiri zinaamini kuwa linarejelea kwenye neno "watu wa hira," ambapo wapo hata sasa katika eneo hili
5. Toleo la Kishamu linabadili consonanti ya neno "ymm" (יממ) kwenda "mym" (מימ) linalomaanisha "maji" (kama vile NKJV)
6. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa neno lile lile kwa ajili ya "punda"(kama vile KJV, ASV, NEB) linarejelewa hapa kwa sababu ni mfano au ni njia ya kinahau ya kusema kuwa kabila hili halikufikia mwisho, yaani., punda hawakuzaliana
7. Torati ya Kisamaria inalibadili neno na kuwa *Emim*, ambalo hutumika katika Kumb. 2:10 kwa ajili ya majitu.

Aina hii pana ya utofauti katika ufasiri unaonyesha tatizo la kujaribu kuelewa maana ya haya manene adimu ya Kiebrania. Uwe mwangalifu usiweze kukamatwa katika aina hizi za maelezo yasioathiri ukweli husika wa kipenge cha fasihi! Yanafurahisha lakini sio ya muhimu.

**36:25** Tambua moja ya majina ya wakeze Esau, Oholibama, linatumika hapa tena kuhusiana na binti wa Ada (kama vile mst. 2). Hili limesababisha matatizo makubwa kwa watoa maoni. Fasihi ya kwenye mimbari inasema kuwa huyu alikuwa ni mtu tofauti, lakini alikuwa ni mpwa wa babake mke wa Esau. Majina yamezoeleka katika familia, mikoa, maeneo na vipindi Fulani. Mara nyingi watu mbalimbali huitwa majina yale yale. Kitu cha kuwatofautisha ni baba zao.

**36:26 "Dishoni"** Andiko la Kiebrania lina "Dishani," lakini kwa sababu ya 1 Nya. 1:41 tafasiri nyingi zimelibadili neno. Kuna uzao mwingine unaojulikana kama "Dishoni" katika mst. 3 au "Dishani" katika 1Nya.1:42.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36: 31-39**
**31 Na hawa ndio wafalme waliomiliki katika nchi ya Edomu, kabla ya kumiliki mfalme ye yote juu ya wana wa Israeli. 32 Bela wa Beori alimiliki katika Edomu, na jina la mji wake ni Dinhaba. 33 Akafa Bela, akamiliki Yobabu mwana wa Zera, wa Bosra, badala yake. 34 Akafa Yobabu, akamiliki Hushamu, wa nchi ya Watemani, badala yake. 35 Akafa Hushamu, akamiliki Hadadi wa Bedadi badala yake, naye ndiye aliyepiga Midiani katika nyika ya Moabu, na jina la mji wake ni Avithi. 36 Akafa Hadadi, akamiliki Samla wa Masreka badala yake. 37 Akafa Samla, na Shauli wa Rehobothi, ulio karibu na mto, akamiliki badala yake. 38 Akafa Shauli, akamiliki Baal-hanani, mwana wa Akbori, badala yake. 39 Akafa Baal-hanani, mwana wa Akbori, akamiliki Hadadi badala yake; na jina la mji wake ni Pau; na jina la mkewe ni Mehetabeli, binti Matredi, binti Mezahabu.**

**36:31 "Na hawa ndio wafalme waliomiliki katika nchi ya Edomu, kabla ya kumiliki mfalme ye yote ya wana wa Israeli"** Mstari huu umesababisha mvurugano mkubwa kati ya watoa maoni wa Agano la Kale. Kwa sababu ya kuwataja wafalme wa Israeli inaonekana kuwa imeandikwa katika kipindi cha baadaye wakati Israeli ikiwa na mfalme. Hii inaonekana kudokeza kuwa kitabu cha Mwanzo, kama hakikuandikwa baadaye, yawezekana kilisanifiwa kipindi cha baadaye. Wale wote wanaoshikilia madhanio yenye kuonyesha hali halisi (wandishi tofauti wanne, J.E.D.P.) wanalitumia hili kama ushahidi imara kwamba Musa hakuwa mwandishi wa mwanzo wa torati. Wale wote wanaotetea uandishi wa Musa wanasema kuwa huu ulikuwa unabii kuhusu siku ambazo mfalme angalionekana. Lazima mtu akubali kuwa Israeli ilitabiriwa kuwa na mfalme katika kitabu cha Mwa. 245 49:10; Hes. 24:7,17; Kumb. 17:14-20. Kwangu mimi ni dhahiri kuwa kuna mtu aliyehariri upya maandiko ya Musa—ikiwa alikuwa ni Yeremia, Ezra, au moja ya shule za kinabii haijulikani, lakini maono sahihi ya kiuhariri kama haya hayaathiri kwa kiasi kikubwa uandishi wa Musa kuhusu torati. Angalia utangulizi, uandishi kwenye Vol. 1A: "Namna vyote vilivyoanza," Mwanzo 1-11.

**36:32 "Bela mwana wa Beori"** Konsonanti za hili jina, Bela (BDB 118), zinafanana na jina la Balaamu,ambae pia anaitwa mwana wa Beori (BDB 129). Huu ni utokeaji wa mara mbili wa jina la babaye (kama vile Hes. 22-24). Kulitambua hili kama ni mtu yule yule ni yumkini, lakini katika orodha ya unasaba huu, hakuna kisichojulikana.

**36:37 "Mto *Frati*"** Hili neno la Kiebrania kwa ajili ya "mto" (BDB 625) limetumika sana kwa mfano kurejerea mto Euphrates (yaani 31:21). Ingawa, katika muktadha lazima lirejeree mto wa mahali kwa sababu hakuna nyaraka za kihistoria zinazoonyesha mfalme kutoka uzao wa Esau aliyewahi kutawala katika nchi ya Mesopotamia.

**36:39** Kwa sababu ya kutajwa kwa wanawake mbalimbali katika mstri wa 39, Albright (Mmarekani wa elimu kale anayetambulika) anadai kuwa palikuwepo na ufanikiwa wa mamamkuu kuwa mfalme wa Edomu. Pale inapodhihirika kuwa hakuna kati ya wafalme hawa ni wana wa wafalme waliopata na kwa sababu wake zao wametajwa, hii yawezekana japo hakuna ushahidi wa kihistoria.

◙ **"Hadari"** Andiko la Kimasoreti lina neno "Hadari" (BDB 214). Hatahivyo, katika 1 Nya. 1:50 limeelezewa kama "Hadadi." Hadadi (BDB 212, kama vile I Fal. 11:14, 17, 21, 25) kikajakuwa cheo kikubwa kwa ajili ya wafalme wa Shamu, lakini katika maelezo haya ni dhahiri hayarejerei Shamu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:40-43**
**40 Na hayo ndiyo majina ya majumbe waliotoka kwa Esau, kufuata jamaa zao, na mahali pao, kwa majina yao.**

**Jumbe Timna, jumbe Alva, jumbe Yethethi, [41] jumbe Oholibama, jumbe Ela, jumbe Pinoni, [42] jumbe Kenazi, jumbe Temani, jumbe Mibsari, [43] jumbe Magdieli, jumbe Iramu. Hao ndio majumbe wa Edomu, kufuata makao yao, katika nchi ya mamlaka yao. Naye huyo ndiye Esau, baba ya Edomu.**

**36:40 "haya ndiyo majina ya wajumbe waliotoka kwa Esau"** Hii inaonekana kuwa sawa na wale watemi waliotajwa mwanzoni, ingawa, hili kundi limechaguliwa kutokana na uhusika wa mahali.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini sura yote nzima inaongelea kuhusu uzao wa Esau?
2. Kwa nini pamekuwepo na mkanganyiko kwenye kuyaandika majina ya wakeze?
3. Kwa nini kuwepo na orodha tano tofauti iliyoandikwa katika sura hii?
4. Kwa kifupi elezea uhusiano kati ya uzao wa Esau na uzao wa Israeli.
5. Elezea uhusiano uliopo kati ya maneno Wahiti, Wahivi, na Wahori.

# MWANZO 37

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Ndoto ya Yusufu | Ndoto ya Ukuu wa Yusufu | Yusufu anauzwa Utumwani | Yusufu na Nduguze | |
| 37:1-2a | 37:1-4 | 37:1-2a | 37:1-2a | Yusufu na Ndugu Zake |
| 37:2b-4 | | 37:2b-4 | 37:2b | 37:2 |
| | | | 37:3-4 | 37:3-4 |
| 37:5-8 | 37:5-8 | 37:5-8 | 37:37:5-7 | 37: 5-11 |
| | | | 37:8 | |
| 37:9-11 | 37:9-11 | 37: 11 | 37:9 | |
| | | | 37:10-11 | |
| | Yusufu anauzwa na Ndugu zake | | Yusufu anauzwa na kupelekwa Misri | Yusufu anauzwa na ndugu zake |
| 37:12-14 | 37:12-17 | 37:12-14a | 37:12-13a | 37:12-14 |
| | | | 37:13b | |
| | | | 37: 14a | |
| | | 37:14b-24 | 37:14b-15 | |
| 37:15-17 | | | | 37:15-17 |
| 37:16 | | | | |
| Njama dhadi ya Yusufu | 37:17 | | | |
| 37:18-24 | 37:18-22 | | 37:18-20 | 37:18-20 |
| | | | 37:21-24 | 37:21-25a |
| | 37:23:28 | | | |
| 37:25-28 | | 37:25-28 | 37:25-28 | 37:25b-27 |
| 37:28-30 | | | | |
| 37:29-36 | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 37:29-36 | | | | |
| | 37:29-3637:29-30 | | 37:29-30 | |
| | | 37:31-32<br>37:33-35 | 37:31-32<br>37:33-35 | 37:31-35 |
| | | 37:36 | 37:36 | 37:36 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI **(angalia ukurasa wa xxvii)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kipengele hiki kinaanza na simulizi la Yakobo na nyumba yake (kwa kangalia maisha ya Yusufu) kwenda katika nchi ya Misri, ambalo litatawala mabaki ya kitabu cha Mwanzo, sura ya 37-50, ikiwa na mihtasari miwili tu iliyotengwa kwenye mabano.
   1. kuhusu Yuda na Tamari (kama vile Mwanzo 38)
   2. kuhusu Baraka za Yakobo za makabila (kama vile Mwanzo 49)

B. Huku kuhamia Misri na matokeo yake kulitabiriwa katika Mwa. 15:13-16

C. Simulizi la Yusufu ni la tofauti na masimulizi mengine ya kihistoria ya kitabu cha Mwanzo.

   1. YHWH hajitokezi moja kwa moja kwa Yusufu (ama malaika)
   2. simulizi ni refu, lenye mtiriko wa vizazi kupitia sura mbalimbali
   3. YHWH hutenda kazi sirini, katika uficho, katika namna za kithiolojia (yaani, “mwanadamu,” wa 3:15-17)
   4. jiografia inabadilika kuanzia nchi ya Uri, Harani, Kanaani hadi Misri

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:1-2a**
**[1]Yakobo akakaa katika nchi aliyosafiri baba yake, katika nchi ya Kanaani. [2]Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo.**

**37:1** Kwa sababu ya kifungu kinachopatikana katika mst. wa 2a, ambacho kinaonekana kuwa njia ya mwandishi ya kukigawa kitabu chake cha Mwanzo, watoa maoni walio wengi wanaamini kwamba mst. wa 1 lazima uendane na sura ya 36. Mstari wa1 kwa hakika ufanano wa makazi ya kijiografia ya Yakobo dhidi ya Esau.

◙ **"katika nchi aliyosafiri baba yake"** Hii ilikuwa sehemu ya ahadi ya ki-Ibrahimu (Mwanzo 12, 15, 17; 28:4). Maisha ya kuhamahama na hatima iliyohaidiwa yalikuwa matendo ya imani.

**37:2"Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo"**Hiki ni kifungu cha mara kwa mara ambacho kinaweka alama ya migawanyo iliyowekwa na Musa katika kitabu hiki (kama vile 2:4; 5:1; 6:9; 10:1; 11:10, 27; 25:12, 19; 36:1, 9; na 37:2). Haijulikani kama kifungu hiki (au wasifu wa mwandishi) kama kinaendelea mbele ama kinarudia maelezo ya nyuma.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:2b-4**
**[2a]Yusufu, aliyekuwa mwenye miaka kumi na saba, alikuwa akichunga kondoo pamoja na ndugu zake; naye alikuwa kijana pamoja na wana wa Bilha, na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. Yusufu akamletea baba yao habari zao mbaya. [3]Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote, maana ni mwana wa uzee wake, akamfanyia kanzu ndefu. [4]Ndugu zake wakaona ya kuwa baba yao anampenda kuliko ndugu zake wote, wakamchukia, wala hawakuweza kusema naye kwa amani.**

◙ **"Yusufu, aliyekuwa mwenye miaka kumi na saba"**Umri wa Yusufu kwa wakati huu wa kuuzwa na nduguze utumwani ni muhimu tunapolinganisha umri wake wakati aliposimama mbele za Farao katika Mwanzo 41:46 (miaka30 ya kuzaliwa). Hatima ya umri wake inaonyeshwa katika 50:26 (miaka 110).

◙ **"naye alikuwa kijana"**Neno hili (BDB 654 II) linaweza kutumika katika maana ya "anayejifunza" au "anayeanza" (kama vile Kut. 33:11, ambapo linatumika kuhusu uhusiano wa Yoshua kwa Musa). Pia inawezekana kwamba wana wa Bilha na Zilpa pia nao walikuwa wameanza. Japokuwa walikuwa nyikani na kutenda kazi kama wachungaji, hawakuwa na jukumu la kipekee kwa hiyo mifugo.

◙ **"Bilha"**Huyu ni msichana wa Raheli. Wengine wanamuona Yusufu kama mwenye kutambuliwa na wanae kwa sababu huenda aliendelea kumwinua zaidi baada ya kifo cha Raheli. Kutokana na Mwan. 30:5-7 tunaona kwamba wana wengine wawili wa Bilhani areDani na Naftali.

◙ **"wana wa Zilpa"** Huyu ni msichana wa Lea na wanae wameorodheshwa katika Mwa. 30:9-13. Nao ni Gadi na Asheri.

◙**"Yusufu akamletea baba yao habari zao mbaya"**asili ya habari yake halisi na yule anayerejelewa, haujulikani (ni aswa na neno lililotumiwana watu kumi walioleta habari katika Hes. 14:37), ukosefu wa hatia kwa Yusufu unaelezwa hapa. Kuna mtiririko wa matendo ambayo yaliwasababisha ndugu zake kumchukia.

1. habari mbaya mst.wa 2
2. kanzu ndefu ya mst. wa 3-4, aliyopewa na Yakobo
3. ndoto zake za kishujaa zilizoandikwa katika mist. ya 5-10

**37:3"Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote"**Jina la Yakobo lilibadilishwa na kuitwa"Israeli" baada ya kushindana mweleka na malaika nje ya kivuko cha Yakobo (kama vile Mwa. 32:22-32).Hili jina bila shaka lina asili kadhaa.Nafikiri mojawapo linaendana na muktadha wa Mwanzo32 ulivyo, "*El* anaweza kiutunza."Angalia Mada Maalum katika 32:28. Ilimpasa Yakobo kuwa kujifunza juu ya matatizo yaliyohusiana na upendeleo wa watoto wake mwenyewe, lakini kwa uwazi hakuwana utambuzi wa jambo hili. Upendeleo wake uliweka mlolongo wa hatua yaYusufu kukataliwa na ndugu zake.

◙ **"maana ni mwana wa uzee wake"**Hiki ni kifungu chenye walakini kidogo kwa sababu Benjamini alikuwa mwana wa Raheli aliyekuwa mdogo kabisa. Hili linaweza kumaanisha baada ya Yusufu kulikuwa na wana wengine wengi. Dhana ya Magharibi ina hatari sana katika kuyafasiri maandiko ya kale ya Kisemitiki. Waalimu wa sheria za Kiyahudi na Targums wanakiona kifungu hiki kama chenye hitilafu na wanakifasiri kama "mwana mwenye hekima

inayotokana na umri aliokuwa amefikia." Andiko lifuatalo linaonyesha kwamba kwa hakika kifungu hiki hakina hakina uyamkini.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kanzu ndefu"** |
| **NKJV** | **"kanzu yenye rangi nyingi"** |
| **NRSV, REB** | **"joho refu lenye mikono mipana"** |
| **TEV** | **"joho refu lenye mikono mikubwa"** |
| **NJB** | **"kanzu yenye kurembwa vizuri"** |
| **LXX** | **"kanzu yenye rangi nyingi"** |
| **Peshitta** | **"joho la kifahari lenye mikono mipana"** |
| **JPSOA** | **"kanzu yenye urembo"** |

Asili ya neno hili la Kiebrania (BDB 509 TUNGO 821) haijulikani.Mara nyingi kanzu lilikuwa vazi lenye mikono mifupi ambalo lilikuwa na urefu uliokuwa unaishia katika goti la mwanamme na mwanamke, hili lilikuwa kwa ajili ya kushindia. Inaonekana kwamba hili kanzu la kipekee kwa vyo vyote lilikuwa refu hadi miguuni, kuanzia mikononi hadi miguuni (BDB 821), ama yote ilikuwa imejaarangi (LXX). Kwa namna yo yote, hii haikuwa kanzu ya kushindia. Rejeo lingine la kipekee kuhusu kanzu hili liko katika II Sam. 13:18, ambapo Tamari alivaa vazi la aina hii hii, ambalo linaelezwa kama lililokuwa maalumu kwa binti za wafalme waliokuwa wanawali, hivyo, kumaanisha hadhi ya kifalme. Inawezekana kwamba Yusufu alihisi kwamba alitakiwa kuwa mwana wa ahadi kwa sababu Reubeni alikuwa amekwisha harimishwa kutokana na tendo alilotenda la kulala na Suria wa Yakobo na Simeoni na Lawi kwa sababu ya mauaji ya Shekemu (Mwanzo 34, kama vile Mwa. 35:22).
Kutokana na Toleo la *IVP Bible Background Commentary* (uk. 68)

"Wachoraji wa ki-Misri wa kipindi hiki wanaeleza kwa kuwachora Wakanaani wenye kuvaa kanzu zenye mikono mirefu, yenye kutaliziwa pembeni hadi kwenye magoti"

**37:4 "Ndugu zake wakaona ya kuwa baba yao anampenda kuliko ndugu zake wote"**Jambo hili linanzisha hatua ya Yusufu kuchukiwa na ndugu zake.

◙ **"wakamchukia"** Hiki KITENZI (BDB 971, KB 1338, *Qal* ya TUNGO KITENZ JINA) kinatumika katika mist. ya 4,5,8; pia angalia Kut. 18:21; 20:5; 23:5; Law.19:17; 26:17; Kumb. 5:9; 7:10,15;12:31; 16:22; 19:11; 30:7; 32:41.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kusema naye kwa amani"** |
| **NKJV, NRSV,** | |
| **LXX** | **"kwa utulivu"** |
| **TEV** | **"katika namna ya amani"** |
| **NJB** | **"kwa neno la kiundugu"** |
| **REB** | **"kwa maneno ya ukali"** |
| **JPSOA** | **"kwa neno la amani"** |

Hii ni NOMINO ya Kiebrania *shalom* (BDB 1022). Ndugu zake wasingeweza kataa kutoa salamu ya kawaida ya kiutamaduni. Hawakutaka apate faraja, apate afya, na hata mali!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:5-8**
**[5] Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia; [6] akawaambia, Tafadhalini, sikieni ndoto hii niliyoiota. [7] Tazama, sisi tulikuwa tukifunga miganda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka ukasimama, na tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu. [8]Ndugu zake wakamwambia, Je! Kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi? Wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto yake, na kwa maneno yake.**

**7:5"Yusufu akaota ndoto"** Inahitajika kusistizwa kwamba, mpaka kufikia hatua hii ya kitabu cha Mwanzo, Mungu amekuwa akiyaeleza mapenzi yake kupitia ndoto na maono (kama vile. 20:3; 28:12; 31:11,24). Watu wa Mashariki ya Karibu ya kale walizitambua ndoto kama chanzo halisi cha ufunuo toka kwa miungu. Ndoto ya Yusufu ilikuwa na asili kama hiyo hiyo, kama kukisafisha kidonda cha ndugu zake waliokuwa na hisia za maumivu ndani ya mioyo yao (kama vile mst. ya 19-20).

**37:7-8"miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu"** Hii ilikuwa maana halisi ya kanzu la Yusufu. Hili linakamilishwa katika Mwa. 42:6; 43:26;na 44:14.

Mstari wa 8 una tabia mbili za kisarufi (KITENZIJINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU kutokana na mzizi ule ule) ambacho kinadokeza uweza.

1. kutawala, BDB 573, KB 590
2. kuongoza, BDB 605, KB 647

Tabia hii hii ya kisarufi pia inatumika katika mst. wa10.

3. uhalisia wa yale yajayo (na kuinama), BDB 97, KB 112

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:9-11**
**[9] Akaota tena ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake, akasema, Angalieni, nimeota ndoto nyingine; na tazama, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikaniinamia. [10] Akawaambia baba yake na ndugu zake; baba yake akamkemea akamwambia, Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je! Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi? [11]Ndugu zake wakamhusudu; bali baba yake akalihifadhi neno hili.**

**37:9** Ndoto hii ni ishara ya utawala ujao wa Yusufu, naYHWH akiwa kama mwezeshaji na mwokozi wa nyumba yake.Hii dhana kwamba mamaye(yaani, ndoto ya usiku) kwamba imekwisha kufa kifasihi haiathiri msukumo wa ndoto.

1. ufunuo wa kinabii wa kuonyesha kwamba Mungu ndite anayeitawala historia
2. hali ya Yusufu kutokuwa na hila
3. namna ya kuwachukulia ndugu zake na kuutekeleza mpango wa Mungu wa kuwa kuwa kama mkimbizi/mtumwa/mtangatangaji wa Kimisri

Muktadha unaweza kuendana na mojawapo ya tafsiri hizi. Si kiini cha similizi katika maelezo haya. Kiini cha simulizi ni YHWH na umilele wake, mpango wa ukombozi wa kumtumia Yusufu kwa ajili ya makusudi yake. Yusufu ni mtu wa mwenendo mwema, lakini kwa namna fulani pia si mwenye hila. Israeli inaokolewa kwa matendo ya YHWH, si kwa nguvu za Yusufu.

**37:10"baba yake akamkemea"**Hili ni neno la Kiebrania lenye nguvu sana (BDB 172, KB 199, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ambalo kwa uasilia wake lilimaanisha "kupaza sauti" (kama vile Yer. 29:27). Neno hili limetumiwa na Mungu mara kwa mara kuyakemea mataifa (yaani, Isa. 17:13). Pia ni neno linalotumiwa na YHWH kumkemea Shetani katika Zek. 3:2.

◙ **"Mimi na mama yako"**Tunahitaji kukumbuka kwamba kwa wakati huu Raheli alikuwa amekwisha kufa (kama vile Mwa. 35:19). Wengine wanadhani kwamba Yakobo bado alikuwa akiendelea kumfikiria au kifungu hiki kinamrejelea Lea, dada aliyefuatiwa na Raheli, au kwa Bilha ambaye alimkuza.

**37:11"Ndugu zake wakamhusudu"**Hiki KITENZI (BDB 888, KB 1109, *Piel*cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatumika katika ufanano na neno "wakachukia" (kama vile mist. 4,5,8). Hiki kipengele cha mst. wa11 kinaunganishwa na mst. wa 28 na 39:21 na 45:4 katika muungano wa nukuu za hotuba ya Stefano katika Matendo ya Mitume 7:9.

◙ **"bali baba yake akalihifadhi neno hili"** Kifungu hiki kinatukumbusha namna Maria alivyolihifadhi moyoni mwake neno lililomhusu Yesu (Kama vile Luka 2:19,51). Yakobo alielewa kwamba Mungu amekuwa akimfunulia mara kwa mara katika ndoto kumthibitisha kwamba yeye ndiye aliyepaswa kuzipokea baraka za ukuu wa watu wote. Yakobo hakutaka kuliamini hili tu, bali pia, matukio ya kihistoria yanaonyesha kuhitimisha kwamba Yusufu

ilimpasa Yusufu kuhaidiwa agano la kuwa mkuu wa nyumba ya Yakobo. Hata hivyo, tunajifunza kutokana na sura zinazofuatia kwamba Mungu hakuwahi kumtokea Yusufu moja kwa moja kama alivyofanya kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakoboya kwamba Yud utakuwa uzao wa Masihi, si si Yusufu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:12-14**
**[12]Ndugu zake wakaenda kuchunga kondoo za baba yao huko Shekemu. [13]Israeli akamwambia Yusufu, Je! Ndugu zako hawachungi kondoo katika Shekemu? Njoo, nikutume kwao. Akamwambia, Mimi hapa. [14]Akamwambia, Enenda, basi, ukaone kama ndugu zako hawajambo, na kundi nalo li salama, ukaniletee habari. Basi akampeleka kutoka bonde la Hebroni, akafika Shekemu.**

**37:13"Israeli akamwambia Yusufu"** Haijulikani ni kwa nini hasa baba yake Yusufu alimtuma kuwaona ndugu zake. Wengine wamekuwa wakidai (1) kwamba alikuwa akijaribu kuwaunganisha ndugu tena au (2) kwamba kwa sababu Yusufu alikuwa amemhabarisha mapema (kama vile. 2), kwamba angefanya hivyo tena kuhusiana na kazi za ndugu zake na kuangalia afya ya mifugo.Kwa kuanzia hapa na kufikiri juu ya sura zilizosalia huu ndia mtiririko wa majibizano kati ya Yakobo na Yusufu liyonukuliwa.

1. "Njoo," BDB 229, KB 246, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. "nikutume," BDB 1018, KB 1511, *Qal* ya WAKATI USIO TIMILIFU unaotumika katika maana ya KAULI YENYE KUTIA MOYO
3. "Mimi hapa," hapa hakuna KITENZI, bali mwonekano wa kawaida wa Agano la Kale, "Mimi hapa," kifungu ambacho toleo la NASB linakitafsri kama "Nitakwenda"
4. "Enenda," BDB 229, KB 246, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
5. "ukaone," BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
6. "ukaniletee habari," BDB 996, KB 1427, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI

**37:14 "ukaniletee habari"** Yusufu alikuiwa amelifanya tendo hili kabla ya mst. wa2

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:15-17**
**[15]Mtu mmoja akamkuta, naye alikuwa anazunguka-zunguka katika nyika; yule mtu akamwuliza, akisema, Unatafuta nini? *[16]*Akasema, Nawatafuta ndugu zangu; tafadhali uniambie mahali wanakochunga. *[17]* Yule mtu akasema, Wametoka hapa, maana niliwasikia wakisema, Twendeni Dothani. Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani.**

**37:15-17"Mtu mmoja akamkuta, naye alikuwa anazunguka-zunguka katika nyika"**Mtu huyu ambaye hakutajwa jina lake anafunua juu ya uwepo wa Mungu katika tukio zima (japokuwa jina lake halikutajwa). Hili limenukuliwa hasa kwa makusudi fulani! Kwa sababu ya maeneo mengine katika kitabu cha Mwanzo ambapo malaika wanaitwa "watu" (yaani, sura ya 18), yawezekana huyu akawa malaika.

**37:17"Dothani"**Jina linalomaanisha "mashimo mawili" (BDB 206). Dothani ni eneo lililo katika njia ya misafara ya biashara ambayo inaanzia Shamu hadi Misri. Tambua katika ramani kuwa Hebroni, Shekemu, na Dothani ni miji mikuu ya ambayo iko katika njia hii ya misafara ya biashara. Baadaye katika historia ya kibiblia, Mungu atadhihirisha tena uwepo wake katika nafasi yake (kama vile II Fal.6).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:18-24**
**[18]Wakamwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue. [19]Wakasemezana wao kwa wao, Tazama, yule bwana wa ndoto anakuja. [20]Haya, twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, Mnyama mkali amemla; kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake. [21] Reubeni akasikia akamwokoa katika mikono yao, akasema, Tusimwue. [22] Reubeni akawaambia, Msimwage damu; mtupeni katika birika hii iliyopo nyikani, wala msimguse; ili apate kumwokoa katika mikono yao, akamrudishe kwa baba yake. [23]Ikawa Yusufu alipofika kwa ndugu zake, wakamvua Yusufu kanzu yake, kanzu ile ndefu aliyoivaa, [24]wakamtwaa wakamtupa katika birika; na hiyo birika ilikuwa tupu, hamna maji.**

**37:18 "Wakamwona toka mbali"** Bila shaka hili linarejelea juu ya kanzu iliyofumwa aliyopewa na baba yake, ambayo aliivaa mara kwa mara.

◙ "**wakafanya shauri juu yake ili wamwue"** Hiki KITENZI adimu (BDB 647, KB 699, cha *Hithpael* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinafanana na ile chuki inayozungumzwa katika Zab 105:25. Hiki KITENZI kilicho katika shina la neno *Piel* kinatumiwa na YHWH kwa Wamidiani katika Hes. 25:18. Hii *Qal* ya KAULI ENDELEVU inatafsriwa kama "tapeli" katika Malaki 1:14. Hii dhambi ya mauaji ya Kaini dhidi ya Abeli (Mwanzo 4) yanathibitishwa tena katika ubinadamu ulioanguka. Ni sababu za maslahi binafsi!

**37:20 "tutasema "** Angalia mst. wa 32. Hapo awali walipanga namna ya kumuua, namna ya kuushughulikia mwili wake, na namna ya kuyafunika matendo yao kwa bba yao.

◙ **"kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake" Hili linaweza kuwa dokezo la shauku yao binafsi ya urithi**, ambayo ilimfanya kumuhofia Yusufu kuwa angekuwa mrithi.

**37:21-22 "Reubeni"** Hatuwezi kufahamu kuhusu shauku halisi ya Reubeni, bali kutokana na kile kilichoandikwa mwishoni wa mst. wa 22, huu unaonekana kuonyesha kwamba huyu alishindwa kutimiza jukumu la kumlinda mdogo wake, yeye kama mwana aliye mkubwa. Inaweza kuwa kuwa hili lingesaidia kumtambulisha upya kwa Yakobo, kwa upande wa Mwa. 35:22.Nafikiri kwamba kwa hakika alitaka kumwokoa Yusufu, tendo ambalo linaweza kuonekana kama mwitikio wake katika mist. ya 29 na 30. Kwa uwazi tukio hili linaonyesha kuwa huyu amepoteza ushawishi na utawala wake miongoni wa ndugu zake. Tambua maneno ya Reubeni.

1. "Tusimwue," mst. wa 21, BDB 645, KB697, *Hiphil wa* KAULI YA WAKATI TIMILIFU unatumika katika maana ya KAULI YENYE KUTIA MOYO
2. "Msimwage damu," mst. wa 22, BDB 1049, KB 1629, *Qal ya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU unatumika katika maana ya kauli amrishi
3. "mtupeni katika birika hii," mst. wa 22, BDB 1020, KB 1527, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
4. "wala msimguse" mst. wa 22, BDB 1018, KB 1511, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU unaotumika katika maana ya KAULI AMRISHI

Tambua kwamba shauku ya Reubeni iliyojificha inaelezwa.

1. Kwamba angemuokoa, BDB 664, KB 717, *Hiphil* TUNGO YA KITENZIJINA HALISI kumrejesha kwa baba yake, BDB 996, KB 1427, *Hiphil ya* TUNGO YA KITENZI JINA HALISI

**37:24 "wakamtwaa wakamtupa katika birika"** Tunaweza kuelewa kidonda alichokuwa nacho huyu kijana mdogo kutokana na kile kilichoandikwa katika Mwa. 42:21, ambacho kinaeleza ombi lake la uhitaji wa msaada.

◙ "**hiyo birika ilikuwa tupu, hamna maji"** Kwa uwazi kabisa kuwa hili ni dimbwi la maji (si chemchemi, bali ni eneo linalokusanya maji), ambalo lilikuwa la kawaida sana katika eneo la Palestina. Walimu wa sheria wanasema kwamba dimbwi hili lilikuwa limejaa nyoka na nge, lakini hili ni dhanio tu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:25-28**

**[25]Nao wakakaa kitako kula chakula; wakainua macho yao, wakaona, msafara wa Waishmaeli wanakuja wakitoka Gileadi na ngamia zao, wakichukua ubani na zeri na manemane, wakisafiri kuvichukua mpaka Misri. [26] Yuda akawaambia ndugu zake, Kwafaa nini kumwua ndugu yetu, na kuificha damu yake? [27] Haya, na tumwuze kwa hawa Waishmaeli, wala mikono yetu isimdhuru, maana yeye ni ndugu yetu, na damu yetu. Ndugu zake wakakubali. [28]Wakapita wafanya biashara Wamidiani; basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini; nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri.**

**37:25"Nao wakakaa kitako kula chakula**" Jambo hili linaonyesha namna walivyokuwa hawa hisia zozote juuya ndugu yao.

◙ **"wakaona, msafara wa Waishmaeli wanakuja wakitoka Gileadi"**Kuna tofauti kati ya asili ya neno lililotumika kutoa ufafanuzi wa wafanya biashara hawa (hili linaonyeshwa na wakosoaji kama ushahidi wa vyanzo vingi).

1. katika mst.wa 25 hawa wanaitwa Waishmaeli
2. katika mst. wa 28 hawa wanaitwa wafanya biashara wa ki-Midiani
3. katika mst wa 28, tena, Waishmaeli
4. katika mst. wa 36 hawa wanaitwa Wamedi (MT)

Haya ni majina tofauti yenye kurejelea kundi hilo hilo kama Amu. 8:22,24inavyoonyesha. Pia, Wamedi na Wamidiani wote walikuwa wana wa Ibrahimu kupitia Ketura (kama vile Mwa. 25:2), lakini kuwataja Wamedi linaweza kuwa tatizo la kiuandishi (Wamedi, מדינים; Wamidiani, מדנים. Msfara huu unaweza kuwa umeundwa na makundi ya nyumba kadhaa na tofauti tofauti ama majina tofauti ili kurejelea watu wale wale.

◙ "**ngamia zao, wakichukua** . . . **wakisafiri kuvichukua mpaka Misri**" Vito hivi na manukato ndivyo vilivyoingizwa Misri kwa sababu vilitumika vilitumika (1) kutunza; (2) kwa ajili ya kufukiza; na(3) kwa ajili ya tiba. Gileadi (huko vilikotoka) ilikuwa maarufu kwa manukato hayo.

**37:26 "Yuda akawaambia ndugu zake"** Hatufahamu kuhusu shahuku halisi ya Yuda, kama tusivyo fahamu shauku halisi ya Reubeni, bali inaonekana kwamba huyu alikuwa akijaribu kumwokoa ndugu yake ili asiuawe ("ni ndugu zetu,"mst. wa 27), ingawa shauku iliyotangulia ni (1) kupata faida na (2) si kuwa na damu isiyo na hatia (yaani, muuaji) kwa upande mwingine.

Ikiwa Yuda anajaribu kumwokoa ndugu wa baba yake kutoka kifoni, hii ni njia chanya ambayo ya kumweleza mwana huyu ambaye angekuwa mmoja wa nyumba ya uzao wa Yesu. Ikiwa Yuda alitenda tendo hili kulingana na sababu zilizoelezwa pia inaonyesha kwamba makusudi ya Mungu hayakujikita katika faida au thamani ya mtu (kama vile Mwanzo 38), bali ni mpango wa YHWH wa ukombozi wa milele kwa watu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5; angalia Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjili katika 12:3).

**37:28 "wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini"** Elewa kwamba hili neno "shekeli" liko katika mlazo, ambapo inamaanisha kuwa neno hili haliko katika andiko la Kiebrania, bali linadhaaniwa (kama vile 20:16; Amu. 17:2-4,10). Hili linarejelea uzito wa fedha. Tunajifunza kutokana na Law. 27:5 kuwa watumwa wenye umri mdogo walikuwa wakiuzwa kwa shekeli ishirini, ambapo watumwa wenye umri mkubwa walikuwa wakiuzwa kwa shekeli arobaini (kama vile Kut. 21:32 au "shekel hamsini (kama vile Law. 27:3)). Pia tunafahamu kwamba biashara ya utumwa ilikuwa uhalisia wa utamaduni wa Misri katika kipindi chote cha historia yake.

Baadhi ya watoamaoni wanawafasiri watu "hawa" kama wafanya biashara wa ki-Midiani waliomwaondoa Yusufu ndani ya shimo na kumuuza kwa Waishmaeli wa mst. 25. Hawa wanadai kuwa jambo hili lilifanyika pasipo wana wa Yakobo kufahamu, hivyo, hili linaieleza mst. ya 29-30 (matendo ya Reubeni kwa Yusufu kabla ya kutupwa ndani ya shimo). Hata hivyo, hali hii haielezi mst. wa 27! Mara nyingi mbinu za wakosoaji wa sasa zinaeleza zaidi kuwahusu na nadhaanio lao la awali kuliko yalivyo masimulizi ya historia ya kale ya Kiebrania.

◙ **"wakamchukua Yusufu mpaka Misri"** Kifungu hiki ni cha kikejeli kwamba msafara walioufuata ulimchukua Yusufu katika maili fupi kutoka hema la baba yake! Hata hivyo, yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa Yusufu kwenda Misri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:29-36**
**29 Akarudi Reubeni birikani, kumbe! Yusufu hayumo katika birika, akararua nguo zake. 30 Akarudi kwa ndugu**
**zake, akasema, Mtoto hayuko, nami niende wapi? 31 Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakachinja mwana-mbuzi,**
**na kuichovya kanzu katika damu. 32 Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao, wakasema,**
**Tumeona hii; basi, utambue kama kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo. 33 Akaitambua, akasema, Ndiyo kanzu**
**ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa. 34 Yakobo akararua mavazi yake,**
**akajivika gunia viunoni, na kumlilia mwanawe siku nyingi. 35 Wanawe wote, na binti zake wote, wakaondoka**
**wamtulize, lakini akakataa kutulizwa, akasema, La! Nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu. Baba**

**yake akamlilia. [36]Nao Wamidiani wakamwuza huko Misri, kwa Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari.**

**37:29 "Akarudi Reubeni birikani…akararua nguo zake"**Hiii ni ishara ya kiutamaduni ya kuomboleza (kama vile 44:13). Ishara za kiutamaduni za kuomboleza zinaweza kuonekana katika mst. wa 34 ambapo Yakobo anajikuta amempoteza Yusufu.Haikumpasa Reubenikutoa maelezo yale yale waliozungumza kuhusu mpango wao ama wakati ndugu zake walipomuuza Yusufu.

## MADA MAALUMU: IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19;Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Ezek. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza , 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa na kuvutwa), Yer. 48:37
13. Kunyoa ndevu za kidevuni kuwa fupi, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani

**37:30"nami niende wapi"**Je! Reubeni angemaanisha nini kwa kujiuliza swali hli

1. naweza kiptata wapi
2. Siwezi kwenda nyumbani pasipokuwa naye
3. Maelezo ya kifasihi yenye maana ya kukosa tumaini

**37:35"Wanawe wote, na binti zake wote, wakaondoka wamtulize"** Jambo hili si la kejeli kwamba wale waliomuuza Yusufu ndio wanaojaribu kumfariji baba yao kwa ajili ya kupoteza. Kumekuwa na baadhi ya madhaanio kuhusu neno "binti zake." Je! Neno hili linamrejelea Dina na wengine ambao walizaliwa baadaye amakinarejelea juu ya shemeji zake?

◙**"*Sheol*"** Neno hili (BDB 982) linatumika kumaanisha"kaburi"ama"maisha baada ya kifo." Inaonekana kuwa na uwezekano wa asili mbili za Kiebrania: (1) "kwenda chini" na (2) "kuuliza," ambazo zinaweza kuhusisha neno*Sheol*kwa maana ya kuuliza zaidi juu ya wanadamu ama kuuliza swali kuhusu neno*Sheol*. Inaonekana kwangu kwamba neno hili katika Agano la Kale na *Hades* katikaAgano Jipya zina shabihiana. Kutokana na fasihi ya sheria za Kiyahudi, na uthibitisho mwingine ulio katika Agano Jipya, inaonekana kutenganishwa katika sehemu mbili, ya haki nay a mdhalimu. Angalia Mada Maalum: Wafu Wako Wapi? katika 15:15.

**37:36"Potifa"** Hili ni jina la Kiebrania ambalo linaonekana kumaanisha "aliyepewa (iliyomaanisha Re, mungu wa jua)" (BDB 806).Muundo mrefu wa jina kama hili unapatikana ukuhani wa Oni katika Mwa. 41:45.

◙ **"akida wa Farao"**Hili neno"akida"kiuhalisia nia "toashi" (BDB 710, kama vile Esta 1:10; 2:3), lakini kwa kuwa alikuwa ndani ya ndoa, hapa neno hili linamaanisha "tarishi" ama "akida" (kama vile I Fal. 22:9;II Fal. 8:6; 24:12) badala ya kuhanithisha.

◙ **“mkuu wa askari”**Kuna uwezekano wa aina mbili kwa sababu kiuhalisia linamaanisha“muuaji mkuu” (BDB 978 TUNGO 371).Wengine wanaamini kuwa neno hili linamaanisha“mpishi mkuu” (BDB 371, yaani, mchinjaji) na hili linajikita katika I Sam. 9:23-24. Wengine wanaamini kwamba neno hili linamaanisha “mkuu wa walinzi” lenye kujikita katika Mwa. 37:36; 39:1; 40:3,4; 41:10,12 na II Fal. 25:8. Kwa hakika inawezekana kwamba wale waliokuwa karibu na mfalme (kama wapishi wake) walichaguliwa kuwa walinzi wake.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini kinaonekana kuwa chanzo cha mvutano kati ya Yusufu na ndugu zake?
2. Fafanua kuhusu joho la kipekee ambalo Yakobo alimtengenezea Yusufu. Je! Linaashiria nini?
3. Kwa nini mwandishi wa kibiblia anaihusisha mst. ya 15-17?
4. Orodhesha ishara za kuomboleza zinazopatikana hapa katika mst. ya 29 na 34 na sehemu zingine za Agano la Kale.
5. Fafanua mtazamo wako kuhusu neno *Sheol* na namna linavyohusiana na neno *Hades* la Agano Jipya

# MWANZO 38

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yuda na Tamari | Yuda na Tamari | Yuda na Tamari | Yuda na Tamari | Hadithi ya Yuda na Tamari |
| 38:1-5 | 38:1-11 | 38:1-11 | 38:1-5 | 38:1-5 |
| 38:6-11 | | | 38:6-11 | 38:6-11 |
| 38:12-19 | 38:12-23 | 38:12-19 | 38:12-14 | 38:12-14 |
| | | | 38:15-16a | 38:15-19 |
| | | | 38:16b | |
| | | | 38:17a | |
| | | | 38:18b | |
| | | | 38:18a | |
| | | | 38:18b-19 | |
| 38:20-23 | | 38:20-23 | 38:20-21a | 38:20-23 |
| | | | 38:21b | |
| | | | 38:22 | |
| | | | 38:23 | |
| 38:24-26 | 38:24-26 | 38:24-26 | 38:24a | 38:24-26 |
| | | | 38:24b | |
| | | | 38:25 | |
| | | | 38:26 | |
| 38:27-30 | 38:27-30 | 38:27-30 | 38:27-30 | 38:27-30 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA

A. Sura ya 38 ni mapumziko ya wazi katika muktadha ya hadithi ya Yusufu. Baadhi wameelezea kwamba imejumuishwa kwasababu ina onyesga kwa mchoro uzao wa kabila la Yuda, ambao ndiyo uzao wa Masihi unaonukuliwa katika Mt. 1:3 na Luka 3:33. Ni wazi kwamba Sura hii inakimbilia katika ukabiliano wa kutengwa na Wayahudi na majivuno ya kikabila. Kujumuishwa kwa mwanamke Mkanaani kama Tamari ni mfano mwingine wa kuchanganywa cha uzao wa Masihi (kama vile Rahabu na Ruthi).

B. Baadhi wamelezea kwamba sababu ya kujumuishwa kwa sura ya 38 ni kuonesha utofautiano kati ya kumomonyoka kwa maadili ya ndugu wa Yusufu na matendo ya kipekee ambayo yameorodheshwa katika Mwanzo 39.

C. Mwanzo ni simulizi inayojitokeza ya namna ya mwanadamu kukimbilia njia moja, lakini mpango ya Mungu kuendesha mingine. Huku kurudishwa kwa hali kutoka kudharauliwa kwenda katika heshima ni tabia ya Mwanzo na Agano la Kale. Kithiolojia inaelezwa utawala wa YHWH na mpango wa ukombozi wa kiulimwengu (yaani Mwanzo 3:15; 12:3c; Kutoka 19:5c). YHWH amekuwa akifanya kazi ya urejesho wa ushirika na uumbaji wake toka Mwanzo 3 (hasa mstari wa 15, ambayo ni ahadi kwa wanadamu wote waliofanywa katika sura ya Mungu, kama vile 1:26-27). Vitu havitokei tu!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:1-5**
**[1] Ikawa wakati ule, Yuda akashuka kutoka kwa ndugu zake, akamfikia mtu Mwadulami, jina lake Hira. [2] Yuda akaona huko binti wa mtu Mkanaani, jina lake Shua. Akamtwaa, akaingia kwake. [3] Naye akapata mimba, akazaa mwana, akamwita jina lake Eri. [4] Akapata mimba tena, akazaa mwana, akamwita jina lake Onani. [5] Akaendelea, akazaa tena mwana mwingine, akamwita jina lake Shela. Naye Yuda alikuwako huko Kezibu, alipomzaa.**

**38:1 "Ikawa wakati ule"** Tungo ya Kiebrania hapa ina utata na muunganiko wa muda halisi kati ya Sura ya 37 na 38 haujulikani. Inawezekana aidha kwa ghafla kuwa baada ya sura ya 37 au baada ya kipindi cha muda. Angalia muunganiko wa muda tofauti tofauti.

1. sasa Yakobo anaishi katika nchi, 37:1
2. ikawa wakati ule, 38:1
3. kisha baada ya muda kidogo, 38:12
4. kisha ikawa baada ya muda wa miezi mitatu, 38:24
5. ikawa baada ya muda kidogo, 38:27
6. kisha ikawa baada ya mambo haya, 40:1
7. kisha ikawa mwishoni mwa miaka miwili, 41:1

Ni wazi kwamba Mwandishi yuko makini juu ya muda, lakini hii sio mfululizo wa historia ya kimagharibi.

◙**"Yuda akashuka kutoka kwa ndugu zake"** Kumekuwa na madhanio mengi juu ya kwanini Yuda aliondoka. Baadhi wanasema ni kwasababu ya kumomonyoka kwa maadili ya ndugu zake au yawezekana namna walivyomtendea Yusufu.

◙**"na akawatembelea"** Hiki KITENZI kibayana ni "kugeuzwa kando," BDB 639, KB 692, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Inamaanisha kuondoka kwa muda mrefu kutoka kwa ndugu zake. Eneo hili hili la kijiografia baadaye litajumuishwa katika ugawanyaji wa Yuda (kama vile Joshua 15:35). Mapango ya Abdullah baadaye yataunganishwa na matukio makubwa ya Daudi katika muunganiko na Sauli (kama vile I Sam. 22:1). Inavyoonekana ilikuwa katika kilima cha nchi ya Yuda, karibu na uwanda wa juu wa pwani.

**38:2 "Shua"** Jina hili (kama Hira, mstari wa 1, BDB 301) linapatikana katika Agano la Kale. Mzizi ule ule wa Konsonanti (BDB 447) inamaanisha "kujitegemea" au "heshimiwa." Ina konsonanti zile zile tatu za ndani kama "wokovu" (BDB 447), lakini kunaonekana kuwepo kwa muunganiko wa kithiolojia.

◙ **"Yuda akaona huko binti wa mtu Mkanaani"** Jina la msichana huwa halitajwi (anaitwa "Bath-shua" katika I Nyakati 2:3, lakini hili sio jina bali uhusika—"binti wa Shua"), lakini hii ni dhahiri kwamba Yuda lazima alizama katika mapenzi kwa kumuona kwake kwa mara ya kwanza. Ndoa hii Kwa Mkanaani haishutumiwi na haswa katika muktadha wa haraka. Yuda alikuwa dhahiri mume mwaminifu kwa mke mmoja (kama vile mstari wa 12).

◙**"Kezibu"** Walimu wanatumia jina la sehemu hii (BDB 469) katika namna ya kushusha hadhi (ni sawa na mzizi "kudanganywa," "uongo," "kitu cha udanganyifu," BDB 469) kumaanisha watoto waliozaliwa na mwanamke. Hatahivyo, ubaguzi wa kiualimu wa kiyahudi dhidi ya mataifa yanayozunguka ni wazi katika maandiko yao yote. Ni jina la mahali tu. Yawezekana ni sawa sawa na Kezibu (BDB 469) katika Yoshua 15:44.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:6-11**
**6 Yuda akamwoza mke Eri, mzaliwa wake wa kwanza, na jina lake huyo mke ni Tamari. 7 Naye Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alikuwa mbaya machoni pa Bwana; na Bwana akamwua. 8 Yuda akamwambia Onani, Uingie kwa mke wa nduguyo, ukamwoe, ukamwinulie nduguyo uzao. 9 Onani alijua ya kwamba huo uzao hautakuwa wake, ikawa, alipoingia kwa mke wa nduguye, akamwagia chini asimpe nduguye uzao. 10 Neno hili alilolifanya likawa baya machoni pa Bwana, basi akamwua yeye naye. 11 Yuda akamwambia Tamari mkwewe, Ukae mjane nyumbani mwa baba yako hata Shela mwanangu atakapokuwa mtu mzima, maana alisema, Asipate kufa yeye kama nduguze. Basi Tamari akaenda, akakaa nyumbani mwa babaye.**

**38:6 "Yuda akamwoza mke Eri, mzaliwa wake wa kwanza"** Yuda hakuruhusu baba yake amchagulie mke, lakini katika desturi za kiutamaduni alimchagulia mke kwa ajili ya mwanawe wa kiume. Ni wazi kwamba kwasababu ya historia ya imani yake kwa YHWH kwamba angeweza kumchagulia mwanamke mwenya maadili. Majina yake ni Tamari, ambayo yanamaanisha "mti wa mnazi" (BDB 1071 II). Kuna wanawake wengine kadhaa katika Biblia ambao wana jina hilohilo.

**38:7 "Naye Eri. . . alikuwa mbaya machoni pa Bwana"** Tathmini hii mbaya inatokea mara kwa mara katika Agano la Kale (kama vile 32:13; Kumb. 4:25; 31:29; Amu. 2:11; 3:7,12; 4:1; 6:1; 10:6; 13:1; I Sam. 15:19; I Wafalme 11:6; 14:22; 15:26,34; 16:19,25,30; 21:20,25; 22:52; II Wafalme. 3:2; 8:18,27; 13:2,11; 14:24; 15:9,18,24,28; 17:2,17; 21:2,6,15,16,20; 23:32,37; 24:9,19). Matokeo ya kuanguka ni mapotofu na yenye uharibifu. Kwasababu ya usambamba unaoonekana kati ya matendo ya Eri na Onani ambayo yanatajwa katika mistari ya 8-10, walimu wa Kiyahudi wanaeleza kwamba wote walikuwa wenye hatia ya dhambi moja (yaani "walimwaga uzao wao katika ardhi"), hii haiko wazi kutoka katika muktadha. Walieleza kwamba Eri hakutaka mke wake kuwa na watoto kwa sababu ingemfanya aonekane kuwa mzee kabla ya wakati wake.

Ni wazi kwamba walitenda katika namna isiyo sahihi, wakivunja misingi na miongozo. Ni wazi pia kwamba Bwana anatumia hukumu ya muda (kama vile Ayubu 22:15-16; Mithali 10:27).

**38:8 "Yuda akamwambia Onani, Uingie kwa mke wa nduguyo, ukamwoe, ukamwinulie nduguyo uzao"** Hii baadaye ni dhana ya ndoa za walawi (kama vile Kumb. 25:5ff.). Tunayo mifano miwili tu ya maandiko haya, hapa na katika kitabu cha Ruth. Haki za kurithi zilikuwa jambo muhimu. Yuda anazaa mwana wake wa pili amri tatu.

1. nenda kwa mke wa nduguyo, BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. kafanye majukumu yako kama shemeji, BDB 386, KB 383, *Piel* KAULI SHURUTISHI
3. Utafute uzao kwa ajili ya ndugu yako, BDB 877, KB 1086, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

Kwa ajili ya mjadala mzuri mfupi wa "desturi za ndoa za kiebrania (kutoka katika lugha ya Kilatini kwa ajili ya "ndugu/kaka") angalia NIDOTTE, vol. 4, ukurasa wa 902-905 na ABD, vol. 4, kurasa 296-297.

**38:9 "Onani alijua ya kwamba huo uzao hautakuwa wake"** Inavyoonekana Onani alikuwa anajali sana kuhusu urithi mkubwa kwa ajili yake mwenyewe kuliko alivyokuwa anajali wa familia ya ndugu yake. Hii ni mbinu ya mpango wa uzazi pekee inayotajwa katika Agano la Kale. Kwasababu ndugu yake alikuwa mzaliwa wa kwanza, sehemu kubwa ya urithi ingekwenda kwa mrithi wake. Sura hii kiuwazi inafunua uovu kati ya wana wawili wa Yuda.

◙**"ikawa, alipoingia kwa mke wa nduguye"** NJEO ya KITENZI cha Kiebrania inamaanisha kwamba alikwenda kwake mara moja tu (VITENZI viwili vya NJEO ZA WAKATI KAMILIFU).

**38:11 "Yuda akamwambia Tamari mkwewe....hata Shela mwanangu atakapokuwa mtu mzima"** Yuda alikuwa na wana watatu tu na wawili kati yao inavyoonekana walikuwa wamekufa kwa kuwasiliana na Tamari. Yuda alikuwa na hofu kwamba mwanawe wa mwisho angekufa na hakuwa na vizazi vya baadaye. Hadithi hii imewekwa katika kumbukumbu kuonesha ni kwa namna gani mababa wote wa imani walijaribu kufanya hila ahadi za Mungu katika muunganiko na Masihi aliyehaidiwa ambaye angezaliwa kutokana na uzao wao. Au, inaweza kuwa ni hofu iliyounganishwa na laana iliyokuwa kwa Tamari. Dhambi inahusiana na ukweli kwamba alidanganya kwa shemeji yake wa kike wakati hakuwa na nia ya kumpatia mwanawe wa kiume wa mwisho, jambo lililokuwa hitaji la kisheria. Ule ukweli kwamba Tamari alirudi katika nyumba ya baba yake (yaani Amri za Yuda, BDB 442, *Qal* KAULI SHURUTISHI) inaonekana kuwa desturi ya kiutamaduni (kama vile Mambo ya Walawi 22:13 na Ruthi 1:8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:12-19**
**[12] Siku nyingi zikapita, akafa binti Shua, mkewe Yuda. Yuda akafarijika, akaenda kwa watu wake wawakatao manyoya kondoo huko Timna, yeye na mwenzake Hira, Mwadulami. [13] Huyo Tamari akapewa habari, kusema, Mkweo anakwenda Timna, akate manyoya ya kondoo zake. [14] Basi akavua nguo za ujane wake, akajivika utaji, akajifunika uso, akakaa mlangoni pa Enaimu, karibu na njia ya kuendea Timna. Maana aliona ya kwamba Shela amekuwa mtu mzima, wala hakuozwa awe mkewe. [15] Yuda alipomwona alimdhania kuwa ni kahaba, maana amejifunika uso. [16] Akamgeukia kando ya njia, akasema, Niruhusu niingie kwako. Maana hakujua ya kuwa ni mkwewe. Akamwuliza, Utanipa nini, ukiingia kwangu? [17] Akasema, Nitakuletea mwana-mbuzi wa kundini. Naye akamwuliza, Je! Utanipa rehani hata utakapomleta? [18] Akasema, Nikupe rehani gani? Akamjibu, Pete yako ya muhuri, na kamba yake, na fimbo yako iliyo mkononi mwako. Basi akampa, akaingia kwake, naye akapata mimba. [19] Akaondoka, akaenda zake, akavua utaji wake, na kuvaa mavazi ya ujane wake.**

**38:12 "akafa binti Shua, mkewe Yuda"** Bado hatupewi jina lake. Yuda alikuwa mtu mwaminifu alikuwa mwenye kujali sana msichana wake huyu Mkanaani.

◙**"Siku nyingi zikapita, Yuda akafarijika, akaenda kwa watu wake wawakatao manyoya kondoo huko Timna"** Kipindi cha kunyoa kilikuwa ni kipindi cha sherehe (kama vile I Sam. 25:4, 36). Ilikuwa kwa baadaye makazi ya kikabila la Yuda (kama vile Yosh. 15:57). Hili eneo la Kijiografia ni maarufu sana kwasababu ya muunganiko wake na Samsoni.

**38:13 "Huyo Tamari akapewa habari"** Ni mawazo yangu kwamba Tamri alitenda zaidi kwasababu za kimungu kuliko inavyowekwa wazi katika maandiko (kama vile mstari wa 26). Kama Rebeka na Yakobo (kama vile 25:23), mtu angeweza kuona mashaka juu ya mbinu za matendo, lakini nyuma ya matendo yao ni sehemu ya imani na tumaini. Kama Ibrahimu na Mababa wote wa imani walivyojaribu kumsaidia Mungu kutimiza ahadi zake, Naamini kwamba Tamari alijiskia mtu mwenye majukumu ya pekee kama mke wa wa mwana mkubwa wa Yuda kuinua uzao. Alikuwa tayari kujiaibisha mwenyewe na kukabiliana na uwezekano wa mauti ili kwamba apate nafasi ya kumzalia mwana Yuda.

**38:14 "Basi akavua nguo za ujane wake"** Kwa uhakika jambo hili lilijumuisha nini haiko wazi, lakini bado alijiskia kuwa kuunganishwa kwenye familia ya Yuda. Alikuwa bado anasubiri Yuda kutimiza neno lake (kama vile mstari wa 11). Lazima ingekuwa kipindi kilichozidishwa muda na alianza kuuliza maswali juu ya Ahadi za Yuda (kama vile mstari wa 14).

◙**"akajivika utaji, akajifunika uso, akakaa mlangoni pa Enaimu"** Kuna utaji wa aina mbili "mashali" (BDB 858, KB 1041) yanayotajwa katika Agano la Kale. Hayakuwa yamezoeleka kabla ya kipindi cha Uislamu. Rebeka alikuwa amevaa moja wakati alipokutana na Isaka (kama vile 24:65) Tamari huvaa utaji. Musa pia alivaa utaji ili kufunika uso wake wakati aliposhuka chini kutoka Mlima Sinai ("utaji," BDB 691, kama vile Kut. 34:33,34,35).

Tunajifunza kutoka katika nyaraka za Kishamu kwamba utaji ilikuwa ni ishara ya matendo ya ukahaba. Pia tulijifunza kwamba ilifanyika muhuri kwa mungu wa kike mwenye utaji aitwaye Ishtari. Inavyoonekana hii ilikuwa ni njia fulani ya kutambua matendo ya kikahaba. Ingawa neno lililotumika na Yuda katika mstari wa 15 ni neno la kawaida lililozoeleka la Kiebrania ("yeye aziniye," BDB 275, KB 275, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU), Neno lililotumika na rafiki yake Hira, Mwadullami katika mistari ya 21-22, ni neno kwa ajili ya ukahaba wa hekalu (BDB 873 I, kama vile Kumb. 23:17-18; Hosea 4:14).

**38:16 "Akamgeukia kando ya njia, akasema"** Kuna vipengele kadhaa vinavyowasumbua wasomaji wa kisasa: (1) kunaonekana kuwa na upendeleo wa dhahiri kati ya usahihi wa matendo ya Yuda na usahihi wa matendo ya Tamari; (2) Imewafanya wafasiri pia wafikirie kuwa Yuda alijua kwa hakika maswali gani ya kuuliza na taratibu ya kulipa gharama za kahaba. Ni lazima tuwe makini kutohukumu ulimwengu wa kale kwa nia zetu, lakini lazima tuwe makini kutambua kumomonyoka kimaadili hata ndani ya kabila la Yuda.

**38:17"Nitakuletea mwana-mbuzi wa kundini"** Kutoka katika matendo makuu ya Samsoni yaliyoandikwa katika Waamuzi 15:1, hii inaweza kuwa gharama iliyozoeleka kwa mambo ya kujamiiana. Hatahivyo, kuna baadhi ya ushahidi wa kale kwamba mbuzi ilikuwa ishara ya mungu wa upendo na hii inaweza kuwa historia ya desturi hii.

**38:18"Akasema, Nikupe rehani gani? Akamjibu, Pete yako ya muhuri, na kamba yake, na fimbo yako iliyo mkononi mwako"** Tamari alikuwa amefikiria sana kwa kina juu ya mpango wake. Muhuri na fimbo vilikuwa vitu vyenye kuonesha utajiri wa mtu katika Mashariki ya Karibu ya kale na vilikuwa pekee kwa kila mmoja. Alama ilimaanisha pete ya muhuri wa mfalme (BDB 368, KB 364, kama vile 41:42), au muhuri wa umbo la mcheduara ambao ulivaliwa katika shingo. Kila mmoja aliyekuwa mtu fulani katika Babeli ya kale alikuwa na moja kati ya mihuri hizi za mcheduara, ambayo iliyokuwa ikitumika katika eneo la sahihi yao (kama vile Strabo XVI, 1, 20).

Ule "mshipi" (BDB 836, KB 990) unatafsiriwa katika Targums kama "joho," lakini inavyoonekana inamaanisha kufanyia kazi kutumika kunyongea aidha katika pete au muhuri katika shingo ya mtu.

Fimbo (BDB 641, KB 573) ilikuwa zaidi kama fimbo ya kutembelea ikliwa na upindo wa kichwa cha kipekee. Mtu angeweza kujihisi hajavaa kama angetembea bila hii fimbo ya kutembelea katika zama za Yuda. Yeye kibinafsi alikuwa tayari kuachana na hizi 261 vifaa hivi vya muhimu kununua gharama/bei ya huyu kahaba! Tamari alivihitaji kama uthibitisho wa mwisho kwamba Yuda alikuwa baba wa uzao wake!

**38:19** Tamari kwa ghafla alikwenda nyumbani jambo linaloonesha kwamba Ukahaba haukuwa kusudio lake au mtindo wake wa maisha!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:20-23**
**[20] Yuda akapeleka yule mwana-mbuzi kwa mkono wa rafiki yake Mwadulami, ili aipate rehani mkononi mwa huyo mwanamke lakini hakumkuta. [21] Akauliza watu wa mahali pale, akisema, Yuko wapi yule kahaba aliyekuwapo Enaimu kando ya njia? Wakasema, Hakuwako hapa kahaba. [22] Akamrudia Yuda akasema, Sikumwona; hata na watu wa mahali hapo walisema, Hakuwako kahaba. [23] Yuda akasema, Na aichukue yeye, tusije tukatiwa aibu; tazama, nimempelekea mbuzi huyu, wala hukumkuta.**

**38:20 "Yuda akapeleka yule mwana-mbuzi kwa mkono wa rafiki yake Mwadulami"** Hira aliuliza maswali machache (kama vile mstari wa 21), lakini si mengi! Hii inaonekana kumaanisha hata siku hizi za leo ukaribu na ukahaba haionekani kuwa jambo linalopendelewa.

**38:23** Yuda anaona shaka kuhusu heshima yake na wala sio matendo yake yasiyo sahihi kwa upande wake. Kunaonekana kutokuwepo namna ya ukahaba kuwa kimaadili au kiroho (hata tabia ya ukahaba, mistari ya 21,22) tatizo kwa kipindi hiki na utamaduni huu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:24-26**
**[24] Ikawa baada ya miezi mitatu Yuda akapewa habari kwamba, Mkweo, Tamari, amefanya uzinifu, naye ana mimba ya haramu. Yuda akasema, Mtoeni ateketezwe. [25] Alipotolewa, alipeleka watu kwa mkwewe, akisema, Mimi nimepewa mimba na mtu mwenye vitu hivi. Akasema, Tambua basi, vitu hivi ni vya nani, pete hii, na kamba hii, na fimbo hii. [26] Yuda akavikiri, akasema, Yeye ni mwenye haki kuliko mimi, kwa kuwa sikumpa Shela, mwanangu. Wala hakumjua tena baada ya hayo.**

**38:24 "Mkweo, Tamari, amefanya uzinifu, naye ana mimba ya haramu"** Huu muundo wa WINGI unaotumika hapa, ambao unaonekana kumaanisha kwamba Tamari lazima alijiingiza katika matendo ya kujamiiana ya kujirudia rudia. Nini kuwepo kwa mtu kujitenga kunakopelekean na kushika mimba? Tabia zake zilitiliwa mashaka kwa asili ya kosa lake.

◙**"Yuda akasema, Mtoeni ateketezwe"** Yuda kama mkuu wa ukoo alikuwa bado anawajibika kisheria kwa adhabu ya mkwilima wake. Wazo la kumchoma linaonekana kuwa adhabu iliyozoeleka kwa mke asiye mwaminifu (kama vile Sheria ya Wa-Hammurabi, japo tofauti katika namna kidogo). Katika utungwaji wa sheria ya Musa ilikuwa ni watoto wa makuhani waliokuwa wakichomwa: watenda makosa wengine walikuwa wakipigwa mawe (kama vile Kumb. 22:20-24; Law. 21:9).

Yuda anatoa Amri kali.

1. mtoeni nje, BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (yaani nje ya nyumba yake kwenda katika jukwaa la wazi)
2. achomwe moto, BDB 976, KB 1358, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumiwa katika HALI YA KUSIHI (hili lilikuwa ni tendo la kijumuiya)

**38:25 "alipokuwa akitolewa nje"** Baadhi wanasema kwamba alisubiri mpaka wakati wa dakika ya mwisho akitarajia kwamba Yuda angefikiria juu ya hukumu yake. Wengine wanaelezea kwamba alisubiri mpaka wakati wa mwisho, wa wazi mbele ya umma kumfedhehesha Yuda. Kama ilivyo katika Agano la Kale na kwa namna hiyo, Agano Jipya nia ya mtu ya kisaikolojia haiwezi kueleweka.

◙**"Tambua basi, vitu hivi ni vya nani, pete hii, na kamba hii, na fimbo hii"** Tamari alimuuliza Yuda "kuchunguza" vile vitu (BDB 647, KB 699, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 25) kama anavyofanya katika mstari wa 26 (BDB 647, KB 699, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). KITENZI kilekile kimetumika hapa ambacho kinatumika katika mstari wa 37:32,33 na 42:7,8 (mara mbili).

Yuda ghafla anatambua mali zake mwenyewe na kutambua matendo sahihi japo kwa namna fulani matendo ya Tamari kisheria na mazingira ya kidini ya siku zake yalikuwa ya kutiliwa mashaka. Neno "haki" (BDB 842, angalia Mada Maalumu katika 15:6) hapa haimaanishi ukweli kwamba hana hatia katika jinsi alivyotenda, lakini alitenda katika njia ambazo zinakubalika zaidi kuliko Yuda. Haya ni matumizi yasiyo ya kithiolojia ya "haki" (kama vile 30:33). Alihatarisha mengi ili kuweza kutunza familia yake! Inavyoonekana yeye na Yuda walikuwa na zaidi ya mahusiano ya kingono. Hakikuwa kitendo cha tama ya mapenzi lakini kwa mawazo yangu, kitendo cha

imani ya kidini (angalia dokezo katika mstari wa 13). Kwa maoni yangu Tamari ni shujaa wa kweli wa simulizi hii yote (kama Rebeka alivyokuwa hapo mwanzo).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:27-30**
***27*** **Ikawa, wakati wake wa kuzaa walikuwapo mapacha tumboni mwake.** ***28*** **Ikawa alipokuwa akizaa, mtoto mmoja akatoa mkono, mzalisha akautwaa uzi mwekundu akaufunga mkononi mwake, huku akisema, Huyu ametoka kwanza.** ***29*** **Ikawa aliporudisha mkono wake, tazama, ndugu yake akatoka. Akasema, Mbona umepita kwa nguvu wewe? Mambo ya nguvu na yakuandame. Kwa hiyo jina lake likaitwa Peresi.** ***30*** **Akatoka ndugu yake baadaye, ana uzi mwekundu mkononi mwake; naye akaitwa jina lake Zera.**

**38:27“walikuwapo mapacha tumboni mwake”** Inanishangaza mimi ni kwa namna gani mara kwa mara wanawake wa mababa wa kiroho hawa katika Mwanzo ni tasa na alafu kwa namna gani mara kwa mara wanazaa mapacha. Mungu anatenda kazi kwa njia za kujirudia rudia! Vizazi vyote humilikiwa na yeye!

**38:28 “uzi mwekundu akaufunga mkononi mwake”** Sababu hasa ya uzi huu haijulikani. Yawezekana ilikuwa kitu kilichozoeleka kama vile kitu cha maana sahihi katika mkono au yawezekana ilikuwa kitendo cha kiutamaduni cha siku zake za nyakati hizo. Wengi wameelezea kwamba ilikuwa ni ishara au kielezeo cha ukombozi ambao ulifuatiwa nyakati zote za Agano la Kale (yaani Yosh. 2:18,21). Binafsi Napata shida kuhusu aina za istiari za ufasiri wa namna hii. Hakika ni maelezo ya kina ya kushuhudiwa na macho.

**38:29 “Peresi”** Jina hili (BDB 829 II) linamaanisha “uvunjaji” au “kutokeza mbele” (BDB 829 I).

**38:30 “Zera”** Jina hili (BDB 280 II) mana yake “kuinuka” au “kutokeza” (BDB 280) kutoka katika muundo wa KITENZI. Tanbihi ya AB , ukurasa wa 297, inasema maana inatoka “kug’aa” (BDB 280, inayopatikana tu katika Isa. 60:3) na ni katika mzizi ule ule wa kikonsonanti na huashiria uzi uliopakwa mg’ao wa rangi (pia angalia, Jewish Study Bible, ukurasa wa 78).

Utambulisho wa mzaliwa wa kwanza ulikuwa muhimu kwa sababu ya haki za urithi. Hatahivyo katika uzao maalumu (yaani uzao wa Kimasihi) wa uzaowa mababa wa imani ni dhahiri kwamba ni uchaguzi wa Mungu na sio mwanadamu! Mungu ana mpango wa ujumla wa ukombozi ambao unafanyiwa kazi katika familia ya Ibrahimu (kama vile 3:15; 12:3c; Kut. 19:5c; Isaya, Mika, Yona).

Katika namna ya kifasihi sura hii inafanya kazi kama kitabu cha Ruthi, kinachotoa vitu vya kiuzao kwa ajili ya uzao wa Yuda, baadaye familia ya Yesse, baba wa Daudi. Kulikuwa na Mataifa, hata Wakanaani katika uzao wa Mfalme Daudi (kama vile Ruthi)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini ni Muhimu kwamba Yuda awaache ndugu zake na kuelekea eneo la Kanaani kuelekea kusini?
2. Je ndoa ya Yuda kwa huyu mwanamke Mkanaani inashutumiwa katika maandiko?
3. Kwanini Yuda alikuwa mwenye hofu kumpa Tamari mwanawe wa tatu wa kiume?
4. Je tunawezaje kuyaelewa matendo ya Tamari? Nini kinaweza kuwa makusudi yao?
5. Je kuna umuhimu wowote kwenye uzi mwekundu unaotajwa katika mstari wa 28?

# MWANZO 39

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Mafanikio ya Yusufu huko Misri | Yusufu anakuwa Mtumwa huko Misri | Mafanikio, Majaribu na Kifungo cha Yusufu | Yusufu na Mke wa Potifa | Yusufu katika Siku za mwanzo huko Misri |
| 39:1-6a | 39:1-6a | 39:1-6 | 39:1-6a | 39:1-6a |
| | | | | Jaribu la Kumtongoza Yusufu |
| 39:6b-18 | 39:7-18 | 39:6b-18 | 39:6b-10 | 39:6b-10 |
| | | | 39:11-15 | 39:11-15 |
| | | | 39:16-18 | 39:16-20a |
| Yusufu Atiwa Gerezani | | | | |
| 39:19-23 | 39:19-20 | 39:19-23 | 39:19-23 | Yusufu kifungoni |
| | | | | 39:20b-23 |
| | 39:21 | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 39:1-6a**
**1 Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua**

**mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko. [2] Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi; naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. [3] Bwana wake akaona ya kwamba Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote mkononi mwake. [4] Yusufu akaona neema machoni pake, akamtumikia. Naye akamweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na yote yaliyomo akayaweka mkononi mwake. [5] Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivyomo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. Mbaraka wa Bwana ukawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba. [6a] Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu wala hakujua habari za kitu cho chote chake, ila hicho chakula alichokula tu.**

**39:1 "Potifa"** Jina hili, katika Misri **,** linaonekana kumaanisha " yeye ambaye mungu jua hutoa" (BDB 806). Huyu anatajwa katika Mwa. 37:36. Hili jina sawa na jina la kike (yaani, Potifera, BDB 806) baadae linaonekana katika Mwa. 41:45,50; 46:20.

◙**"akida wa Farao"** Wafasiri wengi wanadhani kwamba Farao aliyemweka Yusufu katika nafasi ya usimamizi wa Misri ni Hyksos au mfalme mchungaji mtawala (1720-1550 k.k., tazama History Channel Video: The Exodus Decoded). Hawa wavamizi wa kisemiti waliitawala Misri kwa miaka mingi sana. Wanadai kwamba ndio sababu mkuu wa askari huyu anayetambulika kama Mmisri (yaani mst. wa 2) aliwanalinganisha na mtawala msemitiki Hyksos.

◙ **"mkuu wa askari"** Kiuhalisia neno hili lina maana ya "towashi" (tazama muhtasari katika 37:36). Hata hivyo, kwa sababu ya 40:2 tunatambua kwamba Potifa alikuwa na mke. Ni kweli kwamba wanaume waliokuwa hanithi walioa, lakini sio desturi. Hili neno liikuja kutumika kama cheo chenye madaraka rasmi na inaonekana kuwa njia iliyotumika katika kifungu hiki.

◙ **"Farao"** Hiki ni cheo cha wafalme wote wa Misri (BDB 829, kifasihi "nyumba kuu"). Wafalme wa Misri iliaminika kuwa ni wana wa mungu jua, Rejea "nyumba kuu" inahusu kasri la kifalme au hekalu ambalo lilimaanisha dunia hii inaiabudu miungu ya Misri.

◙ **"msimamizi"** Kwa uhalisia hii ina maana "muuaji" au "mchinjaji" (tazama muhtasari katika 37:36). Wengine wanadai kwamba hili neno linalifanana sana na neno mtendaji. Hata hivyo, neno hili natumika, katika Biblia na katika nyenzo za ziada ki-Biblia, hili linaonekana kuhusiana na nafasi ya kijeshi inayohusika na u linzi wa mfalme. Hii ingeweza kumaanisha kwamba Potifa alikuwa wa muhimu sana, mwenye ushawishi, na mtu tajiri.

◙ **"Waishmaeli"** Kumekuwa na maswali mengi juu ya utambulisho wa hawa wafanya biashara walio hamahama. Katika kitabu cha Mwa. 37:36 kwa vyo vyote hawa waliitwa Wamidiani au Wamedi (tazama muhtasari 37:35).Makundi haya mawili yanatambulishwa kwenye kitabu cha Mwa. 37:28 na Amu. 8:22, 24.Walikuwa na muunganiko kati ya Ishimaili na uzao wao.

**39:2 "BWANA akawa pamoja na Yusufu"** Ni muhimu ki**t**hiolojia kwamba ni moja ya neno zuri mno lililotokea mara nyingi YHWH katika sehemu hii ya kitabu cha Mwanzo. Kama ilivyo kweli hili ni tukio tu katika maelezo yenye kumhusu Yusufu. Pia tambua kuwa hili linazungumzia matukio nje ya Kanaani. YHWH hana mipaka katika zuiliwi Nchi ya ahadi (yaani, Mahubiri ya Stephano katika Mdo. 7).

Hiki kifungu "BWANA akawa pamoja na Yusufu" kinaonekana kujirudia rudia (kama vile 39:3, 21, 23) katika sura hii na baraka ambazo zilizongezeka kwake kwa sababu ya hili imekuwa sehemu kubwa ya habari. Mungu, si Yusufu, ndiye kiini cha mhusika!

◙ **"naye akasitawi"** Yusufu alikuwa mmenye "kusitawi;" (BDB 852 II, KB 1026, *Hiphil* ya *K*AULI ENDELEVU) na wale wote waliomzunguka pia walifanikiwa na wakawa nwenye kustawi. Hakika hili ndicho kilichofanyika kwa uwepo wa Yakobo ndani ya nyumba ya Labani. Potifa alishika muktadha Baraka za maana kwa uwepo wa Yusufu (kama vile mst. 3).

KITENZI cha *Hiphil* na *Qal* kinamaanisha kukamilisha kazi ya mafanikio (sio mbali na baraka za kimwili).

1. Mwa. 24:21,40 (*Hiphil*)
2. Amu. 18:5 (*Qal*)
3. 2 Nya. 26:5 (*Hiphil*)
4. Neh. 1:11; 2:20 (*Hiphil*
5. Isa. 53:10; 55:11 (*Qal*)
6. Dan. 8:12, 24; 11:36 (*Qal*)

Kuwa makini na Fafanuzi za lugha ya Kiingereza na vidokezo angalizi vya neno la kujifunzia biblia!

◙ **"naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri"** Hii ni tofautishi ya ukweli kwamba hakuwa kwenye mkono dhalimu au kwamba aliishi kwenye nyumba ya bwana wake badala ya kuishi kwenye makazi ya watumishi.Yusufu alikuwa anaamika sana katika nyumba ya Potifa.

**39:3 "Bwana wake akaona ya kwamba BWANA yu pamoja naye "**Potifa hakumweka kirahisi kwenye usimamizi kwa sababu ya uwezo wake wa kusimamia,lakini kwa sababu ya muunganiko pekee wa Baraka za Mungu.Potifa alifanya hivi hasa hasa kwa faida yake binafsi na sio kwa mtazamo wa kidini.

**39:4** Huduma ya Yusufu inaelezwa katika njia mbili.

1. "awe msimamizi," BDB 1058, KB 1661, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU,inatumika kwa cheo cha juu cha usimamizi,kama vile 2 Sam. 13:17,18; I Fal. 10:5;2 Fal. 4:43; 6:17
2. "na yote yaliyomo," BDB 823, KB 955, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile.2 Fal. 25:23

Leo tunaweza kumuita " msimamizi msaidizi" au "katibu mtendaji" Katika vitabu/maandiko mbalimbali ya Misri kwa wakati huo yana maana "msimamizi juu ya nyumba "

**39:5 "Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu"** Huu unaonekana ni ukweli kupitia kipindi cha agano la kale.Kuna muunganiko kati ya Baraka za kimwili na mmoja mwenye uhusiano na watu wa agano (kama vile Mwa. 12:3; 30:27).

**39:6 "Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu wala hakujua habari za kitu cho chote chake, ila hicho chakula alichokula tu."** Baadhi ya wana historia wanaeleza ya kwamba kulikuwa na utengano wa chakula hasa hasa kati ya wamisri na wageni wote kutokana na msingi na mwongozo wa kidini,kama vile leo Wayahudi na wageni wote.Kwa vyovyote huu ni msingi wa jambo hili la kipee lisiloaminika, lakini utofauti wa utamaduni huu ulikuwa wazi kwenye jamii hii ya kimisri (kama vile Mwa. 43:32).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 39:6b-18**

**7 Ikawa baada ya mambo hayo, mke wa bwana wake akamtamani Yusufu, akamwambia, Lala nami. 8 Lakini akakataa, akamwambia mke wa bwana wake, Tazama, bwana wangu hajui kitu kilichowekwa kwangu nyumbani, na vyote alivyo navyo amevitia mkononi mwangu. 9 Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu cho chote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu? 10 Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku, lakini hakumsikia alale naye, wala aongee naye. 11 Ikawa, siku moja, akaingia nyumbani atende kazi yake, wala hapakuwa na mtu katika watu wa nyumbani humo ndani; 12 huyo mwanamke akamshika nguo zake, akisema, Lala nami. Yusufu akaiacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia, akatoka nje. 13 Ikawa alipoona ya kwamba amemwachilia nguo yake mkononi mwake, naye amekimbia nje, 14 akawaita watu wa nyumbani mwake,**

**akasema nao, akinena, Angalieni, ametuletea mtu Mwebrania atufanyie dhihaka. Ameingia kwangu, ili alale nami, nikalia kwa sauti kuu. [15] Ikawa, aliposikia ya kuwa nimepaza sauti yangu na kulia, aliiacha nguo yake kwangu, akakimbia, akatoka nje. [16] Basi akaiweka ile nguo kwake hata bwana wake aje nyumbani. [17] Naye akamwambia kama maneno hayo, akisema, Yule mtumwa Mwebrania uliyemleta kwetu, aliingia kwangu anidhihaki. [18] Ikawa nilipopaza sauti yangu, nikalia, akaacha nguo yake kwangu akakimbia nje.**

◙ **"Na Yusufu alikuwa mzuri wa sura na umbo"** Hii ni tungo sawa ("mzuri" BDB 421, "sura" BDB 1061, "umbo," BDB 909) inatumika kumwelezea Raheli mama yake (kama vile Mwa. 29:17). Kulikuwa na wanaume wengi wazuri walioelezewa kwenye Agano la Kale waliokuwa na muunganiko na ukoo wa Masihi. Tungo hii pia imetumika kuunganisha Daudi na mwana wake Absalomu. Hata Sauli anaelezewa kuwa ni mrefu, mwanaume mzuri. Kumbuka Mwanamke mrembo/Mwanaume mzuri hubadilika kutoka tamaduni hadi tamaduni na zama hadi zama. Muonekano wa kimwili wa Yusufu ilikuwa ni chanzo cha tatizo lake na mke wa Potifa

**39:7 "Ikawa baada ya mambo hayo, mke wa bwana wake akamtamani Yusufu "** Tunafahamu kutoka kwenye jamii inayoingiliana ya kwamba yawezekana kwa mwanamke wa kimisri kwenye jamii yao kwamba kulikuja kuwa na mithali ya kiutamaduni iliyounganishwa na anasa na upotovu wa maadili wa wanawake wa Kimisri. Mke wa Potifa alikuwa na akili sana kwa namna alivyomkaribia Yusufu. Mpango wake ulionekana alikuwa anavuta muda zaidi na inaonekana alijitongozae (kama vile mst. 10).Hii lazima ilimpa shinikizo kubwa sana kwa kijana mdogo wa kiebrania kwa mwanamke mlaghai kumkaribia siku baada ya siku na ofa ya ngono. Kuna utofauti mkubwa na wa wazi kati ya matendo ya Yuda kwenye sura ya 38 na Yusufu kwenye hii sura!

**39:8-9** Yusufu alionekana kufanya jambo lenye mantiki na la kufaa sana kwa kujipendekeza kwake kwenye mstari huu. Kwanza inaunganishwa na ukarimu wa Potifa jirani naye na, inaonyesha njia, sehemu yake ya pekee haitakiukwa,Yusufu aliona kama Mungu amehusika kwenye maisha yake ya ngono kama alivyohusika kwenye kila eneo la maisha yake . Ni ngono ya uzinzi,kwenye uchaguzi wake,sio tu ni dhambi dhidi ya Potifa na mke wa Potifa ,lakini kwa hakika ni dhidi ya *Elohim*.Kumbuka kwamba alitumia kwa ujumla jina la Mungu (yaani, *Elohim*) kwa sababu mwanamke huyu ni dhahili hakuwa mcha Mungu mtu mjuzi na hakulitambua jina la agano kwa Mungu, YHWH (tazama mada maalumu 12:1)

**39:10 "Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku "**Huu msukumo wa ngono uliendelea kurudiwa kila mara au ni wazi lazimisho la ngono kutoka kwa huyu mwanamke. Yusufu alikuwa ni mtumwa! Hakuwa na uwezo wa haki kushughulikia matendo yake mwenyewe!

**39:11** Kutoka kwenye kidokezo cha maandiko, alipanga kuwaweka nje watumishi wengine muda ambao Yusufu ataingia kuendelea na shughuli zake za kawaida. Waalimu wa sheria wa kiyahudi wanasema kwamba hii ilikuwa ni siku ya sikukuu ya kimisri na akadai kuwa anaumwa ili kubakia nyumbani na kumtongoza Yusufu.

**39:12 "akaiacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia, akatoka nje."** Wengine wanalaumu Yusufu kwa kuwa ukimya kwa sababu aliiacha nguo yake (BDB 93, kulazimishwa kutii kusiko kuwa na mashaka, UBS *A Handbook on Genesis*, ukr. 895,inadai kwamba watumishi wa Misri kwenye siku hii hakuvaa mwili mzima , isipokuwa shati fupi), lakini alitakiwa kufanya nini?! Hii inakubalika, jibu la kiroho la majaribu ya kumtamani mwanamke (kama vile 2 Tim. 2:22; 2 Pet. 1:4).

**39:13-18** Mistari hii unahusu malalamiko ya mke wa Potifa kwake kwa baadhi ya watumishi wa kimisri na kwa mme wake.

**39:14 "akawaita watu wa nyumbani mwake, akasema nao"** Lazima Walikuwa jirani nae,lakini sio ndani ya nyumba. Kuna vitu vingi kwenye maelezo yake ambavyo tunapaswa kuvijua.

1. Alimlaumu mme wake kwa kumleta mtumwa wa kiebrania ndani ya nyumba (kama vile mst. 19)

2. Alifanya fedheha kwasababu ni mwebrania

Ni wazi kutoka kwenye kumbukumbu za Kimisri wao walijihisi ni wakuu zaidi ya watu wageni.

◙ **"Mwebrania"** Neno kwa "Mwebrania" (BDB 720) ni moja lenye uwezekano wa asili mbili: (1) linatokana na Eberi, Uzao ambao familia ya Ibrahimu ilitokana (kama vile. Mwa. 11:16,lilitumiwa na Ibrahimu kwenye 14:13 na uzao wake (kama vile. 39:14,17; 40:15; 41:12; 43:32) au (2) kwa ujumla jina hili lilitokana na jamii ya watu wanao hama hama kutoka ng'ambo ya mto unaoitwa Habiri (mhamiaji) kwenye nyaraka za Tel El Armarna.

◙**"atufanyie dhihaka"** Neno la kiebrania "atufanyie dhihaka" (BDB 850, KB 1019, *Piel TUNGO* YA KITENZIJINA HALISI) kwenye aya hii inaonekana ni mbinu ya tamaduni kwa "kujaribu kutufanyia dhihaka ya kingono" (kama vile 26:8). Hatari ni kwamba Yusufu alifanya hili kwake na likaendelea kwa watu wengine kwenye nyumba ya Potifa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 39:19-23**

**[19] Ikawa bwana wake aliposikia maneno ya mkewe aliyomwambia, akisema, Mtumwa wako amenitendea mambo kama haya, hasira yake ikawaka. [20] Bwana wake akamtwaa Yusufu, akamtia gerezani, mahali walipofungwa wafungwa wa mfalme, naye akawamo humo gerezani. [21] Lakini Bwana akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza. [22] Mkuu wa gereza akawatia mkononi mwa Yusufu watu wote waliofungwa, waliomo gerezani; na yote yaliyofanyika humo ndiye aliyeyafanya. [23] Wala mkuu wa gereza hakuangalia neno lililoko mkononi mwa Yusufu; kwa kuwa Bwana alikuwa pamoja naye. Bwana akayafanikisha yote aliyoyafanya**

**39:20 "Bwana wake akamtwaa Yusufu, akamtia gerezani"** Adhabu ya kawaida kwa aina ya uhalifu huu ni kifo (Toleo la IVP *Bible Background Commentary*, ukr. 71). Inaonekana kwamba Potifa alikuwa na baadhi ya mashaka kuhusu ukweli wa maelezo ya mke wake. Nina uhakika kwamba kwenye hili jambo ndani ya maisha ya Yusufu,hata kama ana imani kubwa kwa Mungu, lazima alistaajabu ni nini kimetokea (kama vile Mwa 40:15)!

◙**"walipofungwa wafungwa wa mfalme, naye akawamo humo gerezani"** Hili ni neno lisilo la kawaida kwa Gereza. Inaonekana linatoka kwenye asili ya "akawamo humo" (kutoka kwenye kitabu cha Wimb 7:2) au "waliomo" (BDB 690, inaonekana pekee kwenye 39:20-23 na 40:3,5) na baadhi ya wafasiri wanadai lilikuwa ni gereza la mduara, wengine wanaamini kuwa ni jengo maalumu la aridhini chini ya ulinzi wa kapteni (yaani Potifa). Kama hii ni kweli tunaweza kuona wazi namna Yusufu alivyohamishwa kutoka katika nyumba ya bwana wake hadi gereza la bwana wake ambapo sio mbali kwa urefu.

◙"**Mkono wa Mungu usioonekana"** ulifanya kazi mwanzo wa kila hatua ya mpango wake.Yakobo alibadilishwa kabisa na imani yake juu ya YHWH tangu sura ya 37.Tunatambuwa Mungu anaathiri tabia na mienendo yetu!

**39:21-23** Uwepo wa Mungu bado uliendelea kuwa na Yusufu kwa upekee na, dhahili, kwa njia inayoonekana wazi. Hii haimaanishi kwamba hakuna magumu sana tunayopitia katika mazoea ya mwili na fahamu, lakini uangalizi ya Mungu ni wa wazi kwake.

**39:23** Ufafanuzi huu ni sawa na wa mst. 6. Yusufu alikuwa makini kwa kila kitu.Alizawadiwa usimamizi na baadae tutajifunza, mfasiri wa ndoto.

# MWANZO 40

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yusufu anafasiri anafasiri Ndoto | Ndoto ya Mfungwa | Yusufu, Mfasiri Ndoto | Yusufu anaifasiri Ndoto ya Mfungwa | Yusufu anaifasiri ndoto ya Watumishi wa Farao |
| 40:1-8 | 40:1-8 | 40:1-8 | 40:1-4 | 40:1-4 |
| | | | 40:5-7 | 40:5-8 |
| | | | 40:8a | |
| | | | 40:8b | |
| 40:9-15 | 40:9-15 | 40:9-15 | 40:9-11 | 40:9-15 |
| | | 40:12-15 | | |
| 40:16-19 | 40:16-19 | 40:16-19 | 40:16-17 | 40:16-19 |
| | | | 40:18-19 | |
| 40:20-23 | 40:20-23 | 40:20-23 | 40:20-23 | 40:20-23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:1-8**

**[1] Ikawa, baada ya mambo hayo, mnyweshaji wa mfalme wa Misri, na mwokaji wake, wakamkosa bwana wao, mfalme wa Misri. [2] Farao akawaghadhibikia maakida wake wawili, mkuu wa wanyweshaji na mkuu wa waokaji. [3] Akawatia katika lindo nyumbani mwa mkuu wa askari, humo gerezani, mahali alipofungwa**

**Yusufu. [4] Mkuu wa askari akamwekea Yusufu watu hao, naye akawahudumu, nao wakakaa siku kadha wa kadha katika kifungo. [5] Wakaota ndoto wote wawili, kila mtu ndoto yake usiku mmoja, kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake, mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa Misri waliofungwa gerezani. [6] Yusufu akawajia asubuhi, akawaona wamefadhaika. [7] Akawauliza hao maakida wa Farao, waliokuwa pamoja naye katika kifungo, nyumbani mwa bwana wake, akisema, Mbona nyuso zenu zimekunjamana leo? [8] Wakamwambia, Tumeota ndoto wala hapana awezaye kuifasiri. Yusufu akawaambia, Kufasiri si kazi ya Mungu? Tafadhalini mniambie**.

**40:1 "mnyweshaji"** Hili neno linatokana na KITENZI "kunywa" (BDB 1052). Mara nyingi hili kinatafsrika kama "mhudumu mkuu wa kutuza vinywaji na kuandaa meza." Tafsri ya Kiaramu ya eneo hili ni "mnyweshaji mkuu." Kuna marejeleo mengine mawili katika utawala huu ulio ndani ya Biblia: (l) katika Neh. 1:11 (BDB 1052 I) na (2) neno "Rabshakeh" (BDB 913 II, kama vile II Fal.18:17,19,26,27,28,37; 19:4,8; Isa. 36:2,4,11,12,13,22; 37:4,8). Kwa uwazi kabisa huyu alikuwa mtawala wa mahakama ya juu sana na mtu mwenye kuaminiwa sana. Huyu ahakujaribiwa katika kumpa mfalme chakula tu, bali pia angetoa ushauri binafsi. Mara kwa mara huyu angekuwa mlinzi wa kila eneo ambalo lingemjeruhi ama kumuua mfalme. Huyu alikuwa mlinzi wa upishi!

◙ **"mwokaji wake"** Huyu mwokaji (BDB 66, KB 78, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU) pia alikuwa kiongozi wa muhimu sana na mtu wa karibu sana katika Mambo ya Mahakama za kale. Hili ni jambo la kweli katika Misri ambapo tunazifahamu aina 38 za keki ambazo mara nyingi ziliokwa pamoja na aina 57 za mikate. Baadhi ya mikate ilipakwa rangi kwa namna tofauti tofauti na kutengenezwa kwa nafaka mbalimbali na katika mionekano ya maumbo mbalimbali zikionekana kama wanyama na sifa za vitu mbalimbali vya Misri.

◙ "**wakamkosa bwana wao, mfalme wa Misri"** Ni kwa namna gani walikosea haielezwi. Hii inaweza kuwa ni pamoja na (1) ubora wa kiwango cha chakula na /au kinywaji au (2) ushauri wao, au ulegevu wa ushauri huo. Hiki KITENZI "wakamkosa" (BDB 306, KB, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kina uwanja mpana wa maana ("kukosea kufunga bao," "dhambi," "kuenenda visivyo," kama vile 39:9; 42:22; 43:9). Rashi (Mtoa maoni wa Kiyahudi wa Zama za Kati) anasema kwamba makosa yaliyokuwa wakizungumziwa yalikuwa: (1) kukutwa wakiifunguliani hewani divai ya mfalme na (2) mkate wa mfalme. Hata hivyo, hii fasiri ya kudhaaniwa tu ama ya kidesturi.

**40:2 "Farao akawaghadhibikia"** Hiki KITENZI (BDB 893, KB 1124, *Qal cha* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) mara nyingi kinatumika kuelezea

1. hasira ya Mungu, Law. 10:6; Hes. 16:22; Kumb. 1:34; 9:19
2. hasira ya mwanadamu
   a. Musa, Kut. 16:20; Law. 10:16; Hes. 31:14
   b. Wakuu wa vikosi vya majeshi ya Wafilisti, I Sam. 29:4
   c. Naamani, II Fal. 5:11
   d. Mwana wa Mungu, II Fal. 13:19
   e. Ahasuero, Esta 1:12
   f. Walinzi wa mfalme, Esta 2:21

Neno hili linadokeza juu ya ile hasira iliyo katika utendaji.Hii ni tofauti na neno linalotokana na 39:19, "hasira yake ikawaka" (BDB354, KB 351).

**40:3 "Akawatia katika lindo nyumbani mwa mkuu wa askari"** Neno "mkuu wa askari," ni cheo kinachomrejerea Potifa (kama vile 37:36; 39:1). Potifa alikuwa mkuu wa gereza (BDB 978) aliyemtia Yusufu gerezani. Ni wazi kwamba hawa wafungwa kisiasa wangeonywa kwa mara ya mwisho kwa sababu kwa sababu kulikuwa na uwezekano mkubwa wangerejeshwa kwa mara nyingine na wangekuwa maadui wakubwa ndani ya mahakama.

◙ **"alipofungwa"** Hili neno "alipofungwa" kiuhalisia ni "kuweka mipaka" (BDB 63, KB 75). Yusufu huenda aliwekewa mipaka kwa kufungwa minyororo (kama vile Zab. 105:18) kwa kindi cha wakati na ijapokuwa Mungu alikuwa pamoja naye, jambo hili lilikuwa gumu, maisha ya ukatili. Hatufahamu ni kipindi gani alichokaa kifungoni—baadhi ya watoa maoni wanasema ni kama miaka 10 (yaani, "wakati mwingine" wa mst. 4).

**40:4 "Mkuu wa askari akamwekea Yusufu watu hao"** Mtu huyu pengine angewataka wakuu hawa wawatunze vema na Yusufu alionekana kuwa mtu mkamilifu katika kazi. Mtu anashangaa ikiwa mtu huyu aliitwa "mkuu wa askari" hili linarejelea

1. Potifa, 37:36; 39:1
2. Mkuu wa gereza, 39:21-23

Inawezekana kuwa kulikuwa na gereza maalum chini ya uangalizi wa Potifa, lakini alimwachia madaraka "mkuu wa gereza" ambaye alimwachia madaraka Yusufu.

Mstari huu unaweka vema mpangilio kifasihi wa hatua ya pili ya Yusufu ya kupata neema ya kufahamika (yaani, ufasiri wa ndoto). Mara kwa mara YHWH alijifunua mwenyewe (ama tMalaika wa Bwana) kwa watu wake kupitia maono, bali watu wasiokuwa wa ahadi za Ibrahmu ,mara alitumia nyingi alitumia ndoto (kama vile 20:3; 31:24; 41:1; Danieli 2).

**40:6-7 "Yusufu akawajia asubuhi, akawaona wamefadhaika"** Hapa ni dhahiri kwamba kwa wakati huu Yusufu alikuwa huru katika kifungo chake na pia alikuwa akiwahudumia watu hawa na alikuwa akiwahudumia kimwili, pamoja na kihisia ("walikuwa wamehuzunika," BDB 277 II, KB *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU), hali.

**40:8** Tena, Yusufu alifunua mtazamo muhimu wa maisha (yaani kwamba Mungu yu katika utawala wa utawala mambo yote, zikiwemo ndoto (kama vile 41:16,25,28; Dan. 2:27-28,45). Kutokana na maisha yake tunafahamu kwamba ndoto ilikuwa njia muhimu sana ya Mungu kuongea naye kama kijana mdogo (kama vile Mwanzo 37), ingwa ndoto hii ilimsababisha kukataliwa na watu wa nyumbani kwao.

Hiki KITENZI "kuambia" (kifasihi. "eleza tena," BDB 707, KB 765, *Piel* ni cha KAULI SHURUTISHI) pia kinaufungua msrari unaofuatia ("akawaambia," *Piel* cha KAULI SHURUTISHI, kama vile 37:10)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:9-15**

**[9] Mnyweshaji mkuu akamhadithia Yusufu ndoto yake; akamwambia, Katika ndoto yangu nimeota, uko mzabibu mbele yangu. [10] Na katika mzabibu mlikuwa na matawi matatu, nao ulikuwa kana unamea, unachanua maua, vishada vyake vikatoa zabibu zilizoiva. [11] Na kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu, nikazitwaa zabibu, nikazikamua katika kikombe cha Farao, nikampa Farao kikombe mkononi mwake. [12] Yusufu akamwambia, Tafsiri yake ndiyo hii. Matawi matatu ni siku tatu. [13] Baada ya siku tatu Farao atakiinua kichwa chako, atakurudisha katika kazi yako; nawe utampa Farao kikombe mkononi mwake, kama desturi ya kwanza, ulipokuwa mnyweshaji wake. [14] Ila unikumbuke mimi, utakapopata mema, ukanifanyie fadhili, nakuomba, ukanitaje kwa Farao, na kunitoa katika nyumba hii. [15] Kwa sababu hakika naliibiwa kutoka nchi ya Waebrania, wala hapa sikutenda neno lo lote hata wanitie gerezani.**

**40:9 "mzabibu mbele yangu"** Watoa maoni wengi wamedai kwamba hii ilikuwa ndoto ya kihistoria kwa sababu Mzabibu divaia iliyotiwa chachu ilikuwa haitumika katika Misri. Hata hivyo, inaonekweli kwamba divai haikuwa kinywaji cha kawaida ndani ya nchi ya Misri, bali ilitumika katika madaraja ya kikuhani na kifalme (tazama *Manners and Customs of the Bible by James M. Freeman*, uk. 45).

**40:11 "nikazikamua"** Hiki KITENZI (BDB 965, KB 1315, *Qal* cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kwa mshangao kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale.

**40:13** Huyu mnyweshaji atarejeshwa katika nafasi yake ya kumhudumia mfalme. Hili neno linalotafsriwa "taratibu zako za awali" kiuhalisia ni neno "hukumu" (BDB 1048), lakini linatumika mara chache katika maana isiyo ya kithiolojia. Mara nyingi linatafsriwa kama "hukumu" ama "haki."

**40:14-15** Kwa huduma na wema wa Yusufu, aliomba nafasi ya upendeleo kwa mnyweshaji. Alitoa maelezo kuhusu ukosefu wa haki katika hali iliyomkumba na kumuomba Farao atoe suluisho. Yusufu hakutakiwa kuchukuliwa kama mfungwa wa Farao kwa sababu walichukuliwa mateka kama mtumwa.

**40:15** Kitu alichokifikiri Yusufu kuhusu kusalitiwa kwake na ndugu zake kinaelezwa katika "kutekwa" (kifasihi. "kuchukuliwa"). Jambo hili linatiwa uchochezi zaidi katika andiko kupitia KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU ya mzizi ule ule (BDB 170, KB 198).

◙ **"kutoka katika nchi ya Waebrania"** Kifungu hiki kingekuwa

1. mhariri anayefuatia/mwandishi mwenye kuongeza maoni haya
2. kingetumika katika maanaya nchi ambapo mababa wa wa imani walimwacha (kama hili ni kweli, kisha Kiebrania kimefafanuliwa tena na kutumika katika maana yenye mipaka sana)

◙**"gerezani"** Neno hili (BDB 92) Ni neno lile lile lililotumika kumaanisha tenki la maji lilolokavu (kama vile 37:24)ndugu zake walilomtupamo huko Kanaani. Halikuwa akiuzwa kutoka shimo moja hadi lingine! Hili neno linatumika kuhusu gereza katika Kut. 12:29; Yer. 37:16, na hapa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:16-19**
[16] **Mkuu wa waokaji alipoona ya kwamba hiyo tafsiri ni ya mema, akamwambia Yusufu, Mimi kadhalika nilikuwa katika ndoto yangu, na tazama, ziko nyungo tatu za mikate myeupe juu ya kichwa changu.** [17] **Na katika ungo wa juu, mlikuwa na kila namna ya chakula kwa Farao, kazi za mwokaji; ndege wakavila katika ungo juu ya kichwa changu.** [18] **Yusufu akajibu, akasema, Tafsiri yake ndiyo hii Nyungo tatu ni siku tatu.** [19] **Baada ya siku tatu Farao atakiinua na kukuondolea kichwa chako, na kukutundika juu ya mti, na ndege watakula nyama yako.**

**40:16** "**Mimi kadhalika nilikuwa katika ndoto yangu, na tazama, ziko nyungo tatu za mikate myeupe juu ya kichwa changu**" Neno la Kiebrania la "mikate myeupe" (BDB 301 I) ni neno hadimu sana ambalo linatokana na mzizi wa Kiaramu na Kiarabu ambao unamaanisha "nyeupe" (NIDOTTE, juzuu 2, uk. 54). Hili linaweza kurejelea juu ya ungo wa mbao ambapo ndege wangetumia kulia mkate kutoka juu na pembeni (kama vile mstari wa17).

Inatia shauku kuelewa kwamba katika Kanaani wanawake walikuwa wakibeba mizigo mizito juu ya vichwa vyao, lakini katika Misri wanaume ndio waliokuwa wakibeba mizigo mizito juu ya vichwa vyao, ambapo wanawake walibeba mizigo juu ya mabega yao. Hii inaonyesha historia ya pekee ya maelezo haya.

**40:17 "kila namna ya chakula kwa Farao, kazi za mwokaji"** Hii ni kweli kabisa kihistoria kama tulivyojifunza kutoka katika kumbukumbu za Kimisri kwamba kulikuwa na aina za keki 38 na aina za mikate 57 iliyojulikana katika Misri (angalia maelezo katika mst. wa 1).

**40:19 "Farao atakiinua na kukuondolea kichwa chako"** Ni dhahiri kutokana na mst. ya 13-19 kwamba kulikuwa na ufasiri unajirudia rudia mara kwa mara wa kifungu hikie "atakiinua kichwa chako" (BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Katika mst. wa 13 kifungu hiki kinamaanisha "kuinua kichwa kwa ajili ya kuetenda wema" (kama vile Hes. 6:26). Hii ni nahau ya neno "kuachilia" (kama vile II Fal. 25:27). Katika mst. wa 19 neno hili linamaanisha "kukiinua kichwa cha mtu ili kukikatilia mbali" (BDB 671, 3,b).

Lakini pia ni dhahiri kwamba mst. wa 19 hauzungumzii kuning'inia kwa sababu ni vigumu kumning'iniza mtu ambaye kichwa chake kimekatiliwa mbali! Huku kununing'inizwa kwa uwazi kunamaanisha kutundika ama kuwekwa hadhrani baada ya kuwa amekufa (kama vile Yos. 8:29; I Sam. 31:9-10; II Sam. 4:12). Hii inaonekana kuwa nia ya moja kwa moja ya huku kuwekwa hadharani kama ambavyo kuelezwa kutoka katika Kut. 21:23. Hili wazo kwamba mwili wa mtu huyu ungeliwa na ndege lingekuwa jamba la kutisha sana kwa Mmisri ambaye alisistizwa kutiwa manukato baada ya kufariki ili kuutunza mwili wake. Mtu anashangaa kama kuna uhusiano kati ya

1. "gereza" (kifasihi. "zunguka") la 39:20-23; 40:3,5
2. "gereza la chini ya ardhi" (kifasihi. "shimo") la 40:15
3. "kuinua"

Je! Gereza linaweza kuwa na shimo kubwa linalozunguka chini ya ardhi?

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:20-23**

[20] **Ikawa siku ya tatu, siku ya kuzaliwa kwake Farao, akawafanyia karamu watumwa wake wote; akakiinua kichwa cha mkuu wa wanyweshaji, na cha mkuu wa waokaji, miongoni mwa watumwa wake.** [21] **Akamrudisha mkuu wa wanyweshaji katika kazi yake ya kunywesha, naye akampa Farao kikombe mkononi mwake.** [22] **Bali akamtundika mkuu wa waokaji, kama Yusufu alivyowafasiria.** [23] **Lakini huyo mkuu wa wanyweshaji hakumkumbuka Yusufu, alimsahau**

**40:20-23** Huu ni utimilifu wa fasiri ya Yusufu na mnyweshaji mkuu kushindwa kukumbuka (BDB 269, KB 269, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU).Tena, hakuna mtu isipokuwa YHWH ndiye awezaye kumuokoa Yusufu. Mungu ndiye mtunzaji pekee!

Tena, hiki KITENZI "kuinua" kinatumika katika njia tofauti (likiwa na utata fulani, kama vile mst. wa 20).

## MASWALI YA MJADALA YA SURA ZA 39-40

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Potifa alimwinua Yusufu?
2. Ni kwa namna gani Yusufu alitofautishwa na Yuda katika sura ilizotangulia?
3. Je! Yusufu alitambua kwamba akitiwa gerezani kwa kusudi fulani?
4. Je! Mara nyingi Mungu huongea na watu kupitia ndoto ama ndoto fulani tu? Je! uwezo wa kufasiri ndoto ni karama ya kawaida ya kiroho ama ina mipaka, ni uzoefu wa Agano la Kale?

# MWANZO 41

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Ndoto ya Farao | Ndoto ya Farao | Ngazi ya Yusufu | Yusufu anaitafasiri Ndoto ya mfalme | Ndoto ya Farao |
| 41:1-8 | 41:1-8 | 41:1-8 | 41:1-8 | 41:1-4 |
| | | | | 41:5-7 |
| | | | | 41:8-13 |
| 41:9-13 | 41:9-13 | 41:9-13 | 41:9-13 | |
| Yusufu anaitafasiri Ndoto | | | | |
| 41:14-24 | 41:14-24 | 41:14-21 | 41:14-15 | 41:14-16 |
| | | | 41:16 | |
| | | | 41:17-24 | 41:17-24 |
| 41:25-36 | 41:25-36 | 41:25-36 | 41:25-32 | 41:25-32 |
| | | | 41:33-36 | 41:33-36 |
| | Yusufu anainuliwa Kuwa kiongozi | | Yusufu anainuliwa kuwa gavana juu ya Misri | Kuinuliwa kwa Yusufu |
| 41:37 | 41:37-45 | 41:37-45 | 41:37-46a | 41:37-43 |
| Yusufu anafanywa Kuwa mtawala huko Misri | | | | |
| 41:38-45 | | | | |
| | | | | 41:44-45 |
| 41:46-49 | 41:46-49 | 41:46-49 | 41:46b-49 | 41:46-49 |
| Wana wa Yusufu | | | | Watoto wa Yusufu |
| 41:50-52 | 41:50-52 | 41:50-52 | 41:50-52 | 41:50-52 |
| 41:53-57 | 41:53-57 | 41:53-57 | 41:53-57 | 41:53-57 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:1-8**
**[1] Ikawa, mwisho wa miaka miwili mizima, Farao akaota ndoto; na tazama, amesimama kando ya mto. [2] Na tazama, ng'ombe saba wazuri, wanono, walipanda kutoka mtoni, wakajilisha manyasini. [3] Na tazama, ng'ombe saba wengine wakapanda nyuma yao kutoka mtoni, wabaya, wamekonda, wakasimama karibu na wale ng'ombe wengine ukingoni mwa mto. [4] Kisha hao ng'ombe wabaya waliokonda wakawala wale ng'ombe saba wazuri, wanono. Basi Farao akaamka. [5] Akalala, akaota ndoto mara ya pili. Tazama, masuke saba yalimea katika bua moja, makubwa, mema. [6] Na tazama, masuke saba membamba, yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakatokeza baada yao. [7] Kisha hayo masuke membamba saba yakayala yale masuke saba makubwa yaliyojaa. Basi Farao akaamka, kumbe! Ni ndoto tu. [8] Hata asubuhi roho yake ikafadhaika; akapeleka watu kuwaita waganga wote wa Misri, na watu wote wenye hekima walioko. Farao akawahadithia ndoto yake, wala hakuna aliyeweza kumfasiria Farao mambo hayo.**

**41:1 "Ikawa, mwisho wa miaka miwili mizima"** Hili, kwa dhahiri, linahusiana na sura ya 40, pale Yusufu alipotafasiri ndoto za watu wawili, wote wakitegemea kuachiwa toka gerazani, na bado, halikuwa na mafanikio. Tarehe ni kutokea pale mtu mmoja alipoachiwa na mwingine kuhukumiwa. Kutokana na habari nzima ya Yusufu, inafurahisha kuwa mwandishi/mhariri anatupatia tarehe mbalimbali: (1) alikuwa na miaka kumi na saba kipindi anauzwa utumwani (kama vile Mwa. 37:2); (2) alikuwa katika nafasi ya pili kwenye mamlaka katika taifa la Misri pindi alipokuwa na mika thelathini (kama vile Mwa. 41:46). Kwa hesabu hizi yaweza kuonekana kuwa alikaa gerezani yapata miaka kumi na mitatu. Hii inatuonyesha namna alivyokaa akitumika kwa Potifa kabla ya tukio na mkewe.

◙**"Farao"** Farao ni cheo cha pamoja kwa ajili ya wafalme wote wa Misri kama Hadadi ilivyokuwa kwa Shamu, Kaisari baadaye akajakuwa kwa Rumi, na Czar kwa Urusi. Asili ya neno haijulikani, lakini wengi wa wanahistoria wa Misri wanadhani ni kutokana na kifungu cha neno "nyumba kubwa" (BDB 829, yaani nyumba ya miungu). Pamekuwepo na mitazamo mbalimbali kuhusu ni lini Yusufu angaliinuka na kuwa mtu wa pili kwenye utawala juu ya nchi yote ya Misri. Wengi wanadhani kuwa yawezakuwa ni kipindi cha Hykson kilichojulikana kama "wafalme wa kichungaji," ambao inavyoonekana walikuwa Wasemiti, na sio Wamisri (angalia AB, uk. 316). Walitawala toka mwaka 1730 mpaka 1570 K.K. Hata hivyo, inafurahisha kuona kuwa mst.1, neno kwa ajili ya "mto," ambalo kwa uwazi linarejerea Mto Nile, linapatikana katika muundo wa kwamba lilitokea kipindi cha utawala wa karne ya 18 au 1546-1085 K.K. Kutokana na nyaraka za Wamisri pia tunajifunza kuwa kupitia historia nzima ya Misri, palikuwepo na Wasemiti kwenye maeneo ya uawajibikaji katika sehemu nyingi za utawala wa Wamisri kuliko zile mbili zilizotajwa.

◙ **"ndoto"** Kuna fasihi pana, sehemu zote za Misri na Mesopotamia, kuhusiana na ndoto na tafsiri zake. Inafurahisha kuona kuwa wale watu wawili wa Kiebrania waliohusika katika kuzitafasiri zile ndoto kila mmoja alifanya kazi kwa mfalme wa kipagani; Danieli huko Mesopotamia na Yusufu huko Misri.
Toleo la NIDOTTE, juzuu ya 2, ukurasa wa 154, linatengeneza hoja ya kufurahisha kuhusu zile ndoto tatu.
1. Usingizi wa kawaida, Zab. 126:1; Isa. 29:7-8; Mhu. 5:7
2. Ufunuo wa uongo, Yer. 23:25,27,32; 27:9-10; 29:8; Zak. 10:2
3. Ufunuo wa kweli, Mwa. 20:3; 28:12; Hes. 12:6; I Fal. 3:5; Dan. 2:28; Mt. 1:20 maono mara zote hutokea wakati wa usiku, lakini yanaonekana kuwa tofauti na ndoto. Mazingira halisi ya tofauti hizi hayajaelezewa. YHWH anawasiliana na akili ya mtu iliyofichika akitumia alama na sitiari ambazo kwake ni za kawaida.

◙ **"Mto Nile"** Hili (BDB 384) ni la kwanza katika orodha ya maneno ya kipekee ya Wamisri. Sio tu ni maneno ya kipekee ya Wamisri, bali muktadha mzima ni wa tamaduni za ki-Misri. Mto huu na mafuriko yake ya kila mwaka

ulikuwa ndio chanzo cha maisha ya Wamisri na ufanisi wao. Ulifikiriwa kuwa ni mungu wa kuridhishwa/kutulizwa (kama vile Kut. 1:22).

**41:2 "ng'ombe saba"** Tunajifunza toka kwa Plutarch, mwana historia wa Kirumi, na Clement wa Iskandaria, kasisi wa mwanzo wa kanisa, kuwa "ng'ombe" (BDB 831) alimaanisha alama ya ukarimu ya nchi huko Misri. Kama ilivyokuwa ng'ombe alikuwa ni mnyama aliyethaminiwa sana huko Misri, na ndivyo ilivyokuwa kwa kondoo huko Palestina. Ng'ombe alikuwa ni chaguo la wazi katika ndoto ya Mmisri kuhusiana na malipo ya ukulima (yaani "mwenye kumelemeta," BDB 421 [hasa "mzuri"] na "mnono," BDB 135).

◙ **"walizilishiza kwenye nyasi za mtoni"** Hili ni neno lingine lililoazimwa na Wamisri. Tunajua toka katika vyanzo vya Wamisri kuwa mifugo ilizama yenyewe ndani ya maji ya mto Nile kwa sababu mbalimbali: (1) kupooza miili yao kwa sababu ya joto; (2) kuwafukuza wadudu waliokuwa wakiwasumbua; na (3) kula majani yaliyostawi vizuri ndani ya mto (BDB 28).

**41:3-4** Ng'ombe hawa walitofautiana na wale ng'ombe wenye afya walioandikwa katika mst. 2

1. Mbaya (hasa. "mbaya kwa kutazamwa"), BDB 948 LINAUNDA NENO BDB 909
2. Aliyekondeana (hasa "mwili wake umekondeana"), BDB 201 LINAUNDA NENO BDB 142

Wao hula (BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU) wale wenye afya nzuri (mst. 4).

**41:5** Ndoto ya pili ni ya kujirudia isipokuwa ng'ombe hubadilishwa na malimbuko ya nafaka (BDB 987 II).

**41:6 "pepo za Mashariki"** Hizi pepo za jangwani (BDB 870), ni za hatari kwa ajili ya uletaji magonjwa kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo, ambazo huitwa "Sirroco" (kwa lugha ya Kiarama) huko Palestina, ambapo huvuma toka kusini Mashariki. Huitwa kwa jina la "Khamsin" huko Misri na zaidi hutokea pande za Kusini, Kusini Mashariki. Zimerejelewa katika Ezek. 17:10 na Hosea 13:15. Vyakula vyote kwa ajili ya mifugo hufa (na vivyo hivyo kwa binadamu) navyo hufa.

**41:8 "roho yake ikafadhaika"** Neno lililotafasiriwa "roho" ni *ruah* (BDB 924), lenye kumaanisha nguvu ya wanyama na binadamu katika dunia hii. Laweza kutafasiriwa kama "upepo," "pumzi," na "roho."
KITENZI "kufadhaika" (BDB 821, KB 952, *Niphal* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU) ni neno adimu. Linatumika kwenye shina la neno *Niphal* katika Zab. 77:4; Dan. 2:1,3, na shina la neno *Qal* linatumika kwa Roho wa Mungu "kuchochea" katika Amu. 13:25. Maana yake ya msingi ni "kuondoa kwa nguvu" au "kusukuma."

◙ **"waganga wote wa Misri"** Hili linaonekana kuwa neno lingine la ki-Misri lililoazimwa linalotokana na mzizi wa neno"kutia nakshi" (BDB 355) na mara nyingi lilitumika kwa mambo ya kimizimu (kama vile Kut. 7:11,22; 8:7,18,19; 9:11). Kwa nini neno la ki-Misri lingalitumika kwa ajili ya makuhani waonaji wa Kibabeli (kama vile Dan. 1:20; 2:2,10,27; 4:7,9) haijulikani. Kwa hiyo, watu hawa walikuwa viongozi, daktari weledi, na waandishi wa vitabu vya kale kuhusiana na utabiri, ufasiri n.k. hayarejerewi tu huko Misri, bali pia huko Babeli (kama vile Is. 44:25; Yer. 50:35; 51:57) na Uajemi (kama vile Esta 1:13 na 6:13). Maneno yaliyotumika katika kitabu cha Danieli ni maneno tofauti, lakini yanamrejerea mtu yule yule.
Kwa mjadala zaidi juu ya utendaji wa ki-Ungu na utafasiri wa ndoto angalia A. L. Oppenheim, *The Interpretation of Dreams in the Ancient Near East*, kur. 184-307.

◙ **"na waganga wote wa Misri"** Hili linarejerea wazee wa baraza (BDB 481 LINAUNDA NENO BDB 314, kama vile. Kut. 7:11; Isa. 19:11,12), sio muhimu kwa daraja la kikuhani la waonaji kurejerewa na neno lile la awali..

◙ **"wala hakuna mtu aliyeweza kumfasiria Farao mambo hayo"** Farao inavyoonekana alikuwa na na wenye hekima wengi waaminifu kuliko Nebuchadnezza, ambaye hakuaamini kwa kiasi kikubwa mamajusi wake kuweza kuwasimlia ndoto yake ili wamtafasirie (kama vile Daniel 2)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:9-13**
**[9] Basi mkuu wa wanyweshaji akamwambia Farao akisema, Nayakumbuka makosa yangu leo. [10] Farao aliwakasirikia watumwa wake, akanitia nifungwe nyumbani mwa mkuu wa askari, mimi na mkuu wa waokaji. [11] Tukaota ndoto usiku mmoja, mimi na yeye; kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake tukaota. [12] Na huko pamoja nasi palikuwa na kijana; Mwebrania, mtumishi wa mkuu wa askari, tukamhadithia, naye akatufasiria ndoto zetu; akamfasiria kila mtu kama ilivyokuwa ndoto yake. [13] Ikawa, kama vile alivyotufasiria ndivyo ilivyotokea; mimi nalirudishwa katika kazi yangu, na yeye alitundikwa.**

**41:9-12 "makosa yangu"** Kifungu hiki kinarejerea kwenye matukio yaliyoandikwa katika kitabu cha Mwanzo 40. Kiwastani inaonekana anazungumza kuhusu Farao mpya.

**41:12 "kijana Mwebrania"** angalia kumbukumbu katika 40:15.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:14-24**
**[14] Ndipo Farao akapeleka watu, akamwita Yusufu, wakamleta upesi kutoka gerezani. Akanyoa, akabadili nguo zake, na kuingia kwa Farao. [15] Farao akamwambia Yusufu, Nimeota ndoto, wala hakuna awezaye kunifasiria; nami nimesikia habari zako, ya kwamba, usikiapo ndoto, waweza kuifasiri. [16] Yusufu akamjibu Farao, akisema, Si mimi; Mungu atampa Farao majibu ya amani. [17] Farao akamwambia Yusufu, Katika ndoto yangu nalikuwa nikisimama ukingoni mwa mto; [18] na tazama, ng'ombe saba wanatoka mtoni, wanono, wazuri, wakajilisha manyasini. [19] Kisha, tazama, ng'ombe saba wengine wakapanda baada yao, dhaifu, wabaya sana, wamekonda; katika nchi yote ya Misri sijaona kama hao kwa udhaifu. [20] Na hao ng'ombe waliokonda, wabaya, wakawala wale ng'ombe saba wa kwanza, wale wanono. [21] Na walipokwisha kuwala haikutambulikana ya kwamba wamewala, bali wakaonekana wabaya kama kwanza. Basi nikaamka. [22] Kisha nikaona katika ndoto yangu, na tazama, masuke saba yanatokeza katika bua moja, mema, yamejaa. [23] Na tazama, masuke saba membamba, dhaifu, yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakatokeza baada yao. [24] Na hayo masuke dhaifu yakameza yale masuke saba mema. Nami nikawaambia hao waganga, wala hakuna aliyeweza kunionyesha maana yake.**

**41:14 "wakamleta upesi kutoka gerezani"** Tena hapa tunalipata neno jingine la Kimisri lililoazimwa (angalia kumbukumbu katika sura ya 40:15) toka kwenye neno "gerezani," linaloonekana kumaanisha "kufungwa jela ndani ya ngome za Kimisri." Inavyoonekana Yusufu aliwekwa pamoja na wafungwa wa kisiasa.

◙ **"akanyoa, akabadili nguo zake"** Hapa tena katika desturi za Kimisri sio tu kwamba walinyoa kichwa, bali mwili wote, na kuusafisha mwili mzima kabla ya kwenda mbele ya Farao.

**41:16 "si mimi, Mungu atampa Farao majibu ya amani"** Hili jibu linafanana kwa karibu na Dan. 2:27- 30. Yusufu alitambua chanzo cha zile ndoto hazikuwa ndani ya uwezo wake wa kuzifasiri au kusoma kutoka kwenye nyaraka za kale, bali zilikuwa katika uweza wa Mungu (kama vile 40:8). Yusufu alikuwa na mtazamo wa kidunia akimtumai Mungu kama kiini cha mambo yote (kama vile mistari ya 25,28,32). Neno lililotafasiriwa kama "vema" ni neno *shalom* (BDB 1022), linaloonyesha "amani," "kuwa sawa," au "vema." Angalia Mada Maalum katika sura ya 15:15. Katika muktadha wa sura ya 41, neno *shalom* laweza kurejea kwa roho ya Farao ("roho yake ikajawa huzuni") katika sura ya 41:8.

**41:17-24** Huu ni muundo mdogo wenye utofauti toka kwenye maelezo ya ndoto ya Farao yaliyopatikana mapema katika sura ya 41. Inaendana na hali yenyewe kiusahihi. Hakuna yeyote ambaye angelisimulia ndoto kwa usahihi pasipo kuongezea maneno mengine na kuondoa mengine. Kwangu mie ni ukumbusho wa historia juu ya habari hii.

**41:18** Neno "mwororo" ni MUUNDO WA NENO la Kiebrania kwa ajili ya neno "mzuri" (BDB 421) na neno "umbo" (BDB 1061). Huu UUNDAJI WA NENO unatumika kwa ajili ya

1. Ng'ombe,
2. mwanamke, Mwa. 29:17; Kumb. 21:11; I Sam. 25:3; Esta 2:7
3. mwanaume, Mwa. 39:6
4. Mti, Yer. 11:16

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:25-36**
**25 Yusufu akamwambia Farao, Ndoto ya Farao ni moja; Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu.26 Wale ng'ombe saba wema ni miaka saba; na yale masuke saba mema ni miaka saba. Ndoto ni moja. 27 Na wale ng'ombe saba, dhaifu, wabaya, waliopanda baada yao, ni miaka saba; na yale masuke saba matupu yaliyokaushwa na upepo wa mashariki, yatakuwa miaka saba ya njaa. 28 Ndivyo nilivyomwambia Farao, ya kwamba Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. 29 Tazama, miaka saba ya shibe inakuja, katika nchi yote ya Misri. 30 Kisha kutakuja miaka saba ya njaa baada yake; na shibe ile yote itasahauliwa katika nchi ya Misri, na njaa itaiharibu nchi. 31 Wala shibe ile haitajulikana katika nchi kwa sababu ya njaa inayokuja baadaye, maana itakuwa nzito sana. 32 Na ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi. 33 Basi, Farao na ajitafutie mtu wa akili na hekima amweke juu ya nchi ya Misri. 34 Farao na afanye hivi, tena akaweke wasimamizi juu ya nchi, na kutwaa sehemu ya tano katika nchi ya Misri, katika miaka hii saba ya kushiba. 35 Na wakusanye chakula chote cha miaka hii myema ijayo, wakaweke akiba ya nafaka mkononi mwa Farao wakakilinde kuwa chakula katika miji. 36 Na hicho chakula kitakuwa akiba ya nchi kwa ajili ya miaka hiyo saba ya njaa, itakayokuwa katika nchi ya Misri, nchi isiharibike kwa njaa.**

**41:25** Yusufu anawahutubia Wamisri wale ambao wasingalimtambua YHWH kwa hiyo alitumia jina linaloeleweka kwa ajili ya Uungu, *Elohim*. Angalia Mada Maalum katika sura ya 12:1.
Mungu huyu yuko tayari na kumtaarifu Farao, mfalme wa kipagani, kuhusu mipango yake ya mbeleni (kama vile mistari ya 25,28,32). Neno "mataifa" mara zote yamekuwa ndio mpango wa Mungu wa milele, na ukombozi (kama vile 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Isaya;
Yona; Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8)!

**41:26-32** Yusufu anaanza kuelezea ndoto ya Farao. Kumbuka katika mst. wa 24 hakuna kati ya waganga wake aliyeweza.

**41:26 "miaka saba"** Katika fasihi ya Mashariki ya Karibu ya Kale mzunguko wa miaka saba ulikuwa ni wa kawaida (kama vile ANET, uk. 31).

**41:27**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"masuke dhaifu"** |
| **NKJV** | **"ng'ombe watupu"** |
| **NRSV, JPSOA** | **"masuke matupu"** |
| **TEV** | **"ng'ombe wadhaifu"** |
| **NJB** | **"masuke yaliyonyauka"** |
| **LXX** | **"masuke yaliyonyauka na kuharibika"** |

Maneno ya Kiebrania ya

1. dhaifu, הדקות;
2. matupu, הרקות;

Herufi d (ד) na r (ר) mara nyingi zinakanganya. Toleo la mwanzo la UBS na repoti ya muda juu ya mradi wa uandishi wa agano la kale la Kiebrania (1979, uk. 62) linatumia neno "dhaifu" na kutoa alama B kwa kupima (baadhi wana mashaka).

**41:32 “suala hilo Mungu amerithibitisha, na Mungu atalitimiliza upesi”** Yusufu anatetea uweza wa Mungu na maarifa ya baadaye yanayohusiana na matukio huko Misri. Waganga wa Kimisri (kama vile Kutoka 7-8), na uhusishaji wa miungu ya Misri, haikuweza kulitambua hili wala kulisimamisha.
YHWH baadaye anatumia mapigo ya Kutoka pia kushusha kiburi cha wamisri. YHWH anawahitaji watu wa Misri wamtambue Yeye!

**41:33-36** Katika mistari hii Yusufu anatoa hekima yake ya kiuelewa kwa kile kinachotakiwa kufanyika ili kujiandaa kwa ajili ya shibe na baadaye njaa kali.
Tambua VITENZI MANENO.

1. “na Farao atafute mtu, mwenye hekima na akili ,” mst. 33, BDB 906, KB 1157, *Qal* HALI YA KUSIHI
2. “Amweke kwenye nchi ya Misri,” mst. 33, BDB 1011, KB 1483, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI
3. “na Farao achukue maamuzi,” mst. 34, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU imetumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI
4. “Awachague wasimamizi,” mst. 34, BDB 823, KB 955, *Hiphil* HALI YA KUSIHI
5. “na kutwaa sehemu ya tano katika nchi ya Misri,” mst. 34, BDB 332, KB 331, *Piel* KAULI TIMILIFU iliyotumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI (NASB)
6. “na akusanye chakula chote cha miaka hii,” mst. 35, BDB 867, KB 1062, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI
7. “Wakaweke akiba ya chakula,” mst. 35, BDB 840, KB 999, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI
8. “na wakakilinde,” mst. 35, BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI TIMILIFU iliyotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI (NASB)
9. “Kitakuwa akiba ya nchi,” mst. 36, BDB 224, KB 242, *Qal* KAULI TIMILIFU iliyotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI (kuna maneno matatu ya *Qal* KAULI TIMILIFU yenye kutenda kazi katika HALI YA KUSIHI katika muktadha huu)
10. Pia kumbuka kifungu “kutakuwa na njaa nzito sana” mst. 31

**41:33** Itambulike kuwa udhihirisho wa YHWH ni kutizamisha miaka saba ya shibe na tena miaka saba ya njaa (ambapo hakuna mtu awezae kuhusika na hili, na bado sio hukumu toka kwa Mungu, bali ni mabadiliko ya hali ya hewa katika ulimwengu ulioanguka) laweza kushughulikiwa kwa makusudi, kitendo cha mwanadamu alichopanga. Huu mwingiliano wa ukuu/maarifa ya Mungu na kazi za mwanadamu ndio tabia ya Biblia. Yote ni ya muhimu (kama vile Kutoka 3, tendo/maarifa ya Mungu katika mistari ya 7-9, lakini Musa alitakiwa kufuata katika mistari ya 10-12).

## MADA MAALUM: UCHAGUZI/KUAMRIWA KABLA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA)

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia haipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile Warumi 10:11,13).
Umuhimu wa huu mvutano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwanadamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelel!
Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mungu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi

kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja (fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. Kuamriwa kabla/mchaguzi dhidi ya utashi huru wa mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. Dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. Kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. Udhihirisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhumu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kithiolojia ya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maeneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

**41:34 "na kutwaa sehemu ya tano ya kile kitakachozalishwa katika nchi ya Misri"**Tambua kuwa kifungu "ya kile kitakachozalishwa" kiko katika herufi mlazo, kikimaanisha hakiko katika andiko la Kiebrania. Kwa hiyo, KITENZI "sehemu ya tano" (BDB 332, KB 331, *Piel* KAULI TIMILIFU) yaweza kurejerea kwenye kodi ya asilimia 20%, tunapojifunza kilikuwa ni kitu cha kawaida katika fasihi za Kimisri, au yaweza kurejerea kwenye ugawaji wa nchi ya Misri katika majimbo matano ya utawala (AB, uk. 313).

Baadhi ya watoa maoni wanafikilia KITENZI kimetokana na KAULI TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA חמש (BDB 332), chenye kumaanisha "jeshi lenye silaha" au "kuwezeshwa" (kama vile Yosh. 1:14; 4:12; Amu. 7:11, AB, uk. 313). Hili linafuatiwa na toleo la JPSOA, "kusimamia nchi ya Misri."

**41:36 "ili nchi isiharibike kwa njaa"** Neno "nchi" (BDB 75) linatenda kazi kama sitiari kwa ajili ya watu na serikali ya Misri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:37-45**

**[37] Neno hilo likawa jema machoni pa Farao, na machoni pa watumwa wake wote. [38] Farao akawaambia watumwa wake, Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake? [39] Farao akamwambia Yusufu, Kwa kuwa Mungu amekufahamisha hayo yote, hapana mwenye akili na hekima kama wewe. [40] Basi wewe utakuwa juu ya nyumba yangu, na kwa neno lako watu wangu watatawaliwa. Katika kiti cha enzi tu nitakuwa mkuu kuliko wewe. [41] Farao akamwambia Yusufu, Tazama, nimekuweka juu ya nchi yote ya Misri.**
**[42] Farao akavua pete yake ya muhuri mkononi mwake, akaitia mkononi mwa Yusufu; akamvika mavazi ya kitani nzuri, na kumtia mkufu wa dhahabu shingoni mwake. [43] Akampandisha katika gari lake la pili alilokuwa nalo. Na watu wakapiga kelele mbele yake, Pigeni magoti. Hivyo akamweka juu ya nchi yote ya Misri. [44] Farao akamwambia Yusufu, Mimi ni Farao, na bila amri yako, mtu asiinue mkono wala mguu katika nchi yote ya Misri. [45] Farao akamwita Yusufu, Safenath-panea; akamwoza Asenathi, binti Potifera, kuhani wa Oni, kuwa mkewe Yusufu akaenda huko na huko katika nchi yote ya Misri.**

**41:38 "mwenye roho ya Mungu ndani yake"** Hili limetafasiriwa toka kwenye maneno ya Kiebrania *ruach Elohim* (BDB 924, na BDB 43). Tambua kuwa Farao alitumia jina lile lile kwa ajili ya Mungu kama ambavyo Yusufu alivyolitumia. Hii inaonekana kuwa uainishaji wa kawaida kwa ajili ya mtu aliyeweza kuzitafasiri ndoto (kama vile Dan. 4:8, 9, 18; 5:11, 14) kwa wale wasio Waebrania.

**41:40**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"toa heshima kuu"** |
| **NKJV** | **"watatawaliwa"** |
| **NRSV** | **"watatoa maagizo wenyewe"** |
| **TEV** | **"atatii mamlaka yako"** |
| **NJB** | **"ataheshimu mamlaka yako"** |
| **LXX** | **"kuwa mtii kwenye maneno yako"** |
| **JPSOA** | **"mwenye kuelekezwa"** |
| **REB** | **"atayaheshimu maneno yako"** |

Asili ya neno hili haijulikani, lakini linaonekana kuhusiana na mzizi wa Kiebrania unaomaanisha "kubusiana kwa mdomo" (BDB 676, KB 30, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU). Laweza kumaanisha (1) "kuwa mtiifu" (KB) au (2) "kubusu ardhi kama ishara ya heshima kuu" (kama vile Zab. 2:12). Wamisri watalitii neno la Yusufu (hasa neno litokalo katika kinywa chake) kama alivyofanya Farao (kama vile kur. 42,43,44). Alifanywa "Afisa mkuu" wa Farao.

**41:42 "pete yake ya mhuri mkononi mwake"** Hili linatokana na mzizi ule ule wa KITENZI cha neno "kuzamisha chini" (BDB 371), ambacho chaweza kurejerea rasmi kwenye pete iliyozama ndani ya udongo au lami ili kuthibitisha kitu fulani kwa wazi (kama vile Esther 3:10,12; 8:8,10).

◙ **"akavikwa kwa mavazi ya kitani nzuri"** Hili ni neno lingine la Kimisri lililoazimwa (BDB 1058 III) ambalo linarejerea mavazi ya kitani nzuri iliyovaliwa na kiongozi wa jamii ya Misri wa daraja la juu.

◙ **"na kumtia mkufu wa dhahabu shingoni mwake"** Hii ilikuwa ni alama ya kimamlaka kwenye historia nzima ya Misri, hasa katika utawala wa karne ya 12 (kama vile Dan. 5:7, 16, 29). Maelezo haya ni ya kweli juu ya tamaduni ya Misri ya wakati huo. Haya ni maelezo ya ushahidi wa macho!

**41:43 "nafasi ya pili"** Hii ilikuwa ni njia ya kurejerea kwa Yusufu kama kiongozi wa pili wa juu katika nchi ya Misri (yaani Kiongozi mkuu). Neno "nafasi ya pili" (BDB 1041) mara nyingi inarejerea kwenye siasa au afisa utawala (kama vile I Sam. 23:17; II Fal. 23:4; 25:18; I Nya. 5:12; 15:18; II Nya. 28:7; 31:12; Nah. 11:17; Esther 10:3; Yer. 52:24).

◙ **"pigeni magoti"** Maana ya neno la Kimisri ("Abrek," kama vile JPSOA) kwa kiasi kikubwa limekuwa likijadiliwa. Linaonekana kufanana na mzizi wa Kiebrania "kupiga magoti." Pamekuwepo na tafasiri mbali mbali zilizopatikana kwa Brown, Driver na Briggs (BDB 7). Hata hivyo, toleo la Kilatini, tafasiri za Kiebrania za Aquilla, Origen wa Askanderia, na mtoa maoni wa Kiyahudi, Kimchi, yote yanamaanisha "kupiga goti," linalotokana na mzizi wa kale wa Kiebrania (BDB 7). Hili linaonekana kimuktadha linafaa zaidi.

**41:44 "mtu asiinue mkono wala mguu"** Hii ni nahau kwa ajili ya kifungu "hakuna kazi au jaribio inayopaswa kuanza au kuendelea pasipo kibari cha Yusufu." Inaonyesha mamlaka kamili.

**41:45 "Farao akamwita Yusufu, Zaphenath-panea"** Hiki ni cheo cha kiofisa (BDB 861) kinachohusiana na Farao mwenyewe (kama vile Mwa. 45:8). Farao kumwita yeye yawezakuwa ni alama ya kitamaduni ya kimamlaka yake juu ya Yusufu. Pamekuwepo na asili ya maneno yaliyopangwa. Lililozoeleka zaidi ni lile "mungu anaongea na anaishi," linaloonekana kurejea kwa Farao kama mwana wa mungu jua, au yumkini Mungu wa Yusufu anaongea na kuiokoa Misri. Uwezekano mwingine ni "yeye ajuaye mambo," ambalo lingalirejerea kwa Yusufu kama mfasiri wa ndoto.

◙ **"akamwoza Asenathi, binti wa"** Hili ni jina lingine la Kimisri lenye kumaanisha "mali ya Neithi" (BDB 62, kama vile 41:45,50; 46:20), ni mungu wa upendo wa kike wa Kimisri.

◙ **"Potipera, kuhani wa Oni"** Hili ni jina lingine la Kimisri linalopanua jina la Potifa, linalopatikana katika Mwa. 37:36; 39:1. Lenye kumaanisha "kwa yeye ambaye humpa" (BDB 806). Farao anamtengeneza Yusufu kuwa mtu wa daraja la juu katika jamii ya watu wa Misri kwa namna ya kumwoza binti wa kuhani maalum (BDB 463).

◙ **"Oni"** "Oni" (BDB 58) ni mji wa mungu jua. Huitwa kwa jina la Heliopolisi katika Kiyunani na Bethi Shemeshi katika Kiebrania (kama vile Yer. 43:13). Mji huu ulikuwa yapata maili saba Kaskazini mwa Kairo, kwenye mpaka wa nchi ya Gosheni.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"Yusufu akaenda huku na huku katika nchi ya Misri"** |
| **NRSV** | **"Yusufu akapewa mamlaka juu ya nchi ya Misri"** |
| **TEV** | **"akatembele sehemu zote za nchi"** |
| **NJB, LXX** | **"na Yusufu akaanza kusafiri katika nchi yote ya Misri"** |
| **REB** | **"utawala wa Yusufu ukaenea katika nchi yote ya Misri"** |
| **JPSOA** | **"hivyo Yusufu akajulikana katika uongozi wa nchi ya Misri"** |

Kifungu hiki kiuhalisia kimetafasiriwa katika matoleo ya NASB na NKJV. Hata hivyo, maana yake haijulikani.

1. Mistari ya 45 na 46 inafanana, kwa hiyo,kifungu "akatembea katika sehemu zote za nchi" (TEV, NJB, LXX, NIV)
2. Katika kitabu cha Esta 1:17 hiki KITENZI kilichozoeleka cha neno "kwenda" au "kuja" (BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU), pia neno *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU, limetumika kwa maana ya kitu fulani kinachoenea (yaani.,ujumbe kuhusu mapungufu ya Vashti). Kwa hiyo hapa umaarufu wa Yusufu na mamlaka yalienea kwa nchi nzima (NRSV, REB).
3. Kwa sababu ya kifungu "juu ya ardhi" kikifuatisha KITENZI kilichotumika katika mistari ya 33, 41, na 43 kikihusishwa na utawala wa Yusufu kama kiongozi/mtawala mkuu, kwa hivyo KITENZI hapa lazima kirejerea (JPSOA)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41: 46-49**
**46 Naye Yusufu alikuwa mwenye miaka thelathini, aliposimama mbele ya Farao, mfalme wa Misri. Yusufu akatoka mbele ya uso wa Farao, akapita katika nchi yote ya Misri. 47 Ikawa katika miaka ile saba ya shibe, nchi ikazaa kwa wingi. 48 Akakusanya chakula chote cha miaka ile saba katika nchi ya Misri. Akaweka chakula katika miji; chakula cha mashamba yaliyouzunguka kila mji, akakiweka ndani yake. 49 Yusufu akakusanya nafaka kama mchanga wa pwani, nyingi mno, hata akaacha kuhesabu, maana ilikuwa haina hesabu.**

**41:46 "miaka therathini"** Hiki kiuhalisia ni "mtoto wa miaka therathini," ambacho ni nahau (kama vile Law. 27:5; II Fal. 8:26; Yer. 52:1).

**41:47-49** Utafasiri wa Yusufu kuhusu ndoto moja kwa moja ulikuwa sahihi. Wingi wa chakula umeelezewa kwa namna mbalimbali.

1. Miaka saba ya shibe, mst. 47
2. Na nchi ikazaa kwa wingi, mst. 47
3. Akakusanya nafaka kwa wingi, kur. 47, 47
4. Kama mchanga wa bahari, mst. 49
5. Hata akaacha kuhesabu, maana ilikuwa haina hesabu, mst. 49

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:50-52**
**50 Kabla ya kuja miaka ya njaa, Yusufu akazaliwa wana wawili, ambao Asenathi, binti Potifera, kuhani wa Oni, alimzalia. 51 Yusufu akamwita jina lake yule aliyezaliwa kwanza, Manase, maana alisema, Mungu amenisahaulisha taabu zangu zote, na nyumba yote ya baba yangu. 52 Na wa pili akamwita jina lake Efraimu, maana alisema, Mungu amenipa uzazi katika nchi ya mateso yangu.**

**41:51 "Manase"** Jina hili (BDB 586) linahusiana na KITENZI cha Kiebrania "kusahau" (BDB 674, KB 728, *Piel* HALI YA KUENDELEA) kwa muaonekano unaofanana. Hili linahusiana na maumivu yenye kuhusiana na matendo ya nduguze. Matukio ya baadaye katika kitabu cha Mwanzo yanaonyesha kuwa Yusufu hajasahau moja kwa moja juu ya chuki ya kisariti ya nduguze.

**41:52 "Efraimu"** Jina hili (BDB 68) linahusiana na neno "yenye kuzaa matunda" au "yenye kuzaa mara mbili" (BDB 826, kama vile 49:22) kwa masihala yaliyozoeleka. Inafurahisha kukumbuka kuwa Israeli ya sasa, ambayo ni Uyahudi inaamuriwa na mama wa Kiyahudi. Kusema ukweli, hawa vijana wawili sio Wayahudi wa kweli! Baadaye watakuja kuwa kabila nusu litakalorithi sehemu mbili za Yusufu na watafanyika moja ya sehemu ya yale makabila kumi na mawili (yaani., kumi na matatu) ya Israeli. Kabila la Lawi halitahesabika kama kabila kwa kusudi la kurithi (kama vile Yoshua)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41: 53-57**
**[53] Miaka ile saba ya shibe ikaisha katika nchi ya Misri, [54] ikaanza kuja miaka ile saba ya njaa, kama vile Yusufu alivyosema. Kukawa na njaa katika nchi zote, bali katika nchi yote ya Misri palikuwa na chakula. [55] Na nchi yote ya Misri ilipoona njaa, watu walimlilia Farao awape chakula. Farao akawaambia Wamisri wote, Enendeni kwa Yusufu; atakavyowaambia, fanyeni. [56] Njaa ikawa katika dunia yote pia. Yusufu akazifungua ghala zote, akawauzia Wamisri. Njaa ikawa nzito katika nchi ya Misri. [57] Watu wa nchi zote wakaja Misri kwa Yusufu; ili wanunue nafaka; kwa sababu njaa imekuwa nzito katika dunia yote.**

**41:53-57** Hili linaelezea kihistoria namna Farao alivyokuja kumiliki nchi ya Misri (kama vile 47:20-26). Wamisri waliuza ardhi yao kwa mfalme ili wanunue chakula cha kujirisha wao wenyewe na familia zao.
Lazima ifahamike kuwa njaa ingaliweza kuonyesha kushindwa kwa dini huko Misri (yaani mungu jua, miungu ya ustawi, na Nile yenyewe) kuweza kuiokoa Misri, bali Mungu angeweza!

**41:56**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, TEV,**
**VULGATE "ghala zote za nyumba"**
**NJB, LXX,**
**REB "maghala yote"**
**JPSOA "yote yaliyokuwa ndani"**

Andiko la Kiebrania kwa uwazi linatafasiliwa na toleo la JPSOA.laweza kurejerea
1. Maeneo yote yalikuwa ni mahala pa Yusufu kuhifadhi mazao yake
2. Sehemu zote za nchi ambazo Wamisri wangaliweza kununua mazao

**41:57** Mstari huu unaelezea kuhusu ukame mkubwa na njaa karibia eneo lote la Mashariki ya karibu na Mediterania. Mataifa mengi yalikuja Misri kununua chakula. Yusufu aliiokoa
1. Misri
2. makundi mengi ya watu yaliozunguka maeneo
3. hasa familia iliyochaguliwa ya Yakobo!

Uwekevu wa Mungu unatenda kazi katika nyanja mbalimbali!
Kumbuka namna kifungu hiki kinavyokuzwa "dunia nzima." Hiki kinafanana na kifungu kilichotumika katika Mwanzo 6-7 kuhusu ukubwa wa mafuriko (kama vile 7:19, 79, ארצ, BDB 75).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Taja maneno yote ya Kimisri yaliyoazimwa katika sura hii na mila pekee za Kimisri.
2. Elezea kuhusu waganga na kazi zao katika Mashariki ya Karibu ya kale
3. Taja njia zote zile zilizoelezea nafasi mpya ya Yusufu katika kur. 41-44.
4. Nini maana ya majina ya wana wa Yusufu na nini umuhimu wake (mst. 50-52)?

# MWANZO 42

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Ndugu zake Yusufu Wanatumwa misri | Ndugu zake Yusufu wanaenda misri | Ndugu zake Yusufu wanaenda misri Wakati wa njaa | Ndugu zake Yusufu wanaenda misri kununua nafaka | Yusufu anakutana na ndugu zake mara ya kwanza |
| 42:1-5 | 42:1-5 | 42:1-5 | 42:1-4 | 42:1-4 |
| | | | 42:5-7a | 42:5-7 |
| 42:6-7 | 42:6-17 | 42:6-17 | | |
| | | | 42:7b | |
| 42:8-17 | | | 42:8-9 | 42:8-17 |
| | | | 42:10-11 | |
| | | | 42:12 | |
| | | 42:13 | | |
| | | | 42:14-17 | |
| 42:18-25 | 42:18-24 | 42:18-25 | 42:18-20a | 42:18-24 |
| | | | 42:20b-21 | |
| | | | 42:22-24 | |
| | Ndugu wanarudi kanaani 42:25-28 | | Ndugu wa Yusufu wanarudi kanaani 42:25-28 | Wana wa Yakobo wanarudi kanaani 42:25-28 |
| 42:26-28 | | 42:26-28 | | |
| Simioni anashikiliwa | | | | |
| 42:29-34 | 42:29-34 | 42:29-34 | 42:29-34 | 42:29-34 |
| 42:35-38 | 42:35-38 | 42:35-38 | 42:35-36 | 42:35-36 |
| | | | 42:37 | 42:37-38 |
| | | | 42:38 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:1-5**
**[1] Basi Yakobo akaona ya kuwa kuna nafaka katika Misri, Yakobo akawaambia wanawe, Kwa nini mnatazamana? [2] Akasema, Angalia, nimesikia ya kuwa kuna nafaka Misri; shukeni huko mkatununulie chakula, tupate kuishi wala tusife. [3] Basi ndugu kumi wa Yusufu wakashuka Misri ili wanunue nafaka. [4] Walakini Benyamini, ndugu wa Yusufu, Yakobo hakumpeleka pamoja na ndugu zake, maana alisema, Mabaya yasimpate. [5] Wana wa Israeli wakaja wanunue chakula miongoni mwao waliokuja, kwa kuwa kulikuwa na njaa katika nchi ya Kanaani.**

**42:1 "Basi Yakobo akaona ya kuwa kuna nafaka katika Misri,"**KITENZI **"**akaona" kimetumika mara mbili kwenye mst . 1.

1. "Yakobo akaona," BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. "kwa nini mnatazamana," *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Hili ni sawa na neno lililotumika kwenye ndoto ya Farao (kama vile 41:19, 22, 28) na Yusufu kwa Farao alipokuwa anawatafuta watu wenye hekima na utambuzi (kama vile . 41:33). KITENZI hiki kimetumika mara nyingi sana kwenye sura hii (yaani mst. 1 [mara mbili],7,9,12,21,27,35). Rashi anasema kwamba alikuwa na maono ya kiroho, lakini huenda aliona kwamba baadhi ya wakanaani walinunua nafaka kutoka kwa Farao (kama vile 47:14).

**42:2** Yakobo anawaamuru watoto wake waende Misri kufuata chakula (yaani , "tupate kuishi na wala tusife") kwa ajili ya familia.

1. Shukeni huko , BDB 432, KB 434, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. mkatununulie chakula, BDB 991, KB 1404, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. Tupate kuishi, BDB 310, KB 309, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye HALI YA KUSIHI. Njaa ilikuwa kali sana na imeenea kote na kali!

**42:3-4** Yakobo bado hakuwaamini kaka zake. Kwa namna gani kifo cha Yusufu kilitokea na hakutaka kuamini chochote kingetokea sambamba kwa Benjamini, mtoto pekee aliyebakia wa Raheli.

**42:4 "Mabaya yasimpate"** Neno "mabaya" (BDB 62) ni adimu (kamavile 44:29;Kut. 21:22,23) na inaonyesha ajali iliyoogopesha maisha. Yakobo alijawa na hofu kuu kwa ajili ya maisha ya mtoto wa pekee wa mpendwa, wake aliyefariki Raheli (yaani Benjamini, mdogo wake na Yusufu wa tumbo moja kuzaliwa). Jambo moja la kustaabisha ni kama Yakobo alifikiria kuwa angekuja kuwa kiongozi wa familia.

KITENZI hiki (BDB 896, II KB 1131 *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kimeumika kwenye maana hasi hapa na kwenye Law 10:19; Kumb. 31:29; Ayu 4:14; Isa. 51:19; Yer. 13:22; 44:23, na ni kawaida itafsiriwe "yasimpate.''

**42:5 "Wana wa Israeli wakaja wanunue chakula miongoni mwao waliokuja"** Wengine wanashangaa kwa nini Yakobo aliwatuma wana wake wote (mwanzoni aligawa familia yake kwa ajili ya usalama, kama vile 32:22-32).Labda kwa sababu (1) kila mmoja mmoja angenunua nafaka nyingi au (2) kwamba kuna usalama wakiwa wengi

◙ **"kwa kuwa kulikuwa na njaa katika nchi ya Kanaani"** Kutokana na historia tunafahamu ya kwamba njaa ya muda huo iliikumba kupitia sehemu hii ya dunia. Ilisababishwa na (1) Ukosefu wa mvua kwa muda muafaka; (2) mvua nyingi sana au baridi; (3) wadudu au (4) maradhi ya mimea,ukungu. Kanaani ilitegemea mizunguko wa asilia , lakini Misri ilitegemea mto Nile (yaani mafuriko)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:6-7**
***[6]* Naye Yusufu alikuwa ni liwali juu ya nchi, ndiye aliyewauzia watu wote wa nchi. Nao ndugu zake Yusufu wakaja, wakainama kifudifudi mbele yake. *[7]* Yusufu akawaona nduguze, akawatambua, lakini alijifanya kama mgeni kwao. Akasema nao kwa maneno makali, akawaambia, Mmetoka wapi ninyi? Wakasema. Tumetoka**

**nchi ya Kanaani, ili tununue chakula**

**42:6 "Nao ndugu zake Yusufu wakaja, wakainama kifudifudi mbele yake"** Sio tu inaonekana aya hii inatimiza ndoto za Yusufu kwenye Mwa 37:6-9, lakini pia 43:28; na 44:14.

**42:7 "akawatambua"** KITENZI "akawaona", "akawatambua" (BDB 647, KB 699) kimetumika mara mbili kwenye mst. 7 (*Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) na mara kwenye mst. 8 (*Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Walikuwa bado na ndevu nyingi na kuvaa mavazi ya kitamaduni kama makabila yanayo hama hama. Kwa upande mwingine Yusufu alikuwa amenyoa ndevu, vazi kupendeza, mahali pa mamlaka, na anaongea kimisri. Vitu hivi vyote vilimfunika barabara kutoka kwa kaka zake.

◙ **"akawatambua, lakini alijifanya kama mgeni kwao"** VITENZI hivi vyote vinatokana na asili moja,

1. akawatambua BDB 647, KB 699, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile. 27:23; 37:33; 38:25,26; 42:7,8 (mara mbili); Kut. 33:9
2. alijifanya mgeni (lit. "alijifanya mgeni"), BDB 649, KB 699, *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile I Fal 14:5,6

Sio ya kawaida kama kuna asili mbili za kiebrania au mbili zimetumika.

◙

**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB "kwa ukali"**
**NKJV "kwa ukali"**
**LXX "maneno makali"**
**AB "kwa mkazo"**

Kivumishi (BDB 904) kina maana "ngumu," au"kali." Kimetumika kwenye I Sam. 25:3 inamuelezea tabia ya Nabali. Hapa inaelezea sauti ya asili ya Yusufu (kama vile. I Sam. 20:10), kama alivyoridhika kwa kuwatuhumu (yaani wao ni wapelelezi).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:8-17**
**[8] Yusufu akawatambua nduguze, bali wao hawakumtambua yeye. [9] Yusufu akazikumbuka zile ndoto alizowaotea. Akawaambia, Wapelelezi ninyi, mmekuja ili mwuone utupu wa nchi. [10] Wakamwambia, Hasha, bwana, watumwa wako tumekuja ili tununue chakula. [11] Sisi sote ni wana wa mtu mmoja tu watu wa kweli sisi; watumwa wako si wapelelezi. [12] Akawaambia, Sivyo, mmekuja ili mwuone utupu wa nchi. [13] Wakamwambia, Sisi watumwa wako tu ndugu kumi na wawili, wana wa mtu mmoja katika nchi ya Kanaani; na mdogo wetu yuko pamoja na baba yetu leo, na mmoja hayuko. [14] Yusufu akawaambia, Ndivyo nilivyowaambia, nikisema, Wapelelezi ninyi. [15] Mtabainika kwa njia hii; aishivyo Farao, hamtoki hapa, asipokuja huku huyo ndugu yenu mdogo. [16] Mpelekeni mmoja wenu, aende akamlete ndugu yenu, na ninyi mtafungwa, hata maneno yenu yahakikishwe, kama mna kweli ninyi; ikiwa sivyo, aishivyo Farao, ninyi ni wapelelezi. [17] Akawatia wote gerezani siku tatu.**

**42:9 "Yusufu akazikumbuka zile ndoto"** Hii inaonyesha Sura ya 37. Yusufu alimpa jina la Manase mwana wake wa kwanza ("kumfanya asahau"), lakini kumbukumbu ya kusalitiwa na kaka zake ilimfanya abubujikwe na machozi

◙ **"Wapelelezi ninyi "** Waalimu wa sheria wa kiyahudi wanasema kwamba Yakobo aliwaambia watoto wake waingie ndani ya mji kwa milango tofauti na Yusufu akaligundua hili na kulitumia kuwalaumu ya kuwa wao ni wapelelezi (BDB 920, KB 1183, *Piel* KAULI ENDELEVU kama vile Yosh. 2:1; 6:22-23; I Sam. 26:4).Alifanya hivi ili kupima nia na tabia zao.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"sehemu ya nchi isiyolindwa"** |
| **NKJV, NRSV,** | |
| **JPSOA** | **"sehemu dhaifu ya nchi"** |
| **TEV** | **"sehemu ya nchi iliyo dhaifu"** |
| **NJB** | **"sehemu sehemu za nchi palipo dhaifu"** |
| **LXX** | **"alama(yaani kutambua njia) za nchi"** |
| **REB** | **"sehemu dhaifu za ulinzi wetu"** |

Hili neno (BDB 788) ni la kawaida"utupu" (kama vile 9:22-23) au "funua." Maana hapa (unabainishwa na muktadha) ni eneo la Misri pasipo ngome au walinzi wa kijeshi.Ni shutuma za uongo za kuwajaribu watoto wa Yakobo.

**42:11 "Sisi sote ni wana" k**weli" (BDB 467 II, kama vile 42:11, 19,31,34) imetumika kwa maana ya kile walichokifanya hapo mwanzoni kwa Yusufu. Walionekana wako wamesimama wima, watu wakweli, lakini njia zao na matendo ni maovu (kama vile Mwa 34, 37).

**42:13 "wana wa mtu mmoja katika nchi ya Kanaani; na mdogo wetu yuko pamoja na baba yetu leo, na mmoja hayuko"** kifungu cha mwisho ni wazi kinamhusu Yusufu. Walikuwa wanaongea kwa kumkejeli mbele ya uso wake bila kujua yeye ni nani.

**42:15 "aishivyo Farao,"** Wafasiri wengi wanamkosoa Yusufu kwa kusema kiapo hiki mara mbili. Ilimfaa kwa kuufunika ukweli! Ni wazi hakutumia maana ya teolojia. Hata hivyo, inaturejesha kwenye utamaduni wa Misri kwamba Farao alikuwa ni mwana wa mungu jua, Re. kiapo hiki kinapatikana kwenye makumbusho ya Misri.

**42:16** Yusufu alifanya maagizo na matakwa mengi.

1 Mpelekeni mmoja wenu, BDB 1018, KB 1511, *QAL* KAULI SHURUTISHI
2 Aende akamlete ndugu yenu, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI
3 Ninyi mtabaki gerezani, BDB 63, KB 75, *Niphal* KAULI SHURUTISHI
4 Hata maneno yenu yahakikishwe, BDB 103, KB 119, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI

**42:17 "Akawatia wote gerezani siku tatu"** Ni wazi Yusufu alitaka wapitie maumivu makubwa kama aliyopitia yeye kwa gharama zao.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:18-25**
**18 Yusufu akawaambia siku ya tatu, Fanyeni hivi, mkaishi, maana mimi namcha Mungu. 19 Kama ni wa kweli ninyi ndugu yenu mmoja na afungwe gerezani, nanyi nendeni mkachukue nafaka kwa njaa ya nyumba zenu, 20 mkamlete ndugu yenu mdogo kwangu; hivyo maneno yenu yatahakikishwa, wala hamtakufa. Ndivyo walivyofanya. 21 Wakaambiana, Kweli sisi tulimkosa ndugu yetu, kwa kuwa tuliona shida ya roho yake, alipotusihi, wala hatukusikia kwa hiyo shida hii imetupata. 22 Reubeni akajibu, akawaambia, Sikuwaambia, nikisema, msimkose kijana? Wala hamkusikia; kwa hiyo damu yake inatakwa tena. 23 Wala hawakujua ya kwamba Yusufu anawasikia, kwa sababu alikuwapo mkalimani kati yao. 24 Akajitenga nao akalia. Kisha akawarudia, na kusema nao, akamtwaa Simeoni miongoni mwao, akamfunga mbele ya macho yao. 25 Yusufu akaamuru kuvijaza vyombo vyao nafaka, na kumrudishia kila mtu fedha yake katika gunia lake, na kuwapa chakula cha njiani.**

**42:18-20** Maagizo na matakwa ya Yusufu yanaendelea

1 Fanyeni hivi,mst. 18, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2 mkaishi,mst. 18, BDB 310, KB 309, *Qal* KAULI SHURUTISHI

3 Ndugu yenu mmoja afungwe, mst. 19, BDB 63, KB 75, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI
4 nendeni, v. 19, BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5 mkachukue nafaka,mst. 19, BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
6 mkamlete ndugu yenu mdogo kwangu,mst. 20, BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI
7 hivyo maneno yenu yatahakikishwa,mst. 20, BDB 52, KB 63, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI

**42:18 "maana mimi namcha Mungu"** Kifungu hiki kinasimulia labda inawezekana kiapo cha Yususfu kilikuwa kwa jina la Farao (kama vile mst. 15,16) au kwa ujumla kuhofia ubashiri wa maelezo dhidi ya hawa watu kumi. Yusufu anatetea, kwenye njia ya kuzunguka, uaminifu wake na mambo ya kiroho (kama vile. 20:11).alikuwa anamheshimu/kumwogopa sana *Elohim*.

**42:20 "yatahakikishwa"** Tazama mada maalumu 15:6 (II. A).

**42:21** "**Wakaambiana**, '**Kweli sisi tulimkosa ndugu yetu**'" Walihisi kwamba Mungu anawaadhibu kwa sababu ya maovu yao dhidi ya Yusufu. Hili ni dhahili kutoka kwenye mst. 21, 22, 28 na 44:16. Ina maana ya kwamba tunavuna tulichokipanda (kama vile. Ayu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mith. 24:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mith. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; I Kor. 3:8; 2 Kor. 5:10; Gal. 6:6-7; 2 Tim. 4:14; I Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12). Hata hivyo, kuna ukweli mwingine pia wa kibiblia kwamba Mungu hawezi kuhusika nasi kwasababu ya maovu yetu (kama vile Zab 103:10). Hatupokei adhabu mara kwa mara kwa maovu yetu yote,au wote tungekufa nab ado kuna nafasi ambapo Mungu atatenda hivi.

**42:22 " Reubeni akajibu, akawaambia, Sikuwaambia, nikisema, msimkose kijana? Wala hamkusikia"** Hii huenda ni mara ya kwanza kwa Yusufu kusikia ya kwamba Reubeni alijaribu kumlinda yeye (kama vile Kut. 37:22-24). Sasa hawa ndugu wanaamini ya kwamba damu isiyokuwa na hatia ya Yusufu inalilia kisasi kama damu ya Abeli ilivyofanya dhidi ya kaka yake kwenye Kut 4.

**42:23 "hawakujua ya kwamba Yusufu anawasikia, kwa sababu alikuwapo mkalimani kati yao"** Walikuwa wanaongea kiebrania;Yusufu ni wazi aliongea kimisri kupitia kwa mkalimani
Tena, hii ni sehemu aliyojificha mpaka alipoweza kuhakikisha kama kaka zake wameshinda chuki iliyosababisha wamtendee maovu yapata miaka ishirini iliyopita.

KITENZI hiki kwa kiebrania kinatafsiriwa "alikuwapo mkalimani" (BDB 539, KB 529, *Hiphil* KAULI ENDELEVU) kwa kawaida inamaanisha dharau au dhihaki. Kwenye *Hiphil* inamaanisha

1. dharau, Ayubu 16:20; Zab. 119:51
2. mkalimani, hapa ni mjumbe, 2 Nya. 32:31

KITENZI hiki kilichotumika kote kwenye Agano la Kale kimetokea kwenye muktadha hasi (kama vile NIDOTTE, juzuu. 2, ukr. 799).

**42:24 "akalia"** Yusufu ni dhahili alikuwa mtu mwelewa (kama vile. 43:30; 45:14,15).

◙ **"akamtwaa Simeoni miongoni mwao, akamfunga mbele ya macho yao"** Ilionekana wazi Reubeni, mzaliwa wa kwanza, alikuwa kiongozi wa kundi na ni wazi alijaribu kumsaidia Yusufu, hivyo basi kwa wazi akachaguliwa Simioni. Alikuwa ni mzaliwa wa pili na wafasiri wengi wanaamini kwamba hasira kali ilionekana wakati wa kushambuliwa kwa wanaume wa Shekemu ( kama vile Kut 34 ) huwenda alihusika kwenye mpango wa kumuumiza Yusufu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:26-28**
**[26] Navyo ndivyo walivyofanyiwa. Wakaweka nafaka yao juu ya punda zao, wakatoka huko. [27] Mmoja wao alipofungua gunia lake ili ampe punda wake chakula katika nyumba ya wageni, aliiona fedha yake; kumbe!**

**Iko kinywani mwa gunia lake. [28] Akawaambia nduguze, Fedha yangu imerudishwa, angalia, imo humo guniani mwangu. Mioyo yao ikazimia, wakageukiana wakitetemeka, wakasema, N'nini hii Mungu aliyotutendea?**

**42:25-29** Hawa ndugu tisa waliogopa kwamba hii itahatarisha kuachiwa huru kwa Simioni. Kuhusu kiwango chao kinaelezewa kwenye

1 mioyo yao ikazimia, mst. 28 (kifasihi. "mioyo yao ikawatoka"), BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2 wakageukiana wakitetemeka, mst. 28, BDB 353, KB 350, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 27:33; I Sam. 16:4; 21:1; I Fal. 1:49

**42:27 "gunia"** kuna maneno mawili tofauti ya kiebrania yanayotafasiri neno "gunia" kwenye aya hii

1. "gunia" (BDB 974) ,ambalo ni neno la kawaida kwa "nguo ya gunia" (imetumika hapa)
2. "gunia" (BDB 607), ambalo limepatikana pekee kwenye habari hii ya Yusufu na nduguze.inamaanisha ni gunia la kubebea nafaka.

Jibu lililotumika kwa maneno mawili labda moja likamaanisha kifuko cha pesa (kama vile. NIDOTTE, juzuu. 3, ukr. 843) na mwingine gunia kwa ajili ya nafaka (kama vile. James W. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, ukr. 49).

**42:28 "N'nini hii Mungu aliyotutendea"** Bado walihisi hukumu ya kiroho kwa matendo yao dhidi ya Yusufu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:29-34**
**[29] Wakaja kwa Yakobo, baba yao, katika nchi ya Kanaani, wakampasha habari za yote yaliyowapata, wakisema, [30] Mtu yule aliye bwana wa nchi alisema nasi kwa maneno makali, akatufanya tu wapelelezi wa nchi. [31] Tukamwambia, Tu watu wa kweli sisi, wala si wapelelezi. [32] Sisi tu ndugu kumi na wawili, wana wa baba yetu. Mmoja hayuko, na mdogo wetu yuko pamoja na baba yetu leo katika nchi ya Kanaani. [33] Yule mtu, bwana wa nchi, akatuambia, Kwa njia hii nitawajua kama ninyi ni watu wa kweli; ndugu yenu mmoja mwacheni huku kwangu, kachukueni nafaka kwa njaa ya nyumba zenu, mwende zenu. [34] Mkaniletee ndugu yenu mdogo; ndipo nitakapojua kama ninyi si wapelelezi, bali ni watu wa kweli; basi nitawarudishia ndugu yenu, nanyi mtafanya biashara katika nchi hii.**

**42:29-34** Ndugu hawa tisa wakampasha habari baba yao, Yakobo, yote yaliyotendeka Misri.

**42:34 "nanyi mtafanya biashara katika nchi hii "** KITENZI hiki (BDB 695, KB 749, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatafasiriwa"biashara" (kama vile Mwa. 23:16), lakini kimetumika kwenye Mwa. 34:10 inadokeza maana ya "kusafiri kwa uhuru." Inawezekana kwamba inaonyesha warudi Misri kwa ajili ya nafaka zaidi itakahitajika (kama vile. 43:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:35-38**
**[35] Ikawa walipomimina magunia yao, kumbe! Bahasha ya fedha ya kila mtu imo katika gunia lake. Nao walipoziona bahasha za fedha zao, wao na baba yao waliogopa. [36] Yakobo baba yao akawaambia, Mmeniondolea watoto wangu; Yusufu hayuko, wala Simeoni hayuko, na Benyamini mnataka kumchukua naye; mambo hayo yote yamenipata mimi. [37] Reubeni akamwambia babaye, akasema, Uwaue wanangu wawili nisipomrudisha kwako; mtie katika mikono yangu, nami nitamrudisha kwako. [38] Akasema, Mwanangu hatashuka pamoja nanyi, maana nduguye amekufa, naye amesalia peke yake; mabaya yakimpata katika njia mtakayoiendea ndipo mtakaposhusha mvi zangu kwa sikitiko mpaka kaburini.**

**42:35-38** Familia walijadili hali hii na wafanye nini.Waliamua kutofanya chochote kwa muda.

**42:35** Tofauti kati ya mst . 27 na mst . 35 ni "kila" mmoja wao kwenye mst . 27 na "wao" kwenye mst . 35. Hii si njozi ya kufanana, lakini ni mkazo wa tatizo lililowaogopesha wao mapema (kama vile .mst. 28)

**42:36 "Mmeniondolea watoto wangu; Yusufu hayuko, wala Simeoni hayuko, na Benyamini mnataka kumchukua naye; mambo hayo yote yamenipata mimi"** Tambua ya kwambaYakobo alichukuwa uangalifu kama kujifedhehesha mwenyewe. Inaonekana inaonyesha lawama kwamba ndugu zake walihusika na kupotea kwa Yusufu.

**42:37 "Reubeni akamwambia babaye, akasema"** Hii ni ofa ya kijinga! Kwa nini Yakobo, kwa sababu ya kupotea kwa wana wake, kuwaua wajukuu wake?! Ni kujaribu kwa Reubeni kumhakikishia baba yake, lakini ilifanyika kinyume hasa. Yakobo alisuburia mpaka (1) ofa ya Yuda kwenye 43:8-9 na (2) kwa kweli kwa kukosekana kwa chakula mwishowe alimruhusu Benjamini kwenda nao.

**42:38 "kaburinil"** Hili neno katika Agano la kale limetumika kama sehemu ya wafu. Mafundisho ya baada ya kifo yamefichwa katika Agano la kale, lakini ni wazi kuwa waliamini familia huwa pamoja baada ya kifo.

Ni ukweli kwamba ilikuwa ni kivuli, inanena kutokuwa na furaha, lakini hali ya kujitambua isiyokuwepo. Neno *Kaburi* linatafsiriwa na neno *kuzimu* kwenye Agano jipya.Ni wazi wanadamu wote wanaenda kushikiliwa kwenye hii sehemu ya wafu. Kwa sababu hii waalimu wa sheria wa kiyahudi wanakisia kwamba kuna sehemu ya wenye haki na sehemu ya waovu ya kuzimu. Tazama mada maalumu 15:15

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Kwanini Yusufu alificha utambulisho wake?
2. Kwa nini Yusufu aliongea kwa ukali na ndugu zake na kuwalaumu kuwa ni wapelelezi?
3. Kutoka kwenye sura hii nini kinatufanya tufikiri Yakobo alitilia mashaka kifo cha Yusufu?

# MWANZO 43

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Kurudi Misri | kurudi Misri pamoja na Benyamini | Safari ya pili kwenda Misri | Ndugu wa Yusufu wanarudi Misri wakiwa na Benyamini | Wana wa Yakobo wanaondoka tena na Benyamini |
| 43:1-10 | 43:1-7 | 43:1-10 | 43:1-2 | 43:1-10 |
| | | | 43:3-5 | |
| | | | 43:6 | |
| | | | 43:7 | |
| | 43:8-14 | | 43:8-10 | |
| 43:11-15 | | 43:11-15 | 43:11-14 | 43:11-14 |
| | | | | Kukutana na Yusufu |
| Yusufu anamwona Benyamini | 43:15-25 | | 43:15-17 | 43:15-17 |
| 43:16-25 | | 43:16-25 | | |
| | | | 43:18-22 | 43:18-23 |
| | | | 43:23 | |
| | | | 43:24-27 | 43:24-25 |
| 43:26-34 | 42:26-34 | 43:26-34 | | 43:26-34 |
| | | | 43:28 | |
| | | | 43:29-34 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:1-10**

**[1] Njaa ikawa nzito katika nchi. [2] Ikawa walipokwisha kula nafaka waliyoileta kutoka Misri, baba yao akawaambia, Rudini huko, mkatununulie chakula kidogo. [3] Yuda akamwambia akisema, Yule mtu alituagizia sana akisema, Hamtaniona uso wangu, ndugu yenu asipokuwa pamoja nanyi. [4] Ukimpeleka ndugu yetu pamoja nasi, tutashuka na kukununulia chakula. [5] Ila usipompeleka, hatushuki, maana mtu yule alituambia, Hamtaniona uso wangu, ndugu yenu asipokuwa pamoja nanyi. [6] Israeli akasema, Mbona mmenitendea vibaya hata mkamwarifu mtu yule ya kwamba mna ndugu mwingine?[7] Wakasema, Mtu yule alituhoji sana habari**

**zetu na za jamaa yetu, akisema, Baba yenu angali hai? Mnaye ndugu mwingine? Nasi tukamjibu sawasawa na maswali hayo. Je! Tuliweza kujua ya kwamba atasema, Shukeni pamoja na ndugu yenu? [8] Yuda akamwambia Israeli babaye, Mpeleke kijana pamoja nami, tuondoke, tuende zetu, ili tupate kuishi, wala tusife, sisi na wewe na watoto wetu. [9] Mimi nitakuwa mdhamini wake, umtake mkononi mwangu. Nisipomleta tena kwako, na kumweka mbele yako, nitakuwa mwenye hatia mbele yako daima; [10] maana kama hatungalikawia, hakika tungaliisha kurudi mara ya pili.**

**43:2** Andiko halisemi ni muda mrefu mrefu kiasi gani malipo ya kwanza ya nafaka yaliisha, lakini Simoni amekuwa gerezani wakati wote na Yakobo hakuwa amefanyia kazi!
Hatimaye wakati nafaka ilipoisha Yakobo alichukua hatua.

1. rudi tena, BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. tununulie chakula kidogo, BDB 991, KB 1404, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**43:3 "Yuda akamwambia"** Wakati huu katika simulizi Yuda atafanyika mwana wa muhimu. Uongozi wa Rubeni umetoweka.

◙ **"alituonya sana"** Huu ni muundo wa kiundani wa kisarufi (yaani KITENZIJINA HALISI na KITENZI KIKAMILIFU wa mzizi uleule ambao unapatikana katika mstari wa 7 [mara mbili] na mstari wa 20). Hiki KITENZI (BDB 996, KB 1427, *Hiphil* KIKAMILIFU) inamaanisha kushuhudia (kama vile Kut. 19:21; Kumb. 32:46) au kuonya (kama vile Kut 21:29; I Wafalme 2:42; Neh. 13:15, 21).

◙ **"kuona sura yangu"** Hii ni nahau kwa wasikilizaji wa Yusufu (kama vile II Sam. 14:24). Alisimamia mauzo ya nafaka. Ikiwa wasingemuona yeye wasingeweza kununua nafaka (kama vile mstari 5).

**43:4-5** Yuda aliendelea kumuita baba yake, JacobYakobo/Israeli.

1. Tutakwenda chini, BDB 432, KB 434, *Qal* HALI YA KUSIHI
2. tutakununulia chakula, BDB 991, KB 1404, *Qal* HALI YA KUSIHI

Yuda (na ndugu zake) matendo yalikuwa yanategemea juu ya maamuzi ya kumtuma Benyamini.

**43:6** Yakobo anawakosoa kwa kuwasjhirikisha taarifa nyingi kuhusu familia. Yakobo anatumia KITENZI chenye nguvu (BDB 949, KB 1269, *Hiphil* WAKATI MKAMILIFU). Maana yake ya msingi *Hiphil* shina ni "kufanya uharibifu" (kama vile Mwanzo 19:9; 31:7; Kut. 5:22-23; Hes. 11:11; 20:15; Josh. 24:20).

**43:7** Ndugu wanajilinda wenyewe kwa hofu

1. Mtu yule alituhoji hasa kuhusu sisi na ndugu zetu, BDB 981, KB 1371, *Qal* KITENZI JINA HALISI na *Qal* KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU cha mzizi ule ule
2. Ni kwa namna gani aliweza kujua. . ., BDB 393, KB 390, *Qal* KITENZIJINA HALISI na *Qal* KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya mzizi ule ule
3. kwamba angesema, "mleteni ndugu yenu huku," BDB 432, KB 434, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

**43:8-10** Yuda (mwana wanne na mzaliwa wa mwisho wa Lea, kama vile 29:35) anafanyika msemaji tena kwa ajili ya kaka zake wakubwa tisa (kama vile 44:14-34; 46:25-34).

1. mtume kijana pamoja nami, BDB 1018, KB 1511, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. Tutaondoka, BDB 877, KB 1086, *Qal* KITENZI CHENYE KUSIHI
3. tutaondoka, BDB 229, KB 246, *Qal* KITENZI CHENYE KUSIHI
4. Ili tuweze kuishi, BDB 310, KB 309, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika kwa namna ya KITENZI CHENYE KUSIHI.
5. Ili tusiweze kufa, BDB 559, KB 562, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya KITENZI CHENYE KUSIHI (kama vile 42:2)

Pale mkate ulipoanza kuliwa ndio ulikuwa wakati wa kufanya maamuzi. Mantiki ya Yuda ina mashiko (kama vile mstari wa kumi 10). Ikiwa hawatakula chakula, wote watakufa akiwemo Benyamini na Yakobo. Msingi wake unashangaza. Walipaswa waende Misri ili kupata chakula zaidi. Yuda anajaribu kumhakikishia baba yake katika mstari wa 9, ambayo inaonekana kumaanisha imani katika maisha yajayo baada ya kifo.

**43:9 "Mimi nitakuwa mdhamini wake"** Neno "mdhamini" (BDB 786 II, KB 876, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 44:32) inaunganisha sura hii na sura ya 38 (kama vile sura ya 17). Yuda anafanyika mtu wa muhimu zaidi na zaidi (kama vile 49:8-12).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:11-15**
**[11] Israeli, baba yao, akawaambia, Kama ndivyo, fanyeni hivi; twaeni tunu za nchi katika vyombo vyenu, mkamchukulie mtu huyo zawadi, zeri kidogo, na asali kidogo, ubani, na manemane, na jozi, na lozi. [12] Mkatwae fedha maradufu mikononi mwenu, na fedha zile zilizorudishwa kinywani mwa magunia yenu zirudisheni mikononi mwenu; labda zilisahauliwa. [13] Mtwaeni na ndugu yenu, mwondoke na kurudi kwa mtu yule. [14] Mungu Mwenyezi na awape rehema usoni pa mtu yule ili awafungulie ndugu yenu huyo mwingine, na Benyamini. Nami nikifiwa na watoto wangu, nimefiwa. [15] Basi hao watu wakatwaa zawadi ile, wakatwaa na fedha maradufu mikononi mwao, na Benyamini; wakaondoka, wakashuka mpaka Misri, wakasimama mbele ya Yusufu.**

**3:11-14** Yakobo/Israeli anatambua umuhimu na kuwaangiza watoto wake wa kiume wakubwa.
1. fanya hivi, mstari wa 11, BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. Chukua baadhi ya . ., mstari wa 11, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. mpelekeeni mtu yule, mstari wa 11, BDB 432, KB 434, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
4. Chukua fedha maradufu, mstari wa 12, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. Chukua fedha ile iliyorudishwa mikononi mwako, mstari wa 12, BDB 996, KB 1427, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (haya ni matumizi ya tatu nan ne ya KITENZI hiki katika muktadha huu)
6. mchukue ndugu yako, mstari wa 13, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
7. inuka, mstari wa 13, BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
8. mrejeeni mtu yule, 13, BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI
9. Mungu awapeni kuhurumiwa machoni pa mtu yule, mstari wa 14, BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU unaotumika katika HALI YA KUSIHI
10. kwamba aweze kumwachilia ndugu yenu, mstari wa 14, BDB 1018, KB 1511, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

**43:11**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"bidhaa bora katika nchi"** |
| **NKJV** | **"matunda bora ya nchi"** |
| **NRSV** | **"uchaguzi wa vinono vya nchi"** |
| **TEV** | **"vitu bora katika nchi"** |
| **NJB** | **"vinono vya nchi"** |
| **REB** | **"baadhi ya mazao ambayo ni maarufu nchini kwetu"** |

Neno (BDB 275 II) linatumika tu katika Agano la Kale. Mizizi mingine inayo karibiana inaweza kuleta visawe katika muktadha huu "chakula cha Wamisri kilichokubaliwa." NIDOTTE, vol. 1, ukurasa wa 119 inasema kuwa inahusiana na "nguvu," lakini hiyo haishabihiani na muktadha huu.

Orodha ya vitu inatolewa ambayo ilikuwa sehemu ya mara kwa mara ya magari ya safari (kama vile 37:25). Yusufu alijua bidhaa vizuri kwakuwa alitakiwa kusafiri na magari haya (kama mtumwa) kwa Misri.

**43:12**

**NASB, TEV**

**NJB, LXX**

**JPSOA "kosa"**

**NKJV, NRSV "dosari"**

Neno (BDB 993) linapatikana hapa. Mzizi unaweza kumaanisha "kupotea" au "kufanya makosa." Katika Ayubu 12:16 inafasiriwa "kupotosha." NIDOTTE, vol. 4, kr. 44, inasema kuwa mzizi unaashiria "kupewa agizo la makusudi la kwenda kutenda matendo yasiyofaa" (kama vile Lawi 4:13; I Sam. 26:21; Zab. 119:21,118; Ezek. 45:20).

**43:14 "Mungu Mwenyezi na awape rehema usoni pa mtu yule"** Yakobo anawatuma waondoke kwa jina la Mungu wa agano. Jina hili, *El Shaddai*, kwa mara ya kwanza lilitumiwa na Ibrahimu (kama vile Mwanzo 17:1; 28:3; 35:11; 43:14; 48:3). Neno *El* ni jina la ujumla la Mungu katika Mashariki ya Karibu ya kale na inaonekana kutokea katika mzizi, "kuwa imara." Neno *Shaddai* inaweza kutokea katika matiti ya mwanamke na ikimaanisha "Mwenye-Utoshelevu wote." Inaonekana kutokea Kutoka 6:3 kwamba neno hili *El Shaddai* lilikuwa limezoeleka kama Mungu wa Mababa wa imani.

**43:15** Kuletea zawadi kulikuwa maarufu kuliko zoeleka kama jambo la kiutamaduni la tabia njema. Vitu hivi vilivyoorodheshwa vingekuwa vya kipekee Kanaani na vingetafutwa huko Misri, lakini havikuwa vinatosha kufanya familia ya mtu na mifugo iendelee na uhai. Kutolewa kwa "zawadi" (BDB 585) ni sawasawa na zawadi za Yakobo kwa Esau katika Mwanzo 32.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:16-25**
**16 Naye Yusufu alipomwona Benyamini pamoja nao, akamwambia msimamizi wa nyumba yake, Uwalete watu hawa nyumbani, ukachinje na kuandalia, maana watu hawa watakula pamoja nami adhuhuri.**
**17 Yule mtu akafanya kama Yusufu alivyomwambia Naye akawaleta watu hao nyumbani mwa Yusufu.**
**18 Lakini watu hao wakaogopa kwa sababu wameletwa nyumbani mwa Yusufu, wakasema, Kwa sababu ya fedha zile zilizorudishwa katika magunia yetu mara ya kwanza tumeletwa humu; apate kutushitaki, na kutuangukia, atutwae sisi kuwa watumwa, na punda zetu.**
**19 Wakamkaribia yule msimamizi wa nyumba ya Yusufu, wakasema naye mlangoni pa nyumba.**
**20 Wakamwambia, Tazama, bwana, kweli tulishuka mara ya kwanza ili tununue chakula.**
**21 Ikawa, tulipofika nyumba ya wageni, tukafungua magunia yetu, kumbe! Fedha za kila mtu zilikuwako kinywani mwa gunia lake, fedha zetu kwa uzani wake kamili; nasi tumezileta tena mikononi mwetu.**
**22 Nasi tumeleta fedha nyingine mikononi mwetu ili tununue chakula; hatujui ni nani aliyezitia fedha zetu katika magunia yetu.**
**23 Akawaambia, Amani iwe kwenu, msiogope; Mungu wenu, naye ni Mungu wa baba yenu, amewapa akiba katika magunia yenu; fedha zenu ziliniwasilia. Kisha akawatolea Simeoni.**
**24 Mtu yule akawaleta wale watu nyumbani mwa Yusufu, akawapa maji, wakatawadha miguu, akawapa punda zao chakula.**
**25 Wakaiweka tayari ile zawadi hata atakapokuja Yusufu adhuhuri, maana wamesikia ya kwamba watakula chakula huko.**

**43:16** Wakati Yusufu alipomuona Benyamini akiandaa mlo wa mchana.

1. waleteni watu nyumbani, BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. chinja *mnyama*, BDB 370, KB 368, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. andaa tayari, BDB 465, KB 464, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

Watu wa Misri zaidi walikuwa wakila samaki na ndege na mboga za majani na mkate/ngano. Kuchinjwa kwa mnyama mkubwa kulifanyika nyumbani na katika shuguli maalumu tu (kama vile James W. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, ukurasa wa 50).

**43:18 "apate kutushitaki"** Hii ni sitiari isiyokuwa ya kawaida na nadra. KITENZI (BDB 164 II, KB 193, *Hithpoel* TUNGO KITENZI JINA) inamaanisha "kukunja" au "kukunjua." Hapa inamaanisha "kumkunja mtu ili kusababisha

mateso." Matumizi mengine katika shina hili yapo tu katika II Sam. 20:12, ambapo inaashiria kukunja katika damu ya mtu mwenyewe.

◙**"kutuangukia"** KITENZI hiki (BDB 656, KB 709, *Hithpael* TUNGO KITENZIJINA), katika shina *Qal* inatumika kwa kuvamiwa (kama vile Yosh. 11:7; Ayubu 1:15) au kuangukia mikononi (nguvu) ya adui (kama vile Waamuzi 15:18). Matumizi ya KITENZI HIKI katika shina hili ni ya kipekee katika andiko.

Ndugu hawa hawakuelewa kwanini walikuwa wanaletwa katika nyumba ya Yusufu na walikuwa wamejaa woga. Walifikiri kwamba ilikuwa inahusuiana na safari yao ya kwanza na fedha iliyokuwa katika magunia (kama vile mistari ya 20-22).

**43:19 "Wakamkaribia yule msimamizi wa nyumba ya Yusufu"** Mtu huyu anaonekana kuwa mtu anayejua sana. Huu si ukweli tu wa maelezo ya mpango wa Yusufu, lakini thiolojia ambayo inatufahamisha imani ya Yusufu. Ni makisio yangu kwamba Yusufu alikuwa amewashirikisha wanafamilia wa nyumba yake na wenzake wa Misri kuhusu imani yake binafsi kwa Mungu wa Agano wa Ibrahimu. Inafurahisha kwamba wana wa Yakobo katika mstari wa 18 wanajawa na shangwe sana mbele ya uzuri wa Misri kwamba wangekuwa na woga wa kichungaji juu ya mtu kutaka kuvamia mifugo yake. Hii ni mfano wa ukweli "jamaa wa shamba waliokuwa wamepata fursa ya kuingia mjini."

**43:20 "kweli tulishuka mara ya kwanza"** Tungo hii imezidishwa na matumizi ya KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI ULIO TIMILIFU cha mzizi ule ule (BDB 432, KB 434, yote *Qal* mashina).

**43:23 "Amani iwe kwenu"** Hakuna KITENZI, ni KIUNGANISHI na NOMINO *shalom*. Ni KAULI SHURUTISHI iliyomaanishwa.

◙**"msiogope"** KITENZI hiki (BDB 431, KB 432) ni *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU inayotumika katika namna ya KITENZI CHA KUSIHI.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:26-34**
**26 Alipokuja Yusufu nyumbani, wakamletea ile zawadi iliyokuwa mikononi mwao nyumbani mwake,**
**wakamwinamia mpaka nchi. 27 Akawaulizia hali yao, akasema, Je! Baba yenu, yule mzee mliyemnena,**
**hajambo? Angali hai? 28 Wakasema, Mtumwa wako baba yetu hajambo, angali hai; wakainama, wakasujudu. 29**
**Akainua macho yake, akamwona Benyamini, nduguye, mwana wa mamake, akasema, Huyu ndiye ndugu yenu**
**mdogo, mliyeniambia habari zake? Akasema, Mungu akufadhili, mwanangu. 30 Yusufu akafanya haraka, kwa**
**sababu moyo wake ulimwonea shauku nduguye, akatafuta pa kulia, akaingia chumbani mwake, akalia humo. 31**
**Akanawa uso, akatoka, akajizuia, akasema, Leteni chakula. 32 Wakamwandalia yeye peke yake, na wao peke**
**yao, na wale Wamisri waliokula pamoja naye peke yao; maana Wamisri hawawezi kula pamoja na Waebrania,**
**kwa kuwa ni chukizo kwa Wamisri. 33 Wakaketi mbele yake, mzaliwa wa kwanza kwa cheo cha kuzaliwa kwake,**
**na mdogo kwa udogo wake; watu hao wakastaajabu wao kwa wao. 34 Wakapelekewa sehemu za chakula**
**kutoka mezani pake, lakini akazidisha sehemu ya Benyamini iwe kubwa mara tano kuliko zao. Wakanywa,**
**wakafanya furaha pamoja naye.**

**43:27,29** Yusufu anauliza mfululizo wa maswali kuhusu familia yao. Lazima walikumbuka hisia za ndani za baba yao kuhusu kutoa siri (kama vile mstari wa 6).

1. Je baba yenu anaendelea vizuri (hakuna KITENZI, kwa *shalom* angalia 29:6)
2. Je bado yuko hai (hakuna KITENZI)
3. Je huyu ni mdogo wenu wa mwisho (hakuna KITENZI)

**43:29 “Akasema, Mungu akufadhili, mwanangu”** Yusufu anamtenga Benyamini kwa ajili ya salamu maalumu (“uwe na neema,” BDB 335, KB 334, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI).

Tazama Yusufu anaelezea mtazamo wake wa kiulimwengu wa kithiolojia.

**43:30 “Yusufu akafanya haraka, kwa sababu moyo wake ulimwonea shauku nduguye”** Hii inafasiriwa kibayana “his compassions were warmedhuruma zake zilipokelewa vyema” (BDB 485, KB 481, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIDU, kama vile Wafalme. 3:26). Neno “huruma” (BDB 933) kifasihi linamaanisha “kuwa na hisia za upendo na huruma baina ya watu watokao katika tumbo moja” (yaani upendano wa kindugu).

**43:31 “Leteni chakula”** Hii kifasihi ni “kuandaa chakula” (BDB 962, KB 1321, *Qal* KAULI SHURUTISHI). Inafurahisha kwamba mistari ya 31-33 kwamba Wamisri walikuwa wakikaa katika viti wakiizunguka meza wakati wa chakula chao, wakati Wakanaani Waebrania walikaa na kuwekea nguzo kishoka chao cha mkono wa kushoto. Kulikuwa na mvutano wa kiutamaduni kati ya Wamisri na Wakanaani (hapa waebrania), kama vile mstari wa 32. Hii inashabihiana na mazingira ya kihistoria kwa uhakika na kuonesha historia ya masimulizi haya (kama vile James M. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, ukurasa wa 52).

**43:32 “Wakamwandalia yeye peke yake”** Inaonekana kwamba Benyamini tu ndiye aliyetenga kwa ajili ya mkao na chakula maalumu na pia chakula cha ziada (kama vile mstari wa 34). Inavyoonekana Yusufu anajaribu kuwafanya ndugu wengine wawe na wivu kuona mwitikio wao. Alikuwa anajaribu kuona ikiwa tabia ileile ambayo ilizalisha hali zao wenyewe na ya kwake miaka ishirini iliyopita kabla ikiwa ilikuwa bado ipo au kama walikuwa wamekwisha kupatana kwasababu ya miaka kupita.

◙**“maana Wamisri hawawezi kula pamoja na Waebrania, kwa kuwa ni chukizo kwa Wamisri”** Hii inaweza kuwa maelezo mazuri ya Mwanzo 39:6 of juu ya kwanini Potifa alijali sana kuhusu chakula chake mwenyewe. Baadhi wanamnukuu Heroditus, 2:41, kama historia ya kuthibitisha kutoa msaada wa ushirikiano wa mtazamo huu. Inaonekana kwamba Wamisri walikuwa na hasira juu ya wale wote waliokuwa wakila mbuzi kwakuwa walichukulia mbuzi kama vitu vilivyotengwa kwa ajili ya ibada, sawa kabisa na wahindu. Hii inaweza kuelezea Mwanzo 46:34 na Kutoka 8:26.

**43:33** Inavyoonekana, Watumwa wa misri waliwakarisha ndugu katika mfuatano kulingana na kuzaliwa kwao. Je walijuaje hili? Yusufu anaendelea kufunua utambulisho wake.

**43:34 “lakini akazidisha sehemu ya Benyamini iwe kubwa mara tano kuliko zao”** Inaonekana kwa uwezekana kwamba namna “tano” ni namba muhimu katika Misri ktika nyakati zote ambazo “tano” inatokea mara kwa mara (kama vile 43:34; 45:6,11,22; 47:2,24). Mtu ananaweza kushangaa kitu gani ndugu walifikiria wakati Yusufu alipo wahudumia mezani na kumpatia Benyamini chakula cha ziada?!

Neno “kiasi” (BDB 673) inaashiria sehemu ya chakula (kama vile II Sam. 11:8; Esta 2:18; Yer. 40:5). Haikuwa nyama!

◙ **“Wakanywa, wakafanya furaha pamoja naye”** VITENZI wiwili (“kunywa,” BDB 1059, KB 1667 na “kulewa,” BDB 1016, KB 1500) inafanana sana kimfanano (kama vile Mwanzo 9:21). Sherehe nzuri kiasi gani waliyokuwa nayo!

# MWANZO 44

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Ndugu zake Wanarejeshwa | Kikombe cha Yusufu | Yusufu Anawajaribu Ndugu zake mara ya Mwisho | Kikombe Kinakosekana | Kikombe cha Yusufu ndani ya Gunia la Benjamini |
| 44:1-5 | 44:1-5 | 44:1-5 | 44:1-5 | 44:1-2 |
| | | | | 44:3-5 |
| 44:6-13 | 44:6-13 | 44:6-13 | 44:6-9 | 44:6-13 |
| | | | 44:10-13 | |
| 44:14-17 | 44:14-17 | 44:14-17 | 44:14-15 | 44:14-17 |
| | | | 44:16 | |
| | | | 44:17 | |
| | Yuda anaomba Radhi kwa ajili ya Benjamini | | Yuda Anamtetea Benjamini | Yuda Anaingilia Kati |
| 44:18-34 | 44:18-34 | 44:18-34 | 44:18-23 | 44:18-34 |
| | | | 44:24-29 | |
| | | | 44:30-34 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:1-5**
[1] **Akamwamuru yule msimamizi wa nyumba yake akisema, Jaza magunia ya watu hawa chakula kwa kadiri wawezavyo kuchukua, utie na fedha ya kila mtu kinywani mwa gunia lake.** [2] **Na kikombe changu, kikombe kile cha fedha, ukitie kinywani mwa gunia la yule mdogo pamoja na fedha ya nafaka yake. Akafanya kama vile alivyomwambia Yusufu.** [3] **Asubuhi kulipopambazuka, hao watu wakapewa ruhusa, wao na punda zao.** [4] **Na walipotoka mjini, wala hawajaendelea sana, Yusufu akamwambia yule msimamizi wa nyumba yake, Ondoka, uwafuate watu hawa, nawe utakapowapata, waambie, Kwa nini mmelipa mabaya kwa mema?** [5] **Je! Kikombe hiki, sicho anyweacho bwana wangu? Naye hufanya uaguzi kwa hicho. Mmefanya vibaya kwa kufanya hivi.**

**4:1 Hii ni mara ya pili kwa Yusufu kutenda jambo hili** (kam vile 42:25).

1. Jaza, BDB 569, KB 583, *Piel* ya KAULI SHURUTISHI
2. utie, BDB 962, KB 1321, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI

**44:2 Kuhamishia kikombe cha fedha cha Yusufu** (kama vile mst. wa 5) ndani ya gunia la Benjamini ni njama mpya. Bado Yusufu anaendelea kuwajaribu ndugu zake ilia one kama wivu wao na fujo zao dhidi ya ndugu yake kamili (watoto wa Raheli) zimemalizika. **Yapaswa kufahamika kwamba hili neno lililotafsiriwa kama** "kikombe" (BDB 149) ni chombo kikubwa, huenda ni bakuli ama gudulia (kama vile Yer. 35:5). Neno la kawaida la "kikombe" lionapatikana katika BDB 468 I (kama vile 40:11,13,21; II Sam. 12:3; Zab 16:5; 23:5; Mit. 23:31).

**44:4 "mjini "** Ni mji gani, unategemeana na alipokuwa Farao. Baadaye katika Mwanzo inaonekana kwamba Yusufu anazungunza na baba yake katika nchi ya Gosheni na Farao alikuwa alikuwa katika makazi yale yale katika siku hizo. Kifungu hiki kinamaanisha makao yaliyokuwa katika eneo delta. Wahyksos walikuwa na makazi yao hapa. Farao aliyefuatia alihamishia makao katika eneo hili la Seti. Hutu alikuwa Farao wa kuwatesa watu wa Israeli kambla ya kipindi cha uhamisho, huenda ni wakati wa utawala wa Rameses II.
Angalia See OT Survey, Introduction to Exodus katika www.freebiblecommentary.org.

◙ Yusufu alitoa amri kwa wasimamizi wake kuyafuatisha matendo yake.

1. ondoka, BDB 877, KB 1086, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. wafuate, BDB 922, KB 1191, *Qal ya KAULI SHURUTISHI*
3. nawe utakapowapata BDB 673, KB 727, *Hiphil* ya *KAULI YA WAKATI TIMILIFU* iliyotumika katika maana ya jambo la muda tu. Hili ni neno la kiuwindaji lenye kumaanisha kumkimbiza mnyama. Hili lilitumiwa na Labani kumkimbiza Yakobo (kama vile 31:25).
4. waambie Kwa nini(kwa kuwauliza swali) !

◙ **"Kwa nini mmelipa mabaya kwa mema"** Toleo la Kale la Kiyunani (LXX) (likifuatiwana toleo la NRSV, TEV) baada ya maelezo haya linaongeza "Kwa nini mmeiba kikombe changu cha fedha?" Toleo la Peshitta halina nyongeza hii.

**44:5 "Kikombe hiki, sicho anyweacho bwana wangu? Naye hufanya uaguzi kwa hicho"** Katika sura hizi tatu zote Yusufu amekuwa akiendelea kutafuta njia ambayo angetumia kuijaribu tabia ya ndugu zake. Hata hivyo, kwa namna Fulani inashangaza kuona yeye anataja neno uaguzi (BDB 638, KB 690 katika muundo wa sarufi uliochochewa wa KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi ule ule, kama vile mst. 15). Hiki kinaweza kuwa kifuniko kingine cha Kimisri, kwa viongozi walio wengi nchini Misri ambapo katika kipindi hiki kungekuwepo na waaguzi ama wangevitumia vikombe hivi. Hili neno kiuhalisia linamaanisha "kunong'oneza" ama "kunyata" (kama vile Law. 19:26 na Kumb. 18:10, ambapo baadaye inachukuliwa hukumu). Katika Toleo la Kale la Kiyuanani neno hili linatafsiriwa kama "ubashiri" ambapo inamaanisha kuyafahamu mapenzi ya Mungu kwakutazama kupaa kwa ndeges.Toleo la Jerusalem Bible inakifafanua kifungu hiki katika tambihi (uk. 67) kwamba uaguzi ulifanywa kwa

1. kwa kumimina maji ndani ya kikombe (kumiminwa)
2. kupitia sauti iliyo sikia wakati wa kumimina maji ndani ya kikombe

3. ule mgawanyiko wa matone yaliyomiminwa ndani ya kikombe (umiminaji) yaliyotumika katika Mashariki ya Karibu ya kale. S. R. Driver anaongeza lingine
4. vipande vya dhahabu, fedha, ama mawe ya thamani vilidondosha ndani ya kikombe na mgawanyiko wao ama mpangilio wao ulichukuliwa kumbukumbu (kama vile UBS, *Handbook on Genesis*, uk. 989).

Habari zaidi kuhusu mbinu za uaguzi zinatoka katika maandiko ya kale ya Babeli (pia tambau mbinu zilizofuatia katika Eze. 21:21). Hakuna habari zaidi zinazohusu njia za uaguzi katika kipindi hiki cha historia ya Kimisri (angalia *James M. Freeman, Manners and Customs of the Bible*, kr. 52-54)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:6-13**

**[6] Akawafuata, akawapata, na kuwaambia maneno hayo. [7] Wakamwambia, Kwa nini bwana wangu anasema maneno kama haya? [8] Hasha! Watumwa wako wasifanye hivi; tazama, hizo fedha mlizoziona kinywani mwa magunia yetu, tumekuletea tena kutoka nchi ya Kanaani. Tuwezeje sisi kuiba nyumbani mwa bwana wako fedha au dhahabu? [9] Atakayeonekana kuwa nacho miongoni mwa watumwa wako, na afe, na sisi nasi tutakuwa watumwa wa bwana wangu. [10] Akasema, Basi na iwe hivyo kama mlivyosema, Mtu atakayeonekana kuwa nacho atakuwa mtumwa wangu, na ninyi mtakuwa hamna hatia. [11] Wakafanya haraka, wakashusha kila mtu gunia lake, na kufungua kila mtu gunia lake. [12] Naye akatafuta, akaanza kwa mkubwa na kuisha kwa mdogo. Kikombe kikaonekana katika gunia la Benyamini. [13] Wakararua nguo zao, wakaweka kila mtu mzigo wake juu ya punda wake, wakarudi mjini.**

**44:6-13 Mistari hii ni majibizano kati ya msimamizi wa Yusufu** (pia angalia 43:16-25) na ndugu zake.

**44:9** Mwitikio huu unafanan sana ule ulioonyeshwa na Yakobo alipokuwa ndani ya nyumba ya Labani (kama vile 31:32). Huu ni mwitikio wa kiuaminifu na bado wataendelea kutubia kosa lao kwa kutumia semi hizi pale kikombe kitakapokutwa ndani ya mfuko wa Benjamini.

**44:10 "Basi na iwe hivyo kama mlivyosema, Mtu atakayeonekana kuwa nacho atakuwa mtumwa wangu, na ninyi mtakuwa hamna hatia"** Kifungu hiki pia kinaonekana kuwa njama ya mwisho ya kuona kama watamtelekeza Benjamini au kama watashirikiana pamoja kama nyumba moja. Kwa namna fulani ingekuwa rahisi kumwacha Benjamini (kama vile mst. wa 17) na kuondoka haraka kwa ajili ya usalama (kama walivyofanya katika kifungo cha Simeoni). Hili neno linalotafsiriwa kama "asiye na hatia" (BDB 667) mara kwa mara linatafsiriwa kama "asiye na mawaa." Hili neno linatumika katika njia kadhaa.

1. katika maana ya kisheria, Kut. 23:7
2. linarejelea kiapo, Mwa. 24:41; Yos. 2:17,20
3. linamrajelea mtu, Ayubu 4:7; 9:23; 17: 8; 22:19,30; 27:17; Zab. 10:8; 15:5; Mit. 1:11 Huu usemi ullionenwa na msimamizi huyu utatabiri semi za Yusufu zilizo katika mst. wa 17.

**44:12 "akaanza kwa mkubwa na kuisha kwa mdogo"** Huu ufahamu wa kuanza na ndugu kulingana na mtiriko wa kuzaliwa kwa mara ya kwanza uliwashangaza (kama vile 43:33). Na sasa msimamizi huyu anatambua hali hii. Msimamizi alikuwa mtu wa karibu na mwenye kuaminiwa sna na Yusufu. Mtu huyu aliyashanga maisha ya Yusufu namna alivyokuwa na imani.

**44:13 "Wakararua nguo zao"** Hakuna neno linaloeleza juu ya hofu yao! Katika utamaduni wa Kitahudi hii ni moja ya ishara za kuomboleza. Angalia Mada Maalum: Ibada za Huzuni katika 37:29.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:14-17**

**[14] Akaja Yuda na ndugu zake nyumbani kwa Yusufu, naye mwenyewe alikuwamo, nao wakamwangukia kifudifudi. [15] Yusufu akawaambia, Ni tendo gani hili mlilolitenda? Hamkujua ya kwamba mtu kama mimi naweza kufanya uaguzi? [16] Yuda akasema, Tumwambie nini bwana wangu? Tusemeje! Tujivutieje haki? Mungu ameona uovu wa watumwa wako. Tazama, sisi ni watumwa wa bwana wangu, sisi na yeye ambaye kikombe kilionekana mkononi mwake. [17] Akasema, Hasha! Nisifanye hivi; mtu ambaye kikombe kilionekana mkononi mwake, ndiye atakayekuwa mtumwa wangu. Nanyi enendeni zenu kwa amani kwa baba yenu.**

**44:15** Huu ni usemi wenye makosa. Huu umetengenezwa ili kuingiza mvutano katika hali hii. Yusufu hakustaajabu juu ya wizi wao; kwani aliusababisha yeye!

**44:16** Yuda udahndiye msemsji wa kundi. Alimuuliza Yusufu maswali kadhaa ambayo alifahamu majibu yake.

1. Tumwambie nini bwana wangu?
2. Tusemeje?
3. Tujivutieje haki (BDB 842, KB 1003, *Hithpael* ya KAULI ISIO TIMILIFU)?
4. mst. wa 18 pia ni swali
5. mst. wa 19 pia ni swali
6. mst. wa 34 pia ni swali

◙ **"Mungu ameona uovu wa watumwa wako"** Hapa tena kipengele cha kithiolojia cha usaliti na kumuuza Yusufu kinaonekana kusababisha hisia za (BDB 730, kama vile 4:13; 15:16; 19:15) mashaka ambazo zilibaki ndani ya mioyo ya ndugu zake kwa miaka yote hii (kama vile 42:21-22,28). Hata hivyo, ndugu zake wanaonekanak ubadilika kiuweki kwa kuwa waliungana katika kumlinda Benjamini naYuda alitumia njia za ziada (kama vile mist. ya 18-34, hasa mist. ya 32-33). Ombi hili liko katika kiwango kile kile kama yalivyo maombi ya Ibrahimu ya kusihi, Musa, na Paulo.

## MADA MAALUMU: MAOMBI YA KUSIHI

I. Utangulizi
   A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
      1. Maombi binafsi, Mk. 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
      2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk. 11:17; Luka 19:46
      3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
   B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
   C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile Yakobo 4:2)
   D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
   E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.
   F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
      1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
      2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
      3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
      4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
      5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba
   G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

II. Taarifa za Kibiblia
   A. Agano la Kale
      1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
         a. Ibrahimu aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22 na kuendelea
         b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
            1) Kutoka 5:22-23
            2) Kutoka 32:9-14,31-35
            3) Kutoka 33:12-16

4) Kutoka 34:9
5) Kumb. 9:18,25-29

c. Samweli akiombea Israel
    1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
    2) 1 Samweli 12:16-23
    3) 1 Samweli 15:11

d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18

2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
    a. Zaburi 66:18
    b. Mithali 28:9
    c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya
    1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho
        a. Yesu
            1) Warumi 8:34
            2) Waebrania 7:25
            3) 1 Yohana 2:1
        b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
    2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi
        a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
            1) Warumi 9:1na kuendelea
            2) Warumi 10:1
        b. Akiliombea kanisa
            1) Warumi 1:9
            2) Waefeso 1:16
            3) Wafilipi 1:3-4,9
            4) Wakolosai 1:3,9
            5) 1 Wathesalonike 1:2-3
            6) 2 Wathesalonike 1:11
            7) 2 Timotheo 1:3
            8) Filemoni, uk. 4
        c. Paulo analiomba kanisa limwombee
            1) Warumi 15:30
            2) 2 Wakorintho 1:11
            3) Waefeso 6:19
            4) Wakolosai 4:3
            5) 1 Wathesalonike 5:25
            6) 2 Wathesalonike 3:1
    3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi
        a. Kuombeana wao kwa wao
            1) Waefeso 6:18
            2) 1 Timotheo 2:1
            3) Yakobo 5:16
        b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
            1) Adui zetu, Mt. 5:44
            2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
            3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
            4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
            5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa
   A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
      1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
      2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
      3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Yuda 20
      4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

   B. Visababishi
      1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
      2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
      3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
      4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3
   C. Mitazamo mingine
         a. Usitahimilivu
         b. Luka 18:1-8
         c. Wakolosai 4:2
      1. Endelea kuomba
         a. Mathayo 7:7-8
         b. Luka 11:5-13
         c. Yakobo 1:5
      2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
      3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo
         a. Zaburi 66:18
         b. Mithali 28:9
         c. Isaya 59:1-2
         d. Isaya 64:7
IV. Hitimisho la kithiolojia
   A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
   B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
   C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

**44:17 "Hasha! Nisifanye hivi "** Haya ni maelezo ya kinahau yakutofanya jambo lo lote ambalo lingeleta machafuko katika maadili au usawa wa kidini (kama vile Mwa. 18:25; Yos. 22:29; 24:16; I Sam. 2:30; 20:2,9;22:15; II Sam. 20:20; 23:17).

◙ **"enendeni zenu kwa amani kwa baba yenu"** Hii amri (BDB 748, KB 828, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI) mara nyingi hotolewa kwa ajili ya kuchochea hali iliyopo. Hawa ndugu wasingeweza kurudi nyumbani pasipokuwa na Benjamini kwa sababu waliogopa kuwa wasababishi wa kifo cha Yakobo (kama vile mst. ya 30-31). Hapa panaonekana kutowepo na tumaini la amani!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:18-34**
[18] **Ndipo Yuda akamkaribia, akasema, Tafadhali, bwana wangu, mtumwa wako na aseme neno moja masikioni mwa bwana wangu, wala hasira yako isimwakie mtumwa wako, maana wewe u kama Farao.** [19]
**Wewe, bwana wangu, ulituuliza watumwa wako, ukisema, Je! Mnaye baba, au ndugu?** [20] **Tukakuambia wewe,**
**bwana wangu, Tunaye baba, naye ni mzee, na mwana wa uzee wake ni mdogo, na nduguye amekufa; amebaki**
**yeye peke yake wa katika tumbo la mamaye, na baba yake anampenda.** [21] **Ukatuambia watumwa wako,**
**Mleteni kwangu, ili macho yangu yamwangalie.** [22] **Tukakuambia, bwana wangu, Kijana hawezi kumwacha**
**babaye, maana akimwacha babaye, babaye atakufa.** [23] **Ukatuambia watumwa wako, Asiposhuka ndugu yenu**
**mdogo pamoja nanyi, hamtaniona uso wangu tena** [24] **Ikawa tulipokwenda kwa mtumwa wako, baba yangu,**
**tukamwarifu maneno yako, bwana wangu.** [25] **Kisha baba yetu akanena, Rudini huko, mkatununulie chakula**

**kidogo.** [26] **Tukasema, Hatuwezi kwenda; ndugu yetu mdogo akiwapo pamoja nasi, tutashuka, maana hatutaweza kuuona uso wa mtu huyo, ndugu yetu mdogo asipokuwa pamoja nasi.** [27] **Mtumwa wako, baba yangu, akatuambia, Mnajua ya kuwa mke wangu alinizalia wana wawili;** [28] **mmoja alitoka kwangu, nikasema, Bila shaka ameraruliwa, wala sikumwona tangu hapo.** [29] **Na mkiniondolea huyu naye, na madhara yakimpata, mtashusha mvi zangu na msiba kaburini.** [30] **Basi, nikienda kwa mtumwa wako, baba yangu, na huyu kijana hayupo pamoja nasi, iwapo roho yake imeshikamana na roho ya kijana;** [31] **itakuwa atakapoona ya kwamba huyu kijana hayuko, atakufa; na watumwa wako watashusha mvi za mtumwa wako, baba yetu, kwa huzuni kaburini.** [32] **Kwa maana mtumwa wako alijifanya mdhamini wa huyu kijana kwa baba yangu, nikisema, Nisipomrudisha kwako, nitakuwa na hatia kwa baba yangu sikuzote.** [33] **Basi, sasa nakusihi, uniache mimi mtumwa wako nikae badala ya huyu kijana kuwa mtumwa wa bwana wangu; na huyu kijana umwache aende pamoja na nduguze.** [34] **Kwa maana nitawezaje kumwendea baba yangu, na huyu kijana hayuko pamoja nami? Nisije nikayaona mabaya yatakayompata baba yangu.**

**44:18-34** Yuda akamwambia tena kile kilichotokea katika mjadala uliohusu safari mbili za ndugu zake kwenda Misri kununua chakula na mvutano uliotokea nyumbani kuhusu safari ya mara yapili akiwa na Benyamini.

**44:18 "masikioni mwa bwana wangu"** Hii ni nahau ya kifungu "naweza kuzungunza vema pamoja nawe" (kama vile 20:8; 23:10,13,16;50:4; Kumb. 5:1; 31:11,28,30).

◙ **"hasira yako isimwakie "** Yuda anaomba (BDB 354, KB 351, *Qal* cha KAULI AMRISHI) Yusufu hakuwa na hasira hata kidogo (kama vile 30:2; 39:19), bali alimtaka aeleze kuhusu hali ya nyumba yao katika uhusiano na huyu ndugu yake mdogo.

**44:28 "Bila shaka ameraruliwa"** Huu ni muundo wa kisarufi ulioimarishwa (KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU cha mzizi huo huo, BDB 382, 380), ambao pia unapatikana katika 37:33.

**44:30 "Basi ,nikienda kwa mtumwa wako, baba yangu, na huyu kijana hayupo pamoja nasi, iwapo roho yake imeshikamana na roho ya kijana"** Hii inaonyesha jambao Fulani ambalo Yakobo analichukua kwa makini kutoka kwa Benjamini. Dhana hii ya maisha iliyowekewa mipaka (BDB 905, KB 1153, *Qal* cha KAULI TENDAJI YA WATI ENDELEVU) pia inatumika kueleza upendo wa ajabu na urafiki kati ya Daudi na Yonathani katika I Sam. 18:1. Yakoboa alikuwa akihuzunika tangu alipompoteza Yusufu na alikuwa anafarijika kwa kumtegemea mwana mwingine wa mke wake aliyekuwa amekwisha kufa ambaye alimpenda sana, Raheli.

**44:33 Hii mistari ina KAULI TATU AMRISHI**. Yuda anaomba kwa ajili ya Benjamini ili aachiliwe na kurudi nyumbani.

1. huyu kijana kuwa mtumwa (yaani, Juda) abaki (kifasihi. "akae"), BDB 442, KB 444, *Qal* ya KAULI AMRISHI
2. huyu kijana umwache aende pamoja na nduguze , BDB 748, KB 828, *Qal* ya KAULI AMRISHI

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yusufu aliwatenda ndugu zeke kwa namna ya ukali?
2. Kwa nini Yusufu anaonekana kufanya mambo ya ajabu katika sura hii katika uhusiano na ndugu zake?
3. Kwa nini Yusufu alimtaka Benjamini aje Misri?
4. Orodhesha maana za kithiolojia za dhanbi iliyokusudiwa inayotawala ubaadaye wa mtu.

# MWANZO 45

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yusufu anawakarimu Ndugu zake | Yusufu anajifunua kwa ndugu zake | Yusufu anajitambulisha kwa ndugu zake | Yusufu anawaambia ndugu zake ye ni Nani | Yusufu anajitambulisha kwa ndugu zake |
| 45:1-3 | 45:1-5 | 45:1-3 | 45:1-8 | 45:1-2 |
| | | | | 45:3-8 |
| 45:4-15 | | 45:4-15 | | |
| | | | 45:9-11 | 45:9-13 |
| | | | 45:12-13 | |
| | | | 45:14-15 | 45:14-15 |
| | | | | Mwaliko wa Farao |
| 45:16-20 | 45:16-20 | 45:16-20 | 45:16-20 | 45:16-20 |
| | | | | Kurejea Kanaani |
| 45;21-23 | 45:21-24 | 45:21-24 | 45:21-24 | 45:21-24 |
| 45:24-28 | | | | |
| | 45:25-28 | 45:25-28 | 45:25-26 | 45:25-28 |
| | | | 45:27-28 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## HISTORIA YA NYUMA

A. Katika sura za 42-44 Yusufu aliwajaribu ndugu zake kuona ikiwa mtazamo wao wa hila hasa juu ya watoto wa Raheli, ulikuwa umebadilika. Hii kimsingi ilioneshwa kupitia matendo yao yaliyohusiaa na Benyamini.

B. Sura ya 45 na 46 inahusiana na ufungaji wa sehemu ya Yusufu kupata mamlaka na kutimilizwa kwa mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wa kimwili wa Yakobo na familia ya agano wakati wa miaka saba ya njaa.

C. Sura ya 45, mistari ya 5-9, inauhusiana mkali sana kama tunavyoona mkono wa Mungu ulivyo dhahiri katika maisha ya Yusufu katika kile kinachoonekana hali au mazingira magumu. Ikiwa tungejifunza kweli hii katika maisha yetu, ni utofauti gani wa aina gani ambao tungeweza kuutengeneza. Hakuna kitu kinachotokea tu kwa watoto wa Mungu (Angalia Hannah Whithall Smith's *The Christian's Secret of a Happy Life*).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:1-3**
**[1] Hapo Yusufu hakuweza kujizuia mbele yao wote waliosimama karibu naye. Akapiga kelele, na kusema, Mwondoeni kila mtu mbele yangu. Wala hakusimama mtu pamoja naye, Yusufu alipojitambulisha kwa nduguze. [2] Akapaza sauti yake akalia, nao Wamisri wakasikia. Watu wa nyumba ya Farao nao wakasikia. [3] Yusufu akawaambia ndugu zake, Mimi ndimi Yusufu; baba yangu angali hai bado? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu, maana waliingiwa na hofu mbele yake.**

**45:1"Hapo Yusufu hakuweza kujizuia mbele"** Hiki ni KITENZI (BDB 407, KB 410, kinachohasisha *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU na *Hithpael* TUNGO KITENZI JINA, BDB 67, KB 80), ambacho kinatumika juu ya Yusufu 43:31, ambapo aliweza kutawala hisia zake. Hapa aliomboleza kwa nguvu sana (kama vile mstari wa 2) kiasi kwamba kila mmoja alimsikia akiomboleza kwa sauti ya juu!

◙**"Mwondoeni kila mtu mbele yangu"** Amri (BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI), yawezekana alizungumza kimisri, ilielekezwa kwa wafanyakazi wote wa Yusufu (hata mawakili wake maalumu). Anabakiwa na ndugu zake tu kumi na moja.

◙**"Yusufu alipojitambulisha kwa nduguze"** Huu ni wakati wa namna gani waliokuwa nao! Yusufu alikuwa mwenye hisia na wao walikuwa wenye hisia (kama vile mstari wa 3).

**45:2 "Akapaza sauti yake akalia, nao Wamisri wakasikia. Watu wa nyumba ya Farao nao wakasikia"** Yusufu alikuwa amewatuma watumwa wake wote waende nje ya chumba. Hii ilikuwa aidha (1) ili wasiweze kuwabugudhi ndugu zake au (2) ili asiweze kuonesha hisia hizo kubwa katika jambo hili lililomuhusu mwenyewe mbele ya wamisri. Hatahivyo tendo la kimashariki hili la kuomboleza kwa sauti kuu ilisikika na watumishi wake waliokuwa karibu sana kuitikia ikiwa Yusufu angewaita. Inavyoonekana, Yusufu alikuwa mtu anayependwa sana katika misri na watumishi wake walikuwa kwa hali zao wote wakimjali au walijali ju ya utaalamu wake na utawala wake wa kiserikali kupotea, walitoa taarifa kwa farao kwa kile walichokuwa wanasikia.

**45:3 "Mimi ndimi Yusufu"** Huu ni mshangao usiokuwa na KITENZI. Ni wazo alilolizungumza kwa lugha ya Kiebrania lakini kwasababu inaonekana wazi kudhani kwamba ndugu zake hawakuzungumza kimisri na kwamba kwa wakati huo kulikuwa hakuna wakalimani, labda Yusufu aliwashangaza kwa kuzungumza nao katika lugha yao ya asili na kutengeneza kauli ya namna hiyo (kama vile mstari wa 4).

◙**"baba yangu angali hai bado?"** Baadhi ya Wafasiri wanatia shaka uhakika wa mstari huu kwasababu katika 43:27 Yusufu aliuliza swali hilohilo. Hatahivyo, inaonekana kwamba neno (BDB 311, kama vile I Sam. 25:6) inaweza kumaanisha zaidi ya maisha ya kimwili. Inavyoonekana alikuwa anamuuliza juu ya hali ya kiafya ya baba yake, ambayo tunajifunza kutoka katika mistari ya baadaye haikuwa katika hali ile ile tokea kifo cha Yusufu (kama vile mstari wa 27).

◙**" waliingiwa na hofu"** Hiki ni KITENZI chenye nguvu (BDB 96, KB 111, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Waamuzi 20:41; I Sam. 28:21; II Sam. 4:1; Ayubu 21:6; 23:15; Zab. 6:3; 30:8; 48:6; 83:17; 90:7; 104:29; Isa. 13:8; 21:3; Ezek. 7:27).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:4-15**
**[4] Yusufu akawaambia ndugu zake, Karibuni kwangu; basi, wakakaribia. Akasema, Mimi ni Yusufu, ndugu yenu, ambaye mliniuza kwenda Misri. [5] Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu. [6] Maana miaka hii miwili njaa imekuwa katika nchi, na iko tena miaka mitano isiyo na kulima wala kuvuna. [7] Mungu alinipeleka mbele yenu kuwahifadhia masazo katika nchi, na kuwaokoa ninyi kwa wokovu mkuu. [8] Basi si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu; naye ameniweka kama baba kwa Farao, na bwana katika nyumba yake yote, na mtawala katika nchi yote ya Misri. [9] Fanyeni haraka, mmwendee baba yangu, mkamwambie, Hivi ndivyo asemavyo mwanao**

**Yusufu, Mungu ameniweka kuwa bwana katika Misri yote, basi unishukie, usikawie. [10] Nawe utakaa katika nchi ya Gosheni, utakuwa karibu nami, wewe, na wanao, na wana wa wanao, na wanyama wako, ng'ombe zako, na yote uliyo nayo. Nami nitakulisha huko; [11] maana bado imesalia miaka mitano ya njaa; usije ukaingia katika uhitaji, wewe, na nyumba yako, na yote uliyo nayo. [12] Na tazama, macho yenu yanaona, na macho ya ndugu yangu Benyamini, ya kwamba ni kinywa changu mimi kinachosema nanyi. [13] Nanyi mtamwarifu baba yangu habari za fahari yangu yote katika Misri, na za vyote mlivyoviona; mkafanye haraka kumleta huku baba yangu. [14] Akaanguka shingoni mwa ndugu yake Benyamini, akalia; Benyamini naye akalia shingoni mwake. [15] Akawabusu ndugu zake wote, akalia nao, baada ya hayo, nduguze wakazungumza naye**

**45:5"Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku"** Neno "alihuzunishwa" (BDB 780, KB 864, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU umetumika katika HALI YA KUSIHI) katika *Niphal* mzizi umetumika katika I Sam. 20:3,34; II Sam. 19:2 na Neh. 8:10,11. Maana ya msingi ni "kuumiza," "maumivu," au "kuhuzunika."

Neno "hasira" ni neno "kuchoma" (BDB 354, KB 351, *Qal* HALI YA KUSIHI, kama vile Mwanzo 31:36; 39:19; Kutoka. 32:11).

Yusufu anakaribia kusema kauli ya imani ya kushangaza kupita kawaida isiyopatikana popote katika Biblia. Mstari huu ni kusudio la kithiolojia la masimulizi ya Yusufu (*Elohim*) kwa imani. Mistari ya 5-9 inatengeneza moja ya ukiri zenye nguvu zaidi za wema na uwepo wa Mungu katikati ya harakati na matatizo ya maisha.

Nyongeza tu ya maoni katika andiko hili zuri sana na lenye nguvu. Swali langu siku zote limekuwa, "Je Mungu huwa anatenda hivi siku zote tu kuwaelekea familia yake ya kiagano?" Ni dhahiri kwamba Mungu htenda chochote akitakacho anachokiona cha muhimu kusaidia familia ya Ibrahimu (kama vile Warumi 9-11), lakini vipi kuhusu waaminio wa kawaida? Je upendo wake ni wa milele (yaani ukombozi) au kwa muda na milele? Je yupo nasi kwa namna hiyo hiyo? Huu ulimwengu ni muovu, sehemu ya uasi (angalia *The Goodness of God* cha Wenham). Waaminio huteseka; waaminio huteswa; waaminio huuliwa! Kutoka katika Agano Jipya inaonekana kweli kwamba Mungu yuko pamoja nasi na hata katikati ya nyakati ngumu zisizoelezeka (angalia *The Christian's Secrets of a Happy Life*, cha Hannah Whithall Smith). Ni dhanio la kiimani na ufunuo wa kimaandiko kwamba waaminio ni wa thamani kwa Mungu! Maisha ni fumbo, lakini yasiyoonekana (yale yasiyojulikana bado) mkono wa Mungu upo pamoja nasi wakati wote. Amani yetu lazima ikae ndani yake, Neno lake, Mwanawe, sio kuweka mawazo yetu katika nyakati ngumu (kama vile I Kor. 10:13; 13:8-13). Tu familia ya Ibrahimu (kama vile Warumi 2:28-29)!

**45:6 "Maana miaka hii miwili njaa imekuwa katika nchi, na iko tena miaka mitano isiyo na kulima wala kuvuna."** Hii inaturejesha nyuma kwa ufunuo kupitia ndoto ya Farao kwamba kungekuwa na miaka saba ya njaa.

**45:7** Kauli za Yusufu katika mstari wa 7, ikimaanisha mabaki (BDB 984) ikilindwa, kuhusiana na shughuli zake, na sio matumizi ya baadaye ya kithiolojia ya neno "mabaki" ambayo linamaanisha kwa wjamii ya watu waaminifu waaminio wa Kiebrania

## MADA MAALUM: MABAKI (BDB 984, KB 1375), NAMNA TATU

Dhana ya Agano la Kale ya kifungu cha "mabaki ya uaminifu" ni kigezo cha sasa cha Manabii (hasa manabii wa karne ya nane na Yeremia). Neno hili linatumika katika maana tatu:

1. wale waliomudu kuishi ndani ya uhamisho (yaani Ezra 9:8,14-15; Neh. 1:2-3; Isa. 10:20-23; 17:4-6; 37:4,31-32; 46:3; Jer. 23:3; 31:7-8; 42:15,19; 44:12,14,28; Mika 2:12; 5:7-8; 7:18; Hag. 1:12-14; 2:2; Zak. 8:6,11-12)
2. wale waliobaki kuwa waaminifu kwa YHWH (mfano Isa. 4:1-5; 11:11,16; 28:5; Yoeli 2:32; Amosi 5:14-15)
3. wale walio sehemu ya matengenezo mapya ya siku za mwisho na uumbaji mpya (mfano Amosi 9:11-15; Zek. 8:6)

Ule mfano wa udongo katika Marko 4:1-20 na Mt. 13:1-23, ambao unanukuu Isa. 6:9-10, ni mfano mzuri wa namna Agano Jipya linavyolielewa neno hili (pia nukuu Rum. 9:6 katika kuirejelea Israeli ya siku za Paulo).

Haya "mabaki" ya Agano Jipya yameundwa na Wayahudi waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:27-29) na Mataifa waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:24-26). Makundi yote yanazungumziwa katika Rum. 9:30-35; 11:11-24,25-32. Kuamini juu ya Israeli si suala la rangi (yaani, Rum. 9:6; 2:18-19), bali kuliamini kundi la wafuasi waaminifu wa mambo mapya wa Mungu, ufunuo kamili katika Yesu. Kulizungumza hili kunaonekana kuwa ni kuyakataa maandiko ya Agano la Kale (yaani, Yer. 31:7-9; Mika 5:7-8) kuhusu taifa la Israeli kuwa mabaki. Tafadhari tazama katika Mada Maalumu yangu: Kwa nini Ahadi za Agano la Agano la Kale Zinaonekana kuwa Tofauti Sana na Ahadi za Agano Jipya? Injili hubadilisha kila kitu!

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | |
| **NJB** | **"kwa wokovu mkuu"** |
| **NRSV** | **"waliookoka wengi"** |
| **TEV** | **"wazao waliookoka"** |
| **LXX** | **"mabaki makuu (vizazi vijavyo)"** |
| **JPSOA** | **"wokovu usiokuwa wa kawaida"** |

Hii kifasihi ni "kutoroka" (BDB 812, kama vile Yer. 25:35) na KIVUMISHI "kuu" (BDB 152). Msaada wa Yusufu kwa familia yake kwa kuinuliwa katika uongozi wa Misri unaelezewa kama ukombozi mkuu ukiendeshwa na YHWH (kama vile mistari ya 5,8; 50:20).

**45:8 "naye ameniweka"** Tatizo la kithiolojia linalohusiana na mafundisho ya kuamriwa kabla si kwamba Mungu anajua na athari za matendo ya mwanadamu (lakini pia na vile vile matukio ya kimwili), lakini ni kwa kiasi gani anawajibika (kukoswa uaminifu) kwasababu ya dhambi za wanadamu? Wanathiolojia (Strong, *Systematic Theology*, Toleo la pili. Ukurasa wa 423-425; Erickson, *Christian Theology*, toleo la pili lililohaririwa. Ukurasa wa 424-426) mejitolea nadharia kadhaa ambazo zinaonesha uhusikaji wa Mungu, lakini sio kuingizwa kwa matendo ya dhambi (kama vile Yakobo 1:14; I Yohana 2:16).

1. anaweza kuzuia kitendo (kama vile Mwanzo. 20:16)
2. anaweza kuruhusu kitendo (kama vile Zab. 81:12-13; Rum. 1:24,26,28)
3. anaweza kuongoza kitendo (kama vile Mwanzo 37:21-22; 45:5,7,8; 50:20)
4. anaweza kuweka mpaka wa kitendo (kama vile I Kor. 10:13)

## MADA MAALUMU: KUAMRIWA KABLA (CALVINISM) DHIDI YA UTASHI HURU WA KIBINADAMU (ARMINIANISM)

Tito 2:11 ni mlinganyo wa vifungu vingine vya Agano Jipya kwenye uchaguzi. Nilifikiri inaweza kuwa ya msaada wa kithiolojia kusaidia kutoa maelezo yangu ya kiufafanuzi kutoka Warumi 8:29 na sura ya 9, pamoja na Waefeso 1.

I. Warumi 8:29 – Paulo anatumia "naliwajua kabla" (*proginōskō*, "kujua kabla") mara mbili, hapa na 11:2. Katika 11:2 inamaanisha upendo wa Agano la Mungu kwa Israeli kabla ya wakati kuanza. Kumbuka kwamba neno "kujua" kwa kiebrania linahusiana na uhusiano binafsi,wa ndani, sio kumwambia ukweli kuhusu mtu fulanii (kama vile Mwanzo 4:1; Yer. 1:5). Hapa ilikuwa imejumuisha katika mlolongo wa matukio ya milele (kama vile Warumi 8:29-30). Neno hili lilihusishwa na kuamuliwa kabla. Hata hivyo, ni lazima ieleweke kwamba maarifa ya Mungu ya mambo yajayo sio msingi wa uchaguzi kwa sababu ikiwa ni hivyo, basi uchaguzi utakua umeegemea katika mwitikio wa baadaye wa binadamu uliyeanguka, ambao utakua utendaji wa kibinadamu. Neno hili pia linapatikana katika Mdo. 26:5; 1 Pet 1:2, 20 na 1 Pet 3:17.

A. "aliowajua tangu asili" (*proginōskō*, "kujua kabla")

Maneno "aliowajua tangu asili" na "aliwachagua tangu asili" yote ni maneno ambatani pamoja na kihusishi "kabla" na, kwa hiyo inapaswa kutafsiriwa, "kujua kabla ," "kuweka mipaka kabla," au "alama kabla ." Vifungu ya uhakika juu ya kuamuliwa kabla katika Agano Jipya ni Warumi 8:28-30; Waefeso 1:13-14; na Warumi 9. Maandiko haya ni dhahiri kusisitiza kwamba Mungu ni Mfalme. Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu vyote. Kuna mpango wa ki-Uungu uliowekwa tayari ili kufanywa kwa wakati. Hata hivyo, mpango huu sio wa kiholela wala kuchagua. Inategemea sio tu juu ya Ufalme wa Mungu na ujuzi wa asili, lakini kwa tabia yake isiyobadilika ya upendo, huruma, na neema isiyostahili. Tazama Mada Maalumu: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele.

Tunapaswa kuwa makini na ubinafsi wetu wa magharibi (Amerika) au moyo wetu wa uinjilisti wa kuulemba ukweli huu wa ajabu. Tunapaswa pia kulindwa dhidi ya kukingamizwa ndani ya historia, kithiolojia kati ya Augustine dhidi ya Pelegius au Calvinism dhidi ya Arminianism.

B. "imeamriwa kabla" (*proorizō*, "kuweka mipaka kabla")

Kuamriwa kabla sio mafundisho yenye maana ya kupunguza upendo wa Mungu, neema, na huruma wala kuwatenga wengine kutoka kwenye injili. Ilikuwa na maana ya kuimarisha wanaoamini kwa kuunda maoni yao ya ulimwengu. Mungu ni kwa ajili ya binadamu wote (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Tim 1. 2:4; Pet 2. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14). Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu vyote. Nani au nini kinachoweza kututenganisha na yeye (kama vile Warumi 8:31-39)? Mungu anaona historia yote mambo yaliyopita kama yapo sasa; binadamu ni kiumbealiyefungwa na muda. Mtazamo wetu na uwezo wa akili ni wenye mipaka/kikomo. Hakuna kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na utashi huru wa mwanadamu, ni muundo wa Agano. Huu ni mfano mwingine uliotolewa katika mvutano wa lahaja. Mafundisho ya kibiblia yanatolewa kwa mtazamo tofauti. Mara nyingi huonekana fumbo la maneno. Ukweli ni mlinganyo kati ya jozi zilizo kinyume. Hatupaswi kuondoa mvutano kwa kuchukua moja ya ukweli. Hatupaswi kutenganisha ukweli wowote wa Kibiblia ndani ya chumba.
Ni muhimu kuongeza kwamba lengo la uchaguzi sio mbinguni tu wakati tunapokufa, lakini mapenzi ya Kristo sasa. (kama vile Rum. 8:29-30; Kor. 2. 3:18; Wagalatia 4:19; Waefeso 1:4; 2:10; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 Wathesalonike 2:13; Tito 2:14; Pet 1. 1:15). Tumechaguliwa kuwa "watakatifu wasio na lawama" Mungu huchagua kutubadili ili wengine waweze kuona badiliko na kuitikia kwa imani kwa Mungu katika Kristo. Majaaliwa sio pendeleo la kibinafsi, bali ni wajibu wa Agano. Huu ni ukweli mkuu wa kifungu hiki. Hili ni lengo la Ukristo. Utakatifu ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini. Uchaguzi wa Mungu ni mapenzi ya Kristo (kama vile Waefeso 1:4), sio msimamo maalumu. Mfano wa Mungu ulotolewa kwa binadamu katika uumbaji (kama vile Mwanzo 1:26; 5:1,3; 9:6), ni kurejeshwa.

C. "kubali kugeuzwa kwa mfano wa mwanawe"— Lengo kuu la Mungu ni kurejesha picha iliyopotea kwenye anguko. Waamini wamewekwa mbele kwa mapenzi ya Kristo kama vile Waefeso 1:4).

II. Warumi 9

A. Warumi 9 ni mojawapo ya kifungu cha Agano Jipya juu ya Ufalme wa Mungu (mwingine kuwa Waefeso 1:3-14), wakati sura ya 10 inasema kuwa uhuru wa binadamu ni dhahiri na hujirudia mara kwa mara (kama vile. "kila mtu" Warumi 9:4; "kila mtu" 9:11, 13; "wote" 9:12 [maradufu]). Paulo kamwe hakujaribu kupatanisha mvutano huu wa kitheolojia. Wote ni wa ukweli! Mafundisho mengi ya Biblia yanawasilishwa kwa fumbo la maneno au jozi za lahaja. Mifumo mingi ya theolojia ni yenye mantiki na nusu ya ukweli. Augustinianism na Calvinism dhidi ya nusu-Pelegianism na Arminianism zina misingi ya ukweli na yenye makosa. Mvutano wa kibiblia kati ya mafundisho ni bora kwa maandishi ya ushahidi, yenye kutangazwa kama imani ya kanisa, ya kimantiki, ya mfumo wa kithiolojia ambayo inasisitiza Biblia kwenye mstari wa ramani iliyoelezea kabla.

B. Ukweli huo huo (unapatikana katika Warumi 9:23) umeelezwa katika Warumi 8:29-30 na Waefeso 1:4, 11. Sura hii ni maelezo yenye nguvu zaidi ya uweza wa Mungu katika Agano Jipya. Haiwezi kuwapo na migogoro kwa vile Mungu ndiye muhusika wa jumla wa uumbaji na Ukommbozi. Ukweli huu mkubwa haupaswi kamwe kufutwa au kupunguzwa. Hata hiyo, ni lazima pawepo na mlinganyo na uchaguzi wa Mungu wa agano kama njia ya kuhusianisha na uumbaji wa mwanadamu, uliofanywa kwa mfano wake. Kama vile Mwanzo 15 isiyokuwa na masharti na haihusiani kabisa na majibu ya mwanadamu, lakini maagano mengine yenye masharti juu ya majibu ya binadamu (mfano Edeni, Nuhu, Musa, Daudi). Mungu ana mpango wa ukombozi kwa uumbaji wake;hakuna mwanadamu anayeweza kuathiri mpango huu. Mungu amechagua kuruhusu watu binafsi kushiriki katika mpango wake. Nafasi hii ya ushiriki ni mvutano wa kithiolojia kati ya Ufalme (Warumi 9) na mapenzi ya Kibinadamu (Warumi 10).

Sio sahii kuchagua msisitizo mmoja wa Biblia na kupuuza mwingine. Kuna mvutano kati ya mafundisho kwa sababu watu wa mashariki wanawasilisha kweli katika lahaja na jozi kujaza mvutano. Mafundisho lazima yafanyike katika mahusiano na mafundisho mengine. Ukweli ni kweli za Musa.

III. Waefeso 1

A. Uchaguzi ni mafundisho ya ajabu. Hata hivyo si wito kwa upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa ajili ya huduma; katika agano jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia haipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa Kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguzi wa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile 10:11,13).

Umuhimu wa mvutano huu wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni “ndiyo” ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo).Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja huja kutokana na kweli zingine, sio kama moja, lisilohusiana na ukweli. Mfuatano mzuri ungalikuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika namna ya kimashariki na sio kimagharibi. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja (fumbo la maneno) za kweli za mafundisho (Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu aliye dhahili: usalama dhidi ya uvumilivu;Yesu aliye sawa na Mungu baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu; Uhuru wa kikristo dhidi ya wajibu wa kikristo kwa mwenzi wa agano, nakadhalika).

Dhana ya kithiolojia ya “agano” inaunganisha Uweza wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa kuweka mswada) wenye mwanzo muhimu na mwendelezo wa mwitikio wa imani ya toba kutoka kwa mtu. Kuwa mwangalifu na uhakiki wa maandiko wa upande mmoja na kupuuza mwingine! Kuwa mwangalifu wa kuthibitisha mafundisho yako pendwa au mfumo wa thiolojia.

B. "alivyotuchagua" katika Waefeso 1:4 ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inasisitiza somo. Hii inalenga katika uchaguzi wa Mungu kabla ya wakati. Chaguo la Mungu halipaswi kueleweka kwa maana ya kiislamu ya falsafa za maamuzi.Mungu aliahidi kuwakomboa wanadamu walioanguka (kama vile Mwanzo 3:15). Mungu alimwita na kumchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5-6).

Mungu mwenyewe alichagua wanadamu wote ambao wangetenda imani katika kristo. Mungu daima huchukua maamuzi mwenyewe katika wokovu (kama vile Yohana 6:44,65). Nakala hii na Warumi 9 ni msingi wa Kibiblia kwa mafundisho ya majaaliwa yaliyosisitizwa na Augustine na Calvin. Mungu alichagua wanaoamini si tu kwa wokovu (kuhesabiwa haki), lakini pia kwa utakaso (kama vile Wakolosai 1: 10-12).

Hii inaweza kuhusiana na (1) nafasi yetu katika Kristo (kama vile Wakorintho 2. 5:21) au (2) Nia ya Mungu kuzalisha tabia yake katika wana wake (kama vile. Waefeso 2:10; Warumi 8:28-29; Wagalatia 4:19). Mapenzi ya Mungu kwa wana wake ni kuwaona wote mbinguni siku moja na kufanana na Kristo sasa!

"katika yeye" ni dhana muhimu ya Waefeso 1:4. Baraka za Mungu, neema, na wokovu hupitia kwa njia ya kristo (kama vile Yohana 14:6). Angalia kurudia rudia kwa umbo hili la kisarufi (ENEO LA MAHALI) katika Waefeso 1:3, "katika kristo" 1:4, "katika yeye"; 1:7, "katika yeye"; 1:9, "katika yeye"; 1:10, "katika kristo," "katika yeye"; 1:12, "katika kristo" na 1:13, "katika yeye" (maradufu).Yesu ndiye mwanadamu aliyechaguliwa na wote wanawezekana kuchaguliwa ndani yake. Wote wa Mungu Baraka za Baba zinapatikana katika Kristo.

Maneno "kabla ya msingi wa Dunia" pia hutumiwa katika Mt. 25:34; Yohana 17:24; Pet. 1. 1:19-20 na Ufunuo 13:8. Inaonyesha nafsi tatu kwa moja ya shughuli ya ukombozi wa Mungu hata kabla ya Mwanzo 1:1. Binadamu anakikomo kwa maana za wakati; kila kitu kwetu ni cha muda uliopita, wa sasa,na wa baadaye, lakini si kwa Mungu.

Lengo la kuamua kabla ni utakatifu sio pendeleo. Wito wa Mungu sio wa wachache waliochaguliwa wa wana wa adamu, bali kwa wote! Wito ulikuwa ni kile Mungu alichotaka mwanadamu kuwa kama yeye mwenyewe (kama vile. 1Wathesalonike 5:23; 2 Wathesalonike 2:13);katika sura yake (kama vile. Mwanzo 1:26-27). Ili kugeuza majaaliwa kuwa katika kanuni ya theolojia badala ya maisha takatifu kuwa janga. Mara nyingi theolojia yetu huzungumza kwa sauti zaidi kuliko maandiko ya Kibiblia.

Neno "wasio na lawama" (*amōmos*) au "bila lawama" linatumika

1. Yesu (kama vile Waebrania 9:14; 1 Pet 1:19)
2. Zekaria and Elisabeti (kama vile Luka 1:6)
3. Paulo (kama vile Wafilipi 3:6)
4. wakristo wote wa kweli (kama vile Wafilipi 2:15; 1 Wathesalonike 3:13; 5:23)

Mapenzi ya Mungu yasiyowezekana kubadilika kwa kila Mkristo sio baadaye mbinguni tu, lakini ni mapenzi ya kristo sasa (kama vile Warumi 8:29-30; Wagalatia 4:19; Pet 1. 1:2). Wanaoamini wanapaswa kuitazamisha tabia ya Mungu kwa ulimwengu uliopotea kwa dhumuni la Uinjilisti.

Kisarufi maneno "katika upendo" katika Tito 2:2 yanaweza kwenda pamoja na Tito 2:4 au 5. Hata hivyo wakati maneno haya yanatumika katika maeneo mengine katika Waefeso daima yanahusu upendo wa Kibinadamu kwa Mungu (kama vile Waefeso 3:17; 4:2,15,16).

C. Katika Waefeso 1:5 neno "alitangulia kutuchagua" ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Neno hili la Kiyunani ni neno ambatani kwa "kabla" na "alama kabla" Inahusu mpango wa ukombozi wa Mungu uliotanguliwa kabla (kama vile Luka 22:22; Mdo 2:23; 4:28; 17:31; Warumi 8:29-30). Majaaliwa ni moja ya ukweli kadhaa kuhusiana na wokovu wa mwanadamu. Ni sehemu ya kikolezo cha kitheolojia au mfululizo wa ukweli unaohusiana. Haikuwa na maana ya kusisitizwa katika kutengwa! Kweli ya Kibiblia imetolewa katika mfululizo wa mvutano wa anguko, jozi za fumbo la maneno. Ufuasi wa kimadhehebu umejaribu kuondoa mvutano wa kiibiblia kwa kusistiza kweli moja tu ya ukweli wa lahaja (majaaliwa dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu ; usalama wa mwamini dhidi ya uvumilivu wa watakatifu; dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari; kutokuwa na dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo; utakaso wa mara moja dhidi ya utakaso wa kuendelea;imani dhidi ya kazi; Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo; Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu wa asili).

Uchaguzi wa Mungu haukutegemea ujuzi wa mbele wa utendaji wa mwandamu, lakini kwa tabia yake ya neema (kama vile Waefeso 1:7,9,11). Alitamani kwamba wote (hapana mmoja kama mwenye mafunuo) angeokolewa (kama vile Ezek. 18:21-23,32; Yohana 3:16-17; 1 Tim 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14). Neema ya Mungu (tabia ya Mungu) ni muhimu kithiolojia kwa kifungu hiki (kama ile Waefeso 1:6a, 7c, 9b), kama huruma ya Mungu ni muhimu kwa kifungu kingine juu ya kuamuliwa kabla kwa mambo, Warumi 9-11.

Tumaini pekee la wanadamu walioanguka ni neema na huruma ya Mungu (kama vile. Isaya. 53:6 na nyingine kadhaa za Agano la Kale zilizotajwa katika Warumi 3:9-18). Ni muhimu sana kwa kutafsiri sura hizi za kwanza za kithiolojia ili kutambua kwamba Paulo anasisitiza mambo hayo ambayo hayahusiani kabisa na utendaji wa mwanadamu: kuamuliwa kabla kwa mambo (Waefeso 1), neema (Waefeso 2), na mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu (Ajabu, Waefeso 2:11- 3:13). Hii ilikuwa ni kusawazisha mkazo wa walimu wa uongo juu ya sifa

| |
|---|
| ya binadamu na kiburi. |

◙**"naye ameniweka kama baba kwa Farao, na bwana katika nyumba yake yote, na mtawala katika nchi yote ya Misri"** Hii inaonekana kuwa maelezo ya pande tatu ya kazi ya Yusufu huko Misri.

1. Alikuwa na uhusiano wa kipekee pamoja na Farao. Hii imekuwa nyaraka ya cheo kilichoandikwa ki akiolojia mika mkama 3000 k.k. Inaonekana kumaanisha nafasi ya mshauri Mkuu wa ufalme.
2. "bwana wa nyumba yake yote" inaonekana kuwa rejea ya utawala na usimamizi wa mali binafsi za Farao (kama vile Mwanzo 41:40; 47:20-26).
3. "Mtawala wa ardhi yote ya Misri" inaonekana kuelezea uhuziano wake katika utawala wa kiserikali (kama vile Mwanzo 41:41, 48-49, 55-56; 42:6-7).

Roland deVaux, *Ancient Israel*, vol. 1, ukurasa wa 49, inaonesha jinsi neno "baba" lilikuja kutumiwa kama cheo kwa mmoja wa washauri wa Farao. Mababa walikuwa walimu wakuu wa watoto baada ya kuwa wamefikia umri wa miaka fulani ya kukomaa, kabla ya hili yalikuwa majukumu ya wamama. Katika ulimwengu wa roho, makuhani walichukua neno "baba" kujielezea wenyewe (Hekima ya walimu wa Kiebrania katika Mithali pia ilichukua cheo hiki kama ilivyofanywa na makuhani katika Waamuzi 17:10; 18:19).

**45:9** Yusufu anawaambia ndugu zake.

1. harakisha, BDB 554, KB 553, *Piel* KAULI SHURUTISHI, kama vile mstari wa 13
2. ondoka, BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. shukeni, BDB 432, KB 434, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. msichelewe, BDB 763, KB 840, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI

**45:10 "Nawe utakaa katika nchi ya Gosheni"** Haijulikani kutoka katika mistari ikiwa hii inamaanisha tangazo kwa niaba ya Yusufu (kama vile 46:31) au tu mantiki juu ya wachungaji walipoishi. Nchi ya Gosheni (BDB 177) ipo upande wa mashariki mwa sehemu ya juu mwa Nile, karibu na ardhi ya Kanaani. Baadaye inaitwa ardhi ya Rameses (kama vile Mwanzo. 47:6, 11). Ilikuwa ni sehemu inayozalisha mifugo ka wingi Misri (kama vile Mwanzo 46:32-34).

◙**"utakuwa karibu nami"** Mstari huu mara kwa mara unatumika kama ushahidi "Wafalme Wachungaji," au Hyksos, aliyeshinda Misri kwa namna ya upinde ambatani na farasi aliyefungiwa gari. Walitawala Misri kati ya mwaka 1720 mpaka 1580 k.k. Tunajua kwamba walikuwa wasemitiki kwa asili na hivyo ingekuwa rahisi kwa Wasemiti wengine kama Yusufu kupanda kicheo. Katika historia ya Kimisri, watu wasemiti walikuwa wanashikilia nafasi nzuri sana za muhimu katika serikali. Ulikuwa katika mji uitwao Tanis au Zoan (kama vile Zab. 78:12, 43). Hii ilikuwa ni karibu sana na Gosheni. Hatahivyo, Mafarao wazawa wa Kimisri waliofuatia waliweka mji mkuu wao maili 400 kusini mwa jiji la Thebes. Tarehe za utawala wa Yusufu Misri bado haijulikani na hii haiwezi kutumika kama ushahidi wa hitimisho.

**45:12 "Na tazama, macho yenu yanaona, na macho ya ndugu yangu Benyamini, ya kwamba ni kinywa changu mimi kinachosema nanyi"** Maana halisi ya kila tungo hizi kwa namna fulani hivi haijulikani (yawezekana hatumii mkalimani), lakini nia ya jumla ni rahisi kuitambua. Benyamini kipekee alihusiana na Yusufu kwasababu wote walikuwa wana wa Raheli. Kifungu cha maneno "kinywa changu" inaonekana kutumika kama nahau kwa mamlaka (kama vile mstari wa 21 na fasiri ya Rashi).

◙**"Benyamini"** Raheli kiasili alimuita "mwana wa huzuni" kwasababu alikuwfa wakati alipokuwa kuwa akijifungua (kama vile Mwanzo 35:18). Hatahivyo Yakobo alibadili jina lake "mwana wa mkono wangu wa kuume." Kwasababu upendo wa kipekee wa Yakobo kwa Raheli, wote wawili Yusufu na Benyamini walikuwa maalumu kwake.

**45:13 "fahari yangu yote"** Hili ni neno la kiebrania *kabod* (BDB 458). Maana yake ya kimsingi (BDB 458 II) ni "zito" (kama vile 41:31, NASB, "isiyonakshiwa"; Kutoka 4:10, "uzito wa ulimi").
Ilikuja kutumika juu ya kile kilichokuwa cha thamani. Tazama matumizi yafuatayo.

1. utajiri, Mwanzo 31:1; Isa. 10:3; 61:6
2. fahari/mafanikio, Mwanzo 45:13
3. uzuri, Isa. 35:2
4. njaa kali, Mwanzo 12:10; 41:13; 43:1; 47:4,13
5. heshima, Hes. 24:11
6. zaidi, Mwanzo. 50:10,11 (yaani kuugua kwa maombolezo)

## MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE)

I. Maana yake ya kimsingi

Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno "utukufu" (*doxa)* Tafsiri ya maandiko ya kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani vipimo). Likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.

II. Ilitumiwa na YHWH

A. Ikajakuwa ndo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa kumfunua YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza wa kifalme (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kihalisia.
B. Ilidokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31
C. Lilitumika katika udhihilisho wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni "utukufu wa Israeli", kama vile 1Sam. 15:29
   1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)
   2) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10
   3) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai
   4) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani
      a. Uasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili, cf. Hes. 14:9-10
      b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21
      c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19
      d. Mgogoro wa maji, kama vile Hes. 26:6
D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23
E. Lilitumika na YHWH mwenyewe (yaani umuhimu wake)
   1) 1Nya. 29:11
   2) Zab 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23
   3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufunuo 21:23; 22:5)
   4) Zek. 2:5,10
F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika
   1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23
   2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 811; 2 Nyakati 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9
   3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61
G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nyakati 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3
H. Lilitumika na YHWH katka hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa

A. Binadamu
   1. Likiendana na "nafsi" (yaani, *nephesh)* kama vile Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1
   2. Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12
   3. Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7
   4. Sifa njema, kama vile Ayubu 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17
   5. Uzuri, kama vile 1 Nyakati 29:12,28; 2 Nyakati 17:5; 18:13; 32:27
B. Mataifa
   1) Misri,

2) Ephrahim, kama vile Hos. 9:11
3) Samaria, kama vile Hos. 10:5

C. Wafalme
1) Ahausuero, kama vile Esta 1:4
2) Israeli, kama vile Zab 21:6
3) Antiochus IV, kama vile Dan. 11:39

D. Majeshi ya mataifa
1) shamu, kama vile Isa. 8:7
2) Israeli, kama vile Isa. 17:4
3) Kedari, kama vile Isa. 21:16

IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho
A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Ezek. 43:2,4,5; 44:4
B. YHWH atauvuta ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19
C. YHWH ataishusha Yerusalemu "mpya" kama vile Isa. 66:10; Zek. 12:7

V. Kusudi la uumbaji ni kumtukuza YHWH
A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake, kama vile Isa. 43:7
B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29
C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1
D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Petro 2:12
E. Maelezo ya kwanza ya Katekismu

**45:14 "Akaanguka shingoni mwa ndugu yake Benyamini, akalia; Benyamini naye akalia shingoni mwake"** Kutia chumvi kwa fasiri ya Kiyahudi, hata kwa Mfasiri mwenye msaada kama Rashi, anaweza kuonekana katika mstari huu. Wanasema kwamba Yusufu alilia kwa uchungu kwasababu ya uharibifu wa hekalu huko Shilo, ambalo lilikuwa katika gawio la baadaye la Yusufu (kama vile Yoshua). Benyamini alilia kwa uchungu kwasababu ya uharibifu wa hekalu kwasababu Yerusalemu ambayo ipo gawio la kikabila la Benyamini. Hii inaonesha hali ya ufafanuzi wa fasihi ya Kiyahudi katika kuondoa kabisa mazingira ya kihistoria ya mstari huu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:16-20**
**[16] Habari ikasikika nyumbani mwa Farao kusema, Ndugu zake Yusufu wamekuja. Ikawa vema machoni pa Farao, na machoni pa watumwa wake. [17] Farao akamwambia Yusufu, Uwaambie ndugu zako, Fanyeni hivi; wachukuzeni mizigo wanyama wenu, mwondoke mwende nchi ya Kanaani; [18] kisha mkamtwae baba yenu, na watu wa nyumbani mwenu, mkanijie; nami nitawapa mema ya nchi ya Misri, nanyi mtakula unono wa nchi. [19] Nawe umeamriwa; fanyeni hivi, mjitwalie magari katika nchi ya Misri kwa watoto wenu wadogo na wake zenu, mkamchukue baba yenu mje. [20] Wala msivisumbukie vyombo vyenu, maana mema ya nchi yote ya Misri ni yenu.**

**45:16** Ndugu wamepona kutoka (1) mshituko wa ufunuo wa Yusufu kuhusu yeye mwenyewe; (2) hofu ya Mungu kwa kile walichofanya kwa Yusufu; na (3) hofu ya Yusufu mwenyewe.

**45:17-20** Huu ni ujumbe wa Farao kwa Yusufu kwa ajili ya familia yake.

1. waaambie ndugu zako, mstari wa 17, BDB 55, KB 65, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. fanya hivi, mstari wa 17, BDB 793 I, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. waachieni mifugo yenu, mstari wa 17, BDB 381, KB 378, *Qal* KAULI SHURUTISHI (KITENZI hiki kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale)
4. nenda katika nchi ya Kanaani, mstari wa 17, BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. njoo (sio katika NASB), mstari wa 17, BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI SHURUTISHI
6. wachukue baba yako na nyumba yako yote, mstari wa 18, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
7. njoni kwangu, mstari wa 18, BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI SHURUTISHI
8. nitakupatia sehemu nono ya ardhi ya Misri, mstari wa 18, BDB 678, KB 733, *Qal* HALI YA KUSIHI

9. mtakula manono ya nchi, mstari wa 18, BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI SHURUTISHI
10. fanya hivi, mstari wa 19, BDB 793 I, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
11. chukua usafiri, mstari wa 19, KITENZI kilekile sawa na #6
12. mleteni baba yenu (kifasihi. kumchukua), mstari wa 19, BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU ikitumika katika namna ya KAULI SHURUTISHI
13. njoo, mstari wa 19, KITENZI vile vile sawa na #5 na #7, lakini *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU ikitumika katika namna ya KAULI SHURUTISHI
14. msijihangaishe wenyewe juu ya mali (kifasihi "angalieni macho yenu yasije yakajuta juu ya vifaa vyenu," mstari wa 20, BDB 299, KB 298, *Qal* HALI YA KUSIHI; nahau ile ile inayotumika katika Kumb. 7:16; 13:8; 19:13,31; 25:12

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:21-23**
**[21] Ndivyo walivyofanya wana wa Israeli. Yusufu akawapa magari kama Farao alivyoamuru, akawapa na chakula cha njiani. [22] Akawapa kila mtu nguo za kubadili; lakini Benyamini, alimpa fedha mia tatu na mavazi matano ya kubadili. [23] Na babaye akampelekea kama hivi, punda kumi waliochukua mema ya Misri, na punda wake kumi waliochukua nafaka, na mikate, na chakula kwa babaye njiani.**

**45:21 "magari"** Hili ni neno la kukopwa la kimisri lenye maana ya "mkokoteni wenye matairi mawili yanayovutwa na wanyama" (BDB 722, kama vile I Sam. 6:7) na wala haimaanisha magari ya farasi ya kivita (BDB 939, kama vile 41:43) ya Misri. Mikokoteni hii ilizoeleka Misri kwasababu ya utambarare wake. Zilikuwa nadra au yawezekana hata zisijulikane katika nchi ya Palestina kwasababu ya mikwaruzo ya miinuko na milima. Sababu moja ya Wafilisti kuwa na uwezo wa kuendesha na kushughulikia maeneo ya pwani ilikuwa ni kwasababu ya matumizi yao ya magari ya chuma. Hatahivyo ushindi wa mapema wa Israeli ulitokea katika nchi ya milima ambapo magari ya farasi yalikuwa hayatumiki. Mikokoteni hii lazima ilikuwa si kawaida kuonekana katika nchi ya Kanaani.

**45:22 "nguo za kubadili"** Hii yawezekana inamaanisha mavazi yenye mapambo (yaani Kutoka 3:22; 12:35), ambayo yalikuwa moja ya vyanzo vya utajiri na mali katika ulimwengu wa kale. Yamkini ilikuwa kuwavisha vizuri ndugu zake katika mazingira ya kidesturi (tabaka la wasomi na wenye heshima wa kimisri, kama vile 41:14). Hatahivyo inaweza kuashiria nguo mpya, sio zile ambazo ni za gharama (yaani Ruthi 3:3).

◙**"lakini Benyamini, alimpa fedha mia tatu na mavazi matano ya kubadili"** Yusufu katika watu wote, lazima alifahamu tatizo linalotokana na ubaguzi na upendeleo, na bado mazingira ya kitamaduni ni kwamba alijipa furaha katika ndugu yake wa damu (kama vile 43:34).

**45:23** Kumbuka namna gani Yakobo alikuwa ametuma zawadi "mtu" wa Misri katika 43:11, hivyo Yusufu sasa anarudisha mategemeo ya kitamaduni.
1. punda kumi waliosheheni vitu bora (BDB 375 TUNGO BDB 595)
2. punda kumi walio sheheni nafaka na mikate

Aisee! Nawaza Yakobo alivyokuwa akifikiria kichwani mwake alpowaona na kuona vitu hivi vikija njiani!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:24-28**
**[24] Akaagana na ndugu zake, wakaenda zao; naye akawaambia, Msigombane njiani. [25] Wakatoka Misri, wakafika nchi ya Kanaani kwa Yakobo, baba yao. [26] Wakampasha habari, wakisema, Yusufu angali hai; naye ndiye mtawala katika nchi yote ya Misri. Moyo wake ukazimia, kwa sababu hakuwasadiki. [27] Wakamwambia maneno yote ya Yusufu, aliyowaambia; na alipoona magari aliyoyapeleka Yusufu, ili kumchukua, roho ya Yakobo baba yao ikafufuka. [28] Israeli akasema, Yatosha! Yusufu mwanangu angali hai; nitakwenda, nionane naye kabla sijafa.**

**45:24 "akawaambia, Msigombane njiani"** KITENZI (BDB 919, KB 1182, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU kikitumika katika HALI YA KUSIHI, kikitumika hapa tu katika Mwanzo na mara mbili tu zaidi katika Torati) inaweza ikafasiriwa ikihusiana na

1. kuchambua shutuma kwa ajili ya matendo yake kumuelekea Yusufu katika Mwanzo 37 (Rashi)
2. hofu (kama vile Kutoka 15:14; Kumb. 2:25) ya kurudi kwa familia nzima na Yusufu kulipa kisasi
3. mawazo yanayoendelea juu ya Benyamini kupata chakula zaidi (43:34) na sasa nguo zaidi na vipande vya shaba (45:22)

Alikuwa anawakumbusha kwa njia ya upole kuwa Mungu mwenyewe alikuwa anaongoza mazingira, si kwamba matendo yao yalikuwa ya kidhambi (kama vile 42:21,28; 44:16), lakini kwamba Mungu alikuwa na kusudi kubwa zaidi (kama vile mistari ya 5,7,8; 50:20; Mdo. 7:9). Mungu anatumia hata uovu kwa ajili ya makusudi yake (kama vile Mdo. 2:23).

**45:26 "moyo wake ukazimia"** Neno hili kiasili lilimaanisha "kutoweza kuongea kwasababu ya baridi" (BDB 806, KB 916, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, kama vile Zab. 77:2; Hab. 1:4). Ni dhahiri kwamba ndugu hawa walikuwa wamekiri kwa baba yao kile ambacho walikuwa wamekitenda miaka ya nyuma japokuwa hii haitajwi kibayana katika maandiko. Inafurahisha kuona kwamba ndoto za Yusufu hatimaye ziligeuka kuwa kweli. YHWH anajua na anashughulikia historia! Ndoto zilizotabiriwa na unabii ni ushahidi wenye nguvu ya upekee wa Biblia na tabia ya Mungu.

◙ **"kwa sababu hakuwasadiki"** KITENZI (BDB 52, KB 63) ni *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU Yakobo naye pia hakuwa ameamini juu ya kifo cha Yusufu (kama vile 37:31-35). Wana wa Yakobo walimdanganya kuhusu kifo cha Yusufu! Angalia Mada Maalum katika 15:6.

**45:27 "roho ya Yakobo baba yao ikafufuka"** Hii inaonekana kumaanisha kwamba tokea kifo cha Yusufu, Yakobo alikuwa mwenye hofu na aliyedhoofu, hakuwa yule mtu aliyekuwa mwanzo. Wakati mwingine kifo cha mtoto anayependwa sana kinaweza kumfedhehesha mzazi mapaka kiwango cha kutopata hata nafuu.

**45:28** Inafurahisha kwamba katika mstari wa 27 "Yakobo," ambaye anazungumzia juu ya maisha yake ya uzeeni, wakati mstari wa 28 anaita kwa jina la "Israeli." Hii yawezekana ni kwasababu ya (1) kufanywa upya kwa mtazamo wake wa imani kumuelekea Mungu na agano lililohaidiwa la Mungu ambalo linaunganishwa na Yusufu au (2) kwasababu Yakobo anakaribia kufanya maamuzi ambayo yataathiri watu wote wa agano.

Jina "Israeli" limekuwa gumu kulifasiri. Baadhi ya nadharia zilizojikita kwenye Mwanzo 32:28-29 ni:

1. "mwache *El* ag'ag'anie"
2. "*El* aweza kutunza"
3. "kutawala na *El*"
4. "mwana wa kifalme wa Mungu"

Angalia Mada Maalum katika 32:28. Sifikirii kwamba majina tofauti kumaanisha vyanzo tofauti tofauti (yaani J.E.D.P.)! Haijalishi chanzo chochote kilicho sahihi, jina hili lilikuja kuwa cheo maalumu kwa watu wa Mungu. Baada ya 922 k.k inamaanisha tu makabila ya kaskazini kumi. Baada ya kutoka uhamishoni katika mwaka wa 538 k.k. Linaanza tena kuwa cheo cha watu wote wa Mungu.

Yakobo anaitikia katika njia nne

1. Inatosha, hakuna KITENZI (BDB 912 I)
2. mwanangu Yusufu bado yuko hai, hakuna KITENZI
3. Nitakwenda, BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA KUSIHI
4. na kumuona, BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU inatumika katika namna ya kusihi

# MWANZO 46

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakobo anaenda Misri | Safari ya Yakobo Misri | Yakobo anahamia Misri | Yakobo na Familia yake wanaenda Misri | Yakobo anakwenda Misri |
| 46:1-4 | 46:1-7 | 46:1-4 | 46:1-2a | 46:1-5 |
| 46:5-7 | | 46:5-7 | 46b-46:3-4 | |
| | | | | 46:6-7 |
| Walio kwenda Misri | | | | Familia ya Yakobo |
| 46:8-27 | 46:8-15 | 46:8-27 | 46:8-15 | 46:8a |
| | | | | 46:8b-15 |
| | 46:16-18 | | 46:16-18 | 46:16-18 |
| | 46:19-22 | | 46:19-22 | 46:19-22 |
| | 46:23-25 | | 46:23-25 | 46:23-25 |
| | 46:26-27 | | 46:26-27 | 46:26-27 |
| | Yakobo anaishi Gosheni (46:28-47:12) | Yakobo na wana wake wanaishi Misri (46:28-47:12) | Yakobo na familia yake Misri (46:28-47:12) | Yusufu anawakaribisha |
| 46:28-34 | 46:28-34 | 46:28-34 | 46:28-30 | 46:28-30 |
| | | | 46:31-34 | 46:31-34 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA MUKTADHA

A. Yakobo alitaka uthibitisho kutoka kwa YHWH kwamba kwenda Misri ni mapenzi yake.Hii inawezekana kwa sababu
   1. Alikumbuka mapokeo ya zamani ya kifamilia juu ya utumwa wa wayahudi katika Misri, ulionenwa na Ibrahimu kwenye Mwa. 15:13-16
   2. Aliogopa kwa sababu Isaka alizuiliwa kwenda Misri
   3. Alisita kuiacha nchi ya ahadi peke yake

B. Tanbihi ya NKJV (Nelson, 1982) ina orodha ya majina mbalimbali kati ya andiko hili na Hesabu 26 na 1 Mambo ya Nyakati 4 na 7.

| HAPA | HESABU /IMAMBO YA NYAKATI |
|---|---|
| 1. Yemueli, mst. 10, Kut. 6:15 | Yemueli, Hes. 26:12; I Nya. 4:24 |
| 2. Ohadi, mst. 10 (haliko kwenye orodha nyingine) | |
| 3. Yakini, mst. 10 | Shauli, 1 Nya 4:24 |
| 4. Sohari, mst. 10 | Sohari, 1 Nya 4:24 |
| 5. Puva, mst. 13, Hes. 26:33 | Puva, I Nya. 7:1 |
| 6. Yashubu, mst 13 | Yashubu, Hes. 26:24; I Nya. 7:1 |
| 7. Sefoni, mst. 16 | Sifoni, Hes. 26:15, LXX |
| 8. Esboni, mst. 16 | Ezboni, Hes. 26:16 |
| 9. Arodi, mst. 16 | Arodi, Hes. 26:17 |
| 10. Hupimu, mst. 21 | Hufamu, Hes. 26:39 |
| 11. Hushimu,mst. 23 | Shuhamu, Hes. 26:42 |
| 12. Yaseeli,mst. 24 | Yaseri, I Nya. 7:13 |
| 13. Shilemu, mst. 24 | Shilemu, I Nya. 7:13 |

C. Kuna maelezo ya kuvutia ya njia mbalimbali namna YHWH alivyojifunua mwenyewe kwenye kitabu cha Mwanzo
   inapatikana kwenye NIDOTTE, juzuu. 4, ukr. 354.
   1. Kwa maneno, 12:1-3; 13:14-17; 21:12-13; 22:1-2
   2. njozi, 15:1-6; 46:2-4
   3. ndoto, 20:3-7; 28:12-15; 31:10-13,24; 37:5,9
   4. kuonekana/ kuonekana kwa Mungu 12:7; 16:7-14; 17:1; 18:1; 26:2,24; 35:1,9; 48:3
   5. malaika wa BWANA,16:7-13;18:2,16,17-33;21:17-19;22:11-12,15-18; 31:11,13;48:15-16

   Kinachonivutia mimi ni kwamba Mungu anajaribu kuwasiliana kwa kila njia inayowezekana kwenye familia hii ya kipekee kupitia kwake ambaye atajifunua mwenyewe kwa ulimwengu mzima. Mungu anawasiliana! Mungu anajifunua mwenyewe!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:1-4**
**[1] Akasafiri Israeli, pamoja na yote aliyokuwa nayo, akaja Beer-sheba, akamchinjia sadaka Mungu wa Isaka babaye. [2] Mungu akanena na Israeli katika ndoto ya usiku, akasema, Yakobo, Yakobo. Akasema, Mimi hapa. [3] Akasema, Mimi ni Mungu, Mungu wa baba yako, usiogope kushuka mpaka Misri; maana nitakufanya uwe taifa kubwa huko. [4] Mimi nitashuka pamoja nawe mpaka Misri; nami nitakupandisha tena bila shaka; na Yusufu ataweka mkono wake juu ya macho yako.**

**46:1 "Akasafiri Israeli, pamoja na yote aliyokuwa nayo, akaja Beer-sheba"** Ni wazi kutoka Mwa. 37:14,alikuwa anaishi Hebroni muda wote huu na sasa anaenda kuweka kituo kwenye mji huu wa kusini yapata maili 25 kusini mwa Hebroni, eneo lenye kisima maalumu. Mwanzo 21:22-31 na 26:33 kuna tofauti mbili za asili za neno "Beer-sheba" (BDB 92). Eneo hili lina mababa wa imani wa pekee wenye mahusiano na Ibrahimu (kama vile Mwa .21:31-33; 22:19) na Isaka (kama vile Mwa. 26:24-25; 28:13).

Yakobo alichukuwa kila kitu akavikusanya (kama vile. mst. 5-7). Kuhamia kwake Misri ilikuwa ni makazi yake ya kudumu.

◙**"akamchinjia sadaka Mungu wa Isaka babaye"** Inavutia kwamba sadaka ya kuchinjwa ilitolewa baada ya Mungu kuonekana kwa mababa wa imani katika njozi, lakini hapa Yakobo anataka uthibitisho kutoka kwa Mungu kuhusika na safari yake ya Misri. Hii inawezekana kwa sababu

1. alikumbuka mapokeo ya zamani ya kifamilia juu ya utumwa wa wayahudi katika Misri ulionenwa na Ibrahimu kwenye Mwa. 15:13-16
2. aliogopa kwa sababu Isaka alizuiliwa kwenda Misri
3. alisita kuiacha nchi ya ahadi peke yake

Tungo "Mungu wa Isaka babaye"haionyeshi upungufu wa imani binafsi wa Yakobo kwa Mungu, lakini inatilia mkazo kwa watu kale, Mungu wa agano aliyemuita Ibrahimu atoke Uri na kumpa uzao kwenye nchi ya ahadi ya kanaani.

**46:2 "Mungu akanena na Israeli katika ndoto ya usiku"** Ijapokuwa Yusufu alikuwa mtu wa maana sana kwenye sura za mwisho za kitabu cha Mwanzo, kamwe Mungu hakuzungumza nae kwa uwazi katika njozi kama alivyofanya kwa baba wa imani Yakobo. Hivyo basi, inafaa zaidi kugawa sura hizi za mwisho za kitabu cha Mwanzo katika eneo pana ambalo linahusika na maisha ya Yakobo. Hii ni njozi ya Mungu ya mwisho kwa baba wa imani.

◙**"Yakobo, Yakobo"** Hii ni ishara ya upendo (kama vile.22:11).

◙**"mimi hapa"** Hii ni njia ya asili ya Mungu kumuita mtu (kama vile 22:1,7,11,18; 27:1,18; 31:11; 37:13; 46:2).

**46:3 "Mimi ni Mungu, Mungu wa baba yako,"** Hili ni jina la agano (kama vile. 26:24; 28:13; 43:23). Kwa kawaida inazungumzia "*El*, Elohim wa baba yako." *El* (BDB 42) ni jina la ujumla la Mungu kwenye Mashariki ya Karibu ya kale, ambalo limetokana na asili "kuwa imara" na WINGI kutoka (*Elohim*, BDB 43) ambalo mara nyingi limetumika sehemu ya mwanzoni kwenye kitabu cha Mwanzo kumwelezea Mungu kama muumbaji. Tazama mada maalumu: majina ya uungu kwenye 12:1.

◙**"usiogope kushuka mpaka Misri;"** wengine wanaona hofu (BDB 431, KB 432, *Qa* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI) kama inavyosimuliwa kwenye

1. Utamaduni wa kifamilia unasimulia njozi ya Ibrahimu kwenye kitabu cha Mwa. 15:13-16
2. Isaka alizuiliwa kwenda Misri (26:2)
3. Hofu yakuondoka nchi ya ahadi.

Kuna ujumbe kadhaa kutoka kwa Mungu unaohusika na neno hili, 15:1; 21:17; 26:24; 46:3.

◙**"maana nitakufanya uwe taifa kubwa huko"** Huu ni ujumbe mpya ambao haukutolewa hapo kabla kwa Ibrahimu au Isaka. Inaonyesha ni utimilifu wa ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu kwenye 12:2; 17:4,6,20; na 18:18 ambao inaelezea uzao wa Ibrahimu kuwa kama nyota za mbinguni, mchanga wa bahari, na mavumbi ya nchi.

Uwepo wa Mungu kwenye familia ya Yakobo ulisababisha wao kuongezeka haraka (kama vile Kut 1), kama vile uwepo wake kwa Yakobo kule Harani ulisababisha wanyama wa Yakobo wenye madoadoa na wenye rangi kuongezeka kwa haraka kwa idadi. Kuongezeka kwa idadi ni mojawapo ya alama za Baraka za Mungu. Ongezeko hili la haraka ndilo lililohimiza baadae matatizo na mamlaka ya Misri (yaani Seti I; Ramesesi 2).

**46:4 "Mimi nitashuka pamoja nawe mpaka Misri"** Uwepo pekee wa Mungu ni ahadi yake kubwa. Inaonyesha kwanza tabia ya Mungu ya kuokoa (kama vile Mwa. 26:3, 24; 28:15; 31:3; Zab. 23:4; 139:7-12).Muundo huu wa

kisarufi(tungo) ni kutilia mkazo kwa kiebrania (kama invyofutia )! Pia inaonyesha YHWH hazuiliwi kanaani. Yeye ni Mungu wa ulimwengu (yaani, Kumb. 32:8).

◙**"nami nitakupandisha tena bila shaka"** Mungu aliahidi nchi ya kanaani kwa mababa wa imani, lakini Yakobo alifanya makazi ya kudumu huko Misri. Hii ni ahadi ya kiroho kwamba wana wa Israeli watarudi tena kanaani (kam vile. 15:16; 28:15).

◙**"Yusufu ataweka mkono wake juu ya macho yako"** Hii ni wazi ni nahau ya kiebrania inayoelezea kuwepo kwa upendo kwa mtu anapokaribia kufa (kama vile. Mwa. 50:1), mara nyingi inahusisha na tendo la kufunika macho kwa aliye kufa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:5-7**
**[5] Yakobo akaondoka kutoka Beer-sheba; wana wa Israeli wakamchukua baba yao na watoto wao wadogo, na wake zao katika magari aliyoyapeleka Farao ili kumchukua. [6] Wakatwaa na wanyama wao, na mali zao walizokuwa wamezipata katika nchi ya Kanaani, wakaja Misri, Yakobo na uzao wake wote pamoja naye.**
**[7] Wanawe, na wana wa wanawe, pamoja naye, binti zake na binti za wanawe, na uzao wake wote, aliwaleta pamoja naye mpaka Misri**

**46:7 "binti zake na binti za wanawe"** wanazuoni wana mashaka kama hii ina maana kulikuwa na binti wengi zaidi ya Dina, au hii inamaanisha binti za wanawe.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:8-27**
**[8] Haya ndiyo majina ya wana wa Israeli walioingia Misri, Yakobo na wanawe: Reubeni, mzaliwa wa kwanza wa Yakobo. [9] Na wana wa Reubeni; Hanoki, na Palu, na Hesroni, na Karmi. [10] Na wana wa Simeoni; Yemueli na Yamini, na Ohadi, na Yakini, na Sohari, na Shauli, mwana wa mwanamke Mkanaani. [11] Na wana wa Lawi; Gershoni, na Kohathi, na Merari. [12] Na wana wa Yuda; Eri, na Onani, na Shela, na Peresi, na Zera; lakini Eri na Onani walikufa katika nchi ya Kanaani. Na wana wa Peresi, ni Hesroni, na Hamuli. [13] Na wana wa Isakari; Tola, na Puva, na Yashubu, na Shimroni. [14] Na wana wa Zabuloni; Seredi, na Eloni, na Yaleeli. [15] Hao ndio wana wa Lea, aliomzalia Yakobo katika Padan-aramu, na Dina, binti yake. Nafsi zote za wanawe na binti zake walikuwa thelathini na watatu. [16] Na wana wa Gadi; Sefoni, na Hagi, na Shuni, na Esboni, na Eri, na Arodi, na Areli. [17] Na wana wa Asheri; Imna, na Ishva, na Ishvi, na Beria, na Sera, umbu lao. Na wana wa Beria ni Heberi, na Malkieli. [18] Hao ndio wana wa Zilpa, ambaye Labani alimpa Lea, binti yake, naye akamzalia Yakobo hao, nafsi kumi na sita.[19] Wana wa Raheli, mkewe Yakobo Yusufu na Benyamini. [20] Walizaliwa kwake Yusufu katika nchi ya Misri, Manase na Efraimu, aliomzalia Asenathi binti Potifera, kuhani wa Oni. [21] Na wana wa Benyamini; Bela, na Bekeri, na Ashbeli, na Gera, na Naamani, na Ehi, na Roshi, na Mupimu, na Hupimu, na Ardi. [22] Hao ndio wana wa Raheli, aliomzalia Yakobo, nafsi zote walikuwa kumi na wanne. [23] Na wana wa Dani; Hushimu. [24] Na wana wa Naftali; Yaseeli, na Guni, na Yaseri, na Shilemu. [25] Hao ndio wana wa Bilha, ambaye Labani alimpa Raheli, binti yake, naye akamzalia Yakobo hao; nafsi zote walikuwa saba. *26* Nafsi zote waliokuja pamoja na Yakobo mpaka Misri waliotoka viunoni mwake, bila wake za wanawe Yakobo, nafsi zote walikuwa sitini na sita. [27] Na wana wa Yusufu aliozaliwa katika Misri walikuwa nafsi wawili. Nafsi zote za nyumba ya Yakobo walioingia Misri walikuwa sabini.**

**46:10-24** Aya hizi zinafanana na orodha ya kwenye kitabu cha Hesabu 26 na 2 Mambo ya Nyakati 4-7. Orodha hizi mbili zina herufi tofauti na kwa maana hiyo,majina tofauti. Tazama tambuzi za muktadha B. ninaamini ya kwamba inaweza kufafanuliwa kwa utamaduni wa kunenwa au kwamba kipindi hiki watu walikuwa na majina mawili tofauti.

**46:10 "Shauli, mwana wa mwanamke Mkanaani"** Kuna majadiliano mengi juu ya hili kwanini mtu huyu amewekwa pamoja. Ni wazi haikuwa kawaida. Rashi anasema kwamba inamaanisha mwana wa Dina, baba wa Shekemu (kama vile Mwa. R. 80).

**46:12** Aya ya 10-27 inachukulia kwamba ni orodha ya watu wote alioenda na Yakobo Misri, lakini majina ya wana wawili wa Yuda waliokuwa tayali wamekufa (yaani Eri na Onani, kama vile Mwa. 38:7,10) inaonyesha kwamba hii orodha iliongezwa muda mwingine. Sio kwamba ni sahihi, lakini sio sehemu ya muktadha huu.

**46:13 "Yashubu"** Wafasiri wengi wana uhakika kwamba hili jina linatakwa "ayubu" ( ויןב) lakini kwenye kitabu cha 1 Nyak. 7:1 na Hes. 26:24 jina lake ni Yashubu ( ןישׁב).

**46:15 "Nafsi zote za wanawe na binti zake walikuwa thelathini na watatu"** Aya ya 15, 18, 22, na 25 orodha yote jumla imegawanywa tofauti kwenye familia ya Yakobo.

1. Kwenye mst. 15 tuna wana na binti wa Lea
2. Kwenye mst. 18 tuna wana Zilpa, mjakazi wa Lea
3. Kwenye mst . 22 tuna wana wa Raheli
4. Kwenye mst. 25 tuna wana Bilha,mjakazi wa Raheli

Jumla ya muungano wa makundi haya unaojitokeza kwenye mst. 26 ni watu "sitini na sita" na kwenye mst. 27 ni watu "sabini."

Kumekuwepo majadiliano mengi ya jinsi gani hesabu hizi mbili zinasimuliwa kwenye orodha. Wengine wanasema hesabu "sabini", jumlisha binti, Dina, wa kwenye mst. 15, ni sawa sawa na "sabini na moja" ukitoa Eri na Onani wa kwenye mst. 12, kama utamwondoa Yusufu na wana wake wawili, Efrahimu na Manase (mst 27). Wengine wanadai kwamba "sitini na sita" kwenye mst. 26, ukiongeza Yakobo, Yusufu na wana wake wawili, ni sawa sawa na "sabini". Inatia shauku kwamba kwenye kitabu cha Mdo. 7:14 Stefano anataja watu sabini na watano. Hata hivyo, Hesabu hii inatokana na tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania, ambayo ni dhahiri inaorodhesha wana watano wa wana wa Yusufu. Tazama Gleason Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, ukr. 378-379; *Hard Sayings of the Bible*, ukr. 521-522.

**46:17 "na Sera, umbu lao"** kuongezwa kwa binti inaonyesha kwamba orodha imekamilika. Huwenda kwamba wana wengi wa kiume walizaliwa kwa wingi kwenye familia hii zaidi ya mabinti.

**46:20** Yusufu alikuwa na wana wawili kwa mwanamke wa kimisri. Wana hawa wawili walitwaliwa na Yakobo na wakawa wake, hivyo inaleta jumla ya hesabu ya wana kuwa kumi na watatu.

Inaonyesha kwamba Yusufu alipewa urithi mara mbili kama akiba ya mzaliwa wa kwanza, lakini hakupewa nafasi ya kiongozi katika familia. Hii nafasi iliwekwa akiba kwa ajili ya Yuda, mwana wa nne wa Lea. Haya maamuzi yasiyo ya kawaida ni ishara ya uongozi wa Mungu katika familia ya agano!

Efrahimu atakuwa mkuu , kabila lenye nguvu kaskazini mwa kanaani, ambapo Yuda atakuwa mkuu na kabila lenye nguvu upande wa kusini.

Toleo la LXX ina nyongeza ya orodha ya uzao wenye muunganiko na aya hii. Baadhi ya wanazuoni wanafikili ni kusudi lililoshindwa na MT kwa sababu ya Kumb. 32:8 (UBS, *Preliminary and Interim Report on theHebrew Old Testament Text Project*, ukr. 70).

**46:21 "wana wa Benyamini"** wana wa Benjamini wanaonekana kuorodheshwa hapa, lakini unapolinganisha hili na I Nya. 7:6, ni wana watatu pekee wametajwa. Baadhi ya wafasiri wanadai kwamba wengine walio-orodheshwa hapa ni wana wa wana (kama vile Hes. 26:38-40; I Nya. 7:6 na kuendelea; 8:1 na kuendelea).

**46:26 "uzao wake wa moja kwa moja"** Hii orodha kwa namna flani inachanganya kwa sababu

1. Ina orodha ya waliokufa mapema
2. Baadhi ya majina ni ya wingi na inaonekana kuwa baadae ni majina ya ukoo wa kikabila
3. Benjamini, kwenye mst. 21, inasema ana wana kumi badala ya zaidi ya watatu kiutamaduni

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:28-34**

***28*** **Yakobo akampeleka Yuda mbele yake kwa Yusufu, ili amwongoze njia mpaka Gosheni. Wakaja mpaka nchi ya Gosheni.** ***29*** **Yusufu akatandika gari lake, akapanda kwenda kumlaki Israeli, babaye, huko Gosheni; akajionyesha kwake, akamwangukia shingoni, akalia shingoni mwake kitambo kizima.** ***30*** **Israeli akamwambia**

**Yusufu, Na nife sasa, kwa kuwa nimekuona uso wako, ya kuwa ungali hai. [31] Yusufu akawaambia ndugu zake na watu wa nyumbani mwa baba yake, Nitapanda mimi nimpashe Farao habari; nitamwambia, Ndugu zangu, na watu wa nyumbani mwa baba yangu, waliokuwa katika nchi ya Kanaani, wamenijia. [32] Na watu hao ni wachungaji, maana wamekuwa watu wa kuchunga wanyama, nao wameleta kondoo zao, na ng'ombe zao, na yote waliyo nayo. [33] Itakuwa Farao atakapowaita, na kuwauliza, Kazi yenu ni nini? *34* Semeni, Watumwa wako tumekuwa wachunga wanyama tangu ujana wetu, na hata leo, sisi, na baba zetu; mpate kukaa katika nchi ya Gosheni; maana kila mchunga wanyama ni chukizo kwa Wamisri**.

**46:28 "Yakobo akampeleka Yuda mbele yake kwa Yusufu"** kuna baadhi ya wasi wasi kwenye MT. Toleo la Revised Standard Version, inafuatiwa na tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania, inasema "akajitokeza mbele zake huko Gosheni." Hii inadokeza

1. Kwamba Yuda alimwongoza Yusufu njia ya kwenda nchi ya Gosheni kwa baba yao
2. Kwamba akajionyesha mbele ya Yusufu katika nchi ya Gosheni

Inaimarisha uongozi wa Yuda kwenye familia.

**46:29 "gari lake"** kuna kama aina tatu za magari yenye matairi mawili yanayokokotwa na wanyama"magari."

1. Mkokoteni unaovutwa na ng'ombea, kama vile. 45:21
2. Gari la vita lenye baadhi ya vyuma kwa ajili ya ngao. Baadhi hubeba mtu mmoja, lakini gari lingine ni kubwa na linaweza kubeba watu wawili; magari mengi ya aina hii huvutwa na farasi (kwa ajili ya mwendo -kasi), kama vile Kut. 14:7
3. Gari la sherehe yanaonekana kwenye kuta za sanaa za Misri, yamepambwa na huvutwa na farasi. Ni alama ya cheo (kama vile punda weupe katika Palestina), kama vile 46:29

**46:34 "maana kila mchunga wanyama ni chukizo kwa Wamisri"** Wengine wanaliona jambo hili kama

1. Wamisri wakaao mjini walikuwa na uadui mkubwa dhidi ya wafugaji wanao hama hama
2. Wamisri walimkubalia Hyksos,au "wafalme wa kichungaji" aliyewatawala wakati wa karne ya 17 wa uzao wa kifalme na ambaye kimsingi ni msemiti, hakuwa Mmisri. Josephus anataja hili kwenye *Antiquities of the Jews* 11.7.5 (Hengstenberg wanadai kwamba taifa la Israeli walitambuwa kuwa wanalindwa na wamisri wenye nguvu na chuki zao kubwa za ufugaji wa wanyama).
3. Wamisri walimwabudu ng'ombe dume, hivyo basi, yeyote aliyekula nyama ya ng'ombe alifanya machukizo kwao ( kama vile. 43:32; Kut. 8:26,kama wahindi wa siku za leo)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, inamaanisha kwamba una wajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yusufu aliwaondoa watumwa wa kimisri kwenye Mwa. 45:1?
2. Elezea maana ya kanuni ya teolojia iliyosemwa na Yusufu kwenye Mwa. 45:5-9.
3. Elezea maana ya maneno "Yakobo" na "Israeli" na ni kwa jinsi gani yametumika kwenye maandiko.
4. Kwa nini Mungu alimutokea Yakobo katika njozi, lakini sio kwa Yusufu
5. Kwa nini orodha ya kwenye kitabu cha Hesabu 26 na I Nya 4-6 ni tofauti na orodha ya uzao unaotajwa kwenye Mwa. 46:8-27?
6. Ni matatizo gani yanahusiana na hesabu "sabini" yanayopatikana kwenye Mwa. 46:27?
7. Ni kwa namna gani Mungu aliwatumia wamisri wenye chuki kuwa waangalizi wa maisha ya waisraeli waliokaa kama wageni?

# MWANZO 47

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Yakonbo na Nyumba yake Wanaishi katika Goshani<br>(46:38-47:12) | Yakobo Anaishi Goshani<br>(46:28-47:22) | Yakobo na Wanae Wanaishi nchini Misri<br>(46:28-47:12 | Yakobo na Nyumba yake nchini Misri | Anaijali halaiki |
| 47:1-6 | 47:1-6 | 47:1-6 | 47:1-3a | 47:1-5a,6a |
| | | | 47:3b-6 | |
| 47:5b,6a-11 | | | | |
| 47:7-12 | 47: 7-12 | 47:7-12 | 47:7-8 | |
| | | | 47:9-12 | |
| 47:12 | | | | |
| | Yusufu Anakabiliana na Janga la Njaa | | Janga la Njaa | Wazo la Kuhusu Kilimo |
| 47:13-19 | 47:13-19 | 47:13-19 | 47:13-15 | 47:13-14 |
| 47:15-17 | | | | |
| | | | 47:16-17 | |
| | | | 47:18-19 | 47:18-19 |
| Efrahimu na Masihi | Kilio cha YusufuUkubalifu na Baraka<br>kwa Yakoboza Yakobo juu ya la Yakobo | (47:27-48:22 | Ombi la Mwisho | Ombi la Mwisho la Yakobo |
| 47:27-28 | 47:27-31 | 47:27-28 | 47: 27-30a | 47: 27-31 |
| 47:29-31 | | 47:29-31 | | |
| 47:30a | | | | |
| 47:31 | | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:1-6**
[1]**Ndipo Yusufu akaja akamwarifu Farao, akasema, Baba yangu, na ndugu zangu, na kondoo zao, na ng'ombe zao, na yote waliyo nayo, wamekuja kutoka nchi ya Kanaani, nao wako katika nchi ya Gosheni.** [2] **Akatwaa watu watano miongoni mwa nduguze, akawasimamisha mbele ya Farao.** [3] **Farao akawauliza hao nduguze, Kazi yenu ni nini? Wakamwambia Farao, Watumwa wako tu wachunga wanyama, sisi, na baba zetu.** [4]**Wakamwambia Farao, Tumekuja kukaa ugenini katika nchi hii, kwa sababu wanyama wa watumwa wako hawana malisho, maana njaa ni nzito sana katika nchi ya Kanaani. Basi, twakusihi, uturuhusu sisi watumwa wako tukae katika nchi ya Gosheni.** [5]**Farao akamwambia Yusufu, akisema, Baba yako na ndugu zako wamekujia;** [6] **nchi ya Misri iko mbele yako, palipo pema pa nchi uwakalishe baba yako na ndugu zako; na wakae katika nchi ya Gosheni. Tena ukijua ya kuwa wako watu hodari miongoni mwao, uwaweke wawe wakuu wa wanyama wangu.**

**47:1"Ndipo Yusufu akaja akamwarifu Farao"** Tendo hili linaonekana kuwepo na utaratibu wa miadi ya Farao Kukutana na nyumba ya Yusufu (kama vile Mwa. 46:33). Hili linadokezwa katika Matendo ya Mitume 7:13.

◙ **"wako katika nchi ya Gosheni"** Sura za 46 na 47 zinaunganishwa kwa pamoja kwa sababu Yusufu alikuwa amekwisha ifundisha nyumba yake kuhusu jambo gani lisemwe na namna ya kulisema ili kwamba waweze kupokea ruhusa ya kifalme ya kuishi katika nchi ya Gosheni. Nchi hii ilijulikana kwa kuwa na majani yenye rutuba. Pia nchi hii iliitwa "nchi bora," mst. 6 na11 (kama vile 45:18).

**47:2"Akatwaa watu watano miongoni mwa nduguze"**Mara nyingi kumekuwa na madhaanio kuhusu sababu iliyomfanya kuchagua watu watano. Waalimu wa sheria za Kuyunani wanasema kwamba aliwachukuwa wale wanyonge na wasio na mvuto ili Farao asiwaingize ndugu zake katika jeshil, lakini hili linaonekana kustajaabisha. Toleo la Fasiri ya Anchor Bible inadai kwamba ukinyume halisi, ni"aliwachukua wale waliosalia" (uk. 350). Kuna jukumu halisi kwamba namba "tano" ina umuhimu wa kipekee kwa Wamisri kwa sababu inatumika mara nyingi katika sura hizi (kama vile 41:34; 43:34;45:22).

**47:3"Watumwa wako tu wachunga wanyama, sisi, na baba zetu**" Ni muhimu sana kutambua kwamba hawa wanadai kuwa wana wa wachungaji (kama vile 13:7,8; 26:20; 46:32,34), kwa hiyo, yote waliyoyajua ni kuchunga. Wana hawa walitarajia katika nyendo za baba zao. Wachungaji (wa wanyama) waliyaangalia baadhi ya mambo haya yaliyotukia Misri kwa dharau (kama vile 43:32; 46:34; Kut. 8:26). Suala hili linamanisha kwamba (1) kupitia majivuno ya rangi ya Wamisri na (2) utamaduni wa kuwachukia wachungaji, watoto wa Yakobo wangeachwa peke yao wangewavutia. Hili lilikuwa muhimu sana kwa sababu ni dhahiri kutokana na kitabu cha Mwanzo 38kwamba hawa waliungana katika utamaduni wa Kikanaani. Kwa hiyo, kuhamia Misri ilikuwa nafasi kwao kujikusanya kama taifa tofauti lenye umoja wa kidini.

**47:4"Wakamwambia Farao"**Hivi ni vipengele vinne vya mwitikio wao ambao ulimaanisha kuodoa woga wo wote ambao Farao angewasababishia: (1) hawa walikuwa wachungaji; (2) hawa walikuwa wahamaji; (3) hawa walilazimishwa kuja Misri; na (4) hawa waliomba kibali cha kuishi katika nchi hii, kwa uwazi kabisa hawa waliishi hapa kwa kipindi kirefu.

**47:5-6** Kuna tatizo moja katika toleo la MT ambalo mara nyingi mtu hulilinganishana matoleo ya kale. Ilimpasa Farao kuzungumza na ndugu hawa watano, si Yusufu.

**47:6 "ukijua ya kuwa wako watu hodari miongoni mwao, uwaweke wawe wakuu wa wanyama wangu**" Farao pia alikuwa na mifugo katika eneo hili la Gosheni. Hii inaweza kuwa njia nyingine ya kuonyesha hali ya kuwajali kwa sababu ya Yusufu. Anaweza kuwa alihitaji utajiri wa kimwili ambao ulikuwa umeunanishwa na Mungu kupitia watu hawa (kama vile 30:27; 39:5)

| ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:7-12 |
|---|
| [7]**Yusufu akamleta Yakobo babaye ndani akamweka mbele ya Farao Yakobo akambariki Farao.** [8] **Farao akamwuliza Yakobo, Je! Siku za miaka ya maisha yako ni ngapi?** [9]**Yakobo akamjibu Farao, Siku za miaka ya kusafiri kwangu ni mia na thelathini; siku za miaka ya maisha yangu zimekuwa chache, tena za taabu, wala hazikufikilia siku za miaka ya maisha ya baba zangu katika siku za kusafiri kwao.** [10] **Yakobo akambariki Farao, akatoka mbele ya Farao.** [11]**Yusufu akawakalisha babaye na nduguze, na kuwapa milki katika nchi ya Misri, katika mahali pazuri pa nchi, katika nchi ya Ramesesi, kama Farao alivyoamuru.** [12]**Naye Yusufu akawalisha babaye na nduguze na nyumba yote ya babaye, kwa kadiri ya hesabu ya watoto wao.** |

**47:7"Yakobo akambariki Farao"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu Yakobo kumbariki Farao mara mbili (kama vile mst. wa 10). Wengine wanasema kuwa hii ni ni kawaida iliyojikita katika ufunguzi na salamu za kuondokea (kama vile 31:55; Ruthu 2:4, NJB). Hata hivyo, si kawaida kwamba tendo hili limetajwa mara mbili.Mara nyingi kilicho bora hukibariki kinyonge (kama vile Ebr.7:7). Martin Luther anasema kwamba Yakobo aliihubiri ijili kwa Farao na kwamba yeye na mahakama yake waliongoka. Anatumia Zab. 105:22 kama uthibitisho wa huu uongofu wake. Kwa sababu ya Baraka za ki-Uungu juu ya nyumba hii ya Ibrahimu na wale waliohusiana naye, hii aina ya Baraka ambayo ilionekana kumsaidia Farao inaonekana kuwa za maana sana (kama vile matoleo ya NRSV, TEV, NIV). Toleo la Jewish Study Bible, uk. 93, inaorodhesha mistari ambapo wengine wanabarikiwa kwa kuwa na uhusiano wa karibu na nyumba yenye agano (kama vile 12:3; 22:18; 26:4; 28:14; 30:27-30; 39:5,23, uk. 93).

**47:9** "**miaka ya kusafiri kwangu**" Hakika Yakobo alikuwa amekumbana na msongo wa matatizo katika miaka iliyopita ya maisha yake. Roho ya huzuni yake (iliyoletwa na taarifa za kifo cha Yusufu) inafunuliwa katika mstari huu.

**47:11** "**na kuwapa milki katika nchi ya Misri, katika mahali pazuri pa nchi, katika nchi ya Ramesesi, kama Farao alivyoamuru**"Ni wazi kwamba "nchi ya Ramesesi" (kama vile Kut. 1:11; 12:37; Hes. 3:3) na nchi ya Gosheni ni eneo lile lile. Kulitaja eneo la Ramesesi kwa vyo vyote ni (1) ni nyongeza iliyowekwa na mwandishi au (2) kulikuwa na mji ulioitwa kwa jina hili kabla ya Waebrania kujenga hapa kwa mara nyingine katika heshima ya Ramesesi II. Ramesesi II anaonekana kuwa Farao wa lile zoezi la uhamisho wa Waisraeli na anaoneka kuthibitisha kile kipindi kama ilivyo 1290 K.K. hili si sawa kwa sababu ya eneo la makazi ya Kimisri wakati wa kipindi cha Wahyksos ambao walikuwa karibu na nchi ya Gosheni, lakini pia kwa ushahidi wa wataalam wa mambo ya kale wa ujio wa Wapelestinayapata miaka 1250 B.K.

**47:12**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa kadiri ya hesabu ya watoto wao"** |
| **NKJV** | **"kulingana na idadi ilio ndani ya nyumba zao"** |
| **NRSV** | **"kwa kadri ya watoto wao"** |
| **TEV** | **"wakiwemo wadogo sana"** |

| | |
|---|---|
| **NJB** | **"kutoka chini hadi aliye wa mwisho"** |
| **JPSOA** | **"kutoka chini hadi kwa aliye mdogo"** |
| **LXX** | **"kwa kila mtu"** |
| **Peshitta** | **"kadri ya nyumba zao"** |

Neno "aliye mdogo" (BDB 381, KB 378, kama vile Hes. 14:3,31; 31:17) linaweza kumrejelea kila aliye kuwa ndani ya nyumba ambaye alikuwa na uezo wa kula chakula(kama vile 45:11). Walimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwamba watoto walikuwa wakitupa mikate mingi na hii ni nahau ya kuonyesha kwamba Yusufu aliwagawia kwa utele. Inawezekana kwamba hili neno "aliye mdogo" nistiari ya watu wote walio ndani ya nyumba ya agano (kama vile mst. wa 24)

**ANDKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:13-19**
**[13]Wala hapakuwa na chakula katika nchi yote, kwa kuwa njaa ilikuwa nzito sana, hata nchi ya Misri, na nchi ya Kanaani zikataabika, kwa sababu ya njaa. [14]Yusufu akakusanya fedha zote zilizoonekana katika nchi ya Misri na katika nchi ya Kanaani, kwa nafaka waliyoinunua. Yusufu akazileta zile fedha nyumbani mwa Farao. [15] Fedha zote zilipokwisha katika nchi ya Misri na katika nchi ya Kanaani, Wamisri wote walimjia Yusufu, wakisema, Tupe sisi chakula, kwa nini tufe mbele ya macho yako? Maana fedha zetu zimekwisha. [16]Yusufu akasema, Toeni wanyama wenu, nami nitawapa chakula badala ya wanyama wenu, kama fedha zenu zimekwisha. [17] Wakaleta wanyama wao kwa Yusufu; Yusufu akawapa chakula badala ya farasi, na badala ya kondoo, na badala ya ng'ombe, na badala ya punda, naye akawalisha chakula badala ya wanyama wao wote mwaka ule. [18]Na mwaka ule ulipokwisha wakamjia mwaka wa pili, wakamwambia, Hatumfichi bwana wetu ya kwamba fedha zetu zimekwisha, na makundi ya wanyama ni mali ya bwana wetu, hakikusalia kitu mbele ya bwana wetu, ila miili yetu na nchi zetu. [19]Kwa nini tufe mbele ya macho yako, sisi na nchi yetu? Utununue sisi na nchi yetu kwa chakula, na sisi na nchi yetu tutakuwa watumwa wa Farao; kisha utupe mbegu, tuishi wala tusife, wala nchi yetu isipotee.**

**47:13-26** Watoa maoni wengi wmekuwa wakidai kwamba Yusufu aliwatenda Wamisri kwa ukali. Hata hivyo, Yusufu alikuwa akitenda katika utaratibu wa kawaida wa dai la Farao kithiolojia, kama mwakilishi wa mungu jua Re, aliyeimiliki nchi ya Misri, na kuileta katika usawa.

**47:13"zikataabika"** Hiki KITENZI (BDB 529, KB 520, *Qal*cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale. Maana yake ya msingi ni "kunyong'onyea." Nchi ya Kanaani si yenye kuzalisha.Hiii ilitokana na matokeo ya laana ya Mwa.3:17-19 (kama vile Rum. 8:20-22), sehemu ambayo ni asili ya mzungukko wa mambo yasiyo sahihi. Katika hali hii, YHWH analitumia (anatumia si kusababisha) kwa ajili ya makusudi yake. Hali hii ya kukabiliana nahali ya hewa pia inaakisiwa ka tika kipengele cha"kulaani na kubariki" cha Kumbukumbu (kama vile 28-29). Janga la njaa lilisawazika (kama vile 12:10; 41:31;43:1; 47:4,13).

**47:16"Toeni wanyama wenu"**Tayari walikuwa wamekwisha kuuza kila kitu ("toeni," BDB 396, KB 393, *Qal*ya KAULI SHURUTISHI, kama vile mist. ya 15,16) walikuwa katika agizo la kuuza chakula. Sasa, mifugo yao ilikuwa hatarini. Kiukweli,uchuaji wa mifugo, ambayo wasingeweza kuilisha na ambayo ilikuwa inaelekea kupoteza uhai, ni sehemu ya wema wa kimamlaka, si unyonyaji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:20-26**
**[20]Basi Yusufu akamnunulia Farao nchi yote ya Misri; maana Wamisri waliuza kila mtu shamba lake; kwa sababu njaa ilikuwa imewazidi sana, nchi ikawa mali yake Farao. [21] Akawahamisha hao watu, akawaweka katika miji, tangu upande huu wa Misri hata upande huu. [22] Ila nchi ya makuhani hakuinunua; maana makuhani walikuwa na posho yao kutoka kwa Farao, wakala posho yao waliyopewa na Farao. Kwa hiyo hawakuuza nchi yao.**
**[23] Yusufu akawaambia watu, Angalieni, nimewanunua leo, ninyi, na nchi yenu, kuwa mali ya Farao; basi mbegu zenu ni hizi, zipandeni katika nchi. [24]Itakuwa wakati wa mavuno mtampa Farao sehemu ya tano, na**

**sehemu nne zitakuwa zenu wenyewe, kuwa mbegu za nchi, na chakula chenu, na chakula chao waliomo nyumbani mwenu, na chakula cha watoto wenu. [25]Wakasema, Umetulinda hai, na tuone kibali machoni pa bwana wetu, nasi tutakuwa watumwa wa Farao. [26]Yusufu akaifanya sheria kwa habari ya nchi ya Misri hata leo, ya kwamba sehemu ya tano iwe mali ya Farao. Ila nchi ya makuhani tu haikuwa mali ya Farao.**

**47:20"Yusufu akamnunulia Farao nchi yote ya Misri" Katika mwaka wa sita wa janga la njaa**, baada ya mifugo kuwa imeuzwa, waliuza ardhi yao na kujiuza wenyewe kwa Farao (BDB 888, KB 1111, kama vile mist. ya19,20,22,23). Hakika, walikuwa watumikiaji (kama vile mist. ya 23-24). Tunafahamu, si kutokana na Mfumo wa kanuni zaHammurabi, bali ni kutokana na ugunduzi wa wataalamu wa mambo ya kale huko Ugarit na and the Vibao vya Sheria za Nuziujakazi lilikuwa jambao la kawaida, utata wa kiutamaduni wa watu wa Mashariki ya Karibu ya kale. Wadhifa wa Yusufu umetajwa katika 41:40 na 45:8 unamaanisha kwamba huyu alikuwa mtawala wa mambo binafsinya Farao. Mistari ya 20-26 inaonyesha namna yeye binafsi alivomfaidi Farao alipokuwa akiitawa Misri. Zoezi zima "kwa namna fulani" limenukuliwa kutoka kumbukumbu za kihistoria za Misri.

**47:21** "**Akawahamisha hao watu, akawaweka katika miji, tangu upande huu wa Misri hata upande huu**" Watoa maoni wengi wamedai kwamba tendo hili lilifanyika kwa ajili ya kuwezesha zoezi la mgao wa chakula kwa sababu wasingeifanyia ardhi kazi yo yote ile. Hata hivyo, Toleo la Kale la Kiebrania na Vitabu vitano vya mwanzo vya Kisamaria vinaeleza "wengine aliwafanya watumwa" ("kutoka miji hadi," BDB 746, לערים, "watumwa," BDB 713, לעבדים). Tafsiri hii inafuatiwa naRevised Standard Version na inaoneka kuendana na muktadha wa mist. ya 19 na 25, pamoja na kuwapa ugawaji wa mbegu katika mist. ya23. Rashi anasema kwamba aliwahamisha ili kuwahakikishia kuwa hawakuwa wamiliki wan chi hiyo. Toleo la Peshitta na Targum Ongelos lina kifungu "aliwahamisha kutoka mji hadi miji,"ambapo ni kinyume cha MT.

**47:22** Mali ya kidini na vitu vya watu binafsi havikuguswa (kama vile mst. wa 26).

**47:24 "wakati wa mavuno mtampa Farao sehemu ya tano"**Kutoka katika Vibao vya sheria zaHammurabi, maandiko kutoka katika Ugariticana ugunduzi wa wataalamu wa mambo ya kale wa Nuzi, huu haukuwa unyonyaji uliokithiri. Kutokana na kumbukumbu za ki-Mesopotamia nakumbukumbu zingine za kihistoria tunafahamu kwamba kuanzia asilimia arobaini hadi stini hazikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Yusufu alikuwa akiwachukulia watu hawa kwa usawa mkubwa. Walifahamu kwamba, kama ulivyo mst. wa25 mara nyingi unaakisi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47: 27-28**
***[27]* Israeli akakaa katika nchi ya Misri, katika nchi ya Gosheni. Wakapata mali humo, wakaongezeka na kuzidi sana. *[28]*Yakobo akaishi katika nchi ya Misri miaka kumi na saba, basi siku za miaka ya maisha yake Yakobo ilikuwa miaka mia moja na arobaini na saba.**

**47:27** Tendo hili linaunganisha hatua inayoelekea katika hatua ya utawala wa Kimisri ambao ungewaogofya Waisraeli.

**47:28 "Yakobo akaishi katika nchi ya Misri miaka kumi na saba"** Hii ni moja ya mistari kadhaa katika kitabu cha Mwanzo chote ambayo imetumika kuonyesha kipindi Fulani cha matukio makuu. Inatia nshauku kwamba Yakobo alifikiri kwamba ana kwenda kufa baada ya kuishi kwa muda mrefu kabla ya hapo, kama alivyofanya baba yake Isaka, katika Mwa. 27:2. Tendo hili linaonyesha kwamba ijapokuwa hawa walikuwa watu wa Mungu wanye ukuu, bado walikuwa na udhaifu wa kimwili uliohusiana na uzee pamoja na wasiwasi wa kisaikolojia. Kmjua Mungu hakumruhusu mtu kuepukana na matatizo ya uzee.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:29-31**
***[29]*Siku za kufa kwake Israeli zikakaribia; akamwita mwanawe Yusufu, akamwambia, Kama nimeona kibali**

**machoni pako, weka mkono wako chini ya paja langu, ukanifanyie rehema na kweli; nakusihi usinizike katika Misri. [30] Lakini nitakapolala pamoja na baba zangu, unichukue toka Misri, unizike katika kaburi lao. Akasema, Nitafanya kama ulivyosema. [31]Akanena, Niapie. Naye akamwapia. Israeli akajiinamisha kwenye mchago wa kitanda.**

**47:29 "Siku za kufa kwake Israeli zikakaribia"** Kifo kiko mkononi mwa Mungu, si bahatisho, si hatima, si uovu. Hakuna "mvunaji aliye sahihi" ni malaika wa Mungu peke.Kifo si adui, bali uunganishaji mwingine kwa wale walio na uhusiana na YHWH. Katika Biblia si kifo kinacheleta huzuni, bali kifo cha awali au kifo chenye usumbufu. Baada ya anguko la Mwanzo 3 (kama vile Mwanzo 5) kifo ni mwisho wa maisha ya kimwili. Mtu afikishapo umri, kifo huwa baraka!

◙"**weka mkono wako chini ya paja langu**"Kifungu hiki kinaonekana kuwa kanuni ya kiapo cha kinahau miongoni mwa Waebrania wa kale (kama vile 24:2). Kuna uwezekano wa kuwepo ufundi wa aina mbili za mazungumzo ya vitendo : (1) paja ni msuli mkubwa sana mwilini, hivyo, hii ninahusiana na wazo la kuhimarishwa au (2) paja li karibu na viungo vya Yakobo vya uzazi,inarejelea ahadi "uzao" wa ahadi. Hoja ya mwelekeo huu inaonekana kusistiza juu ya vizazi vya Yakobo kama jambo la kweli la kula kiapo. Kwa uwazi kabisa jambo hili lilishikiliwa katika agano la ahadi za Mungu kwa ajili ya uzao, kurudi Kanaani, (kama vile Mwa. 12:1-3).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"rehema na kweli"** |
| **NKJV** | **"kwa rehema na kwa kweli"** |
| **NRSV** | **"utiifu na kweli"** |
| **NJB** | **"uaminifu wa pendo"** |
| **LXX** | **"huruma na ukweli"** |
| **Peshitta** | **"kwa neema na kweli"** |
| **REB** | **"utiifu na uaminifu"** |
| **JPSOA** | **"pendo lisilo na kikomo"** |

Haya ni maagano maalum ya neno *Hesed* (BDB 388, חסד(kama vile 20:13; 21:23) na *emeth* (BDB 54, אמת). Angalia Mada Maalum: Wema katika 19:19.

## MADA MAALUM: KUAMINI, TUMAINI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE(אמו)

VI. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

C. Watu binafsi na jamii
D. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

C. Ibrahim na uzao wake
D. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

VII. Asili kuu iliyotumika

D. אמן (BDB 52, KB 63)
    4. KITENZI
        d. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
        e. Shina la neno *niphal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
            4) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
            5) Kwa vitu, Isa. 22:23
            6) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
        f. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
            7) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
            8) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
            9) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
            10) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
            11) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
            12) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
    5. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
    6. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.

E. אמת (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
    4. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
    5. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
    6. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16

F. אמונה (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
    5. Katika mikono, Kut. 17:12
    6. Katika muda, Isa. 33:6
    7. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
    8. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

VIII. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale
    C. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).
    D. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (אמן).
        4. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
        5. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
            c) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
            d) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
        6. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IX. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale
    C. Petro anaunganisha
        4. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
        5. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
        6. Zab. 118:22 – 1 Pet. 2:7 (jiwe lililokataliwa)
    D. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
        4. Kumb. 10:15; Isa. 43:21

5. Isa. 61:6; 66:21
6. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1Petro. 2:5,9)

2. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii
   C. Utumiaji wake

Neno “akaamini" linatokana na neno la Kiyunani *pisteuō* ambalo pia laweza kutafasiliwa “ kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

D. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi
   6. *eis* inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
      h. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
      i. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
      j. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
      k. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
      l. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
      m. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
      n. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
   7. *ev* inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mk 1:15; Mdo 5:14
   8. *epi* ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
   9. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
   10. *hoti*, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
      l. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
      m. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
      n. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
      o. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
      p. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
      q. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
      r. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
      s. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
      t. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
      u. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
      v. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

X. Hitimisho
   D. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
      5. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
      6. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
      7. Utii
      8. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)
   E. Imani ya Kibiblia ni
      4. Uhusiano binafsi (imani ya awali)

5. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
6. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba "urafiki wa karibu." Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za "kifamilia" (yaani utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia "moyo mpya" na "roho mpya" inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!
Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

F. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusianona Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10) Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

**47:30 "unichukue toka Misri"** Jambo hili linatabili Uhamisho. Yakobo atakuwa amelifahamu kutokana na utamaduni wa Ibrahimu kurdi katika nyumba ya ndugu zake (kama vile Mwa. 15:12-16). Pia inaonekana kumaanishwa katika Mwa. 48:21. Yakobo alifahamu kwamba hatima ya Waebrania haihusiani na kuishi Misri kwa muda mrefu.

**47:31"Niapie"** Yakobo alikuwa na uwezo sana (BDB 989, KB 1396, *Niphal*ya KAULI SHURUTISHI) kwamba hakutaka kubaki Misri na alimuomba mwanae, si kuapia kwa kuweka mkono wake chini ya paja tu,bali kuapa kwa vitendo pia.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, JPSOA** | **"juu ya tendegu la kitanda chake"** |
| **NKJV, NRSV** | **"juu ya tendegu la kitanda chake"** |
| **LXX** | **"akajiinamisha juu ya nguzo yake"** |
| **Peshitta** | **"juu ya kichwa cha nguzo yake"** |
| **REB** | **"kwa kichwa cha kichwa kitanda chake"** |

Neno la Kiyunani la neno "kitanda" ni *mittah*(BDB 641) na "nguzo" ni *matteh* (BDB 641). Tambua kuwa si suala la konsonanti, bali ni suala la irabu. Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu tafsiri hii katika Maandiko ya Masoreti. Toleo la Kale la Kiyunani (kama vile Ebr. 11:21, ambali linafuata XXL) linaibadili stiari hii kuwa "kichwa cha nguzo." Jambo hili linaonekana kuwa na uwezekano kwa sababu nguzo ilikuwa alama ya mamlaka katika Misri ya kale, kwa hiyo, hili lingemaanisha kwamba Yakobo aliinamisha paji la uso wake na kuigusa nguzo ya Yusufu.
Jambo hili linaweza kuwa limeashiria

1. Yakobo kutimiza ndoto ya Yusufu ya Mwa. 37:6-9
2. ukuu wa Yakobo kwa Yusufu kama utimilifu wa mpango wa Mungu kwaajili ya kuiokoa nyumba yake
3. ishara ya Yakobo kuutambua ukuu wa Yusufu (kama vile 48:2; I Fal. 1:47)

## MASWALI YA MJADALA YA SURA YA 39-40

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yusufu angelitaka nyumba yake iishi nchini Gosheni?
2. Kwa nini Yusufu aliwachukuwa ndugu zake watano tu kwa ajili ya kuwakutanisha na Farao?
3. Kwa nini Yakobo alikuwa na huzuni katika mst. wa 9?
4. Kwa nini Yakobo alimbariki Yakobo mara mbili?
5. Kwa nini hili jina Ramesesi lililo katika mst. wa 11 lili saidia katika kipindi cha Uhamisho?
6. Je! Yusufu aliwachukulia kwa ukatili watu wa Misri wakati wa miaka hii ya njaa?
7. Kwa nini Yakobo alimtaka Yusufu kuapia katika namna mbili tofauti kwamba angemchukua kutoka Misri?

# MWANZO 48

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata MT)** |
| Siku za mwisho za Israeli | Yakobo anawabariki wana wa Yusufu | | Yakobo anawabariki Efrahimu na manase | Yakobo anawachukua Wana wawili wa Yusufu Anawabariki |
| 48:1-7 | 48:1-7 | 48:1-7 | 48:1-4 | 48:1-6 |
| | | | 48:5-7 | |
| | | | | 48:7 |
| 48:8-16 | 48:8-16 | 48:8-16 | 48:8 | 48:8-12 |
| | | 48:9a | | |
| | | | 48:9b-12 | |
| | | | 48:13-16 | 48:13-16 |
| (15-16) | (15-16) | (15-16) | (15-16) | (15-16) |
| 48:17-22 | 48:17-22 | 48:17-22 | 48:17-18 | 48:17-19 |
| | | | 48:19 | |
| (20) | | (20) | 48:20 | 48:20 |
| | | | (20) | (20) |
| | | | 48:21-22 | 48:21-22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48:1-7**
**[1] Ikawa, baada ya mambo hayo, Yusufu akaambiwa, Tazama, baba yako hawezi; akawatwaa wanawe wawili, Manase na Efraimu, pamoja naye. [2] Naye akaarifiwa Yakobo ya kwamba, Angalia, mwanao Yusufu anakuja kwako. Israeli akajitia nguvu, akaketi juu ya kitanda. [3] Yakobo akamwambia Yusufu, Mungu Mwenyezi**

**alinitokea huko Luzu, katika nchi ya Kanaani, akanibariki, [4] akaniambia, Mimi hapa, nitakuongezea uzao wako, na kukuzidisha, nami nitakufanya uwe kundi la mataifa; kisha nitawapa wazao wako nchi hii baada yako, iwe milki ya milele [5] Basi sasa wanao wawili uliozaliwa katika nchi ya Misri kabla sijaja kwako Misri ni watoto wangu, yaani, Efraimu na Manase watakuwa wangu, kama Reubeni na Simeoni. [6] Na wazao wako utakaozaa baada ya hawa watakuwa wako; kwa jina la ndugu zao wataitwa katika urithi wao. *7* Na mimi nilipokuja kutoka Padan, Raheli akanifia katika nchi ya Kanaani, njiani, si mwendo mkubwa kabla ya kufika Efrathi. Nikamzika katika njia ya Efrathi, ndio Bethlehemu.**

**48:1 "Yusufu akaambiwa"**Waalimu wa sheria wa kiyahudi wanasema kwamba Efrahimu alijifunza kila siku na babu yake Yakobo na ndiye aliyemwambia Yusufu, lakini huu ni mfano mmoja wa maoni ya waalimu wa sheria wa kiyahudi ambao msingi wake wa ni wa kukisia, sio muktadha au taarifa ya maandiko.mara zote ni haki kuuliza wale ambao wanadai kuzungumza kwa ajili ya Mungu, "nionyeshe hili imelipata wapi kutoka kwenye maandiko matakatifu."

◙ **"akawatwaa wanawe wawili, Manase na Efraimu, pamoja naye"** Vijana hawa walikuwa nusu-mmisri, lakini ni wazi hii ilikuwa inaandaa mahali kwa ajili ya Baraka za mkuu wa kaya ( yaani kitendo cha kupanga mtoto) ambapo itawahusisha na wao kuwa warithi kamili.

**48:3 "Yakobo akamwambia Yusufu, Mungu Mwenyezi"** Hili ni jina la utamaduni la wakuu wa kaya kwa Mungu ( kama vile Kut. 6:3).Ni *El Shaddai*; *El* kutoka jina la jumla la Mungu kutoka kwenye asili ya " kuwa imara" na *Shaddai* kutoka kwenye asili ya "titi la mwanamke" ambalo linaonekana linaamisha "mtoshelevu wa vyote" Tazama muhtasari mzima kwenye mada maalumu 12:1.

◙ **"alinitokea huko Luzu, katika nchi ya Kanaani, akanibariki"** Luzu ni jina la kanaani kwa ajili ya Betheli (kama vile Mwa. 17:19; 35:9-15). Ni dhahiri, kuwa YHWH alimbariki Yakobo, na Yakobo sasa anaenda kuwabariki wana wa Yusufu.

Ni jambo la kuvutia kwamba, kama Yusufu alivokuwa mcha Mungu, YHWH hakumtokea yeye kama alivyofanya kwa wakuu wa kifamilia (tazama muhtasri wa 46:2), ambapo inaonyesha hiki kitu cha kawaida kinachohusiana na Yusufu ni dhahili ni kikubwa katika sehemu ya maisha ya Yakobo.

**48:4 "nitakuongezea uzao wako, na kukuzidisha"**Kuna Baraka tatu bayana hapa ambazo zina mahusiano na Baraka za Ibrahimu kwenye kitabu cha Mwa. 12:1-3: (1) Nitakuongezea uzao wako na kukuzidisha; (2) Nami ntakufanya uwe kundi la mataifa; na (3) Nitawapa uzao wako nchi hii. Ni dhahili Yakobo alitoka nje ya masharti kutoka kwenye 35:11 (mst 5), "na wafalme watatoka viunoni mwako," kwa sababu ni dhahili kipengere hiki ni kwa ajili ya Yuda (kama vile 49:10). Mali na wingi wa vitu unaonyesha picha ya familia; lakini wafalme watakuja kutoka katika Yuda (yaani masihi, Isa 9:6-7; Mika 5:2).

◙ **"iwe miliki ya milele" H**ili ni neno la kiebrania *'olam*. Ni lazima litafasiriwe katika mwanga wa muktadha. Mmoja anapokumbuka kipindi cha uhamisho ni wazi kwamba neno hili halikuwa na maana ya kudumu. (Tazama mada maalumu 13:15).

**48:5 "Efraimu na Manase watakuwa wangu, kama Reubeni na Simeoni."** Ni kweli hasa kwamba kwenye mst. 1 Manase anatajwa kabla ya Efrahimu, lakini kutoka mst. 5 na mst. 14 Efrahimu anaonekana mbele ya Manase. Hii inaonekana ilipangwa na Yakobo (kama vile mst. 13-14). Efrahimu na Manase wanachukua nafasi ya Simioni na Reubeni kama wazaliwa wa kwanza, warithi wa awali wa yakobo.( I Nya. 5:1). Efrahimu mdogo atakuwa na nguvu za wawili. Hii haitaathiri uongozi wa Yuda kwenye familia ( kama vile I Nya. 5:2)! Hii ni adhabu ya Reubeni ( kama vile 35:22; 49:4; I Nya. 5:1) na simeoni ( kama vile 34:25; 49:5-7) kama ilivyojumlishwa kwa pamoja kwa wana wa Yusufu. Sio tu kulikuwa na upinduaji uliotazamiwa kati ya Manase na Efrahimu ( kama ilivyokuwa kwa Esau na Yakobo), lakini upinduaji huu unaotazamiwa unafanana kati ya Yusufu na Yuda unaoenda kutokea (kama vile.

49:8-12). Yusufu ni dhahili alichaguliwa kwa ajili ya uongozi wa familia, lakini mchaguzi ni YHWH, sio desturi (yaani kumbuka Daudi na ndugu zake).

**48:6 "Na wazao wako utakaozaa baada ya hawa watakuwa wako"H**ii inadokeza kwamba Yusufu atakuwa na watoto wengi, lakini kama alifanya hivyo hatuna kumbukumbu yao ndani ya Biblia.

**48:7** Haya ni maelezo ya kihistoria juu ya mama yake Yusufu.Kifo cha Raheli kilikuwa na maumivu na kilimtetemesha Yakobo.Aliwaangalia hawa wana wa Yusufu mwana wa kwanza wa Raheli,kama ilivyokuja kutoka kwa Raheli mwenyewe. Walikuwa wakiangalia kwa makini "wana" (kwa maana ya urithi) wa Raheli. Angekuwa na furaha kwa hili hata baada ya kufa kwake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48:8-16**
**[8] Israeli akawaona wana wa Yusufu, akasema, Ni nani hawa? [9] Yusufu akamwambia babaye, Hawa ni wanangu, Mungu alionipa hapa. Akasema, Tafadhali uwalete kwangu nami nitawabariki. [10] Na macho ya Israeli yalikuwa mazito kwa uzee, wala hakuweza kuona. Akawaleta kwake, naye akawabusu, na kuwakumbatia. [11] Israeli akamwambia Yusufu, Sikudhani ya kwamba nitakuona uso wako, na Mungu amenionyesha na uzao wako pia. [12] Yusufu akawatoa katika magoti yake, naye akainama kifudifudi [13] Yusufu akawaweka wote wawili, Efraimu katika mkono wake wa kuume, kuelekea mkono wa kushoto wa Israeli; na Manase katika mkono wake wa kushoto, kuelekea mkono wa kuume wa Israeli, akawasogeza karibu naye. [14] Israeli akanyosha mkono wake wa kuume akauweka juu ya kichwa cha Efraimu, aliyekuwa mdogo, na mkono wake wa kushoto akauweka juu ya kichwa cha Manase, huku akijua atiavyo mikono; maana Manase ndiye aliyezaliwa kwanza. [15] Akambariki Yusufu, akasema, Mungu ambaye baba zangu, Ibrahimu na Isaka, walienenda mbele zake, yeye Mungu aliyenilisha, maisha yangu yote, hata siku hii ya leo, [16] naye Malaika aliyeniokoa na maovu yote, na awabariki vijana hawa; jina langu na litajwe juu yao, na jina la baba zangu, Ibrahimu na Isaka; na wawe wingi wa watu kati ya nchi.**

**48:8 "Israeli akawaona wana wa Yusufu,"**Tunajifunza kutoka mst. 10 kwamba uwezo wa kuona wa macho yake ulikuwa hafifu, lakini sio kiwango cha kupofuka kabisa.Yakobo (alikumbuka udanganyika wa baba yake) alitaka kujua kwa uhakika ni nani atambariki!

**48:9 "Yusufu akamwambia babaye, Hawa ni wanangu, Mungu alionipa hapa"** Waalimu wa sheria wa kiyahudi wanasema kwamba Yakobo alimwonyesha Yakobo hati ya ndoa kumshawishi baba yake kwamba mke wake amebadilika.Hata hivyo,kwangu inaonyesha kwamba aya hii inatia mkazo kwenye maeneo yote, Yusufu aliona mkono wa Mungu kwenye maisha yake.

**48:10 "naye akawabusu, na kuwakumbatia"** Haya ni mapatano maalumu kama haki (kama vile mst . 12) uzoefu.

**48:12**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"akawatoa katika magoti yake"** |
| **NKJV** | **"akawaleta kutoka jirani na magoti yake"** |
| **TEV, REB** | **"akawatoa mapajani mwa Yakobo"** |
| **LXX** | **"akawaleta kutoka katikati ya magoti yake"** |
| **Peshitta** | **"akawaondoa mbele ya magoti yake"** |

Hii ni ibada ya kuthibitishwa umiliki, ambayo inatajwa kwenye mst. 5. Kumpitisha mtoto chini ya viuno inaonekana ni njia kwenye hii jamii ya kale namna ya kupanga mtoto (yaani mwanamke apate uzao kupitia magoti yao, 30:3; Ayub 3:17, tanbihi ya JB,uk. 73).

**48:14 "lakini Israeli akanyosha mkono wake wa kuume akauweka juu ya kichwa cha Efraimu"** Huu ni mwelekeo wa kupishanisha mikono yake kwa maana kwamba mkono wake wa kulia-mkono wa mamlaka—utambariki mwana mdogo ambae atakuwa na mamlaka juu ya ndugu yake (kama Yakobo na Esau). Kinyume cha utamaduni unaotalajia uchaguzi (kama vile mst. 18) inaonyesha mamlaka na Enzi ya Mungu (kama vile mst. 19). Hii ni Baraka

ya kwanza katika Biblia kwa jumuiya kuwekewa mikono. Kutokea hapo na kuendelea ikawa ni utekelezaji wa kawaida.

**MADA MAALUM: KUWEKEA MIKONO KATIKA BIBLIA**

Hii ishara ya kujumuishwa inatumiwa sana katika njia mbalimbali katika Biblia.

1. kula kiapo (yaani mkono katika uvungu wa paja [kama vile Mwanzo 24:2,9; 47:29])
2. kuchukua uongozi wa familia (kama vile Mwanzo 48:14,17,18)
3. kutambua kifo cha dhabihu ya mnyama kama mbadala
   a. Makuhani (kama vile Kutoka 29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
   b. kuwalaza watu (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nyakati. 29:23)
4. mtu wa kukaa pembeni kumtumikia Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au huduma (kama vile Hes. 8:10; 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
5. kushiriki katika kurusha mawe kwa kimahakama kwa kumpiga mwenye dhambi (kama vile Law. 24:14)
6. mkono katika mdomo wa mtu huashiria ukimya au tafakari (kama vile Waamuzi. 18:19; Ayubu 21:5; 29:9; 40:4; Mika 7:16)
7. Mkono wa mtu ukiwa katika kichwa chake humaanisha huzuni/ombolezo (2 Sam. 13:19)
8. kupokea Baraka za afya, furaha na utauwa (kama vile Mt. 19:13,15; Marko 10:16)
9. ikihusiana na uponyaji wa mwili (kama vile Mt. 8:3; 9:18,20; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo. 9:17; 28:8)
10. kupokea Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:17-19; 9:17; 19:6, angalia Kumb. 34:9)

Kwa kushangaza kuna ukosefu wa mfanano katika vifungu ambavyo kihistoria vimekuwa vinatetea kuwekwa wakfu kwa viongozi kwa ajili ya kazi ya injili (yaani kuwekwa wakfu, angalia Mada Maalum: Kuwekwa Wakfu).

1. Katika Mdo. 6:6 Ni mitume wanaoweka mikono yao kwa ajili ya huduma ya watu saba ya kanisa la mahali pamoja.
2. Katika Mdo. 13:3 Ni Mitume na Walimu wanaoweka mikono juu ya Barnaba na Paulo kwa ajili ya huduma ya kimishenari.
3. Katika Mdo. 1 Tim. 4:14 Ni viongozi wa kanisa la nyumbani (wazee) waliojumuishwa katika wito wa kwanza na kuwekwa rasmi.
4. In Katika 2 Tim. 1:6 Ni Paulo anayemuwekea mikono juu ya Timotheo.

Mtawanyiko na utata huu unaonyesha kukosekana kwa mpangilio katika kanisa la karne ya kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa zaidi katika kuendelea na kubadilika badilika na mara zote likitumia karama na vipawa vya roho vya waamini (kama vile Wakorintho 12; 14). Agano Jipya kwa ufupi tu limeandikwa kutetea au kushusha mfano wa serikali (Angalia mtawanyiko huu katika Mdo 15) au taratibu za kuwekwa wakfu. Mpangilio wa desturi za kikanisa ni muhimu lakini sio kibiblia. The Uuungu wa uongozi ni zaidi kiumuhimu kuliko mfumo ya uongozi (yaani dola).

**48:15-16** Aya ya 15-16 ni nyongeza ya Baraka juu ya familia iliyoandikwa kwenye Mwa 49.Kwenye Baraka za mwisho za Yakobo kwa familia nzima hakutaja wana wawili wa Yusufu kwa majina (kama vile 49:22-26). Baraka hizi ziko katika muundo wa kishairi (kama mst. 20). Fahamu alama tatu za Mungu. Mungu anaonekana kama (1) Mungu mkuu wa kaya; (2) Mchungaji; na (3) Malaika. Ni dhahili kwamba malaika kwenye mst. 16 lazima atakuwa ni malaika wa BWANA ambaye alijidhihilisha kimwili (kama vile Mwa. 16:7-13; 18:2, 16, 17-21, 22-23; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16. Tazama mada maalumu 12:7).

**48:15 "Akambariki Yusufu"**Ni dhahili wana hawa wawili (mst. 16) walipokea Baraka za ukuu wa familia ya Yusufu (mst. 15). Kutoka Mwa 49 inaonekana Yusufu alipokea haki ya urithi mara mbili (kama vile. 49:22-26) ya mzaliwa wa kwanza, ambapo Yuda alipokea uzao wa kimasihi (kama vile. 49:8-12)

◙"**kutembea"** KITENZI hiki (BDB 229, KB 246) mara nyingi ni alama kwa ajili ya maisha ya imani (kama vile 5:22,24; 6:9; 24:40; Efe. 4:1,17; 5:2,15). Mungu alidai hivyo (kama vile 17:1).M ungu alitaka mtu atakaye akisi

tabia yake kwa dunia iliyopotea na yenye uhitaji (yaani mataifa). Mababa wa imani, na makosa yao yote, waishi mbele za YHWH kwa utiifu, wakitubu, waaminifu katika njia zao,

Kuwa na njia nyingine, uzima wa milele ni kwaida inayotazamiwa. Tumeokolewa, sio tuwe na Mungu pale tunapokufa, lakini tuwe na Mungu kuanzia sasa! Lengo la imani ya kibiblia ni kufanana na kristo sasa ( yaani Rum. 8:28-29; Efe. 1:4; 2:10; 4:13)! Agano la Biblia lina mahitaji kama;

1 Imani (kwanza na kila siku)
2 kutubu (kwanza na kila siku)
3 utiifu (mtindo wa maisha )
4 maisha ya uvumilivu

Haya yamefafanuliwa kwenye Kumb. 8:6; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16!

**48:16 "aliyeniokoa na maovu yote,"** Neno hili *Go'el* (BDB 145 I, KB 169, *Qal* KAULI ENDELEVU, kama vile Kut. 6:6; 15:13), ambalo limetumika kwa mkombozi wa kiume (Ruthi 4:6) au kisasi cha damu (kama vile Kut. 19:6; Yosh. 20:3). Ina maanisha kwamba ndugu wa kiume aliyelipizwa kisasi au aliyenunuliwa kutoka utumwani, kuharibika kwa fedha, au mateka wa kivita. Neno hili limetokea pia kwenye Ruthi 4:6; Hes. 5:8; I Fal. 16:11; Ayubu 19:25.

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

. AGANO LA KALE

A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
   1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linawakilishwa kithiolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
   2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
      a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
      b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
      c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)

B. Dhana ya kithiolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
   1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
      a. Kimaumbile
      b. Kijamii
      c. Kiroho (kama vile Zab. 130:8)
   2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
      a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
      b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
   3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
   4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
      a. Baba
      b. Mme
      c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

. AGANO JIPYA

A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kithiolojia.
   1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisi ni wa Kristo.
   2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laana" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
   3. *Luō,* "kuweka huru"
      a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
      b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
         1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
         2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
         3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
      c. *Lutrōsis,* "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
         1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
         2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
         3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
   4. *Apolytrōsis*
      a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Mdo. 3:19-21)
         1) Luka 21:28
         2) Warumi 8:23
         3) Waefeso 1:14; 4:30
         4) Waebrania 9:15
      b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
         1) Warumi 3:24
         2) 1 Wakorintho 1:30
         3) Waefeso 1:7
         4) Wakolosai 1:14
   5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kithiolojia katika Agano Jipya.

   1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
   2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
   3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
   4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
   5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, thiolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa

ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!

6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

◙ **"jina langu na litajwe juu yao"** Hii labda inamaanisha mtazamo wa watu wa kale kwamba mtu aliweza kuishi kwa watoto wake (yaani , 2 Sam. 18:18; NIDOTTE, juzuu. 3, ukr. 677), au kuelekea zaidi,kwamba agano la imani ya Yakobo (kama vile. mst. 16, uzao wa 3) itapita kwa hawa wana wawili.

VITENZI vitatu vya mwisho wa mst . 16 ni KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kwenye KITENZI AMRISHI (yaani , "ruhusu. . .")

1. baraka, BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. litajwe, BDB 894, KB 1128, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. likue, BDB 185, KB 213, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48:17-22**
**[17] Yusufu alipoona kwamba babaye anaweka mkono wake wa kuume juu ya kichwa cha Efraimu, ikawa vibaya machoni pake. Akauinua mkono wa babaye auondoe katika kichwa cha Efraimu, ili auweke juu ya kichwa cha Manase. [18] Yusufu akamwambia babaye, Sivyo, babangu, maana huyu ni mzaliwa wa kwanza; weka mkono wako wa kuume kichwani pake. [19] Babaye akakataa, akasema, Najua, mwanangu najua, yeye naye atakuwa taifa, yeye naye atakuwa mkuu; lakini ndugu yake mdogo atakuwa mkubwa kuliko yeye, na uzao wake watakuwa wingi wa mataifa. *20* Akawabariki siku ile akasema, Katika ninyi Waisraeli watabariki, wakisema, Mungu na akufanye kama Efraimu na Manase. Akamweka Efraimu mbele ya Manase. [21] Israeli akamwambia Yusufu, Angalia, mimi ninakufa, lakini Mungu atakuwa pamoja nanyi, naye atawarudisha mpaka nchi ya baba zenu. [22] Nami nimekupa wewe sehemu moja zaidi kuliko ndugu zako, niliyoitwaa katika mikono ya Waamori, kwa upanga wangu na upinde wangu**

**48:17 "ikawa vibaya machoni pake"** KITENZI hiki kwenye *Qal* shina (BDB 949, KB 1269, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ni imara

KITENZI kinamaanisha hisia za Yusufu juu ya hali ya kinyume. KITENZI kinaweza kuelezea

1. huzunika, Mwa. 21:11,12
2. chukiza, Hes. 11:10; Yosh. 24:15; I Sam. 8:6; 18:8; 2 Sam. 11:25; Neh. 2:10
3. sikitiko,Kumb. 15:10; I Sam. 1:8; Neh. 2:3
4. uhasama, Kumb. 15:9; 28:54,56
5. uovu, Mwa. 38:10; 2 Sam. 11:27
6. akaugua Zab. 106:32; 2 Sam. 20:6

Ni dhahili namba #2 inafaa na ni bora kwenye huu muktadha, lakini ni neno gumu. Hisia ya Yusufu juu ya nini Yakobo anachoenda kufanya halikuwa jambo dogo! Aliingilia Baraka na kujaribu kuuhamisha mkono wa Yakobo. Hata Yusufu muda mwingine hakujuwa njia za BWANA.Yakobo, sio Yusufu, ni mkuu wa kaya wa agano la familia.

**48:19** KITENZI "najua" (BDB 393, KB 390,mbili *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinarudiwa mara mbili kwa mkazo .Yakobo alitambua anafanya nini (ni wazi kwa uongozi wa kiroho).Upinduaji uliotarajiwa utaendelea.

**48:20 "Israeli"** "yeye" uzao wa kwanza unamaanisha Yakobo/Israeli, lakini Israeli kwenye uzao wa pili inaweza kumaanisha taifa (ya pamoja, kama vile TEV).

◙ **"Mungu wangu na ukufanye wewe kama Efrahimu na Manase"** Hii ni Baraka inayothibitishwa bila hoja ambayo ilitumiwa na watu wa Mungu.

**48:21 "Angalia, mimi ninakufa, lakini Mungu atakuwa pamoja nanyi, naye atawarudisha mpaka nchi ya baba zenu "** "mimi" ni mkazo . Yakobo ni mkuu wa kaya. Hili ni dokezo jingine la jambo ya kwamba familia nzima itakombolewa kutoka Misri na watarudi katika nchi ya ahadi (kama vile Mwa. 15:12-16).

**48:22 "Nami nimekupa wewe sehemu moja zaidi kuliko ndugu zako"** Hili neno "sehemu moja zaidi" (BDB 1014 I) hasa ni "bega" kwa kiebrania. Ni jina la mji wa shekemu. Wengine wanafikiria inamaanisha eneo la kijiografia kwasababu ya mabaki ya mst. 22, ambayo inamaanisha mauaji ya watu wa shekemu, lakini hii inaonekana sio kawaida kwa sababu kwenye kitabu cha Mwanzo inakanusha matendo hayo. Wengine wanasema kwamba neno "bega" ina maana kwamba walikuwa warefu wa kimo ,yaani rithi zaidi— urithi mara mbili kwa mzaliwa wa kwanza. Wengine wanasema kwamba inamaanisha kuwa eneo la shekemu ambalo Efraimu atarithi na wengine wanasema kwamba inamaanisha shekemu eneo ambalo Yusufu atazikwa (kama vile .Yosh. 24:32). Manase atarithi sehemu mbili za Yordani (kabila pekee lililofanya hivyo). Efraimu litakuwa kabila la watu wengi na nchi itagawanywa (la pili Yuda). Efraimu atatawala sehemu ya kaskazini ya kanaani, kama Yuda atakavyofanya kusini. Kiongozi Yoshua alitoka Efraimu , hata Samweli!

◙**" niliyoitwaa katika mikono ya Waamori, kwa upanga wangu na upinde wangu"** Hili linaonekana ni tukio la kihistoria, lakini hatuna kumbukumbu yake. Waalimu wa sheria wa kiyahudi wanakisia kwamba baada ya mauaji ya washekemu kwamba baadhi ya wafalme wa kanaani walikuja kinyume na Yakobo na akapigana nao kwenye vita. Hakuna kumbukumbu ya hili.

Neno waamori ni mkusanyiko wa neno kuelezea makabila yote ya wakanaani (kama vile Mwa. 15:16). Tazama mada maalumu: Wakazi wa kwanza wa Israeli wa kwanza Palestina katika 12:6.

# MWANZO 49

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (Inafuata MT)** |
| Unabii wa Israeli Kuhusu wanawe | Maneno ya mwisho ya Yakobo kwa wanawe | Baraka za Yakobo kwa wanawe kumi na wawili | Neno la mwisho la Yakobo | Agano la Yakobo |
| 49:1-2 | 49:1-27 | 49:1-27 | 49:1-27 | 49:1-27 |
| (2) | (2) | (2) | (2) | (2) |
| 49:3-4 | (3-4) | (3-4) | (3-4) | (3-4) |
| (3-4) | | | | |
| 49:5-7 | (5-7) | (5-7) | (5-7) | (5-7) |
| (5-7) | | | | |
| 49:8-12 | | | | |
| (8-12) | (8-12) | (8-12) | (8-12) | (8-12) |
| 49:13 | (13) | (13) | (13) | (13) |
| (13) | | | | |
| 49:4-15 | | | | |
| (14-15) | (14-15) | (14-15) | (14-15) | (14-15) |
| 49:16-18 | | | | |
| (16-18) | (16-18) | (16-18) | (16-17) | (16-17) |
| | | | (18) | (18) |
| 49:19 | (19) | (19) | (19) | (19) |
| (19) | | | | |
| 49:20 | | | | |
| (20) | (20) | (20) | (20) | (20) |
| 49:21 | | | | |
| (21) | (21) | (21) | (21) | (21) |
| 49:22-26 | | | | |
| (22-26) | (22-26) | (22-26) | (22-26) | (22-26) |
| 49:14:27 | (27) | (27) | (27) | (27) |
| (27) | | | | |
| 49:28-33 | 49:28 | 49:28 | 49:28 | 49:28 |
| | Kifo na mazishi ya Yakobo (49:29-50:14) | Kifo cha Yakobo na siku ya mwisho ya Yusufu (49:29-50:26) | Kifo na mazishi ya Yakobo (49:29-50:14) | Muda wa mwisho wa Yakobo na mauti |
| | 49:29-33 | 49:29-33 | 49:29-33 | 49:29-32 |
| | | | | 49:33 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Huu ni ushairi uliomgumu kuufasiri. Andiko la Kimasoreti na matoleo ya kale hayalikubali hili. Andiko la Kiebrania ni gumu kwa sababu ya
   1. Maneno adimu
   2. Ushairi mfanano
   3. Nahau mbalimbali
B. Inasaidia kulinganisha huu ubainishaji wa tabia za kitanda cha maiti cha makabila yaliyotoka kwa wana wa Yakobo na wale waliochukua tabia za kipekeyake za wana za kipindi hicho, na ubainishaji wa kitanda cha mauti cha Musa wa makabila katika Kumbukumbu la Torati 33.
C. Ingawa kuna masuala mengi magumu, kwangu mimi mstari wa 10 ni wa muhimu. Watafasiri lazima mara zote wawe waangalifu kwa yale mafundisho wanayoyapenda au muundo wa kithiolojia au desturi za kimadhehebu zinataka andiko la kusema au kuthibitisha. Pale yote yanaposemwa na kufanyika
   1. Kimuktadha
   2. Kivifungu mfanano
   3. Akili lazima zimwongoze kila mmoja wetu katika haya maandiko yaliyo magumu na muhimu
D. Orodha ya wana inawasilishwa kuhusianishwa na mamaye
   1. Lea (aliyeorodheshwa kwenye utaratibu wa kuzaliwa)
   2. Zilpa (mjakazi wa Lea)
   3. Bilha (mjakazi wa Raheli)
   4. Raheli (wote wawili wameorodheshwa katika utaratibu wa kuzaliwa)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:1-2**
**1 Yakobo akawaita wanawe, akasema, Kusanyikeni, ili niwaambie yatakayowapata siku za mwisho. 2**
**Kusanyikeni, msikie, enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israeli, baba yenu.**

**49:1-2** Kuna mlolongo wa amri katika mistari hii ya ufunguzi.

1. kusanyikeni, mst. 1, BDB 62, KB 74, *Niphal* KAULI SHURUTISHI
2. msikieni, mst. 1, BDB 616, KB 665, *Hiphil* HALI YA KUSIHI
3. kusanyikeni pamoja, mst. 2, BDB 867, KB 1062, *Niphal* KAULI SHURUTISHI
4. sikieni. . .sikilizeni, mst. 2, zote BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**49:1 "Yakobo akawaita wanawe, akasema"** Hii ni Baraka ya mwisho ambayo imebainishwa na viongozi wakuu wa kaya. Kitamaduni inachukuliwa kwa uzito/uzingativu mkubwa. Isaka alifanya kitu kama kile kile katika Mwanzo 27; Musa katika Kumbukumbu la Torati 33; Yoshua katika kitabu cha Yoshua 24; na Samweli katika 1 Samweli 12.

Orodha hii inaonekana kuwataja wana wa Lea kwanza na wana wa Raheli mwishoni. Kuna utata mwingi katika Baraka hizi. Uko katika muundo wa ushairi na umeegamia juu ya masihala (kama vile Mwa. 29:30-30:24). Hii Baraka ya wazee ni kwa ajili ya kila mmoja kati ya wana kumi na wawili. Dokezo la sura hii nzima ni kuwa Mungu si tu yuko katika udhibiti wa hatma za mataifa bali hata katika mtu mmoja mmoja (hasa "nini kitatokea kwenu katika siku za mwisho")!

◙
**NASB "siku zijazo"**
**TEV "siku za mwisho"**

Katika andiko la Kimasoreti kifungu (BDB 31 KINAUNDA NENO 398) kimetumika kuhusiana na siku za mwisho (kama vile Hes. 24:14; Isa. 2:2; Ezek. 38:16), lakini muda huo haukubaliani na muktadha. Andiko hili linaelezea makabila kumi na matatu (Yusufu akajakuwa wa Efrahimu na Manase) tofauti na Yakobo. Kwa hiyo, lazima lihusiane na ushindi (Yoshua) na ukaajia (Waamuzi, kama vile Kumb. 31:29) wa Kaanani. Kama mstari wa 10 hauelezei kuhusu utawala wa Daudi toka Yudea, hivyo inawezekana kuwa ni kipindi kile cha mwanzo cha utawala wa kifalme (1 Samweli)

**49:2 "Yakobo. . .Israeli"** Yanafanana kwa uwazi. Yanasema zaidi kuhusu watoa maoni wa sasa na madhanio yao kuwa wanadhani majina haya yanawakilisha waandishi wawili tofauti (kama ilivyofanyika kwa *Elohim* naYHWH). Kiebrania cha kale kilikuwa na miundo, nahau na vipengere vyake vya fasihi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:3-4**
**[3] Reubeni, u mzaliwa wangu wa kwanza, Nguvu zangu, na malimbuko ya uwezo wangu. Umewapita wengine kwa ukuu na kwa nguvu. [4] Umeruka mpaka kama maji, basi usiwe na ukuu, Kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako, Ukakitia unajisi; alikipandia kitanda changu.**

**49:3 "Reubeni"** Mstari wa 3 umeandikwa kwa maneno yanayokua (hakuna KITENZI) na umuhimu wa kijana wa kwanza wa Yakobo, lakini mst. 4 ni wenye madhara makubwa yenye umuhimu wa kuweza kuonyeshwa. Reubeni alifanya matendo ya aibu kwa kutembea na suria la baba yake, Bilha (kama vile Mwa. 35:22). Hapa inaonyesha hisia kali zenye kupitiliza. Wakati baadhi wanaliona kama jaribio la kurithi mapema kile alichonacho Yakobo, inaonekana kutumia zaidi hisia kali za kujamiiana kuliko ulafi.

**49:4**
**NASB, NJB "zisizozuilika"**
**NKJV, NRSV "zisizo imara"**
**LXX "mtukutu," "mtundu"**
**Peshitta "alipotoka"**

Neno hili (BDB 808) laweza kumaanisha
1. mzembe (Kiarabu, kama vile Amu. 9:4; Yer. 23:32)
2. mwenye majivuno (Akkadia)
3. mdhaifu
4. mtundu (kama vile Zef. 3:4)

BDB inalibainisha neno kama "maji yanayochemka" yanayomwagwa juu ya chombo. Ukataaji wa moja kwa moja wa namna za tabia zinazotarajiwa. Inabainisha shauku binafsi juu ya ujizuiaji wa kawaida.
◙
**NASB "usiwe na ukuu"**
**NKJV, Peshitta "usiwe mwenye kuwazidi wengine"**
**NRSV, JPSOA "hutawazidi tena wengine"**
**TEV "hutakuwa mtu muhimu zaidi"**

**NJB** **"hutakuwa mkuu"**
**LXX** **"usifoke kwa fujo"**

KITENZI (BDB 451, KB 451, *Hiphil* KITENZI AMRISHI) katika shina la neno *Hiphil* lenye kumaanisha

1. ondoka, Kut. 10:15; Ruth 2:14,18; II Fal. 4:43; II Nya. 31:10
2. saza mabaki, Ezek. 6:8
3. uwahifadhi, Zab. 79:11 (pekee)
4. mwenye kuzidi wengine, Mwa. 49:4 (hapa tu)
5. walivyokuwa navyo vilikuwa vyatosha, Kut. 36:7; II Fal. 4:43; II Nya. 31:10
6. uwe na wingi, Kumb. 28:11; 30:9

NOMINO imetumika katika mst. 3 mara mbili! Hii inaonyesha umuhimu wa Reubeni, lakini kutokana na mistari ya 2 na 3, vipawa vyake vyote vilipotea. Dhambi ina madhara na huacha makovu ya muda mrefu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49: 5-7**
**5 Simeoni na Lawi ni ndugu; Panga zao ni silaha za jeuri. 6 Nafsi yangu, usiingie katika siri yao, Fahari yangu usiungane na kusanyiko lao, Maana katika ghadhabu yao walimuua mtu, Na kwa ukaidi wao walikata mshipa wa ng'ombe; 7 Ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali, Na hasira yao, maana ilikuwa haina huruma. Nitawagawa katika Yakobo, Nitawatawanya katika Israeli.**

**49:5 "Simeoni na Lawi ni ndugu"** Hawa ndugu wa damu inavyoonekana wao ndio walipanga mpango wa kummua mtu wa Shekemu (kama vile Mwa. 34: 25-30). Andiko hili hata linajumuisha ukweli kwamba, hata kwa ghadhabu zao, (BDB 60 and BDB 720), walikata mshipa wa ng'ombe, ambacho ni kitu tusichojifunza toka katika Mwanzo la 34 au yawezakuwa ni nahau kumaanisha watu muhimu wa mji.

◙ Hakuna VITENZI katika mst. 5 katika andiko la asili.

◙
**NASB, NRSV** **"maneno yao"**
**NKJV** **"mazingira"**
**NJB** **"mipango"**
**LXX** **"maamuzi yao"**
**REB, JB** **"mabaraza"**
**Peshitta** **"asili"**

Katika Kiebrania (BDB 468) halijulikani, lakini neno (linapatikana hapa tu) likimaanisha "vifaa." Baadhi wanadhani kuwa waliingia Shekemu wakiwa wamebeba vifaa vyao vya kulimia na hakuna mtu alifikiria kuwa walikuwepo kwa ajili ya kujeruhi mpaka pale walipoanza kutumia vifaa vyao dhidi ya watu wa kawaida. Mwanzoni ,mwa toleo la UBS na katikati ya taarifa juu ya andiko la kiebrania la Agano la Kale linatupatia chaguzi mbili ambazo zote zinatumia konsonanti ile ile, מכרתיהם

1. 1.panga zao (wasomi wanabashiri toka kwenye ufanano na neno la Kiyunani, NRSV)
2. uharibifu wao

Unachagua chaguo la pili, lakini inatoa alama "C" (panafikiriwa kuwepo na mashaka). Kuna chaguo la tatu toka katika mzizi toka Kushi wenye kumaanisha"kushauri" (kama vile James Barr, *Comparative Philology and the Text of the Old Testament*, uk. 57, kama vile JB, REV).

◙
**NASB** **"vifaa"**
**NKJV** **"vyombo"**
**NRSV, TEV** **"silaha"**

Neno hili (BDB 479) kimsingi linamaanisha "vyombo vya nyumbani," "chombo." Laweza kurejerea

1. vitu vya nyumbani
2. pesa
3. mzigo
4. mapambo
5. silaha za kuwindia
6. silaha za vita
7. ala za mziki
8. nira
9. mfuko wa mchungaji
10. chungu cha kupikia

Kwa wazi neno hili lina elimu –maana pana. Linafanana na neno “upanga” (au chochote BDB 468 inachomaanisha) katika andiko la Kimasoreti neno hili (BDB 479) ni la kwanza BDB 468. Toleo la JPSOA lina kifungu “silaha zao ni panga za jeuri.” Mkanganyiko wa huu mstari unaweza kuonekana katika Nyanja pana za matoleo ya kale.
Hata hivyo, ni dhahili kuwa linarejerea hawa ndugu wawili waliomuua mtu wa Shekemu (kama vile Mwanzo 34).
Mwanzo wa toleo la UBS na katikati ya taarifa juu ya andiko la Kiebrania la Agano la Kale linaorodhesha namna mbili ya kukielewa kifungu hiki cha Kiebrania.

1. כליחמס = silaha za jeuri
2. כלוחמס = wakaamua juu ya

Yanaunganisha chaguzi mbili “silaha za jeuri,”lakini likitoa alama “B” katika kulipima (baadhi wanakuwa na mashaka).

**49:6**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“nafsi yangu. . .utukufu wangu”** |
| **NKJV** | **“nafsi yangu. . .fahari yangu”** |
| **NRSV, Peshitta** | **“Mimi. . .Mimi”** |
| **NJB, REV** | **“nafsi yangu. . .moyo wangu”** |
| **JPSOA** | **“nafsi yangu. . .utu wangu”** |
| **LXX** | **“nafsi yangu. . .sehemu zangu za ndani”** |

Neno la kwanza (BDB 659) ni *nephesh*, lenye kumaanisha “nafsi ya mtu au mnyama” (yaani., ile ambayo hutoa pumzi). Limetumika mara kadhaa katika sura ya 46 (46:15,18,22,25,26 [mara mbili], 27 [mara mbili]), lakini limetafasiriwa kwa namna mbalimbali.
Neno la pili (BDB 458) “*kabod*,” linamaanisha “utele,” “fahari,” au “utukufu” (angalia Mada Maalum katika 45:13). Muundo huu wa mzizi wa neno linajitokeza hapa tu, 31:1, na 45:13. Haya maneno mawili yale yale yanaonekana pamoja katika Zaburi. 7:5. Hata hivyo, katika muktadha huu linarejerea kwa Yakobo mwenyewe na linafanana na neno *nephesh*.
Maneno yote yanaonekana kuwa katika vishazi AMRISHI. Hii mistari miwili ya ushairi katika mst.6 iko katika namna ya kinahau ya Yakobo kutokutaka kuhusiana na mipango au matendo iliyotolewa na wanawe wawili wa kiume katika mauaji yaliyodhamiriwa juu ya wanaume wote wa Kikanaani kwenye mji wa Shekemu.

◙ **“kwa sababu ya hasira zao wakawachinja wanaume”** Yakobo hakutaka kutambulika kuwa na matendo ya kikatili ya hawa wanawe wawili.

◙ **“kwa matakwa yao wenyewe waliamua kuwachinja ng’ombe”** Huu unafanana na ule mstari wa 3. Inavyoonekana unarejerea kwenye mauaji ya kule Shekemu katika namna ya kinahau. Hawa ndugu wawili waliwatendea wanaume wa Shekemu kama vile walikuwa wanyama. Hata yawezakuwa ni dokezo la ugoigoi wa nyendo zao (siku tatu baada ya kutahiriwa).

**49:7 “laana”** Hii (BDB 76, KB 91) ni KAULI TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA ikitumika kama alama ya mshangao (kama vile 3:14,17; 4:11; 9:25; 27:29; Hes. 24:9; Kumb. 27:15-26; Amu. 21:18; I Sam. 14:24,28). Ina matumizi maalum katika Mwa. 12:3 na 27:29 yahusianayo kwenye agano la Ibrahimu, lakini hapa haiwezi kuwa

maana hiyo kwa sababu hawa wana wawili ni sehemu ya agano! Laana lazima ihusiane na kukataliwa kwao kama viongozi wa familia (mzaliwa wa kwanza). Ni "hasira" zao (BDB 60) zilizolaaniwa, na sio wana wenyewe. Hata hivyo, tambua kuwa ni YHWH mwenyewe ("atakayewagawa/kuwaondoa toka kwa Yakobo," BDB 323, KB 322, *Piel* KAULI ISIOTIMILIFU, NAFSI YA KWANZA UMOJA).
Tambua udukuzu mfanano wa wazi kati ya mstari 1 na 2 na mstari wa 3 na 4 kwenye kifungu cha 7. Huu ni mfano mzuri wa namna ambayo ushairi wa Kiebrania umeundwa (angalia uhariri juu ya ushairi wa Kiebrania)

◙ **"nitawagawa katika Yakobo"** Tunatambua kutoka kwenye historia kuwa kabila la Simeoni, katika kupokea eneo la kikabila karibu na Wafilisti (kama vile Yosh. 19:1-9), kwa haraka liliangamizwa na kusimilishwa kwenye kabila la Yuda. Kabila la Lawi likachukua ule uzaliwa wa kwanza (kama vile kutoka 13) na likajakuwa na makuhani ambao wakatawanyika sehemu kubwa ya nchi, hasa miji arobaini na nane ya Kilawi. Sababu moja ya kuamini ukale wa hizi Baraka ni kwa sababu hakuna Baraka zinazoonekana juu ya Lawi waliogawanywa kama ilivyo katika Baraka za Musa kwa makabila kwenye Kumbukumbu la Torati 33.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:8-12**
**[8] Yuda, ndugu zako watakusifu, Mkono wako utakuwa shingoni mwa adui zako. Wana wa baba yako watakuinamia. [9] Yuda ni mwana-simba, Kutoka katika mawindo, mwanangu, umepanda; Aliinama akajilaza kama simba, Na kama simba mke; ni nani atakaye mwamsha? [10] Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfanya sheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja Yeye, mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii. [11] Atafunga punda wake katika mzabibu, Na mwana-punda wake katika mzabibu mzuri. Amefua nguo zake kwa mvinyo, Na mavazi yake kwa damu ya zabibu. [12] Macho yake yatakuwa mekundu kwa mvinyo, Na meno yake yatakuwa meupe kwa maziwa.**

**49:8-12 "Yuda"** Neno Yuda (BDB 397) linamaanisha "sifa" (BDB 393, kama vile 29:35). Inavyoonekana kama kabila imara la kijeshi (kama vile mistari ya 8-9) vile vile utawala wa kifalme (kama vile mistari ya 10-12) ya wana wa Yakobo. Sitiari hii inaendelea mpaka kwa Yuda kama mwana- simba (BDB 158 LINAUNDA NENO BDB 71). Haimaanishi mtoto wa simba kwa namna hiyo, bali ni yule mwana- simba mwenye uwezo (kama vile Hes.24:9).

**49:8 "maadui"** Neno hili (BDB 33, KB 38, Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA) ni la kawaida katika Agano la Kale, lakini zaidi ya mara arobaini limetumika hasa kwa maadui wa mfalme (kama vile toleo la NIDOTTE, juzuu ya 1, uk. 366). Kwenye Baraka hizi za kifalme ni ushahidi mwingine wa ukuu wa Yuda

◙ "**wana wa baba yako watakuinamia"** KITENZI (BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* [Agano la Kale Mwongozo wa uainishaji] au *Hithpael* [Owen, maelezo ya kichanganuzi] KAULI ISIOTIMILIFU kinaonyesha kitendo cha heshima kubwa) ni kama kile kile kilichotumika katika ndoto ya Yusufu katika sura ya 37:7 na 9. Ndugu (pamoja na Yuda) hawakufurahishwa na wazo la kumwinamia mmoja wa ndugu yao, lakini hapa Yakobo anadai kuwa watamwinamia Yuda huko Kaanani kama walivyomwinamia Yusufu huko Misri. Yuda litakuwa kabila la kifalme!

**49:10 "fimbo ya enzi . . .fimbo ya mfalme"** Hizi (BDB 986 na BDB 349, KB 347, *Poel* KAULI ENDELEVU) ziko katika ushirika mfanano zikidokeza kuwa mfalme wa makabila yaliyoungana atatoka Yuda. Kifungu "fimbo ya enzi kati ya miguu yake"yapasa kueleweka katika uwazi wa taswira ya kale ya mtawala wa Mashariki ya Karibu ya Kale ikiashiria alama ya madaraka (mara nyingi fimbo au mkuki) kati ya miguu yake kama kiti chake cha enzi. Lazima ikumbukwe kuwa neno linamaanisha alama ya kimamlaka ya kiongozi wa kijeshi (kama vile Hes. 21:18).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"hata atakapokuja yeye"** |
| **NRSV** | **"hata heshima itakapomjilia"** |
| **TEV** | **"mataifa watampa heshima"** |
| **NJB** | **"hata atakapopewa heshima"** |
| **LXX** | **"hata vitu vilivyotunza kwa ajili yake vitakapokuja"** |
| **Peshitta** | **"hata atakapokuja Yule ambaye fimbo ya Enzi I mikononi mwake"** |

**JPSOA** **"ili kwamba apewe heshima"**
**REB** **"hata apokee kile anachostahili"**
**Fasiri ya Young** **"mpaka uzao wake ujapo"**

Pamekuwepo na majadiliano mengi juu ya namna ya kukielewa hiki kifungu.

1. Lingaliweza kuwa ni jina halisi (Sanh 98b)
2. Lingaliweza kuwa ni jina la mahali, lakini hili lingalikuwa si la kawaida kwa sababu hakuna tukio kubwa lililotokea kwenye huu mji mdogo katika ufalme wa Kaskazini, si Yuda wala katika maisha ya Daudi, au ya Masihi.
3. Baadhi wamedai kuwa ni namna ya ufupisho wa kuandika kifungu hiki "hata atakapokuja Yeye"; hii ni njia ya tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania na Targum Onkelos yanakitafasiri hiki kifungu
4. Baadhi wamesema kuwa hii ni nukuu toka katika Ezek. 21:26-27 kwa maana ya "hata ufalme wa haki wa Daudi/Yuda utakapokuja," ambao ungalimrejerea Masihi; hii ndiyo namna kifungu hiki kimetafasiriwa katika *Revised Standard Version*
5. Baadhi ya toleo la Targums linakitafasiri kifungu hiki "hata Masihi atakapokuja ambaye ataumiliki ufalme"
6. Kuna uwezekano unaopishana kuwa neno Shilo linatokana na mzizi wa Kibabeli unaomaanisha "mwana wa mfalme"

Andiko la Kiebrania la UBS linaonyesha orodha ya chaguzi.

1. יבאשילה, hata atakapokuja Yeye au Yeye atakapokuja
2. יבאשלה, hata atakapokuja Yeye amilikiye (badiliko la voweli)
3. יבאשילה,heshima atapewa Yeye.

Inaupa mstari wa #1 alama "A" (uwezekano mkubwa) na kuunganisha Yeye kwa mwana wa Yuda (mwenye kuitwa "Shela," kama vile 38:5,11,14,26; 46:12; Hes. 26:20; I Nya. 2:3; 4:21).

Mstari huu unarejerea juu ya Masihi kutoka katika ukoo wa Daudi, lakini maana yake halisi haijulikani. Masinagogi ya kale na makanisa yanafikiri ilikuwa ni Masihi. Yuda inakwenda kuyatawala makabila kumi na mawili, lakini Masihi (ukoo wake) unakwenda kutawala falme zote za dunia (kama vile Ufu. 11:15).

Wazo la mfalme wa Israel ambalo lingaligonganisha wanadamu wote linatabiriwa katika kitabu cha Mwanzo.

1. Unabii kwa Ibrahimu, Mwa. 17:6,16
2. Unabii kwa Yakobo, Mwa. 35:11
3. Unabii kwa Yuda, Mwa. 49:8-12
4. Unabii wa Balaamu kuhusu Israeli, Hes. 24:7
5. Maelezo ya Musa kwa ajili ya mfalme, Kumb. 17:14-20
6. Ahadi maalum kwa Daudi, II Samueli 7

◙
**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"mataifa watamtii"**
**TEV** **"watamwinamia wakitii mbele yake"**
**NJB** **"mataifa watamwinamia"**
**JPSOA** **"heshima ya mataifa itakuwa kwake"**
**LXX** **"ni tarajio la mataifa yote"**
**Peshitta** **"kwake yeye watu wa mataifa watamwangalia"**

Andiko la Kimasoreti lina kifungu "na mataifa watamtii" (BDB 429 LINAUNDA NENO 766), ambalo halina KITENZI. Tafasiri ya andiko la kalae la Kiebrania na toleo la Kishamu(Peshitta) yanafanya uainishaji wa kimasihi wa kiulimwengu (yaani., "mataifa," BDB 766 liko katika WINGI [kama vile 27:29] mara kwa mara linalitafasiri neno "mataifa" likirejerea watu wasio wa Ibrahimu wazi [waatu wa mataifa]) katika Zab. 2:8; Dan. 7:13-14!

**49:11 "Atafunga punda wake katika mzabibu, na mwana-punda wake katika mzabibu mzuri"** Mistari ya 11 na 12 inaunda nahau ambayo inarejerea kwenye ustawi. Kuna mizabibu mingi ya kuchagua ambayo mtu hajari ni upi amufunge mnyama wake ambao aweza kuung'oa ili apate njia.

◙ **"amefua nguo zake kwa mvinyo, na mavazi yake kwa damu ya dhabibu"** Huu ni ufanano wa muundo wa Kiebrania ambao unazungumzia utele wa matunda ya mzabibu. Hata hivyo, yaweza kurejerea kwa Yuda kama wakala wa Mungu juu ya hukumu (kama vile Isa. 63:1-6; Ufu.19:13,15).

**49:12 "macho yake yatakuwa mekundu kwa ajili ya mvinyona meno yake yatakuwa meupe kama maziwa**" Hii ni sitiari nyingine kwa ajili ya ustawi ambayo inazungumzia juu ya utele wa mvinyo (TEV, "macho mekundu kama damu [BDB 314]") na kuwa meupe kama maziwa (yaani., mifugo wenye afya).angalia Mada Maalum: Mtazamo wa Kibiblia juu ya Ulevi na Kileo katika sura ya 14:18.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:13**
***13*** **Zabuloni atakaa pwani ya bahari, Naye atakuwa kama pwani za kuegesha merikebu, Na mpaka wake utakuwa kando ya Sidoni.**

**49:13-14 "Zebuloni. . .Isakari**"Kama ilivyo Simioni na Lawi wanavyohusiana pamoja, ndivyo ilivyo kwa Zabuloni na Isakari. Zabuloni linakwenda kuwa kabila lililofanikiwa kibiashara, wakati Isaka anakwenda kuwa kabila lenye nguvu lakini inavyoonekana lisilokuwa na makuu.

**49:13**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"atakaa pwani ya bahari"** |
| **NKJV** | **"atakaa karibu na mahali salama pa bahari"** |
| **NRSV** | **"atakaa pwani ya bahari"** |
| **TEV** | **"ataishi karibu na bahari "** |
| **NJB** | **"atakaa karibu na pwani ya bahari"** |
| **LXX** | **"atakaa kando ya pwani"** |

Kifungu hiki kiuhalisia kinatafasiriwa "pwani ya bahari" (BDB 342 LINAUNDA NENO 410). Kabila hili kamwe halikuishi kando ya bahari (kama vile Yosh. 19:10-16) kwa sababu Asheri yupo kati yao na bahari. Hata hivyo, walijihusisha katika biashara na miji ya Tiro na Sidoni (kama vile mst. 13c; Kumb. 33:19c na d)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:14-15**
***14*** **Isakari ni punda hodari, Ajilazaye kati ya mazizi ya kondoo;** ***15*** **Akaona mahali pa raha, kuwa pema, Na nchi, ya kuwa ni nzuri, Akainama bega lake lichukue mizigo, Akawa mtumishi kwa kazi ngumu.**

**49:14 "Isakari ni punda hodari, ajilazaye katika mazizi ya kondoo"** Mistari hii miwili ya ushairi imetafasiriwa kwa namna mbili.

1. Baadhi yanalichukulia toka kwenye mzizi unamaanisha "vibarua wa siku" (TEV)
2. Wengine wanafikiri linamaanisha ni wavivu kwa sababu hujilaza chini kati ya vilima, mfuko wa kutengenezea vyombo vya baiskeli (TEV), au mazizi (NRSV, NJB) na kugeuzwa katika utumwa (kama vile toleo la NIDOTTE, juzuu ya 2, uk. 994, #4)

Dokezo la wazi halijulikani, lakini hoja ni kuwa walikataa kuchukua fursa za hali zao. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yanalitafasiri kwa namna ya hali chanya.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV,** | |
| **NJB, JPSOA** | **"mazizi"** |
| **NKJV** | **"mizigo miwili"** |
| **TEV (NASB)** | **"mifuko wa vyombo vya kutengenezea baiskeli"** |
| **LXX** | **"kati ya warithi"** |
| **Peshitta** | **"njia kuu"** |
| **REB** | **"boma la ng'ombe"** |

Neno la Kiebrania.המשפתים laweza kumaanisha

1. BDB 1046
   a. Sehemu za moto
   b. Lundo la majivu (yaani., vijiji)
   c. zizi (kama vile Amu. 5:16)
2. KB 652
   a. Mifuko miwili (matumizi mawili ya Kiebrania) kwa ajili punda (Kiarabu na Albright)
   b. Birika juu ya mafiga
   c. Zizi lililotenganishwa (kama vile Zab. 68:13)

Ndiyo, watu wa kisasa wangalipenda kujua haswa hili linamaanisha nini, lakini pamoja na utata, muktadha unajaribu kupamba taswira. Lazima tutegemee juu ya ile picha mpaka habari za kimisamiati au kihistoria ipatikane. Hili sio suala muhimu!

**49:15** Kuna njia mbili tofauti za kuuelewa mstari huu.

1. Isakari alikuwa mvivu na kuwa mtumwa.
2. Isakari alitambua ustawi wa urithi wao na kufanya kazi kwa bidii na kuwa na mali nyingi.

Yote hayo aliyafanya akiwa "amelala chini."je hili linarejerea kwenye uvivu au pumziko baada ya kufanyika bidii kubwa?

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:16-18**
**[16] Dani atahukumu watu wake, Kama moja ya makabila ya Israeli; [17] Dani atakuwa nyoka barabarani, Bafe katika njia, Aumaye visigino vya farasi, Hata apandaye ataanguka chali. [18] Wokovu wako nimeungoja, Ee Bwana.**

**49:16 "Dani"** Huu ni mzaha juu ya jina Dani (BDB 192), lenye kumaanisha "mwamuzi" (BDB 192), kama lilivyo jina Dina (BDB 192) katika muundo wa kike na lenye kumaaanisha "mwamuzi wa kike." Ikiwa hii ni kweli kifungu kinarejerea kwa Dani kama aliye mdogo lakini mwenye sumu.

**49:17 "Dani atakuwa nyoka barabarani"** Mmoja wa watoa maoni wa agano la kale nimpendaye, Leupold,anaichukulia mistari ya 17 na 27 katika maana iliyo chanya(kumbuka mstari wa 18). Hata hivyo, kutokana na muktadha yawezakuwa katika hali iliyo kinyume. Tunayo baadhi ya mifano ya kibiblia ya wale ambao walitoka katika kabila la Dani (kama vile Waamuzi 18). Kwa vile Waamuzi 18 ni wa kwanza kutokea kwenye ibada ya sanamu katikati ya makabila yaliyoko katika biblia na kwa vile Dani aliondoka toka katika ardhi ya kwao aliyopewa na Yoshua, wengi wamedai kuwa dani anapaswa kushutumiwa kwa ajili ya kitendo hiki. Dani hakujumuishwa katika orodha ya makabila yaliyoko katika Ufu. 7:5-8. Wengi wa makasisi wa mwanzo, Irenaeus, Ambrose, Augustine, na Theodore, wanadai kuwa mpinga Kristo angalikuja toka katika kabila la Dani.

**49:18 "Wokovu wako nimeunngojea, Ee Bwana"** Kusudi haswa la mlipuko huu wa maombi ndani ya muktadha huu haukuwekwa wazi. Unatoka kwa Yakobo au Dani? Ni shukrani kwa ajili ya uangalizi wa Mungu (lililotumika tu kwa YHWH katika Mwanzo 49) ulioingia kwenye fikra za watu kwa kumtaja "nyoka," mst. l7, ukirejerea kwenye Mwanzo 3? Yumkini ni ombi kuwa kabila la Dani lingalitambua uasi wao na ile hali ya kurejea kuamini katika ulinzi na ukombozi wa YHWH (yaani., sehemu za mwanzo za kikabila huko Palestina zilizokuwa na udhibiti).

## MADA MAALUM: WOKOVU

Neno hili (BDB 447, KB 446, yote katika NOMINO YA KIUME NA KIKE), ambayo kimsingi yanamaanisha "kuwa hodari na mwenye bidii" au "kuwa huru," lina vidokezo mbalimbali.

1. usalama, 2 Sam. 22:3; Ayubu 5:11; Zab. 12:5
2. ustawi, mafanikio, Ayubu 30:15
3. wokovu wa Kiungu wenye kujumuisha ukombozi wa mwili na kiroho
   a. Mwa. 49:18

b. Kumb. 32:15
c. 2 Sam. 23:5
d. Zab. 3:2,8; 22:1; 35:3; 62:2; 69:29; 70:5; 78:22; 80:3; 89:26; 91:16; 106:4; 140:7
   a. Isa. 12:2; 33:2; 51:6,8; 52:7,10; 56:1; 59:11; 60:18; 62:1,11
4. wazo la ukombozi wa kimwili na kiroho kwa wazi kabisa liko katika kitabu cha Yona 2:9-10
5. ushindi, Kut. 14:30; 15:2; 1 Sam. 14:45; Zab. 20:6; 21:5; 44:4-5; 68:19-20; 118:14,15,21; Isa. 12:2; Hab. 3:8
6. mara nyingi neno "kufurahi" linahusianishwa kwenye wokovu wa YHWH, 1 Sam. 2:1; Isa. 25:9; 26:1; Zab. 9:14; 13:5; 21:1; 35:9; 118:15,21

Wokovu unajumuisha uanzishaji wa jamii na mahusianao ya mwanzo ya YHWH aliyoyakusudia na viumbe vyake vya kibinadamu. Unahusianisha ujumla wa kibinafsi na kijamii!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:19**
**[19] Gadi, jeshi litamsonga, Lakini atawasonga wao mpaka visigino.**

**49:19 "Gadi, jeshi litamsonga, lakini atawasonga wao mpaka visigino**" Kuna mzaha wa wazi juu ya mzizi wa jina (BDB 151), linaloonekana mara nne katika mstari huu. Gadi atakuwa katika sehemu ya kikabila ambayo kiurahisi itavamiwa na mataifa jirani (yaani., Mashariki mwa Yordani), lakini atawafuata na kuokoa mateka (yaani., wenye bahati, waliofanikiwa).Andiko la Kiebrania lina neno "kisigino" (BDB 784, I,a), lakini BDB inataja kuwa neno lawezakuwa עקבמ(מ toka kwenye herufi ya kwanza ya mstari unaofuata wa ushairi, mst. 20). Kama ndivyo, hivyo basi mstari usingelipaswa kusomeka "kisigino," bali "atawasonga wao visigino" (BDB 784, I,c).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:20**
**[20] Asheri, chakula chake kitakuwa kinono, Naye atatoa tunu za kifalme.**

**49:20 "Asheri"** Maana ya kimsingi ya jina Asheri linaonekana kuwa "mwenye furaha" (BDB 81). Hili lawezakuwa linadokeza kwenye udhibiti wa njia za kibiashara kupitia sehemu yao ya ardhi iliyotokana na Yoshua, ambayo iliwafanya kuwa na mali nyingi. Pia, rutuba ya ardhi yao inamaanisha kuwa watatoa chakula kwa ajili ya meza ya kifalme (kama vile Kut.33:24-25).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49: 21**
**[21] Naftali ni ayala aliyefunguliwa; Anatoa maneno mazuri.**

**49:21**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"ayala aliyefunguliwa"** |
| **NKJV, JPSOA** | **"mbawala aliyefunguliwa"** |
| **TEV** | **"mbawala anayekimbia huru"** |
| **NJB** | **"paa akimbiaye haraka"** |
| **LXX** | **"shina linalotambaa"** |
| **Peshitta** | **"mjumbe akimbiaye haraka"** |
| **REB** | **"mwaloni unaotambaa"** |

KITENZI (BDB 1018, KB 1511, *Qal* KAULI TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA) yaweza kumaanisha
1. toa
   a. watu
   b. vitu
   c. ujumbe
2. tuma

3. sambaza (yaani., kuusambaza, kama vile LXX, REB)
4. kumwondoa (kama vile Mwa. 3:23)
5. poteza (kama vile Zab. 50:19)

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“anatoa maneno mazuri”** |
| **NKJV, Peshitta** | **“anatoa maneno ya ki-Mungu”** |
| **NRSV, TEV,** | |
| **NJB, JPSOA** | **“huonyesha furaha na upendo”** |
| **LXX** | **“hutoa uzuri juu ya matunda yake”** |
| **REB** | **“huyatanguliza matawi yake yapendezayo”** |

Neno lililotafasiliwa kama “uzuri” au “lakupendeka” (BDB 1051 I, שפר, cf. Ps. 16:6), consonanti zile zile tatu, pia zaweza kutafasiliwa kama “pembe,” שפר (kama vile Rotherham’s Emphasized Bible).
Toleo la UBS *handbook on Genesis* hutengeneza maelezo yenye msaada, “mabadiliko toka kwenye‘paa’ hadi ‘mvinje’na ‘furaha na upendo’ hadi ‘maneno’ yanajumuisha badiliko la voweli” (uk. 1094). Pale sitiari ya mnyama, na sio ya mmea, ni ya kawaida katika Mwanzo 49 na pale panapokuwepo na ufanano kati ya mistari ya ushairi, mst.21, “paa wazuri” au “paa wenye uzuri” linaonekana kuwa zuri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49: 22-26**
**[22] Yusufu ni mti mchanga wenye kuzaa, Mti mchanga wenye kuzaa karibu na chemchemi, Matwi yake yametanda ukutani. [23] Wapiga mishale walimtenda machungu, Wakamtupia, wakamwudhi, [24] Lakini upinde wake ukakaa imara, Mikono yake ikapata nguvu, Kwa mikono ya Mwenye Enzi wa Yakobo; Kwa jina la mchungaji, yeye jiwe la Israeli, [25] Naam, kwa Mungu wa baba yako atakaye kusaidia; Kwa mibaraka ya mbinguni juu. Mibaraka ya vilindi vilivyo chini, Mibaraka ya maziwa, na ya mimba. [26] Mibaraka ya baba yako Imepita mibaraka ya milima ya kale, Vitu vinavyotamanika vya vilima vya milele; Na vikae juu ya kichwa cha Yusufu, Juu ya utosi wa kichwa chake aliye mkuu kati ya ndugu zake.**

**49:22-26 “Joseph”**Kama ilivyo Yuda alipoondolewa peke yake kati ya wana wa Lea kwenye kupokea uongozi wa familia (yaani ukoo wa Masihi), kwa hiyo Yusufu anaondolewa kati ya wana wa Raheli kupokea urithi mara mbili (yaani., Efraimu na Manase). Hili limekaa kishairi na bado ni maelezo yenye kusisitiza kuhusu nafasi ya Yusufu.

**49:22** Kuna masihala na sitiari katika mstari huu.
1. Neno *Qal* KAULI TENDAJI YENYE HALI YA KUENDELEA, BDB 826, KB 963, inajirudia mara mbili
2. Katika mstari wa 1 “tawi” kiuhalisia linamaanisha “mwana,” lakini katika mstari 3 “tawi” ni “binti”

Hizi sitiari ni za kilimo kwa ajili ya ukuwaji mzuri na mimea yenye kuzaa matunda (kama vile Kumb. 33:13-16).
Baadhi ya watoa maoni wana mashaka juu ya hamisho toka kwenye sitiari ya wanyama (kama vile mistari ya. 9,14,17,21,27,na ufanano katika Kumb. 33:17) na kubadili taswira kumwelekea punda wa mwituni juu ya upande wa kilima (kama vile JPSOA, TEV). Ushairi katika lugha ya kale ikitumia maneno adimu ni kitu cha kuteleza!
Mstari wa 22 una maswali mengi ukiwa na andiko la Kiebrania!

**49:23-25** Mistari hii inazungumuzia kiistiari kwa
1. Uzoefu wa Yusufu akiwa na kakaze na Potifa na maisha ya jela
2. Kabila la wana wa Yusufu (yaani., Efraimu na Manase) na kushinda kwao juu ya mgawanyo wa kikabila huko Kaanani (Yoshua)

Tambua tofauti ya majina kwa ajili ya Mungu.
1. Mwenye Enzi wa Yakobo, mst. 24, BDB 7 UNAUNDA NENO 784, kama vile Zab. 132:2,5; Isa. 49:26 (mwenye Enzi wa Israeli, Isa. 1:24)
2. Mchungaji, mst. 24, BDB 944, KB 1258, *Qal* KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA, kama vile Zab. 23:1; 80:1 (yenye kufanana na nahau za kichungaji, Zab. 78:52)

3. Jiwe kuu (au Mwamba) wa Israeli, mst. 24, BDB 6 UNAUNDA NENO 975, kama vile Isa. 30:29; yumkini inahusianishwa na cheo cha Kimasihi "Jiwe kuu la pembeni" katika Zab. 118:22; Isa. 28:16 (angalia Mada Maalum ifuatayo)
4. Mungu wa baba zenu, mst. 25, kama vile Mwa. 26:3,24; 28:13; 32:9 (yaani Ibrahimu, Isaka; tambua HALI YA UMOJA ni msisitizo juu ya Mungu wa Yakobo)
5. Mwenye Enzi (hasa El Shaddai, kama vile toleo la JPSOA), mst. 25, BDB 994, kama vile 17:1; angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika sura ya 12:1

## MADA MAALUM: JIWE KUU LA PEMBENI

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu kinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi, kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
   B. Alafu baadae lilianza kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
   C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 INAUNDA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
   D. Hii iliendelezwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
      1. Jiwe la msingi, linalowekwa kwanza, ambalo liliwekwa kuhakiki usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia lililoitwa" jiwe kuu la pembeni"
      2. Ingaliweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe la msingi," kutoka katika neno la Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
      3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya mlango wa kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya
   A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)
   B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiihusianisha na YHWH kuwakataa Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)
   C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 akirejerea kwa Kristo
   D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

III. Maelezo ya Kithiolojia
   A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliachwa katika ukiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!
   B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa mtu binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, yakielekezwa kwa dini ya Kiyahudi.
   C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama ilivyo masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).
   D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo

kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).

E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani Alfa na Omega). Bado, pia ni jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na sehemu ya malidhiano hapa!

**49:25-26 "mibaraka"** Tambua ni mara ngapi neno hili limetumika.

1. Ambaye hukubariki, mst. 25, BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI ISIOTIMILIFU, kama vile 28:3; 48:3
2. Kwa mibaraka ya mbinguni juu, mst. 25, BDB 139, kama vile 27:28; Kumb. 33:13
3. Mibaraka ya vilindi vilivyo chini, mst. 25, BDB 139, kama vile Kumb. 33:13
4. Mibaraka ya maziwa, na ya mimba, mst. 25, BDB 139
5. Mibaraka ya baba yako, mst. 26, BDB 139
6. Imepita mibaraka ya mababu, mst. 26 (kifungu kigumu cha Kiebrania na hakijumuishi tena "mibaraka")

Mibaraka ilikuwepo kwa ajili ya kuwahakikishia wazee uwepo wa Mungu kwao (kama vile Mwa. 12:2; 22:17; 24:1; 26:12; 30:30) na kuwabariki wengine kupitia kwao (kama vile Mwa. 12:2-3; 22:18; 30:27; 39:5). Hili ndilo lilikuwa kusudi la mwanzo la Mungu kwa ajili ya uumbaji (kama vile 1:22,28)! Huu sio ulimwengu ule Mungu alioukusudia uwe (kama vile Mwanzo 3). Uchaji Mungu wa Yusufu ulimwezesha Mungu kuonyesha kusudi lake la mwanzo kwake na familia yake.

**49:25 "kwa mibaraka ya mbinguni juu,**
**Kwa mibaraka ya vilinndi vilivyo chini**
**Mibaraka ya maziwa, na mimba**" Huu ni msisitizo mara tatu juu ya utele wa mazao, mifugo, na ongezeko la watu. Hili ndilo YHWH alihitaji kulifanya kwa ajili ya mwanadamu pale bustani ya Edeni. "mbingu" na "chini ya vilindi" ni sitiari kwa ajili ya mibaraka mikubwa, na mingi. Yote ingalizungumzia unyevu kwa ajili ya uwepo tele wa mazao na nyasi za mifugo (kama vile Kumb. 33:13).

**49:26** Kuna ufanano kati ya mstari wa 2 na wa 3, lakini yote ina ugumu wake katika Kiebrania.

1. Mibaraka ya milima ya kale (הריעד, BDB 249) au ya mababu (הוריעד, BDB 223 pia inadhaniwa kuwa inarejerea kwenye mfanano wa milima ya kale, kama ifanyavyo tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania na ufanano kwenye Kumb. 33:15; andiko la Kimasoreti lina neno "mababu," lakini muundo huu unapatikana hapa tu)
2. Mibaraka ya vilima vya milele

Katika muktadha wa ufanano mistari yote yumkini inazungumzia juu ya milima na vilima, ambayo ilikuwa ni nahau kwa ajili nguvu na ukaaji wa kudumu.

◙**"aliye mkuu kati ya ndugu zake**" Neno"aliye mkuu" (BDB 634) linatokana na mzizi kwa ajili ya neno "Nazareti," ambalo linamaanisha "kutenga kitu" (kama vile TEV) au "kuwekwa wakfu." Yumkini laweza kuonyesha mwana wa mfalme au afisa (kama vile Nahumu 3:17). Laweza kurejerea kwenye nafasi ya uongozi wa Yusufu huko Misri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:27**
**27 Benyamini ni mbwa-mwitu mwenye kurarua-rarua Asubuhi atakula mawindo, Na jioni atagawanya mateka**.

**49:27 "Benyamini"** Ameelezewa kama mbwa-mwitu (BDB 382, KB 380, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU). Baadhi wanasema kuwa alikula chakula chote cha watu watano kilichowekwa mbele yake (kama vile Mwa. 43:34). Baba yake alijua tabia ya ulaji wake! Mstari wa 27 uko kinyume, kumbuka Waamuzi 19-21. Leupold anaitafasiri mistari ya 17 na 27 kwa namna chanya. Ushairi wa Kiebrania una utata katika namna ya uwasilishaji wake na utumiaji adimu wa maneno yaliyotumika kutengeneza mapigo yake (utamkaji wa silabi).

◙**"mawindo"** Mzizi wa neno עד (BDB 723 I) mara nyingi humaanisha milele (yaani., Mwa. 49:26; nasana sana katika Zaburi na Isaya), lakini katika baadhi ya maandiko (kama vile hapa; Isa. 33:23; Zeph. 3:8) humaanisha mateka waliochukuliwa katika vita wakitumia sitiari ya "mawindo."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:28-33**
**28 Hizo zote ndizo kabila za Israeli kumi na mbili. Na hayo ndiyo aliyowaambia baba yao, na kuwabariki; mmoja mmoja kwa mbaraka wake aliwabariki. 29 Akawaamuru, akasema, Mimi ninakwenda kukusanywa pamoja na watu wangu; mnizike pamoja na baba zangu, katika pango iliyomo shambani mwa Efroni, Mhiti; 30 katika ile pango iliyomo shambani mwa Makpela, iliyo mbele ya Mamre katika nchi ya Kanaani, aliyoinunua Ibrahimu pamoja na shamba kwa Efroni Mhiti, pawe milki yake ya kuzikia. 31 Humo walimzika Ibrahimu, na Sara mkewe; humo wakamzika Isaka, na Rebeka mkewe; nami humo nikamzika Lea; 32 shamba na pango iliyomo lililonunuliwa kwa wazawa wa Hethi. 33 Basi Yakobo alipokwisha kuwaagiza wanawe, akakunja miguu yake kitandani, akafa, akakusanywa pamoja na watu wake.**

**49:29 "kukusanywa pamoja na watu wangu"** Hii ni nahau kwa ajili ya kifo na mazishi (kama vile 25:8,17; 35:29; 49:33; Hes. 20:26; 27:13; 31:2; Kumb. 32:50; Amu. 2:10; II Fal. 22:20). Ikiwa hili linadokeza kuunganika tena kwa familia huko Sheoli haijulikani. Yawezakuwa ni namna ya kurejerea kwenye mapango au makaburi ya familia. Lakini kwa sababu ya kuabudu vinyago (kama vile 31:19,34,35, angalia Mada Maalum katika sura ya 31:19) yawezakuwa na maana kubwa (kama vile Mt. 22:31-32).
Angalia *Hard Sayings of the Bible,* kur. 127-129, kwa ajili ya mjadala stahiki juu ya kifungu kinachodokeza maisha baada ya kifo.

◙**"ndani ya pango"** Hili linarejerea mahali pa maziko ya wazee wao paliponunuliwa toka kwa Efroni Mhiti, lililodokezwa kwenye Mwa. 23:1-19. Kuna maana pale agano la kifamilia linapounganishwa na maisha baada ya kifo.
Yakobo analitetea kwa namna ya kulizunguka ili kwamba familia yake isingalikaa Misri, lakini kwa namna Fulani angalirejea Kaanani (kama vile 15:12-21). Yusufu anafanya aina kama ile ile ya ombi la kinabii katika sura ya 50:24-25. Misri yalikuwa ni makazi ya muda ambayo yangaliwasababisha wanyonywe.

**49:31 "Rebeka. . .Lea"** Hii ni habari ya kwanza ya maziko ya hawa wawili. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa Yusufu angalikasirika kwa vile mama yake alizikwa kando kando ya njia, lakini hili linaonekana kuwa dokezo la kinabii kipindi wakati makabila ya Kaskazini yaliingia kwenye utumwa na Raheli atalia kwa ajili ya wanawe pale anapowaona wakipita kwa vile amezikwa kando ya njia na wangalimchukua pindi wanapopita kwenda uhamishoni (kama vile Yer. 31:15).

**49:33 "akakunja miguu yake kitandani**" Ikiwa Yakobo alikuwa amekaa kwa muda wote hii inaonyesha alikuwa amejilaza; vinginevyo inaonyesha kurejerea namna ya mauti. Baadaye avute pumzi ya mwisho (ni nahau kwa ajili ya mauti).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yakobo alikubaliana na Efraimu na Manase?
2. Nini umuhimu wa majina matatu ya Mungu yaliyopatikana katika Mwa. 48:15-16?
3. Ni namna gani ya mibaraka ya sura ya 49 inahusiana na majina ya wana hawa wanaopatikana katika Mwa. 29:30-30:24?

4. Ni wapi kati ya wale wana wawili wanaoonekana kupokea mibaraka mikubwa na ni nini dhima ya mibaraka tunayoikumbuka?

# MWANZO 50

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB (inafuata)** |
| Mauti ya Israeli | kifo na maziko ya Yakobo (49:29-50:14) | Kifo cha Yakobo Na siku ya mwisho Ya Yusufu (49:29-50:26) | Kifo na maziko ya Yakobo (49:29-50:14) | Msiba wa Yakobo |
| 50:1-3 | 50:1-3 | 50:1-3 | 50:1-3 | 50:1-3a<br>50:3b-6 |
| 50:4-6 | 50:4-11 | 50:4-6 | 50:4-5<br>50:6 | |
| 50:7-11 | 50:7-14 | 50:7-9 | 50:7-9 | |
| Maziko huko Makpela | | | 50:10-11 | 50:10-11 |
| 50:12-14 | | 50:12-14 | 50:12-14 | 50:12-13<br>50:14 |
| | Yusufu anawahakikishia Nduguze | | Yusufu anawahakikishia nduguze | Toka kwenye mauti ya Yakobo mpaka mauti Ya Yusufu |
| 50:15-21 | 50:15-21 | 50:15-21 | 50:15-17<br>50:18<br>50:19-21 | 50:15-17<br>50:18-21 |
| Mauti ya Yusufu | Mauti ya Yusufu | | Mauti ya Yusufu | |
| 50:22-26 | 50:22-26 | 50:22-23<br>50:24-26 | 50:22-26 | 50:22-25<br>50:26 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xxiv)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:1-3**
**[1] Yusufu akamwangukia babaye usoni, akamlilila, akambusu. [2] Yusufu akawaagiza watumishi wake waganga, kwamba wampake baba yake dawa asioze. Waganga wakampaka dawa Israeli. [3] Siku zake arobaini zikaisha, maana hivyo hutimizwa siku za kupaka dawa. Wamisri wakamlilia siku sabini.**

**50:1** Mstari huu unaonyesha alama tatu za masikitiko zinazohusiana na kifo.
1. Akamwangukia babaye usoni, BDB 656, KB 709, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU, inayofanana na 33:4
2. akamulilia, BDB 113, KB 129, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU
3. akambusu, BDB 676, KB 730, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU

**50:2 "waganga"** Hili ni neno *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU la KITENZI "kuponya" (BDB 950, KB 1272, kama vile II Nya. 16:12). Palikuwepo na watu wenye weledi wa kutia mafuta maiti wasioze, lakini Yusufu yumkini alitumia waganga ili kwamba kuweka pembeni maoni ya kidini ya watia manukato maiti wa Kimisri (*NASB Study Bible*, uk. 73). Yakobo alilindwa ili kwamba baadaye aweze kuzikwa kwenye mapango ya kifamilia huko Kaanani (kama vile 49:29-32).

◙**"kupaka dawa"** KITENZI hiki (BDB 334, KB 333, *Qal* KITENZIJINA CHENYE MUUNDO WA MANENO) kinamaanisha "viungo," "kuweka vionjo"(kama vile Wimbo ulio Bora 2:13),au "kutia dawa maiti isiharibike." Hii ilikuwa ni namna pekee ya Wamisri, inayopatikana hapa tu katika Agano la Kale. Ilikuwa na mahusiano ya kidini ya Osiris (yaliyoanza yapata mwaka wa 2700 K.K.) na imani ya Wamisri baada ya mtu kufa ilijumuisha.
1. Uondoaji wa viungo vya ndani vya mtu na walivihifadhi kwenye mitungi
2. Baadaye tena ubongo wa mtu ulitolewa na kutunzwa kwenye mtungi mwingine tofauti
3. Mwili ulizungushiwa na nguo ya kitani safi

Habari iliyoandikwa ni namna gani utiaji wa dawa ya maiti ulikuja toka kwenye hadithi za zamani za Herode, *History* 2:85-90 and Diodorus Siculus, *History*1.91. Kwa ajili ya mazungumzo mapana zaidi angalia ABD, juzuu 2, kur. 490-495, na James M. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, kur. 56-58. Mazungumzo haya hayamaanishi kwa namna yeyote kuelezea vitendo vya utiaji dawa maiti wa sasa. Hapana vidokezo vyovyote vya kidini kama zilivyofanyika ibada za Kimisri. Wengi wamefikiri kuwa maelezo ya laana katika Mwa. 3:19 bado yanatumika. Binafsi nafikiria kuhusu mabaki ya mwili (yaani., mwili wa binadamu) sio vya muhimu kihivyo!

## MADA MAALUM: UCHOMAJI MAITI

I. MAELEZO YA KALE

A. Uchomaji (uteketezaji) maiti ilikuwa moja ya njia nne za kutoa adhabu kubwa katika Mambo ya Walawi (kama vile Law. 20:14; 21:9, Mwa. 38:24 na Yos. 7:15,25).

B. Watu waliokuwa na upendo kwa Sauli, waliutwaa mwili wake na miili ya wanae watatu kutoka kwa Wafilisti na kuiteketeza (BDB 976, LXX) kabla ya kuizika mifupa yao katika nchi ya Benjamini (kama vile 1 Sam. 31:12-13, kimechukuliwa katika ufanano na 1 Nya. 10:12). Andiko hili ndilo lenye kuonyesha tendo la uchomaji maiti katika Agano la Kale *Encyclopedia Judaica*, juzu 5, uk. 1074). Pia tendo hili linaweza kurejelea juu ya mchanganyiko wa manukato katika eneo la mazishi (kama vile 2 Nya. 16:14; 21:19; Yer. 34:5).

C. Uteketezaji wa miili ilikuwa ishara ya hukumu.

1. Nabii wa Yuda alitabiri juu ya makuhani wa Betheli kuiteketeza dhabihu juuya madhabahu (kama vile 1 Fal. 13:2)
2. Katika siku ya mwisho wale waliouvamia mji wa Kanaani watateketezwa na kuunguzwa (kama vile Eze. 39:11-16)

3. Katika uhusiano na pigo la hukumu ya Amosi 6:10 (yaani, andiko gumu)

D. Suala la uchomaji maiti kwa wakati mwingine limehusianishwa kimakosa na matumizi Agano la Kale ya moto kama stiari ya hukumu (kama vile Isa. 30:33). Stiari za uchomaji maiti (yaani, "kimbwi") zinatumika kusistiza juu ya dai la matukio ya siku za mwisho.
E. Uchomaji maiti ulionekana kama unyanyasaji (kama vile Amos 2:1).
F. Maziko yalifanywa na nchi zote za Mashariki ya Karibu ya Kale (kama vile Roland de Vaux, *Ancient Israel,* juzuu. 1, uk. 57).

II. SHERIA ZA DINI YA KIYAHUDI

A. Walimu wengi wa sheria za dini ya Kiyahudi wanadai kwamba tendo la kuzika limeamriwa na Kumb. 21:23.
B. Uchomaji maiti umezuiwa katika Talmud (Sanh. 7:2,24b) na Mishna ('Abodiah Zarah 1.3).
C. Dini ya Kiyahudi ya sasa inaruhu wale waliochomwa kuwekwa katika makaburi ya Kiyahudi (kama vile *Encyclopedia Judaica*, juzu 5, uk. 1074), huenda dini hii imeshawishiwa na uchomaji maiti wa Wayahudi unaofanywa na Wanazis.

III. UYUNANI NA RUMI

A. Mabadiliko yote haya yalikuwa ya zoezi la uchomaji maiti.

1. Uyunani mara kwa mara (Sophocles, *Electra*, 1136-1139)
2. Roma kama watendaji, lakini si sheria, hiari (Cicero, *Deleg* 2,22,56)

B. Utamaduni wa ki-Mediterranea ulikuwa na mtazamo tofauti kuhusu uchomaji wa maiti kuliko tamaduni za Mashariki ya Karibu ya Kale. Tacitus anataja kwamba maziko ya Wayahudi, si ya kuteketeza miili ya maiti (*Hist.* 5.5)

. AGANO JIPYA

Hakuna mjadala ama maelezo yo yote ya jambo hili katika Agano Jipya. Mwonekano wa mwili unatazamwa kama vazi la muda (kama vile 2 Wakorintho 5). Wale waliolala mauti watakuwa pamoja na wale walio hai katika kuja kwake Bwana, lakini hakuna ufafanuzi ama maelezo ya (kama vile 1 Thes. 4:13-18). Tendo hili halimaanishi suala la "imani na matendo" kwa Wakristo. Kama walivyo Wayahudi wa Agano la Kale, waamini wa Agano Jipya wanaeleza juu ya ufufuo wa miili. Katika siku mwisho kutakuwa na mwonekano wa kimwili, lakini ni kwa namna gani aukwa nini, haibainishwi! Hali ama mabaki ya haiwaathiri wale watakuwa pamoja na Yesu. Imani katika Kristo ndio kiini, si mabaki ya mwili!

## MADA MAALUM: TARATIBU ZA MAZIKO

I. Mesopotamia
A. Mazishi sahihi yalikuwa muhimu sana kwa maisha ya baadae yenye furaha ambayo daima yalitazamwa kama mwendelezo wa maisha yaliyopo hapa, (tazama Mada Maalumu: Wafu wako wapi?).
B. Mfano wa laana ya watu wa Mesopotamia ni, "Ardhi haiwezi kuzipokea maiti zenu "

II. Agano la Kale
A. Mazishi yaliyo sahihi yalikuwa muhimu sana (kama vile Mhu. 6:3).
B. Yalifanyika haraka sana (kama vile Sara katika Mwanzo 23 na Raheli katika Mwa. 35:19 na tazama

Kumb. 21:23).

C. Mazishi yasiyo sahihi yalikuwa ishara ya kukataliwa na dhambi.
1. Kumbukumbu la torati 28:26
2. Isaya 14:20
3. Yeremia 8:2; 22:19

D. Mazishi yalifanyika kama iwezekanavyo, katika vyumba vya familia vya ndani kwa ndani katika maeneo ya nyumbani (yaani , alilala na babazake").

E. Hapakuwa na mafuta ya kupaka maiti isioze kama ilivyo kuwa Misri. Mwanadamu alitoka mavumbini na atarudi mavumbini (mf.Mwa. 3:19; Zab. 103:14; 104:29 Pia angalia Mada Maalumu: Uchomaji maiti.

F. Katika sheria za dini za Kiyahudi ilikuwa vigumu kuweka usawa wa heshima kamili na kuukabili mwili katika dhana ya kuinajisi sherehe kunakohusishwa na maiti.

III. Agano Jipya

A. Mazishi ya haraka yalifuatia kifo, kwa kawaida ilikuwa ndani ya masaa ishirini na nne.Wayahudi kwa kawaida walilinda kaburi kwa siku tatu, wakiamini kuwa nafsi ingeweza kuurudia mwili ndani ya siku hizo (kama vile Yohana 11:39).

B. Mazishi yalijumuisha kuosha na kufunika maiti kwa manukato(kama vileYohana 11:44; 19:39-40).

C. Hapakuwa na utofauti katika taratibu za maziko kati ya Wayahudi na Wakristo (au kitu kilichowekwa kaburini) katika karne ya kwanza huko Palestina.

**50:3 "siku arobaini"** Namba 40 (BDB 917) yaweza kuwa halisi au ya kiujumla. Waebrania walimlilia kwa siku 30 (kama vile Hes. 20:29; Kumb. 34:8) kwa ajili ya viongozi wa kitaifa. Ilikuwa alama ya heshima.

◙**"siku sabini"** Yakobo alipokea maziko ya kifalme. Farao mwenyewe aliombolezewa kwa muda wa siku sabini (mwana historia wa Kiyunani, Diodorus [1.72]). Wamisri walimlilia kwa ajili ya Yakobo nje ya utaraibu wa Yusufu.

## MADA MAALUM: VIWAKILISHI VYA NAMBA KATIKA MAANDIKO

A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.

1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchinne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
   a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
   b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
   c. makanisa saba, Ufu. 1:20
   d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
   e. taa saba, Ufu. 4:5
   f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
   g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
   h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
   i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
   j. ngurumo saba, Ufu. 10:3,4
   k. elfu saba, Ufu. 11:13
   l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
   m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
   n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9

o. wafalme saba, Ufu. 17:10

5. Kumi– ukamilifu
    a. matumizi katika Injili
        1) Mt. 20:24; 25:1,28
        2) Marko 10:41
        3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
    b. matumizi katika Ufunuo
        1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
        2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
        3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
    c. Vigawe vya 10 katika Ufunuo
        1) 144,000 = 12x12x1000, kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
        2) 1,000 = 10x10x10, kama vile Ufu. 20:2,3,6
6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
    a. Wana kumi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumi na mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
    b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
    c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
    d. mikate kumi na miwili, ju ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
    e. Watu kumi na wawili, Kumb. 1:23;
    f. mawe kumi na mawili, Yos. 4:2,3,4,8,9,20
    g. miktume kumi na wawili, Mt. 10:1
    h. matumizi katika Ufunuo
        1) makakabila kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri, Ufu. 7:5-8
        2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
        3) milango kumi na mikwili, malaika kumi na wawili, makabila kumi na mawili, Ufu. 21:12
        4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
        5) Yerusalemu mpya ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufu. 21:16
        6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
        7) mti wa uzima uzaao matunda, aina kumi na mbili, Ufu. 22:2
7. Arobaini –namba za nyakati
    a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
    b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
        1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
        2) Musa juu ya Ml. Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
        3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
        a) miaka arobaini ndani ya Misri
        b) miaka arobaini jangwani
        c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
        4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
    c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Bibia!
8. Sabini – namba ya jumla ya watu
    a. Israeli, Kut. 1:5
    b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
    c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
    d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
    e. msamaha (70x7), Mt. 18:22

B. Marejeo mazuri
1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:4-6**
**4 Siku za kumlilia zilipopita, Yusufu alisema na watu wa nyumba ya Farao, akinena, Kama nimeona neema machoni penu, tafadhalini mkaseme masikioni mwa Farao, mkinena, Baba yangu aliniapisha, akisema, 5 Mimi ni katika kufa, unizike katika kaburi langu nililojichimbia katika nchi ya Kanaani. Basi tafadhali uniruhusu niende sasa nikamzike babangu, nami nitarudi. 6 Farao akasema, Uende, ukamzike baba yako, kama alivyokuapisha.**

**50:4 "kama nikipata neema machoni penu"** Hii ni lahaja ya uthibitisho (kama vile 18:3; 47:29; Kut. 33:13). Hii lahaja mara zote imetumiwa na mtu wa chini akitaka kumuuliza mtu wa juu (yaani Ruth 2:13). Hapa Yusufu anaonyesha heshima kwa Farao.

**50:5-6** Katika mst. 5 Yusufu anashirikisha kiapo chake (BDB 989, KB 1396, *Hiphil* WAKATI TIMILIFU, kur. 5,6) kwa babaye, Yakobo (#1,2) na ahadi ya kurudi kwake (#3).
1. niende, BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI
2. unizike, BDB 868, KB 1064, *Qal* HALI YA KUSIHI
3. nami nitarudi, BDB 996, KB 1427, *Qal* HALI YA KUSIHI

Katika mst. 6 anamkubalia ombi lakelinalohusiana na kiapo chake.
1. nenda, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. kamzike, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**50:5 "nililojichimbia"** Muundo wa fasihi ya sheria za Kiyahudi (Peshitta na REV) inafanya mbadala wa neno "nunuliwa" (kama vile Mwa. 23:17-20; 47:27-31; 49:29-32). Mizizi miwili ya Kiebrania inafanana
1. chimba, BDB 500 I, kama vile 26:25; Hes. 21:18
2. nunua, BDB 500 II, kama vile Kumb. 2:6

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:7-14**
**7 Basi Yusufu akaenda amzike babaye, na watumwa wote wa Farao wakaenda pamoja naye, wazee wa nyumbani mwake, na wazee wote wa nchi ya Misri. 8 Na nyumba yote ya Yusufu, na nduguze, na nyumba ya babaye; wakawaacha watoto wao tu, na kondoo zao, na ng'ombe zao, katika nchi ya Gosheni. 9 Kisha wakaenda pamoja naye wapanda farasi, na magari; wakawa jeshi kubwa sana. 10 Wakaja mpaka sakafu ya Atadi, iliyo ng'ambo ya Yordani. Wakaomboleza huko maombolezo makuu, mazito sana. Akafanya matanga ya babaye siku saba. 11 Nao waliokaa katika nchi, wale Wakanaani, walipoyaona matanga katika sakafu ya Atadi, wakasema, Matanga haya ya Wamisri ni makuu kwa hiyo mahali pale paliitwa Abel-Misri, iliyo ng'ambo ya Yordani. 12 Wanawe wakamfanyia kama alivyo waagiza; 13 kwa kuwa wanawe wakamchukuwa mpaka nchi ya Kanaani, nao wakamzika katika pango ya shamba la Makpela, iliyo mbele ya Mamre, aliyoinunua Ibrahimu pamoja na shamba kwa Efroni Mhiti, pawe milki yake pa kuzikia. 14 Yusufu akarudi Misri, yeye na ndugu zake, na wote waliyokwenda pamoja naye kumzika babaye, baada ya kumzika babaye.**

**50:7-8** mistari ya 7-8 inaonyesha ni kwa ukubwa kiasi gani msiba ulifanyika huko Kaanani.
1. Yusufu
2. Watumishi wa Farao
3. Nduguze wa nyumbani mwake
4. Wazee wa nchi ya Misri
5. Watu wa nyumbani mwa Yusufu
6. Nduguze Yusufu
7. Watu wa nyumbani mwa Yakobo

8. Misafara ya kijeshi, mst. 9

Mstari wa 9 unadokeza kuhusu msafara wa kijeshi uliowasindikiza. Yawezakuwa pia ni njia ya Farao ya kuwahakikishia washauri wake kurudi salama.

**50:8 "wakawaacha watoto wao, na kondoo, na ng'ombe zao"** Hii ilikuwa ni namna ya kuwahakikishia kurudi kwao!

◙**"katika nchi ya Gosheni"** angalia kumbukumbu katika 45:10; 46:28.

**50:10 "Atadi"**Kiuhalisia hii ni "miiba" (BDB 31). Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema ilikuwa ni namna ya utoaji wa ulinzi. Eneo hili halijulikani. Jerome anasema lilikuwa pande za Yeriko. Ilikuwa ni sehemu ya ibada ya maombolezo, na si kihivyo kuwa ilikuwa ni sehemu ya maziko!

◙ mkazo wa machungu yao umeelezewa kwa

1. maombolezo yaliyokuwepo
2. Kwa uchungu
3. na kilio
4. maombolezo
5. kwa kudumu siku saba
6. kumbuka mst. 11

◙**"ng'ambo ya Yordani"** Kifungu hiki , "eneo la" (BDB 81 INAUNDA NENO BDB 719 I, kama vile mst. 11), Haibainishi ikiwa ilikuwa ni Mashariki au Magharibi mwa kingo za mto. Inategemea na mahali mzungumzaji alipoelekeza.

**50:11** Huu ni mzaha wa neno "Abeli" (BDB 5 II), ambalo linamaanisha "konde la majani" (hasa " kijani kibichi"), na "Abeli" (BDB 5 I), likimaanisha "kuomboleza" (AB inaoredhesha chaguo namba tatu, "mfereji wa maji," uk. 376).

**50:12-14** Huu ni muhtasari wa maelezo ukielezea ahadi ya Yakobo.

**50:13 "pango"** Pango hili ni lile lililorejerewa katika sura ya 23:16-20.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:15-21**

**15 Ndugu zake Yusufu walipoona ya kwamba baba yao amekufa, walisema, Labda Yusufu atatuchukia; naye atatulipa maovu yetu tuliyomtenda. 16 Wakapeleka watu kwa Yusufu, kunena, Baba yako alitoa amri kabla ya kufa kwake, akasema, 17 Mwambieni Yusufu hivi, Naomba uwaachilie ndugu zako kosa lao na dhambi yao, maana walikutenda mabaya; sasa twakuomba utuachilie kosa la watumwa wa Mungu wa baba yako. Yusufu akalia waliposema naye. 18 Nduguze wakaenda tena, wakamwangukia miguu, wakasema, Tazama, sisi tu watumwa wako. 19 Yusufu akawaambia, Msiogope, je! Mimi ni badala ya Mungu? 20 Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo. 21 Basi sasa msiogope; mimi nitawalisha na watoto wenu. Akawafariji, na kusema nao vema.**

**50:15** mkazo wa uhusika wa nduguye umeelezewa katika

1. KITENZI "kuchukuliana na machungu" (BDB 966, KB 1316), ambayo yalitumika mwanzoni kwa Esau (27:41) na kudokezwa katika sura ya 49:23. Pia ilitumiwa na Ayubu 16:9; 30:21. Ni KITENZI chenye nguvu.
2. kifungu "na atatulipa maovu yetu tuliomtendea," ambacho ni neno *Hiphil* KITENZIJINA HALISI na neno *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU ya mzizi ule ule (BDB 996, KB 1427).

**50:16-17** Huu unatambulisha rejeo lisilojulikana toka kwa Yakobo ambalo nduguye alitumia kurejea ili kuwahakikishia fadhira za Yusufu.

**50:17** mstari unajaribu kuonyesha kipindi kwa ajili ya maelezo ya imani ya Yusufu katika mistari ya 19-20. Hofu ya nduguze na shauku kwa ajili ya msamaha waweza kuonekana katika

1. kuomba msamaha, BDB 609, KB 724, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. tunakuomba (toleo la NASB linaelezea zaidi )
3. makosa na dhambi za nduguze (kama vile 37:18-28)
4. tulikutenda vibaya
5. tunaomba uwaachilie kosa lao
6. mst. 18

sababu pekee ya ombi lao ilikuwa ni

1. maneno ya Yakobo, mistari ya 16-17
2. ni watumishi wa Mungu wa Yakobo, mst. 17

**50:19**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV,** | |
| **NRSV** | **"mimi ni badala ya Mungu"** |
| **TEV** | **"siwezi kujiweka kuwa badala ya Mungu"** |
| **NJB** | **"ni vema kwangu kujiweka badala ya Mungu"** |
| **LXX** | **"je mimi ni Mungu"** |
| **Peshitta** | **"mie ni mtumishi wa Mungu"** |
| **JPSOA** | **"je mie ni badala ya Mungu"** |

Hii ilikuwa ni namna ya Yusufu ya kusema kuwa alijiona mwenyewe kama sehemu ya njia ya Mungu ili kuitunza familia ya Ibrahimu (kama vile 45:5-15; Zab. 105:16-24)! Alilielezea hili katika mst.20. Hakujiona yeye mwenyewe kutenda kama mwamuzi, ni Mungu ndiye angelilifanya hili! Swali katika Kiebrania linategemea jibu la "hapana". Maelezo ya aina ile ile yanapatikana katika sura ya 30:2.

**50:20 "mlikusudia mabaya juu yangu"** Yusufu hakuzifunika dhambi za nduguze, bali aliona "mkono usioonekana" wa Mungu katika maisha yake na matukio! Aha ambacho tungaliweza, kwa imani, kuutambua "mkono usioonekana" katika maisha yetu! Kwa ajili ya makala mazuri juu ya Mungu akitumia dhambi za mwanadamu kulitimiza kusudi lake, angalia Millard Erickson, *Christian Theology*, toleo la pili., kur. 425-426.

◙**"Mungu aliyekusudia kuwa mema"** Huu ni mfano mzuri wa maana ya Warumi 8:28-29.

50:21 Yusufu akawambia nini atakifanya kwa ajili ya familia.

1. Msiogope, BDB 431, KB 432, *Qa*l KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa maana ya KUSIHI, kama ilivyo mst. 19
2. Mimi nitawalisha, BDB 465, KB 463, *Pilpel* KAULI ISIOTIMILIFU, kama vile 45:11; 47:12
3. Nitawalisha na watoto wenu, BDB 465, KB 463, *Pilpel* KAULI ISIOTIMILIFU, kama vile 45:11; 47:12
4. akawafariji, BDB 636, KB 688, *Piel* KAULI ISIOTIMILIFU
5. na kusema nao vema (hasa "akiongea toka rohoni," kama vile 34:3; Amu. 19:3; Ruth 2:13)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:22-26**

**[22] Akakaa Yusufu katika Misri, yeye na nyumba ya babaye. Akaishi Yusufu miaka mia na kumi. [23] Yusufu akaona wana wa Efraimu hata kizazi cha tatu; na wana wa Makiri, mwana wa Manase, walizaliwa magotini mwa Yusufu. [24] Yusufu akawaambia nduguze, Mimi ninakufa, lakini Mungu atawajia ninyi bila shaka, atawapandisha toka nchi hii, mpaka nchi aliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo. [25] Yusufu akawaapisha wana wa Israeli, akasema, Bila shaka Mungu atawajia ninyi, nanyi mtaipandisha huko mifupa yangu. [26] Basi Yusufu akafa, mwenye miaka mia na kumi; wakampaka dawa, wakamtia katika sanduku, huko Misri.**

**50:22 "miaka mia na kumi"** Huu ulikuwa ni umri muafaka katika fasihi za Kimisri.

**50:23 "Makiri"** Pia angalia Yoshua 17:1 na Waamuzi 5:14. Jina laweza kuhusiana na mzizi unaofanana na neno

"bidhaa" au "thamani" (BDB 569).

◙"**walizaliwa magotini mwa Yusufu"** Kwa wazi kabisa hili halikupaswa kuchukuliwa kikawaida. Ni lahaja za kitamaduni za Mashariki ya Kale ya Karibu zilizotumika kwa ajili ya makubaliano (kama vile 30:3; 48:12) au kumpokea mtu kwenye familia.

**50:24 "Mungu atawajia ninyi"** Yusufu aliamini katika uangalizi aliouahidi Mungu kwa familia ya Ibrahimu (kama vile Mwa. 15:16)! Yusufu alikuwa ni chombo cha Mungu, lakini kama akiondoka katika maisha haya, atainua mwingine (yaani Musa, Haruni, Yoshua, n.k.).maneno ya Yusufu yametiwa mkazo na neno *Qal* KITENZIJINA HALISI na neno *Qal* KITENZI KISICHO TIMILIFU cha mzizi wa aina ile ile (BDB 823, KB 955, hasa, neno "kuwajia," lililotumika hasa kwa maana ya uwepo wa Mungu na uangalizi, kama Kut. 3:16; 4:31; Ruth 1:6; Zeph. 2:7). Muundo huu unapatikana kote katika mistari ya 24,25!

**50:25 "mtaipandisha mifupa yangu"** Alijua wangalirudi kwenye nchi ya ahadi na alitaka azikwe huko kama baba yake alivyofanya (kama vile Kut. 13:19; Yosh. 24:32).

**50:26 "sanduku la maiti"** Neno hili (BDB 75) laweza kurejerea

1. sanduku (la agano, yaani Kut. 25:22; 26:33; 30:6; Hes. 10:33; Kumb. 10:8; 31:9; Yosh 3:3), sanduku takatifu la kidini
2. sanduku, hapa tu (Waisraeli hawakutumia sanduku)
3. sanduku, kwa ajili ya pesa (yaani., II Fal. 12:10; II Nya. 24:8,10,11)

Neno lingine lililotafasiliwa katika Kiingereza neno "sanduku la agano" (BDB 1061) linarejea kwa

1. safina ya Nuhu (yaani Mwa. 6:14)
2. Kikapu cha mafunjo alichowekwa Musa (yaani Kut. 2:3)


## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Yusufu alipewa maziko ya kifalme huko Misri?
2. Kwa nini nduguze Yusufu hawakumwamini?
3. Kwa nini mistari ya 19-20, ikilinganishwa na 45:5-15, ni ya muhimu?

# KIAMBATISHO CHA KWANZA
## MCHORO WA AGANO LOTE LA KALE
**(katika kurasa inayofuata)**


MALAKI
ARTAXERXES I (P)
XERXES I – AHASUERO (P)
EZRA 7-10
NEH.
ESTA
10
UKUTA WA YERUSALEMU – NEHEMIA
KURUDI MARA YA TATU – EZRA
9
UAJEMI
DARIO I (P)
CAMBECE II (P)
KORESHI II (P)
OBADIA
YOELI
HAGAI
ZAKARIA
EZRA 1-6
8
KURUDI MARA YA PILI – ZERUBABELI
KURUDI MARA YA KWANZA – SHESHBAZA
BELSHAZA (B)
NABONIDA (B)
KUKIMBILIA
UHAMISHONI
7
BABELI
NEBUKADREZA (B)
NABOPOLASA (B)
YEREMIA
EZEKIELI
DANIELI
NAHUMU
HABAKUKI
SEFANIA
p – GEDALIA (P)
o – ZEDEKIA (J)
n – YEHOAKINI (J)
m – YEHOAKIMU (J)
l – YEHOAHAZI (J)
k – YOSIA (P)
j – MANASE (J)
i – HEZEKIA (J)
h – UZIA (J)
g – YEROBOAMU II (I)
ASHURU
ASUR-BANI-PALI (A)
ESAR-HADONI (A)
SENAKERIBU (A)
SAGONI II (A)
YONA
SHALMANESA V (A)
TIGRATH-PILESERI III (A)
AMOSI
HOSEA
g
6
ISAYA
MIKA
h i j k l m n o
1 & 2 WAFALME
2 MAMBO YA NYAKATI
STAMU
FILISTIA
KANAANI
MISRI
ELIYA
ELISHA
e
f
ISRAELI
YUDA
5
4
(abc) d
Yash. (SDS)
3
1 & 2 SAMWELI
1 MAMBO YA NYAKATI
f – AHABU (I)
e – YEROBOAMU I (I)
d – REHOBOAMU (J)
c – SULEIMANI (UM)
b – DAUDI (UM)
a – SAULI (UM)
Law. Kut.
Kumb. Hes.
2
Mwa. 12-50
1
AYUBU
MWANZO 1-11
1 – MNARA WA BABELI (4)
1 – GHARIKA YA NUHU (3)
1 – ANGUKO LA MWANADAMU (2)
1 – UUMBAJI (1)
DR. BOB UTLEY
BIBLE LESSONS INT'L 96

**Matukio yasiyo na Wakati (Mwanzo 1-11**)

1. Uumbaji (Mwa. 1-2)
2. Anguko la Mwanadamu (Mwa. 3)
3. Gharika la Siku ya Nuhu (Mwa. 6-9)
4. Mnara wa Babeli (Mwa. 10-11

**Matukio yenye kuonyesha Wakati**

1. Kipindi cha Mababa wa Imani (Mwa. 12-50 na Ayubu) 200 K.K
2. Kipindi cha Uhamisho wa kutoka Misri (Kutoka) 1445 au 1290 K.K
3. Kuiteka Kanaani (Yoshua) 1440 au 1250 K.K
4. Falme za Israeli zilizoungana (Sauli, Daudi, Suleimani) 1000 K.K
5. Falme za Israeli Zilizogawanyika Ashuru (Rehoboamu-Yeroboamu 922 K.K
6. Kuanguka kwa Samaria 722 K.K
7. Kuanguka kwa Yerusalemu 586 K.K
8. Amri ya Koreshi (Uajemi) juu ya Babeli 538 K.K
9. Hekalu kujengwa Upya 516 K.K
10. Kipindi cha Ukimya wa Agano la Kale (Malaki) 430 K.K

**Orodha ya Wafalme**

A. Falme za Israeli
   1. Sauli (a)
   2. Daudi (b)
   3. Suleimani (c)
   4. Senakaribu (705-681)

B. Israeli
   A. Yeroboamu I (e)
   B. Ahabu (f).
   C. Yeroboam uII (g)
   2. Nebukadreza (605-562

C. Yuda
   1. Rehoboamu (d)
   2. Uzia (h))
   3. Hezekia (i)
   4. Manase (j)
   5. Yosia (k)
   6. Yehoahazi (l)
   7. Yehoahakimuz (m)
   8. Yehoakimni (n)
   9. Sedekia (o)
   10. Gedalia (p)

D. Ashuru
   1. Tigrath-Pileseri III (745-72)
   2. Shalmanesa V (727-722)
   3. Sargoni II (722-705)
   5. Esar-hadoni (681-669)
   6. Asur-bani-pali (669-663)

E. Babeli
   1. Nabopolasari (626-605)
   3. Nabonida (556-539)
   4. Belshaza

F. Uajemi
   1. Koreshi II (550-530)
   2. Cambees
   3. Dario
   4. Ahasuero I (486-465)
   5. Artashasta I (465-424)

# KIAMBATISHO CHA PILI
# KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milele kwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.

9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

   Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo."